# TAARIFA YA TUME YA MAREKEBISHO YA KATIBA YA KENYA

# YALIYOMO

CHAGUO LA WANANCHI ........................................... **Error! Bookmark not defined.**
DIBAJI ........................................................................................................ iii
MUHTASARI WA MAPENDEKEZO ............................................................ iv
SURA YA KWANZA ........................................................................... 21
MSINGI WA KENYA ........................................................................... 21
HALI YA MALIASILI ........................................................................... 22
ULINGANIFU KIENEO ........................................................................ 24
SURA Y A PILI ................................................................................... 26
TUME YA MAREKEBISHO YA KATIBA YA KENYA .................................. 26
UTEUZI NA UANACHAMA .................................................................. 26
KUJADILI UTARATIBU MUHIMU WA MAREKEBISHO ................................ 27
SURA YA TATU .................................................................................. 38
MAENDELEO YA KIKATIBA NCHINI KENYA ............................................ 38
KATIBA YA UHURU ........................................... **Error! Bookmark not defined.**
HITIMISHO ........................................................................................ 57
SURA YA NNE .................................................................................... 57
MIJADALA NA UTARATIBU WA MAREKEBISHO YA KATIBA ......................... 57
SURA YA TANO ................................................................................... 83
MUKTADHA WA MAREKEBISHO KIJAMII, KIUCHUMI NA KISIASA ................ 83
SURA YA SITA .................................................................................. 100
KUMILIKI UTARATIBU WA MAREKEBISHO .............................................. 100
HOJA KUMI NA TATU MUHIMU KUTOKA KWA WANANCHI ........................ 103
KUWATILIA WANANCHI MAKINI ............................................................ 107
SURA YA SABA: TARATIBU ZA KATIBA ................................................. 112
SURA YA NANE ................................................................................ 135
SHERIA YA HAKI .............................................................................. 135
SURA YA TISA .................................................................................. 165
TAIFA NA MFUMO WA KISIASA ............................................................ 165
SURA YA KUMI ................................................................................. 225
UTAWALA HUSISHI ........................................................................... 225
SURA YA KUMI NA MOJA ................................................................... 265
VYOMBO VYA SERIKALI ..................................................................... 265
SURA YA KUMI NA MBILI ................................................................... 324
KUPUNGUZA NA KUSAMBAZA MADARAKA .............................................. 324
SURA YA KUMI NA TATU .................................................................... 360
MAZINGARA NA RASILMALI ASILI ......................................................... 360
SURA YA KUMI NA NNE ..................................................................... 381
HAKI ZA ARDHI NA MALI .................................................................... 381
SURA YA KUMI NA NNE ..................................................................... 400
HAKI ZA ARDHI NA MALI .................................................................... 400
SURA YA KUMI NA TANO .................................................................... 435

RASILMALI ZA UMMA NA KUJENGA UWEZO WA UFANYI KAZI.................. 435
SURA YA KUMI SITA........................................................................................ 479
KUSIMAMIA UKATIBA.................................................................................... 479
SURA YA KUMI NA SABA.............................................................................. 510
HITIMISHO NA MUHTASARI WA MAPENDEKEZO ........................................... 510
NYONGEZA ................................................................................................. 528
IBARA YA 3A ............................................................................................... 528
SEHEMU YA KWANZA – DIBAJI..................................................................... 528
SEHEMU YA PILI – KUANZISHWA NA KUUNDWA KWA TUME...................... 528
SEHEMU YA TANO – MATUMIZI YA SHUGHULI ZA MAREKEBISHO ............ 529
SHERIA YA 3A ............................................................................................. 531
SHERIA ZA MAREKEBISHO YA KATIBA YA KENYA ......................................... 531
SEHEMU YA PILI – KUANZISHWA NA KUUNDWA KWA TUME...................... 535
KIAPO CHA AFISI YA KAMISHNA.................................................................. 556
KAMISHNA .................................................................................................. 556
JAJI MKUU .................................................................................................. 556
TAMKO LA DHATI LA KAMISHNA ................................................................. 557
KAMISHNA .................................................................................................. 557
JAJI MKUU .................................................................................................. 557
KIAPO CHA AFISI YA KATIBU AU NAIBU WA KATIBU..................................... 558
KATIBU/NAIBU WA KATIBU.......................................................................... 558
JAJI MKUU .................................................................................................. 558
TAMKO LA DHATI LA KATIBU NA NAIBU WA KATIBU .................................. 559
KATIBU/NAIBU KATIBU................................................................................ 559
JAJI MKUU .................................................................................................. 559
KANUNI YA MAADILI YA WANATUME NA WATUMISHI WA TUME............. 560
JEDWALI LA TATU ............................................................... Na.2 ya 2001561

## DIBAJI

Tume ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya ina furaha kuichapisha na kuitangaza taarifa hii ya kazi yake, na mapendekezo kuhusu Katiba mpya. Toleo hili ni moja kati ya taarifa kadha zilizochapishwa na Tume ya Marekebisho ya Katiba. Tume imechapisha nakala fupi ya Taarifa hii, Mswada wa Katiba – kwa hakika kubadilisha Katiba iliyopo – mfululizo wa taarifa kutoka vikao vya maeneo ya kikatiba – taarifa kutoka kila eneo. Taarifa hizi zinajadiliwa nchi nzima ili kujiandaa kwa Kongamano la Kitaifa la Katiba.

Ni heshima kubwa kwa Tume kutunukiwa ama kuaminiwa kuifanya kazi hii. Imetambua umuhimu mkubwa wa kuwapo kwa Katiba Mpya wakati ambapo awamu ndefu ya kazi ya urais wa Rais Daniel arap Moi inapofika kikomo na wakati Wakenya wanapotazamia maisha mapya ya baadaye. Tumesikiliza kwa makini maoni ya Wakenya kote nchini. Tumeguswa na kusikitishwa na maelezo yao, na kugundua busara nyingi kwenye mapendekezo yao. Tumechambua maendeleo ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kikatiba nchini Kenya kwa miongo minne iliyopita,na kujaribu kuwaza na kufikiria maisha ya baadaye ambayo kwayo Katiba mpya itatumika.

Kwetu sote Wanatume hii pia imekuwa ni safari ya kujitambua.Tumejifunza mengi ambayo hatukuyafahamu kuhusu watu na nchi yetu. Ingawa tulishangazwa na kiwango cha umaskini unaowakumba Wakenya wengi, masikitiko ya kuporomoka kwa uchumi,ukabila katika siasa na ghasia zinazoambatana nazo, tunaamini kuwa tukipata utaratibu unaofaa wa utawala na uongozi mwema unaojali malengo ya umoja na maendeleo yenye usawa, Kenya inaweza kurudia nafasi yake ya awali kama taifa ambalo limeendelea kiuchumi barani Afrika. Tumeweka wazi malengo yetu kwenye taarifa hii tunayotarajia kuyatimiza kupitia mapendekezo yetu kikatiba, yanayowaweka wananchi katika shina la siasa na maendeleo.

Tunafahamu kwamba watu wana matumaini makubwa ya marekebisho na tunaelewa kuwa katiba mpya inatoa ahadi nyingi sana kwao. Tunaamini kwamba ikiwa mapendekezo yetu yatatekelezwa kihaki, ahadi hizo zinaweza kutimizwa. Tunawasihi viongozi wetu, wasiwavunjie wananchi matumaini yao.

**Yash Pal Ghai**
**Mwenyekiti**

**Septemba 18, 2002**

## MUHTASARI WA MAPENDEKEZO

Muhtasari ufuatao, ndio wenye mapendekezo, ambayo Tume imerekebisha na kuyaunganisha katika mtindo wa mswada wa katiba. Haya ni kama yafuatayo:-

**Katika Ukuu wa kikatiba, Katiba mpya lazima -**

1. iwe na masharti madhubuti, ambayo hata Bunge lenyewe halitakuwa na uwezo wa kuunda sheria pasi kupata maoni kwanza kwa wananchi.
2. ishughulikie masuala ya uhusiano katika viungo vya serikali na ni sharti vishughulikie usawazishaji na usambazaji madaraka.
3. iwe na ibara katika ukuu na sharti ieleze kwamba katiba inawaunganisha watu wote na viungo vyote vya serikali katika viwango vyote.
4. isipokuwa kama sehemu ya (1) hapo juu, iliyopendekezwa na irekebishwe na angalau asilimia 75% ya wabunge.

**Katika ufafanuzi wa katiba, katiba mpya -**

5. iwe na ibara fafanuzi ambayo itawasaidia wafasiri ili wapendezwe na maadili ya kimsingi ya kikatiba bila kutoa ubunifu wa mahakama ambao unaruhusu katiba kuwa haki ya kudumu.
6. iwe na masharti ambayo yanaelezea kanuni za utawala fafanuzi ambao ni lazima ujumuishe kupanda cheo kwa maadili yanayoweka wazi demokrasia katika jamii, katika msingi wa haki za binadamu, usawa na uhuru.
7. ibuni mahakama kuu ya kutoa uamuzi juu ya ufafanuzi wa katiba.

**Katika uhuru wa wananchi kujitawala, katiba mpya -**

8. itambue uhuru wa wananchi kujitawala.
9. itambue kwamba serikali inapata nguvu kutoka kwa wananchi.

**Katika utaifa na uraia, katiba mpya -**

10. impe mume wa mke usawa kulingana na uraia hata kama mke ameolewa na Mkenya ama Mkenya amemwoa mke mgeni.
11. ielezee kwamba raia wote wana haki ya kupata kitambulisho cha kitaifa na paspoti ya usafiri.

12. itoe uraia maradufu, kwa kuzaliwa, kusajiliwa na katika hali ya makao ya kudumu.

13. kuunda na kubuni shirika huru litakalokuwa na jukumu la kushughulikia masuala ya uraia ili kuzuia usumbufu wa haki za uraia.

14. itoe uraia kwa watoto wa kupanga na wa kihalali

15. itoe uraia kwa watoto walio na umri fulani waliopatikana humu nchini ambao wazazi wao hawako (hawapatikani).

16. itoe usawa kwa raia wote bila kujali asilia ya rangi, kabila, umri, mahali pa kuzaliwa, jinsia ama tofauti zozote zilizopo.

**Katika utawala na ulinzi, Katiba mpya -**

17. ibainishe maeneo ya kimataifa ya Kenya na kutangaza utawala kwenye maeneo hayo.

18. ibuni walinzi na jeshi la usalama ambalo haliungi mkono vyama vyoyote vya siasa, wenye nidhamu, wazalendo na ambao watadhibitiwa na umma.

19. ielezee kikamilifu namna ambavyo hali ya kivita inavyoweza kutangazwa, ama vikosi vya usalama wa taifa vyenye utendaji kazi nje ya maeneo ya Kenya.

**Katika maadili ya nchi, malengo na itikadi katiba mpya -**

20. iwe na utangulizi ambao pamoja na mengine: unatambua umuhimu wa Mungu kwa watu wa Kenya; unatambua harakati za kupigania uhuru na majukumu ya wapiganiaji uhuru, kutambua umuhimu na utawala wa wananchi katika kubuni katiba na kuweka mbinu za utawala wao na vizazi vya baadaye, msingi wa kidini, utamaduni na madhehebu mbali mbali ya Kenya, kuthibitisha kuwepo kwa Kenya kama taifa lisilogawanyika, linalonuia kuponya majeraha baada ya uhuru yaliyosababishwa na vita vya kisiasa, kuthibitisha uwajibikaji katika haki za jamii, na kuthibitisha uwajibikaji katika kupata demokrasia, kikatiba na sheria ya uongozi.

21. pia iwe na kanuni zinazoelekeza sera za nchi zinazomtaka kila mtu na vyombo vya serikali, kuheshimu sheria ya uongozi, kulinda kanuni za demokrasia, kulinda haki za kimsingi, kutekeleza mamlaka kwa haki na kutawala maliasili ya nchi vema.

22. ibuni maadili mazuri ya utawala katika taifa, demokrasia na sheria ya uongozi
23. kutangaza kwamba Kenya ni Jamhuri huru ambayo hupata mamlaka yake kutokana na kugawa mamlaka hayo kwa manufaa ya kila mwananchi.
24. kutangaza kwamba Ujamhuri huu utakuwa wa demokrasia ya vyama vingi vyenye kutaka kushirikisha kila mwananchi katika utawala wa masuala ya umma moja kwa moja ama katika njia nyingine isiyo dhahiri.
25. kutangaza kwamba mamlaka yote yatumikayo yatatekelezwa kwa niaba ya wananchi.
26. kufafanua wazi na kueleza kanuni na itikadi za kimsingi za kitaifa na maadili ambayo yanaelekeza jamii mpya, kisiasa, utamaduni, kiuchumi na ugawaji wa kimazingira.

**Katika mfumo wa kisheria, katiba mpya iweze -**

27. kufafanua wazi asili ya sheria za Kenya.
28. kutambua kuwepo na maadili ya sheria ya utamaduni wa Afrika, sheria ya Kiislamu na ile ya Wahindu.
29. kutangaza sheria za utamaduni wa kimataifa na mikataba inayowaunganisha Kenya ni mojawapo ya sheria za jamii.

**Katika mswada wa Haki, Katiba mpya ihakikishe -**

30. pamoja na haki za wa siasa na kiraia, izingatie haki za jamii, kiutamaduni, kiuchumi na maendeleo.
31. ufafanuzi kwamba sheria ya haki haiathiri watu waliopo serikalini pekee bali kati ya watu pia.
32. mahakamani kunafikika na kwamba kuna utawala wa haki.
33. kubuni kuweko kwa asasi mbali na mahakama ya usimamizi wa mswada wa kisheria.
34. kueleza hasa haki na mahitaji ya wanawake na watoto.
35. inaweka masharti yatakayotambua haki za walemavu.
36. inaweka masharti yatakayotambua haki za wazee.
37. inatambua haki za wakimbizi.

38. serikali itachukua msimamo mkali kuhusiana na makundi ya wachache yaliyokandamizwa kijinsia, kiidadi, kilemavu, umri ama sababu zilizobuniwa kihistoria, kimila au kidesturi.

39. kubuni utaratibu/mpango wa kisheria utakaothibitishwa na habari ifaayo, matumizi ya mbinu na malengo yatakayoendeshwa kwa uwazi na muda ukizingatiwa na kuchunguzwa mara kwa mara.

40. ifutilie mbali adhabu ya kifo.

41. itoe kinga ya kimsingi ya faragha katika familia, kukubaliana na njia nyingine za mawasiliano.

42. itoe kinga katika vyombo vya utangazaji, pamoja na kinga dhidi ya serikali kutatiza mashirika hayo.

43. itambue maadili ya lugha nchini, haki za watu kutumia lugha hizo, na jukumu la serikali kuwasiliana na kuzitumia na kubuni mbinu za maendeleo panapohitajika .

44. itoe hakikisho la kufikika katika habari za serikali, labda kwa sababu zisizoepukika kwa minajili ya usalama wa nchi, na habari muhimu zilizofichwa na wengine ili kushinikiza haki.

45. ilinde haki ya utawala.

46. ilinde haki ya watu walio kizuizini ama korokoroni.

47. ihakikishe haki za wateja katika matumizi bora ya bidhaa kutoka kokote, utangazaji ufaao na mashauriano bora.

**Katika utamaduni, dini na lugha mbalimbali, Katiba mpya inapaswa**

48. kuhakikisha kwamba uhuru wa kuabudu hautumiwi kuasi uhuru wa dini za watu wengine.

49. kufafanua kwamba hakuna kipimo cha kidini kitakachohitajika kama mojawapo ya sifa ili kupata mamlaka ama ithibati ya umma chini ya serikali ya Kenya.

50. kutangaza kwamba Kenya ni taifa lisiloendeshwa na dini, kwamba Kenya itafanya lolote iwezalo kusaidia, kutia moyo ama kukuza dini fulani.

51. kuweka mbinu ambazo zitakwamua vikwazo vinavyohusiana na utamaduni na maadili ya jamii, dini, pamoja na kuleta maadili ya kitaifa na umoja wake.

52. kuhakikisha kwamba hakuna mtu hata mmoja atakayelazimishwa kushiriki katika shughuli yoyote ama tambiko ama kula kiapo, kumiliki silaha, kufanya kazi ama kusomea wakati wowote, na iwapo hayo yote hatatendwa basi huo utakuwa ukiukaji wa uhuru wa mtu dini na mawazo yake.

53. kubuni sera mwafaka ya lugha na kutekeleza mbinu zifaazo.

54. kutambua Kiswahili kama mojawapo ya lugha za kitaifa na kuipa kipaumbele wakati wa sherehe za kitaifa.

55. kutambua lugha zote, Kiswahili na Kiingereza, kama lugha rasmi za kitaifa na kuhakikisha kwamba taarifa za kitaifa vitawasilishwa katika lugha hizo mbili.

56. katika harakati za ukabidhi wa mamlaka, Kiswahili kitambuliwe, Kiingereza, lugha ya ishara na lugha nyinginezo, zilizopendekezwa, za maeneo fulani kuwa lugha rasmi katika kiwango cha wilaya.

57. kubuni utekelezaji wa sheria katika asasi za kuendeleza Kiingereza, Kiswahili, lugha ya ishara na ile ya breli itumiwayo na vipofu.

58. kutoa jukumu kwa serikali ili itenge fedha fulani ili kuendeleza lugha za kitaifa, lugha ya ishara na ile ya breli ya vipofu.

59. kulinda haki za isimu za lugha na utamaduni wa wananchi wote.

**Katika vyama vya kisiasa, Katiba mpya inapaswa -**

60. kulinda haki za Wakenya wote katika kubuni vyama vyao vya kisiasa.

61. kuruhusu vyama vya kisiasa vinavyonuia kugombea uchaguzi, viweze kujisajili kwa Tume ya Uchaguzi.

62. kuruhusu Tume ya Uchaguzi kusajili na kusimamia vyama vya kisiasa.

63. kukataza vyama vyovote vya kisiasa vinavyobuniwa katika misingi ya kidini, kilugha, msingi wa rangi, kabila, jinsia, kimashirika ama misingi ya kimaeneo.

64. kukataza vyama vya kisiasa kushiriki katika vitendo vinavyotatiza taratibu za umma ama amani ya umma.
65. kutaka vyama vyote vya upinzani pindi vinaposajiliwa, viweze mara moja kufuata kanuni za kisheria zilizowekwa.
66. kufafanua namna na jinsi gani ambapo chama cha kisiasa chaweza kufutiliwa mbali ama kusajiliwa upya.
67. kufafanua masharti yanayowezesha vyama vya kisiasa, kulingana na shughuli zao, jinsi vinavyoweza kupewa pesa za umma, ama msaada zaidi.
68. kwamba kila mtu yuko huru kujiunga na chama chochote cha kisiasa, hakuna sharuti ya chama; na hivyo basi raia pekee ndio wanaoweza kuwa wanachama wa chama fulani.
69. kukataza kupokeza majukumu ya kitaifa kwa, ama matumizi ya rasilimali za nchi na, vyama vya kisiasa.
70. kutaka uchaguzi wa mamlaka na kamati za vyama vya kisiasa kushughulikia na kusimamiwa na tume ya uchaguzi.
71. kutoa masharti katika utumizi wa fedha kwa vyama vya kisiasa.
72. kutaka vyama vya kisiasa kubuni mbinu zitakazohakikisha kwamba nidhamu imedumishwa kulingana na kanuni za demokrasia, haki na sheria ya uongozi.
73. kuzuia vyama vya kisiasa kutoadhibu wabunge kutokana na misingi ya kuchangia hoja bungeni pamoja na upigaji kura kinyume na matakwa ya chama pendekezi.
74. kumtaka Rais na wakuu wa serikali kutokuwa na nyadhifa zozote kuu katika vyama vyao vya upinzani.
75. kutaka vyama vya kisiasa kuchapisha manifesto ya chama kabla ya kushiriki uchaguzi.
76. kulitaka Bunge kutekeleza sheria kuhusu vyama vya kisiasa.

**Kwenye taifa na mfumo wa kilimwengu, katiba mpya inapaswa -**

78. kulitaka Bunge kutekeleza sheria itakayosaidia kuunganisha malengo yanayohusu uchumi wa Kenya katika ulimwengu na maeneo ya kiuchumi, kwa njia yenye umakini na ufahamu.

79. itake Kenya kukubali mtazamo uwili wenye uwezo sawa katika utaratibu wa kuweka mkataba (makubaliano) yanayohusu jukumu maalum la Bunge kama sehemu yake ya "pembejeo" katika ama usimamizi wa mamlaka ya uwezo wa makubaliano hayo.

**Katika ushiriki na utawala, Katiba mpya inapaswa -**

80. kuthibitisha umuhimu wa wananchi na asasi zao katika kukuza demokrasia na kanuni za Jamhuri, maadili na utekelezaji.
81. kutaka kwamba Wakenya wote wawe na haki ya kushiriki katika masuala ya serikali ama moja kwa moja au kupitia uchaguzi huru wa wawakilishi.
82. kutaka kwamba ni jukumu la maafisa wa umma kukuza mtu binafsi na jamii katika kushiriki kwenye shughuli mbalimbali na kushawishi uamuzi unaowaathiri.
83. kubuni mbinu mwafaka ili kuhakikisha uwajibikaji wa serikali katika viwango vyote na kuwawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika utawala wa nchi.
84. kubuni mbinu za kuwezesha watu kufanya uamuzi kwenye maswala ya kikatiba kupitia ukabidhi wa mamlaka ama vinginevyo.
85. kutaka asasi za kitaifa kuongoza uchunguzi wa umma kabla ya kuundwa au kutekeleza masuala nyeti yanayoathiri maslahi ya umma.
86. kumpa mtu ama makundi haki ya kuwasilisha ombi au malalamishi yake katika asasi za umma na wenye mamlaka likiwemo bunge na kusisitiza kwamba hayo yashugulikiwe.
87. kulipatia Bunge jukumu la kutekeleza sheria itakayofafanua jukumu la uongozi wa kitamaduni, sheria ya kitamaduni na mila za jamii.
88. kubuni mbinu na njia zitakazowawezesha wananchi kuchunguza uwezo wa wawakilishi waliochaguliwa na kuwaachisha mamlaka iwapo kazi zao hazifani.

**Katika mfumo wa uchaguzi katiba mpya inapaswa -**

89. kukubali mfumo wa mseto wa uwiano kwa uchaguzi wa wawakilishi bungeni unaohusisha:

- kubakiza maeneobunge 210 kupitia mbunge mmoja katika maeneobunge hayo
- kutambulisha wawakilishi 90 wenye usawa huku orodha ya chama ikizingatiwa kupata viti sawa baina ya wanaume na wanawake bila kusahau kwamba Kenya ni taifa lenye makabila mengi kutona maeneo tofauti.

90. kutaka kwamba theluthi tatu ya wagombea uchaguzi wawasilishwe na vyama vya kisiasa, theluthi nyingine kuchaguliwa ama kuteuliwa katika nyadhfa hizo kutoka katika asasi za umma, na kuhifadhiwa wanawake.

**Katika utaratibu wa uchaguzi, Katiba mpya inapaswa -**

91. kufafanua kwamba ni haki ya kimsingi na jukumu kwa kila raia wa nchi hii kupiga kura ama kushiriki kikamilifu katika utaratibu wa uchaguzi.
92. taifa kulinda haki ya kila raia, katika kutekeleza jukumu la haki katika upigaji kura.
93. kuona kwamba vifaa vya upigaji kura, vituo vya kupigia kura na msimamizi wa upigaji kura yuko karibu na wapiga kura walemavu, jamii zenye kuhamahama na zile za walio wachache.
94. kusisitiza kanuni kwamba kura zitakuwa za siri.
95. kudhamini haki ya kupiga kura ya majeshi yenye nidhamu, watu walio vizuizini, wafilisi na wale walio hospitali.
96. kuona kwamba usajili wa wapiga kura uwe na taratibu zinazofululiza bila kuwekewa muda fulani (maalum).
97. kuona kwamba katika uchaguzi wa urais mpiga kura aliyejisajili anaweza kupigia kura kokote katika jamhuri bila kujali kituo alichojisajili.
98. kujua kwamba uchaguzi wa ubunge utengewe siku maalum ama kukadirika kila baada ya miaka mitano.
99. kuwapa uwezo wapigaji kura ili kuwatimua wajumbe wao katika baraza na maeneo ya ubunge kwenye Tume Maalum au kuachishwa mamlaka kulingana na sheria mwafaka zilizowekwa.

100. kuhitaji kiwango fulani cha elimu kwa wagombeaji uchaguzi na wawe na sifa nyingine na kuwasilisha taarifa nyingine ambazo sheria za Tume zitahitaji.

101. kuacha huru wagombeaji wa kiti cha urais na kile cha uchaguzi wa ubunge.

102. kutaja hali maalum ambayo inamkataza mgombeaji katika kushiriki uchaguzi.

103. kuwa kwamba wafanyikazi wa serikali wapewe likizo ya kutofika kazini ili kushiriki katika uchaguzi, maadam wafanyikazi wa umma wanakubaliwa kufanya hivyo kikatiba.

104. kubuni sheria inayoorodhesha maadili ya utawala wa uchaguzi na tabia ya mgombea na kuweka adhabu maalum kwa wagombea wanaovunja sheria hizo.

105. kutaka vyombo vya habari nchini kuvipa vyama vya kisiasa muda sawa ama watu wanaoshiriki uchaguzi.

106. kutambua na kurahisisha haki za raia na mashirika mengine ya kijamii na asasi zote kushiriki katika usimamizi wa uchaguzi, pamoja na msaada wa kifedha.

**Katika usimamizi wa uchaguzi, katiba mpya inapaswa -**

107. kubuni tume huru na Tume ya Uchaguzi ya haki, inayojumuisha makamishna wenye maadili walioteuliwa na Rais baada ya kupata idhini kutoka bungeni na kupata fedha moja kwa moja kutoka Hazina kuu ya Serikali.

108. kupendekeza kwamba makamishna wahudumu kwa muda wa vipindi viwili vya miaka mitano na wapewe ulinzi wakiwa bado wanashikilia nyadhfa hizo.

109. Tume ipewe mamlaka/uwezo wa kushughulikia mizozo ya uchaguzi na makosa mengine kwa haraka.

110. kubuniwa kwa Tume Maalum ya maeneo kati ya kipindi cha miaka miwili ijayo ili kuchunguza mipaka ya maeneobunge na maeneo yenye kuhitaji

maeneo mengine kuongezewa kulingana na kigezo maalum cha kimsingi katika sheria za uchaguzi.

**Katika sheria, katiba mpya -**

112. iwe na mabunge mawili, moja lijulikane kama Bunge la Juu yaani Baraza la Kitaifa na Bunge la Chini yaani Bunge la Kitaifa. Mabunge haya yatakuwa na jina moja – Bunge.
113. Baraza la Kitaifa liwe na wanachama 100 ambapo wanachama 70 watachaguliwa katika wilaya zote (pamoja na Nairobi) na wanawake 30 kuchaguliwa katika mikoa yote (4 kutoka kila mkoa na 2 kutoka mkoa wa Nairobi.
114. kupendekeza kwamba baraza la kitaifa lijumuishe kama ilivyo kwenye nambari 89 hapo juu.
115. kupendekeza kipindi cha Bunge kuwa miaka mitano kutoka uchaguzi mmoja hadi mwingine.
116. kufafanua kwa undani majukumu ya Bunge.
117. kupendekeza kwamba vyama vya kisiasa vyenye wanachama wengi au vyama hivyo pamoja viunde serikali (Mseto)
118. kupendekeza Bunge liwe na uwezo usio na mipaka kwenye taratibu zao na liwe na uwezo kabambe kwenye takwimu yao.
119. kupendekeza kwamba wabunge wafanye kazi kwa muda kamili.
120. kueleza kwamba Bunge lina mamlaka ya kupiga kura ya kutokuwa na imani na serikali.
121. kuwataka wabunge kubuni afisi za maeneobunge.
122. kuelezea kwamba afisi ibuniwe ya kiongozi wa chama cha wasio wengi na kutambuliwa na Bunge.
123. kuzidisha uwezo wa Bunge ili kusimamia utendaji kazi wa mamlaka ya matawi.

**Kuhusu mamlaka ya nchi katiba mpya -**

124. itekeleze mamlaka katika matawi yanayojumuisha Rais, Baraza la Mawaziri likiongozwa na Waziri Mkuu.

125. ielezee kwamba mgombea wa Urais ateuliwe na chama cha kisiasa au awe mgombea huru mwenye umri wa miaka kati ya 35 hadi 70, msomi kutoka chuo kinachotambulika, mwenye maadili mema na tabia njema.

126. ielezee kwamba Rais achaguliwe na watu moja kwa moja katika misingi ya upigaji kura kwa wote.

127. ielezee kwamba mgombea urais, atakayeibuka na wingi wa kura asilimia 20% katika angalau mikoa mitano ya jumla ya kura asilimia hamsini (50%) ya kura zote zilizopigwa nchini, atangazwe kuwa mshindi na iwapo hapana mshindi, uchaguzi utarudiwa kati ya wagombea wawili wa kwanza. Atakayeshinda kati yao ndiye atakayetangazwa kuwa mshindi.

128. kufafanua bila kuchanganya, mamlaka ya Rais na hali inayoweza kumfanya ayaache mamlaka na utaratibu wa kutenguliwa.

129. mgombea urais amteue mtu mwenye sifa bora kuwa Naibu wake, ambapo katika harakati za uchaguzi atakuwa makamu wake.

130. ielezee kwamba kifo kinapotokea, kutenguliwa ama kujiuzulu kwa Rais, makamu wake atachukua wadhfa huo kwa muda uliosalia.

131. ielezee kwamba iwapo afisi ya Makamu wa Rais imebakia wazi, Rais atateua Makamu kati ya wabunge waliochaguliwa.

132. ielezee kwamba katika harakati za kifo cha Rais na Makamu wake, Spika wa Bunge atachukua wadhfa wa Urais.

133. ielezee kuteuliwa kwa Waziri Mkuu atakayewajibika kwa Bunge na mkuu wa Baraza la mawaziri katika serikali ya Kenya.

134. ielezee kwamba Waziri Mkuu ateuliwe kutoka chamani au vyama vya mseto vilivyo na wanachama wa muda mrefu katika bunge, na atakuwa kiongozi wa Baraza la Mawaziri.

135. Ielezee kwamba Waziri Mkuu atakuwa wa kudumu katika Bunge, lakini endapo atajiuzulu, afe ama kuachishwa kazi na Bunge baada ya kura kupigwa ya kutokuwa na imani naye.

136. ielezee kwamba manaibu wawili wa Waziri Mkuu wateuliwe ili kumsaidia katika kutekeleza majukumu yake.

137. ielezee kwamba mawaziri wasiwe zaidi ya kumi na watano na mawaziri hao wateuliwe nje ya Bunge lakini Bunge liwaidhinishe.

138. ielezee uteuzi wa mtu mwenye sifa kuwa jaji wa Mahakama kuu na Mwanasheria Mkuu awe Mshauri Mkuu wa Kisheria wa Serikali.

139. ielezee kuwepo kwa Afisi tofauti na huru za Mkurugenzi Mkuu Mwendeshaji Mashtaka ya Umma.

**Kuhusu mahakama, sheria mpya yapaswa -**

140. kubuni Afisi ya Jaji Mkuu ambaye atakuwa kiongozi na mwanachama wa Mahakama na Rais wa Mahakama ya Juu.

141. kubuni Tume Huru ya Huduma za Mahakama na kufafanua uanachama wake na majukumu hayo.

142. ibuni mfumo mpya na mahakama unaojumuisha -

    Mahakama ya Juu
    Mahakama ya Rufani
    Mahakama Kuu
    Mahakama ya Kadhi
    Mahakama Ndogo
    Mahakama Maalumu

143. ielezee kwamba Mahakama ya Juu iwe Mahakama ya kikatiba na ya mahakama ya mwisho ya rufaa kwa vyovyote vile.

144. ielezee kuhusu kubuniwa kwa mahakama maalum yanayojumuisha wazee wa mitaa ili kuamua masuala yanayohusu Ardhi sheria ya kibinafsi na katika kiwango cha mitaa.

145. Ifafanue waziwazi kiwango cha elimu inayohitajika katika uajiri na maafisa katika ngazi yoyote ya kisheria.

146. Itenge umri wa miaka 65 kuwa muda rasmi wa kustaafu wa Majaji, Makadhi au Mahakimu.

147. Kadhi Mkuu atambuliwe katika kiwango sawia na Jaji wa Mahakama Kuu.

148. Ihakikishe kwamba mara inapoanza kutumika, Majaji wote wa Mahakama Kuu, Mahakama ya Rufani na Kadhi Mkuu wanazingatia kanuni na masharti ya muda wao wa kuhudumu kama yanavyoelezewa katika hali yake ya utekelezaji.

**Kuhusu huduma ya umma, Katiba mpya -**

149. Ianzishe Tume Huru ya Utumishi wa Umma na kuelezea ni kina nani wanaofaa kuwa wanachama, wajibu wake, mamlaka na masharti ya uteuzi.

150. Ihakikishe kwamba uteuzi wote katika Utumishi wa Umma unatekelezwa na Tume hiyo na pia iwe ya kipekee inayohakikisha nidhamu ya watumishi hao.

151. Ihakikishe kwamba watumishi wote wa umma hawana budi kustaafu watimiapo umri wa miaka 65.

**Kuhusu upunguzaji na usambazaji madaraka, Katiba mpya -**

152. Ihakikishe utaratibu wa daraja nne za mamlaka katika ngazi za mikoa, wilaya, kata na vijiji.

153. Ihakikishe kwamba Nairobi liwe jiji kuu la Kenya na kuongozwa kuambatana na sheria maalum.

154. Ihakikishe kwamba sehemu nyingine za manispaa ziongezwe kwa kutambua sheria iliyobuni ngazi (nne) hizo za utawala.

155. Ihakikishe sheria ya taratibu za upunguzaji na usambazaji wa madaraka.

156. Ihakikishe kwamba punde baada ya kuanza kutumika utawala wa mikoa ufutiliwe mbali.

**Kuhusu usimamizi wa maliasili, Katiba mpya sharti -**

157. Iweke maliasili yote ikiwa ni pamoja na madini, maji, ardhi, misitu, uvuvi na sehemu chepechepe mikononi mwa Wakenya wenyewe isipokuwa pale umilikaji umo mikononi mwa watu wengine au wananchi katika sheria hii.

158. Ihakikishe kwamba serikali chini ya usimamizi wa bunge inawajibika katika kusimamia rasilmali za nchi kwa niaba ya raia.

159. Ihakikishe kwamba kumeanzishwa utaratibu mwafaka ambapo jamii mbalimbali zinapata fursa ya kushiriki katika usimamizi wa raslimali za kitaifa.

**Kuhusu mazingira Katiba mpya**

160. Ihakikishe kwamba kuna haki maalum kuhusu uhifadhi wa mazingira pamoja na kanuni za kuzingatiwa katika kutekeleza wajibu na uhifadhi wa mazingira.

161. Ihakikishe kwamba ipo sheria zinazompa kila Mkenya haki ya kuishi katika mazingira safi, kwa manufaa ya vizazi vya sasa na hata vijavyo.

162. Ihakikishe kwamba tume maalum imebuniwa kusimamia masuala yote yanayohusiana na uhifadhi wa mazingira.

**Kuhusu ardhi, Katiba mpya sharti:**

163. Ihakikishe kwamba umilikaji wa ardhi unawekwa mikononi mwa raia binafsi au jamii ya Wakenya.

164. Ihakikishe kwamba watu wasiokuwa raia wa Kenya hawaruhusiwi kumiliki ardhi hapa nchini, isipokuwa tu wanaweza kukodisha.

165. Ihakikishe kwamba ardhi imechukuliwa kuwa mali ya umma, jamii ama watu binafsi na ziwekwe kanuni za kufuatwa katika utambuzi wa umiliki wa ardhi katika viwango hivyo vitatu.

166. Ihakikishe kwamba imetoa ulinzi wa haki ya umilikaji ardhi kwa wenye ardhi wote, bila kuzingatia muda wa mapatano.

167. Ianzishe Tume ya Kitaifa ya Ardhi ili, pamoja na mengine, imiliki na isimamie ardhi ya umma.

168. Ihitaji Bunge kuanzisha utaratibu wa kuchunguza na kutwaa ardhi yote ya umma inayomilikiwa kiharamu na ichunguze utolewaji ardhi wakati wa ukoloni na hali nyingine.

169. Ihitaji serikali kuunda na kuchapisha sera ya kitaifa ya ardhi.

170. Ihakikishe usalama wa haki za ardhi kwa wamiliki ardhi wote bila kujali muda wa ukodishaji.

171. Ihitaji serikali katika viwango vyote ianzishe mfumo wa uwajibikaji na usio na gharama kubwa ya usimamizi wa ardhi.

172. Ihakikishe kwamba inaheshimu sheria ya kitamaduni katika haki za kumiliki ardhi na kupokezwa kwa haki hiyo kwa vizazi vijavyo kama sehemu ya sheria ya kibinafsi ya wananchi wa Kenya.

173. Itambue haki ya mali ya waliooana na kuwa na haki ya mali kama hayo kwa maharusi wakati na baada ya kuoana.

**Katika haki za kitaaluma, Katiba mpya lazima:**

174. Ihifadhi elimu za kimsingi na vipawa na kuviendeleza kwa kuvidhibiti.

175. Bunge lihakikishe kwamba sheria ya kuukuza utamaduni, viwanda na taaluma bunifu za kisayansi ili kuwavutia wawekaji rasilmali ambazo pia zitawafaidi waanzilishi kwa juhudi zao.

**Katika usimamizi wa fedha na mapato, Katiba mpya lazima:**

176. Ianzishe Baraza la Kushughulikia Ufufuzi wa Uchumi uliozorota na usimamizi wa hazina kuu litakalowajumuisha wataalamu katika taaluma husika na wakati huo huo kudumisha mamlaka hayo au kutekeleza jukumu hilo kama itakavyofafanuliwa katika sheria.

177. Ianzishe Kamati ya Bajeti ya Bunge ambayo itafanya kazi kwa ushirikiano na Hazina Kuu ya Serikali kuboresha mgao wa Bajeti wa Matumizi ya pesa za Serikali kwa mwaka.

178. Ihakikishe kuanzishwa kwa afisi ya Bunge kuhusu bajeti ambayo itatoa ushauri mwafaka kwa Kamati ya Bajeti kuhusu usimamizi wa kifedha na uhasibu.

179. Ihakikishe Benki Kuu ya Kenya imekuwa asasi ya kujisimamia ambayo itakuwa Hazina Kuu ya pesa za Kenya, ikiongozwa na Gavana na Msaidizi ya Gavana watakaokuwa na mamlaka ya kutekeleza majukumu yao kama itakavyoratibiwa katika sheria.

180. Izuie ongezeko la ushuru wa mara kwa mara bila idhini ya Bunge.

181. Izuie kuwepo kwa deni la umma katika Serikali ya Kenya kabla haijaidhinishwa na Bunge kwanza.

182. Ihakikishe kubuniwa kwa afisi mbili za kisheria, ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu na ya Msimamizi wa Bajeti na hatimaye kuelezea jukumu la kila mojawapo ya afisi hizo.

**Katika usimamizi wa wafanya kazi Katiba mpya lazima:**

183. Ilihimize Bunge lipitishe sheria itakayohakikisha kuwapo kwa sekta ya utumishi wa umma thabiti, yenye uadilifu na inayowajibika.

184. Iwahakikishie Wakenya kwamba elimu ya shule ya msingi itakuwa ni ya bila malipo na ya lazima.

**Katika muundomsingi wa kijamii Katiba mpya sharti:**

185. Iweke katika sheria ya haki ya kimsingi ya afya, nyumba na miundomisingi ya kuutosheleza umma.

**Katika sayansi na teknolojia, Katiba mpya sharti:**

186. Ihakikishe Kenya imebuni na kutekeleza mfumo wa Sayansi na Teknolojia ili kuuboresha mfumo wa taifa wa utafiti na uvumbuzi.

**Katika Tume na afisi za kikatiba, Katiba mpya sharti -**

187. Ibuni na kuelezea uwezo na uwajibikaji wa Tume na afisi za kikatiba kusimamiwa Kikatiba.

188. Ibainishe wazi kwamba uteuzi wa maafisa katika tume na afisi za kikatiba, upitishwe na Bunge.

189. Ianzishe Tume ya Mishahara na Marupurupu ili kubainisha kiwango cha marupurupu na masurufu kinachostahili kuliwa wahudumu katika afisi za kikatiba.

**Katika uongozi wa jamii, Katiba mpya lazima:**

190. Ibuni mfumo wa kutathmini uwajibikaji katika afisi zote za umma ikiwa ni pamoja na wale wanaozisimamia afisi zote za kikatiba.

191. Ianzishe Tume ya Maadili na Hadhi ili kusimamia kanuni za uongozi.

**Katika urithi na upokezaji mamlaka, katiba mpya sharti -**

192. Ibuni mwongozo mwafaka unaohusiana na usimamizi wa upokezanaji mamlaka kama inavyostahili punde baada ya kuanza kazi.

193. Ieleze kwamba mtu yeyote ambaye alikuwa akishikilia wadhfa wa urais zaidi ya awamu mbili chini ya Katiba ya zamani apigwe marufuku kuwania wadhifa huo chini ya Katiba hiyo.

# SEHEMU YA KWANZA

# UTANGULIZI

## SURA YA KWANZA

## MSINGI WA KENYA

### 1.1 HALI YA KIJIOGRAFIA NA KISIASA

#### 1.1.1. HALI YA NCHI KIJIOGRAFIA

*Kenya inapatikana kwenye ikweta upande wa Mashariki ya Pwani ya Afrika. Inapakana na Somalia upande wa Mashariki na Kaskazini Mashariki, Ethiopia na Sudan kwa upande wa Kaskazini, Uganda kwa upande wa Magharibi, Tanzania upande wa Kusini na Bahari ya Hindi upande wa Kusini Mashariki inachukua eneo la kilomita mraba 583,000 (maili mraba 225,000). Jiji kuu la Kenya, Nairobi, lina idadi ya watu karibu milioni mbili na nusu. Miji mingine mikuu au maarufu ni Mombasa, bandari kuu kando ya Bahari ya Hindi, jiji lenye idadi ya watu 700,000; na Kisumu, kando ya Ziwa Viktoria wenye kiasi cha idadi ya watu 450,000. Kenya imegawanywa katika mikoa minane ya utawala ambayo ni, Mkoa wa Kati, Mkoa wa Pwani, Mkoa wa Mashariki, Mkoa wa Nyanza, Mkoa wa Kaskazini Mashariki na Mkoa wa Magharibi.*

Kila mkoa umegawanywa katika wilaya. Kwa sasa nchi imegawanywa katika maeneobunge 210. Ramani inayoonyesha mipaka ya nchi kiutawala na kisiasa imechorwa humu katika Mchoro I.

#### 1.1.2. Hali ya Takwimu ya Idadi ya Watu

Idadi ya watu kwa sasa nchini Kenya ni kama milioni thelathini na moja na laki tisa (31.9) na inaongezeka kwa karibu kiasi cha asilimia 1.9 kwa mwaka. Kiwango cha wanaozaliwa kinakisiwa kuwa 34.6 kwa 1000 ambapo kiwango cha vifo ni kama 4.7 kwa 1000. Idadi halisi ya wanaohama ni watu 0.34 kwa watu 1000. Na makisio ya vifo vya watoto ni 59.07 kwa watoto 1000 wanaozaliwa karibu asilimia 44 (44%) ya idadi ya watu ni wenye umri wa miaka kati ya sufuri na kumi na mitano (0-15) ambapo asilimia 53

(53%) ya idadi ya watu wako katika umri wa miaka 15-64. Idadi ya watu wenye umri wa miaka 65 na zaidi inakisiwa kuwa milioni moja na inatarajiwa kuongezeka hadi milioni 1.3 kufikia mwaka 2008. Kwa upande wa jinsia kuna mwanamume mmoja kwa wanawake 1.2. Muda wa kuishi miongoni mwa watu ni miaka 49.3 ingawa hali hii hutofautiana kutoka mkoa mmoja hadi mwingine. Mwelekeo wa idadi ya watu tangu mwaka 1969 inaonyeshwa katika Jedwali I.

**MCHORO**

**1. MIPAKA YA KISIASA YA KENYA**

**JEDWALI 1: MWELEKEO WA TAKRIMU YA IDADI YA WATU TANGU 1969**
**(Insert see pg 23)**

## 1.2 HALI YA MALIASILI

Katika ardhi ya Kenya ni asilimia kumi na saba tu (17%) inayolimika. Asilimia mbili nukta mbili (2.2%) ya ardhi inayolimika ni ya huduma za misitu. Karibu asilimia themanini (80%) ya nchi ni kame na kame kiasi. Sehemu hizi zinahifadhi zaidi ya asilimia themanini na tano (85%) ya jumla ya idadi ya wanyamapori na karibu asilimia thelathini (30%) ya idadi ya watu wanashughulikia ufugaji wa wanyama wengi kwa kuhamahama na umiliki wa mashamba makubwa ya mifugo. Sehemu kame na kame kidogo zinaweza kuongeza jangwa na kwa sababu ya uchache wa wanaoishi huko, ongezeko lo lote dogo la idadi ya watu linaweza kusababisha utumiaji mbaya wa rasilmali. Kwa sababu ya mabadiliko ya hali ya anga mnamo miaka ya hivi majuzi, misingi ya mvua haitabiriki. Jambo hili linaweza kuwa na athari mbaya kwa taifa la Kenya, nchi inayuotegemea maliasili kwa ajili ya chakula na viwanda. Rasilmali zote za nguvu ya maji ya Kenya zinazidi mahitaji kwa mwaka. Lakini nafasi yake, wakati wake na ubora wake ni hafifu. Rasilmali ya maji safi ya Kenya ni pamoja na mito, maziwa,

ardhi chepe na visima.  Uhitaji wa ardhi ya kilimo na makao hata hivyo, umesababisha hali ya kuingilia na kupunguza sehemu za kuchotea maji, ardhi chepe, chemchemi na mikondo ya maji pamoja na uwezo wa ardhi wa kuzuia mafuriko na ukame.  Bonde la Ziwa Viktoria pekee linatumiwa na karibu nusu ya idadi ya wananchi wote.  Ingawa eneo la ardhi yenye uwezo wa kunyunyiziwa maji linakadiriwa kuwa hekta 539,500 ni karibu asilimia kumi (10%) tu inayoweza kutumika.  Isitoshe kilimo cha unyunyuzaji maji, hasa kwenye ardhi ya serikali tangu mwaka 1989 kimepungua kwa kiwango cha asilimia saba (7%) kila mwaka.

Rasilmali za pwani na za majini zikiwa ni bandari, delta na ghuba, misitu, fuo za bahari, mikoko na miamba ya matumbawe vimo hatarini.  Hasa miamba ya matumbawe iko katika tishio la kuzibwa na tope.  Rasilmali za uvuvi wakati mwingine zinatumiwa vibaya na vyombo visivyodhibitiwa na nchi.

Ingawa Kenya ina jamii za wanyama zaidi ya 35,000, mimea na wadudu, mara nyingi, imepoteza baadhi ya viumbe vyake maarufu vya maliasili zaidi kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu, uharibifu wa mazingira, upungufu wa ardhi, kuenea kwa majangwa, utumiaji mbaya wa jamii ya viumbe na kubadilisha ardhi chepe kwa ajili ya kilimo na makao. Mifumo asilia inayotunza maji, udongo au mimea ya kipekee na wanyama vimebadilishwa kwa matumizi mengine.  Baadhi ya mimea na wanyama hutumiwa kupita kiasi, na kwa hakika baadhi wametoweka.  Licha ya kuwa asilimia themanini (80%) ya eneo la ardhi inayovutia, iliyohifadhiwa kwa ajili ya wanyamapori, bado baadhi ya makao muhimu hayajahifadhiwa.  Tatizo hili limechangiwa na uhaba wa mitambo ya kuchunguza na kusawazisha uingizaji wa bidhaa, uvamizi wa jamii za kigeni na viumbe vilivyobadilishwa maumbile.

Misitu iliyohifadhiwa imeenea karibu asilimia mbili nukta tano (2.5%) ya eneo ardhi ilhali misitu yenyewe ina asilimia hamsini (50%) ya jamii ya miti nchini, asilimia arubaini (40%) ya wanyama na asilimia ishirini na tano (25%) ya ndege.  Sehemu ya ardhi inayofunikwa na misitu imepungua kwa kiasi kikubwa kutoka asilimia ishirini na nane (28%) mwaka 1993 hadi kufikia eneo la sasa kiasi cha asilimia mbili nukta tano

(2.5%). Hii inatarajiwa kupungua zaidi kufikia asilimia mbili (2%) katika mwaka 2005. Kufikia mwaka wa 2005 eneo linalofunikwa na mimea (miti) litapungua kwa kiasi cha asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani ya hekta 160,000 ya mwaka 1995 misitu ya kienyeji iliyoandikishwa kwenye gazeti rasmi la Serikali inapoteza hekta 5,000 kwa mwaka katika maeneo madogo ambapo ushindani wa matumizi ya ardhi hupunguza misitu mingine inayopatikana chini ya ardhi amana. Rasilmali za kawaida za jamii pia zinaathirika kwa haraka sana.

## 1.3. ULINGANIFU KIENEO

Katika nchi za Afrika Mashariki, Kenya ilikuwa ya mwisho kupata uhuru kutoka utawala wa kifalme wa Uingereza na Ireland ya Kaskazini, mwaka 1963. Tanzania au Tanganyika (wakati huo) na Uganda zilipata uhuru mnamo 1961 na 1962 mtawalia. Ramani inayoonyesha mipaka ya kisiasa ya nchi tatu za Afrika Mashariki iko kwenye Mchoro II hii. Kwa kuwa nchi hizi zilikuwa chini ya utawala sawa wa kikoloni, kwa zaidi ya miongo minne, zimekuwa na ushirikiano fulani hasa kifedha na kiuchumi ambao baadaye ulibadilishwa kuwa kiungo cha ushirikiano kieneo.

**MCHORO 11: Mipaka Ya Kisiasa Ya Afrika Mashariki**

Licha ya kuwa Jumuia ya Afrika Mashariki, ilivyoitwa, haikudumu kwa mwongo mmoja, ilikuwa na itabaki kuwa alama maarufu ya mshikamano ambao umestawisha mataifa matatu yashirikiane kitamaduni na kisiasa. Kuvunjika kwa jumuia ya Afrika Mashariki pengine kulichangia, kwa kiasi kidogo, maendeleo na uimarishaji wa taifa lililojitenga kisheria na kikatiba na katika kupanga au tuseme kwa mikondo mikali ya kihistoria ya iliyochukuliwa na kila nchi katika miongo minne iliyopita. Maendeleo ya kikatiba Kenya na shinikizo la mabadiliko yanayotokea nchini Uganda na Tanzania, kwa hivyo, hayawezi kueleweka vyema bila ya kuzingatia kigezo hiki cha siasa ya nchi kidunia.

**SURA Y A PILI**

**TUME YA MAREKEBISHO YA KATIBA YA KENYA**

## 2.1. UTEUZI NA UANACHAMA

Suala kuwa Katiba ya sasa ya Kenya irekebishwe au la, ama iundwe upya, limezungumziwa sana kwa zaidi ya mwongo mmoja. Baada ya miaka mingi ya majadiliano makali, pamoja na mashauriano miongoni mwa vyama vya kisiasa, vyombo vya ushirika wa raia, makundi ya kidini na washikadau wengine, mfumo wa kisheria wa Marekebisho ya Katiba hatimaye ulikubaliwa mnamo Novemba, 2000.

Tume ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya (tunayoiita Tume) baadaye iliteuliwa na kuandikwa kwenye gazeti rasmi la serikali tarehe 10, Novemba, 2000. Tume hii ilikuwa na wanachama wafuatao:

- Prof. Yash Pal Ghai - Mwanatume na Mwenyekiti
- Bi Kavetsa Adagala - Mwanatume
- Kasisi Zablon Ayonga - Mwanatume
- Bi Phoebe M. Asiyo - Mwanatume
- Bwana John M. Kangu - Mwanatume
- Bwana Ahmed I. Hassan - Mwanatume
- Askofu Bernard N. Njoroge - Mwanatume
- Dkt Githu Muigai - Mwanatume
- Prof. H.W.O. Okoth-Ogendo - Mwanatume
- Bw Domiziano M. Ratanya - Mwanatume
- Prof. Ahmed I Salim - Mwanatume
- Dkt. Mohamed Swazuri - Mwanatume
- Bw. Keriako Tobiko - Mwanatume
- Bw. Paul. M. Wambua - Mwanatume
- Bi. Alice Yano - Mwanatume
- Mkuu wa Sheria - Mwanatume

- Bw. Arthur O. Owiro - Mwanatume kwa wadhifa wake na Katibu

Katika mkutano wake wa kwanza tume ilimchagua Prof. Ahmed I. Salim kama makamu wa mwenyekiti. Hii ilifuatiwa na kuundwa kwa kamati mbili za kusudi maalum zifuatazo:

- Kamati ya Bajeti na Mikakati, na
- Kamati ya Kuandaa Miswada

Kamati hizi zilipewa jukumu la kupendekeza muundomsingi bora na bajeti kwa matumizi ya Tume. Kamati nyingine zikaanzishwa ili kufaulisha maendeleo au mafanikio ya shughuli za Tume katika maeneo mbalimbali. Shughuli za Tume ziliongozwa kupitia kamati hizi hadi hapo vyombo vingine vilipobuniwa kwenye chapisho la Tume ya Marekebisho ya Katiba (Kanuni za Jumla) 2001 (Nambari ya Kisheria, 12/2001) tarehe 23 Julai, 2001.

## 2.2 KUJADILI UTARATIBU WA PAMOJA WA MAREKEBISHO

Wakati Tume ilipoundwa uamuzi wa kurekebisha Katiba ya sasa pia ulianzishwa sambamba na mashirika ya kijamii, vikundi vya kidini pamoja na washikadau wengine wa mashirika yasiyo ya kiserikali. Kundi lililojulikana kama *Kundi la Ufungamano*, liliundwa katika misingi kuwa muundo na agizo la Tume ilivyoagizwa kisheria halikutimizwa ilivyohitajika kwani halikuwashirikisha wala kutokana na wananchi wenyewe.

Kwa hivyo kundi la Ufungamano liliteua Tume ya Watu wa Kenya na kujitolea kufanya kazi muhimu inayofanana na ile ya Tume iliyoundwa kisheria bungeni. Tume hii ilikuwa na wanachama wafuatao: *(insert list on pg. 28 of English)*

Kuwapo kwa Tume na *Kundi la Ufungamano* pekee ni ithibati ya mgawanyiko mkubwa katika siasa ya nchi ya Kenya. Ukweli kuwa Tume ilipokelewa kama chombo cha chama tawala na *Kundi la Ufungamano* kama wapinzani wake, ilikuwa ni ishara wazi ya

ukosefu wa mapatano katika heshima na kuwajibika kwa kile ambacho ni muhimu sana kisiasa katika historia ya miaka arobaini ya uhuru wa nchi yetu ya Kenya.

Kwa hivyo, Mwenyekiti wa Tume alikubali kutangaza makubaliano kati ya washikadau wanaohusika ili kufaulisha muungano wa asasi hizo mbili, zenye malengo sawa ya kurekebisha Katiba. Majadiliano zaidi yaliyoandaliwa na washikadau wote wanaohusika kati ya Novemba 2000 na Mei 2001 yalileta matokeo ya uamuzi wa kuunganisha Tume kama ilivyoundwa awali na bunge na *Kundi la Ufungamano*. Taratibu za pamoja zilikubaliwa kuwa muungano uwajibike katika kanuni zifuatazo:-

Kwamba Serikali ya Jamhuri ya Kenya, vyombo vya kurekebisha Katiba, Vyama vya Kisiasa, Mashirika yasiyo ya Serikali na Wakenya wote:-

i. Watatambua umuhimu wa kujijenga, imani na kustawisha mapatano ya kitaifa kwa minajili ya harakati za marekebisho;
ii. Watakubali kuepuka ghasia au vitisho vya ghasia au vitendo vingine vya uchochezi wakati wa harakati za marekebisho;
iii. Watakubali kutoingilia haki ya mtu ya kufanya au kuhudhuria mikutano ya hadhara au jumuiko, haki na uhuru wa mtu, uhuru wa kutoa maoni na kuwaza wakati wa harakati za marekebisho isipokuwa katika kutii sheria;
iv. Watahakikisha kuwa polisi watalinda usalama wa kila mtu anayehudhuria mikutano au mazoea mengine ya haki dhidi ya fujo kutoka kokote
v. Watahakikisha kwamba mikutano yote ya vyombo vya marekebisho itafanywa kwa amani;
vi. Wataheshimu uhuru wa Tume na wanachama wake; na
vii. Watakoma kufanya vitendo vya kisiasa au kiutawala ambavyo vitaathiri vibaya maendeleo au mafanikio kwa harakati za marekebisho.

Ili kuhakikisha uingishaji wa maktaba katika sheria, Mwanasheria Mkuu baada ya kuombwa na Tume Teule ya Bunge ya Marekebisho ya Katiba na Baraza tekelezi la *Kundi la Ufungamano* aliunda kamati ya mswada yenye wanakamati wafuatao:

- Prof. H.W.O Okoth-Ogendo
- Dkt. Oki Ooko-Ombaka
- Bw. J. Mutakha Kangu; na
- Bi. Abida Ali-Aaroni

Kamati hii ilitoa mswada wa kurasmisha muunganohuu. Baada ya kuidhinishwa Mei 2001, Sheria ya Tume ya Kenya ya Marekebisho ya Katiba ilirekebishwa katika Kifungo cha Sheria (Na. 2/2001) ili kuipanga upya Tume na kupanua idadi ya wanachama kutoka kumi na saba hadi ishirini na tisa (17-19). Wanatume kumi na mmoja wapya waliotangazwa kwenye gazeti rasmi la serikali tarehe 11 Juni, 2001 ni:-

- Bw.Abubakar Zein Abubakar
- Bi. Abida Ali – Aroni
- Dkt. Charles M. Bagwasi
- Bi. Nancy M. Baraza
- Dkt. Wanjiku M. Kabira Dkt.
- Mosonik arap Korir
- Bw. Isaac Lenaola
- Bw. Ibrahim A. Lethome
- Bi. Salome W. Muigai
- Dkt. Abdirizak A. Nunow
- Dkt. Oki Ooko-Ombaka
- Bw. Riunga L. Raiji

Sheria pia ilibuni afisi mbili zaidi za naibu mwenyekiti, ambapo mmoja angeitwa Naibu wa Kwanza wa Mwenyekiti na afisi nyingine ingechukuliwa na Kamishina mwanamke.

Katika mkutano wa kwanza, Tume iliyopangwa upya ilimchagua Dkt. Oki Ooko – Ombaka kuwa Naibu wa Kwanza wa Mwenyekiti na Bi Abida Ali – Aroni kuwa Naibu Mwenyekiti wa Wanawake. Ili kufaulisha, shughuli Tume mpya, hali kadhalika, ilibuni kamati za kudumu kama ziafuatazo:-

(a) Kamati Elekezi
(b) Kamati ya Elimu, Mawasiliano, Utangazaji na Habari
(c) Kamati ya Utafiti, Kuandika na Msaada wa Kiufundi
(d) Kamati ya Maendeleo ya Rasilimali na Bajeti
(e) Kamati Jumuishi na Nyangaji

(see pg. 31)

Kanuni za jumla za kuongoza kazi za Tume pia ziliandikwa kwenye gazeti rasmi la serikali tarehe 23 Julai, 2001.

Kati ya Juni 2001 na Septemba 2002 mabadiliko mawili muhimu yalitokea katika uanachama wa Tume mpya. Kwanza ni kujiuzulu kwa Bw Arthur O. Owiro kama katibu wa Tume na wadhifa huo kuchukuliwa na P. L.O. Lumumba. Pili ni kifo cha ghafla cha Naibu wa Kwanza wa mwenyekiti Dkt Oki Ooko – Ombaka tarehe 15 Julai, 2002. Nafasi hiyo wazi ya Mwanatume ilijazwa na Dkt.Androniko O. Adede ambaye aliteuliwa na kuandikwa katika gazeti rasmi la Serikali mnamo tarehe 16 Agosti, 2002.

Katika uwasilishaji wa Ripoti hii, wanatume kamili ni wafuatao:-

- Prof. Yash Pal Ghai - Mwanatume na Mwenyekiti
- Prof. Ahmed I. Salim - Mwanatume na Naibu Mwenyekiti
- Prof. H.W.O. Okoth-Ogendo - Mwanatume na Naibu Mwenyekiti
- Bi Abida Ali – Aroni - Mwanatume na Naibu Mwenyekiti
- Dkt. Abdirizak Arale Nunow - Mwanatume
- Bw. Abubakar Zein Abubakar - Mwanatume
- Dkt. Andronico O. Adede - Mwanatume
- Bw. Ahmed Isaac Hassan - Mwanatume
- Bi. Alice Yano - Mwanatume
- Askofu Bernard N. Kariuki - Mwanatume
- Dkt Charles M. Bagwasi - Mwanatume

| | | |
|---|---|---|
| ▪ Bw. Domiziano M. Ratanya | - | Mwanatume |
| ▪ Dkt. Githu Muigai | - | Mwanatume |
| ▪ Bw. Ibrahim Lethome | - | Mwanatume |
| ▪ Bw. Isaac Lenaola | - | Mwanatume |
| ▪ Dkt. Mosonik arap Korir | - | Mwanatume |
| ▪ Bi. Kavetsa Adagala | - | Mwanatume |
| ▪ Bw. Keriako Tobiko | - | Mwanatume |
| ▪ Dkt. Mohamed A. Swazuri | - | Mwanatume |
| ▪ Bw. Mutakha Kangu | - | Mwanatume |
| ▪ Bi. Nancy M. Baraza | - | Mwanatume |
| ▪ Kasisi Zablon Ayonga | - | Mwanatume |
| ▪ Bw. Musili P. Wambua | - | Mwanatume |
| ▪ Bi Phoebe M. Asiyo | - | Mwanatume |
| ▪ Bw. Riunga L. Raiji | - | Mwanatume |
| ▪ Bi. Salome W. Muigai | - | Mwanatume |
| ▪ Mwanasheria Mkuu | - | Mwanatume kwa mujibu wa wadhifa wake |
| ▪ Patrick L.O. Lumumba | - | Katibu na Mwanatume kwa mujibu wa wadhifa wake |

## 2:3 Agizo la Tume

Toleo lililoimarishwa la Sheria ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya (Sura ya 3A, Sheria za Kenya) limefafanua wazi Agizo la Tume na vyombo vingine vya Marekebisho. Agizo muhimu zaidi la Tume ni kuhakikisha kuwepo kwa Marekebisho kamili ya Katiba iliyoko "na wananchi wa Kenya". Hasa, sheria inaagiza kuwa nia na malengo ya kurekebisha Katiba ni kuhakikisha kuweko kwa masharti katika:

a) kudumisha amani, umoja wa taifa na hadhi ya Jamhuri ya Kenya, ili kulinda maslahi ya watu wa Kenya;
b) kuanzisha mfumo huru na wa kidemokrasia wa serikali unaojumuisha utawala mwema, ukatiba, uongozi kwa mujibu wa sheria, haki za binadamu na usawa wa kijinsia;
c) kutambua na kugawa majukumu miongoni mwa vyombo mbalimbali vya serikali pamoja na mamlaka ya nchi, bunge, na mahakama ili kuunda vipimo na visawazishi baina yake na kuhakikisha uwajibikaji wa serikali na maafisa kwa wananchi wa Kenya;
d) kuendeleza kushiriki kwa wananchi katika utawala wa taifa kupitia uchaguzi huru, wa haki na wa kidemokrasia na kupunguza na kusambaza mamlaka na utekelezaji wa madaraka;
e) kuheshimu kuwepo kwa makabila mengi, maeneo mengi na haki za wanajamii, pamoja na kupanga na kushiriki katika shughuli za utamaduni na namna ya kujitambulisha;
f) kuhakikisha utoaji wa mahitaji ya kimsingi kwa Wakenya wote kupitia kuanzishwa kwa utaratibu wa usawa wa maendeleo ya kiuchumi na ufikiaji wenye usawa wa rasilmali za taifa;
g) kuendeleza na kuwezesha ushirikiano wa kieneo na kimataifa ili kuhakikisha maendeleo ya kiuchumi, amani na utulivu na kuunga mkono demokrasia na haki za binadamu;
h) kuimarisha umoja na utangamano wa taifa;
i) kuandaa mazingira mwafaka ya kubadilishana mawazo;

j) Kuhakikisha kushiriki kikamilifu kwa wananchi katika usimamizi wa shughuli za umma; na
k) kuwawezesha Wakenya kusuluhisha masuala ya taifa kwa masikilizano.

Katika utekelezaji wa majukumu kwa mujibu wa Sheria, Tume na vyombo vingine vyote vya marekebisho havina budi, pamoja na mengine:

a) kuwajibika kwa wananchi wa Kenya;
b) kuhakikisha kwamba utaratibu wa marekebisho unazingatia kuwepo kwa Wakenya wa aina mbalimbali – pamoja na hali ya kijamii na kiuchumi, rangi, kabila, jinsia, imani ya kidini, umri, kazi, elimu, walemavu na wasiobahatika;
c) kuhakikisha kwamba utaratibu wa marekebisho:
    i. unawapa wananchi wa Kenya fursa ya kushiriki ipasavyo, na kwa njia huru na yenye maana, katika kutoa na kujadili mapendekezo ya kubadilisha Katiba;
    ii. unaendeshwa wazi, kwa mujibu wa sheria hii, na
    iii. unaongozwa na heshima kwa kanuni za ulimwengu za haki za binadamu, usawa wa jinsia na demokrasia;
d) Kuhakikisha kwamba matokeo ya mwisho ya utaratibu wa marekebisho yanaonyesha bayana matumaini ya wananchi wa Kenya.

Hasa, Tume inalazimika kuhakikisha kuwa katika kurekebisha Katiba, wananchi wa Kenya:

(a) wanachunguza na kupendekeza kuundwa kwa vyombo vya serikali na majukumu yake pamoja na mamlaka na utendakazi wake, ili kutumia vyema vipimo na visawazishi vyao na kuhakikisha uhuru;
(b) wanachunguza miundo na mifumo mbalimbali ya serikali, pamoja na mfumo wa serikali ya shirikisho na wa serikali ya umoja, na kupendekeza mfumo unaofaa kwa taifa la Kenya;
(c) wanachunguza na kupendekeza uboreshaji wa Tume za kikatiba, asasi na afisi zilizoko, na uanzishaji wa nyingine, ili kufaulisha utawala wa kikatiba

na heshima kwa haki za binadamu na usawa wa jinsia nchini Kenya, kama sehemu muhimu na isiyotengeka ya mazingira ya maendeleo kiuchumi, kijamii, kidini, kisiasa na kitamaduni;

(d) wanachunguza na kupendekeza uboreshaji wa mfumo wa kupiga kura nchini Kenya;

(e) bila kuathiri aya (i), kuchunguza na kutoa mapendekezo kuhusu mahakama kwa jumla na hasa kuanzisha mahakama na upeo wake, ili kuweka hatua zinazofaa za kuhakikisha kuaminika, kuwajibika, ufanisi, nidhamu na uhuru wa mahakama;

(f) wanachunguza na kurekebisha nafasi ya serikali ya wilaya katika utaratibu wa Katiba ya Jamhuri ya Kenya na kiwango cha kupunguza na kusambaza madaraka kwa serikali za wilaya;

(g) wanachunguza na kurekebisha nafasi ya umilikaji wa mali na haki za ardhi ikiwemo ardhi ya mtu binafsi, ardhi ya serikali, na ardhi amana katika utaratibu wa Katiba na sheria ya Kenya na kupendekeza uboreshaji utakaohakikisha kufurahia kabisa haki za ardhi na haki ya mali nyinginezo;

(h) wanachunguza na kurekebisha usimamizi na matumizi ya fedha za umma na kupendekeza uboreshaji wake;

(i) wanachunguza na kurekebisha haki ya uraia na kupendekeza uboreshaji ambao hasa utahakikisha usawa wa jinsia katika kupata haki hii;

(j) wanachunguza na kurekebisha vizuizi vya kijamii na kitamaduni vinavyoendeleza aina mbalimbali za ubaguzi na kupendekeza uboreshaji ili watu wote wapate haki sawa;

(k) wanachunguza na kurekebisha haki za watoto na kupendekeza taratibu za kuzilinda;

(l) wanachunguza na kurekebisha upokezanaji wa afisi na kupendekeza mfumo unaofaa wa kupokezana madaraka kwa njia iliyo shwari na yenye hadhi baada ya uchaguzi au vinginevyo;

(m) wanachunguza na kupendekeza madaraka ya jamhuri ya kuweka na kutekeleza mikataba na mambo mengine yoyote, ili kuimarisha utawala

mwema na utekelezaji wa wajibu wa Kenya kwa mujibu wa sheria ya mataifa;

(n) wanachunguza na kutoa mapendekezo kuhusu kanuni elekezi za sera ya taifa.

(o) kuanzisha na kuimarisha kanuni ya uwajibikaji kwa umma miongoni mwa afisi za umma na siasa;

(p) wanachunguza na kutoa mapendekezo kuhusu jambo lolote linalohusiana au linalogusia haya yaliyotangulia na linalofaulisha lengo la utaratibu wa marekebisho ya Katiba.

Maelezo ya kina na uchanganuzi wa agizo hili yanapatikana katika Sura ya Nne ya taarifa hii.

## 2.4 Utaratibu wa Tume wa Kufanya Kazi

Kanuni pana zinazoelekeza utaratibu wa Tume wa kufanya kazi zimefafanuliwa katika Kifungu cha 17 cha Sheria kinachoiagiza Tume:

(a) kutekeleza na kufaulisha elimu ya uraia ili kuchochea mjadala miongoni mwa wananchi na ufahamu wa masuala ya kikatiba;

(b) kukusanya na kuweka pamoja maoni ya Wakenya kuhusu mapendekezo ya kubadilisha Katiba na, katika misingi hiyo, kuandaa mswada wa kubadilisha Katiba utakaowasilishwa bungeni;.

(c) kuendeleza masomo, utafiti na tathmini kuhusu Katiba na Katiba nyinginezo na mifumo ya kikatiba, vitu ambavyo kwa maoni ya Tume vinaweza kuielekeza Tume na Wakenya kuhusu hali ya Katiba ya Kenya.

Sehemu ya 18 pia inaiagiza Tume:

(a) kutembelea kila eneobunge nchini Kenya ili kupokea maoni ya wananchi kuhusu Katiba;

(b) bila kizuizi au pingamizi, kupokea memoranda, kuandaa vikao vya umma na vya watu binafsi kote nchini Kenya na, kwa njia nyingine yoyote, kukusanya na kuweka pamoja maoni ya Wakenya walioko nchini au nje ya Kenya, na

kwa nia hii Tume inaweza kuitisha mikutano ya umma ya wenyeji wa eneo lolote ili kujadili suala lolote, linalohusiana na shughuli ya Tume;

(c) kumwita afisa yeyote wa umma ili ahojiwe faraghani au mbele ya kamati au atoe waraka au kitu au habari zinazoonekana kuhusiana na shughuli ya Tume.

Kufuatana na kanuni hizi na ili kuhakikisha utekelezaji kamili wa agizo, Tume ilitumia wakati na rasilmali nyingi kuandaa miundomsingi imara ya kitaifa ili kuhamasisha, kujadili na kukusanya maoni ya umma.

Hii ni pamoja na Vituo vya Nyaraka katika wilaya zote za utawala, utaratibu wa kuratibu wilayani, Kamati za Vikao katika maeneobunge 210 ya Kenya, na elimu ya uraia na mipango ya nyanjani kupitia vyombo vya habari. Ukusanyaji wa maoni ulitekelezwa na Wanatume katika utaratibu wa wanajopo watatu watatu, waliotembelea maeneobunge ya mikoa yote nchini.

Maelezo yenye kina kuhusu utaratibu wa Tume wa kufanya kazi pamoja na njia za kuchanganua data, mpango wa kuandika ripoti na kutayarisha mswada, mjadala kuhusu ripoti na mswada wa sheria katika Kongamano la Taifa la Katiba, na kuwasilishwa kwake bungeni, yametolewa katika Juzuu ya Tatu ya taarifa hii.

# SEHEMU YA PILI

# MAENDELEO NA MAREKEBISHO YA KATIBA

# SURA YA TATU

## MAENDELEO YA KIKATIBA NCHINI KENYA

## 3.1 AWAMU KABLA YA UHURU

## 3.2 KATIBA YA UHURU

### 3.2.1 Mambo muhimu

Asili ya Katiba iliyopo inategemea pakubwa vyombo vya uhuru uliopatikana Disemba 12,1963. Kutoka wakati huo Katiba imebadilishwa mara 38. Kimsingi, maadili na maelekezo ya Katiba iliyopo yanatofautiana na yale ya Katiba ya Uhuru licha ya maendeleo ya kisheria. Katiba ya Uhuru ilikuwa ni matokeo ya majadiliano makali ya vyama vya kisiasa vya humu nchini na serikali ya Uingereza. Katiba hiyo iliangazia mahitaji ya vyama mbali mbali na jinsi amabvyo mahitaji hayo yalivyogawanywa na kusawazishwa.

Wakenya, hasa wa Kiafrika, walikuwa na umoja wakati wa kupigania Uhuru. Lakini wakati Uingereza ilipokubali kanuni za Uhuru katika kongomano jijini London mwaka wa 1960 na majadiliano kuhusu Katiba ya nchi huru ya Kenya kuanza, tofauti zilijitokeza.

Kufikia miaka ya 1960, tofauti kubwa za maendeleo kikatiba zilidhihirika katika makundi ya jamii za rangi tofauti. Mipango ya Katiba wakati huo ilikuwa katika msingi wa wapiga kura wa kijamii na viti kwa kutimiza matakwa ya Wazungu, Wahindi na Waafrika.
Ilipodhihirika kwamba Kenya itapata uhuru, siasa za msingi wa rangi zilikosa muelekeo kufuatia mgawanyiko wa baadhi ya wanasiasa wa Kiafrika waliokuwa na kiu cha uongozi.

Ijapokuwa baadhi ya Wazungu walipigana vita vya pembeni, Wazungu na Wahindi wengi walijishughulisha na kulinda maslahi yao, badala ya kupigania uongozi wa kisiasa.

Katika sehemu nyingi, Wazungu walizingatia kanuni za kuwalipa wakulima fidia Wazungu na wafanyikazi wa umma waliotaka kuihama Kenya, pamioja na usalama wa wale ambao wangetaka kuzidi kuishi humu nchini.

Wahindi nao walikuwa na lengo hilo la kulinda maslahi yao; lakini kwa kuwa hawakuwa watu wa kuhama kuhama, dhamira yao kuu ilikuwa ni kuzingatia haki zao za kuishi na kufanya kazi humu nchini chini ya masharti yanayowafaa.

Migawanyiko ya Waafrika ilitokana na vikwazo na kuzuiwa vya kuanzisha vyama vya kisiasa kote nchini. Msingi wa vyama ulipatikana katika wilaya na viliegemea katika imani za kikabila. Mawazo ya kikabila pia yaliamshwa zaidi, na sera za kikoloni zilizotumia kabila kama kiungo cha utawala na pia kuwazuia Waafrika kutembea na kuwasiliana.

Baada ya vikwazo dhidi ya vyama vya kisiasa kuondolewa, viongozi wa Kiafrika walifanya juhudi za kuunda chama cha kisiasa cha Kitaifa. Wakati majadiliano kuhusu katiba yalipochacha, tayari kulikuwa na vyama viwili vikuu vya kisiasa: Kenyan African National Union (KANU), ambacho kimsingi kiliungwa mkono na Wakikuyu na Waluo (walioonekana kuwa makabila makubwa) – kingine kilikuwa Kenya African Democratic Union (KADU) kilichotokana na kuungana kwa vyama vingine vilivyowakilisha "makabila madogo madogo": Muungano wa Kisiasa wa Wakalenjin (Kalenjin Political Alliance); Muungano wa Wamaasai (The Maasai United Front); Umoja wa Watu wa Pwani; (the Coast People's Union); Umoja wa Kisiasa wa Waluhia; (Baluhia Political Union) na Baraza la Kitaifa la Wasomali (The Somali National Assembly).

Makabila madogo madogo yaliogopa kutawaliwa na makabila makubwa ambayo yaliungwa mkono na KANU. Hata hivyo, kwenye mkutano wa katiba jijini London, matarajio yao yalilenga kuwako kwa haki za walio wachache, lakini Waarabu wa Pwani na Wasomali kutoka Kaskazini Mashariki walitaka kujitenga. Hata hivyo, malalamiko hayo ya waliotaka kujitenga, na madai ya Waamasai kwamba maeneo yao yabakie chini ya utawala wa Waingereza yalikataliwa na Waafrika pamoja na Waingereza. Hata hivyo,

baada ya kushinikizwa na serikali ya Waingereza, KANU ilikubali baadhi ya masharti ya kuwalinda walio wachache. Katika mkutano wa 1960, wajumbe walikubaliana kwamba Kenya ingekuwa taifa linalofuata utaratibu wa bunge la kidemokrasia. Baadaye madhumuni au kanuni hizo mbili za Katiba ya Uhuru zilikuwa demokrasia ya Bunge na mgawanyo wa madaraka kama chombo cha kuwalinda walio wachache.

***(a) Demokrasia ya bunge***

Utaratibu wa Demokrasia ya Bunge kama ilivyokubaliwa katika enzi za uhuru ulilinganishwa na kanuni za mfumo wa Waingereza ambao Rais na Mkuu wa Serikali. Rais ambaye anaweza kutoka katika ukoo wa kifalme, Gavana Mkuu ama Rais mstahiwa ingawa anatekeleza wajibu muhimu katika kuunda na kuvunja na pia kulivunja bunge. Yeye ndiye anayemteua kiongozi wa Serikali anayeitwa Waziri Mkuu, ingawa ana uwezo mdogo iwapo chama ama muungano wa vyama una wabunge wengi bungeni.

Mara nyingi Mkuu wa Serikali huunga mkono maelekezo ya Waziri Mkuu. Wanachama wa mamlaka ya nchi, Waziri Mkuu na baraza la mawaziri huteuliwa kutoka miongoni mwa wabunge walio na uwakilishi mwingi. Licha ya kuteuliwa, huendelea kuwa wabunge.

Ijapokuwa Waziri Mkuu ndiye kiongozi wa Baraza la Mawaziri na huwachagua mawaziri hao na pia ana uwezo wa kuwatimua Mawaziri, wanachama wake na madaraka ya serikali yamo mikononi mwa baraza la mawaziri. Kwa njia hii, madaraka hayo hutekelezwa na baraza zima la mawaziri wala si na mtu mmoja.

Mamlaka ya nchi inawajibika kwa bunge, kumaanisha kwamba ni lazima ifafanue na kutetea sera zake bungeni, ijibu maswali kuhusu tabia yake, na kutafuta uungwaji mkono katika mipango yake bungeni. Njia moja muhimu ya kuhakikisha kwamba mamlaka hayo yanawajibika kwa bunge ni kupitia kura ya kutokuwa na imani.

Kama kura hiyo itapitishwa basi, Serikali inahitajika kujiuzulu au kumwomba mkuu wa serikali kulivunja bunge.  ama kutoka mamlakani na Rais aombwe kuvunja bunge.

Mwanzoni uhusiano uliendelea na mfalme wa Uingereza. Malkia wa Uingereza aliedelea kuwa mtawala wa Kenya na aliwakilishwa na Gavana Mkuu. Gavana Mkuu alipewa uwezo kamili wa kuhakikisha kwamba Serikali inawajibika bungeni ili kudhibiti utulivu na kuendelea kwa utawala wa usimamizi bora. Haya yalihusisha uwezo wa :

- Kumwondoa Waziri Mkuu ikiwa hajajiuzulu ama kuomba bunge livunjwe, siku tatu baada ya kura ya kutokuwa na imani.
- Kulikataa ombi la Waziri Mkuu la kuvunjwa kwa bunge baada ya kura ya kutokuwa na imani au wakati mwingine wo wote ikiwa Gavana Mkuu atakapoonelea Serikali iendelee bila kuvunjwa endapo kuvunjwa huko si kwa manufaa ya wananchi.

Bunge lilikuwa na Kumbi mbili : Ukumbi wa wawakilishi, ambao uliwakilisha maeneobunge ya kitaifa; na Ukumbi wa Seneti uliowakilisha maeneo (kama mikoa iliyoitwa). Kutokana na hofu ya walio wengi kushika hatamu, Bunge la Kenya na mamlaka ya nchi vilikabiliwa na masharti yasiyo ya kawaida katika mfumo wa bunge.

Bunge lilitarajiwa kusimamia Mamlaka ya Nchi, kwa njia nyingi.. Ukumbi wa Seneti ndio uliowasilisha matakwa tofauti tofauti kutoka kwa Ukumbi wa wawakilishi.. Na Maseneta walikuwa na usalama wa kazi kwa awamu ya miaka sita. Kwa mujibu wa uundaji sheria, Seneti hiyo ilikuwa na vipimo vya majukumu. Kwa maana kwamba, haja ya kutenga muafaka katika sehemu zote mbili za bunge kwa miswada ilikuwa wazi, kwani sheria zisingaliharakishwa bungeni.

Seneti ilipewa jukumu la kulinda utaratibu wa ushirikiano, ambapo palikuwa na vikwazo vingi kupitia uwezo wa Serikali Kuu. Katika ulinzi wa kawaida wa uchaguzi wa uhuru na haki, Mahakama huru, huduma ya umma isiyobagua ilitambuliwa na kuasisiwa kwa upeo wa juu.

Kwa mfano, ijapokuwa hapakuwa na masharti ya moja kwa moja kuhusu mfumo wa vyama vingi, hali hii ilikuwa ya uhakika hata kulingana na mswada wa haki ambao ulilinda uhuru wa kujieleza na kushirikiana. Hata hivyo, haki ya kutaka kupigiwa kura bila ya kuzingatia mshawasha wa kivyama na haki ya kupiga kura ilizingatiwa. Shughuli za uchaguzi ziliachiwa Tume ya Uchaguzi ya kibinafsi iliyokuwa na uwezo wa kuweka mipaka ya maeneobunge na kusimamia usajili wa wapiga kura.

Uhuru wa mahakama ulilindwa na Tume ya Kibinafsi ya Huduma za Mahakama iliyoweza kuwateua Majaji ambao wasingetimuliwa ila kwa utendakazi duni ama kutokuwa na uwezo wa kutekeleza kanuni za wajibu wao kama walivyoagizwa na kamati ya Majaji wa Jumuiya ya Madola. Tume ya Kibinafsi ya Huduma za Umma iliundwa ili kulinda huduma za umma bila ya kupendelea upande wo wote. Tume hiyo ilikuwa na uwezo wa kuteua, kutia adabu na kuwatimua wahudumu wote, ila tu wahudumu wachache maalum wa umma. Uhuru wa polisi ulipewa usalama kupitia mchanganyiko wa kazi zilizokuwa zimegubikwa katika Tume ya Huduma huru na Tume ya Kibinafsi ya Huduma za Polisi. Masharti maalum yaliwekwa ili kulinda shughuli za kujitawala kwa Inspekta Mkuu wa Polisi na kuondoa misimamo ya kisiasa katika utekelezaji wa masharti hayo. Afisi muhimu kama ya Mwanasheria Mkuu, Msimamizi na Mkaguzi wa Fedha za Serikali au Mhasibu Mkuu zilipewa hadhi ya uhuru wa Kikatiba.

Hatimaye, mswada wa haki ulilinda watu wengi katika haki za uraia na kisiasa; na Uhuru kama ule wa kutobaguana na kujiepusha na utesaji; uhuru wa kuwaza na dini, kutoa maoni na uhuru wa kutembea popote. Hata hivyo, haki hizo ziliambatana na vizuizi ama kuahirishwa iwapo kuna dharura. Katika hali ya mkoa wa Kaskazini Mashariki, Katiba ilimpa uwezo Gavana Mkuu kuimarisha, kupitisha, kutenga au kuahirisha masharti ya mswada wa haki ama sheria nyingine yoyote, aliyoiona yenye umuhimu, na kusimamia sehemu fulani kwa agizo la kisheria.

### *(b) Kupunguza na Kusambaza Madaraka*

#### *(i) Mfumo wa Majimbo*

Waingereza walichukulia kwamba Sheria ya Haki iliwahakikishia raia wote usawa wa haki na ingetosha kuwalinda walio wachache. Walio wachache, waliohimizwa na kuunganishwa na Wazungu, walipigania zaidi uwezo wa taifa ambao walidhania kwamba ungewafaa hasa kwa kugawanywa kwa madaraka hadi mikoani.

Walinufaika kwa jitihada zao ambazo matokeo yake yalikuwa ni mfumo wa kikatiba wa *"majimbo"*, ambao kila eneo katika maeneo saba lilipata bunge na mamlaka yake; kupitia hakikisho fulani la uwezo na mapato. Seneti iliundwa ili kulinda maslahi na uwezo mikoani, hasa kwa kulinda masharti ya kikatiba kuhusu *Majimbo* ili yasibadilishwe.

Kila eneo lilikuwa na bunge lake, lenye wanachama maalum na wale waliochaguliwa. Kufaulu kwa wapigakura kulifanywa ili kuhakikisha kwamba waliokuwa na misingi ama shughuli halali katika eneo hili ndio wapige kura, na wala hakuna mgombeaji wa uchaguzi ambaye angeweza kuteuliwa kihalali, kama hajajiandikisha katika eneo hilo kama mpigaji kura. Mipaka ya maeneo yale isingaliweza kubadilishwa na mamlaka ya nchi pekee. Hii ingefanyika tu kupitia kwenye mfumo wa taratibu nyeti zilizohusisha masikilizano na makubaliano baina ya wahusika walio kwenye eneo linalobadilishwa.

Mamlaka kuu ya eneo ilikabidhiwa Kamati ya Fedha na Maendeleo ya Bunge, iliyosimamiwa na Afisa Mkuu Mtendaji. Maeneo pia yalikuwa na huduma zao za umma na vikosi vya polisi vinavyosimamiwa kwa pamoja na serikali kuu, pamoja na Afisa mkuu mtendaji. Maeneo pia yalikuwa na huduma zao za umma na vikosi vya polisi vilisimamiwa kwa pamoja na serikali kuu na Inspekta Mkuu. Maeneo yalikuwa na uwezo wake yenyewe, wakati mwingine ukigawanywa kati ya maeneo hayo na serikali kuu. Maeneo hayo yalihakikishiwa kupewa fedha kutoka katika mapato ya taifa na yalipewa uwezo mdogo wa kuchangisha pesa kwa njia ya utozaji kodi. Hata hivyo, ukilinganishwa uwezo huo muundomsingi wa taasisi, katika maeneo, inadhihirika wazi kwamba haukuwa na umuhimu wowote. Uwezo ambao maeneo hayo yalipewa ndio uliokuwa na umuhimu mkubwa, na ungekuwa chimbuko la mamlaka makuu kwa maeneo hayo, ikiwa serikali kuu ya nchi ilihitaji kusaidia kuendeleza serikali ya kimaeneo.

Mabaraza ya kimaeneo yalikuwa na utendakazi bora kuliko mamlaka ya kiwilaya, na yaliongoza katika kazi yake na kujisimamia katika masuala yake ya kijumla.
Katiba ilihakikisha utaratibu wa Serikali za Kiwilaya pamoja na muundo wake wa kimsingi. Iliwapa uwezo wa kutosha kuhusu ardhi, hasa Ardhi Amana.

Ijapokuwa uwezo kamili wa kimaeneo ulikuwa na masharti fulani na mamlaka kuu ilikuwa na uwezo wa kuingilia kati shughuli za maeneo na uwezo wa serikali kuongoza baadhi ya shughuli hizo, mfumo wa serikali ya majimbo uliihitaji serikali kuu kushauriana na, pia wakati mwingine, kupata idhini ya mamlaka ya kieneo kabla ya kutoa uamuzi fulani (kwa mfano kuhusu ardhi, mahakama na polisi).

Uamuzi kuhusu masuala fulani ulihitaji watu wengi zaidi ili kwamba anayeamua angehamasisha uungwaji mkono wa kutosha wa sera zake. Utaratibu huu ungefanikisha kufanywa kwa uamuzi wa pamoja na kupunguza uholela.

***(ii) Mfumo wa Uchaguzi***

Katika ngazi za kitaifa na kimaeneo, wanachama wa bunge walichaguliwa kulingana na utaratibu wa mwanachama mmoja kutoka kila eneobunge. Mtindo wa upigaji kura haukuelezwa vyema kwenye Katiba, lakini bunge lilipitisha kwamba yeyote ambaye atafaulu kwa wingi wa kura basi bila shaka atakuwa mshindi hata kama idadi kubwa haikuwa ya walio wengi (kumaanisha zaidi ya asilimia 50% ya wapiga kura).

Kihistoria, mfumo huu wa kupiga kura unaofahamika kama “Aliyefika Mbele Ndiye Mshindi” hauwawakilishi walio wachache. Hata hivyo hapa nchini Kenya ambako jamii nyingi huishi katika maeneo tofauti ya kijiografia, mfumo huu haungehakikisha kuwakilishwa kwa jamii ndogo zinazoishi na jamii kubwa kutoka maeneobunge sawa. Pia hautawakilisha wachache walioishi katika maeneo ya miji yenye makabila mengi. Hali kama hiyo hutumika pia kuwakilisha makundi mengine, kama vile wanawake na walemavu. Hata hivyo, inaonekana kwamba kuna ushahidi mdogo kuwa mitindo mingine ya uchaguzi au kupiga kura ilihitajika ama kujadiliwa.

### *(iii) Utaratibu wa Marekebisho*

Mipango changamano ya Katiba ya Uhuru ilikuwa kwa kiasi, na utata. Katiba ilihakikisha kuwa haikuwa rahisi kubadilishwa ama kuondolewa.

Kwa madhumuni ya marekebisho, masharti ya Katiba yaligawanywa katika vitengo viwili : Masharti ya kawaida na masharti yaliyokita zaidi.

Kura ya kusawazisha ya robo tatu ya wanachama katika kila kitengo bungeni ndiyo iliyorekebisha masharti ya kawaida. Masharti ya kawaida yalirekebishwa kwa kura sawazishi za kiasi cha thuluthi tatu za wanachama wa kila ukumbi wa bunge. Kama mswada utakosa kuungwa mkono, unapelekwa kwa wapiga kura wote waliosajiliwa. Ikiwa sheria haikupata kiwango cha kuungwa mkono, basi inarudishwa kwenye mkutano wa kura ya maoni, wa wapigaji kura wote waliosajiliwa; ikiwa umeungwa mkono na thuluthi tatu ya wote waliopiga kura, basi inaweza kurudishwa Bungeni tena na kufanywa sheria na idadi kubwa ya watu waliopo, kwa kura ya kila ukumbi.

Masharti hayo yaliyojikita zaidi yanaweza kurekebishwa kwa kura ya kiasi cha robo tatu ya wanachama wote wa ukumbi wawakilishi ama Maseneta. Masharti haya yaliyohusisha sura juu ya uraia, haki za kimsingi na, mahakama yalishughulika zaidi na *Majimbo* na Seneti.

Ijapokuwa taratibu zote zilikuwa nyeti, kwa kiasi kikubwa, utendakazi ulionyesha wazi kwamba ni rahisi kurekebisha Katiba. Hii ni kwa sababu ya kuwa punde tu baada ya Uhuru KADU iliungana na KANU, na kwa njia zote za utenda kazi, bunge lilikuwa na chama kimoja cha kisheria.

Kufikia mwaka wa 1965, Serikali iliungwa mkono kwa kiasi kilichofaa kuwawezesha kurekebisha utaratibu wenyewe wa marekebisho ili nyakati zijazo, kura ya thuluthi mbili, ya wanachama wote itosheleze masharti ya katiba, hivyo kuondoa tofauti zilizopo baina ya masharti ya kawaida na masharti yalijikita.

### 3.2.2 Tathmini ya Jumla ya Katiba ya Uhuru

Kimsingi Katiba ya Uhuru ilikuwa na kasoro katika baadhi ya mambo ndani yake. Kwanza, Katiba hiyo haikurejelea jitihada za wananchi za kupigania Uhuru, wala kuweka wazi maadili, nia na matamanio ya kitaifa, ama kanuni kwa kutekeleza uwezo wa serikali na vyombo vyake.

Pili, ijapokuwa Katiba ilihusisha maadili muhimu, mengi yalifutwa na mtindo wa uandishi, mtindo huu ulifanya katiba isieleweke na Wakenya wengi, hata mawakili!

Tatu, ijapokuwa Katiba ilitoa mfumo wa kidemokrasia, palikuwa na upungufu katika kutenganisha mamlaka na hali ya kutosheleza ya kuwahusisha wananchi katika shughuli za serikali.

Nne, mfumo wa *Majimbo* na Serikali za wilaya ambao ulikuwa sura muhimu ya la Katiba hiyo ni kwamba, ilikuwa na mambo mengi na magumu ambayo utekelezaji wake ulihitaji mbinu za hali ya juu za usimamizi, na ukubalifu wa viongozi wa karibu katika viwango vyote kufikia makubaliano. Aidha, ilitoa fursa kwa serikali kuu kuingilia masuala ya kimaeneo jambo ambalo lingekuwa kiini cha mafarakano makubwa.

Mwisho, sheria ya Haki za Binadamu ilibainika kwa maono yasiyo mapana; ilitoa nafasi ya upungufu mwingi na kupuuza haki za kijamii na uchumi. Ingawa dhamira yake kuu ilikuwa kutoamini uwezo wa Serikali, hapakuwa na vipengele vya kutosha vya kupokea malalamiko dhidi ya mamlaka ya umma.

## 3.3 <u>Mabadiliko ya Katiba Baada ya Uhuru</u>

### 3.3.1 Aina za Mabadiliko ya Katiba

Kutoka wakati ya Uhuru, mabadiliko ya kikatiba yanaweza kugawanywa vitengo vitatu. Kitengo cha kwanza kilielekezwa kuirudisha hali ya kimamlaka kwenye serikali kuu

katika kila sehemu zote nchini. Matokeo yalikuwa kutegemea usimamizi wa mikoani na kuondolewa kwa *Majimbo*.

Kitengo cha pili kilikuwa na marekebisho yaliyoelekezwa upande wa kuimarisha Mamlaka ya Nchi hasa Mamlaka ya Rais, mara nyingi kwa kutojali kanuni za Katiba za demokrasia na uwajibikaji. Kitengo cha tatu kilielekezwa upande wa kurudisha baadhi ya masharti yaliyoanzishwa kwa ajili ya kuongeza mamlaka ya nchi na rais, kwa kurejesha vipengele vya demokrasia na uwazi.

Vitengo viwili vya kwanza vilianzishwa kufuatia juhudi ya serikali ya wakati huo. Kufuatia shinikizo la serikali. Ni kutokana na kilitokana na msukumo wa raia na upinzani wa kisiasa; hususan, mahitaji na masharti ya asasi za kimataifa za kifedha na wafadhili wa kitaifa.

***(a) Kurudisha Mfumo wa Serikali ya Umoja***

Badiliko la kimsingi la kuadhimisha kumbukumbu ya kwanza ya uhuru lilibadilisha Kenya kutoka hali ya mamlaka ya ubunge hadi hali ya kuwa jamhuri, na kupata rais mtendaji. Hatimaye Malkia aliyewakilishwa na Gavana Mkuu, aliacha kuwa kiongozi wa serikali. La muhimu zaidi, kulikuwa na mabadiliko ya mfumo wa serikali. Marekebisho hayo yaliunganisha afisi za kiongozi wa serikali na ile ya mkuu wa utawala na kuhamisha uwezo wa Malkia na kumpa aliyekuwa Waziri Mkuu, Hayati Mzee Jomo Kenyatta. Hata hivyo, mabadiliko hayo hayakuanzisha masharti ya kawaida katika mfumo wa urais, kama vile kutenganisha uwezo wa Mamlaka ya Nchi na Bunge, ama utenguzi wa Rais. Badala yake, sasa Rais alikuwa na madaraka ya kuvunja bunge katika wakati wowote na kwa uamuzi wake mwenyewe. Alikuwa na uwezo wa kupiga kura ya turufu ama kuvunjilia mbali miswada ya bunge, ambao Gavana Mkuu hakuwa nao.

Muungano wa afisi za Waziri Mkuu na Gavana Mkuu ulibua cheo cha urais kilichokuwa na uwezo mwingi. Uwezo huu limetiliwa mkazo katika marekebisho ya baadaye, kama yanavyojadiliwa hapo chini. Hali changamano ya mfumo wa kisiasa ilitokea. Hali ya Rais kuwa mbunge na kuwa na majukumu ya eneobunge, ilizua hali ya kuweza

kupingwa kwa kupigiwa kura ya kutokuwa na imani. Jambo hili lilianzisha migogoro ya kimaslahi na kuweka utandu ulioziba uwajibikaji na kupunguza pamoja na mengine jukumu la bunge na uwezo wake wa kudhibiti na kuchunguza mamlaka ya nchi.

Kuhusu "*Majimbo*", serikali kuu ilitatiza kuanzisha vyema utawala wa kimajimbo. Serikali ilifanya hivi kwa kuwanyima uhuru wa vituo vya uratibu na rasilimali za kifedha.

Zaidi ya hivyo, yaelekea kulikuwepo na makubaliano miongoni mwa viongozi, kwamba masharti ambayo hawakuyaafiki ama ambayo waliyaona kwamba yalilazimishwa kwao na Waingereza yangebadilishwa mara tu uhuru utakapotolewa. Kwa hivyo, uwezo mwingi wa kimaeneo ambao haukuwa umejikita, uliondolewa wakati wa kuadhimisha kumbukumbu ya kwanza ya uhuru. Uwezo juu ya polisi na huduma kwa umma ulirejeshwa kwa serikali kuu.

Muda mfupi baadaye utaratibu wa kuyahakikishia maeneo mapato ya kudumu uliondolewa. Kwa hivyo mfumo wa M*ajimbo* ulitupiliwa mbali mwaka mmoja tu baada ya uhuru.

Katiba iliyolinda ufufuaji wa mipaka ya kimaeneo na ubadilishaji wa mipaka au utaratibu wa Katiba wa kuzuia uundaji wa maeneo mapya au wilaya mpya uliondolewa mnamo miaka ya 1964 na 1968. Hatimaye kufikia mwaka wa 1968, taasisi za maeneo zilizokuwa hazina uwezo wowote tena ziliondolewa kabisa. Seneti hiyo ambayo kimsingi iliundwa kulinda mfumo wa Majimbo iliondolewa mwaka wa 1968 na maseneta wote wakapewa viti kwenye bunge jipya ambalo liliongezewa awamu yake kwa muda wa mwaka mmoja zaidi.

Sababu muhimu ya kuvunjilia mbali utaratibu wa kimaeneo na serikali ilikuwa ni kurejesha mfumo wa utawala wa kimkoa uliokuwa umewezesha mamlaka makuu ya nchi kusimamia shughuli zote za nchi na hivyo kusababisha ulimbikizaji mkuu wa madaraka katika serikali kuu. .

***(b) Kuimarisha Uwezo wa Urais***

Mara tu mfumo wa serikali wa kimaeneo ulipobanduliwa na mfumo wa utawala uliokuwa na misingi yake katika utawala wa kikoloni kuwekwa, mabadiliko ya Katiba yalielekezwa katika kuimarisha uwezo wa rais. Hii ilifanywa kwanza kwa kupunguza mamlaka ya Bunge, kisha kuweka vikwazo vingi katika siasa, na kisha kuwadunisha waliokuwa wakishikilia afisi za kikatiba kutegemea mapenzi na matakwa ya Rais. Mambo haya yalitendeka katika njia mbali mbali. Chini ya marekebisho ya mwaka wa 1966, taratibu mpya zilizomtaka mbunge aliyechaguliwa kupitia usaidizi wa chama kujiuzulu ama kukiwacha chama wakati kilipokuwa kama chama cha bunge, ulipitishwa.

Ijapokuwa palikuwa na jaribio la kutaka kudhihirisha kanuni kwa misingi ya nadharia za kidemokrasia na uwakilishi, marekebisho yalihamasishwa na mshawasha wa kupinga upinzani dhidi ya KANU ukiongonzwa na hayati Oginga Odinga, aliyeanzisha Chama cha Kenya People's Union (KPU) kilichokuwa tayari kimewavutia baadhi ya wabunge wa KANU. Marekebisho hayo yalipitishwa bungeni mbio mbio kwa muda wa siku moja bila kufuata Kanuni za Bunge zinazohitajika kutoa ilani ya kuletwa kwa mswada Bungeni.

Mabadiliko mengine ya mwaka 1967 yaliyotolewa kuwashika wabunge waliogura na waliopeleka malalamiko mahakamani kuhusu kuondolewa kwenye viti vyao vya ubunge kwa kuwa marekebisho hayo hayakuhusu mambo yaliyopita. Marekebisho mengine yalifanywa haraka haraka na kupitishwa bungeni ili kuyajumuisha hata yale mambo yaliyokuwa yamepita huku mahakama ikiwa bado inashughulikia suala hilo. Pia mnamo 1966 marekebisho yalimfanya mbunge kupoteza kiti chake cha ubunge baada ya kukosa vikao vinane mfululizo vya bunge bila ya ruhusa ya Spika.

Katika hali ambayo si ya kawaida Rais alipewa uwezo kuingilia kati suala hili. Ukweli wa kwamba Rais angeingilia kati suala hilo badala ya Spika inaonyesha nia ya mabadiliko hayo ilikuwa kukabiliana na wabunge sugu. Vile vile ilikuwa mbinu nyingine

ya kumwongezea Rais mamlaka. Marekebisho mengine yalileta kuondolewa kwa mbunge ambaye alipatikana na hatia na kufungwa gerezani kwa kipindi cha muda wa miezi sita au zaidi. Huku tukizingatia udhibiti wa serikali juu ya mashtaka ilidhaniwa kwamba marekebisho hayo yalisukumwa na hali ya kisiasa.

Mwaka huo huo vipimo na visawazishi vilivyokuwa vimewekwa katika Katiba ya Uhuru kupunguza matumizi ya mamlaka ya dharura vilipunguzwa zaidi. Wakati ambapo awali mamlaka ya serikali yangewezesha makubaliano ya kuidhinisha matumizi ya uwezo wa dharura, katika kipindi cha siku saba baada ya kutangaza hali ya hatari, kupitia marekebisho ya katiba ya 1964, muda huo uliongezwa na kuwa siku 28.

Vile vile, kanuni ya asilimia 65% ya wabunge waliohitajika kupitisha uwezo wa dharura ilipunguzwa na kuwa ushindi wa kawaida wa wabunge wanaopiga kura. Marekebisho ya mwaka wa 1966 yaliruhusu udunishaji mkubwa wa uhuru wa haki na uhuru wa kimsingi kuliko ilivyokuwa awali. Baadaye, uwezo uliodhaniwa kuwa utakuwa wa dharura uligeuka kuwa uwezo wa usimamizi wa raia. Kwa upande wa mkoa wa Kaskazini Mashariki, uwezo huu ulitengwa mkoani humo na wilaya za jirani. Kanuni hizo za mwaka wa 1966 zilitumika kukandamiza haki za kimsingi na kuchochea ukatili kwa zaidi ya miongo miwili na nusu. Ukatili huu ni pamoja na mauaji ya Bula Kartasi wilayani Garissa mnamo 1980, mauaji ya Wagalla wilayani Wajir mnamo 1984 na mauaji ya Malka Mari wilayani Mandera mnamo 1987. Mnamo mwaka wa 1968, Katiba ilibadilishwa kumpa nguvu Rais ili kuyasimamia mambo ya bunge kumpa uwezo wa kuwateua wabunge 12 maalum. Awali wabunge hawa walijulikana kama wajumbe maalum waliochaguliwa, walichaguliwa na bunge lenyewe.

Mwaka wa 1975 Katiba ilipitishwa ili kumpa Rais uwezo wa kubadilisha uamuzi au hukumu ya kutoshiriki katika uchaguzi kwa miaka mitano, kwa kupatikana na hatia ya kufanya kosa kuhusu uchaguzi. Marekebisho haya yalipitishwa siku moja wakati Paul Ngei alipopatikana na hatia ya kutenda kosa la uchaguzi. Rais alitumia marekebisho hayo na kumwondolea Paul Ngei vikwazo. Uwanja wa shughuli kisiasa ulikuwa finyu sana wakati Kenya ilipobadilika kuwa utawala wa chama kimoja kimazoea na kuwa utawala

wa chama kimoja kisheria. Haya yalitimizwa kupitia marekebisho yaliyofanywa mwaka wa 1982 yaliyoharamisha mfumo wa vyama vingine vya kisiasa na kubakisha chama cha KANU (Kenya African National Union). Shabaha kuu ilikuwa ni kukomesha majaribio ya Oginga Odinga, George Anyona na wanasiasa wengine wengi kuunda vyama vya kisiasa, na hivyo kumaliza kipindi cha Kenya kuwa chini ya utawala wa chama kimoja kikawaida.

Kuambatana na marekebisho haya, mtu aliyetaka kujiingiza katika ulingo ama afisi ya kisiasa alilazimika kuwa mwanachama wa KANU. Ghafla, vyama vyote vya upinzani viliondolewa (na wanasiasa wakuu na wengine waliopinga serikali walizuiliwa bila ya kupelekwa mahakamani). Hivyo basi, nguzo kuu ya utaratibu wa kidemokrasia, haki ya kuunda vyama vya kisiasa ama mashirika kama hayo, kushinikiza kuundwa kwa sera za sheria tofauti na zile za serikali, maoni ya umma, kuchunguza na kukosoa vitendo vya utawala, usimamizi na kuomba mabadiliko katika serikali kupitia kura ya kutokuwa na imani au uchaguzi mkuu ulitupiliwa mbali mara moja. Udunishaji wa wanaoshikilia afisi za kikatiba kutegemea mapenzi ya Mamlaka ya Nchi, ulitimizwa kupitia uondoaji wa mbinu za kuhakikisha kuwapo kwa utawala wa haki, kutoegemea upande wowote kwa taasisi za umma, uwajibikaji wa serikali na ulinzi wa haki kwa jumla.

Kwanza, mabadiliko haya yaliondoa kutoegemea upande wowote kwa Huduma ya Umma. Mnamo mwaka wa 1964, mpango wa kuwateua wanachama wa Tume ya Huduma kwa Umma ulichukuliwa kutoka kwenye Tume ya Huduma za Mahakama na kukabidhiwa Rais. Mwaka wa 1966 Rais alipewa uwezo wa kuteua na kutimua wafanyikazi wa umma. Kufikia mwaka wa 1968, kwa maafisa wa umma kuchaguliwa kujiunga na Tume kuliondolewa. Mnamo mwaka wa 1988, usalama wa kazi kwa wanatume pia uliondolewa.

Pili, mwaka wa 1966 ndio wakati ambapo uhuru na hadhi ya kikosi cha polis uliathirika kwa kutupiliwa mbali, Tume ya Huduma za Polisi na misingi yao ya kikazi pamoja na usalama wa awamu ya Inspekta Mkuu wa Polisi. Hii ilisababisha kuzua hali ya kisiasa katika utendakazi wa shughuli za Polisi, ukizingatia wanyanyasaji wa haki wapinzani.

Tatu, mwaka wa 1986 marekebisho mengine yaliondoa usalama wa kazi wa Mkuu wa Sheria kwa hivyo angeweza kutimuliwa na Rais. Taratibu za majukumu ya afisi yake, yaliyohusisha utoaji wa kibinafsi wa maoni ya kisheria kwa serikali na mashtaka yasiyobagua, yalichagizwa katika ukumbi wa kisiasa. Ni katika mwaka huo huo ambapo awamu ya Msimamizi wa Fedha na Mkuu wa Uhasibu ulipoondolewa na hivyo basi kutatiza uhuru wa mamlaka yake. Mnamo 1988, usalama wa kazi ya Majaji wa Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani uliondolewa. Hali hii ilifanya shughuli zao za kikazi kutegemea pakubwa uamuzi wa Rais.

***(c) Kupunguza Ulimbikizaji wa Madaraka ya Taifa***

Katiba ya uhuru ilikuwa imeunda mfumo wa kimaeneo wa serikali ya bunge yenye mamlaka ya nchi, mahakama huru yenye usalama wa kazi; na Tume huria ya uchaguzi; serikali ya siasa ya mfumo wa vyama vingi; mswada wa haki na uhuru; na kulinda haki ya walio wachache, pamoja na yakiwepo *Majimbo*.

Utenganishaji wa vipimo na visawazishi ulikuwa kiini chake. Kufikia mwaka wa 1998 masharti mengi tayari yalikuwa yameondolewa ama kufifishwa na kuzungukwa na utawala wa chama. Hakuna shaka kwamba Katiba ya wakati wa uhuru ilikuwa ngumu na isiyoeleweka wazi, kwani ilihitaji kurahisishwa kidogo. Hata hivyo, uchambuzi wa Katiba ulikiuka mipaka ya kuirahisisha. Kulikuwa na ulimbikizaji wa madaraka katika sehemu moja.

Katiba ilitumiwa kudunisha na kuondoa upinzani kabisa. Haki za watu na jamii zilianza kuwekwa kapuni, kuzuiliwa bila ya kufunguliwa mashtaka ikiwa ndiyo mbinu kuu ya kuvunja upinzani. Katiba haikuwa tena ni waraka muhimu wa kuleta umoja na kujenga misingi ya mkataba wa serikali. Ukatiba ukawa hauthaminiki tena.

Mabadiliko yakawa ni yenye kulenga na kuhakikisha manufaa ya kisiasa kwa chama kinachotawala ama kushughulikia na watu waliokuwa na maoni tofauti ya kisiasa. Marekebisho yalifanywa kwa kuangalia Katiba ilivyokuwa awali, wakati ambapo sababu

fulani fulani za kisiasa zilihitaji chama kinachotawala kufanya hivyo. Marekebisho mengi yalijitokeza hata bila ya taarifa yoyote na kupitishwa bungeni kwa muda wa saa chache, hasa kwa kuondoa ama kusimamisha kanuni fulani zilizopo. Mbali na kuwa Mkataba au chombo cha kidemokrasia na uwajibikaji, Katiba iliyumbishwa na kufanywa chombo kinachoweza kuelekezwa vyovyote vile na kwa ukandamizaji. Kwa hali hii ufisadi nao ukazidi.

Na watu nao wakapoteza imani ya Katiba na uhakika wa taratibu za kisiasa. Asasi chache za kitaifa zilifurahia uhalali huo na nyingine kupoteza uwezo wa makubaliano na mwafaka baina ya watu na vyama vya kisiasa ili kupata maafikiano. Watu walishindwa kupinga thamani ya mfumo wa kikatiba kwani hawakuwa na jukumu lolote katika kuiunda. Kilio cha uhitaji wa kurekebisha Katiba kilijitokeza kutoka kwa wale ambao hawakutosheka na njia ya kupuuza thamani za Katiba na kuondolewa asili ya uwezo wa Katiba.

Matatizo mengi ya kisiasa, kijamii na kiuchumi nchini yalitokana na mfumo wa Katiba na siasa. Huu pia ulikuwa ndio wakati ambao katika mataifa mengine mfumo wa kijeshi na ule wa utawala mkongwe ulikuwa ukiondolewa. Kadri jamii zilivyoanza kuelewa maendeleo haya na misukumo ya mageuzi huku wadhamini wakipigania mageuzi, ndivyo serikali ilivyokuwa na wakati mgumu sana kukataa mabadiliko hayo. Katika kipindi cha mwongo wa miaka ya tisini marekebisho yote yaliyotolewa miongo mitatu iliyopita ya uhuru, yalijadiliwa na kupitiwa upya.

Mwaka wa 1990, usalama wa kazi ya mahakama, Mkuu wa sheria, Msimamizi na Mkaguzi wa Fedha za Serikali na Tume ya Huduma ya Umma ulirejeshwa kwa kipindi cha miaka miwili iliyofuata. Masharti ya mfumo wa chama kimoja cha utawala yaliondolewa, na marekebisho yakapitishwa kwamba hakuna mtu yeyote atakayeshika hatamu katika afisi ya rais kwa zaidi ya vipindi viwili vya miaka mitano kwa kila kipindi. Mwaka wa 1997, Kenya ilipitisha mfumo wa kitaifa wa vyama vingi. Mwaka huo huo:

(i) Uwezo wa kuwateua Wabunge ulipitishwa mara moja hadi kwa vyama vya kisiasa, vilivyochagua wawakilishi kulingana na sehemu yao ya uanachama, "wakizingatia kanuni za usawa wa kijinsia."

(ii) Uanachama wa Tume ya Uchaguzi uliongezwa hadi ukafika 24 kwa lengo la kuhakikisha usawa na uhuru wake katika chama chochote kile.

(iii) Masharti ya kutobagua yalirekebishwa ili kuingiza hali ya "jinsia" ya kuharamisha kubaguana, na

(iv) Baadhi ya Vifungu vya Sheria vilivyopinga haki za kijamii na za kisiasa vilitupiliwa mbali na kurekebishwa. Vifungu hivi ni pamoja na Sheria ya Uzururaji (Sura 58), Kusimamia Wilaya Jirani (Sura 104), Sheria ya wilaya maalum (utawala) (Sura105), Sheria za Kulinda Usalama wa Umma. Sheria ya Kanuni ya Jinai (Sura 63), Sheria ya Jamii (Sura 108), Sheria ya Utulivu wa Raia (Sura 56), Sheria ya Mamlaka ya Machifu (Sura 128), Sheria ya Filamu na Michezo ya Jukwaani (Sura 222), na sheria ya Kituo cha Utangazaji cha Kenya (Sura 221).

### 3.4 Tathmini ya Katiba Iliyopo

Ingawa marekebisho hayo yalilenga masuala kuhusu udemokrasia na hali bora ya kulinda haki, na kulikuwa na uhuria maalumu wa upanuaji wa vyombo vya habari, ilibakia tu kwamba taratibu hizo zifanywe hatua kwa hatua, kanuni na shabaha yake ikiwa ni kujenga msingi ambao ni muhimu katika marekebisho kwenye demokrasia kamili, jamii yenye kusisimua, na kuhusika kwa watu.

Tatizo linalojitokeza wazi kabisa ni lile la mamlaka ya Rais katika mfumo wa kikatiba. Licha ya uwezo mwingi aliopewa Rais katika sheria za kawaida, Katiba nayo imempa uwezo na shughuli nyingi tofauti anazoweza kuzitekeleza kadri anavyopenda mwenyewe. Muhimu kati ya hizo ni kwamba Rais:

1. Ni kiongozi wa taifa na mkuu wa majeshi. Ni kiongozi wa serikali na mhifadhi wa mamlaka ya nchi, ni mwanachama wa bunge la taifa na anayeweza kuhudhuria vikao vya bunge kama mbunge. Rais anachukuliwa kama sehemu ya bunge na ana kinga

dhidi ya mashtaka anapokuwa afisini. Anaweza kutangaza hali ya hatari kuambatana na sheria ya usalama wa wananchi, na hubakia afisini kwa miezi kadhaa baada ya muda rasmi wa kuwa rais kumalizika.

2. Anateua Makamu wa Rais na mawaziri na kuchunguza mienendo yao ndani na nje ya nchi. Anateua makatibu wa kudumu na wote walio na wadhifa kikatiba pamoja na jaji mkuu, majaji, Makamishna wa Tume ya Uchaguzi, Makamishna wa Polisi, Mwanasheria Mkuu, Msimamizi na Mkaguzi Mkuu wa Fedha za Serikali, Makamishna wa Tume ya Huduma za Umma na wanachama wa mahakama maalum za kuchunguza kuwaondoa mamlakani wanaoshikilia wadhifa wa afisi hizi.
3. Ana uwezo wa kuanzisha afisi za umma na kuwaajiri maafisa.
4. Ana mamlaka juu ya bunge pamoja na kura ya turufu juu ya sheria ambazo bunge linaweza kubadilisha kwa wingi wa theluthi mbili za wanachama wote. Anaweza pia kuzuia bunge kushughulikia sheria au mabadiliko ya sheria yenye mielekeo ya matumizi ya fedha. Aidha anaweza kuitisha kikao cha bunge, kuahirisha au kuvunja bunge wakati wowote, anaweza kuamrisha kwamba mbunge aliyepoteza kiti chake kwa kukosa kuhudhuria vikao vinane mfululizo au kwa kuhukumiwa akihifadhi kiti hicho.
5. Ana uwezo wa kusamehe hatia anapotaka.
6. Rais anaweza kuchukua ardhi amana kwa nia maalum (sehemu ya 118).

Matokeo ya huku kulimbikiza uwezo kwa Rais ni kuwa anaweza kujichukulia vyombo vingine vyote vya utawala wa nchi kinyume na kanuni za kugawanya na kusawazisha madaraka. Mamlaka ya kuahirisha na kuvunja bunge na kura ya turufu dhidi ya miswada ya bungeni, huzorotesha Bunge la kitaifa ilhali Bunge inapaswa kusimamia na kudhibiti mamlaka ya nchi. Ukosefu wa kujiamini kwa polisi (na jeshi la polisi kukosa kuwajibikia wananchi) ni rahisi sana kuibadilisha Polisi kuwa chombo cha kukandamiza wapinzani wa utawala mkongwe. Watumishi wa serikali wamekuwa wakitumiwa vibaya na Rais na kupoteza sifa ya kutopendelea. Tume ya huduma za mahakama haithaminiwi tena kuwa ni ya haki, kwa hivyo mahakama yanaonekana kama yasiyojimudu yakipata shinikizo kutoka kwa serikali. Jumla ya wajibu wa Mwanasheria Mkuu kwa mujibu wa cheo chake cha ubunge, baraza la mawaziri na mshauri mkuu wa serikali; vyote vimewekwa hatarani.

Ukosefu wa uwezo wowote wa kujitenga humaanisha kuwa Rais anaweza kuvunja sheria na kwenda kinyume cha Katiba na sheria, na kutumia uwezo wake vibaya kwa ujabari kwa kutoweza kuadhibiwa. Katiba inahimiza kumiliki uwezo ambao ni kinyume cha ukatiba. Ukosefu wa vyombo vyovyote vya kuwajibika vinavyofanya kazi unachangia kuzidi kwa ufisadi na aina nyingine za uharibifu ama udhalilishaji wa rasilimali za umma. Katika kuongezea hali ya kujipatia uwezo, Katiba ina kasoro nyingi kwa namna nyingine.

Kwanza, haibainishi kanuni za matumizi ya uwezo wa serikali au malengo ya kitaifa na mwamko, wala haina utaratibu ya kutosha kushughulikia malalamiko dhidi ya Mawaziri au maafisa wa serikali. Njia pekee ya kushughulikia malalamiko ni mahakama, ambayo si rahisi kufikiwa na Wakenya wengi.

Pili, uwezo wote umewekwa katika serikali kuu na hakuna utaratibu wa kuwepo kwa serikali za wilaya. Utawala wa mkoa ambao ndicho kifaa muhimu cha mamlaka kuu katika matumizi ya uwezo wake haupo kwenye Katiba.

Tatu, Sheria ya Haki ina udhaifu ufuatao:

- Haki zinaweza kutatizwa ama kuondolewa kwa urahisi mno;
- Haitambui kanuni za usawa wa kijinsia;
- Hailindi haki za kiuchumi na kijamii ambazo ni muhimu kwa mahitaji ya kimsingi ya kundi kubwa la watu;
- Haina mbinu mwafaka za kutekeleza haki; na
- Majukumu ya raia na maafisa hayakubainishwa.

Nne, mfumo wa uchaguzi ulio na msingi wake katika kanuni ya mwakilishi mmoja kutoka kila eneobunge na mfumo wa kupiga kura wa “atanguliaye kufika ndiye mshindi” haufanikishi uwakilishwaji wa walio wachache.

Tano, sheria za uraia zinawabagua wanawake, na utekelezaji wa sheria unawabagua walio wachache.

Sita, hakuna mbinu ama asasi za kuwahusisha wananchi katika masuala ya taifa, licha ya kupiga kura kila baada ya miaka mitano.

Saba, hakuna utaratibu wa kushughulikia uundaji wa sera kuhusu masuala nyeti kama vile ardhi, uhusiano na mataifa ya kigeni, utaratibu wa kuweka mikataba au hata elimu. Kanuni za kubadilisha Katiba hazitoi kikamilifu ulinzi wa asasi au taratibu wala hazitambui masharti fulani kama ya kimsingi kuliko mengine ili kuyahami zaidi.

**HITIMISHO**

Nia kuu ya Katiba ya Uhuru ilikuwa kutangaza na kutilia mkazo uhuru wa watu wa Kenya na kubadilisha taifa la kikoloni lililokuwa chombo cha kutawala kimabavu, kuwa taifa la demokrasia linalohudumia wananchi. Lakini kwa sababu ya kuzingatia zaidi taratibu za kitawala zilizokuwepo nyakati za ukoloni pamoja na mabadiliko mengi ya Katiba ya kumpa Rais aliyechaguliwa mamlaka sawa na gavana wa kikoloni, mielekeo ya serikali za kikoloni ilirejeshwa na kuimarishwa. Mielekeo hii ilikuwa ni pamoja na mpangilio wa utawala wa siasa katika msingi wa kikabila (inayoondoa uzingatiaji wa sera za kijamii na kisiasa), kushiriki kwa kiwango cha chini miongoni mwa wananchi katika shughuli za serikali, urasimi katika kudhibiti rasilimali, kutokuwa na uhuru miongoni mwa vikosi vya usalama, kukosa uwajibikaji serikalini na la muhimu zaidi, kukosa kuzingatia kanuni za kimsingi za Katiba.

## SURA YA NNE

## MIJADALA NA UTARATIBU WA MAREKEBISHO YA KATIBA

## 4.1 Shinikizo za Marekebisho ya Katiba

### 4.1.1 Muktadha wa Kilimwengu

Shinikizo za marekebisho ya Katiba hasa katika mwongo wa mwisho wa karne ya ishirini hazikuwa tu nchini Kenya. Zilikuwa sehemu ya wimbi la kilimwengu la demokrasia na marekebisho ya Katiba lililodhihirika katika mifumo yote ya siasa kote ulimwenguni. Kilichokuwa muhimu zaidi kwa bara la Afrika kuhusiana na wimbi hilo ilikuwa kuvunjika kwa Muungano wa Usovyeti na mataifa yaliyofungamana nao, mwishoni mwa miaka ya themanini na kusababisha kuundwa kwa uhusiano mpya wa kisiasa na kijiografia kati ya mataifa ya bara Ulaya, Amerika na Asia. Shinikizo hizo pia zilitokana na kuwepo kwa mabadiliko ya kikatiba na demokrasia katika sehemu nyingine. Utaratibu mpya ulimwenguni uliotawaliwa na mfumo wa mataifa mengi yamepita mabadiliko mengi ya kimapinduzi, ama kupitia kupinduliwa kwa ukomunisti, au kukomeshwa kwa utawala wa chama kimoja au wa majeshi.  Kwa hivyo ilikuwepo sababu kubwa ya kutaka vifaa vipya vya kikatiba. Mabadiliko haya hasa yalitokana na mapambano ya raia waliothamini zaidi kuhusishwa kwa umma katika utawala. Hivyo basi kutokana na hali katika safu ya kimataifa na pia katika mataifa binafsi, dhana ya Katiba huria ilikubaliwa katika mataifa mengi. Mkazo mkubwa uliwekwa katika kuzifanya Katiba kuwa za kidemokrasia zaidi, kumaanisha kwamba mkazo huo uliwekwa kwenye kanuni za kikatiba na asasi ambazo zingetumiwa kufanikisha demokrasia.

Mkazo katika mabadiliko ya kikatiba uliwekwa katika sehemu tatu kuu. Sehemu ya kwanza ilikuwa bunge, ambapo Katiba mpya ziliandaliwa kwa njia ambayo ilitoa mamlaka kamili ya kisheria kwa bunge lililoteuliwa, na jukumu la kuanzisha na kuendeleza uwezo mkuu wa serikali. Vyama vya kisiasa, kwa hivyo, ndivyo vilivyokuwa kifaa kikuu cha uwakilishi na uongozi.

Pili, mkazo uliwekwa kwenye juhudi za kupunguza na kusambaza madaraka yaliyotokana na sababu kuwa kushikilia mfumo wa serikali moja kuu  barani Ulaya kabla, ya Vita Vikuu vya Pili vya Dunia, kulikuwa mojawapo ya sababu zilizosababisha

kuzuka kwa vita. Hata hivyo, miundo ya serikali ya kishirikisho ilitofautiana katika mataifa mbalimbali kutegemea historia ya kila taifa husika. Tatu, mkazo mkubwa pia uliwekwa kwenye kujitambulisha kiraia na kisiasa, huku nyingi ya Katiba zilizoundwa baada ya vita zikitambua haki za kimsingi za kiraia na za kisiasa.

### 4.1.2 Muktadha Barani Afrika

Matukio haya yaliathiri pakubwa siasa za Afrika kwa njia mbili. Kwanza, yalisababisha kusambaratika kwa kundi la mataifa ya Mashariki, na kwa kiasi fulani kutenga Muungano wa Mataifa ya Amerika, kutokana na masuala ya Afrika, na kwa hivyo, kusababisha kuondolewa kwa usaidizi wa kiuchumi, kijeshi na kisiasa kwa baadhi ya mataifa barani Afrika.

Pili, yalisababisha kusambaa kwa dhana ya uhuria wa mpangilio wa taifa, na hivyo kimsingi, kujitokeza kama changamoto kwa itikadi ya taifa ya kimaendeleo iliyokuwa ikiimarika miongoni mwa wasomi wengi barani Afrika.

Athari ya mara moja iliyotokana na matukio haya ilikuwa kutoa fursa ya majadiliano kuhusu siasa katika mataifa mengi barani Afrika, na hivyo kufikia kuanza kwa shinikizo za kutaka mabadiliko ya Katiba. Shinikizo hizo za kupigania “uhuru wa pili” barani Afrika ziliongozwa na mashirika ya kutetea haki za raia, maandamano ya wasomi waliopoteza imani na utawala, na vyombo vya habari, kuulazimisha utawala kuzingatia maadili huria ya kikatiba.

Kutokana na hali hiyo, kumekuwa na mabadiliko makubwa ya kisiasa barani Afrika kuanzia mapema miaka ya tisini. Hali ya mapinduzi iliyoshamiri mnamo miaka ya sabini na themanini ilianza kutoweka na kutoa fursa ya utaratibu bora wa kupishana mamlaka.

Kufikia mwishoni mwa mwongo wa miaka ya themanini, mataifa mengi barani Afrika yalikuwa yameshughulikia mabadiliko ya Katiba na kuanzisha upinzani unaokubalika kisheria katika siasa, na pia hatua kubwa kupigwa katika kuleta mabadiliko kwenye mfumo wa uchaguzi. Aidha, serikali zimeonekana kupunguza udhibiti wa shughuli za

raia katika siasa, pamoja na kuzingatia uhuru wa raia wa kutoa maoni na kushirikiana, na uhuru wa vyombo vya habari.

Kuambatana na mabadiliko yaliyotokea katika mwongo wa miaka ya themanini, yaelekea bara la Afrika sasa limeingia katika hatua mpya ya maendeleo ya kikatiba. Maendeleo haya ni kuhakikisha kuwa maadili ya Katiba yanakuwa sehemu ya maisha. Hata hivyo, hali imeonekana kutatizwa na mambo matatu makuu. Kwanza, ni hali ya vyama tawala kuonekana kukosa kujitolea kuzingatia utaratibu mpya wa kisiasa na kikatiba uliotokea katika mwongo wa mwisho. Pili, ni kukosa kujitolea kufanya marekebisho ya kisheria ili kuleta usawazisho kati ya Katiba na sheria zilizopo. Mwisho, ni kuendelea kuvunjwa kwa sheria zilizopo, ikiwa ni pamoja na kanuni za kikatiba, na wanaovunja sheria kukosa kuchukuliwa hatua yoyote.

Suala jingine ni lile la kutoa fursa sawa kwa wanasiasa wote, na kuwekwa huru na kuzifanya asasi muhimu zilizo na jukumu la kusimamia utaratibu wa kikatiba kama mahakama na mashirika ya uchaguzi, kutopendelea upande wowote. Sifa kuu ya hali hii ni jinsi utaratibu wa kikatiba unavyofuatiliwa kwa makini, kupitia msisitizo kuwa Katiba mpya inapasa kuwa ile inayozingatia hali halisi nchini Kenya, pamoja na kuzingatia haki zilizotangazwa na kukubaliwa kote ulimwenguni, na pia kuzingatia hali za kisiasa, kijamii na kiuchumi nchini Kenya. Utaratibu wa sasa wa marekebisho ya Katiba nchini Kenya ni juhudi kubwa ya kuyakabili maswala haya.

### 4.1.3 Muktadha Nchini Kenya

Kwa miaka mingi sasa, Wakenya wamekuwa wakitaka Katiba yao irekebishwe kwa kuwa wanaonelea kwamba Katiba iliyopo haiwahudumii ipasavyo. Kumekuwa na kutoridhika na jinsi mambo muhimu yalivyoondolewa katika Katiba ya Uhuru na kumlimbikizia Rais uwezo mwingi. Kwa hakika, matatizo mengi ya kisiasa, kijamii na kiuchumi yanayolikabili taifa hili mara nyingi yalihusishwa na udhaifu wa Katiba.

Vuguvugu la kupigania marekebisho ya Katiba nchini Kenya baada ya mwaka 1990 lilitokana na matukio ya kilimwengu na kimaeneo na kuongozwa na mashirika ya kutetea

haki za raia kwa kuunda ajenda ya mabadiliko.  Lakini Kenya ilitofautiana na mataifa mengine yaliyounda Katiba mpya kabisa. Kenya ilikuwa na uthabiti wa kisiasa na kwa hivyo shinikizo za mabadiliko zilitokana na haja ya kuifanyia marekebisho Katiba iliyopo ili kuiimarisha, na wala si haja ya utaratibu mpya wa kijamii na kiuchumi. Kwa hivyo, kinyume na ilivyokuwa nchini Uganda, au Afrika Kusini, au hata Mashariki mwa Ulaya, hapakuwa na shinikizo za kutaka Katiba mpya kabisa. Madai ya kutaka Katiba irekebishwe kupitia utaratibu fulani hayakutolewa kuanzia hivi majuzi tu. Madai kama hayo yaliwahi kutolewa kwa kamati ya KANU ya Marekebisho iliyokuwa ikiongozwa na Makamu wa Rais Profesa George Saitoti. Shaka ilitiliwa kuhitajika kwa baadhi ya mambo yaliyokuwa yameingizwa katika Katiba ya Uhuru, kama vile utawala wa vyama vya kisiasa, kuzuiwa bila kupelekwa mahakamani, kuondolewa kwa Usalama wa kazi ya majaji, Mkuu wa Sheria na msimamizi na Mhasibu Mkuu wa fedha za serikali, na kudhoofika kwa kanuni ya kutenganisha madaraka. Hata hivyo, hakuna hatua iliyotekelezwa na kamati hiyo kwani iliyachukulia masuala hayo kwamba yalikuwa nje ya maagizo yake.

Shinikizo za Marekebisho ziliongezeka wakati vuguvugu la kupigania kurejeshwa kwa mfumo wa vyama vingi lilipoanza mapema miaka ya tisini likiongozwa na muungano wa raia wa kupigania mabadiliko (4Cs) na mashirika ya kidini.

Mashirika mengi yalijiunga na vuguvugu hilo yakiwemo makundi ya kisiasa, Baraza la Kitaifa la Makanisa ya Kikristo, Chama cha Maaskofu wa Kanisa Katoliki, Chama cha Wanasheria, Tume ya Kimataifa ya Majaji (International Commission of Jurists - ICJ), na Shirika Lisilo La Kiserikali La Kutetea Haki za Binadamu (KHRC). Baadhi ya makundi yalitaka Katiba ifanyiwe marekebisho ya kina kabla ya uchaguzi mkuu wa 1992, lakini hayakufua dafu. Shinikizo za mabadiliko ya Katiba zilishika kasi tena baada ya uchaguzi kwani iligunduliwa kuwa kuondolewa kwa mfumo wa utawala wa chama kimoja pekee hakungeweza kufanya siasa ziwe na demokrasia, kuimarisha uwajibikaji wa maafisa, pamoja na kuhakikisha kuundwa kwa sera zinazozingatia uhalisi wa mambo. Mnamo mwaka wa 1994, Maaskofu wa Kanisa Katoliki walitoa barua wakitaka Katiba mpya iliyobeba kihakika utawala wa mfumo wa vyama vingi.

Wakati huo huo, Katiba mpya iliyopendekezwa ilitayarishwa na kusambazwa na Tume ya Kutetea Haki za Binadamu Nchini Kenya (KHRC), Chama cha Wanasheria cha Kenya (LSK) na Tume ya Majaji wa Kimataifa (ICJ). Katiba hiyo iliyopendekezwa ilitumiwa na makundi ya kutetea raia na makundi ya kidini na ya kisiasa kama msingi wa mashauriano na pia katika warsha kuanzia 1994. Katiba hiyo iliyojulikana kama *Proposal For a Model Constitution* (Pendekezo la Katiba) ilidai kuwa raia wana haki ya kutaka Katiba ifanyiwe marekebisho. Mnamo Januari 1995, serikali ilitangaza mpango wa kuwaalika wataalamu wa kigeni kuandika Katiba ambayo ingejadiliwa na bunge. Hata hivyo, tangazo hilo halikuzingatiwa, na shinikizo za raia za kutaka mabadiliko ya Katiba ziliendelea kupamba moto. Hali hii ilileta kufanywa kwa maandamano yaliyosababisha ghasia na baadhi ya watu wakafariki. Ni wakati huo ambapo vyama vya kisiasa vilivyokuwa na wabunge bungeni, vikiwemo vile vilivyounga mkono Mapatono ya Kitaifa kwa Mabadiliko ya Katiba (National Convention for Constitutional Change) vilipounda Kundi la Vyama vya Wabunge (Inter-Parties Parliamentary Group -IPPG) mnamo Agosti mwaka 1997.

Kundi hilo la IPPG lililojumuisha vyama vya kisiasa vilivyokuwa na wabunge bungeni lilikubaliana kuhusu mabadiliko fulani ambayo yangetekelezwa kabla ya uchaguzi mkuu, yakiwemo kuwekwa huru kwa Tume ya Uchaguzi, kubadilishwa kwa sheria zilizokuwa zikitatiza haki za uraia na zile za kisiasa na kufuta kosa la kuasi. Ilikubalika pia kuwa hatua nyingine zingechukuliwa kuimarisha uhuru wa kushirikiana, uhuru wa vyombo vya habari na uhuru wa vyama vya kisiasa.

Marekebisho haya yalikuwa machache tu ya kuwezesha uchaguzi kufanywa kwa njia iliyo huru na ya haki. Marekebisho ya kina yangefanywa baada ya uchaguzi kwa msingi wa msimamo rasmi wa serikali. Hata hivyo, kutokana na kuvunjwa mapema kwa bunge, marekebisho yote hayo hayakutekelezwa. Lakini kutegemea makubaliano ya kundi la IPPG, Sheria ya Marekebisho ya Katiba mwaka 1997 iliundwa kutoa njia zilizohitajika kufikia malengo ya marekebisho ya Katiba baada ya uchaguzi.

Hata hivyo, sheria hiyo ya 1997 haikuyatosheleza makundi yote husika. Kwa kuwa sheria hiyo ilitayarishwa na Mkuu wa Sheria, Kiongozi wa Upinzani Rasmi pamoja na raia hawakupata fursa ya kutoa ushauri kuhusu masuala nyeti yaliyojumuishwa kwenye sheria hiyo. Kwa hivyo, Wakenya waliukataa utaratibu huo wa marekebisho ya Katiba, pamoja na sheria yake, wakisema hiyo ilikuwa mbinu ya serikali ya kuwalaghai, na kudai fursa ya kushiriki katika utaratibu wa marekebisho ya Katiba. Kutokana na hali hiyo, idadi kubwa ya washikadau walifanya mashauriano kuhusu njia bora ya kuendesha utaratibu huo wa marekebiasho katika hoteli ya Safari Park na pia katika Bomas of Kenya kati ya mwezi Juni na mwezi Oktoba, mwaka 1998. Mashauriano hayo yalisababisha Sheria ya Marekebisho ya Katiba kufanyiwa marekebisho ili kujumuisha masuala nyeti yaliyokubaliwa na washikadau wote wakati wa mashauriano hayo. Sifa kuu za marekebisho hayo zilikuwa kuwekwa kwa utaratibu ufuatao:

1) Kuundwa kwa Tume ya wanachama ishirini na watano walioteuliwa kiusawazisho na washikadau na wala si Rais;

2) Utaratibu wa uteuzi unaozingatia wakati;

3) Kuteuliwa kwa wanachama wa Tume baada ya kuchaguliwa na rais;

4) Utekelezaji wa sera ya thuluthi moja ya wawakilishi wanawake; na

5) Miundo ya utaratibu wa Marekebisho ya Katiba ainayodhihirisha mkabala wa “kutoka mashinani”, unaendeshwa na umma.

Utaratibu huo hata hivyo, haukuzingatiwa baadaye kwani washikadau, na hasa vyama vya kisiasa, vilishindwa kuafikiana kuhusu mpango wa uteuzi wa makamishna. Tofauti hiyo ilipokita, makundi yote mawili yaliyokuwa yakipingana yaliamua kuendelea na utaratibu huo wa marekebisho kwa kufuata njia zao wenyewe.

Kundi la kwanza, *Ufungamano*, lililoungwa mkono na mashirika ya kitaifa ya kidini na mashirika ya kutetea haki za raia liliunda Tume ya Wananchi wa Kenya (People’s Commission of Kenya - PCK) kwa misingi ya utaratibu uliotolewa na sheria ya marekebisho ya Katiba iliyokuwa imefanyiwa marekebisho. Licha ya kukabiliwa na

tatizo la ukosefu wa fedha na kutoungwa mkono na bunge, *Kundi la Ufungamano* liliendelea na shughuli ya kukusanya maoni ya Wakenya kuhusu Katiba.

Kundi la pili lilikuwa bunge. Kundi hili lililoungwa mkono hasa na KANU na vyama vingine vya kisiasa vilivyokuwa vikishirikiana na KANU liliteua Kamati ya Bunge kuamua ni vifaa vipi vingehitajika ili kufanikisha marekebisho ya kina ya Katiba. Hii ilisababisha Sheria ya Marekebisho ya Katiba kufanyiwa marekebisho mnamo mwaka 2000. Marekebisho hayo ya mwaka 2000 yalijumuisha masuala nyeti katika utaratibu wa kisheria wa marekebisho ya Katiba kama ilivyokuwa imekubaliwa mwaka 1998. Miongoni mwa marekebisho hayo ni kuwa:

- Idadi ya makamishna ilipunguzwa kutoka ishirini na watano hadi 15 pamoja na wanachama wawili kwa mujibu wa vyeo vyao.
- Makamishna hawa wangeteuliwa kutegemea ubora wao baada ya kamati ya bunge kuhusu marekebisho ya Katiba kupitia maombi yao na kufanya mahojiano.
- Kuwepo kwa makabila mengi na maeneo mengi ya kijiografia na kijamii kungezingatiwa wakati wa uteuzi.
- Rais angewateua makamishna baada ya kuchaguliwa na Kamati ya Bunge kuhusu Marekebisho ya Katiba.

Kufuatia marekebisho hayo, Tume ya Kurekebisha Katiba ya Kenya iliundwa na makamishna kumi na watano wakateuliwa mwezi Novemba mwaka huo. Bila shaka kuwepo kwa makundi mawili ya kurekebisha Katiba nchini halikuwa jambo la kuridhisha. Kulikuwepo hatari ya makundi hayo mawili kuzidisha mzozo wa kisiasa nchini, na hata pengine ghasia, na kuwa Katiba ambazo zingeundwa na makundi hayo hazingekubaliwa kwani makundi yote mawili hayakuwa na uungwaji mkono wa kutosha bungeni. Juhudi za kuleta pamoja makundi yote mawili zilifanywa na mwenyekiti wa Tume ya Marekebisho ya Katiba (Constitution of Kenya Review Commission - CKRC) kwa kuandaa mashauriano kati ya kamati iliyokuwa ikiendesha shughuli za kundi la Ufungamano, na Kamati ya Bunge kuhusu Marekebisho ya Katiba. Baada ya kutambua

kuwa Wakenya walihitaji makundi hayo kuungana kwa ajili ya umoja na amani ya taifa, pamoja na haja ya kutayarisha Katiba ambayo ingepokelewa vyema na raia wote kote nchini, wahusika walijasirika na kuchukua hatua muhimu zilizosababisha kuungana kwa makundi yote mawili. Sheria ya Marekebisho ya Katiba ilifanyiwa marekebisho mengine mnamo Mei mwaka 2000 ili kujumuisha masharti ya muungano wa makundi hayo mawili. Marekebisho hayo yalisababisha kuongezwa kwa makamishna wengine kumi na wawili katika uanachama wa Tume ya Marekebisho ya Katiba. Hakuna Tume iliyosimama wima wakati wa mashauriano. Kufikia wakati wa kuungana, Tume ya PCK ya kundi la Ufungamano ilikuwa imezuru jumla ya mikoa saba na kukusanya maoni kutoka kwa mashirika, makundi na watu binafsi. Tume ya Marekebisho ya Katiba, (CKRC) nayo ilikuwa imeandaa utaratibu mwafaka wa kamati, na nyingi ya kamati hizo zilikuwa zimekutana mara kadha kujadili mpango wa elimu ya uraia, uhusiano mwema na umma, utafiti, nayo kamati ya fedha ilikuwa imekamilisha majadiliano kuhusu marupurupu ya makamishna na kuanza kununua magari. Tume ilifaidika pakubwa baada ya makundi hayo kuungana na kuanza kufanya kazi kwa pamoja.

Moja kati ya mambo muhimu ya mashauriano ya kina kati ya makundi hayo mawili ni kwamba warsha na mikutano kadhaa iliandaliwa wakati huo kujadili Katiba iliyopo na kujadili malengo ya mabadiliko. Mashirika kadha, hasa mashirika yasiyo ya kiserikali, yalitakiwa kufanya utafiti kuhusu masuala mbali mbali yaliyolengwa na shinikizo za marekebisho ya Katiba kama vile mfumo wa uchaguzi, ardhi, bunge, haki za binadamu, jinsia na makundi ya walio wachache, ulemavu, umaskini na haki za kimsingi, mazingira, ufisadi na uwajibikaji kwa umma, na uchumi.

## 4.2 Utaratibu wa Kisheria wa Marekebisho.

### 4.2.1 Ari ya Sheria ya Marekebisho

Wakati Kenya ilipojinyakulia uhuru, Katiba haikuundwa moja kwa moja na wananchi. Mashauriano yalifanywa mjini London katika bunge la Lancaster kati ya serikali ya Uingereza na wawakilishi wa vyama vya kisiasa nchini Kenya waliokuwa wanachama wa Baraza la Bunge (Legislative Council). Wakenya hawakuhusishwa na Katiba yenyewe haikuidhinishwa na bunge la Kenya bali iliidhinishwa na bunge la Uingereza. Tangu wakati huo, Katiba imebadilishwa mara kadhaa ijapokuwa baadhi ya marekebisho yamegeuzwa tena. Wananchi hawakuhusishwa moja kwa moja katika marekebisho hayo, ambayo mengi yalipitishwa harakaharaka na bunge bila ya kutoa fursa kwa wananchi kuyajadili.

Kinyume na hali hiyo, msingi wa ari na mwelekeo wa Sheria ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya ni tofauti kabisa. Sheria hii imewapa fursa wananchi wote kushiriki katika utaratibu wa marekebisho ya Katiba. Ni kutokana na sababu hii ndipo utaratibu huu ukajulikana kama "utaratibu unaoongozwa na wananchi", kwa maana ya kulenga kuwahusisha wananchi kikamilifu. Kwa kuwa Katiba ni mapatano kati ya wananchi kuhusu usimamizi wa jamii yao, masuala mawili yanajitokeza kuwa muhimu katika uundaji wa Katiba. Suala la kwanza ni *utaratibu* unaofuatwa katika mashauriano na kukubaliwa kwa mapatano hayo, nalo suala la pili ni *yaliyomo* (maudhui) katika mapatano hayo; haya ndiyo matokeo ya utaratibu huo. Kuhusu utaratibu, Sheria ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya inaelezea wazi vyombo vya marekebisho na utaratibu vinaopasa kufuata. Vile vile kuhusu maudhui, Sheria ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya imeelezea wazi madhumuni na malengo ya marekebisho kutokana na makubaliano ya washikadau wakuu waliohusika. Madhumuni na malengo ya utaratibu wa marekebisho yanafungamanisha vyombo vyote vya marekebisho.  Lakini kanuni na asasi za kufikia malengo hayo zinaamuliwa na wananchi.

### 4.2.2 Madhumuni na Malengo ya Marekebisho

Tunaanza kwa kuchunguza maongozi ya matokeo ya utaratibu wa marekebisho. Ni jambo la kawaida kufanya jinsi Kenya ilivyofanya katika kutambua na kubainisha maadili fulani ambayo ni lazima yajitokeze kwenye Katiba. Katiba zote za kisasa zinalingana kwa njia moja; zinashughulikia mada fulani zinazolingana. Kuna makubaliano kote ulimwenguni kuhusu matumizi, upeo na uwezo wa umma, pamoja na kulingana kwa maoni kuhusu

jinsi malengo hayo yanavyoweza kutekelezwa kupitia sheria na asasi mbali mbali. Hata hivyo ni lazima Katiba iambatane na utamaduni na uhalisia wa mambo katika jamii inamoundwa. Hii inahakikisha kuwa makubaliano ya kitaifa, kama ilivyodhihirika wakati wa mashauriano na mikutano kadha ya washikadau, yanazingatiwa kama ilivyokwishaelezwa. Malengo ya marekebisho yanayoonyesha kile kinachochukuliwa kuwa udhaifu wa Katiba iliyopo, na yanayofungamanisha vyombo vyote vya marekebisho yamefafanuliwa katika Sehemu ya Tatu ya Sheria ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya.

***(a) Umoja wa Taifa na utambuzi wa Kikabila***

Lengo muhimu la marekebisho ni *kuhakikisha kuwepo kwa amani, umoja wa taifa na uadilifu* katika Jamhuri ya Kenya kwa kulinda maslahi ya wananchi (sehemu ya 3(a) na 3(h). Lengo hilo hilo ndilo msingi wa shabaha nyingine ya marekebisho ya kuwawezesha Wakenya kutatua masuala ya kitaifa kwa misingi ya makubaliano (sehemu ya 3(k)).

Isitoshe, Sheria ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya inaitarajia Katiba mpya *kuheshimu kuwepo kwa makabila na maeneo mengi pamoja na haki za kijumla,* ikiwemo haki ya jamii kuandaa na kushiriki katika shughuli za kitamaduni na kudhihirisha utambulisho wao (sehemu ya 3(e)). Malengo haya yanatambua kuwa watu wana utambulisho tofauti, licha ya vitambulisho wa kitaifa na uraia. Utambulisho huo unatokana na misingi yao ya kikabila au kieneo, kidini, kilugha, kijinsia au hata kitaaluma.

Umuhimu wa utambulisho huu sasa umekubaliwa kama vile zilivyo haki za walio wachache, na kukiri kwamba haupaswi kutishia umoja wa taifa, na kwamba kinyume na hofu hizo, hatua hiyo inaweza kuimarisha umoja wa taifa kuwepo kwa wingi wa tamaduni na hali za kijamii.

Hata hivyo utambulisho huo wa kikabila na kimaeneo ukitiliwa mkazo zaidi unaweza kutatiza umoja wa taifa kama ilivyotokea Yugoslavia ya zamani, na pia katika baadhi ya mataifa jirani. Kwa hivyo, changamoto muhimu kwa utaratibu wa Katiba ni kusawazisha

utambulisho huo katika viwango vidogo na vile vya kitaifa. Usawazisho huo ambao mataifa mengi yamelazimika kuufanyia jitihada zaidi unaweza kuzua mzozo na tofauti kubwa. Dhana za kikatiba zinazotumiwa ni zile za uraia na haki za watu binafsi na za makundi.

Uraia ni kigezo muhimu cha uanachama wa jamii ya kitaifa na, kwa hivyo, utambulisho wa kitaifa. Ili kuwa taifa la haki na linaloheshimiwa na wananchi wake, ni muhimu kwa raia wote kuwa na haki na majukumu sawa. Sheria ya Marebisho ya Katiba inahitaji haki za uraia kuchunguzwa na kufanyiwa marekebisho (sehemu 17(d)(ix)). Kanuni ya uraia sawa inaweza kutatizika wakati makundi ya walio wachache, kikabila na kijamii, yanapodai haki maalum zinazotambua na kuimarisha utamaduni wao ama njia zao tofauti za kuishi. Makundi kama hayo yanaweza kuchukulia "usawa" ama "usawa wa haki" kama njia ya kuwabagua. Huenda hata makundi fulani yakataka maadili yao ya kijamii yatiliwe mkazo zaidi kama haki za makundi kuliko haki za kila mtu, au haki za uraia wa wanachama wao. Kanuni ya usawa pia hutatizwa na madai ya makundi kutaka hatua fulani kuchukuliwa kuwasaidia, kama vile kitendo kisawazishi, ili kuondoa ubaguzi ama matatizo ambayo yamekuwa yakiwakabili.

***(b) Demokrasia, Utawala Mwema na Kanuni za Sheria***

Ni lazima Katiba mpya ibainishe mfumo wa serikali ya kidemokrasia, na Sheria ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya imeelezea baadhi ya mbinu zinazoweza kutumiwa kufikia lengo hili (sehemu ya 3(b)). Kwanza ni lazima uwepo utawala mwema. Hii ni kumaanisha kuwa:

- Ni lazima utaratibu wa utawala uwe wazi;
- Ni lazima mamlaka ya umma yawajibike kwa wananchi;
- Ni lazima uongozi uwe wa haki;
- Ni lazima maafisa wa umma wakiwemo mawaziri, waepukane na ufisadi na matumizi mengine mabaya ya madaraka;

- Ni lazima raslimali za taifa zisimamiwe vyema; Sheria ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya yanahitaji kuimarishwa kwa mfumo wa usimamizi na matumizi ya fedha za umma (sehemu 17(d)(viii)).

- Na mashirika ya raia yanapaswa kuwa na jukumu la kutekeleza katika usimamizi wa masuala ya umma.

Pili, ni lazima uwezo utenganishwe ili uwezo wa taifa ugawanywe kati ya vyombo vyake tofauti. Vyombo hivi vinapasa kujisimamia na panapaswa kuwepo vizuizi na visawazishi vya kutosha kati ya vyombo hivyo (sehemu ya 3(c) na sehemu ya 17(d)(i)). Neno "kizuizi" linatumiwa kumaanisha kuwa chombo kimoja kitakuwa na uwezo unaolingana na kingine (kwa hivyo mahakama zitachunguza na ziweze kuondoa sheria zinazopitishwa na bunge), nalo neno "visawazishi" linamaanisha kuwa ni lazima uwezo wa chombo kimoja usawazishwe na uwezo wa chombo kingine (kwa mfano afisa aliye na mamlaka makuu anaweza kuwateua maafisa wakuu, mradi uteuzi huo uidhinishwe na bunge).

Ni lazima msingi wa mfumo wa serikali wa kidemokrasia uwekwe kwenye uchaguzi ulio wazi na wa haki (sehemu 17(d)(iv)) na kujumuisha ukatiba, kanuni za sheria, haki za binadamu na usawa wa jinsia. Kanuni za sheria hazihitaji uwezo wa taifa usio na msingi maalum na unaobagua, na kwamba ni lazima vyombo vyote vya taifa vifuate sheria. Mahakama zinapaswa kujitegemea ili kuhakikisha kuwa serikali inafuata sheria kila wakati. Sheria ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya imezungumzia uwezo na muundo wa mahakama kama mada ya marekebisho, ikilenga kuchukuliwa kwa hatua zitakazohakikisha uwezo, uwajibikaji, ubora, nidhamu, na uhuria wa mahakama (sehemu 17(d)(iv)).

Dhana ya ukatiba, inayokaribiana na ile iliyokwishazungumziwa, ni pana mno na inamaanisha kuwa ari na kanuni za kuwepo kwa serikali ya haki na iliyo njema zinapaswa kuheshimiwa na wote, ikiwemo serikali. Uwezo wa vyombo vya taifa unahitaji kuwekewa mipaka. Njia moja ya Sheria ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya

kuhakikisha kuwa utawala wa kikatiba utashughulikiwa ni kwa kuanzishwa ama kuimarishwa kwa Tume huria za kikatiba (sehemu 17(d)(iii)) (tazama chini).

***(c) Haki za Binadamu***

Katiba zote za kisasa zinazingatia haki za binadamu. Na kuna mikataba kadhaa ya kimataifa na kimaeneo inayozilazimisha serikali kulinda haki. Sheria hiyo inachukulia kulindwa kwa haki za binadamu na usawa wa kijinsia, pamoja na utawala wa kikatiba 'kama sehemu muhimu ya kutoa fursa bora ya maendeleo ya kiuchumi, kijamii, kidini, kisiasa na kitamaduni' (sehemu ya 3 17(d)(iii)). Umuhimu wa haki za binadamu umeonyeshwa katika lengo lingine linalotoa nafasi mwafaka ya kubadilishana mawazo (sehemu ya 3(i)). Kupitia mikataba ya kimataifa, Kenya imekubali kulinda haki za binadamu na Sheria ya Marekebisho ya Katiba inataka wajibu zaidi wa kimataifa kutekelezwa (sehemu 17(d)(xiii)). Hii inajumuisha haki za wanawake na watoto, ambazo sheria inaagiza zishughulikiwe kwa njia maalum. Moja kati ya majukumu ya lengo jingine ambalo ni ushirikiano wa kieneo na kimataifa ni kuhakikisha kuwepo kwa demokrasia na haki za binadamu (sehemu 3(g)).

***(d) Haki sawa kwa Wote***

Sheria ya Marekebisho ya Katiba inatilia mkazo kanuni ya haki za binadamu. Kuhusu suala hili utaratibu wa marekebisho unatarajiwa 'kuchunguza na kurekebisha vizuizi vya kijamii na kitamaduni vinavyoendeleza njia mbali mbali za ubaguzi na kupendekeza njia za kuwahakikishia watu wote usawa' (sehemu ya 17(d)(x)). Hii inaonyesha kuwa utaratibu wa marekebisho hauhusiki tu na utoaji wa fursa ya haki hizo kirasmi, bali pia kuchunguza na kuondoa vizuizi vinavyotatiza kuwepo kwa haki sawa kwa wote. Baadhi ya vizuizi hivyo ni kama vile umaskini, ufisadi, udhalimu wa polisi, au sheria za tawala za mikoa na wilaya zisizo na msingi.

***(e) Usawa wa Kijinsia***

Sheria ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya pia inashughulikia usawa wa kijinsia kama lengo muhimu la marekebisho. Kauli ya usawa wa kijinsia inachukulia kuwa wanaume

na wanawake ni sawa, hasa kuhusiana na utoaji wa fursa ya kuhusika katika masuala ya umma, biashara na maisha ya kijamii ikiwa ni pamoja na familia.

Inachukulia kuwa wanaume au wanawake (hasa wanawake) hubaguliwa.

Wanawake wanaweza kubaguliwa chini ya sheria za kifamilia na kimila, kuhusu haki zinazohusiana na malezi ya watoto, urithi, sheria za biashara, hasa katika masuala yanayohusu mikopo na kadhalika. Aidha, kunaweza kuwepo mapendeleo ya kijamii dhidi ya kuhusishwa kwa wanawake katika siasa ama biashara. Wanawake nchini Kenya wanaathiriwa na mapendeleo na sheria kama hizo.

Usawa wa kijinsia unahusu juhudi za kuhakikisha kuwa wanawake kupitia mabadiliko ya kisheria na kijamii wanawezeshwa kuepuka vizuizi hivi na kufurahia haki sawa na wanaume, hata ikiwa italazimu hatua maalum kama vile vitendo visawazishi kuchukuliwa kuwasaidia.

Sheria ya Marekebisho ya Katiba inatilia mkazo usawa wa kijinsia unaochukuliwa kama sehemu ya mfumo wa kidemokrasia (sehemu ya 3(b), na kuwa ni muhimu kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi (sehemu ya 17(d)(iii)). Kwa mfano haki na sheria za uraia zinapaswa kuchunguzwa ili kuhakikisha kuwa zinazingatia usawa wa kijinsia (sehemu 17(d)(ix)).

***(f) Mahitaji ya Kimsingi kwa Wakenya Wote***

Lengo muhimu la marekebisho ni kuhakikisha kuwa kanuni za mahitaji ya kimsingi kwa Wakenya zinatolewa katika Katiba (sehemu ya 3(f)). Mahitaji ya kimsingi ni yale ambayo ni muhimu kwa maisha ya binadamu katika faraja na hadhi. Mahitaji haya yanajumuisha chakula cha kutosha, afya, makazi, elimu, mazingira safi na salama, utamaduni, na usalama wa kiuchumi. Kwa kawaida mahitaji haya hutolewa na taifa kupitia ulinzi wa haki za kijamii, kiuchumi na kitamaduni. Sheria ya Marekebisho ya Katiba inaelezea wazi kuwa lengo hili linapaswa kutekelezwa kupitia kuanzishwa kwa utaratibu wa usawa wa kukuza uchumi na fursa ya kufikia raslimali za kitaifa. Hii ni

muhimu zaidi nchini Kenya hasa ikichukuliwa kuwa asilimia sitini ya Wakenya wanaishi katika hali ya umaskini. Hali ya umaskini inafanywa kuwa mbaya zaidi na sera za kiuchumi zinazohusiana na utandawazi zinazopinga misaada ya serikali kwa elimu, afya, kilimo na makazi, kama ilivyoelezwa na sera mpya za kiuchumi barani Afrika ya Mradi ya Kurekebisha Miundo (Structural Adjustment Programmes - SAPs) na masharti ya makundi ya ufadhili. Vile vile, ili kutimiza haki za kijamii na kiuchumi nchini Kenya pana haja ya kushughulikia tofauti kubwa iliyopo katika umiliki wa mali na uwezo wa kufikia rasilmali inayodhihirika kutegemea viwango vya kijamii pamoja na kidini.

***(g) Uhusika wa Wananchi katika Serikali***

Lengo la kuhakikisha kuwa wananchi wanahusika kikamilifu katika usimamizi wa masuala ya umma linahusiana na demokrasia pamoja na haki za binadamu (sehemu 3(j)). Sheria inasisitiza uwajibikaji wa serikali kwa maafisa wake na kwa wananchi (sehemu ya 3(c)). Uhusika wa wananchi katika utawala wa nchi unatarajiwa kufanikishwa kupitia uchaguzi wa kidemokrasia, ulio wazi na wa haki, na kupunguza na kusambaza madaraka katika mamlaka za maeneo, miongoni mwa njia nyingine (sehemu ya 3(d)). Mataifa mengi (isipokuwa Uswizi, India, Ufilipino, Thailand na California) hayana Katiba inayojumuisha utaratibu wa kuwahusisha wananchi moja kwa moja katika usimamizi wa masuala ya umma. Hata hivyo ni wazi kuwa uchaguzi unaofanyika tu baada ya kipindi fulani, sio njia tosha ya kuwahusisha wananchi katika utawala. Pana haja ya kutambua njia zinazowahusisha zaidi na kila wakati.

***(h) Kupunguza na kusambaza madaraka***

Utaratibu wa marekebisho unahitajika kuchunguza na kurekebisha nafasi ya serikali za wilaya kikatiba nchini Kenya, na kiwango cha kupunguza na kusambaza madaraka katika mamlaka za maeneo. Utaratibu huo unahitajika kufikiria iwapo Kenya itakuwa na mfumo wa Kishirikisho au wa Serikali ya Umoja (sehemu 17(d)(ii)).

Kupunguza na kusambaza madaraka kunamaanisha kuwa mamlaka ya kikatiba ya serikali kuu yanapunguzwa na kusambazwa katika kiwango cha maeneo. Hii inaweza kufanyika kupitia njia tofauti tofauti; kuundwa kwa halmashauri za kuunda sheria katika kiwango

cha mashinani au kuwepo uwezo wa kufanya uamuzi na utekelezaji katika kiwango cha maeneo. Katika muktadha wa Kenya, viwango hivyo vya mashinani vinaweza kuwa mikoa, wilaya au hata katika kiwango cha chini zaidi. Kitu muhimu ni kuwa kiwango fulani cha madaraka kinawekwa katika maeneo, na kwamba uwezo huo unapasa kujumuishwa katika Katiba ili usiondolewe wakati fulani. Kupunguza na kusambaza mamlaka kwa aina fulani kunaweza kumaanisha msisitizo wa kijumla kuhusu ukatiba, uhusika na uwajibikaji wa serikali kwa umma, jambo ambalo ni rahisi kutekelezwa endapo uwezo umesongezwa karibu zaidi na umma.

***(i) Afisi na Tume za Kikatiba***

Sheria inaagiza kuwa shughuli za marekebisho zichunguze Tume na afisi zilizopo za kikatiba, na asasi ili kutoa mapendekezo ya jinsi ya kurekebisha na kupata vyombo vipya ambavyo vitasaidia katika kujenga utawala wa kikatiba na kudumisha haki za binadamu na usawa wa jinsia (Sehemu 17(d)(iii)). Mifano ya Tume za namna hii ni pamoja na Tume ya Huduma za Sheria ambayo humshauri Rais kuhusu uteuzi wa baadhi ya mahakimu, Tume ya Huduma za Umma ambayo ina majukumu ya kushughulikia uteuzi na nidhamu za wafanyi kazi wa umma, Tume ya Uchaguzi ambayo ina majukumu ya kuongoza uchaguzi wa kitaifa na wa wilayani, na Msimamizi na Mhasibu Mkuu wa Serikali ambaye jukumu lake ni kuhakikisha kuwa serikali inafuata kanuni zilizowekwa kuhusu fedha na kuongoza ukaguzi wa matumizi ya fedha. Licha ya haya, upeo wa majukumu yao pamoja na uhuru wao unaweza kuongezeka ili kuwafanya wawajibike hata zaidi. Tume mpya zinaweza kuwa pamoja na zile ambazo zitapokea na kuchunguza malalamishi kuhusu utumizi mbaya wa madaraka ya uongozi au viongozi wa umma, kutekeleza na kusimamia utetezi wa haki za binadamu, au kuendeleza haki na maslahi ya wanawake au watoto.

Katiba za kisasa zimepiga hatua dhidi ya ugawaji wa jadi wa madaraka katika viwango vya Mamlaka ya Nchi, Bunge na Mahakama kwa kubuni Tume na afisi huria hasa zinazohusu masuala nyeti kisiasa, kama vile uwekaji wa mipaka kwa maeneobunge au uongozi wa upigaji kura na maamuzi ya yanahusu mashtaka. Tume zimetumika vilevile ili kuhakikisha uwajibikaji wa mawaziri na viongozi wa umma kwa kutekeleza kanuni za

maadili na sheria dhidi ya ufisadi. Tatu, zinatumiwa ili kuendeleza uhifadhi wa haki za binadamu au Tume za usawa ambazo huchangia ulinzi unaotolewa na mahakama.

***j) Mambo Ya Kigeni Na Ushirika Wa Kimaeneo Na Kimataifa***

Sheria inaagiza kuwa Katiba ikuze na kudumisha ushirikiano wa kimaeneo na kimataifa ili kuhakikisha maendeleo ya kiuchumi, amani na usalama na pia kuunga mkono demokrasia na haki za binadamu (Sehemu 3(g)). Kimshabaha zaidi, marekebisho yapendekezwe kuhusu namna ya kuweka mikataba na utekelezaji wa mamlaka ya serikali na mambo mengine yoyote yanayodumisha utawala mwema na kuzingatia majukumu ya Kenya katika sheria ya kimataifa (17(d) (iii)). Haya yanaonyesha uwajibikaji kwa utawala wa sheria katika mahusiano ya kimataifa na yanaweka misingi ya kuimarishia majukumu ya bunge la taifa na vyombo vingine vya kitaifa kwa njia ambayo taifa huyapokea na kuyatimiza majukumu yake ya kimataifa kuwa muhimu kadri ushirikiano wa kimataifa unavyoongezeka. Kwa wakati wa sasa, Katiba haiwezi kuwa suala la kitaifa tu. Nchi nyingi zinashiriki katika mashirika ya kimaeneo na kimataifa. Ushirika huu huziwekea nchi na wananchi wake haki na majukumu yao kuhusu masuala ambayo hatimaye huingizwa katika Katiba, kama vile haki za binadamu. Namna ambavyo nchi hutimiza majukumu haya na kuyatekeleza huathiri sana sera za kitaifa na asasi zake.

### 4.2.3. Utaratibu Wa Marekebisho

***(a) Namna ya Kurekebisha***

Siri moja ambayo inaweza kusababisha kufanikiwa kwa harakati za marekebisho ya Katiba imo katika utaratibu unaofaa wa hatua za marekebisho. Hatua ya kwanza ni kuchunguza na kuafikiana kuhusu haja na kanuni za marekebisho. Kama tulivyoona, hili lilichukua muda mrefu sana kufikiwa nchini Kenya.

Hatua inayofuatia ni ya kukubaliana kuhusu mbinu za marekebisho. Kenya ilikabiliana na ubishi mkubwa kulihusu jambo hili. Kwa upande mmoja, serikali ilipendelea mwelekeo wa marekebisho kufanywa kutoka juu. Kwa mfano, ilipendelea yafanywe kimsingi na tabaka la wanasiasa, jinsi ilivyo katika bunge, na wasaidiwe na wataalamu. Raia na

viongozi wa dini nao, kwa upande mwingine, walitaka utaratibu ambao ungeongozwa na wananchi ili mwananchi wa kawaida, (ambaye hatimaye aliwakilishwa na *'Wanjiku'*), ashikilie nafasi muhimu katika kufikia maamuzi, katika kutoa maoni na katika kuteua wawakilishi wao katika mkutano wa kiatiba ili kuipokea Katiba mpya. Labda uainishaji huu unapotosha kwa sababu, marekebisho na ukubalifu wa Katiba ni vitu nyeti na vyenye mielekeo mingi inayohitaji ujuzi, vipawa na namna mbalimbali za ushirikiano.

Kuna nafasi ya wasomi, na ya watu wa kawaida; ya wataalamu na wasio wataalamu. Siri nyingine ya utaratibu mzuri imo katika usahihi wa kuwashirikisha na kuwasawazisha wote wanaohusika.

Vipengele vya msingi vya utaratibu huu ni kuandaa mswada wa mapendekezo ya marekebisho ya Katiba au Katiba mpya ambayo itakubalika. Katika hali ya kawaida, kikundi cha wataalamu ndicho ambacho huandaa mswada wa mapendekezo na kikundi cha wawakilishi kikayapokea na kuyaidhinisha, iwe ni kikundi cha wabunge au cha mkutano maalum utakaoundwa. Misingi ya uandalizi wa mswada inaweza kuwa ujuzi wa kamati (au hata wa mtu maalum), inayofanya kazi katika kiwango fulani cha uhuru wa kujitegemea au kwa kuhusisha mjadala mpana wa kitaifa ambao utatoa maoni rasmi yatakayowasilishwa kwa kikundi cha wataalamu.

Katika jadi ya kihistoria, karibu kila mahali, harakati za kuandaa Katiba, uandishi na ukubalifu wake ulikuwa umetengwa kama shughuli ya kiusomi. Hivi sasa, dhana ya uhuru wa wananchi imekita mno katika matamshi ya umma kiasi kuwa ni lazima utaratibu uwashirikishe, uwe wazi na uwajumuishe. Majukumu ya wataalamu hivi sasa ni ya kuyasikiliza maoni ya wananchi ili baadaye wayafasiri na kuyaweka katika dhana za kikatiba, kwa kuzingatia kanuni na thamani za marekebisho. Ikilazimu, ni muhimu wananchi wafunzwe mambo kuhusu Katiba kupitia elimu ya uraia, ili kuwawezesha kushiriki. Itabidi pia mswada unaotolewa na wataalamu upitiwe kwa makini na wananchi kabla ya kuwasilishwa bungeni au kwa kikundi maalum kilichoteuliwa. Hatimaye, ni lazima wananchi wauidhinishe mswada kupitia kura ya maoni au kwa kuyapigia kura masuala ambayo yatakuwa hayajasuluhishwa moja kwa moja katika vikao maalum

(mwelekeo huu wa kura ya maoni ambao umekadiriwa ulikuwepo Afrika Kusini na Uganda, ingawa katika hali zote mbili kura ya maoni iliepukika kwa sababu ya makubaliano ya kuridhisha yaliyofikiwa katika mikutano hiyo).

Umuhimu unaowekewa kushiriki kwa wananchi unatokana na hali ya Katiba kuwa ni mkataba baina ya wananchi kuhusu utawala. Faida za kushiriki kwa umma ni pamoja na:

- kuongeza uelewa wa watu kuhusu masuala ya kikatiba;
- kuwawezesha wananchi kuizoea Katiba mpya;
- kuandaa ajenda inayofaa ya marekebisho (uhusika wa umma huwa na mwelekeo wa kuipanua ajenda hasa kuhusu masuala ya haki za kijamii);
- kuwawezesha wananchi kutekeleza haki zao na kutimiza wajibu wao uliomo katika Katiba;
- Kufaulisha utekelezaji wa Katiba;
- Kuhakikisha uhalali wa Katiba mpya na ukubalifu wake kama mwongozo wa kukuza makubaliano kuhusu uundaji na utekelezaji wa sera za kitaifa na usuluhishaji wa tofauti zozote.

Sheria ya Marekebisho, kwa vile ilivyozidi kubadilishwa, hivi sasa inatosheleza kwa kiasi kikubwa kanuni za uandalizi wa Katiba.

Ni muhimu kuzisisitiza baadhi ya kanuni za msingi zinazohusu utaratibu unaohitajika katika Sheria hii. Mwanzo ni kuwa, utaratibu wa marekebisho uwe ni wa kueleweka. Hii inamaanisha kuwa licha ya maadili na asasi maalum zinazotajwa katika sheria ya marekebisho na ambazo zinahitaji kuchunguzwa, ikiwezekana, pawe pia na fursa ya kuyachunguza masuala mengine.

Pili ni kwamba, ni lazima utaratibu huu uwe jumuishi na unaotambua hali mbalimbali za Wakenya, ‘ikiwemo hali za kijamii na kiuchumi, rangi, kabila, jinsia, imani za kidini, umri, kisomo, ulemavu na hali ya kutobahatika.’ (Sehemu 5(b)). Tuliona kuwa, kuundwa kwa vyombo vya Marekebisho kumelenga umuhimu wa kutambua wingi wa tofauti hizi.

Muungano wa Tume mbili mnamo Juni 2001 ulifanya nia ya marekebisho kulikaribia lengo hili.

Tatu ni kwamba, utaratibu uwe wa *wazi, wa kidemokrasia na wa kuwajibika* kwa umma (Sehemu 5(a) na (c)(ii)). Mikutano ya Tume ya kupokea mapendekezo ya umma ni lazima iwe katika vikao vya wazi (Sehemu 21(3)).

Ni lazima kumbukumbu za Tume ziufikie umma kupitia maktaba ya umma, vituo vya nyaraka na vyombo vingine vya habari (Sehemu 22). Ni lazima utaratibu wo wote wa marekebisho uongozwe na heshima kwa kanuni za ulimwengu za haki za binadamu, usawa wa kijinsia na demokrasia (Sehemu (5)(c)(iii)).

Nyongeza ya tatu ya Sheria hii inaainisha Kanuni za kuwepo Utaratibu Thabiti wa Kidemokrasia kuhusu Marekebisho ya Katiba ambao Serikali, vyama vya kisiasa, mashirika yasiyokuwa ya serikali, Wakenya na vyombo vya marekebisho vimedhamiria kuzingatia (Nyongeza hii imenakiliwa mwishoni mwa sura hii).

Kanuni hizi zilitambua umuhimu wa kujenga makubaliano ya kitaifa kuhusu utaratibu wa marekebisho. Pia, kanuni hizi zinaafikiana kuhusu kutoshiriki matumizi ya nguvu, wala kutishia matumizi ya nguvu, au vitendo vingine vya uchochezi wakati wa marekebisho, na kutomnyima wala kuziingilia haki za mwananchi za kuitisha au kushiriki mkutano wa umma na mikutano mingine au haki na aina nyingine za uhuru.

Nne ni kwamba utaratibu mzima utegemee makubaliano baada ya maoni yote kutolewa kwa uwazi na uhuru. Hii ni ili kuhakikisha kuwa utaratibu huu na matokeo yake unaungwa mkono kwa wingi iwezekanavyo na mwananchi wa Kenya. Licha ya hayo tuliyoyaorodhesha, kanuni za mamlaka katika vyombo vya marekebisho zinahitaji kuashiria umuhimu wa makubaliano. Ni lazima uamuzi kuhusu mabadiliko ya kikatiba ufanywe kwa makubaliano lakini endapo hakutakuwa na makubaliano katika kiwango cho chote, uamuzi ufikiwe na makubaliano ya thuluthi mbili za washiriki wote wa asasi husika (Sehemu 21(6) ya Tume na Sehemu 27(5) ya Kongamano na Sehemu 47 ya

Katiba ya Bunge). Hali ya kusisitiza makubaliano inaonyesha mwelekeo kuwa ni lazima Katiba iwe ya kukubalika na wengi kote nchini kwa sababu ndiyo msingi wa utawala, sheria na sera ambazo zinawahusu Wakenya wote. Endapo maamuzi yatafikiwa kwa makubaliano, umoja wa kitaifa pia utaimarika.

Tano ni kwamba umuhimu wa hali ya juu umewekewa uhusika wa umma. Ni lazima chombo cha marekebisho kiwawezeshe wananchi kushiriki moja kwa moja, kwa njia huru na kwa kuchangia katika kuibua na kujadili mapendekezo yatakayolenga kuibadilisha Katiba (Sehemu 5(d)).

Kanuni hizi, ambazo ni za msingi kwa utaratibu wa marekebisho, ni muhimu si tu katika kuhakikisha kuwepo kwa matokeo mazuri na ya kukubalika bali pia katika kuibua mienendo ya mijadala ya haki na yenye ufahamu ili kuondoa utengano uliopo katika jamii na kusuluhisha tofauti kwa kuhusisha mazungumzo na mapatano, na kuimarisha umoja wa kitaifa na dhamiri ya kitaifa ya kutambua na kuzingatia matatizo yanayoikabili Kenya.

Endapo utaratibu huu utayatimiza malengo haya, utakuwa umeweza kuchangia katika uwekaji wa mazingira bora na utamaduni wa kisiasa ambamo Katiba mpya itakita na kunawiri.

***b) Vyombo Vya Marekebisho***

Sheria ya Marekebisho inaidhinisha kuwepo kwa vyombo kadha vya marekebisho na kuvipatia majukumu na uwajibikaji maalum. Vyombo hivi ni:

- Tume ya Marekebisho ya kikatiba ya Kenya (Tume au CKRC)
- Baraza la kikatiba la Maeneobunge
- Kongamano la kikatiba la Taifa
- Kura ya Maoni
- Bunge

*(i) Tume*

Tume ambayo ni chombo cha msingi cha marekebisho ya Katiba ina Wanatume, (wawili wao, Mkuu wa Sheria na Katibu wa Tume wakiwa washiriki kwa ajili ya nyadhifa zao). Wanatume wateuliwe na Raisi baada ya kupendekezwa na Bunge. Raisi atamteua mwenyekiti kutokana na Wanatume. Tume inahitaji kuwakilisha tofauti zilizomo nchini Kenya kwa mujibu wa makabila, maeneo ya kijiografia, tamaduni, siasa, jamii, uchumi, na kuzingatia kanuni za usawa wa kijinsia (Sehemu 6(5)).

Pia Wanatume wateuliwe kwa kuzingatia ustahiki wao au tajriba zao katika masuala ya umma (Sehemu 8(i) na (b)). Tume inatarajiwa kuwa huria na haiwezi kushurutishwa na mwingine ye yote ambaye atayachukua majukumu yake. Muda wa kudumu kwa Wanatume ni mpaka pale ambapo utaratibu wa marekebisho utakamilika (Sehemu 33). Wanatume wanaweza tu kufukuzwa na Tume yenyewe kwa sababu ya malengo yenye nia njema (Sehemu 15). Wanatume wanawekewa mipaka na kanuni za maadili ili kuzuia mizozo na usumbufu mwingine wo wote. Vigezo hivi ni muhimu ili Tume iweze kutekeleza wajibu wake ambao ni wajibu mkuu wa kuandaa mswada wa Katiba.

*(ii) Baraza la Kikatiba la Eneobunge*

Mabaraza ya kikatiba ya maeneobunge yaliwekwa kwa kila eneobunge ili kuwezesha mijadala, mazungumzo, ukusanyaji na ulinganishi wa maoni ya wananchi (Sehemu 20). Mabaraza haya pia yaliweka misingi ya kushauriana na Tume. Tume ilifaulisha uundaji wa mabaraza haya lakini ushiriki na miundo ya mabaraza haya uliamuliwa na wananchi katika maeneobunge wakishirikiana na viongozi wao wa kisiasa na wengineo.

*(iii) Kongamano la Taifa kuhusu Katiba*

Kongamano la taifa kuhusu Katiba (Kongamano kuhusu Katiba) ndicho kitakachokuwa chombo cha kujumuisha tofauti zipatikanazo nchini Kenya. Majukumu yake ni kuwezesha makubaliano kuhusu Katiba. Kongamano hili lina washiriki 629.

- Wabunge 223
- Wawakilishi wa wilaya walioteuliwa na mabaraza ya wilaya 210

- Wanatume ( kama washiriki wasiopiga kura) 29
- Wajumbe 42, kila mmoja akiwakilisha chama cha kisiasa.
- Wawakilishi wa dini, wataalam, makundi ya wanawake, vyama vya wafanyi kazi na mashirika yasiyo ya serikali (Sehemu27(2)) na wengine watakaoteuliwa kwa mujibu wa masharti yatakayowekwa na Tume, 125

*(iii) Kongamano la Kura ya Maoni*

Kongamano la kura ya maoni ni kama uchaguzi mkuu lakini badala ya kuwapigia kura watu ili wawawakilishe, wapiga kura wanatoa maoni kwa masuala maalum. Kongamano la kupiga kura litaitwa tu ili kuamua masuala ambayo yatakuwa hayajaamuliwa katika Kongamano La Taifa Kuhusu Katiba.

*(iv) Bunge*

Hatimaye Bunge litatekeleza mabadiliko yatakayoifanya Katiba kuwa sheria. Litasaidiwa na kamati teule ya Marekebisho ya Katiba (Sehemu 10).

*(v) Hatua Za Marekebisho*

Sheria ilitaraji kuwa utaratibu wa marekebisho ufuate hatua saba ambazo zimeelezwa kwa undani katika juzuu II ya ripoti hii. Hizi ni:

*Hatua I: Elimu ya Uraia: kuwatayarisha Wananchi ili Washiriki*

Hatua ya kwanza ilikuwa ya kuwaandaa Wanatume na wananchi kwa marekebisho. Ilibidi Tume ichunguze agizo lake, uadilifu na kanuni za kufanya kazi. Haya yangewawezesha kufaulisha utekelezaji wa elimu ya uraia ili kuweza kuchochea mijadala ya umma na ufahamu wa masuala ya kikatiba (Sehemu 17(a)).

Wananchi wangewezeshwa kuelewa na kujadili Katiba iliyopo na pia kupata uzoefu wa Katiba za nchi nyingine (Sehemu 17(c)). Hali ya kuwafahamisha wananchi kuhusu masuala ya kikatiba na maendeleo ya marekebisho ya Katiba yangefaulishwa na uwekaji wa Vituo Vya Nyaraka katika kila wilaya, (Sehemu 23) pamoja na matumizi ya vyombo

vya kimtambo. Wanatume walitimiza hatua hii ya agizo lao kupitia mseto wa juhudi zao wenyewe na pia kupitia elimu iliyotolewa na wengine.

*Hatua II: Utafiti, usomaji na Semina: kufafanua masuala*

Tume ilifanya utafiti mwingi kuhusu masuala ya kikatiba, kijamii na kisiasa, ili kufafanua na kuanza kutekeleza agizo. Pia Tume ilifanya semina nyingi na yaliyotokea yanapatikana katika Juzuu la 5 taarifa ya Tume.

*Hatua III: Ushauri wa Umma: Kuwasikiliza Wananchi*

Kisha ulifuata ushauri baina ya Tume na wananchi ili kupata maoni na mapendekezo yao kuhusu mabadiliko ya kiKatiba kwa njia ya moja kwa moja na pia kupitia mashirika na makundi maalum. Tume ilitakikana kutembelea kila eneobunge (Sehemu 18(1)(a)) na pia kuandika memoranda au mawasilisho ya kimasimulizi kutoka kwa Wakenya katika sehemu za miji na za mashambani. Baada ya kushauriana, Tume ilitakikana kuandaa taarifa na mapendekezo, ukiwemo mswada wa sheria ya kubadilisha Katiba (Sehemu 26(7)).

Sheria ilihitaji kuwa taarifa ya Tume na mapendekezo yake yawakilishe maombi ya wananchi jinsi yalivyowasilishwa kwao (Sehemu 5(d)). Ujuzi na uhuru wa Tume unatakikana kuhakikisha kuwa malengo ya marekebisho jinsi yalivyo katika Sheria, yanazingatiwa na pia kuwa maslahi ya taifa yanapewa umuhimu kuliko maslahi ya vyama na ya vikundi vingine vidogo vidogo.

*Hatua III: Kuandika Taarifa na Kutayarisha Mswada wa Sheria*

Tume iliagizwa kuyafafanua na kuyalinganisha maoni ya umma na kwa misingi ya maoni haya iandike ripoti na kutayarisha mswada wa sheria ambao utaibadilisha Katiba. Sambamba na utekelezaji wa agizo hili, Tume iandae mpango wa uchanganuzi ambao utaiwezesha kuchanganua data yote iliyoipata na kuiwasilisha katika viwango vya kitaifa, kimkoa, wilaya na maeneobunge.

*Hatua IV: Kujadili ripoti ya Wanatume na Mapendekezo*

Hatua ifuatayo ya marekebisho ilihusu usambazaji wa ripoti, mapendekezo na mswada wa sheria uliotayarishwa na Tume kwa umma na kuendeleza elimu ya umma.

## 4.3. <u>HITIMISHO</u>

Sheria ya Marekebisho ya Katiba ni mojawapo ya mifumo ya kisheria ya urekebishaji Katiba iliyo na undani wa maelezo inayopatikana kokote ulimwenguni. Utaratibu ambao tumeueleza unasisitiza uhuru na hali ya kujitawala ya mfumo wa marekebisho. Sheria inabainisha muundo na majukumu ya vyombo tofauti vya marekebisho. Inapendekeza ratiba za aina tofauti katika utekelezaji wa kazi. Chombo huria mno miongoni mwa hivi, ambacho ni Tume, kina majukumu ya kuhakikisha kuwa taratibu na ratiba iliyowekwa vinafuatwa. Mara tu taarifa yao na mswada wa Katiba vitakapokuwa tayari, vipelekwe moja kwa moja kwa bunge bila kupitia kwa serikali. Taarifa, (na nyaraka nyinginezo) za Tume zitatolewa moja kwa moja kwa wananchi. Nafasi maalum na ya msingi imetolewa kwa wananchi katika utaratibu huu. Malengo ya marekebisho – demokrasia, utawala wa sheria, msambao na uwajibikaji wa mamlaka ya nchi, utetezi wa haki na uhuru, kutimiza mahitaji ya kimsingi ya Wakenya wote – yanaungwa mkono na wananchi. Kinachosisitizwa kila mahali ni masikilizano.

# SURA YA TANO

## MUKTADHA WA MAREKEBISHO KIJAMII, KIUCHUMI NA KISIASA

### 5.1 Kufafanua Muktadha

Utaratibu wa Marekebisho ya Katiba ulifanywa wakati wa matatizo makubwa ya kijamii, kiuchumi, na shinikizo la kisiasa katika viwango vyote vya serikali. Ijapokuwa matatizo mengi yalisababishwa na usimamizi dhaifu wa kiuchumi na utawala mbaya kwa muda wa miongo kadhaa, ujumla wa hali na kuzorota kwa uchumi Afrika pia vilichangia kwa kiasi kikubwa. Katika sura hii tunachunguza mielekeo muhimu ya shinikizo hili kama dhihirisho la hofu na matarajio yaliyowasilishiwa Tume na Wakenya, kwenye utaratibu wa mawasilisho katika vikao vya hadhara na uwasilishaji wa memoranda.

### 5.2 Muktadha wa Kijamii

Muelekeo muhimu wa shinikizo umebakia ule wa mazingira ya kijamii ambamo maslahi ya maisha hugombaniwa na kusuluhishwa. Mambo muhimu ya kuzingatia hapa yanahusu maslahi ya kijamii, uhifadhi wa chakula, afya na matibabu, elimu na makao.

#### 5.2.1 Maslahi ya Jamii

Ingawa lengo muhimu zaidi la serikali lilikuwa kupata mahitaji ya kimsingi ya huduma za jamii kufikia mwisho wa 2015, ni dhahiri kwamba lengo hili halitaweza kufikiwa. Kwanza, matumizi ya fedha katika sekta ya kijamii, kama asilimia ya Jumla ya Pato la Taifa (GDP) yamekuwa yakipungua haraka katika kipindi cha miaka kumi iliyopita. Tena uwekezaji wa kila mwaka katika sekta ya kijamii umepungua. Awali ya marekebisho ya kiuchumi, serikali ilitoa vipengele vilivyoahidi usalama wa maskini. Ahadi hii haikujiri kwa sababu ya utekelezaji mbaya wa kiuchumi na kupungua kwa fedha za kutoka nje. Utafiti uliofanywa mwaka wa 1998 na serikali kuhusu *Huduma za Msingi za Jamii Kenya*, ulidhihirisha upungufu wa matumizi ya wananchi katika huduma msingi za jamii

kutoka asilimia ishirini (20%) mwaka 1980, hadi asilimia kumi na tatu (13%) mnamo mwaka 1995. Hisa ya matumizi ya serikali kwa huduma msingi za jamii katika Jumla ya Pato la Taifa, (GDP) ilipungua kutoka asilimia tano (5%) mwaka 1980 hadi takriban asilimia nne na nukta tano (4.5%) mwaka 1995. Matokeo yamekuwa ni kuongezeka kwa ukiukaji wa haki za binadamu, rushwa na vitendo vya kigaidi, pamoja na kutovumiliana kijamii na kidini, na visa vya vita vya kikabila.

### 5.2.2 Uhifadhi wa Chakula

Haja ya kuangamiza njaa ilitambuliwa mara tu baada ya uhuru katika makala ya *Kikao Na.10 (Sessional Paper No.10)* cha 1965. Makala yalieleza kwamba njaa itamalizwa tu kwa njia ya kuongeza uzalishaji wa chakula na kushughulikia maslahi ya nchi yanayojumuisha ngawo wa ardhi, kuunganisha watu, uhamisho na makao mapya ya kuishi. Makala ya Kikao Na. 1 (Sessional No.1) cha 1986 kuhusu *Usimamizi wa Uchumi kwa Maendeleo Mapya ya kuichumi*; *Uhifadhi wa Chakula kwa Familia na Sera ya Lishe Bora ya 1988;* pamoja na *Mpango wa Maendeleo ya Taifa 1984-1988* (National Development Plan 1984-1988) yalitambua umuhimu wa kushughulikia masuala ya uhifadhi wa chakula mashinani. Uchanganuzi wa awali na wa sasa unaonyesha hivi, ijapokuwa Kenya imedhibiti uwezo wa kulisha watu wake; kuzalisha chakula cha ziada kwa soko na kujitosheleza upande wa vyakula kwa jumla, bado sehemu kubwa ya idadi, ya watu wamebaki na njaa na katika hali ya utapiamlo. Hata mapato ya ziada katika ongezeko la jumla la vyakula hayakugawanywa kwa usawa. Kiasi cha sehemu isiyopuuzika ya idadi ya watu wana tajriba ya ukosefu mwingi wa chakula na kutokuwa na malisho bora. Kwa ajili hii, visa vinavyoongezeka vya njaa kali, utapiamlo na ukosefu wa chakula, vimebaki kama tisho dhidi ya juhudi zinazolenga kufanikisha shabaha lengwa za maendeleo ya kitaifa na kumaliza njaa.

Usugu wa kutokuwa na lishe bora umedhihirishwa na tofauti za asilimia thelathini na mbili na nukta moja (32.1%) mwaka 1987, hadi asilimia thelathini na nne (34%) mwaka 1988 *(Mpango wa Maendeleo ya Taifa 1997 – 2001), [National Development Plan 1997-2001].* Kulingana na pendekezo la Shirika la Chakula na Kilimo la Ulimwengu Shirika

La Afya la Ulimwengu (FAO/WHO), kuhusu kipimo kinachokubalika cha kalori 2250 kwa siku kwa mtu mzima, kisa cha umaskini wa chakula kilikadiriwa kuwa asilimia hamsini na moja (51%) katika sehemu za mashambani na asili mia thelathini na nane (38%) katika sehemu za mijini mnamo mwaka wa 2000 [Wizara ya Fedha na Mipango (Ministry of Finance and Planning 2000)]. Kenya imeshuhudia ongezeko la kiasi katika utumiaji wa kila siku wa kalori kwa mwaka; kutoka kalori 1887 kwa siku mnamo 1990 hadi kalori 1968 kwa siku mwaka wa 1998; lakini bado iko chini sana ya kiasi kinacholengwa cha kalori 2300 kwa siku.

Ingawa ukosefu wa uelekevu wa kisera umelaumiwa kwa ajili ya kuzorota kwa uhifadhi wa chakula na hali ya lishe bora nchini Kenya, bado athari za maskini zinatatanisha zaidi kwa ajili ya uzorotaji wa uwekezaji katika sekta ya kilimo. Kenya haina vyakula vya ziada tena kwa manufaa ya kujikinga na athari za ukosefu wa mazao kutokana na hali zinazogeukageuka za anga zinazosababishwa na ukame, mafuriko na hali mbaya ya anga kwa jumla. Tena, ongezeko la haraka katika gharama ya vifaa vya kilimo limesababisha upungufu katika uzalishaji wa chakula.

### 5.2.3 Afya na Matibabu

Mwanzoni mwa miaka ya 1980, ilikuwa wazi kwamba siasa zilizoshughulikiwa na serikali zilielekea moja kwa moja katika uboreshaji wa hali ya afya ya Wakenya. Takwimu jumuishi zilionyesha kwamba idadi isiyosawazishwa ya vifo ilipungua wakati wa uhuru kutoka watu ishirini (20) kwa kila elfu moja (1000) hadi kumi na mbili (12) kwa kila elfu moja (1000) mwaka wa 1993, na idadi isiyo-sawazishwa ya kuzaliwa ilipungua kutoka watu 50 kwa kila elfu moja (1000), hadi 46 kwa kila elfu moja (1000) kwa muda wa kipindi hicho. Hali kadhalika vigezo vya kimsingi vya hali ya afya vimeonyesha maendeleo mazuri kuhusu idadi ya vifo vya watoto wachanga na muda wa kuishi (Wizara ya Afya 1994) [Ministry of Health 1994], vikiambatana na upanuzi mkubwa wa miundomsingi ya afya. Hivyo kulikuwa na matumaini mengi ya kufikia lengo la Afya kwa Wote kufikia mwaka wa 2000.

Tajiriba za miaka ya 1990 zilionyesha uzorotaji wa hali ya afya kwa sababu ya matokeo ya hali ngumu ya magonjwa ya mlipuko, jamii, uchumi, siasa na mambo ya utandawazi, yaliyoleta matatizo katika mahitaji na huduma za afya. Hivi sasa, Kenya imeorodheshwa kama nchi mojawapo ulimwenguni iliyo na hali mbaya zaidi ya afya na utoaji wa huduma za afya ya umma. Kiasi cha idadi ya vifo vya watoto kimeongezeka kutoka watoto 70 kwa 1000 waliozaliwa hai mwaka 1990, hadi 76 kwa 1000 ya watoto waliozaliwa hai mwaka 1999. Lengo lilikuwa ni kupunguza kiasi cha idadi hadi 47 kwa 1000 kufikia mwaka wa 2000, chini ya shabaha iliyolengwa ya 50 kwa 1000. Kiasi cha idadi ya vifo vya watoto waliochini ya miaka mitano (5) kiliongezeka kutoka 97 hadi 1000 mwaka wa 1990 na kuendelea hadi 118 kwa 1000 ya watoto waliozaliwa hai. Kiasi hiki kiko chini ya shabaha lengwa ya ulimwengu ya 70 kwa 1000 watoto waliozaliwa hai kufikia mwaka wa 2000. Shabaha iliyolengwa ya mwaka wa 2015 imewekewa kiasi cha 39 kwa 1000 cha watoto waliozaliwa hai.

Kiwango cha vifo vya kina mama nchini Kenya ni takriban 549 kwa 100,000 kwa watoto wanaozaliwa hai, kikilinganishwa na kiasi wastani ulimwenguni cha 193 kwa 100,000 cha watoto waliozaliwa hai. Kenya ina lengo la watoto 295 kwa 100,000 kwa mwaka wa 2000 na 148 kwa 100,000 kufikia mwaka wa 2015.

Asilimia thelathini (30%) ya magonjwa yanahusiana na malaria. Serikali imejitolea kupunguza vifo na maradhi yanayosababishwa na malaria kwa angalau asilimia thelathini (30%) ya kiwango cha mwaka wa 1995, kufikia mwaka wa 2004. Magonjwa ya malaria na yale yanayohusiana na upumuaji kwa jumla yanachukua asilimia hamsini (50%) ya ripoti za waliopimwa katika vituo vya afya. Ugonjwa wa kuhara umezidisha asilimia hii hadi asilimia sitini (60%) *(Mpango wa Maendeleo ya Taifa 1997-2002 [National Development Plan 1997-2001]).* Matatizo ya ujauzito na afya ya kina mama yanachukua kiasi cha asilimia ishirini na saba (27%) ya mzigo wote wa magonjwa, yakichunguzwa kwa mujibu wa masharti ya miaka ya uhai iliyopotea

Kama ilivyokadiriwa, Wakenya wanaopata milioni 2.2 wanaishi na Virusi vya UKIMWI (V.V.U), ambapo karibu watu 700 wanakufa kwa ugonjwa huo kila siku. Kwa sasa Virusi

vya UKIMWI vimeenea kiasi cha asilimia saba (7%) miongoni mwa watu wazima. Katika maeneo ya mijini maenezi yake yanakadiriwa kuwa kati ya asilimia kumi na mbili, na kumi ya tatu (12-13%). Ilipotambua matatizo yanayoongezeka kuhusu UKIMWI na Virusi vya UKIMWI, Serikali ya Kenya ilitangaza hali ya hatari kuhusu UKIMWI mwishoni mwa mwaka wa 1999. Kipindi cha kuishi na UKIMWI kilipungua kutoka miaka 60 mnamo mwaka wa 1993 hadi takribani kiasi cha hivi sasa cha miaka 47. Kuja kwa UKIMWI na Virusi vya UKIMWI kuliongeza tatizo la kifua kikuu (TB) nchini Kenya. Watu waliopata virusi vya UKIMWI hushikwa na kifua kikuu (TB) kwa urahisi. Kenya ni miongoni mwa nchi 22 zilizogandamizwa zaidi. Nchi hizi zina jumla ya visa asilimia themanini (80%) vya kifua kikuu (TB) ulimwenguni.

### 5.2.4 Elimu

Serikali imetangaza msimamo wake wa kujitolea kuelimisha na kutoa kiasi cha asilimia themanini na saba nukta mbili (87.2%) cha matumizi yake ya jamii kwa minajili ya elimu ya kimsingi. Licha ya tangazo wazi la sera ya serikali kuhusu Elimu kwa Wote (EFA), nafasi ya wote kupata elimu imekuwa ikipungua.

Katika miaka ya 1990 usajilishaji wa jumla katika shule za msingi ulipungua kimaeneo kwa kipindi fulani, kutoka kiasi kikubwa cha kawaida cha asilimia tisini na tano (95%) mwaka 1989 hadi asilimia themanini na nane nukta tisini na moja (86.91%) mwaka 1999. Usajilishaji ulipungua kutoka asilimia tisini na mbili nukta kumi na tisa (92.19%) mwaka 1990, hadi asilimia themanini na saba nukta themanini na nne (87.84%) mwaka 1993 na asilimia sabini na nane (78%) mwaka 1996. Hii inamaanisha kwamba watoto wengi waliofikia umri unaofaa kwenda shuleni bado wako nje ya shule.

Hali kadhalika, kiasi cha wanaotoka shule kabla ya kuhitimu imeongezeka. Kwa mfano, ni asilimia arobaini na tatu nukta moja (45.1%) ya wavulana wote waliosajiliwa na kungia darasa la kwanza mwaka 1989, ndio waliomaliza darasa la nane mwaka 1996. Kiasi cha wanafunzi wanaomaliza shule kimebakia chini ya kiasi cha asilimia hamsini (50%).

Ingawa pengo la kijinsia katika kiwango cha shule za msingi limekaribia kuzibwa katika ujumla wa kujiandikisha wa kiasi cha asilimia arobaini na tisa (49%), na asilimia hamsini na moja (51%) ya wasichana na wavulana kama ilivyo, ni asilimia thelathini (30%) tu ya wanawake, ndio wanaojisajilisha na kuingia vyuo vikuu vya kitaifa. Usajilishaji katika shule za sekondari pia umebakia wa chini kiasi cha asilimia ishirini na mbili nukta nane (22.8%). Wanafunzi wengi wa shule za msingi hawaendelei na elimu ya juu kwa sababu ya umaskini na nafasi chache katika shule za sekondari za Serikali. Kati ya miaka ya 1960 na 1980, serikali ilitoa fedha za usaidizi wa elimu kwa njia za vitabu na vifaa. Msaada huu uliziwezesha familia kuwaacha watoto wao waendelee na masomo.

### 5.2.5 Makao

Katika kipindi cha mwongo mmoja uliopita, idadi ya watu mijini iliogezeka kutoka milioni tatu na elfu mia nane (milioni 3.8) mwaka 1989 hadi milioni tisa na elfu mia tisa (milioni 9.9) mwaka 1999. Hiki ni kiasi cha asilimia thelathini na nne (34%) cha idadi yote kwa jumla. Idadi ya watu wa mijini yakadiriwa kuongezeka hadi milioni 16 kufikia mwaka 2005. Matokeo ya uanzishaji wa miji haraka umezua matatizo makubwa hivi sasa nchini na kuongezeka haraka kwa makao yasiyo rasmi, hali ya kutokuwa na usalama na ukaidi, uharibifu wa mazingira na uzorotaji wa viwango vya afya ya umma.

Licha ya haya, shughuli za maendeleo ya makao na makazi ya binadamu bado hazijapewa umuhimu wowote. Katika makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Serikali ya miaka ya 1990, makao kawaida hayakupata zaidi ya asilimia moja (1%). Jambo hili inasemekana limetokana na ukosefu wa sera ya wazi ya usimamizi wa miji, pamoja na sheria za jadi tatanishi, zisizotosheleza za kudhibiti maendeleo na mikakati.

Katika miongo mitatu iliyopita, utekelezaji wa sekta ya makao nchini Kenya haukuwa wa dhati. Data inayopatikana yaonyesha kwamba zaidi ya asilimia hamsini (50%) ya idadi ya wanaoishi huishi katika makao yasiyokuwa rasmi na yanayochukua kiasi cha asilimia tano (5%) cha ardhi ya makao. Sehemu hii ya idadi ya watu huishi katika hali ambazo ni

hatari kwa afya, na zenye msongamano na mazingira ya hatari. Vitengo vya nyumba za mijini, nyumba asilimia sitini hadi themanini (60-80%) huwa ni za sekta isiyokuwa rasmi na nyingi yazo zina upungufu wa miundomsingi.

Karibu asilimia sitini (60%) ya vitengo vya nyumba mpya vilijengwa kwenye ardhi isiyokuwa na hati za kumiliki na upangaji ni asilimia themanini (80%). Ufadhili rasmi wa kifedha (matumizi ya fedha) unaohitajika kwa nyumba za mijini ni asilimia ishirini (20%) tu, ambapo asilimia themanini (80%) iliyobakia inafadhiliwa kwa njia zisizo rasmi. Data inayolingana na hii kuhusu makao ya mashambani haipo ingawa hali za ujenzi ni mbaya zaidi ya zile za mijini.

## 5.3 Muktadha wa Utamaduni

Mazingira ya kijamii yaliyofafanuliwa hapo juu yameongezwa utata na wingi wa tamaduni zinazopatikana nchini Kenya. Hakuna takwimu zinazolingana, lakini yasemekana kwamba Kenya ina zaidi ya makabila 70 yaliyogawanyika katika makundi 42. Makundi haya yanadhihirisha wingi wa tamaduni, historia, eneo, itikadi, lugha na dini.

Ingawa tangu jadi makabila yameishi pamoja kwa mapatano na kuheshimiana, hivi karibuni utamaduni wa kikabila umeingizwa katika siasa, jambo ambalo limeleta ugomvi na vita baina ya makabila katika sehemu nyingi za nchi. Ugomvi huo ni miongoni mwa tofauti za kihistoria zinazotokana na mbinu za utawala wa utengano ulioendelezwa na mamlaka ya wakoloni.

Kwa mfano tofauti za kufanikisha maendeleo ya kisiasa kwa njia ya elimu na ajira wakati wa ukoloni na baada ya kipindi cha ukoloni zimetumiwa kuleta uchochezi baina ya makabila. Hili limeleta matatizo ya mielekeo, dhana na dhuluma miongoni mwa maeneo ya kitamaduni, na hata hisia za chuki na utengano za makabila ya walio wachache miongoni mwa baadhi ya jamii.

Madaraka ya kisiasa tangu uhuru yamekuwa yakitahadharisha kuwa ukabila ni hali ya kuhatarisha umoja wa taifa inayoweza kutumiwa vibaya ili kuleta ugomvi, mgogoro na hata vita vya wenyewe kwa wenyewe. Tena serikali mpya ilipochukua wananchi kama kitengo maalumu cha utaratibu wa serikali, haikutambua makabila kama sehemu muhimu ya maisha ya jamii katika kujieleza kisiasa. Sasa, na hata zama hizo, uananchi unaonekana kama kipengele kinacholeta uhusiano moja kwa moja baina ya mtu na serikali. Kanuni ya msingi ya serikali ni urasmi wa usawa wa wananchi wote kama watu binafsi, wala si wa kijamii. Kwa sababu tamaduni za kitaifa zilionekana kuwa pingamizi za kuleta umoja wa taifa na maendeleo ya kisasa, serikali ilisisitiza ubinafsi na umuhimu wa kitengo cha utaifa mbali na kuwepo kwa wingi wa tamaduni na haki za jamii. Matokeo ni kwamba hakuna kanuni maalum zilizowekwa kwenye Katiba, ama katika sheria nyinginezo, kuhusu haki za mila kuambatana na sera ya kabila, lugha na utamadunin, na kwa hivyo hapana utamaduni dhahiri unaotambulisha na kujumuisha kitaifa. Hata kuvaa mavazi ya kitamaduni mahali "rasmi" kama vile Bunge kulipigwa marufuku.

Asasi za utawala wa kitamaduni kama vile mabaraza ya wazee, zimepuuzwa, kudhalilishwa na kutohimizwa. Kutovumiliana kitaifa kunadhihirika katika baadhi ya kanuni za sera na sheria, kuhusu shughuli za kiuchumi na kitamaduni kama vile uchungaji wa kuhamahama, uwindaji na ukusanyaji.

Hata hivyo, kuna mwamko mkubwa kuambatana na utaratibu wa marekebisho nchini Kenya unaothibitisha mazoea itikadi na imani za watu kuwa sehemu muhimu katika ujenzi wa mfumo changamano wa utawala wa vyama vingi vya, taifa la kidemokrasia, kama kule kustawisha na kuonyesha dhahiri jinsi Kenya inavyojita-mbulisha kibinafsi kama taifa huru. Kwa ajili hii lengo mojawapo 'la Sheria ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya ni kuhakikisha heshima kwa wingi wa makabila na maeneo, na haki za jamii, pamoja na haki za jamii za kupanga na kushiriki katika shughuli za kitamaduni na kujitambulisha dhahiri. Ni katika mwelekeo huu ambapo utaratibu wa marekebisho hauna budi kutazama:

- Kaida za tabia za jamii zilizoambatanishwa na mila, sheria na imani ambazo zinaweza kuwa pingamizi kubwa katika kupata ufanisi wa maendeleo ya kitaifa;
- Kaida za kitamaduni na kimaadili zonazoweza kukusanywa na kutumiwa kwa maendeleo ili miongozo iliyopendekezwa ya utawala na maendeleo, iweze kuongozo utaratibu wa marekebisho na mabadiliko;
- Kuweka wazi mipaka ya wajibu wa serikali na jamii na kaida za kitamaduni. Mipaka hii itachochea na kufaulisha hali ya kusisimua maisha ya taifa, jamii, uchumi, siasa na maendeleo ya nchi.

## 5.4 <u>Muktadha wa kiuchumi</u>

Katika shina la shida za jamii ya kisasa, kitamaduni na kijamii, pameibuka uzorotaji mwingi katika sekta za uchumi. Katika mwongo wa kwanza wa uhuru, Kenya ilijipatia sifa tunu kama nchi iliyoendelea kwa haraka na kuwa na usimamizi bora zaidi, wa uchumi katika eneo hili. Kwa kweli Kenya ilikuwa kiwango sawa na mababe wa Asia waliojikita miongoni mwa mataifa mapya yanayotegemea mfumo wa viwanda. Kuongezeka haraka kwa Jumla ya Pato la Taifa (Gross Domestic Product - GDP) ulio na kiwango wastani cha asilimia saba (7%) kwa mwaka kulifanikisha maslahi ya wananchi. Ni dhahiri kwamba uchumi unaendeleza uwezo halisi wa wananchi wa ununuzi kwa kiasi cha asilimia tatu (3%) kila mwaka. Pamoja na uwezo huu ni kuongezeka kwa Jumla ya Pato la Taifa (GDP) kwa asilimia saba (7%). Hii ni zaidi ya ukuaji wa idadi ya watu inayokadiriwa kuwa asilimia tatu nukta tano hadi nne (3.5% - 4%) kila mwaka.

Hata hivyo, uchumi wa Kenya umekuwa ukizorota katika miongo miwili iliyopita. Ukuaji wa uchumi umeshuka katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, kutoka asilimia nne nukta sita (4.6%) mwaka wa 1996, hadi uchumi kudumaa na kufikia kiasi cha asilimia sufuri nukta tatu (0.3%) mwaka wa 2000. Kadhalika, kwa kipindi cha miongo mitatu iliyopita, kiwango cha Jumla ya Pato la Taifa (GDP) kimeendelea kupungua kutoka kiasi wastani cha asilimia tano nukta mbili (5.2%) kwa mwaka kati ya 1974–

1979, hadi asilimia nne nukta moja (4.1%) mnamo miaka ya 1980–1985 na 1990–1995. Viwango hivi vilifika kiasi cha asilimia moja nukta tisa (1.9%) kati ya 1996–2000. Hadi sasa, Kenya imeorodheshwa baada ya Zimbabwe, kama nchi mojawapo ya Afrika iliyo na uchumi unaozorota haraka zaidi. Ongezeko Jumla ya Pato la Taifa la kila mwaka limekuwa dogo zaidi ya kiasi wastani cha ongezeko la idadi ya watu (asilimia mbili nukta nane (2.8%) kwa mwaka). Mchango wa kilimo kwa Jumla ya Pato la Taifa (GDP) ulipungua kutoka asilimia thelathini na tano (35%) hadi asili mia ishirini na nane (28%) kati ya miaka ya 1970 na 1990. Tena mchango wa viwanda kwa Jumla ya Mapato ya Taifa (GDP) ulipungua kutoka zaidi ya asilimia ishirini (20%) hadi asilimia kumi na sita (16%) kwa kipindi hicho kimoja. Ongezeko la huduma za serikali na vipengele rasmi vya usalama vimepungua kufikia asilimia sufuri nukta nane (0.8%) mwaka wa 1997 na asilimia moja nukta mbili mwaka wa 1998. Kufikia mwaka wa 2000, kiwango cha kukosa ajira, mojawapo ya vigezo muhimu vya maendeleo ya jamii, kukosa ajira kilifikia asilimia thelathini na sita (36%).

Kipindi cha kutoendelea kwa uchumi kimesababisha uzorotaji katika sekta zote za uchumi. Matokeo yake ni uchache wa kazi na ajira na kwa hivyo kuongezeka kwa hali ya kukosa ajira; viwango vya riba vinavyobadilikabadilika na kuleta hali ya wasiwasi, hasara za biashara zinazoongezeka (bidhaa nyingi za kutoka nje na bidhaa chache za kuuzwa nje); ongezeko la mkopo unaoathiri uwekezaji; shilingi inayopungua thamani na umaskini uliozidi. Imedhihirishwa kuwa ongezeko la kiasi cha asilimia saba (7%) kwa mwaka ni muhimu ili kufanikisha uondoaji wa umaskini, na malengo ya maendeleo na shabaha inayolengwa. Ingawaje, uwezekano wa kufikia kiwango hiki cha uwezo wa kiuchumi hivi karibuni, katika hali ya ongezeko wastani la asilimia mbili (2%) la miaka ya 1990, ni hafifu.

## 5.5 <u>Muktadha wa Kisiasa</u>

Shinikizo muhimu zaidi imekuwa katika eneo la kisiasa. Wakati wa uhuru, Kenya ilirithi mfumo wa siasa zilizojikita katika kanuni za serikali huru. Kanuni hizi zilijumlisha utawala na mamlaka ya nchi, uhuru wa kupanga asasi za serikali, uwezo wa

kuamua shughuli za ndani ya nchi na haki ya kushiriki katika shughuli za kimataifa. Katiba ya Kenya yatarajia taifa la kidemokrasia na lenye vyama vingi ambamo serikali imejikita kwenye maadili ya utawala wa kisheria, usawa, haki ya jamii na ujamhuri. Kufuatana na kanuni ya ujamhuri, uchaguzi mkuu umekuwa ukifanywa mara kwa mara na upokezanaji madaraka baada ya uchaguzi umekuwa wa nidhamu na amani, tangu tujinyakulie uhuru.

Tukichunguza demokrasia ya mataifa mapya, tunaona kwamba ijapokuwa msingi wa demokrasia unaanza kuimarika na mfumo wa kisiasa uliorithiwa na wa kiutengani usioshirikisha, na wenye udhalimu umeanza kujibadilisha na kufuata ushirikishi, ukabila katika siasa umeibua tatizo la mvutano baina ya waliowengi na waliowachache.

Kwa sababu hakuna itikadi imara ya kisiasa inayofungamanisha mfumo wa kiutawala na kisiasa uliokita katika misingi ya ukoo upatikanao miongoni mwa Wakenya wengi, na uhusiano wa madaraka ya serikali ya kisasa, ukabila umekuwa kioo cha kuangazia siasa miongoni mwa wananchi. Uhusiano wa kikabila aghalabu unazidi imani kwa taifa na mwelekeo wa siasa za taifa unaegemea, kwa hali isiyopendeza, baina ya makundi ya kikabila na vyama vya kisiasa vya 'taifa'. Mwishowe, makundi ya kikabila yanajikita kwenye mtego wa udhalimu, hali ya kisiasa inayotokana na ukoloni, wasiyoifahamu ndewe wala sikio.

Kutokana na hali hii, pameibuka tatizo la imani miongoni mwa viongozi wa kisiasa ambapo viongozi wanaonekana kupendelea na kufuata maslahi ya kieneo na kufurahia manufaa ya muda mfupi ya kisiasa, badala ya malengo mapana yenye manufaa kwa taifa zima. Wingi wa ufisadi wakati wa uchaguzi ni kielelezo kimojawapo cha udhalilishaji wa taratibu za kisiasa kinachosababisha utawala dhaifu katika viwango vya taifa na wilaya.

Utaratibu wa demokrasia katika awamu ya baada ukoloni haujaimarisha uwezo wa kujitawala na Wakenya wameshindwa kudhibiti vyema mwelekeo na uhuru wao wa kijamii, kisiasa na kiuchumi. Mfumo wa kisiasa umeudunisha uhuru wa Wakenya na

kuufanya uonekane kama kwamba ni haki tu ya kupiga kura wakati wa uchaguzi kila baada ya miaka mitano. Pia, serikali, kupitia vyombo vyake vya urasimi imeidhalilisha jamii na kuwanyima wananchi uwezo wa kujiendeleza. Katika hali nyingi, wingi wa tofauti zilizoko nchini Kenya haujitokezi kwenye asasi za kidemokrasia. Tena kushiriki kwa Wakenya, pamoja na wanawake na makundi ya waliowachache katika usimamizi wa masuala ya umma hauwiani hata kidogo na idadi yao.

Kwa hivyo, ufikiaji kamili wa malengo ya haki ya kijamii na kiuchumi, kwa mujibu wa ahadi ya uhuru wa kisiasa iliyotolewa wakati wa kutwaa uhuru, umebaki ndoto isiyotimilika. Hali hii imesababisha hisia za kutengwa daima miongoni mwa wananchi wengi walionyimwa nafasi ya kisiasa, kijamii na kiuchumi. Upande wa pili wa mfumo huu wa kisiasa ni ule uliokita katika ukoo na uraia usiorasmishwa na unaofanya kazi sambamba na taratibu za makundi ya huduma za jamii, mpango wa jadi wa kisiasa na makundi na vyama vya kisiasa, vyenye misingi ya kikabila. Mfumo huu ndio unaojiimarisha kama utaratibu wa siasa za taifa.

## 5.6 <u>Muktadha wa Wanawake</u>

Sehemu muhimu ya shinikizo la kijamii, kiuchumi na kisiasa lililoenea nchini katika mwongo uliopita linahusu hadhi ya wanawake.

### 5.6.1 <u>Wanawake katika uchumi wa Kenya</u>

Wanawake wa Kenya wamejitahidi kuchangia maendeleo ya kiuchumi ya nchi hii. Wengi wao wameunda vyama katika viwango vya mashinani ili kushughulikia mahitaji ya msingi ya familia zao, na wengine wameunda mashirika na mifumo mingineyo ili kuathiri sera na kushirikisha jinsia katika mielekeo tawala, hasa katika uundaji wa sera.

Wanawake hawajafanikiwa sana kuziathiri sera za kiuchumi kwa sababu si jambo rahisi kuhusisha uchanganuzi wa mahusiano ya kijinsia na mifumo ya sera za kiuchumi. Hii ni kwa sababu ya hali ya kuyafumbia macho masuala ya kijinsia katika mijadala ya

kiuchumi. Mahusiano ya kijinsia yanaweza kufafanuliwa katika miktadha ya kutambua maingiliano yaliyopo baina ya jadi za wakati uliopita zinazotofautishwa kwa mujibu wa nadharia za uke na uume, na itikadi, jadi za kiasasi na hali za kiamali zinazorejelea ugawaji wa amali katika misingi ya kijinsia. Mahusiano ya kijinsia hutokana na miundo ya kijamii ambayo inatofautisha na kusisitiza nyenzo maalum kwa wanawake na wanaume.

Kwa muda mrefu, uhusiano baina ya vyombo vya sera na mishabaha yao haujachanganuliwa katika misingi ya kutenganishwa kijinsia kwa kutambua juhudi za kazi zisizolipiwa ujira hasa zinazofanywa na wanawake na zile za kulipiwa ujira. Uhusiano uliopo baina ya uchumi-zalishi na uchumi-zalishi-maradufu, ambao mara nyingi ni eneo la wanawake, haujatiliwa makini. Wanawake ni watu walio na haki za kijamii na wala si vyombo vya kuzalisha mali. Njia hii ya kuingiza ufahamu wa jinsia katika mifumo ya sera za kiuchumi nchini Kenya huenda ikawafaidi baadhi ya wanaume pamoja na wanawake kadri inavyoonyesha kutambua maslahi na haki katika taratibu za uundaji na utekelezaji wa sera.

Uundaji na utekelezaji wa sera zinazoyafumbia jicho masuala ya kijinsia umechangia katika kushusha thamani ya kazi za wanawake. Uhalisia wa historia ya maisha ya jamii na kiuchumi ni kuwa ni uzalishaji mali wa wanawake ambao umeusetiri uchumi wa nchi hii na nchi nyinginezo. Licha ya haya, kazi ya wanawake haijatambulika, na kwa kiasi pia haijapimika.

Udhati na udhahania wa kufafanua uzalishaji unaopendekezwa na wataalamu wa uchumi na wapangaji hauzingatii kazi za wanawake. Kuna haja ya kuibuka na mwelekeo mpya ambao unatambua uhusika wa wanawake katika uchumi. Itabidi mwelekeo huu uhusishe masuala yanayohusu dhana, mbinu, na ufundi endapo wanawake nchini Kenya watawajibika kuathiri kikamilifu uchumi wa nchi hii kwa manufaa ya wote.

Juhudi zinazolenga uundaji wa sera za kiuchumi zinazotambua umuhimu wa jinsia umo katika Makala ya Serikali ya Upunguzaji wa Umasikini *(Poverty Reduction Stragegy*

*Paper, PRSP)* kimsingi, zinaashiria maono mapya ya elimu ya uchumi yanayotambua kuwa sera za kiuchumi zina umuhimu mkubwa katika kueneza na kuibua upendeleo wa kijinsia. Mwelekeo mwingine wa kufafanua elimu ya uchumi inayotambua umuhimu wa jinsia ni ule unaohusu uhusiano baina ya mielekeo ya kukua na miktadha tofauti ya ukosefu wa usawa wa kijinsia. Ingawa uhusiano baina ya ukosefu wa usawa wa kijinsia na kukua kiuchumi unatatanisha, imebainika wazi kwa sasa kuwa baadhi ya miktadha ya ukosefu wa usawa wa kijinsia, kama vile katika elimu na afya, ina athari kubwa viwango vya kukua kwa uchumi.

### 5.6.2 Umaskini Kuhusishwa na Wanawake

Hali ya kuuhusisha umaskini na wanawake na Kenya na Afrika kwa jumla huenda imetokana na mambo mengi, kama vile upungufu wa ujuzi na maarifa, miundo ya masoko yasiyovutia ambayo huwaweka wanawake katika viwango vya kazi zinazochukua muda mrefu, japo malipo yake ni ya chini, na pia kuwazuilia kupata rasilmali na mikopo. Isitoshe, miundo ya jadi ya familia huendeleza ukosefu wa usawa wa jinsia kupitia kaida za mirengo ya kuumeni ya umilikaji wa mali na urithi, ubaguzi katika masuala ya umma na kutotambulika kwa thamani ya kazi ya wanawake.

Mielekeo ya kiuchumi, kidemografia na kisiasa imo katika kubadilisha sura ya mashambani na kuathiri shughuli zinazofanywa na wanawake. Wanawake wana upungufu wa elimu na ujuzi wakilinganishwa na wanaume. Wana muda mchache wa kushughulikia uzalishaji wa rasilmali na hawana mamlaka juu ya rasilmali muhimu, kama vile shamba na fedha. Mipaka ya jinsia katika ugawaji wa kazi nchini Kenya huwazuia wanawake kuzalisha mimea ya mauzo, ingawa bado wanawake wanashikilia kiwango kikubwa cha kazi za kilimo.

Ni wazi kuwa wanawake nchini Kenya hawajapata fursa ya kupata maarifa na teknolojia ambazo zingewawezesha kushiriki zaidi katika uzalishaji mali. Ni muhimu basi kuondoa vizuizi vya kisheria, kiutawala kijamii, kiuchumi na kimwelekeo ambavyo huwazuia

wanawake kupata na kudhibiti rasilmali.  Ni muhimu pia kujenga sera za kiuchumi ambazo zinautambua jinsia.

### 5.6.3. Wanawake Katika Siasa

Licha ya kukosa kushiriki kwa njia yenye matokeo ya kufaa katika uchumi, bado wanawake hawajapiga sana hatua kisiasa. Sababu ya msingi imetokana na jinsi ambavyo Kenya, ambayo ni jamii ya utawala wenye mrengo wa kuumeni, imeendelea kuwachukulia wanawake katika uwanja wa kisiasa. Kinadharia, haki ya kugombea uchaguzi, kuwa mgombea kiti na kuweza kuchaguliwa ina misingi katika haki ya kupiga kura. Ukweli ni kwamba, haki ya wanawake ya kupiga kura bado inazuiliwa kwa sababu moja kuu, ambayo ni kuwa, wagombezi wa pekee wanaostahili kupigiwa kura mara nyingi huwa ni wanaume. Si kawaida kupata wanawake wakijitokeza kwa vyeo vya kupigiwa kura kwa sababu ambazo zimejadiliwa na wasomi kwa wingi.

Hali hii ya kukosa usawa katika kushirikisha vyombo vya kisheria inaonyesha kuwa uwakilishi wa wanawake, badala ya kuwa kielelezo cha demokrasia ni kielelezo cha uhifadhi wa hali iliyopo. Sababu hizi ni pamoja na utamaduni, mifumo ya jamii zenye mrengo wa kuumeni, miundo ya asasi za kisiasa, na mitindo ya uchaguzi miongoni mwa mambo mengine.

**WABUNGE KATIKA MISINGI YA JINSIA: 1969-1999**

| Mwaka | Wanawake | Waume | Jumla | (%) Asilimia Ya Wanawake |
|---|---|---|---|---|
| 1969 | 2 | 165 | 167 | 1.2 |
| 1974 | 7 | 162 | 169 | 1.4 |
| 1979 | 4 | 166 | 170 | 2.4 |
| 1983 | 3 | 167 | 170 | 1.8 |
| 1988 | 3 | 197 | 200 | 1.5 |
| 1992 | 7 | 193 | 200 | 3.5 |
| 1997 | 8 | 214 | 222 | 3.6 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1998 | 9 | 213 | 222 | 4.1 |

*Asili ya jedwali: Tume ya uchaguzi, 1998*

Ingawa Kenya imefuata kwa dhati utaratibu wa uchaguzi katika misingi ya kutambua ushindi wa walio wengi, matokeo ya kushiriki kwa wanawake yamekuwa ya kusikitisha. Mpango wa kitendo Kisawazishi (Affirmative Action) kinachopendekeza umuhimu wa kuongeza kushiriki katika uwakilishi bungeni na tawala za wilayani haujafua dafu.

Uwakilishi wa chini wa wanawake katika taratibu na tawala za kisiasa unaweza kufafanuliwa katika misingi kadha mingineyo ikiwemo mielekeo na makatazo ya kijamii na kitamaduni, ukosefu wa fedha, ukosefu wa kujitolea kisiasa, kutofahamu na nia njema za kisiasa, na kwa jumla, ukosefu wa miundomsingi katika maeneo ya mashambani. Katika hali kama hii, wanawake wengi wananyimwa nafasi ya kutekeleza nyadhifa zao za kiuchumi na kiakili kikamilifu, licha ya zile wanazozitekeleza za kuwa mke na mama. Ingawa wanawake wengi hushiriki katika taratibu za uchaguzi kama wapiga kura, ni wachache mno ambao wanajitolea kama wagombezi uchaguzini. Kizuizi kingine kwa ushiriki wa wanawake katika taratibu za tawala za kisiasa ni hali ya juu ya kutojua kusoma na kuandika miongoni mwao nchini Kenya. Hili limeathiri ufahamu wa wanawake na pia viwango vyao vya kushiriki katika maisha ya kisiasa.

Ushiriki haba wa wanawake katika maisha ya kisiasa pia unahusishwa na mambo mengine yasiyoonekana wazi kama vile ugawaji usio sawa wa nafasi na majukumu ya wake na waume, hali ya kushikilia tofauti katika nyanja za mafunzo, kazi na utegemezi wa kiuchumi wa wanawake. Licha ya kuwa na sheria ya kisiasa iliyo wazi, uwekaji wa sera za kufaa kama vile sera za Kitendo-Kisawazishi na juhudi maalum za kuweka mfumo wa uchaguzi na asasi kama vile vyama vya kisiasa, vitachangia pakubwa katika kuhakikisha usawa wa kijinsia katika uwakilishi wa bunge, utawala wa wilayani na asasi nyinginezo. Taratibu za urekebishaji wa Katiba zinatoa nafasi kwa wanawake kujadili mkataba wa pande mbili. Itabidi serikali ifanye juhudi maalum ili kuhakikisha kuwepo

kwa uwezekano wa kiuchumi na kisiasa na kudumisha usawa wa kijinsia kwa manufaa ya taifa.

## 5.7. Hitimisho

Wakati wa kuwasilikiliza wananchi kote nchini, Tume iliweza kuthibitisha kuwa wananchi hawakuyaona mengi ya masuala haya kama matokeo ya msingi wa utawala mbaya tu bali yalikuwa pia matokeo ya mfumo wa Katiba iliyokuwa na dosari. Katika sura ya sita, tunaangalia baadhi ya mambo kuhusu masuala haya na ambayo wananchi waliona kuwa yangeweza kusuluhishwa kupitia mfumo wa mgawo mpya wa kikatiba.

# SURA YA SITA

# KUMILIKI UTARATIBU WA MAREKEBISHO

## 6.1. Utaratibu Ushirikishao Wananchi

Kanuni inayoiongoza Tume chini ya Sehemu ya 5 ya Sheria ya Marekebisho ni ile inayohusu uwajibikaji kwa wananchi wa Kenya na kuhakikisha kuwa utaratibu wa marekebisho unazingatia wingi wa tofauti zilizopo miongoni mwa Wakenya, na kuwapatia Wakenya hawa nafasi ya kushiriki kikamilifu, na kwa uhuru, katika taratibu za mijadala. Iliagiza kuwa utaratibu wa marekebisho ufanywe kwa kanuni za kilimwengu za haki za binadamu, usawa wa kijinsia, demokrasia, na matokeo yake yawe kielelezo kinachoonyesha uaminifu kwa matumaini ya wananchi wa Kenya.

Isitoshe, kifungu cha 17 (d) kinataka Tume ihakikishe kuwa Wakenya wanatoa maoni na mapendekezo yao kuhusu masuala kadha yakiwemo masuala yanayogusia miundo na majukumu ya vyombo vya serikali, miundo ya serikali, tume za kikatiba, mfumo wa uchaguzi, mahakama, tume za wilayani, serikali za wilaya, haki za ardhi na mali, matumizi na usimamizi wa fedha za umma, uraia na vizuizi vya kijamii na kitamaduni miongoni mwa vingine. Inapendekeza kuwepo kwa ushauriano baina ya vyombo vya marekebisho na wananchi.

Maoni ya wananchi yaliyowasilishwa kwa Tume yalikuwa mengi na mapana na yalitofautiana kwa namna nyingi; yaliathiriwa vile vile na sababu na hali mbalimbali kama vile wasiwasi kuhusu utaratibu wenyewe wa marekebisho, namna za maisha yao na sababu nyinginezo. Kwa hakika, maoni ya wananchi yalitokana na matumaini yao, hofu na wasiwasi waliokuwa nao na pia mipaka ya utaratibu wa marekebisho.

## 6.2. Matarajio ya Wananchi

### 6.2.1 Kuhusu utaratibu wa marekebisho

Matumaini ya wananchi yalikuwa mengi na ya kutofautiana. Kwa jumla, wananchi walitaraji kuwa utaratibu wa marekebisho ungewapatia nafasi ya kutakasa hisia za taifa na kupima utendaji wa serikali. Hili lilitokana na hali kuwa uhuru umo katika wananchi na ni wao ambao wana haki ya kujitawala kulingana na Katiba ambayo wameibuni, wakaifanya kuwa sheria na wakaitoa kwao wenyewe na ambayo ni wao tu waliokuwa na uhalali wa kuitayarisha.

Matarajio ya kimsingi basi yalikuwa kwamba Katiba mpya ingekuwa kiwakilishi kiaminifu cha matumaini ya wananchi na kuwa ingeanzisha mwelekeo mpya wa kisiasa, bunge jipya na mahakama mpya. Katiba hii mpya pia ingekuza uwazi na uwajibikaji, haki ya kimaumbile, kuheshimu haki za binadamu, demokrasia, ushiriki kamilifu katika utawala, kuhakikisha upataji wa mahitaji ya msingi, kuondoa umaskini na kuinua hali ya maisha ya umma. Matarajio na matumaini ya wananchi yanabainihsa yaliyomo katika agizo la Tume ya Marekebisho jinsi ilivyo katika kifungu cha 3 cha Sheria ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya.

Wananchi wa Kenya walitaraji kuwa utaratibu wa marekebisho utafanywa kwa njia ya wazi na uongozwe na kanuni za heshima kwa haki za binadamu, jinsia, usawa na demokrasia. Walitaraji pia kuwa utaratibu wa marekebisho ungetambua tofauti zao ikiwemo tofauti za hali za kijinsia, imani za kidini, umri, kazi, kisomo, ulemavu na wasiobahatika. Wananchi walitarajia Tume na vyombo vyake kujitolea katika hali ya kutopendelea, uhuru, hadilifu, kutochelewa, uaminifu, nia njema na kwa maslahi ya umma.

Wananchi, wakiwa wamiliki wa utaratibu wa marekebisho, walitaraji kupewa nafasi ya kushiriki kikamilifu na kwa uhuru katika kuanzisha na kujadili mapendekezo yatakayoibadilisha katiba. Walitaraji kuwa Tume ya Marekebisho ingeyasikiliza maoni

yao na kuyashughulikia na katika misingi ya maoni haya, Tume ingeibuka na ripoti ambayo ingeweza kutekelezwa. Kwa njia maalum, wananchi walitaka kuhakikishiwa kuwa:

- Pesa za walipakodi zingetumiwa kwa njia ya kuwajibika na ya busara katika utekelezaji wa Marekebisho;
- Kila mtu angepewa muda usiokadiriwa ili atoe maoni yake na kuwa Tume ingesikiliza kwa makini na kutochelewa;
- Raia wote wangeshiriki katika mazungumzo – lakini katika hali halisia wasomi wengi hawakutoa maoni yao;
- Utaratibu wa marekebisho ungekuwa huru na kutoingiliwa na ama serikali au vyombo vyake;
- Ni wananchi ambao hatimaye wangetoa uamuzi wa mwisho kuhusu ukubalifu wa Katiba;
- Ni wananchi tu ambao wangekadiria muda wa kuchukuliwa na marekebisho.

Tashwishi inayotokana na hali ya mpito na mizozo ya kisiasa kuhusu endapo utaratibu wa marekebisho ufanywe au usifanywe zimeipatia Tume ugumu wa kutekeleza marekebisho kwa kufuata kwa dhati matarajio ya wananchi.

### 6.2.2. Matarajio kuhusu matokeo

Wananchi walitaraji Katiba mpya ipatikane kwao kwa lugha ya kufahamika ambayo wangeielewa kwa urahisi. Kwa wananchi wengi, Katiba iliyoandikwa kwa lugha ya kisheria haingeweza kutimiza mahitaji yao vizuri. Walitarajia pia kuwa Katiba iliyorekebishwa ingezingatia matumaini ya wasiobahatika na wanajamii waliowekwa pembeni. Kwa njia nyingi walitaraji kuwa katiba mpya ingeweza kusuhulisha matatizo chungu nzima ya kijamii na kiuchumi na kuibua mabadiliko makubwa katika hali yao ya maisha katika miktadha ya kuondoa umaskini, ufisadi, kuwahakikishia chakula, makazi, afya, elimu, maji, kazi na ardhi kwa kila Mkenya.

**HOJA KUMI NA NNE MUHIMU KUTOKA KWA WANANCHI**

Tupatieni nafasi ya kuishi maisha ya heshima: Tupate mahitaji ya msingi ya chakula, maji, mavazi, makao, ulinzi na elimu ya msingi; ambavyo tutavilipia na juhudi zetu kwa kusaidiwa na serikali;

Tunataka jamii yenye amani na utulivu na isiyokuwa na uhalifu;

Tunataka mfumo wa haki utakaotuwezesha kupata ardhi kwa siku zijazo na kutendewa haki kwa maovu yaliyopita;

Tupatie nafasi ya kuhibiti maamuzi yanayotolewa kuhusu maisha yetu karibu na umma – tusaidie kuelewa vizuri maamuzi ambayo hatuwezi kuyafanya wenyewe lakini yanayohusu maisha yetu kwa undani;

Hatutaki mtu mmoja kumiliki uwezo mwingi;

Tunataka wabunge wetu wafanye kazi kwa bidii, watuheshimu na waheshimu maoni yetu – na tupewe uwezo wa kuwatimua kama hawatayatimiza haya;

Tunataka tuweze kuwachagua viongozi ambao wana sifa za kuwa weledi, wanaokuwa na uadilifu na wa kujali maslahi ya wengine; sifa ambazo zitawafanya kuwa viongozi wa kustahiki;

Tunataka tuumalize ufisadi;

Tunataka polisi wanaowaheshimu raia na ambao wanaweza kuheshimiwa na raia.

Tunataka wanawake wapate haki na usawa wa kijinsia;

Tunataka watoto wawe na siku za usoni za kuweza kutegemewa – ikiwa ni pamoja na mayatima na watoto wa mitaani;

Tunataka walemavu wapewe heshima na kutunzwa kwa heshima;

Tunataka jamii zote ziheshimiwe na ziwe huru kuzingatia tamaduni na imani zao;

Tunasisitiza haki yetu ya kuzitaka sehemu zote za serikali yetu kuwajibika – na tunataka asasi zilizo aminifu na za kuweza kufikiwa ili kuhakikisha uwajibikaji.

## 6.3. Hofu na Wasiwasi wa Wananchi.

Katika mawasilisho kwa Tume, wananchi wa Kenya walizungumzia hofu na wasiwasi za aina mbalimbali kuhusu utaratibu wa marekebisho na masuala yanayowahusu. Baadhi ya wasiwasi hizi zilikuwa wa aina ya kikatiba, na mwingine ulikuwa wa kaida za kisheria na bado pia mwingine ulikuwa wa kisera na kiutawala.

### 6.3.1. Hofu na Wasiwasi Kuhusu Utaratibu wa Marekebisho

Kuhusu utaratibu wa marekebisho, aina mbalimbali za hofu na wasiwasi zilielezwa kwa makini. Hofu na wasiwasi kubwa kabisa ilihusu hali ya kuwa Tume haikushinikizwa katika Katiba. Waliogopa kuwa, bila kushinikizwa katika Katiba, Tume ingevunjwa wakati wowote na serikali.

Pili, kulikuwa na wasiwasi, hasa nyakati za awali, kuhusu uhuru wa utaratibu wa marekebisho. Wananchi walihofu kuwa haingewezekana kuwa na marekebisho yasiyokuwa ya kupendelea bila kuingiliwa na serikali. Hofu ilitokana pia na wasiwasi kuwa utaratibu wa marekebisho haungekuwa shirikishi, na pia kwa sababu ya kutojua, utaratibu wa marekebisho ungetekwa nyara na wasomi na kwa hivyo Katiba iliyorekebishwa ingebeba maoni ya wasomi. Kadri muda ulivyopita ndivyo hofu na wasiwasi hii ulivyoondolewa na imani ya wananchi ikaongezeka.

Tatu, kulikuwa na hofu kuwa Tume haikuwa na muda wa kutosha wa kutekeleza kazi yake. Kwa maoni yao, Tume ilikuwa inafanya kazi kwa kuwekewa mipaka ya wakati iliyofungamana na awamu ya bunge ambalo lingevunjwa wakati wowote kwa hiari ya Rais, na ambaye uwezo wake kwa hakika umewekwa na Katiba iliyopo. Wananchi wengi waliona kama kwamba marekebisho ya kina hayangewezekanan katika hali kama hii.

Nne, hali ya kuwa nchi ya Kenya imekuwa na Tume nyingi sana ambazo ripoti zao hazijatolewa kwa umma wala kutekelezwa ilikuwa sababu tosha ya kuwaletea wananchi

wasiwasi. Walihofu kuwa utaratibu wa marekebisho ya Katiba ulikuwa tu ujanja mwingine wa serikali. Kwa mujibu wa mshiriki mmoja wa umma:

> "…….*kuna ripoti zaidi ya tano na moja muhimu ni inayotokana na Tume ya Ardhi ya Njonjo. Hazijaidhinishwa na mtu yeyote, hakuna mtu anayezifanyia kazi na watu wanatoa malalamishi kwa kila kamati inayokuja katika eneo hili. Haya yataendelea mpaka lini?'*

Tano, kulikuwa pia na wasiwasi kuwa Tume haingeweza kushirikisha wingi wa tofauti za kimaadili miongoni mwa Wakenya. Walisisitiza kuwa maadili yao ya kitamaduni hayangebadilishwa hata na Katiba. Kwa mujibu wa mwasilishaji mmoja.

> *"……kwa nini tuambiwe kuwa hatujaelimika, tuna wasomi lakini tukisema kuwa tunataka kwenda katika madrassa tukiwa Waislamu kuna mtu ……Katiba ya Marekebisho inasema, 'Aha' Waislamu ni nini? Tunataka maadili yetu, tunataka watambuliwe kwa haya."*

### 6.3.2. Hofu Na Wasiwasi Kuhusu Masuala Yaliyoibuka

Katika kutoa maoni kuhusu masuala ya kuzingatiwa na Tume, wananchi waliongozwa na mambo mawili muhimu. La kwanza ni matarajio kuwa mara tu marekebisho ya Katiba yatakapokamilika, maisha yao yangebadilika sana na viwango vyao vya maisha kuimarika. Matokeo ni kuwa, wasiwasi wao ulihusu utawala kwa kuuhusisha na hali duni za maisha ya wananchi.

Katika mawasilisho yao, wananchi wengi waliamini kwa dhati kuwa hali zao za umaskini hazikusababishwa tu na utawala mbaya bali zingeweza kuondolewa na kukubalika kisheria kwa Katiba mpya. Walilalamika kuwa serikali ilikuwa imeshindwa kutekeleza sera ambazo zililenga kuzingatia maslahi ya kijamii ya wananchi. Basi ndipo wakawa na matumaini kuwa mipango mipya ya kikatiba kuhusu utawala ingeboresha hali zao za maisha kwa kuwapatia usalama wa hali bora za maisha kijamii, kisiasa na kichumi.

Walihitaji kuhakikishiwa kuwa katika siku za baadaye serikali ingefuata na kutii haki zao na wakawa na matumaini kuwa, wakiwa na Katiba iliyorekebishwa, hali zao za maisha zingeimarika na matatizo yao yangekwisha.

Hofu na wasiwasi maalum uliofungamana na hali ya serikali kuwa ufunguo wa kuboresha hali za maisha ya wananchi ulikuwa:

***(a) Kukosa Usawa Katika Kufikia Rasilmali.***

Wasiwasi muhimu ilihusu jinsi ambavyo rasilmali iligawa na kusimamiwa. Walitaka usawa wa kijinsia kuzingatiwa katika kusimamia na kugawanya rasilmali kwa uwazi na uwajibikaji.

***(b) Ukosefu Wa Haki Za Kiuchumi Na Kijamii.***

Wasiwasi ulielezwa kuhusu matatizo ya kufikia nyenzo za uchumi na maendeleo ya kijamii, na hasa kufikia elimu, makao, afya, chakula, na usalama wa kijamii na mahitaji mengine ya msingi. Walitaka uhuru kutoka kwenye minyororo ya umaskini na ukosefu wa usawa uliotokana na utawala mbaya ambao ulikuwa umegawa na kuzitenga sehemu za jamii mbali na mikondo maalum ya maendeleo. Mzee mmoja Moyale aliieleza hali yake ifuatavyo:

> *"Tulisikia kuwa uhuru ulikuja miaka arobaini (40) iliyopita na kuwa uhuru huu umefika Isiolo. Hatujui ni lini utafika huku"*.

***(c) Ukosefu wa Uwazi na Uwajibikaji***

Uwazi na uwajibikaji wa serikali viliwatia wananchi hofu kuu. Kwa maoni yao, serikali iliyopo haikutimiza uwajibikaji na uwazi katika shughuli zake kuhusu masuala ya umma, utoaji wa uamuzi, matumizi ya rasilmali za kitaifa, matumizi ya fedha, utoaji-wa-zabuni na usimamizi wa miradi ya umma, uendelezaji wa vyombo vya serikali, uchaguzi na utekelezaji wa haki na wa sheria. Wananchi walitaka Katiba ambayo ingeifanya serikali kuwajibika kwao na Katiba ambamo pia ingemlazimisha kila mtu kufuata sheria.

*(d) Ukosefu wa Heshima kwa Utawala wa Kisheria.*

Mara kwa mara wananchi waliiambia Tume hakuna mtu aliyepaswa kuwa nje ya sheria. Walitaka raia wote wawe sawa chini ya sheria, bila kumwacha yeyote nje, na wakawa na matumaini kuwa Katiba iliyorekebishwa ingewahakikishia utawala wa haki na wa sheria kwa Wakenya wote. Walihofu kuwa kama nguvu za serikali hazikutekelezwa kwa kufuata sheria, utawala mwema ungepuuzwa.

## 6.4 Kuwazingatia Wananchi

### 6.4.1 Kuchanganua maoni ya wananchi

Hali ya matarajio makubwa miongoni mwa wananchi kuhusu utaratibu wa marekebisho ilikuwa msukumo mkuu katika kuendesha mawasilisho, uchanganuzi wa data na uandalizi wa ripoti ya Tume, pamoja na Mswada wa Sheria. Tume iliwaajiri watafiti wengi wachanganuzi, makarani wa data na wachapishaji wa hatimkato ili kunakili hifadhi za mawasilisho na kuyachanganua haya pamoja na mawasilisho mengineneyo. Ripoti za vikao vya kikatiba vya maeneobunge ikiwemo mikhutasari na nakali za maoni ya wananchi zilitayarishwa na kupelekwa kwa kikundi hiki. Kwa kutumia programu za kompyuta ambazo zilitayarishwa kwa njia maalum ili kutumiwa na Tume ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya, mawasilisho yote yalichanganuliwa na kuratibishwa. Haya yaliiwezesha Tume kwa mtazamo mmoja kupata mapendeleo ya Wakenya kuhusu masuala mengi katika viwango vya maeneobunge, wilaya, mikoa na kitaifa. Mapendeleo yao pia yaliaishwa katika misingi ya jinsia, hali ya mtu au kikundi kilichotoa mawasilisho. Majedwali jumuishi na yaliyotenganishwa yalitolewa kwa Tume wakati ilipoanza kazi yake. Wanatume waliangalia kwa makinin maoni ya wananchi na wakajaribu kadri walivyoweza kuyawakilisha katika taarifa, mapendekezo na mswada wa sheria.

Uchanganuzi wa ndani wa mawasilisho, malengo ya marekeboshi katika nyanja maalum, na masharti yaliyowekwa vilizingatiwa katika kamati za mada kuu sita ambazo ziliwekwa na Tume. Taarifa na mapendekezo yao vilijadiliwa na Tume katika vikao vya jumla, ambavyo vilitoa uamuzi wa mwisho. Ripoti za kamati zilipitiwa tena ili kushirikisha maoni ya Tume. Kikundi cha waandalizi wa miswada kilikaa katika vikao vyote vya Tume katika harakati zake na hatimaye kutoa nakala ya kwanza ya mswada wa Katiba ambao uliangaliwa kwa makini na Tume ibara baada ya ibara.

Maoni ya Wakenya yamezingatiwa kadri iwezekenavyo na kuhifadhiwa. Yamepewa uzito unaostahiki hasa katika utayarishaji wa Katiba mpya. Pale ambapo maoni ya wananchi hayajazingatiwa, imekuwa ni kwa sababu Tume iliona kuwa namna tofauti ya kuyazingatia ilifaa zaidi hasa katika muktadha na kanuni za jumla za uundaji wa Katiba na demokrasia. Isitoshe, Tume imezingatia kwa makini hofu na wasiwasi wa wananchi na kuzitilia makini katika uandalizi wa Katiba mpya. Ingawa hofu na wasiwasi nyingi haziwezi kuhusishwa katika muktadha wa uandalizi wa katiba, imeelezwa kwa makini katika taarifa kuwa, njia tofauti kuhusu sera, utawala na kanuni za kisiasa zimetumika katika kuyashughulikia.

### 6.4.2 Maoni ya Wananchi katika Uandalizi wa Katiba

Ili kushirikisha malengo yaliyomo katika sheria ya marekebisho ya Katiba na maoni ya wananchi, ni muhimu kuibuka na waraka wa Katiba ambao, kimsingi, ni mpya. Tume inatambua ya kuwa dhima ya Katiba nchini Kenya si kuleta mseto wa mahusiano baina ya aina mbalimbali za uwezo na miundo yake. Katiba inalenga kuwezesha kuwepo kwa mabadiliko ya kijamii na ya kiuchumi ambayo wananchi wanataka na ambayo ni muhimu katika kuhakikisha kuwepo kwa demokrasia, ushiriki, na jamii ya haki. Tunaamini kwamba mengi ya mabadiliko haya yatatimizwa kupitia asasi mpya na taratibu za utawala za kufanya uamuzi na uwajibikaji ambazo tunapendekeza. Lakini, kwa kuzingatia mazoea yetu ya Katiba, itabidi tupige mbizi hata tuzipate asasi hizi. Tumeweka malengo na matumaini ya taifa na kanuni ambazo zinahitaji kutawala utekelezaji wa nguvu za serikali.

Tunapendekeza matumizi ya Katiba ili kuimarisha hali ya kuwa katika jamii moja ya kisiasa. Katiba inatoa vichochezi vitakavyotuwezesha kuvuka mipaka finyu ya siasa za kikabila kupitia sheria za uchaguzi na kanuni za miundo na uundaji wa serikali. Ni lazima tuhakikishe kuwa utambuzi wa wingi wa tofauti za kikabila, kimaeneo na kidini hautafikiwa kwa kupuuza umoja wa kitaifa. Mahali pa kusherehekea wingi wa tofauti ni katika nyanja za kijamii na za faragha, bali si za kisiasa. Isitoshe, tunatambua kuwa umoja wa kitaifa haufikiwi ikiwa jamii zetu zote hazitatendewa haki – na kuhisi kwamba zimetendewa haki. Tunapendekeza kuwa jamii ambazo zimenyimwa nafasi za kufaidi kutokana na maendeleo ya kijamii na kiuchumi zisaidiwe ili ziweze kufikia haki ya maisha inayofurahiwa na Wakenya wa hali zilizo bora. Tunapendekeza kuwa, kuhusu masuala ya ardhi na mengineyo, dhuluma za jadi lazima zizingatiwe na tunapendekeza kanuni na mbinu za kuyatekelezea haya.

## 6.5 Hitimisho

Tume imefurahi kwa jinsi wananchi walivyoitikiwa mwito wa kushiriki katika marekebisho. Inashukuru kwa namna ambavyo wananchi wame unga Tume mkono, jambo ambalo limeiwezesha Tume kuvuka vizuizi kadha wa kadha na kustahimili juhudi za kutaka kuvuruga mkondo wa marekebisho. Tunaamini kuwa utaratibu wa marekebisho hadi sasa umekuwa wenye manufaa mengi. Daima tumeona kuwa marekebisho haya yamekuwa zaidi ya harakati za kukubaliana tu kuhusu kanuni za Katiba mpya. Yamehusu pia hali ya kujitambua upya na utambulisho wetu. Imekuwa ni kuwapatia wananchi nafasi ya kuongea na kudhihirisha umuhimu wao. Imekuwa ni kuwapatia nafasi ya kutafakari juu ya historia ya taifa letu na ya katiba yetu. Imekuwa pia namna ya kupima taifa letu na serikali, na namna ya kwanza ya pekee na ya dhati ya kutathmini kumbukumbu za tawala zetu za sasa na zilizopita. Ni utaratibu wa kutambua jinsi ambavyo mwananchi wa kawaida anavyofafanua kinachomaanishwa na kuwa Mkenya, huku wakieleza kwa uwazi vitambulisho vyao vya umoja na wingi wa tofauti zao. Ni kusisitiza azimio letu la kutaka Kenya iliyoungana na dhamira ya kupata mfumo utakaoziwezesha jamii kudumu kwa pamoja. Ni kukubaliana kuhusu, na kuimarisha

maadili na malengo ya kitaifa.  Ni kupata kwa pamoja mbinu ambazo zitatuwezesha kutambua maoni yetu kuhusu maslahi ya kila mmoja, yenye utu na ya haki  katika jamii.  Mambo haya ni muhimu hasa wakati ambapo nchi inajaribu kujibadilisha ili idumishe utaifa.  Wajibu wa katiba si tu kutupatia kielelezo cha mfumo wa jamii bali pia ni kuishikamanisha au kuipatia jamii yenyewe uhai.  Tunaamini kuwa utaratibu wa marekebisho umekuwa wa muhimu katika kufanikiwa kwa malengo haya.

# SEHEMU YA TATU

# SAUTI ZA WANANCHI

# SURA YA SABA

# TARATIBU ZA KATIBA

## 7.1 <u>Agizo la Tume</u>

Sababu muhimu zaidi iliyowafanya Wakenya kutaka marekebisho ya katiba ya sasa ni kuwa walionelea katiba hiyo haiwalindi. Kwa sababu ya mabadiliko mengi yaliyofanyiwa katiba yenyewe tangu mwaka 1963, imetumika zaidi kama sheria zilizotungwa za kawaida tu wala si kama sheria kuu za nchi. Lengo muhimu la marekebisho lilikuwa ni kuunda tena katiba yenye taratibu na ukuu. Kwa hivyo masuala mbalimbali yalitolewa kwa umma ili yajadiliwe kama vile ukuu wa Katiba, ufafanuzi wa Katiba, uhuru wa kujitawala wa wananchi, utaifa na uraia, muundo wa taifa la kijamhuri, maadili ya kitaifa, malengo na mfumo wa sheria.

## 7.2. <u>Ukuu wa Katiba</u>

Kwanza lilikuwa ni suala la Ukuu wa Katiba na kiasi ambacho uwezo huu ungehifadhiwa katika katiba mpya au katika toleo jipya (la katiba).

### 7.2.1. Kanuni za Kijumla

Mantiki ya Ukuu wa Katiba ni kwamba serikali imeundwa na wananchi. Wananchi ndio wanaounda vyombo vya serikali, huvipa uwezo, na kwa kufanya hivyo hupunguza upeo ambao kwao wanafanya kazi. Wananchi hutarajia na kunuia kueleza uwezo wa mamlaka yao kupitia kwenye Katiba. Serikali inaundwa na wananchi kupitia Katiba. Kwa sababu inatokana na chombo chenye ukuu, basi Katiba ni sheria ambayo ni kuu. Ukuu wa Katiba unategemea kwa kiasi kikubwa namna kanuni zake zinavyoweza kubadilishwa.

Tajriba ya Afrika imeonyesha kuwa japo si vigumu kuunda Katiba njema, ni vigumu kuitekeleza na kuitii na ni rahisi mno kuibadili na kuitupilia mbali. Jambo hili lilikuwa nyeti wakati wa kutolewa maoni na wananchi na masuala yafuatayo yalibuka mara kwa mara:

- Tukizingatia wepesi wa kubadili Katiba ya uhuru, tunawezaje kuilinda Katiba mpya kutokana na hatima hiyo?
- Tunawezaje kuzuia kudhofika kwa asasi za Katiba na vyombo vya serikali kama ilivyotokea katika Katiba ya sasa?
- Tunawezaje kuhakikisha kuwa mabadiliko yaliyoletwa na Katiba mpya yatatekelezwa?
- Tunawezaje kuhakikisha kuwa mabadiliko yaliyoletwa na Katiba mpya yatatekelezwa?
- Tunawezaje kuhakikisha kuwa uwezo wa Katiba mpya hautumiwi vibaya?
- Tunawezaje kuhakikisha uwejibikaji wa mawaziri na wafanyi kazi wa umma kwa sera na vitendo vyao?
- Wananchi wapate fidia zipi baada ya ukiukaji wa haki zao?
- Tutahakikisha vipi kuwa majaji wanafafanua sheria na kutoa hukumu bila mapendeleo?
- Tufanye nini ili tuwe na uchaguzi huru na wa haki?
- Tulinde vipi maadili ya Katiba kama maafikiano, ushiriki wa watu, uhuru wa afisi za Katiba, na mashirika?
- Tutamaliza vipi ufisadi, unaosababisha wananchi kunyimwa haki zao na kuzidisha umaskini?

Ni muhimu Katiba ilindwe kutokana na mabadiliko ya kiholela. Ikiwa utaratibu wa kubadilisha ni rahisi, unaondoa imani ya wananchi katika Katiba. Lakini kinyume chake pia ni kweli ikiwa ni vigumu mno kubadili Katiba, pana uwezekano wa kusababisha mbinu za kimapinduzi za kuleta mabadiliko badala ya kutumia njia za kikatiba. Ni muhimu kuwa na utaratibu wa koti.

Kuna vigezo vya Katiba inayoweza kubadilika na isiyoweza kubadilika katika sheria ya Katiba.

Katiba isiyoweza kubadilika huweka mihimili inayozuia mageuzi, kupitia utaratibu au idadi ya watu watakikanao. Mihimili hii ni pamoja na:

a. Kutaja kuwa mabadiliko kupitia bunge sharti yaidhinishwe na idadi fulani ya wabunge;
b. Kuidhinishwa na bunge kabla na baada ya uchaguzi; na
c. Kuidhinishwa na bunge na wananchi katika kura ya maoni.

Katiba inayobadilika haihitaji mihimili kama hiyo. Inafuata imani ya ukuu wa bunge, lenye uwezo wa kubadili sheria, pamoja na Katiba. Hakuna utaratibu maalum wa kisheria unaohitajika kubadili Katiba. Hii ndiyo hali iliyoko uingereza.

### 7.2.2. Ukuu chini ya katiba ya sasa

Katiba ya uhuru ilihakikisha utaratibu wa kulinda na kutekeleza kanuni za Katiba.

Kwanza, ilitoa vigezo viwili vya mabadiliko – ya kawaida na kanuni zilizokitishwa. Mabadiliko ya kawaida yalihitaji robo tatu ya kura ya wabunge. Yaliyokitishwa yalihitaji mswada kusomwa mara mbili na tatu; na asilimia 90% ya wajumbe wa seneti. Yalihusu haki, uraia, uchaguzi, seneti na mahakama.

Kifungu cha 3 cha Katiba ya sasa kinataja kwamba: *" Katiba hii ni ya Jamhuri ya Kenya na itakuwa na nguvu kamili ya sheria katika Kenya nzima na kwa mujibu wa kwenye kifungu cha 47 cha sheria, ikiwa sheria yoyote unakinzana na Katiba hii, Katiba itafuatwa na sheria yoyote nyingine kupuuzwa kwa kadri ya ukinzani wake.*

Kifungu cha 47 cha sheria kinatoa mabadiliko ya Katiba Bungeni. Kinahitaji uungwaji mkono wa angalau asilimia sitini na tano (65%) ya Wabunge (hasa walio wengi). Bunge lina uwezo wa kubadilisha sehemu yoyote ya Katiba.

Ukuu wa Katiba unahitaji mahakama ipuuze matumizi yoyote ya uwezo usiokubaliana na hali iliyoagizwa au isiyolingana na Katiba inayotoa uwezo huo.

### 7.2.3 Ukuu wa Katiba katika Katiba nyingine

Kanuni zinazotaja ukuu wa Katiba zinapatikana katika mataifa mengi. Mifano ya hivi majuzi ni Uganda, Afrika Kusini na Ghana. Kwa mujibu wa Ibara 2 ya Katiba ya Uganda (1995),

(1) Katiba hii ndiyo Sheria Kuu ya Uganda na itakuwa na uwezo juu ya mamlaka na watu wote wa Uganda;
(2) Endapo sheria ua kaida yoyote inakinzana na kanuni yoyote ya Katiba hii, Katiba itafuatwa na sheria nyingine yoyote au kaida itapunzwa kwa kadri ya ukinzani huo.

Katika lugha nyingine, Katiba ya Afrika Kusini (1994) inataja katika ibara ya 2, kuwa: *Katiba hii ndiyo Sheira Kuu ya Jamhuri, sheria yoyote au kaida inayokinzana nayo imeharamishwa na masharti yaliyoamrisha nayo lazima yafuatwe.*

Katiba ya Ghana inataja kuwa Katiba ni Sheria Kuu ya Nchi, na imelindwa na kanuni fulani zilizokitishwa ambazo zinaweza kurekebishwa tu kupitia kura ya maoni kuhusu masharti yaliyomo humo.

### 7.2.4 Walivyosema Wananchi

**Wananchi walielezea Tume kwamba:**

(i) Marekebisho ya Katiba yanahitaji asilimia sabini na tano (75%) ya Wabunge

(ii) Uwezo wa Bunge wa kubadilisha katiba upunguzwe, kwa mfano, ambapo hawawezi kupata 75%, wananchi waitwe kuamua kwa kupiga kura ya maoni iliyoandaliwa na mahakama. Hii ifanywe tu baada ya wananchi kuhamasishwa vyema;

(iii) Wananchi washirikishwe katika mabadiliko ya kanuni fulani za katiba kupitia kura ya maoni hasa kuhusu sehemu za dini, ndoa talaka na urithi.

(iv) Pawe na tofauti baina na kanuni zilizokitishwa kwenye Katiba na zisizokitishwa na kuwe na utaratibu wa kuongoza mabadiliko ya sehemu zilizokitishwa. Sehemu zilizokitishwa ziwe ni pamoja na ukuu wa Katiba, Sheria ya Haki, Ardhi, Mahakama, Usalama, Fedha, mfumo wa serikali.

(v) Kuhusu ni nani atakayehusika katika kura ya maoni, maoni yalitanda tangu: Tume ya Uchaguzi, Tume huru ya Katiba, Wabunge, mashirika yasiyokuwa ya serikali na mashirika ya dini.

### 7.2.5 Uchanganuzi

Idadi kubwa ya Wakenya waliotoa maoni ni dhihirisho kuwa Katiba ni uti wa mgongo wa maisha ya Wakenya. Ilidaiwa Katiba iendelee kuwa sheria kuu. Jambo hili lilizua fikra kuhusu mabadiliko ya Katiba na namna yanavyoweza kutokea. Wakenya wengi walihofu kuwa bunge linauwezo kubadilisha Katiba na kupunguza pakubwa juhudi. Aidha, ilionekana kuwa kanuni iliyoko ya mabadiliko ya Katiba ni rahisi mno na inaweza kutumiwa kutoa madaraka zaidi kwa Mamlaka ya Nchi.

Wananchi kwa hivyo walitaka mpango imara ambao itakuwa lazima washirikishwe ili kuubadilisha. Kwa maoni yao, Katiba mpya irekebishwe tu kufuata utaratibu uliozingatiwa wakati wa kuinda.

### 7.2.6 Mapendekezo

Kwa hivyo Tume inapendekeza kwamba:-

(i) Katiba mpya iwe na baadhi ya masharti yaliyolindwa humo, kwa mfano yanayohusu haki za binadamu ili kwamba Bunge lisiwe na uwezo wa kubadilisha.

(ii) Katiba mpya iongee juu ya masuala ya uhusiano miongoni vya vyombo mbalimbali vya serikali na lazima ishughulikie vipimo na visawazishi vya utawala.

(iii) Katiba mpya inapaswa kuwa na ibara kuu zinazoeleza kwamba katiba inawaunganisha wananchi wote na vyombo vyote vya serikali na katika viwango vyote.

(iv) Katiba itabadilishwa tu na angalau asilimia sabini na tano (75%) ya wanabunge.

(v) Mabadiliko ya masharti yafuatayo yafanywe tu kupitia kura ya maoni:

- utangulizi
- masharti ya uraia
- kanuni elekevu za sera za taifa
- eneo la taifa
- kanuni za mgawanyo wa uwezo
- Mswada wa Sheria ya Haki
- masharti yanayohusu kura ya maoni

### 7.4.6 Mapendekezo

Tume, kwa hivyo, inapendekeza kwamba:

(i) Kuwe na utambuaji katika kitangulizi kwamba wananchi wana uwezo juu ya serikali;

(ii) Katika kanuni elekezi za sera ya Taifa, serikali itambue kwamba uwezo wake unatoka kwa wananchi;

(iii) Masuala fulani muhimu ya kikatiba yaingizwe kwenye Katiba na yasiweze kubadilishwa ila katika mkutano wa kitaifa.

## 7.5 Utaifa na Uraia

### 7.5.1 Kanuni za Jumla

Suala la utaifa ni la msingi katika maendeleo ya mshikamano wa ndani na uimara wa nje wa taifa. Hivyo, suala hilo halitegemei uaminifu pekee bali pia kuendelea kuwepo na kudumu kwa taifa.

### 7.5.2 Utaifa na Uraia katika Katiba ya sasa

Chini ya katiba ya sasa, uraia unaweza kupatikana kwa kuzaliwa, kuandikishwa, kusajiliwa na nasaba. Hata hivyo, kuna mambo yenye udhaifu katika masharti ya uraia ambayo Tume ilikusudia kuyachunguza. Kwanza kulikuwa na suala la uraia maradufu. Mtu akifikisha umri wa miaka 21 na ana uraia wa nchi nyingine anahitajika kutupilia mbali uraia wake wa nchi nyingine, la sivyo atapoteza uraia wa Kenya. Licha ya hivyo, mtu akifikisha umri wa miaka 21 na ni raia wa Kenya, akitaka uraia wa nchi nyingine, basi kwa vyovyote atatakikana autupilie mbali uraia wa Kenya.

Suala la pili ni ubaguzi wa jinsia katika kutolewa uraia. Kulingana na Kifungu cha Sheria ya Katiba "kila mtu aliyezaliwa Kenya baada ya Desemba 11, 1962 atakuwa raia wa Kenya, ikiwa wakati wa kuzaliwa kwake, mmoja wa wazazi wake alikuwa Mkenya." Kifungu cha Sheria sehemu 90, kwa upande mmoja husema kuwa mtu aliyezaliwa nje ya Kenya baada ya tarehe 11 Desemba 1963 atakuwa raia wa Kenya endapo katika tarehe hiyo, baba yake alikuwa raia wa Kenya. Kifungu cha sheria cha 91 zaidi kinataja kuwa

mwanamke aliyeolewa na raia wa Kenya ana haki ya kusajiliwa kuwa raia wa Kenya. Tukio la kanuni hizo ni kwamba mwanamme aliye raia wa Kenya anaweza:

- Kupitisha uraia wake kwa mkewe ambaye si Mkenya.
- Kupitisha uraia kwa watoto wake hata kama walizaliwa Kenya au nje ya Kenya

Mwanamke aliye katika hali hiyo:

- Hawezi kupitisha uraia kwa mumewe akiwa si Mkenya; na
- Anaweza tu kupitisha uraia kwa mtoto wake endapo mtoto huyo alizaliwa Kenya. Kama mtoto alizaliwa nje ya Kenya na baba asiye Mkenya, basi mtoto huyo hapati uraia wa Kenya.

Baadhi ya Wakenya walio wachache na makundi yanayoishi mipakani yamenyimwa vitu muhimu vya kimsingi kama vile vitambulisho na paspoti. Wamelazimika kuchunguzwa kabla ya kupewa nyaraka hizo. Ambao hawakuweza kuzipata nyaraka hizo, baadaye walinyimwa haki zao za kupiga kura.

### 7.5.3 Utaifa na Uraia katika Katiba nyingine

Masharti ya Utaifa na Uraia kwa kawaida yanafanana katika mataifa mengi. Haswa dhana hizi mbii hutumiwa kama shilingi kwa ya pili, japo neno uraia hutumika zaidi katika muktadha wa kikatiba. Kwa kanuni, Katiba nyingi hutoa uraia (utaifa) kwa msingi wa kuzaliwa (au nasaba), ndoa, kuandikishwa au kusajiliwa. Hivi ndivyo ilivyo Zambia, Namibia na Nigeria, pamoja na mataifa mengine. Mataifa mengi ya Afrika, hata hivyo, huzuia uraia maradufu ila katika hali chache, kama vile endapo uraia wa awali ulikuweko katika kuzaliwa au ndoa.

Mfano wa kanuni inayozuia uraia maradufu ni Ibara 15 ya Katiba ya Uganda, kama ifuatavyo;

(1) Kwa mujibu wa Ibara hii, raia wa Uganda hatakuwa na uraia wa nchi nyingine sambamba na uraia wa Uganda; na

(2) Raia wa Uganda atakoma kuwa raia wa Uganda endapo, akitimisha umri wa miaka kumi na nane, anachagua kimakusudi isipokuwa kupitia ndoa, kuchukua au kuendelea kuwa na uraia wa nchi nyingine, isiyokuwa Uganda.

### 7.5.4 Wananchi walivyosema

Maoni ya wananchi kuhusiana na uraia yanaweza kuorodheshwa hivi:

*(i) Kanuni za jumla*

a) Raia wapewe haki sawa bila kujali hali au njia wanazotumia kuwa raia

b) Nyaraka zote ambazo mtu hupatiwa kwa kuonyesha kitambulisho zafaa kutumiwa kama ushahidi wa uraia

*(ii) Uraia kiutomatiki (wa kujitekeleza)*

a) Mtoto aliyezaliwa na baba Mkenya.

b) Mtoto aliyezaliwa na mama Mkenya.

c) Mwanamke aliyeolewa na mume Mkenya.

d) Mwanamume aliyemwoa mke Mkenya.

*(iii) Uraia moja kwa moja*

a) Watu wanaoishi Kenya kwa zaidi ya miaka 10 mfululizo.

b) Mfanyibiashara mwenye shilingi milioni kumi aliyewekeza kwenye uchumi wa Kenya, aliyekwishatupilia mbali uraia wake wa awali.

c) Yeyote aliyezaliwa na angalau mzazi mmoja Mkenya ni raia wa Kenya.

*(iv) Kujiandikisha*

Mtu atakuwa raia wa Kenya kwa kujiandikisha ikiwa mtu huyo ana umri wa miaka kumi na minane, na amekuwa akiishi kisheria Kenya kwa kipindi cha miaka saba kabla ya kutuma maombi; na adhihirishe kuwa mwenye tabia na nia njema akipewa uraia wa kusihi Kenya.

*(v) Ndoa*

Yeyote anayemwoa Mkenya ana haki ya kuwa raia wa Kenya kwa mujibu wa ndoa hiyo.

*(vi) Uraia Maradufu*

Uraia maradufu unaruhusiwa hasa kwa jamii zinazoishi mipakani na wanaoishi ng'ambo.

### 7.5.5 Uchanganuzi

Suala la utaifa na uraia lilikuwa nyeti kwa wanawake na jamii zinazoishi mipakani, hasa ya Ethiopia na Somalia. Kuna Wakenya wengi ambao wameoa nje ya taifa hili na jambo hili limesababisha mataifa mengi kwa waume ambao wake zao ni Wakenya na watoto wa Wakenya ambao waume zao si Wakenya. Isitoshe, kuna jamii nyingi zinazovuka mipaka, kwa mfano, Wamaasai, Wateso, Waborana na Wasomali na jambo hili husababisha matatizo ya kipekee katika ujitambulishaji na utoaji hati za uraia. Kwa kawaida, matumizi ya sheria iliyopo ni ya kibaguzi na hayana haki. Katika hali fulani, matumizi hayo yalisababisha usumbufu na ukatili mipakani mwa nchi.

### 7.5.6 Mapendekezo

Tume inapendekeza kwamba:

i) Katiba iwahudumie sawa wanaume na wanawake kuhusu utoaji wa uraia.

ii) Katiba itaje kuwa raia wote wana haki ya kupata vitambulisho za kitaifa na paspoti.

iii) Katiba itoe uraia maradufu, kwa kuandikishwa, kusajiliwa na kutokana hadhi ya makazi ya kudumu.

iv) Halmashauri huru libuniwe na kuimarishwa katika Katiba kuchunguza wajibu wa masuala ya uraia ili kuzuia kuingilia haki za uraia.

v) Katiba itoe uraia kwa mtoto wa kupanga na uhalalishaji.

vi) Katika utambuzi wa haki ya mtoto kuwa na utaifa, pengine tungesema kwamba watoto wa umri fulani wanaopatikana Kenya ambao wazazi wao hawawezi kupatikana, wapewe uraia.

vii) Usawa wa raia wote bila kuzingatia rangi, asili ya kikabila, umri, mahali pa kuzaliwa, jinsia au tofauti nyinginezo ni mambo ambayo yanastahili kutiliwa mkazo na kuimarishwa imara katika katiba.

## 7.6 <u>TAIFA LA KIJAMHURI</u>

### 7.6.1 Kanuni za Kijumla

Sifa za taifa, eneo lake na vitambulishi vyake na namna usalama wake na hadhi yake hulindwa kutokana mashambulizi ya ndani na nje ni swala muhimu la kikatiba. Kwa hakika utawala wa kikoloni ulitegemea kwa kiwango kikubwa utekaji wa mipaka.

### 7.6.2 Taifa katika Katiba iliyopo

Licha ya kuitangaza Kenya kama taifa huru, Katiba iliyopo inaeleza sifa za kisheria za taifa kwa uchache mno. Mwanzo kabisa, mipaka ya kimataifa ya Kenya haikutajwa; kwa jumla ni kama ile ya utawala wa kikoloni ambayo ilitenga mipaka ya maeneo ya taifa kutokea ile ya Uganda, Ethiopia, Somalia na Tanzania. Hili ni pengo kubwa katika uhusiano wa Kimataifa.

Hali kadhalika, Katiba iliyopo inagusia kwa uchache sana usalama na uadilifu wa Taifa, licha ya ukweli kwamba kimsingi kundi kubwa la vikosi vya usalama vimeanzishwa kwa lengo la usalama wa ndani, na kulinda sheria na utangamano.

### 7.6.3 Taifa katika Katiba nyingine

Kwa sababu nzuri, Katiba za nchi nyingi huru za Afrika zinatangaza uhuru wa kujitawala. Baada ya kujikomboa kutoka kwa ukoloni lilikuwa jambao la busara kutangaza kifaa hiki cha kisiasa. Tangazo hilo bado linatokeza katika Katiba za majuzi za kimapinduzi au zitokanazo na wananchi. Kwa hivyo, Katiba ya Uganda, Ibara 5 (1) inatangaza kuwa Uganda ni nchi huru na Jamhuri. Kanuni kama hizo zimo katika Katiba

za Afrika kusini, Ethiopia, Eritrea, na Nigeria. Vifaa hivi vinaendelea na kutaja aina ya taifa, hasa mipaka yake, lugha rasmi, ulimwengu, ishara za taifa na falsafa ya siasa. Katiba ya Ethiopia, 1995, kwa mfano, inataja katika Ibara 1 kwamba:

> *"Katiba hii inaunda taifa la shirikisho na Demokrasia. Kwa hivyo, taifa la Ethiopia litaitwa Shirikisho la Demokrasia la Jamhuri ya Ethiopia".*

Ibara 2 inaongeza kwamba:

> *"Mipaka ya taifa itakuwa eneo la wanachama wa shirikisho na mipaka yake itafuata mikataba ya kimataifa".*

### 7.6.4 Watu walivyosema

Tume ilipokea maoni mengi yaliyozungumzia uadilifu katika mipaka ya kimaeneo nchini Kenya na kulinda usalama wa nje na ndani ya nchi kutoka jamii za mipakani na wale waliohisi kwamba vikosi vya usalama viwekewe kanuni za maadili zilizoundwa ili kuzuia matumizi ya uwezo kupindukia, kudumisha nidhamu na kuhakikisha uwajibikaji kwa umma.

*(i)* *Kuhusu mipaka, Tume iliambiwa kwamba:*

a) Serikali irekebishe mipaka iliyopo na ifanye mabadiliko yanayofaa;
b) Mpaka unaogawanya Kenya na Tanzania katika Ziwa Viktoria upigwe ramani upya ili kuipa Kenya na Wakenya fursa ya kuzifikia rasilmali zilizopo;

*(ii)* *Kuhusu usalama wa ndani ya nchi walisema kuwa:*

a) Maafisa wa Polisi kufanya misako na kushika watu bila sababu, kukomeshwe.
b) Kuongezeka kwa wizi wa kimabavu humu nchini. Hakuna utiifu wa sheria.
c) Kusambazwa kwa bunduki na risasi haramu katika baadhi ya maeneo humu nchini kuzuiwe.
d) Ukiukaji wa haki za binadamu ikiwa ni pamoja na unajisi unaofanywa na maafisa wa usalama wakiwa kazini, uchunguzwe na kuzuiwa, na
e) Uzembe wa jumla walio nao wanajeshi wakati wa usalama.

#### 7.6.5 Uchanganuzi

Suala la mipaka lilikuwa nyeti miongoni mwa wanajamii wanaoishi viungani mwa ziwa Victoria. Walieleza kuwa hushambuliwa mara kwa mara na majeshi ya Uganda na wakalalamika kuhusu ukosefu wa msaada wa mara moja kutoka kwa serikali ya Kenya. Wengine wao walisema kuwa hii ni ishara kwamba serikali haijali hauwalindi na kwa hivyo ni muhimu kubadilisha vyombo vya serikali. Si ajabu kuwa mpaka wa Kenya na Uganda haujamarishwa na kufikiwa maafikiano.

#### 7.6.6 Mapendekezo

Tume inapendekeza kwamba:

*i) Hatua zichukuliwe ili:*

a) Kufafanua mipaka ya Kenya kwa kutumia utaratibu wa kijiografia,
b) Kusuluhisha madai yaliyopo maeneo baina ya, au dhidi ya, majirani
c) Kuweka orodha ya mipaka hiyo kwenye Katiba mpya,
d) Kutangaza kikamilifu haki ya Kenya kujitawala mipakani.

*(ii) Katiba iwe na kanuni za wazi kuhusu vikosi vya usalama ili kuhakikisha:*

a) kutopendelea upande wowote kisiasa
b) heshima ya Kanuni za Sheria, demokrasia na haki za binadamu
c) kuwajibika kwa kuzingatia Katiba
d) uwazi na uwajibikaji
e) uaminifu kwa maagizo ya kisheria pekee
f) nidhamu na uzalendo
g) kudhibiti uraia.

### 7.7 <u>Maadili na Malengo ya Taifa</u>

#### 7.7.1 Kanuni za kijumla

Katiba nyingi huelezea maadili na malengo ya kupimia utendakazi wa utaratibu wa utawala. Haya huwekwa kwenye utangulizi, au kirasmi hufahamika kama kanuni elekezi za sera ya taifa.

Utangulizi ni maelezo ya awali yanayofafanua maono na maelekezo. Hivyo basi, utangulizi unahitajika kuwazungumzia, wanasheria, mahakimu, wasimamizi na wananchi wa kawaida, kutangaza maono ya jumla ya taifa, maelekezo, hamu na maadili ya pamoja.

Utangulizi unaelekeza jinsi ya kusisitiza kanuni za kimsingi ambazo watu wamewajibika kwazo kwa kuweko malengo ya kitaifa na ya kifalsafa. Si hoja ni miundo ya aina gani ya utawala imewekwa na wananchi, ama uwiano wa miundo hiyo kwa niaba ya wananchi na taratibu ambazo muundo huo unachukua, msingi wake lazima uwe na malengo ya taifa kama ulivyofafanuliwa katika utangulizi.

Utangulizi huandikwa ikichukuliwa kwamba, watu walio kwenye taifa wamewekwa pamoja katika maadili ya jumla, asili ya kihistoria ama ujuzi ambao ni muhimu na wazi kwa wananchi. Utangulizi unaweza kuwahakikishia watu kuhusu yale yaliyoyafanya ili kuepukana na hali mbaya, kwa mfano ukoloni nchini Kenya ama ubaguzi wa rangi nchini Afrika Kusini, na kwa sababu ya hakikisho hili njia ya kuinukia na maendeleo hujitokeza.

Kwa jumla, utangulizi hutekeleza majukumu mengi:

- Hutaja chanzo cha mamlaka ya Katiba. Inaweza kudai mamlaka haya yanatokana na wananchi au Mungu.
- Hutaja maadili na matumaini ya wananchi yatakayoendelezwa na Katiba.
- Unaweza kutaja historia ya Katiba na utaratibu wake (hasa ikiwa katiba imeandikwa baada ya vita vya uhuru au mabadiliko ya kidemokrasia).
- Unaweza kutaja sababu za kuundwa kwa Katiba.
- Unaweza kutaja sifa za taifa, k.m ni la kidemokrasia, lisilofuata dini, la vyama vingi.
- Unaweza kuonyesha muktadha wa Katiba, kisiasa, kijamii na kiuchumi.

- Ambapo utagulizi umeundwa ili kuondoa tofauti, unaweza kuonyesha kujitolea kwa pamoja kufuata maadili.

Kanuni elekezi za sera ya taifa ni kanuni zinazofaa mno na zinazotumiwa kupimia shughuli za serikali . Kanuni elekezi zinalengwa kufikia shabaha mbali mbali.Ya kwanza ni kuelezea sifa za taifa.

La pili ni kuunda majukumu katika sera za taifa. Kanuni elekezi za taifa ni nguzo za Taifa zinazotegemewa kutangaza maslahi na hali ya kimaisha ya watu. Zinajenga umbo la sera na sheria za serikali, hasa katika kuutambua uchumi, jamii, tamaduni na haki za mazingira, uwajibikaji wa serikali katika kuzilinda na kuzikinga kikamilifu kwenye hali na miundo yote ya maisha ya kitaifa. Kwa muhtasari , kanuni hizo huhitaji taifa kuelekeza sera zake katika kulinda matokeo bora ya maslahi ya watu kama kanuni ya kimsingi. Ingawa hazina uwezo wa kutetewa, Katiba nyingi zinahitaji kwamba kanuni kama hizo zichukuliwe katika upangaji wa mamlaka wa vyombo vyote vya taifa.

### 7.7.2 Malengo na maadili katika Katiba

Katiba iliyopo haina utangulizi wala haina maelezo kuhusu kanuni elekezi za sera ya taifa. Kwa kugusia tu, Katiba inaeleza kuhusu maadili na malengo kwenye kifungu cha 1 na kifungu cha 1A kinachotangaza Kenya kama Jamhuri huru na demokrasia ya vyama vingi.

### 7.7.3 Malengo na Maadili katika Katiba Nyingine

Katiba nyingi (za zamani na za kisasa) zinataja maadili na malengo yaliyounda taifa na yanayopasa kufuatwa. Haya hupatikana ama kwenye kanuni za utangulizi au katika ibara zilizotengwa kwa ajili hiyo. Mifumo ya kanuni hizo imo katika Katiba nyingi kama vile Marekani, Uganda, Ghana, Afrika Kusini, Fiji, na Nigeria. Kwa mfano katika kanuni za utangulizi, Katiba ya Eritrea inatangaza:

*"Kwa Shukrani za Daima…..maelfu ya.…waliojitoa mhanga kwa ajili ya …..haki na uhuru na……. ujasiri na kutokata tamaa kwa……wazalendo wa Eritrea…"*

Katiba kisha inaendelea katika Sura II kufafanua malengo ya taifa na kanuni elekezi. Baadhi yake ni:

- Umoja katika wingi;
- Utuluvi na maendeleo ya taifa;
- Hali za maendeleo yenye usawa ya kiuchumi na kijamii;
- Imani za kidemokrasia;
- Hali za kuendeleza utamaduni wa taifa;
- Mfumo wa haki wenye uhuru, uwezo na uwajibikaji;
- Huduma ya utumishi wa umma yenye wepesi, uhodari na isiyokubali ufisadi; na
- Vikosi vya ulinzi na usalama vyenye uaminifu.

Kanuni kama hizi zinapatikana katika Katiba za mataifa mengi yasiyokuwa ya Ulaya.

### 7.7.4 Watu Walivyosema

Watu walieleza Tume kwamba wanataka Katiba iliyo na kumbukumbu ya historia, inayotangaza matumaini yao kwa wakati ujao na kufafanua kanuni za jumla ambazo wangependa ziwatawale.

*i) Kuhusu utangulizi walisema:*

a) Katiba itambue kwamba nchi ya Kenya si taifa bali ni mkusanyiko wa mataifa mengi. Utangulizi uonyeshe ukweli huu na Katiba ikubali kuwepo kwa makabila mbali mbali
b) Sisi tunajichukulia kuwa sawa, licha ya maoni ya kisiasa, rangi, imani ama hali za kijamii na tutaungana ili kujenga taifa lenye amani na lililo madhubuti.
c) Iwape heshima wale waliopigania Uhuru wa Kenya.
d) Isifu maadili ya wazi ya kidemokrasia, uwajibikaji, heshima ya haki za binadamu na haki za kijamii.

Baadhi ya wananchi walipendekeza kwamba Tume ihusishe maelezo ya Utangulizi kama ifuatavyo:-

- "Sisi watu wa Kenya, ili kuunda demokrasia ya vyama vingi, kuimarisha haki, kuhakikisha utulivu wa kinyumba, kulinda haki za raia, kutangaza maslahi na usalama wa baraka za uhuru kwetu sisi na kizazi cha baadaye, tunaamini na kufuata Katiba hii na mtu yeyote aliye chini ya mamlaka ya Katiba hii atafanya hivyo kwa baraka za watu."

- **Sisi Watu Wa Kenya…**

**TUKIFAHAMU** kwamba serikali huundwa ili kuhudumia na kupigania amani, mafanikio, usalama, furaha, uadilifu wa kimazingira na hadhi ya maisha ya watu,

**TUKIZINGATIA** kwamba hapo awali malengo bora yalivurugwa na udhalimu, udikteta, ufashisti na serikali za kiimla,

**TUKIJUA** kwamba uendelevu wa demokrasia unahitaji kulindwa na watu ili kuhakikisha utangamano wa kijamii na asasi za utawala bora kama vile mahakama huru, huduma za jamii za kitaaluma na uwakilishi bora wa kisheria;

*(ii)* *Kuhusu na masuala ya kanuni elekezi, wananchi walitoa maoni kuwa kanuni ziwepo ili:*

a) Kuwaelekeza raia wote, mamlaka ya wilaya na Bunge, mamlaka ya nchi, mahakama na vyombo vingine vyote vya taifa na wahusika wanaotekeleza ama kufasiri Katiba na sheria nyingine yoyote ama kutekeleza maamuzi ya sera katika kuunda na kutangaza maadili mema ya kidemokrasia na maadili ya usawa wa kiuchumi.

b) Kutambua kwamba uwezo na mamlaka unatokana na Wakenya wenyewe na watu watatawaliwa kwa hiari na masikilizano.

c) Kuelekeza kwamba daima Kenya itakuwa taifa lenye demokrasia ya wengi (taratibu zote ambazo si za demokrasia ya wengi, hasa mfumo wa chama kimoja ama wa kijeshi si halali) na mgawo uliowazi wa madaraka na uongozi wa kisheria na haki.

d) Kuifungamanisha na elimu ya kisiasa, kitamaduni, ukatiba, maadili ya sheria na uwajibikaji, kulinda haki za wanawake, umoja wa kitaifa, haki za kibinadamu, kulinda haki za walemavu, uhusiano mwema wa kimataifa, malengo ya kijamii, malengo ya kielimu, malengo ya kitamaduni, malengo ya kiuchumi, haki ya ardhi, kujihusisha kwa masuala ya kiuchumi ya kitaifa, kulinda mazingira na ukuu wa Katiba.

### 7.7.5 Uchanganuzi

Isipokuwa Katiba ambazo zimefuata muundo wa Katiba ya Ufaransa ya 1958, Katiba nyingi hazina utangulizi au kanuni elekezi za sera ya serikali. Kutokana na taathira ya siasa baridi za miaka ya 1960 na 1970, nchi fulani za kiafrika zilianza kuingiza utangulizi kwenye Katiba. Katika awamu ya uundaji Katiba baada ya kuporomoka kwa Urusi, ni jambo la kawaida kuingiza utangulizi kwa sababu Tume ilishugulikia suala hili kwa njia maalum watu wengi. Waliliona kuwa zuri.

### 7.7.6 Mapendekezo

Hivyo basi, Tume inapendekeza kuwa Katiba mpya iwe na:-

*(i) Utangulizi ambao, pamoja na mengine:*

a) Unatambua umuhimu wa Mungu kwa Watu wa Kenya.

b) Unatambua upiganiaji wa uhuru na nafasi ya wale waliopigania uhuru wenyewe.

c) Unatambua uhuru wa watu katika kutunga Katiba na kuunda utaratibu bora wa utawala wao na wa vizazi vya baadaye.

d) Unatambua tofauti za dini, tamaduni na makabila katika maeneo mbali mbali ya Kenya.

e) Unasisitiza kutogawanyika kwa Wakenya kama taifa.
f) Unajaribu kuponya vidonda vya wakati wa baada ya uhuru vilivyosababishwa na ghasia za kisiasa
g) Unasisitiza uwajibikaji kwa haki za kijamii
h) Unasisitiza uwajibikaji kwa demokrasia, ukatiba na uongozi wa kisheria.

*(ii) Kanuni elekezi za sera za taifa zinazowahitaji watu wote na vyombo vyote vya taifa:*

a) Kuheshimu maadili ya sheria, kulinda demokrasia na asasi za kidemokrasia, kulinda uhuru na haki za raia.
b) Kuiheshimu kauli na imani ya masharti ya kikatiba inayohusu usawa na utawala bora.

(iii) Kauli kwamba vyombo vya taifa visitumie uwezo kiholela ama kiubaguzi.

(iv) Kuhakikisha uhuru, usawa wa haki kwa watu wote.

(v) Kueleza vyombo vya taifa katika usimamizi bora wa rasilimali ya nchi, kuheshimu tofauti za kikabila na kimaeneo na haki za jamii ikiwa ni pamoja na haki za jamii kupanga na kuhusika kwenye masuala ya kitamaduni na kujitambulisha kwa kujieleza.

## 7.8 <u>Mfumo wa Kisheria</u>

### 7.8.1 Kanuni za Kijumla

Aina na muundo wa mfumo wa sheria ni suala muhimu kwa sababu mbili. Kwanza, mfumo wa kisheria kama ulivyo sasa unatangulia Katiba ya uhuru ijapokuwa haukujengwa na Katiba hiyo. Pili, hata kama mamlaka ya kimsingi ipo katika utekelezaji wa shughuli za kisheria ili kuboresha falsafa maalum ya sheria humu nchini, haikuimarika.

### 7.8.2 Mfumo wa Sheria Katika Katiba iliyopo

Ijapokuwa Katiba iliyopo inataja ukuu wa Katiba na kulipa Bunge uwezo na kutunga sheria, haina masharti kuhusu mfumo wa sheria za Kenya na haina nafasi ya sheria nyingine.

Miongoni mwa sifa bora za mfumo wa sheria ni watu kukubali na kuzitii sheria zenyewe. Kupata ukubalifu na utii kama huo, watu lazima wazikubali sheria na mfumo wenyewe kwa jumla na Katiba ikiwa ni matakwa ya watu, lazima ieleze mfumo wa Sheria.

Badala ya msimamo wa kikatiba wa Kenya asili ya sheria za Kenya, sheria ya mahakama (Kifungu cha 8) inaorodhesha yafuatayo kama chanzo cha sheria za Kenya:-

- Katiba ya Kenya;
- Sheria inayohusisha vifungu vya sheria ya Bunge la Kenya kama ilivyo kwenye sheria za Kenya zilizopitishwa na Bunge, na vifungu maalum vya Sheria ya Bunge la Uingereza kama ilivyo katika sheria ya mahakama;
- Sheria ndogo;
- Kipengee cha Sheria ya Mazoea Kanuni za Usawa na Sheria za Jumla iliyokuwa ikitumika Uingereza Agosti 12,1897; na
- Sheria za kitamaduni katika mambo ya kijamii, bora tu zisipingane na haki na uadilifu ama na sheria iliyoandikwa.

Kwa sababu watu ndio chimbuko la uwezo ambao mfumo wa sheria unatekelezea shughuli zake, ni muhimu kwamba utaratibu huo ufafanuliwe kwenye Katiba kama msingi wa matakwa ya watu ili kuendesha kazi na kuilinda.

Katiba nyingi za kisasa kama vile Papua New Guinea zimeanzisha misingi kama hiyo.

### 7.8.3 Mfumo wa Sheria katika Katiba Nyingine

Ijapokuwa Katiba nyingi zimeachia sheria au hali maalum itakayotokea, suala la aina ya mfumo wa sheria, pamoja na uchaguzi wa vikao au kanuni za sheria, baadhi ya vifaa vya hivi majuzi, hasa vya jamii zenye tamaduni nyingi, zinatoa nafasi kwa suala hili. Lengo ni kuhakikisha uhalali wa mila za kisheria zinazojenga mfumo wa sheria wa taifa. Katiba ya Papua New Guinea inataja, kwa mfano, kwa sheria zake ni:

- Katiba hii;
- Sheria za asilia;
- Sheria za Bunge;
- Masharti ya Hali ya Hatari;
- Sheria za mikoa;
- Sheria zilizotupwa chini au zilizotokana na Katiba hii;
- Sheira iliyopo; na
- Si nyingine yoyote.

Katiba nyingine zinazotaja uzingatifu wa sheria maalum kama sehemu ya mfumo wa sheria. Kwa hivyo, Ibara 186 ya Katiba ya Fiji, 1997, inataja kuwa:

(1) Bunge sharti liwe na kanuni zinazoruhusu matumizi ya sheria za mila na utatuzi wa migogoro kwa mujibu wa utaratibu wa jedi;

(2) Bunge sharti lizingatie, wakati likifanya hivyo, mila, tamaduni, matumizi, maadili na matamanio ya wananchi.

### 7.8.4 Walivyosema Watu

Ijapokuwa suala hili, halikuulizwa watu moja kwa moja, palikuwa na haja kuu ya kuwepo kwa sheria za asili na za kidini katika maeneo yanayohitaji tahadhari.

Watu waliiambia Tume kwamba:-

| | |
|---|---|
| (i) | Sheria za Kitamaduni zinazotofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine ziwe na umuhimu mkubwa katika kutatua migogoro inayoambatana na mila na tamaduni za jamii inayohusika. |
| (ii) | Sheria zote za kitamaduni ziandikwe na zitambuliwe kama sheria ndogo na ziundwe upya ili ziingane na mahitaji ya Katiba mpya. |
| (iii) | Sheria za kitamaduni zisitumiwe kuwanyima watu nafasi ya kufurahia haki. |
| (iv) | Tume ya Marekebisho ya Katiba itupilie mbali sheria za kikoloni zisizo na manufaa kabala ya marekebisho ya Katiba. |

### 7.8.5 Uchanganuzi

Kwa sababu mfumo wa sheria wa Kenya unatokana na kanuni na maadili ya sheria ya Uingereza, pamekuwa na mazoea ya kudumiza sheria, mazoea, na maadili ya kitamaduni. Jambo hili limesababisha kuwepo kwa tamaduni zisizolindwa na sheria hasa katika masuala ya ardhi na uhusiano wa watu. Matukio kadha ya hivi majuzi yamedhihirisha kiwango cha tamaduni hizo. Kwa sababu hakuna jambo lililofanywa tangu wakati wa uhuru kuunda utaratibu imara wa maendeleo ya sheria ya kitamaduni, mfumo wa sheria wa Kenya umekumbwa na mvutano mingi ya ndani kwa ndani.

### 7.8.6 Mapendekezo

Tume inapendekeza kuwa:-

*(i) Katiba inafaa kueleza wazi chimbuko la Sheria za Kenya kama:*

a) Katiba na zizingatie
b) Sheria ya Bunge
c) Sheria ya Tamaduni za Kiafrika
d) Sheria ya Kibinafsi ya Kiislamu
e) Sheria ya Kibinafsi ya Kihindu
f) Sheria ya jumuiya ya Afrika Mashariki

g) Sheria ya Kimataifa

(ii) *Sheria za Uislamu, Sheria za Kihindu na Kitamaduni* lazima zipimwe kwa sheria ya mtu binafsi.

(iii) *Mfumo wa sheria unapaswa kuhakikisha usawa* kwa wote mbele ya sheria, na

(iv) *Korti zitahakikisha kuweko* na kuendelea kwa sheria ya mazoea ya Kenya.

# SURA YA NANE

# SHERIA YA HAKI

## 8.1 Agizo la Tume

Sheria ya Tume imetoa kipaumbele kwa haki za binadamu na mahitaji ya kimsingi na imehakikisha kuwepo kwa ajenda inayopauka katika urekebishaji wa Katiba. Ajenda hiyo ni pamoja na:-

- Kulinda haki za binadamu na demokrasia
- Usawa wa jinsia
- Kutoa mahitaji ya kimsingi kupitia uanzishaji wa mpango wa usawa katika maendeleo ya kiuchumi na ufikiaji maliasili
- Uwajibikaji wa watu katika masuala ya serikali na umma
- Ushiriki wa watu katika masuala ya serikali na umma
- Uchuguzi huru na haki
- Utambuaji wa tofauti, makabila na ujitambulishaji kimaeneo na haki za kishirika
- Hali ya kuridhisha ya kubadilishana mawazo
- Kupata haki sawa kwa wote (kuondoa vizuizi vya kutobaguana)
- Haki za watoto
- Uzingatifu nchini Kenya wa majukumu ya haki za binadamu za kimataifa
- Ushirikiano kimaeneo na kilimwengu ili kudumisha demokrasia na haki
- Kuendeleza uwezo na uhuru wa mahakama.

## 8.2 Upeo wa Sheria ya Haki

### 8.2.1 Kanuni za Kijumla

***(a) Upeo Unaopanuka***

Kihistoria, haki hutokana na kuimarika kwa mataifa na masoko (kwa utumbuzi kuwa taifa na soko huwaweka watu katika hali ya uwezo kudhulumiwa na kunyanyaswa na kwamba uhakikisho fulani ni muhimu ili kufaulisha uchumi wa soko). Katika miaka ya karibuni, dhana ya haki imepanuka ili kuingiza ustahiki aina mbalimblai, kama mahitaji ya kimsingi ya kumlinda na kumtosheleza binadamu wa ulimwengu wa kisasa.

Haki za kujumuika (kama haki za jamii nzima) zilitambuliwa. Haki ya mazingara safi, yenye afya na endelevu, haki ya amani, kuendeleza utamaduni na maendeleo. Haki hizi ni muhimu kwa jamii na mtu binafsi.

Viwango hivi vinaashiria aina za haki na kwa kiwango fulani kuwakilisha itikadi tofauti za kiuchumi na kifalsafa – japo kama tutakavyoona tofauti hizi si kutwa mno:

- Haki za kiraia na kisiasa zinaelekezwa katika kuhakikisha kuwa kuna nafasi kwa watu kufuata maadili na maslahi yao na kuzuia serikali isiwaingilie sana maishani mwao;
- Haki za kiuchumi, kijamii na kitamaduni, kwa upande mwingine, huenda zikahitaji serikali kuchukua hatua maalum ili kufaulisha upatikanajji wa haki na kwa hivyo kutarajia serikali inayoonekana. Serikali haitajiwi kutoa elimu bali au huduma za matibabu moja kwa moja n.k. bali ifuata sera zinazowasaidia watu, familia, na makundi kupata ruzuku za maisha na kuhakikisha vifaa hivi vinapatikano kwa kutoa utawala mwema, kugawa mali kwa njia sawa na sera nzuri.
- Kiwango cha tatu cha haki kinahitaji serikali inayoonekana, kama mashauri. Kinahitaji serikali na mamlaka mengine kufuata sera zinazofaa na zisizoharibu maliasili au fedha kwa kununua silaha, lakini kujenga hali ya amani na kuishi kwa

maelewano na kuandaa nafasi kwa watu na makundi ili kufuata maslahi yao ya kiuchumi na kijamii kwa njia ya haki, usawa na amani.

Utaratibu wa kikatiba kuhusu haki za binadamu umeendelea kuwa wa kina na wa kueleweka; utaratibu wa kitaifa kuhusu haki za binadamu umejalizwa na kusisitizwa na mapatano ya kimataifa yanayotoa majukumu kwa mataifa na vitengo vingine kuimarisha na kulinda haki, na kuandaa mbinu za ukaguzi wa kimataifa wa utekelezaji wa kitaifa wa majukumu hayo. Haki za binadamu zinafafanua na kuwekea mipaka upeo wa uwezo wa serikali, na kutoa maongozi kuhusu matumizi ya uwezo huo. Ni mojawapo ya njia muhimu za kutangaza maadili ya kitaifa na kueleza madhumuni ya taifa. Hivi leo ni vigumu sana kufikiria kuwepo kwa katiba isiyo na sheria ya haki:

Haki ni muhimu kwa mifumo ya kikatiba na kisiasa kwa sababu kadhaa zifuatazo.

Kwanza, haki zinachukuliwa kuwa anazo binadamu kimaumbile na kwamba hazitolewi kwa taifa wakati watu wanapounda jamii. Pili, haki ni muhimu, ili watu waishi katika hadhi, watimize uwezo wao, watosheleze mahitaji yao ya kimwili na kiroho. Tatu, kuunda jamii ya kisiasa ili kuhakikisha kuwa wanapata haki zao hasa haki ya usalama wa kimwili na kulinda mali na familia ipasavyo. Nne, haki ya kufafanua uhusiano wa watu kwa taifa. Kupitia njia hii, zinatoa umbo la katiba nzima.

Tano, haki huwapa raia au wakazi uwezo, kwa kuwapa jukumu muhimu katika kufanya uamuzi katika vyombo vya serikali na haki ya kushiriki na kwa kulinda mahitaji yao dhidi ya kukiukwa na serikali.

Mwishowe, haki hupunguza uwezo wa serikali na kuzuia kupindukia kwa walio wengi. Saba, haki huhalalisha makundi madogo madogo, na jamii zisizobahatika kutunzwa kwa njia iliyo maalumu, na nane, haki ni muhimu kwa kuanzisha na kulinda demokrasia, ikiwa ni pamoja na uwajibikaji wa mamlaka. Vile vile kuheshimu haki hupunguza mizozo ya ndani na nje, na kuimarisha umoja wa taifa.

Ulindaji wa haki katika katiba za sasa umepitia hatua kadhaa. Mwanzoni, haki zilizolindwa zilikuwa haki za kibinafsi, hasa za kiraia na kisiasa, kama vile kulindwa kwa maisha na uhuru, kushirikiana, kujumuika, uhuru wa kujieleza, haki za kupiga kura, na haki ya kugombea wadhifa katika uchaguzi, na haki ya kuhusika katika masuala ya umma. Baadaye, kundi jipya la haki za kijamii, kiuchumi na kitamaduni zilipata kulindwa katika vyombo vya taifa, na katiba za kitaifa. Haki hizi zilipewa umuhimu mkubwa na mifumo ya kijamaa iliyozingatia zaidi masuala ya haki ya jamii na hali nzuri ya maisha kwa watu wote. Zilijumuisha haki ya kupata elimu, haki ya kuajiriwa, haki ya makazi na chakula.

Mwisho, haki zinajulikana hivi sasa kama haki za jamii nzima; zile zinazojumuisha jamii, nzima kwa jumla. Haki hizi zilijumuisha haki ya mazingira safi, ya kufaa na yanayoweza kuendelezwa, amani, utambulisho wa kitamaduni na maendeleo kwa ujumla wake. Ni muhimu kutambua kwamba utaratibu huu wa haki hauwakilishi mfumo wa msonge wa maadili. Hivi leo inatambuliwa kuwa makundi yote ya haki ni muhimu kwa maisha ya hadhi na amani, na kuwa haziwezi kutofautishwa, na zinategemeana. Kwa mfano, elimu na kujua kusoma na kuandika (zinazoainishwa kama haki za kijamii) ni muhimu kwa uhuru wa kujieleza (zinazoainishwa kama haki ya kiraia) ili mtu aweze kusoma na kuwasiliana. Vivyo hivyo, mazingira safi ni muhimu kwa afya na haki ya kuishi kwa ujumla wake. Uhuru wa kujieleza na kushirikiana ni muhimu kumkinga mtu binafsi au kundi fulani la watu kutokana na kunyanyaswa na serikali.

***(b) Mikabala***

Hivi sasa haki za binadamu si suala la kushughulikiwa tu kama maslahi ya taifa. Kuna mfumo wa haki wa kimaeneo au kimataifa unaoyafungamanisha, au unaojumuisha mataifa yote: kaida na mapatano ya kimataifa. Utekelezaji wa kaida hizi unasimamiwa na kamati za kimataifa na kimaeneo, ingawa mara nyingi kamati hizi huweza tu kutafsiri wajibu wa serikali, lakini hushindwa kulazimisha utekelezaji wa maamuzi yake. Vile vile, mbinu za kimataifa za kuendeleza haki na kuingilia kati kwa misingi ya kibinadamu pia unawezekana na mahakama maalum za kimataifa zimeundwa kufanikisha kutolewa kwa adhabu dhidi ya wale wanaovuka mipaka katika ukiukaji wa haki; ya hivi punde

zaidi, ikiwa mapatano ya Urumi kuunda mahakama ya kudumu ya uhalifu, ya kimataifa. Hivi majuzi, utaratibu mpya wa mamlaka ya kisheria ya kimataifa wa kutangaza uwezo wa mahakama za kitaifa kuwafungulia mashtaka na kuadhibu raia wa taifa lolote lile kwa uhalifu dhidi ya ubinadamu (kesi ya Pinochet) unaendelea kukubalika.

### 8.2.2 Sheria ya Haki Katika Katiba Iliyopo

Utaratibu kuhusu haki za binadamu wa kulinda Haki za msingi na uhuru wa Mtu Binafsi (Protection of Fundamental Rights and Freedoms of the Individual) unapatikana katika sura ya 5 ya Katiba ingawa haki ya kupiga kura na kuwania wadhifa katika uchaguzi imeshughulikiwa katika sehemu ya 5 (sifa za mtu anayestahili kuwania urais); sehemu ya 34 (sifa za anayestahili kuwania kiti cha ubunge); na sehemu 43 (sifa za anayekubaliwa kupiga kura katika uchaguzi wa urais na ule wa ubunge). Utaratibu huo unahakikisha:

- Haki ya kuishi na uhuru;
- Haki ya kulindwa dhidi ya utumwa, shokoa, kuteswa, kutendewa kinyama ama kushushiwa hadhi;
- Ulinzi wa haki ya mali ya kibinafsi;
- Haki ya kulindwa dhidi ya msako na kukamatwa kiholela;
- Ulinzi wa haki za kuwaza, kujieleza, kujumuika, na kwenda kokote;
- Haki ya kutobaguliwa kwa msingi wa jinsia, rangi, kabila, mahali unakotoka au unakokaa, au uhusiano wowote wa kieneo, maoni ya kisiasa, rangi au imani;
- Haki ya mashtaka ya haki na mahakama huru iliyoundwa kupitia sheria katika kesi ya uhalifu, ikiwa ni pamoja na haki ya kuchukuliwa kutokuwa na hatia hadi unapopatikana na hatia, na haki ya kutetewa na mwanasheria.

Sheria ya Haki kama ilivyo katika Katiba iliyopo ina matatizo.

Kwanza, upeo wa ulinzi wa sheria ya haki ni finyu mno kutegemea haki zinazolindwa na watu wanaowajibika kwa majukumu yanayohusiana na haki hizo. Ni haki za uraia na

siasa pekee zilizolindwa; hakuna utaratibu wa haki za kijamii na kiuchumi; na hakuna hali yoyote, ama kwa njia ya maagizo au haki inayohitaji serikali kuwahakikishia Wakenya mahitaji ya kimsingi. Hakuna chochote kuhusu haki za jumla (amani, maendelo, au mazingira); na haki za kitamaduni zilizopo zina upungufu. Ni sehemu ndogo tu ya sehemu ya haki za kijumla au haki za kijamii kuhusu ardhi na sheria ya desturi inayotambuliwa. Hakuna chochote kuhusu makundi ya waliowachache, watoto na wazee au walemavu. Mwisho ulinzi dhidi ya ubaguzi unahusu raia wa Kenya pekee. Udhaifu mwingine wa sheria ya sasa ya haki ni pamoja na:-

- Haki ya mshtakiwa kutendewa haki katika uendeshaji mashtaka haiwajibishi serikali kumpa mashtakiwa mwanasheria wa kumtetea haki katika mashtaka ambapo adhabu ya kifo inaweza kutolewa.
- Hakuna utambuzi wa faragha, au haki za ushiriki wa kisiasa au njia nyingine zozote.
- Baadhi ya haki zinafafanuliwa kijuujuu na zingekuwa wazi na kufaa zaidi iwapo zingeelezwa kwa undani zaidi; kwa mfano haki inayohusu vyombo vya habari.
- Hakuna chochote cha wazi kinachosemwa kuhusu makundi ya kijamii na kiuchumi kama vile makundi ya wafugaji, wateja, wafungwa na watu waliotiwa nguvuni, wakimbizi na watetezi wa wafanyikazi.
- Haiwapi raia haki ya kupata habari iliyo mikononi mwa serikali.
- Haiyapi mashirika au wahusika wengine wa kibinafsi wajibu wa kuheshimu na kuimarisha haki za kimsingi, na
- Si wazi ni kufikia kiwango kipi ambapo sheria ya haki inapaswa kufuatwa na mahakama katika kutekeleza na kuunda Sheria za Wote zinazoundwa na majaji na wala si bunge. Pili, katiba yenyewe inatoa njia nyingi za kuepukwa kwa hatakuwa sheria inazounda yenyewe. Kwa hivyo sheria zifuatazo zinaweza kuondolewa wakati wa vita au hali ya hatari inapotangazwa:-
  - uhuru wa mtu binafsi
  - ulinzi dhidi ya kusakwa kiholela au kuingia
  - uhuru wa kujieleza

- uhuru wa kujumuika na kushirikiana
- Uhuru wa kwenda utakako, na
- ulinzi dhidi ya kubaguliwa

Katika utekelezaji wake, kuondolewa kwa sheria hizi humtegemea rais, kwa kuwa yeye ndiye hutangaza vita ua hali ya hatari. Kutangaza hali ya hatari hutekelezwa wakati Rais anapotumia sehemu III ya sheria Utunzaji wa Usalama wa Umma (Ibara 57). Agizo la Rais linapaswa kuidhinishwa na bunge katika kipindi cha siku 28, lakini baada ya kuidhinisha bunge haliweki tarehe ya kumalizika kwa hali hiyo hatari. Kukosa kuweka mipaka ya muda au kipindi cha kuwapo hali ya hatari si jambo la kawaida na hutatiza sana ufurahiaji wa haki. Chini ya sheria hiyo, Rais anaweza kuwatia watu kizuizini, bila ya kuwafanyia mashtaka ya haki, kutangaza hali ya hatari katika baadhi ya sehemu za taifa na hivyo kuondoa haki zote na kuviruhusu vikosi vya wanajeshi kuchukua hatua zinazokiuka haki za kimsingi na uhuru unaotolewa na katiba.

Tatu, sheria ya haki ni dhaifu kwa misingi ya usasa katika upande wa utaratibu na taasisi za utekelezaji. Kwa mfano, hakuna makundi maalum ya kuimarisha au kuhakikisha utekelezaji wa haki kama vile Mpokea Malalamishi au Tume ya Haki za Binadamu. Sheria hiyo pia ina upungufu mkubwa katika upande wa mahakama kulinda na kutekeleza haki. Isitoshe, utaratibu mpya wa kimataifa wa utekelezaji wa haki za binadamu umeundwa tangu sheria hiyo ilipotayarishwa, na utaratibu huo unapaswa kijumuishwa katika katiba.

Nne, serikali haitekelezi majukumu yake iliyopewa katika katiba ipasavyo. Mabadiliko yaliyofanyiwa katiba mwaka 1997 kulitaka bunge kuweka utaratibu wa kutoa msaada wa kifedha kwa raia yeyote maskini anayepigania haki zake za kikatiba mahakamani bado hayajatekelezwa. Kenya imekuwa ikifanya vibaya katika utekelezaji wa majukumu ya kimataifa na kieneo.

Katika kuongezea zaidi:-

- Uamuzi wa mahakama umekuwa ukikiuka haki;

- Utawala umeshutumiwa kutotilia mkazo haki kimaksudi;
- Katika vipindi kadhaa baada ya uhuru, kuzuiliwa bila kushtakiwa na kuteswa kumedhihirika mno;
- Asasi muhimu za kulinda haki kama vile polisi na mahakama ndizo zinazokiuka haki hizo hata zaidi;
- Mamlaka za umma haziwajibiki kwa umma kila wakati;
- Watu hawafahamu haki zao na jinsi ya kuzitekeleza; na
- Kutekeleza sheria ya Haki kwa mujibu wa Sehemu ya 84 ya Katiba kumezuiliwa na ukosefu wa kanuni za mahakama, ambazo hazikuwekwa kwenye gazetu ka serikali na Jaji Mkuu hadi 2001.

### 8.2.3 Sheria ya Haki katika Katiba Nyingine

Hakuna Katiba iliyoaandikwa isiyokuwa na sheria ya Haki. Tofauti iliyoko ni kwamba, wakati vifaa vya mwanzoni – kabla ya 1966 – vilisisitiza haki za uraia na siasa, vya hivi majuzi vina kina na vinajumuisha maadili, kanuni na kaida zinazopatikana katika mikataba na maafikiano ya kimataifa.

Jedwali lifuatalo linajumuisha kanuni za sheria ya Haki katika Katiba nyingine:

| **Kiwango** | **Yaliyomo** | **Taifa** |
|---|---|---|
| Uraia na siasa | Maisha, uhuru, heshima, usawa, siri, n.k. | Katiba zote zenye Sheria ya Haki |
| Uchumi, jamiii na utamaduni | Huduma za jamii, kushiriki kiuchumi, lugha, utaifa, n.k. | Eritrea, Ethiopia, Uganda, Brazil, Afrika Kusini, Ghana. |
| Familia | Haki ya kuoa/kuolewa na kuwa na familia. | Eritrea, Uganda, Ethiopia |
| Wanawake | Haki ya heshima kamili na sawa, haki ya kitendo-kisawazishi | Uganda, Afrika Kusini, Ethiopia |
| Watoto | Kulindwa kutokana na matumizi ya nguvu, udhalimu, unyanyasaji, haki ya | Afrika Kusini, Brazil, Uganda, Namibia, Ghana |

| | | |
|---|---|---|
| | afya, utaifa, n.k. | |
| Maendeleo na Mazingira | Haki ya mazingira safi, maendeleo endelevu, kufikia rasilmali na utendekazi kwa njia sawa. | Afrika Kusini, Uganda, Eritrea, Ethiopia, Malawi, Tanzania |
| Mali | Kulindwa kutokana na matumizi ya mali bila malipo. | Mataifa mengi |
| Kufikia haki | Haki na mfumo wa haki usio ghali na wa haraka. | Afrika kusini, Eritrea, Ethiopia, Uganda |

#### 8.2.4 Walichosema Wananchi

Mawasilisho mengi yaligusia haki za binadamu moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Malalamiko na, au madai yalipokelewa kuhusu:-

(i) haja ya kuondoa vikwazo katika haki
(ii) polisi kuwajibika zaidi
(iii) maafisa kutawala kiholela hasa machifu
(iv) kupata au kufikia habari iliyo mikononi mwa serikali
(v) ubaguzi wa serikali dhidi ya makundi ya walio wachache na upendeleo wa umma
(vi) sheria ya kibaguzi na njia nyingine zinazotumiwa kuubughudhi umma hasa katika mikoa ya Kaskazini-Mashariki na Mashariki
(vii) kukosa kulinda, ipasavyo, uhuru wa dini, siku na njia za kuabudu na pia njia za kuvaa
(viii) kutaka hatua za kitendo-kisawazishi kuchukuliwa ili kuyawezesha makundi yasiyobahatika kwenda sambamba na makundi mengine katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi
(ix) ukabila na mapendeleo ya kikabila
(x) serikali kupendelea baadhi ya jamii fulani na kubagua nyingineulinzi bora wa mali, hasa ardhi

| | |
|---|---|
| (xi) | kulinda ardhi kwa ajili makao |
| (xii) | kuhakikisha kuwepo kwa makao |
| (xiii) | ukosefu wa vifaa vya usafiri, na hali mbovu ya barabara hasa katika maeneo ya mashambani |
| (xiv) | usawa wa haki na kupata ardhi |
| (xv) | kulinda haki za walemavu |
| (xvi) | hadhi maalum na kulinda haki za wazee |
| (xvii) | kulinda na kuwarekebisha watoto wanaorandaranda mitaani, na mayatima |
| (xviii) | kutambua haki za wafanyikazi |
| (xix) | kuwalinda wanahabari, na kwa ujumla uhuru wa vyombo vya habari |
| (xx) | elimu ya msingi ya bure na ya lazima, na elimu iliyopunguzwa gharama baada ya ya elimu ya msingi |
| (xxi) | huduma za afya za bure na zilizopunguzwa gharama |
| (xxii) | ukosefu wa maji safi na salama |
| (xxiii) | ukosefu wa lishe bora |
| (xxiv) | fursa ya kuajiriwa au kujiajiri kibinafsi |
| (xxv) | kufikia mahakama kwa njia iliyo bora zaidi |
| (xxvi) | ukosefu wa mahali au kituo ambapo wanaweza kupeleka malalamiko kuhusu utawala mbovu wa kiholela |
| (xxvii) | wafungwa na wanaozuiliwa kuchukuliwa kama binadamu wengine |
| (xxviii) | kuteswa na polisi |
| (xxix) | kuzuiliwa kwa muda mrefu ukingoja kufikishwa mahakamani |
| (xxx) | kuheshimu mapatano ya kimataifa kuhusu haki za binadamu |
| (xxxi) | kubuni njia au mbinu bora zaidi za kulinda haki zao, na |
| (xxxii) | kuhusishwa zaidi katika kufanya uamuzi unaoathiri maisha yao ya kila siku |
| (xxxiii) | kulinda watoto kwa jumla |
| (xxxiv) | kutiwa nguvuni na kusakwa kiholela |
| (xxxv) | ukosefu wa usalama |
| (xxxvi) | kukosa kutambua makundi fulani wakati wa kuhesabu watu |

| | |
|---|---|
| (xxxvii) | haki kamili za uraia ikiwa ni pamoja na kupata vitambulisho, kadi za kupiga kura, na pasi ya kusafiria |
| (xxxviii) | baadhi ya raia kutojumuishwa katika ajira ya umma, kwa mfano Wagoa (Goans), na Wanubi. |

### 8.2.5 Uchanganuzi

Ni dhahiri kwamba Katiba mpya sharti iwe na:

***(a) Umbo la sheria mpya za haki***

Mapendekezo haya yanaashiria uzito wa matokeo kuhusu umbo la sheria mpya za haki nchini Kenya. Vipengele vya marekebisho na mapendekezo ya wananchi yanasisitiza haki za jamii na mahitaji ya msingi ya binadamu. Tume inahakika kwamba haya yanaweza kupatikana ikiwa haki za uchumi na kijamii zitahalalishwa. Tumechunguza maendeleo ya kiuchumi na kisheria nchini Afrika Kusini. Hawa waliamua kutekelezwa kwa usawa haki hizo: aina zote za haki, na wameshawishika kwamba hakuna tofauti za dhati katika sifa zake, zinazoweza kuhitaji viwango tofauti vya katiba.

Haki zilizopendekezwa hapa zinajumlisha zile zinazopatikana katika katiba iliyopo, zilizofafanuliwa katika sehemu nyingine kulingana na ufahamu wa kisasa wa haki za binadamu. Baadhi ya haki hazikurejelewa kabisa katika katiba iliyopo, mapendekezo yote yanazingatia mawasilisho yaliyotolewa kwa Tume, kutokana na masharti na tajriba za nchi nyingine, kuambatana na sheria ya hivi majuzi na pendekezo la sheria, na hasa kwa majukumu ambayo Kenya tayari imeyachukua chini ya mikataba mbalimbali ya haki za binadamu, pamoja na zile zinazohusu haki za kiuchumi kijamii na kitamaduni, kwa wanawake na watoto.

Kwa hivyo, Tume inapendekeza kwamba kanuni za kwanza lazima zijaribu kuingiza haki za binadamu katika sera ya taifa na uamuzi kwa matumizi ya vyombo vya umma. Ionyeshe kwamba vyombo vya serikali lazima vichukulie sheria ya Haki za Binadamu

kuwa kiini cha vipengele vyao; kwamba serikali lazima ipange malengo ya wazi na kustawisha viwango vinavyofaa; lazima itambue nafasi ya raia. Aidha, lazima ishughulikie tatizo lililosababishwa na jukumu la kutoa manufaa elekevu katika baadhi ya miktadha kwa mfano maamuzi magumu lazima yafanywe katika jamii zote kwa sababu haiwezikani kuwa mahitaji yote yanaweza kutoshelezwa. Pamoja na vigezo, pia kushughulikia masuala yasiyo na ubishi kama yale yaliyomo katika katiba iliyopo. Imependekezwa kwamba masharti pia yafanywe katika makubaliano kuhusu masuala/hoja zifuatazo:

a) hadhi ya utu wa binadamu
b) usawa, usawazishaji na kutobagua hasa kuhusu kabila ama makundi ya kitamaduni ya waliowachache
c) kitendo sawazishi (Affirmative Action) katika hali zifaazo

Mawasilisho mengi yalitoa wito wa kitendo sawazishi kwa niaba ya wanawake, walemavu na hata kwa niaba ya sehemu za nchi zilizobaguliwa kiasi, ama zinazohitaji maendeleo maalumu. Hata hivyo, imependekezwa kwamba mipango ya kitendo sawazishi kilichothibitishwa na data kamilifu kwa kutumia mbinu na malengo mwafaka, itekelezwe kwa uwazi, iwekewe mipaka ya wakati na kusimamiwa kwa hali toshelevu. Aidha, yasifikie hali ya ubaguzi wa upendeleo.

***(i) Haki za Wanawake***

Masuala ya wanawake yalidhihirika wazi katika mawasilisho yaliyotolewa kwa Tume. Masuala yaliyozushwa na wanawake – na waume kwa niaba yao yalikuwa ya maeneo mapana, kutokana na hoja kwamba wanawake watachukua asilimia nne nukta moja (4.1%) za viti vya Bunge kuhusu matumizi ya nguvu majumbani na ujinsia, ubaguzi katika eneo la urathi, na kiwango cha chini cha kusajiliwa shuleni. Kuna maoni ya kinyume yaliyotolewa; wanaume waliosema kwamba kwa upande za Biblia, mwanamume ndiye kiongozi wa nyumba; watu waliosema kwa sababu wanawake ndio wengi kiidadi nchini, wangeshindania vyeo vya kisiasa n.k. pamaoja na wanaume; na baadhi waliosema kuwa wanawake wasirithi mali kutoka kwa baba

zao – ama ikiwa hawakuolewa – au kutoka kwa waume wao. Wengine walisema kuwa wanawake wangepata ardhi katika maeneo yaliyo na wanyama mwitu.

Imependekezwa kwamba kuwe na masharti yanayofafanua wazi haki za wanawake. Madai ya wanawake kuhusu kutendewa usawa, yaliyoungwa mkono na waume mahali pengi, yameelezwa kinaganaga, na hisia za maonevu ya wakati uliopita ni nyingi, hivi kwamba, japokuwa yameingilia na kanuni ya kutobagua kwa jumla, yaonekana kuwa jambo hili ni halali, katika juhudi za kuhakikisha kauli wazi ya nafasi ya zaidi ya asilimia hamsini (50%) ya idadi ya wananchi, ambayo ni wanawake.

- Ipige marufuku kisheria ubaguzi kuambatama na ujinsia, ujauzito, na hati ya ndoa.
- Kutaifisha misimamo ya kimataifa inayohusu haki za wanawake.
- Kuchukulia haki za wanawake kuwa tofauti na haki za watoto na za ndoa.
- Kutambua ubaguzi mara dufu unaokabili wanawake pamoja na
- Iruhusu kitendo sawazishi kinachopendelea wanawake
- Iwape wanawake haki sawa za kumiliki ardhi; kutambua urithi
- Kuwapa wanawake haki sawa za kuwapitishia watoto uraia.
- Kuondoa masharti kwamba wanawake lazima watoe sahihi ya waume zao ili wapate kitambulisho wakitumia jina la ndoa.
- Kutupilia mbali tabia za kitamaduni zinazobagua ama kuwadhuru wanawake.
- Kulinda maslahi ya wanawake yanayohusu wadhifa wa kuwa mama.
- Kutambua haki za wanawake wa Kiislamu walioingia eda baada ya kufariki kwa mume au baada ya talaka.
- Kupunguza mzigo ulioandama wanawake kwa sababu ya mahari, ama
- Kutambua changizo la kiuchumi na kipawa cha uwezo wa wanawake.
- Kuhakikisha haki za afya pamoja na upangaji uzazi – tazama hapo chini kuhusu haki za afya.
- Kulinda haki za wafungwa wanawake.

- Kubaresha usimamizi wa haki kwa kuwapa wajane mawaidha ya kisheria, pamoja na suluhu badalia za migogoro; tazama hapo chini kuhusu kupata haki.
- Kuunda utaratibu wa kisiasa wa kusimamia haki za wanawake.

### *(ii) Haki za wazee*

Thibitisho la kuwatenga wazee peke yao latokana na jinsi wanavyopuuzwa, na pia kuwa kwa namna mbalimbali ndiyo sehemu ya watu wanaweza kudhuriwa katika jamii. Jamii nyingi, hasa za kiafrika husisitiza kuwa wana heshima maalumu kwa wazee. Lakini mara kwa mara wazee huhisi kwamba hawapewi heshima wanayostahili, au kwamba hawatambuliwi kuwa ni wanachama kamili wa jamii zao, wenye haki za kuhusishwa humokwa hali zote. Kuna ushahidi kwamba wazee wengi nchini Kenya huwa katika hali ya kutengwa na wakati mwingine hu dhulumiwa, pamaoja na kutoshirikishwa kikamilifu katika jamii.

Yapasa kuwa na utambuzi wa jumla wa haki za wazee zinazoshirikisha wananchi wengine muongoni mwa jamii, pamoja na kutaja haki zakushiriki, kuendeleza maendeleo yao ya kibinafsi, kufanya kazi, kuwa huru kutokana na aina zote za unyanyasaji na dhuluma (matusi, kuishi kwa hadhi ya utu na hesima). Kuweza kujitengemea wenyewe na kutunzwa inavyostahili na kusaidiwa na familia na serikali. Wapange kustaafu kwao; wagawe ujuzi na ufahamu wao wa watu wengine, na wabaki wakifanya shughuli zao miongoni mwa jamii. Mashirika ya umma/kitaifa yachukue nafsi maalumu ya kujifunza na kujitayarisha kuwaelewa wazee na jinsi ya kushughulikia maswuala yanayowahusu.

Sheria lazima lifafanue wazi kwamba vyombo vyote vya umma viko chini ya uamuzi wa sheria ya Haki za Binadamu, na kwamba mahakama lazima iunde Sheria ya Mazoea (Common Law) – sheria iliyoundwa na jaji – kuhusu hoja hizi pia.

### *(iii) Haki wa Watoto*

Katiba iliyopo ya Kenya haisemi chochote maalumu kuhusu watoto. Sheria mpya, sheria ya watoto iliyopitishwa mwaka 2001 iliingiza katika sheria ya Kenya kanuni za

makubaliano ya kimataifa ya Haki za Mtoto, pamoja na mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Maslahi ya Mtoto. Ingawa sheria hii ina kiini lake mahali panapofaa, ipo haja ya kuendelea zaidi ya hapo.

Sheria za Bunge zinaweza kutupiliwa mbali kama zinavyoundwa. Kwa hivyo ni muhimu Katiba iweze kulinda watoto, kisheria. Ijapokuwa sheria inasema kuwa Bunge itoe kipaumbele kwa maslahi ya watoto, haiwezi kuwa na uwezo wa kuathiri Bunge wakati ikiunda sheria siku za usoni. Sheria za sasa haiwezi kuzuia sheria ya baadaye – ni Katiba tu inayoweza kufanya hivyo. Sheria haiweki ulazima wa kisheria kwa serikali, lakini Katiba inafanya hivi.

### *(iv) Familia na haki za binafsi*

Tume inapendekeza kuwa sharti la jumla kuhusu umuhimu wa familia liwe sawa na haki za kuoa/kuolewa, haki sawa katika ndoa, na wajibu wa jumla kwa wanafamilia, kila mmoja kwa mwenziwe, litaonyesha matumaini ya Wakenya. Hii huenda ikaruhusu matumizi ya ushahidi wa kisayansi katika mahakama, kuhusu uhusiano wa kifamilia; na serikali itajitahidi kugharimia jambo hili. Inapasa pia kuwa na haki ya jumla ya kuwa na jina na uraia, na kusajiliwa kwa kuzaliwa kuwao, endapo ni Wakenya.

### *(v) Haki za walemavu*

Kutokana na maoni yaliyowasilishwa na watu binafsi na mashirika, maandishi ya aina mbalimbali na taarifa ya Kikosi Tume kilichoundwa na Mkuu wa Sheria na kuongazwa na Bw. Jaji Aganyanya, na kilichowasilisha ripoti mnamo 1997, ni wazi kwamba walemavu wa Kenya wanakumbwa na matatizo mengi. Matatizo hayo yanatokana na sheria zinazobagua kimapendeleo ama kutekelezwa kwa njia ya ubaguzi. Baadhi yanatokana na ukosefu wa rasilimali iliyotengwa kwa huduma za ulemavu. Mengine yanatokana na huruma au ‘imani’ iliyopotoka. Mielekeo hii inaweza kutokana na kutojua, itikadi, woga wa kitu ‘tofauti’ au kielelezo cha utamaduni miongoni mwa jamii fulani, ujumbe unaotoka kwa walemavu hivi leo ni kwamba hawataki na hawana sababu kamwe ya kudhaniwa kuwa kama vitu, vya

kuonewa huruma au kupewa msaada, au hata sera zilizotungwa na wengine. Wanahitaji heshima, haki, sauti na uraia wao kamili kutambuliwa.

Ijapokuwa serikali ya Kenya iliadaa mswada wa sheria ya mlemavu ya 1977 bado haujawasilishwa bungeni. Ni muhimu katiba iingize masharti ya kulazimisha kuwepo kwa sheria kama hii. Ufafanuzi wa ulemavu uhusishe hali kama za kifafa, uzeruzeru, virusi vya ukimwi na hali nyingine zinazosabibisha ubaguzi lakini ambazo si lazima ziwe msingi wa kupunguza ujuzi.

***(vi) Haki za Wakimbizi***

Ijapokuwa hakuna kauli maalum kuhusu wakimbizi katika sheria ya marekebisho (hata katika katiba iliyoko), suala la wakimbizi linahusika katika usalama wataifa, na pia katika majukumu ya Kenya kwenye sheria ya kimataifa; mambo yaliyotajwa na sheria ya marekebisho ya katiba. Kama mataifa mengi ya Afrika, Kenya imepokea idadi kumbwa ya wakimbizi – tukiwa na maana ya watu waliotoroka makzi yao kwa sababu yoyote ile. Mwanzoni mwaka wa 2002 Shirika la Umoja wa Mataifa la Wakimbizi, Kenya ilikuwa na wakimbizi 239,221 ambapo 69,804 walitoka Sudan, 144,221 walitoka Somalia na 13,541 walitoka Ethiopia. Wengi wao wanaishi karibu na mpaka (Dadaab katika mkoa wa Kaskazini-Mashariki na Kakuma katika Bonde la Ufa). Ufafanuzi uliozoeleka wa mkimbizi ni mtu aliyetoroka nchi yake kwa sababu ya hofu ya kudhuriwa. Lakini Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Wakimbizi unatumia dhana hii kujumuisha pia watu waliolazimika kuhama makazi yao kwa sababu ya matukio yanayochafua sana utaratibu wa maisha katika nchi yake ya asili. Ufafanuzi huu unaweza kutumika kuelezea wakimbizi wa Kenya.

Wakimbizi kwa kawaida wanaishi katika kambi walizotengewa na wanaweza kuondoka tu kwa sababu maalum, kama vile kwa matibabu. Wengine hufaulu jukiepusha na agizo hili, kwa njia ya ufisadi, au kujificha wasionekane wanapojikaidi. Wanakumbana na ukatili wa polisi na usumbufu, na wakati mwingine wanashtakiwa kwa kuwa wageni wasiohalali hata kuwekwa gerezani na

kurejeshwa makwao kinyume na kanuni za sheria ya Kimaitaifa. Serikali ya Kenya haina sera ya wazi ya kushughulikia wakimbizi wala utaratibu wa kisheria. Inasikitisha kwamba rekodi ya serikali ya Kenya kuhusu wanavyotendewa wakimbizi haipendezi kamwe katika viwango vya kimataifa na heshima ya binadamu. Sio kwamba tunapuuza usumbufu unaosababishwa na wakimbizi au mzigo wanaotwika nchi ya Kenya na mataifa mengine ya Afrika uliozidi ule wa mataifa ya 'magharibi' kama Ulaya na Australia, au rekodi ya mataifa hayo ya Kimagharibi ambayo mara kwa mara inakashifiwa.

Masharti yawekwe kwenye katiba kuthibitisha kuwa wakimbizi wana haki ya kutorudishwa nchini kwao ambako wana hofu inayodhihirika ya kuteswa au kutendewa kwa hali inayohalalisha ukimbizi wao. Haki ya kimsingi ya watu waliotoroka nchi zao kwa hofu ya kuteswa na haki isiyovumilika, inayosababishwa na mizozo au ukame, na inayodhuru heshima ya binadamu (jambo hili tumelieleza kwa undani ili pasiwe na tatizo katika kufahamu kama mtu ni mkimbizi au la).

### *(vii) Kuondolewa adhabu ya kifo*

Mbali na masharti ya kawaida ya haki ya kuishi, adhabu ya kifo yafaa kuondolewa. Nchi kadha za Afrika zimefanya hivyo hivi majuzi pamoja na Afrika Kusini (mahakama ya kisheria). Baadhi ya katiba pia zimepiga marufuku adhabu ya kifo (kwa mfano Ureno na Brazili) katika nchi nyingi raia wengi wanaamini kuwa adhabu ya kifo itumike. Ushahidi pia unapendekeza kwamba adhabu ya kifo haiwezi tena kuzuia uhalifu kikamilifu kuliko kufungwa gerezani.

Kwa kuwa hakuna tena utekelezaji wa adhabu ya kifo nchini Kenya tangu mwaka 1984, kuondolewa hakutabadilisha hali ilivyo sasa. Kwa hakika hali iliyopo kwa sasa inazidisha madhara makubwa kwa waliohukumiwa kifo pamoja na familia zao, kwani wanaweza kubaki kwenye "safu ya kifo" kwa miaka mingi bila kunyongwa au kusamehewa.

### *(viii) Ulinzi wa faragha*

Lazima pia yawepo masharti yanayotoa ulinzi wa jumla wa faragha za nyumbani, za mtu, barua na njia nyingine za mawasiliano. Hii ni muhimu kwa tabia za mawakala wa kudhibiti sheria na pia kwa raia wenzetu.

### *(ix) Kufikia vyombo vya habari*

Kusema kweli, pengine si muhimu kutoa utambuzi maalum kwa vyombo vya habari, ila umuhimu wao ni katika maisha ya sasa, na ukweli kuwa serikali kila mara inajaribu kuviingilia vyombo hivyo ili kuzuia haki zinazothibitisha masharti maalum. Hii itaongeza ukweli kwamba watu wengi katika kutoa maoni yao kwa Tume walitaka "Uhuru wa vyombo vya utangazaji" maana yake ni kwamba utoaji wa leseni kwa redio na televisheni usitumiwe kama mbinu za kuwanyima wananchi nafasi ya kusikia au kuona vipindi vya kampuni zenye uwezo zinazotaka kutangaza kufikia mbali. Uhuru wa kujieleza na demokrasia vimestawi kutokana na uhuru wa kubadilishana mawazo, wala si mawazo kutoka katika chanzo kimoja tu. Kwa upande mwingine, uwezo wa habari na utangazaji ni mkubwa mno wala si vyombo vyote vinavyowajibika.

Kwa hivyo inapasa kuwa wazi kwamba uhuru lazima uandamane na uwajibikaji. Hii inajumuisha wajibu wa kuendeleza maadili ya kikatiba, ikiwa ni pamoja na, hasa, kustahimili na kuheshimu haki za binadamu. Inapendekezwa sifa za utaratibu huo ziwe kulinda vyombo vya habari kwa ujumla, kutokana na kuingiliwa kati na serikali; kupewa leseni awali kunapaswa kutumiwa tu katika hali zisiso za kawaida; utoaji wa leseni ya kutangaza au vyombo vingine vya utangazaji unapaswa kuendeshwa na kitengo fulani kisicho na upendeleo wowote kuhusiana na maslahi ya kisiasa na kiuchumi, na kutekelezwa na lengo la kutoa uhuru kamili wa watu kupokea habari. Kwamba lazima kuwe na matumizi ya haki ya vituo vya utangazaji – ili nafasi ya kutangaza isinunuliwe na watu wachache na kuitawala; kwamba masharti ya kufaa katika maswala ya kudhibiti hotuba ya chuki, picha za ngono, kulinda usalama wataifa, kuanisha filamu n.k., inakubaliwa mradi tu masharti hayo yanafaa.

***(x) Kupata afya, usafi, maji na chakula***

Kama haki ya kiuchumi na kijamii inatambuliwa kuwa serikali inapaswa kutenda zaidi ya rasilimali zake zinavyoiwezesha. Kwa kutazama kiwango cha juu cha umaskini humu nchini, ni muhimu kwa Katiba kuzingatia haki hizi za kupata afya,usafi, maji na chakula. Isitoshe, kunyimwa haki hizi huathiri haki nyingine. Kwa mfano, jukumu gumu linalohusisha wanawake wa Kenya la kutembea mwendo mrefu kutafuta linamaanisha kwamba suala hili lina umuhimu kwa usawa wa kijinsia na hadhi ya utu. Usafi ni suala linalohusiana na afya, na lilishughulikiwa zaidi na wengi waliowasilisha maoni yao kwa Tume, hasa watu wanaoishi katika mitaa ya mabanda. Ushahidi pia ulionyesha wazi gharama ya kuzika wafu – hili kwa hakika ni jambo mojawapo la kuhusu hadhi ya utu. Haki hizi ni miongoni mwa zile ambazo zilisisitizwa sana na kuhitajiwa na wananchi wa kawaida walitaka.

***(xi) Haki ya usalama wa kijamii***

Hii pia ilikuwa mada kuu katika mawasilisho mengi; kulindwa kwa wazee, maskini, walemavu na watu wasio na kazi. Hili pia linaweza tu kutendeka hatua za kufaa na pia kutegemea rasilimali zilizopo. Sekta isiyo rasmi inapaswa kushirikishwa.

***(xii) Haki ya mazingira yenye Afya***

Mawasilisho mengi yaliyotolewa kuhusu umuhimu wa kulinda mazingira yalieleza malalamishi kuhusu uondoaji wa taka jijini Nairobi na pia mabaki ya uchafu wenye sumu katika maeneo ya Mkoa wa Kaskazini Mashariki na uharibifu wa misitu katika sehemu nyingi za nchi. Kwa mujibu wa haya, kuna mapendekezo ya masharti yatakayoweka kanuni za msingi ikiwemo: Haki ya Mazingira yenye afya na kanuni za msingi za maendeleo endelevu. Masharti mengine kuhusu ulinzi wa mazingira yanapatikana katika sehemu inayohusu Ardhi na maliasili.

***(xiii) Haki za Makao na Nyumba***

Wakazi wa mitaa ya mabanda na wafanyikazi za shambani huwa katika hatari ya kufukuzwa na kusumbuliwa na wenyenyumba na wengineo. Haiwezekani Katiba kuweka mfumo wa kuikarabati mitaa ya mabanda, lakini kiwango kikubwa cha watu

waishio katika miji, na ambao hupatikana katika mitaa ya aina hii (labda asilimia sitini na tisa - 69% - mjini Nairobi) wanahitaji kuitazamia katiba kama chanzo cha kudai haki ya kuwa na hali ya maisha yaliyo bora. Si wakaazi wa sehemu za miji tu walio katika hatari ya kufukuzwa, au wanaoishi katika hali duni kama vile Ogiek, au maskwota wa matava ambao walifukuzwa kutoka milima ya Chyulu wanaweza kutoa ushahidi.

***(xiv) Haki ya Elimu***

Hii ni haki mojawapo ya msingi ambayo ilizungumziwa mara kwa mara katika mawasilisho kwa Tume.

***(xv) Ulinzi wa Lugha na Utamaduni***

Sheria ya Marekebisho inaagiza utambuzi na ukuzaji wa dini, tamaduni na wingi wa tofauti za kikabila pamoja na umoja wa kitaifa. Ni muhimu kuwa, kwa mfano, kiswahili kikuzwe kama lugha ya taifa. Umoja wa kitaifa utakuzwa tuendapo wananchi wataona kuwa tamaduni zao zinaheshimiwa. Hili basi ni sharti mojawapo litakalokuwa muhimu katika kuzingatia hifu na wasiwasi ya walio wachache na jamii ambazo zimezungumziwa awali katika sehemu ya **"Usawa na kutobagua"**. Uhuru wa jumla wa kidini, na kutobagua utachangia katika kuyatimiza malengo haya lakini inapendekezwa kuwa katiba ipige hatua zaidi na itambue haki za lugha na uelezaji wa utamaduni.

***(xvi) Kufikia Habari***

Kenya ilirithi, kutoka kwa utawala wa kikoloni, tamaduni za usiri ambazo hata sasa zinaendelea, ingawa nchi nyingi katika miaka ya hivi majuzi zimechukua mwelekeo wa kuwa wazi kiasa hasa kuhusu kuwapatia wananchi habari. Sheria za usiri zilizopo sasa zina misingi katika sheria za vingereza ambazo zimebadilishwa kwa kiasi kikubwa katika miaka ishirini (20) iliyopita, na huko uingereza na katika nchi nyinginezo. Uhuru wa habari ni muhimu kwa ushiriki wa wananchi, mijadala ya umma yenye ufahamu na kadhalika. Wananchi waliilalamikia Tume kuhusu usiri – hasa walilalamika kwa dhati kuhusu mazoea ya serikali kuwanyima wananchi

matokeo ya uchunguzi uliowekwa na serikali kwa kutumia pesa za umma unatozwa ushuru/kodi.

Tume yapendekeza kuwe na haki ya kuipata habari za kitawala, isipokuwa yamayohusu usalama wa kitaifa, na kuhusu habari zinazohitadhiwa na wengine, ambazo ni muhimu katika kutekeleza haki. Wakati wa kutosha uliokadiriwa ungetolewa kwa marudio ya sheria iliyopo sasa, na kuanzishiwa kwa sheria mpya na mbaina zinazofaa.

***(xvii) Kuhitajika kwa kitendo cha usimamizi wa haki***

Mawasilisho yalilalamikia si tu ufisadi katika huduma za umma (tatizo kubwa) bali pia kutojimudu kazini, mapendeleo na kutokuwapo na muelekeo unaojali watu kwa jumla. Katiba ya Afrika Kusini inatoa mfano wa awali katika muundo wa kuwa na kitendo cha haki ya usimamizi – ya kisheria, tafakuri na utaratibu wa usawa. Imependekezwa kuwa sharti kama hili likubaliwe kuingizwa nchini Kenya. Kanuni kama hiyo itatatua, tatizo kutoka shinani na hivyo kupunguza wingi wa kazi katika mahakama ama asasi nyinginezo zinzoshughulikia malalamiko. Pia ingeusaidia utawala kufanya uamuzi bora.

***(xviii) Haki za waliowekwa vizuizini***

Miongoni mwa mawasilisho yaliyotolewa kwa tume, kulikuwa na mengi yaliyo fahamisha kwamba hali za magereza nzuri kwa binadamu. Kulikuwa na baadhi waliolalamika kuwa walitendewa kinyume cha imani zao za kidini, kama vile, kutowaruhusu wanawake kuvaa mavazi yaliyo pendekezwa na dini zao, ama kunyoa nyele na/ama kidevu cha Muisilamu, sikh au waumini wa kanisa la Dandora. Idadi ya mawasilisho ya wananchi wa kawaida kuhusu hali mbaya za jela yadhihurisha waziwazi vile ambovyo wakenya wamehamasika vilivyo kuhusu kuhitajika kwa hadhi ya utu kwa wote. Hata maafisa wa jela walisema jinsi hali zilivyokuwa mbaya kwa wafungwa. Na tukumbuke kwambo, watu wengi waliotiwa kuzuizini hawajahukumiwa bali wanangojea kushtakiwa. Kamati kuu (Standing Committee) ya haki za binadamu ilitoa ripoti mwaka 2002, kwamba zaidi ya asilimia arubaini (40%)

ya waliomo jela wako katika kitengo hiki. Pia kuna wengi waliozuiliwa katika korokoro za mapolisi. Ushahidi waonyesha kwamba hitimaye watu wengi hawahukumiwi kamwe. Kwa hivyo ni lazima tuchukulie kuwa hawana hatia lakini huwa wamewekwa katika hali hizi mbaya mara nyingi kwa muda mrefu. Isitoshe, adhabu ni hali ya mtu kupoteza uhum wake: kama inavyosemekana mara nyingi "wafungwa wako gerezani kama adhabu, sio kwa ajili ya adhabu". Wafungwa wengi hatimaye wataachiliwa na pikumu moja kubwa la kifungo linapswa kuwa kuwatayarisha ili wawe wanajamii wanaotekeleza nyadhifa zao; hali gerezani zinapaswa kusaidia kufikia madhumuni haya. Katika jamii inayoheshimu haki za binadamu, ni makosa kwamba wafungwa wanyanymwa heshima za kimsingi kama kamati kuu yenye mamlaka (Standing Committee) ilivyosema, "Wafungwa si binadamu duni kuliko wengine"

Tume inapendekeza kwamba kanunu za msingi ziimarishwe na katiba.

***(xix) Haki za wateja***

Kila mtu katika jamii ni mteja wa mali na utumishi unaotelewa na serikali au ujasiri wa kibinafsi, au hata na mashirika yasiokuwa ya serikali. Ingawa kuna ukweli katika msemo kuwa "unakipata unachokilipia", ukweli ni kuwa, nchini Kenya leo, wateja hawapati kile wnachokilipia katika huduma nyingi, hasa zile zinzotolewa na vyombo vya srikali kama malipo ushuru, kodi za mitaa, na malipo mengine. Wateja wenyewe wana jukumu la kuwa waangalifu, na kudai wapewe kile wanachokistahili, lakini inafaa pia katiba kama hii inayotarajiwa kufanya marekebisho kamili, ulinzi sharti utolewe kwa wateja.

***(b) Kanuni za Utekelezaji***

Ni muhimu kuzipa asasi uwezo wa kutosha ili kutekeleza haki. Inapasa watu waweze kwenda mahakamani, lakini jambo hili ni ghali na linatumia wakati mwingi. Haki ya kuweza kuleta mashtaka lazima iagizwe na katiba, lakini kwa njia isiyozuia mtu yeyote. Mahakama yamefafanua agizo hili kwa njia finyu sana. Hasa, inapendekezwa kuwa agizo

hili limefikiria uanzishaji wa aina ya mashtaka yanayosisitiza haki yenye upana kuliko mahitaji ya kirasmi, ikiwa haki za binadamu ziko hatarini.

Chombo muhimu cha utekelezaji wa sheria ya haki ni kuzingatia uoaji taarifa kilimwengu na masharti ya kufuatilia. Ijapokuwa taarifa hutolewa na vyombo vya mikataba vinayohusika, na wakati mwingine kauli kali zinaweza kutolewa, jukumu muhimu la mfumo lilikuwa ni kuuhitaji mataifa binafsi kurekebisha utendakazi wake. Maandishi kuhusu mfano yanaonyesha kwamba ili kuripoti kuwe na nguvu, utayarishaji wa taarifa sharti uwe tukio la kitaifa, ambapo raia wanapewa fursa kushiriki na kutoa maoni kuhusu utaratibu wake. Kwa bahati mbaya nchini Kenya hata utayarishaji na uwasilishaji haujafanywa.

Inapendekezwa kwamba Katiba ijaribu kuhakikisha kuwa serikali inatoa taarifa (uwe wajibu katika Katiba) na jukumu la kuripoti lionekane kuwa la manufaa kitaifa. Wananchi washirikishwe kikamilifu, pamoja na wabunge. Tena Katiba iundwe ili ihakikishe kuwa serikali inakusanya habari, na kuandaa dhana na vigezo vya kufuatilizia vitakavyosaidia utaratibu wa kuripoti na uchanganua. Kwa hivyo wajibu utoe utaratibu kwa masharti ya kijumla ya haki za binadamu yanayofafanuliwa katika sheria za haki.

***(c) Mipaka ya haki***

Katika katiba nyingine kila haki katika sheria za haki imeandamana na agizo kuhusu mipaka yake. Huu ni mkabala wenye usumbufu na kuna hatari ya kuweka mapengo. Inapendekezwa kuwa kuwe na agizo la jumla linalosema kuwa haki zinaweza kuwekewa mipaka lakini masharti yawe makali: yaliyofikiriwa na yenye maana katika jamii iliyo wazi na ya kidemokrasia na yenye msingi wa heshima kwa binadamu, usawa na uhuru, kwa kuzingatia hali zote zinazohusika na kauli muhimu zionyeshwe kwa manufaa ya mahakama.

Hali mahsusi zinaweza kutokea na kusababisha uwekaji mipaka wa muda au upunguzaji wa haki.

Katiba nyingi zina masharti mengi kuhusu hoja hizi. Kanuni ya jumla kwamba sharti katiba itekelezwe na ifafanuliwe ili ifikie imani iliyoiongoza, itatumika katika hali za kipekee ambazo haziwezi kuingizwa moja kwa moja kwenye maneno ya masharti haya.

***(d) Wajibu na majukumu ya kimsingi***

Japo ni muhimu katiba kuagiza ulinzi kamili wa haki za kimsingi, inahitajika kukubali wajibu na majukumu ya wananchi na wakazi. Kupitia mapendekezo yetu kuhusu mipaka ya haki tumetoa kaida na taratibu za kusawazisha maslahi ya mtu binafsi na maslahi ya jamii. Lakini tungetaka kusisitiza majukumu ya wananchi katika uundaji wa taifa linalojali na lenye utu. Hatupaswi kuitegemea mno serikali, na hatupaswi kujiona kama uhusiano wetu na serikali ni wa kupingana. Jukumu la kuhakikisha jamii inayojali yenye haki na utu ni la serikali, raia, na watu binafsi. Majukumu ya mtu binafsi kwa familia na jamii yake hayana mizizi yake katika utamaduni wa jamii wa Kiafrika (kama vile ilivyo katika masharti ya mtu binafsi). Kutojali kwa mtu binafsi kuhusu heshima kwa maadili ya taifa na demokrasia yamekuwa msingi wa kuporomosha utawala kwa sheria na kusababisha ufisadi nchini mwetu. Katiba mpya itaimarika tu, endapo wananchi watajitolea kuitetea na kuitekeleza.

### 8.2.6 Mapendekezo

Tume inapendekeza kuwa Katiba mpya:

*(i) Kama sharti la jumla:*

(a) haki ya kuishi ihakikishwe
(b) ulinzi wa hadhi ya binadamu uhakikishwe
(c) kulinda haki ya kuchagua kazi na kujiunga na mashirika
(d) kuweka haki ya kupata 'dhamana' ijapokuwa pakiwepo sababu tosha ya kuamini kuwa mtu huyo hatafika mahakamani kujibu mashtaka dhidi yake. Zingatia kuwa hii

ni tofauti na hali iliyopo sasa ambayo ni dhaifu kuhusu haki za kuachiwa huru kwa dhamana

(e) ushahidi uliopatikana kupitia kuteswa na polisi, na misako isiyo halali usikubaliwe

(f) Kujumuisha kanuni za kimsingi zilizopo katika maongozi ya wastani ya Umoja wa Mataifa kuhusu jinsi ya kuwatendea wafungwa

(g) kutoa utaratibu wa kuwalinda watumizi

(h) kuweka utaratibu wa kuongoza mahakama na makundi mengine kwa ujumla katika kutafakari sheria ya haki kwa kuzingatia katiba na sheria ya kimataifa n.k.

(i) eleza kuwa sheria ya haki haitumiwi tu kwa walioko serikalini lakini kwa watu wote, na kuweka utaratibu kuwa sheria ya haki inawafungamanisha watu katika mashirika ya umma na kuwa ni lazima mahakama zitoe uamuzi kuambatana na sheria hizo

(j) kuacha utaratibu unaosinya wa kuwekea mipaka haki, na kuzingatia utaratibu wa kijumla unaoelezea kuwa haki zinaweza kuwekewa mipaka; lakini masharti ya mipaka hiyo yanapaswa kuwa magumu

(k) kuweka mipaka kuhusu hali ambapo hali ya hatari inaweza kutangazwa, wakati na yule anayaweza kuitangaza hali hiyo

(l) hakikisha wafungwa wa hali ya hatari:

(m) wanaweza kufika mahakama

(n) wana uwezo wa kufikia taasisi kama Tume ya Haki za Binadamu na utawala

(o) kuanzisha mashirika au vituo mbalimbali kama vile Mpokea Malalamiko ili kuimarisha na kutekeleza utekelezaji wa haki.

(p) hakikisha kuwa vyombo vyote vya serikali vinalazimika kutambua sheria ya haki kama sehemu muhimu ya madhumuni yao, ni lazima taifa lielezee malengo kamili na kuandaa vigezo.

(q) kuwapatia raia fursa ya kushiriki na kutoa maoni juu ya utaratibu wa usimamizi na utoaji wa ripoti kuhusu mikataba na vifaa vya kimataifa.

(r) katiba lazima ihakikishe kwamba utawala hautoi ripoti tu, bali inaelekeza jukumu ya ripoti katika kunufaisha taifa.

(s) inatoa maagizo ya majukumu na wajibu wa raia. Inasisitiza kuwawajibisha watu binafsi kwa ajili ya jamii yenye utu na upendo; yenye kutarajia maafikiano kuhusu kanuni za uraia katika kanuni za kujali umma.

(t) kutoa mbinu za kutaifisha vigezo na mikataba ya kimataifa
(u) kuwa hakikishia wafanyikazi wote haki za kuwa na vyama vya wafanyikazi n.k.
(v) kutambua kutogawanyika na kuingiliana kwa haki zote za kisiasa, na kiuchumi; haki za jamii na kitamaduni; haki za mazingira na maendeleo na kuzithibitisha.
(w) kuunda sera na asasi (mf. Mpokeamalalamishi na Tume ya Haki za Binadamu, Tume ya ujinsia n.k.), kuendeleza juhudi za wananchi katika kujipatia elimu, afya, makazi na chakula.
(x) kuanzisha utaratibu kwa haki za kiuchumi, jamii na kitamaduni, zinazohitaji serikali igawanye rasilimali kwa njia ya uangalifu ili kupunguza uharibifu na ufujaji, na wakati huo huo kulenga utekelezaji wa mahitaji ya kimsingi ya Wakenya.
(y) kuzuia ubaguzi katika haki za kijamii na kiuchumi kuambatana na ujinsia, ujamzito na hali ya ndoa.

*(ii) Kuhusu Wanawake*

(a) Kutambua na kulinda wanawake kama kundi maalumu la watu walio na haki maalumu na mahitaji, ambayo ni pamoja na hadhi yao ya kipekee ya kuwa akina mama katika jamii.
(b) Kuwapa wanawake nafasi pana itakayowawezesha kufikia upeo wa vipawa vyao na maendeleo.
(c) Kutambua haki za kitendo kisawazishi (Affirmative Action) kwa wanawake; kushughulikia upya hali za kutolingana zilizosababishwa na historia, mila ama sheria. Hasa, katika Serikali ingechukua uwezo wa kisheria utawala (usimamizi) na mbinu nyinginezo ili kuhakikisha kwamba:

- Angalau thuluthi moja (1/3) ya wanaoshikilia vyeo kwa njia ya uchaguzi, katika afisi za kikatiba wawe ni wanawake.
- Kuna haki za usawa na ugawanyaji sawa kuhusu urathi na uraia.
- Itikadi haribifu za kitamaduni zinazochimba utu, afya na hadhi ya wanawake zimekomeshwa.
- Wanawake walio na mahitaji maalumu, pamoja na wanawake wa kiislamu walioingia kwenye eda (muda wa kutenganishwa baada ya

kufiliwa na mume ama kupewa talaka), wanawake wafungwa, wanawake walemavu, wajane, wanawake wazee n.k. watambuliwa na kupewa ulinzi maalumu na serikali na jamii.

- Ndoa zilizohalalishwa kwa njia yoyote ile zinatambulika, kusajilishwa na hati kutolewa.
- Kuna Tume ya Ujinsia ya kusimamia uhamasishaji na Haki za Ujinsia.
- Kuhakikisha kwamba wananwake wana uwezo wa kujitambulisha kibinafsi, pamoja na kuwa na haki ya kuchagua jina.

*(iii) Kuhusu Watoto*

(a) Ishughulikie hasa haki na mahitaji ya watoto ambao ni kitengo maalumu katika jamii yetu.

(b) Kukita masharti maalumu kwa Sheria ya Watoto ya 2001.

(c) Kuwekea masharti mamake na babake mtoto wawe wameoana ama la, kulinda na kumlea mtoto.

(d) Kuagiza hususan kwamba kila mtoto ana haki ya:

- Kuishi
- Kupata jina na utaifa na kusajiliwa mara tu wanapozaliwa.
- Kulelewa na wazazi wake ama kupata malezi badala ambapo mtoto ametenganishwa na wazazi wake.
- Kupata elimu ya bure, ambayo itakuwa ya lazima.
- Kulindwa kutokana na ubaguzi, mila haribifu za kitamaduni na itikadi, unyanyasaji, kupuuzwa ama kudhulumiwa.
- Kulindwa kutokana na aina zote za unyanyasaji na kazi yoyote inayohatarisha maslahi ya mtoto.
- Kupata chakula bora, makao, huduma za kimsingi za afya na huduma za kijamii.
- Uhuru wa kutokuwa na adhabu ya viboko, ama aina nyingine za matumizi ya nguvu au ukatili, na matendo yasiyo ya kiutu shuleni na taasisi nyinginezo zinazoshughulikia malezi ya watoto.

- Kutoshiriki katika mapambano ama kuandikishwa katika ghasia za matumizi ya silaha.
- Kutoshikwa ama kuzuiliwa isipokuwa kama ni hatua ya mwisho ambapo mtoto ameshikwa ama kuzuiliwa. Hapo azuiliwe kwa kipindi kifupi iwezekanavyo; atenganishwe na watu wazima anapokuwa kizuizini; apewe msaada wa kisheria na serikali; na apewe haki ya kusikilizwa.
- Kutoa sheria ya kuwawajibisha wazazi ambayo itahakikisha kwamba akina baba na akina mama watawajibika kulea na kulinda matoto hata kama wameoana au la.

*(iv) Kuhusu Walemavu*

(a) Itoe masharti yanayotambua haki za watu walemavu kama kitengo maalumu cha wananchi wenye mahitaji maalumu, yanayofaa utambuzi maalumu na ulinzi wa serikali na jamii.

(b) Kuafiki makubaliano ya kimataifa yanayohusu watu walemavu.

(c) Kuona kwamba watu walemavu wanapewa vifaa mwafaka na nafasi za kuweza kufikia upeo wa vipawa vyao na maendeleo.

(d) Kutambua kwamba watu walemavu wana haki ya kitendo kisawazishi kitakachowawezesha kushughulikia hali za kutolingana zilizosababishwa na historia, mila na sheria; na serikali lazima uchukue sheria, usimamizi na mbinu nyingenezo kuhakikisha kwamba:

- utu na heshima vipo.
- Haki ya hadhi ya utu na heshima inatambuliwa kuhusu watu mashuhuri walemavu.
- Kuelimisha makabila katika jamii juu ya visababishi vya ulemavu na mahitaji ya heshima na hadhi ya utu kwa watu wenye vilema.
- Kuhakikisha kwamba elimu, vyuo na vifaa vya matumizi ya walemavu vimejumuishwa katika jamii kwa ujumla, kulingana na panapofaa kwa manufaa ya walemavu.

- Kuhakikisha kwamba wanaweza kufika mahali popote, kufikia mahali pa usafiri wa umma, kupata taarifa, mawasiliano na nyumba za walio walemavu.
- Kuhimiza uendelezaji na matumizi ya lugha ya ishara, Breli na matumizi ya mbinu nyingine mwafaka za mawasiliano.
- Kuondoa katika matumizi rasmi ya lugha yoyote ile, maneno yanayodunisha yanapoelekezwa kwa walemavu; vile vile kuondolewa katika matumizi ya lugha ya faradha.
- Urahisi wa kupata vifaa saidizi kwa matumizi ya walemavu.
- Walemavu watumie haki zao za kupiga kura na kushiriki kikamilifu katika utaratibu wa uchaguzi.
- Walemavu waliokifungoni na gerezani wanapewa haki maalumu kama wafungwa wengine kama ilivyoelezwa katika katiba hii.
- Walemavu wanapewa nafasi za kazi kuambatana na mafunzo na ujuzi wao.

*(v) Kuhusu Wazee*

(a) Kutoa masharti ya kutambua haki za wazee kama kitengo cha watu maalumu, wenye mahitaji maalumu yanayotaka kutambuliwa na kulindiwa na serikali na jamii.

(b) Kutaka serikali uchukue uwezo wa kisheria, usimamizi, na mbinu nyinginezo kuhakikisha kwamba wazee:

- wanashiriki kikamilifu katika jamii
- kuendeleza maendeleo yao ya kibinafsi
- kutekeleza haki zao za ufanyikazi
- wako huru kutokana na aina zote za ubaguzi na unyanyasaji wa dhuluma
- wanaishi kwa hadhi ya utu na heshima
- wanaendelea kujitegemea
- kufurahia haki nyingine zozote zilizoorodheshwa katika sheria za Haki za Binadamu

- wanapokuwa hawawezi kujikimu na/ama kutosheleza wanaowategemea wanahaki ya kupata usaidizi kutoka kwa serikali na jamii.

*(vi)* *Kuhusu Wakimbizi:*

(a) Inahitaji serikali kutoa masharti ya kutambua haki za wakimbizi kama kitengo cha watu walio na mahitaji maalimu, yanayotaka kutambuliwa na kulindwa na serikali.

(b) Kutaka serikali ichukue uwezo wa kisheria, usimamizi na mbinu nyinginezo kuhakikisha kwamba:

- haki ya wakimbizi ya kupewa hifadhi imetambuliwa na itatolewa kulingana na sheria na utekelezaji wa kimataifa.
- Hakuna mtu atakayehamishwa kutoka Kenya hadi nchi nyingine, ikiwa atashitakiwa kwa kosa ambalo adhabu yake ni kifo.
- Mnamo mwaka mmoja wa utekelezaji wa katiba mpya, kuna maafikiano kamilifu na sheria ya kimataifa na utelezaji unaomiliki kanuni za kuwapa wakimbizi hifadhi nchini Kenya.
- Kuidhinisha na kutaifisha makubaliano yote ya kimataifa yanayoshughulikia haki za wakimbizi.
- wakimbizi wana haki ya kutorudishwa nchi ambamo wanahofu za kimsingi kuhusu kuteswa ama kutendewa mambo yatakayowafanya wastahili kuwa wakimbizi.

*(vii)* *Kuhusu jamii zilizowekwa pembeni:*

(a) Kutaka serikali ichukue kitendo kisawazishi kuhusu makundi yaliyotengwa (yaliyowekwa pembeni) kwa ajili ya ujinsia, idadi, ulemavu, umri ama sababu nyingine inayotokana na historia, itikadi na mila.

(b) Mipango ya kitendo kisawazishi, iliyothibitishwa na data kamilifu kwa kutumia mbinu mwafaka na malengo, zilizotekelezwa kwa uwazi; zenye mipaka ya wakati na kusimamiwa kwa hali toshelevu si ubaguzi wa upendeleo.

## SURA YA TISA

## TAIFA NA MFUMO WA KISIASA

### 9.1. Agizo La Tume

Agizo la Tume chini ya sheria hii ni kuhakikisha kuwa masharti yamewekwa katika Katiba:

- yanayounda mfumo wa utawala ulio huru, wa kidemokrasia na ambao unaheshimu utawala mwema, katiba, utawala wa sheria, haki za binadamu na usawa wa jinsia:
- yanayokuza kushiriki kwa wananchi katika utawala wa nchi kupitia uchaguzi huru, wa haki na wa kidemokrasia.

Sheria inaendelea kutaja kuwa kanuni ziwekwe katika Katiba. "... zinazoheshimu wingi wa tofauti za kikabila na kieneo na haki za kijamii, pamoja na haki za jamii kujiandaa na kushiriki katika shughuli za kitamaduni na kuutambulisha ubinafsi wao". Isitoshe, sehemu 3(h) inaiagiza Tume kushirikisha kanuni za "… kuimarisha ushirikiano na umoja wa kitaifa."

Tume inawajibika pia "…. kuchunguza na kupendekeza kuhusu uwezo wa Jamhuri wa uwekaji na utekelezaji wa mikataba na mambo mengine muhimu yatakayochangia katika kuimarisha utawala mwema na uzingatiaji wa majukumu ya Kenya katika sheria ya kimataifa.

### 9.2. Itikadi ya Taifa

#### 9.2.1 Kanuni za Jumla

Tume inashauriwa kuwa si lazima Katiba mpya ijengwe katika misingi ya filosofia muafaka ya maisha tu, bali pia ijengwe katika misingi ya itikadi ambayo itatuhakikishia amani endelevu, usalama, umoja, ustawi, uhuru, maslahi na hali ya wema wa wananchi wote wa Kenya. Itikadi ni mkusanyiko wa imani na kanuni za sheria za kijamii ambazo

hutamkwa na kikundi au mwelekeo wa kisiasa ili kutimiza malengo yake. Katika muktadha huu, itikadi ni jumla ya matumaini ya kitamaduni na hata kitaifa ambayo yameratibishwa, imani na shughuli ambazo huwawezesha wananchi kuwa na mielekeo ya kifikra kuhusu ukubalifu wa falsafa ya pamoja au mwelekeo wa pamoja kwa masuala yanayowahusu.

Itikadi basi ni chombo muafaka cha kuleta pamoja ufahamu unaofaa miongoni mwa umma wa baadhi ya masuala ya kimsingi kuhusu majukumu ya kijamii, kisheria na kisiasa ambayo yanaikabili jamii siku, baada ya siku ili iweze kutimiza malengo yake muhimu katika mwito wake ambao tayari umewekwa na uliomo katika makubaliano ya kijamii. Itikadi hubainisha maono na wito wa taifa ikiwemo pia mbinu za kuyatimizia haya (maono na wito).

### 9.2.2 Itikadi Katika Katiba Ya Kenya

#### *(a) Katiba ya Uhuru*

Wakati wa uhuru, Kenya ilitangazwa kuwa Jamhuri na mojawapo ya masharti ya uhuru ilikuwa kwamba taifa hilo huru liibuke na serikali iliyoweka msingi katika wananchi na mfumo wa utawala uliotawanyika, *Majimbo*. Lengo halikuwa tu kumpatia kila mmoja ulinzi wa kisiasa bali pia kuwaleta walio wachache katika ukuruba wa ugawaji uwezo na kushiriki katika utawala wa Taifa jipya. Mfumo wa utawala uliotawanywa haukupendelewa sana na viongozi wapya na matokeo yakawa mfumo wa *majimbo* ulivunjwa mara tu baada ya uhuru na badala yake pakawekwa mfumo wa utawala mkuu uliokuwa na makao makuu Nairobi.

Mfumo wa *majimbo* ulipoondolewa pakaingia mfumo wa *Ujamaa wa Kiafrika* ambao kiini chake kilikuwa mwito wa kujisaidia wenyewe, au *Harambee*. Uliibuka kama kiitikio na upinzani wa hali iliyokuwa ikiongezeka ya kupendelea ukomunisti na ujamaa

wa mrengo wa kimashariki. *Ujamaa wa Kiafrika* ulisisitiza utambuzi wa turathi bora zaidi za Kiafrika nchini Kenya na urithi wa kiuchumi wa kikoloni. Ulilenga kuwaleta pamoja wananchi ili kuungana, na kwa dhati na mpango maalum, kuukabili umaskini, maradhi na kutojua. Lengo kuu lilikuwa kupata *uhuru kutokana na uhitaji, magonjwa, na unyonyaji; kupata haki za kijamii, utu, nafasi sawa, usawa wa kisiasa, usawa wa kiuchumi na maslahi ya wote kupitia uponyaji mwema, mwelekeo, udhibiti na ushirikiano.*

Licha ya uwazi wa mwelekeo huu, hata hivyo, Ujamaa wa Kiafrika haukudumishwa na kukuzwa kama itikadi ya Taifa inayohusu uendeshaji wa mielekeo ya Kenya ya kisiasa, kijamii, kitamaduni na kiuchumi. Punde si punde, mienendo ya kisiasa na utawala wa Taifa, kimsingi, vikaenda sambamba na kanuni kuu na malengo ya Ujamaa wa Kiafrika. Ufisadi, ukabila, kutovumiliana kisiasa na sifa nyingine za utawala mbaya, kama vile ulimbikizaji wa uwezo na mali katika mikono ya wachache, zikaota mizizi.

Wakati Rais Moi aliposhika hatamu mnamo 1978, alianzisha na kupendekeza kile ambacho hatimaye kilifahamika kama Mwito wa Nyayo (kufuata nyayo) ambao ulikuwa na misingi katika *kujali maslahi ya watu wengine*. Mwito wa Nyayo ulipendekeza *Amani, Upendo na Umoja* na kulikuwa na juhudi, hasa katika miaka kumi ya kwanza ya Enzi ya Nyayo, za kujaribu kuibuka na falsafa ya kisiasa ya utawala iliyoenda sambamba na mwito huu. Hata hivyo, juhudi hizi hazikunasa kikamilifu fikra na mienendo ya watu wengi wa Kenya. Katika enzi ya Nyayo, Kenya ilibadilika na ikawa Taifa la chama kimoja kisheria hadi sheria hii ilipofutiliwa mnamo 1992, na maovu ya ukabila, kutovumiliana, kisiasa, ufisadi na umaskini vikafikia kilele.

Miaka ya 1990 ilishuhudia kuibuka kwa misukumo ya itikadi za kimataifa za upya wa mabadiliko na mawazo yasiyojifunga na yaliyo huria. Uhuria huu uliendezwa na utandawazi. Itikadi ya upya wa mabadiliko na mawazo yasiyojifunga haukukashifu tu kanuni za serikali kuhusu aina zote za masoko bali pia ilihoji kuwa ukosefu wa usawa ulikuwa sifa changizi kadri ulivyoendeleza kukua na kujilimbikizia mali ya binafsi.

Ilionekana kuwa ilikuwa muhimu sana kuvunja uwezo wa ushirika wa kibiashara na, kwa jumla, miondoko ya wafanyakazi.

Ni wazi kuwa, itikadi za upya wa mabadiliko na mawazo huria zinaenda kinyume na juhudi za walio wengi na zinaelekea kuthibitisha, kwa upande mmoja, soko la jumla na kwa upande mwingine, taifa lisiloingilia, ambalo halifanyi cho chote ili kusuluhisha hali ya kutolingana katika jamii. Ni mfumo wa kiteknokrasia, wa walio mabingwa katika huduma za mtaji wa kimataifa. Ni itikadi iliyotolewa kwa Ulimwengu wa Tatu na Benki Kuu ya Dunia, IMF, na Wakala nyingine za kimataifa. Inafahamika kuwa nchi kama vile Japan, Korea au Taiwan hazifuati na hazijawahi kufuata mwelekeo wa upya wa mabadiliko na mawazo yasiyojifunga.

Ujumuishi wa tajriba za kiitikadi za Kenya tangu kupata uhuru unaibua hali ya kuvutia hasa katika muktadha wa Urekebishaji wa Katiba, hasa kuhusu suala la mahusiano baina ya serikali na wananchi, pamoja na maadili na falsafa ambayo inatakikana kuongoza majukumu ya serikali.

- Ingawa miaka ya sitini na sabini ilikuwa kipindi cha matumaini na utaifa, miaka ya themanini na tisini imeshuhudia hali ya kukata tamaa katika serikali ambayo inatambulika mno na wananchi wengi kushindwa kuandama kwa mafanikio mienendo ya "Maendeleo" na kuongezeke kwa umaskini. Tuhuma za dhati zimeibuka kuhusu uhalali wa serikali katika kutekeleza madaraka na uwezo ambao inapata kutoka kwa wananchi, ikiwa haiwezi kuzingatia maslahi na mahitaji ya wananchi hao.

***(b) Katiba iliyopo***

Sehemu 1 ya Katiba ya Kenya inasema kuwa *"Kenya ni Jamhuri huru"* na inaendelea katika sehemu 1A kusema kuwa *"Jamhuri ya Kenya itakuwa Taifa la kidemokrasia la vyama vingi"*. Kanuni hizi mbili zinatoa ramani ya kiitikadi ya jinsi ya kusimamia masuala ya Jamhuri na nafasi ya wananchi huru wa Kenya. Matokeo ya moja kwa moja ya kanuni hizi ni kuwa, kuwepo wa Jamhuri ya Kenya kunahitaji kuwekwa katika msingi imara wa idhini ya wananchi. Kwa hivyo, mkondo wa uwezo na madaraka ya kitaifa

sharti utokane na wananchi ambao wanastahili kuheshimiwa. Hali ya kuleta pamoja jamii tofauti za Kenya katika taifa moja huru inaashiria kujitolea kwa hiari na kwa pamoja kwa nguvu na uwezo wa wananchi na kuimarisha taifa ambalo linatarajiwa kudumisha na kuwahakikishia maslahi yao. Ikiwa Jamhuri, Nchi ya Kenya inatarajiwa kuwa chombo cha kuwakilisha maslahi ya wanajamii wote. Sifa za msingi za asasi ya aina hii ni kuwa inahakikisha:-

- Maslahi na uhifadhi wa binafsi wa kila mwanajamii.
- Usimamizi unaofaa na ugawaji sawa na wa mara kwa mara wa rasilmali,
- Mwitikio wa kimantiki kwa mahitaji ya jamii;
- Kuingilia kati kunakofaa na kwa wakati unaofaa kwa niaba ya wote, hasa wanajamii walio wanyonge;
- Kuwa na matumaini ya kufanana na ya wananchi; na kudumisha hali ya kuwategemea panapotokea haja na pia kuwa na huruma ya dhati kwa wananchi;
- Uwakilishi unaofaa wa wananchi; na
- Kudumisha amri ya Katiba na utawala wa sheria.

### 9.2.2. Waliyoyasema wananchi

Ingawa suala la hali ya Taifa halikuwasilishwa kwa wananchi kidhahania jinsi ambavyo tumeeleza hapo juu, hakuna shaka kuwa Kenya haikuwa na sifa hizo. Mawasilisho katika sehemu nyingi za nchi yalianza na orodha ya ama yale ambayo serikali inatakikana kuwafanyia wananchi lakini haikuwa ikiyafanya, maovu ambayo ilikuwa imedumisha kwa wananchi au yale ambayo serikali mpya, ambayo ilikuwa ikijengwa sasa na Katiba, iliwajibika kutimiza!

Kwa hakika, wananchi wengi walifikiri kuwa vyombo vya serikali vilikuwa:

i) vya kunyanyasa na visivyojali

ii) mbali sana nao

iii) vikiwanyonya zile rasilmali chache ambazo bado waliweza kuzizalisha,

iv) havikufaa na vilijaa ufisadi, na

v) kwa jumla havikuweza kuyalinda maslahi yao.

### 9.2.3 Itikadi katika Katiba Nyingine

Ufafanuzi wa wazi wa kanuni za itikadi zinazounda taifa ulianza kujitokeza kwenye katiba zilizoundwa na Mapinduzi ya Bolshevik ya Russia ya 1917. Mfano wake (kama ilivyobadilishwaw 1992) ni katiba ya Jamhuri ya Cuba inayohakikisha kuwa:

1. Cuba ni taifa la kijamii la wafanyakazi, lililohuru na lenye uwezo wa kujitawala, lililoundwa na wote kwa maslahi ya wote; kama Jamhuri ya moja ya deokrasia.
2. Chama cha kikomunisti cha Cuba, kimaksi na kimaksi-Lenin, ambacho ni kiongozi cha jamii na mpango wa serikali na ndicho kinacho uongozi juhudi za pamoja za kufarikisha malengo ya ukatiba na ujamaa na uendelezaji wa jamii ya kikomunisti.

Ijapokuwa awamu ya itikadi ya kijamaa na kikamunishi imekaribia kwisha, katiba nyingi, hata katika mfumo huria, hutaja aina ya itikadi zinayoifuata. Kwa hivyo, Katiba za Uganda, Ethiopia, Ghana, Eritrea, Tanzania, na Afrika Kusini, pamoja na nyingine zimetangaza kuwa taifa limeundwa kwa misingi ya kanuni za demokrasia, haki ya kijamii na utawala wa kisheria.

Katiba ya Tanzania imesema hivi:

> *3 (1) Jamhuri ya Muungano ni taifa la kidemokrasia na kijamaa, linalofuata mfumo wa vyama vingi;*
>
> *9. Lengo la Katiba hii ni kuwezesha……… ufuatilizaji wa sera ya ujamaa na kujitegemea, inayosisitiza matumizi ya kanuni za kijamaa wakati ikizingatia hali iliyoko katika Jamhuri ya Muungano*.

### 9.2.4. Uchanganuzi

Wananchi wa Kenya, kupitia mawasilisho ya hadharani na memoranda, wameomba kwa dhati kuwa wapate serikali ya kujali na kutegemewa ambayo italinda na kudumisha maslahi yao.

Kwa kuzungumzia nia ya wananchi, ni muhimu kutilia maanani mambo mawili. Kwanza, nia ya asili na kimaumbile na tamaa ya kila binadamu kuishi, kuwa imara kuwa salama na kujihifadhi. Hii ni nia ambayo inapatikana kwa wingi miongoni mwa wote licha ya umri, jinsia, kabila, rangi, nafasi katika jamii na dini. Ni tisho, hasa kwa nia hii, ambalo lilisababisha uanzilishi wa jamii ya kisiasa, ya kisheria na ya utawala. Pili, nia ya mpito inayotokana na wachache katika hali ya uwakilishi, kwa niaba ya wananchi, inahitaji kufahamishwa na nia ya kwanza – ya wananchi. Huu ndio unatakikana kuwa msingi wa serikali yoyote.

### 9.2.5. Mapendekezo

Kwa hivyo, Tume inapendekeza kuwa: –

i) Kenya ichukue mwelekeo wa Itikadi ya Kijamhuri ambayo imejengwa na kudumishwa na misingi ya wema kwa wote, faida za wote, maslahi na hali ya maisha ya wananchi.

ii) Katiba itashinikiza kanuni za kijamhuri za utawala.

iii) Kenya ni Jamhuri huru ambayo inapata uwezo wake wote kutokana na, na pia inayoshiriki katika matumaini ya jumla ya wananchi wake.

iv) Jamhuri itakuwa nchi ya kidemokrasia ya vyama vingi ambayo imejitolea kudumisha ushiriki wa kamilifu wananchi katika kusimamia masuala ya umma kwa njia ya moja kwa moja au isiyokuwa ya moja kwa moja.

v) Katiba ieleze wazi na kubainisha kanuni zetu na maadili ya kimsingi ya itikadi ya kitaifa ambayo yatakuwa pamoja na –

a) Utawala wa Sheria
b) Heshima kwa haki za binadamu ikiwemo haki za raia, kisiasa, kijamii, kiuchumi na kitamaduni
c) Uadilifu wa kitaifa
d) Usawa wa kijinsia
e) Utawala mwema ulio shirikishi
f) Uwazi na uwajibikaji

g) Viwango vilivyobainishwa vya ufikiaji wa mahitaji ya maslahi ya wananchi
h) Utambuzi wa uwezo wa kibunifu wa wananchi wetu miongoni mwa mambo mengine
i) Utenganishaji wa uwezo
j) Vipimo na visawazishi
k) Utawala shirikishi
l) Uchaguzi wa kidemokrasia
m) Kudhibiti washikaafisi za umma kwa kuwafanya kushikilia afisi kwa vipindi maalum, wakati wa kuruhusiwa na wananchi na wakati wanapotimiza tabia njema.

## 9.3. Wingi wa Tofauti za Kitamaduni, Kidini na Lugha

### 9.3.1. Kanuni za Jumla

#### *1. Wingi wa tofauti za kitamaduni na kidini*

Maadili ya kitamaduni na kidini huwapatia watu motisha ya kutimiza mafanikio maalum. Kimsingi, dini zilitokana na maadili, kwa mfano, haki, upendo, usalama na fadhila. Hatimaye ilifuatia uainishaji wa kimatabaka, kanuni, na mikataba iliyowekwa na uungu ili kudumisha uathirifu.

Majukumu ya viongozi wa kitamaduni na kidini ni muhimu katika utaratibu mgumu, na ambao mara nyingi ni wa mwendo wa pole, wa marekebisho ya itikadi na maadili. Wanatekeleza uwezo wao katika miktadha ya utawala wa kidini. Kile ambacho wananchi wanaonekana kukataa – kwa kufahamu au kutofahamu – ni kukuza mno mielekeo ya kilimwengu ambayo huanza kwa kuweka uwili wa maslahi baina ya maada na nafsi, mwili na roho. Uwili huu unatenganisha imani za kidini na elimu kutokana na "sayansi" na huishia, kiutendaji, na ukanushaji wa uyakinifu wa yote yasiyoweza kupimika na kuuzika.

Kuna watu wanaotafuta “maadili mapya ya kiutandawazi”, baadhi wanatafuta tu maadili ya “wema wa wote” au maadili ya “haki ya jamii” na wengine wanatafuta maadili ya kawaida au ya mazoea. Bado kuna wengine ambao hawaridhiki na misingi ya kimaadili. Wanatafuta misingi ya kidini na imani inayopindukia ambamo wanakita matumaini na vitendo vyao. Katika viwango vya binafsi mno, watu wengi huguswa na makisio ya ndani ya maadili na imani ambayo yanaashiria na kueleza uhalisia, na ambayo yanaunga mkono maadili ambayo yanaongoza maamuzi kuhusu iwapo watabadilika au hawabadiliki.

Maadili na dini vina uhusiano wa karibu hasa katika muktadha wa jamii yenye imani ya kidini. Dini mbalimbali zilifanywa rasmi na kuainishwa au vinginevyo zimetumia itikadi ili kushinikiza mifumo yao ya kimaadili, mwanzo, kwa washiriki wake, na pili, kwa wengine wanaoathiriwa na dini hiyo. Tokeo la manufaa kutokana na uhusiano baina ya maadili na dini limekuwa amani ya kupenyeza kwa wema katika jamii, vikundi vya kijamii na hata nchi.

### *2. Wingi wa Tofauti za Lugha na Sera ya Lugha*

Lugha ni sifa bunifu ya kibinadamu ambayo ni muhimu katika mawasiliano ya kimtagusano, umoja wa kitaifa na ushirikiano wa kimaeneo. Ina majukumu ya kitaashira na ya kiutekelezaji. Katika kiwango cha kuashiria, lugha ni muhimu katika ufafanuzi wa nafsi na undani wa hali ya kuwa jamii. Kiutekelezaji, ni chombo cha msingi kwa mazungumzo ya kitaifa na maendeleo.

Mara nyingi lugha kama sehemu ya utamaduni huelezwa kama chombo cha kuwasilisha utamaduni. Lugha ina dhima muhimu katika kuamua kiwango ambamo raia wanaweza kushiriki katika masuala ya kitaifa, elimu na uenezaji wa habari. Uteuzi wa lugha una athari za kudumu kwa maendeleo ya kisiasa, kitamaduni, kijamii na kiuchumi ya taifa. Uteuzi unaozingatia matumaini ya wananchi hudumu na unaweza kusababisha utimizaji wa haki muhimu na za kimsingi za watu binafsi na za jamii. Uteuzi wa aina hii unahitaji kuongozwa na

hali ya kuzingatia ushiriki wa wananchi katika maisha ya kitaifa, ikiwemo haja ya kuimarisha hadhi yao ya kijamii na kiuchumi.

Kenya ni nchi yenye lugha na nyingi na makabila mengi. Katika hali ya kukosa takwimu za kutegemewa, hatuna habari tosha za idadi ya watu wanaozungumza kila lugha zilizo nchini Kenya. Licha ya haya, tunajua kuwa, idadi ya watu katika kila kikundi cha lugha haina usare na inapatikana baina ya wazungumzaji mia chache hadi yapata wazungumzaji milioni tatu.

Kuna karibu lugha sabini nchini Kenya ambazo huzungumzwa na makundi maalum ya kikabila. Makabila haya yana maeneo yao, tamaduni zao na historia yao. Kwa jumla, jina la kila lugha hubainisha utamaduni wa wazungumzaji wake wa asili. Kwa hivyo, Dholuo, kwa mfano, inarejelea si lugha tu bali pia utamaduni maalum wa Waluo. Licha ya haya kuna haja ya kutofautisha umilisi wa lugha na umilisi wa utamaduni.

Wakati wa uhuru, Kenya ilikikubali Kiingereza kama lugha rasmi. Imekuwa lugha ya serikali, elimu, haki, utawala na mfumo wa kitaifa kwa jumla kwa muda wa miaka mingi. Sababu ya kuweka Kiingereza kama lugha rasmi ya pekee ina misingi katika mjadala kuwa kuna ukabila mwingi na lugha nyingi. Imani ya jumla ni kuwa, uteuzi wa lugha moja dhidi ya nyingine utazusha wivu wa kikabila na kuhatarisha umoja wa kitaifa. Kulikuwa na imani ya kupotosha kuwa lugha ya kigeni ingeleta umoja na ushikamano.

Matokeo ya hadhi ambayo Kingereza kilipewa ni kuwa, wasomi walijenga misimamo hasi (isiyopendeza) kwa lugha za Kiafrika. Walichukulia kuwa usasi na maendeleo yangepatikana tu kupitia Kiingereza. Hivi sasa, imekubalika na wengi kuwa wingi wa lugha – jambo ambalo ni la kawaida – hakumaanishi kuwa lazima pawe na utengano, na usare wa lugha, haumaanishi kuwa patakuwa na ushikamano wa kijamii au wa kitaifa. Ukweli ni kwamba, baadhi ya nchi nyingi za Kiafrika ambazo hazina umoja ni nchi zenye lugha moja, kwa mfano, Rwanda,

Burundi na Somali. Si lazima wingi wa tofauti za lugha uwe unawakilisha tisho kwa upangaji lugha katika jamii zenye lugha nyingi.

Kwa hivyo, sera ya lugha ni muhimu katika utulivu wa kisiasa na uhalali wa Taifa. Nchi nyingi za Kiafrika sasa zinakumbana na matatizo makuu ya kiuchumi, kijamii na kisiasa na zinaonyesha dalili nyingi za matatizo katika elimu kwa sababu Waafrika wengi huendesha serikali zao na masuala ya mataifa yao katika lugha ambazo hawazielewi.

Kuna haja ya dharura ya kulitilia makini suala la lugha barani Afrika. Kwa hakika, hakuna nchi ulimwenguni kote ambayo imewahi kutimiza viwango endelevu vya maendeleo katika misingi ya lugha ya kigeni pekee; ambayo wengi wa wananchi wake hawaielewi.Nchi nyingi, kama vile India na Tanzania zimechukua hatua za kuendeleza na kutekeleza sera ya lugha kwa nchi zao. Hali katika nchi hizi inaonyesha kuwa:

- Hata kama wingi wa lugha na tofauti za kikabila ni changamoto kwa sera ya lugha na upangaji wa lugha katika nchi, tofauti nyingi zinahitaji kuzingatiwa kama hali ya kawaida ya maisha, bali si kama maradhi au ndwele.
- Upangajilugha katika hali ya jamii ya wingilugha si lazima ulenge usare wa lugha. Ni lazima ihusishe wingilugha.
- Ni lazima upangajilugha uafikiane na uhalisia wa kiisimujamii wa nchi ambamo upangajilugha unafanywa.
- Kimsingi, suala la upangajilugha ni suala linalohuhusu nia ya kisiasa. Si lazima lifaulu katika jaribio la kwanza.

### 3. *Taifa na Dini*

Suala la uhusiano baina ya dini na taifa ni muhimu. Masuala kadha yanaibuka hapa.

*(i) Mtazamo mpana wa kuelewa imani za kidini na maadili ya Kinafsi*

Pale ambapo wengine watazitazamia imani za kidini ili kujinufaisha kiroho na kujipa moyo tu; wengine watazitazamia asasi za kidini na mifumo yake kwa maongozi ya kibinafsi na mafunzo ya kijamii; na mwisho, wengi wataziona asasi za kidini kama ambazo zina dhima maalum katika kudumisha majukumu ya kijamii na maadili katika jamii. Isitoshe, baadhi huamini kuwa dini na maadili ya kidini huhusisha ama uathirifu mzuri au mbaya kwa maendeleo ya kisasa, ambayo wanayaona kuwa muhimu na wanaamini lazima yazingatiwe wakati wa kutafitia na kuweka taratibu za maendeleo katika jamii zao.

*(ii)* *Jamii isiyokuwa ya Kidini dhidi ya Ulimwengu wa Kiroho*

Ni lazima ieleweke kuwa jamii isiyokuwa ya kidini inatokana na hali ya kujinufaisha ya jamii za kimagharibi na bado haifahamiki katika jamii nyingi za Asia na Afrika. Katika tamaduni hizi, dhana ya utakatifu, Mungu na ya pepo bado zinatawala maisha ya kila siku ya watu wengi. Katika Afrika kwa jumla na hasa Kenya, hata wale wenye kisomo na wataalamu huchukua muda mwingi na nguvu nyingi na hata rasilmali zao kufurahisha "wafu wanaoishi". Yaelekea, si Uislamu, Ukristo na itikadi na mwelekeo wa Benki ya Ulimwengu hazijafaulu katika kuuondoa, kuutangamanisha na kuuelekeza upya au hata kuelewa undani wa nguvu hizi upingi.Waafrika hujitolea muda wao kila siku ili kujishughulisha na ulimwengu wa pepo ambao unaendelea kuwa kipengele muhimu cha kutambulisha Uafrika.

*(iii)* *Taifa la Kilimwengu au la Kidini*

Taifa la kilimwengu si jambo la kukataliwa hasa ikiwa inamaanisha kuwa taifa halitatawaliwa na asasi ya kidini. Taifa la kilimwengu litamaanisha hali ambamo taifa haliingilii katika masuala ya kidini na papo hapo dini haitaingilia masuala ya taifa. Lakini, haitafaa kupuuza marejeleo yote ya kidini na kutotilia maanani maadili ya kidini na kimungu kama desturi na tamaduni zisizokuwa na mantiki. Wananchi wanazitaka serikali zao na washiriki wenzao wa kigeni kuheshimu imani zao hata kama hawaziafiki na wanaomba kuwa muda na nafasi vitolewe ili

mbinu hizi zitimize majukumu yao katika kushirikisha maadili mapya na mienendo mipya ya maendeleo.

Ushiriki wa viongozi wa kidini na wa kiroho katika kufafanua mabadiliko muhimu kutaongeza kukubalika kwao. Haya yatawezekana tu katika taifa la kilimwengu, ikilinganishwa na taifa la kidini.

### 9.3.2. Tofauti za kitamaduni, kidini na za lugha katika Katiba

Katiba iliyopo ya Kenya haijazungumzia wazi suala la lugha isipokuwa katika sehemu 53(1) ambapo inataja lugha rasmi za Bunge. Sehemu hii inasema: "Kwa mujibu wa sehemu hii, lugha rasmi za Bunge, zitakuwa Kiswahili na Kiingereza na shughuli za Bunge zinaweza kuendeshwa katika mojawapo ya lugha hizi". Sehemu ndogo zinazofuatia, (2) na (3) zinaendelea kutaja matumizi ya Kiingereza kwa maamuzi, marekebisho, nyaraka na manukuu yo yote ambayo yatafanywa na Bunge.

Lugha hizi pia zinakinzana kwa mujibu wa ustadi wa lugha unaotarajiwa kwa wabunge. Sehemu 34(c) ya Katiba inahitaji kuwa wakati wa kuteuliwa kwa uchaguzi wa Bunge, mgombezi, "aweze kuongea, na isipokuwa pale ambapo amepungukiwa kwa sababu ya upofu au maumbile ya kimwili, aweze pia kusoma lugha ya Kiingereza vizuri kiasi cha kuweza kuitumia katika mazungumzo". Hakuna kanuni inayohusu mahitaji ya lugha kwa wasiojiweza. Wagombezi wasiokuwa na umilisi wa Kiingereza wamezuiliwa kisheria kugombea uchaguzi. Wabunge wanaruhisiwa kujadili katika Kiingereza miswada ya sheria ambayo imeandaliwa katika Bunge.

Ingawa Kiingereza ni lugha rasmi ambayo inatimiza majukumu ya kuwa lugha ya serikali, Kiswahili kinatimiza majukumu ya kuwa kama lugha rasmi ya Bunge. Nyaraka za kitaifa, kwa mfano, fomu za usajili wa vitambulisho vya kitaifa na vyeti vya usafiri zinapatikana katika lugha hizi mbili. Hata hivyo, Kiswahili hakichukuliwi kama lugha ya Taifa, jambo ambalo ni muhimu kwa ushikamano wa Umoja wa kitaifa. Katiba iliyopo na ambayo inafanyiwa marekebisho haikitambui Kiswahili kama lugha rasmi licha ya

umuhimu wake kitaifa, kieneo na katika bara zima. Isitoshe, Katiba iliyopo haisemi chochote kuhusu dhima ya lugha nyingine za Kenya na hakuna mbinu za kuzilinda, kuzikuza na kuziendeleza.

Kimsingi, Kenya ni taifa lenye dini nyingi na lina uhuru wa kiurazini. Ulinzi wake umekita kwa dhati na kwa mapana katika Katiba. Dini za Kenya zinaweza kuainishwa kama za Kikristo ambazo zinashirikisha watu wengi, Waislamu ambao wanachukua nafasi ya pili, na wakifuatwa na wanajadi au wanamaumbile (Kama vile Dini ya Musambwa, na Hema la Mungu Aishiye n.k). Kuna pia dini nyingine licha ya Ukristo na Uislamu kama vile Kihindu, Kibudha, Kibahai na nyinginezo. Hivyo basi, Katiba inapendekeza, katika sehemu 73 kuwa –

1. Isipokuwa kwa uamuzi wake mwenyewe, mtu hatazuiliwa kufurahia uhuru wake wa kurazini, na kwa madhumuni ya sehemu hii, uhuru huo unashirikisha uhuru wa mawazo na wa kidini, uhuru wa kubadili imani ya kidini na uhuru ama wa binafsi au wa ujamaa na wengine, na pia, hata kama ni hadharani au faraghani, kubainisha na kuendeleza imani yake ya kidini katika kuabudu, kufundisha, kutenda na kushuhudia.
2. Kila jamii ya kidini itakuwa na wajibu, kwa gharama zake, kuweka na kulinda mahali pa elimu na kupasimamia mahali pa elimu ambapo inapalinda. Hakuna jamii ya aina hii ambayo itazuiwa kutoa mafunzo ya kidini kwa mtu wa jamii hiyo katika somo lolote linalotolewa mahali pa elimu ambapo wamepasimamia au katika kazi yoyote ya elimu ambayo wanaitoa.
3. Isipokuwa kwa idhini yake (au kama bado ni mtoto, kwa idhini ya mlinzi wake), hakuna mtu anayehudhuria mahali pa elimu atahitajika kupokea mafunzo ya kidini au kushiriki au kuhudhuria sherehe ya kidini au kuishuhudia ikiwa mafunzo, sherehe au kushuhudia huko kunahusiana na dini nyingine ambayo si yake.

### 9.3.3 Wingi wa Tofauti za Kitamaduni, Kidini na Lugha katika Katiba Nyingine

Vifaa vya kikatiba, hasa katika jamii zenye kabila au tamaduni nyingi, hutaja waziwazi kanuni zinazousu utamaduni, dini na lugha. Kanuni kuhusu utamaduni aghalabu ni za kimatamanio na hutokeza au kwenye utangulizi ama kama kanuni elekezi za sera ya taifa. Utamaduni pia unatambuliwa kama haki ya kimsingi katika Sheria ya Haki ya Katiba nyingi. Katiba ya kisoshalisti, kama Sura ya Tano ya Katiba ya Jamhuri ya Cuba, hutaja kanuni pana kuhusu utamaduni. Lugha na sera ya lugha zimeanza kudhihirika katika Katiba nyingi za nchi. Ibara 6 ya Katiba ya Afrika Kusini, kwa mfano, inataja kwamba:

(1) Lugha rasmi ya Jamhurini Sepedi, Sesotho, Setswana, Siswati, Tshirenda, Xitsonga, Afrikaans, Kiingereza, IsiNdebele, IsiXhosa, na IsiZulu;
(2) Tukitambua hali dhaifu kihistoria ya matumizi na hadhi ya lugha asili za watu wetu, taifa lazima lichukue hatua za kiutendaji za zenye mwelekeo mwema kuinua hadhi na kuendeleza lugha hizi.

Katika Katiba ya Ethiopia, haki ya kuongea kuandika na kuwasiliana kwa lugha ya mtu binafsi kunalindwa. Kuhusu dini, vifaa vingi vya kikatiba hutofautisha vitu viwili. Kwanza ni utambuaji wa uhuru wa dini kama haki ya kimsingi. Hii hutajwa kama ni pamoja na haki ya kuwa na au kufuata dini au imani; kuonyesha dini au imani hiyo katika ibada kufuata na kuifundisha; kuanzisha asasi za kidini; elimu au utawala ili kuendeleza au kupanga dini. Pili ni sifa ya taifa la kilimwengu. Ila tu katika katiba ya mataifa fulani ya Kiislamu ambapo taifa na dini hazitengwi, katiba nyingi hutenganisha dini na uwanja wa raia. Kwa hivyo, sheria ya II ya Katiba ya Ethiopia imehakikisha kuwa:

a. Taifa na dini ni vitu mbali;
b. Hakutakuwa na dini ya taifa; na
c. taifa halitaingilia masuala ya kidini na dini haitaingilia maswala ya serikali.

Isipokuwa kama ilivyotajwa hapo juu, Katiba nyingi zinatambua kama Ibara 5 ya Katiba ya Visiwa vya Fiji kuwa:

*“Ijapokuwa dini na taifa ni vitu mbali, watu wanatambua kuwa ibada na kumwogopa Mungu ndio msingi wa serikali njema na uongozi mwema”.*

### 9.3.4 Waliyoyasema wananchi

Yale ambayo wananchi waliiambia Tume yanaweza kuainishwa katika mada zifuatazo:-

*i) Kuhusu dini kuwa-*

a) Katiba iwahakikishie Wakenya wote uhuru wa kuabudu.
b) Katiba iwahakikishie Wakenya wote uhuru wa kutembea, wa kujieleza, wa kukutana, wa kushirikiana na wa kurazini.
c) Katiba ishinikize haki za kijamii, za kiuchumi na za raia.
d) Waislamu waruhusiwe kuheshimu Ijumaa kama siku yao ya ibada na Jumamosi kwa wale ambao ni Waumini wa Siku ya Sabato (Seventh Day Adventists).
e) Uhuru wa kuabudu uwekewe mipaka.
f) Uhuru wa kuabudu ufutiliwe mbali.

*ii) Kuhusu lugha na utamaduni*

*a. Je tuwe na lugha mbili za kitaifa?*

- Wakenya wengi hawana kisomo kwa hivyo hawawezi kusoma wala kuongea Kiingereza.
- Mahitaji ya walemavu hayajazingatiwa katika miktadha ya lugha ya taifa.
- Hali ya kuwa na lugha mbili za kitaifa itawatenganisha Wakenya badala ya hali ya lugha moja ya kitaifa ambayo itawaunganisha Wakenya wote.
- Kiingereza ni kama mabaki ya ukoloni na kwa hivyo ni salata kwa utamaduni wa nchi.

- Kukubali lugha mojawapo ya asili kama lugha ya taifa kutadumisha ukabila.
- Wakenya wengi walisema kuwa Kiingereza kikubaliwe kama lugha ya taifa.
- Baadhi walipendekeza kuwa Kiingereza, Kiswahili, lugha ishara na Breli zikubaliwe kama lugha za taifa.
- Wakenya wachache walisema kuwa Kiswahili kikubaliwe kama lugha ya taifa ilhali Kiingereza kihifadhiwe kama lugha rasmi.

b. *Je Katiba itambue na kukuza lugha za asili?*

- Utamaduni wa Kenya kwa mujibu wa lugha unafifia
- Ukuzaji wa lugha za asili utawagawanya Wakenya katika misingi ya kikabila na kwa hivyo kukuza ukabila.
- Ukuzaji wa lugha za asili hautakuza maendeleo.
- Wakenya wengi walipendekeza kuwa Katiba itambue na ikuze lugha za asili.
- Lakini, baadhi walisema kuwa Katiba inawajibu wa kukuza lugha za asili.
- Wakenya wengine walisema kuwa Katiba ina wajibu wa kutambua na kukuza lugha za asili.

### 9.3.5 Uchanganuzi

Yale ambayo wananchi waliiambia Tume yanapendekeza kuwa ingawa tofauti nyingi za kidini na kitamaduni zimetetewa kwa dhati, bado tuko mbali sana na kuweza kukuza sera ya lugha ya kitaifa iliyo wazi. Isitoshe, mjadala na utafiti unahitajika kuhusu jinsi ambavyo suala hili linaweza kutekelezwa.

### 9.3.6 Mapendekezo

Hivyo basi, Tume inapendekeza –

i) *Kuhusu dini kuwa -*

a. Ingawa uhuru wa kuabudu umo katika Katiba ya Kenya, uzingatiaji wa baadhi ya madhehebu ya kidini ambao unakiuka haki za wengine unazidi kuongezeka.

b. Dini yo yote ambayo inachochea wafuasi wake dhidi ya raia wengine, inawaelekeza wafuasi wake katika mienendo isiyofaa na kuwafanya wafuasi hawa wa dhati kutoa panga zao dhidi ya wafuasi wa dini zingine, kwamba dini ya aina hii si dini katika hali zote za dhana ya neno dini.

c. Ingawa wananchi wana uhuru wa kuabudu kadri wanavyoongozwa na maoni yao, itahitajika dini zote ziheshimu utu na maumbile huku wakitekeleza majukumu ya kiuadilifu kwa wafuasi wake. Wanahimizwa kukuza uvumilivu, amani na fadhila.

d. Katiba ihakikishe kuwa uhuru wa kuabudu hautumiwi ili kuingilia uhuru wa watu wengine wa kuabudu na kwa hivyo, kuna haja ya kuwa na maarifa ya kisheria kuhusu dini, ambayo yatakuwa shirikishi bali si ya kupendelea katika utekelezaji wa haki.

ii) *Kuhusu ubaguzi kwa mujibu wa dini kuwa –*

a. Katiba ihakikishe kuwa hakuna mtihani wa kidini utakaohitajika ili mtu astahili kushika afisi yoyote au amana ya umma katika serikali ya Kenya.

b. Hakuna mtu atakayeumia kwa sababu ya imani yake ya kidini wala msimano.

iii) *Kuhusu uhusiano baina ya Taifa na Dini kuwa –*

a. Licha ya kutoa misingi ya uhuru wa kuabudu, mipaka ambamo masuala ya kidini na kitaifa yatashughulikiwa inahitaji kubainishwa wazi katika Katiba.

b. Katiba ibainishe kuwa Kenya ni taifa la kilimwengu na kuwa serikali haitafanya chochote kusaidia au kukuza dini yoyote maalum.

c. Kuna haja ya kumtambua Mungu katika Katiba.

d. Kuna haja ya kuweka mbinu zitakazohakikisha uondoaji wa vizuizi vya kijamii, kitamaduni na kidini ambavyo huzuia umoja na ushikamano wa kitaifa.

e. Kuna haja ya kutambua siku za ibada za makundi tofauti ya kidini na papo hapo kuheshimu mikataba ya wafanya kazi kimataifa, I.L.O. kuhusu siku za kupumzika.

f. Kuna haja ya kubainisha wazi kuwa mtu atawajibika kushiriki katika shughuli au tambiko au kula kiapo au kuwa na silaha au kufanya kazi siku yoyote, endapo kufanya hivyo kutadhuru uhuru wa dini au imani.

*(vi) Kuhusu utamaduni na lugha kwamba:*

(a) Katiba iwe na sera iliyo wazi na utaratibu wa utekelezaji wake unaozingatia mawanda yafuatayo:

- Sera ya elimu inayoendeleza ufundishaji na matumizi ya lugha za kiasili,
- Sera ya vyombo vya habari inayoendeleza matumizi ya lugha za kiasili;
- Sera ya kutawala inayoendeleza matumizi ya lugha za kiasili katika shughuli za umma;
- Sera ya kiuchumi inayotabua thamani ya kiuchumi ya lugha ya taifa na lugha za kiasili;
- Sera ya lugha inayohimiza na inayoendeleza matumizi ya lugha ishara ya breli;

(b) Katiba itambue Kiswahili kama lugha ya taifa na kuipa hadhi yake katika shughuli za kitaifa;

(c) Katiba itambue Kiswahili na Kiingereza kama lugha rasmi za taifa. Nyareka zote za kitaifa ziandikwe kwa lugha zote mbili;

(d) Katika muktadha wa upunguzaji na usambazaji madaraka, katiba itambue Kiswahili, Kiingereza lugha ishara na lugha zinazopendelewa kieneo kama lugha rasmi wilayani;

(e) Katiba ilazimishe bunge kutunga sheria ya uundaji wa asasi za kukuza Kiswahili, Kiingereza, lugha ishara na breli. Baraza la Taifa la Kiswahili na Taasisi ya utafiti wa Kiswahili ziundwe kisheria.

(f) Ufahamu wa Kiswahili uwe ni kigezo muhimu cha kutoa uraia na vibali vya kazi kwa wageni.

(g) Katiba ilazimishe serikali kuwa na mfuko wa fedha zitakazotumiwa kukuza lugha za kiasili, lugha ishara na breli.

(h) Huku tukitambua umuhimu wa Kiswahili katika uchumi, kieneo na kimataifa, pana haja ya Katiba kupitia sheria mbali mbali kuelekeza na kuhimiza Kiswahili.

(i) Nchi ya Kenya ihimize umuhimu wa kufundisha Kiswahili katika mataifa ya kigeni na ikihitajika ishirikiane na mataifa yanayozungumza Kiswahili ili kuunda taasisi zitakazofundisha Kiswahili, kibiashara.

(j) Katiba ilinde kuwepo kwa lugha na tamaduni nyingi kufungamana na Azimio la Kilimwengu la Haki za Binadamu na Mkataba wa kimataifa wa Haki za Kiuchumi, kijamii na kitamaduni, ili kusisitiza umuhimu wa utamaduni na lugha.

(k) Upangaji lugha nchini Kenya uzingatie tofauti za kijiografia na kisiasa, na mfumo unaopendekezwa wa upunguzaji na usambazaji serikali unaweza kuwa msingi wa mradi wa kupanga lugha.

## 9.4 Vyama vya Kisiasa

### 9.4.1 Kanuni za Jumla

***(a) Fafanuzi***

Ili demokrasia istawi lazima pawe na mifumo ya vyama vya kisiasa yenye uthabiti na usimamizi mwema. Jambo hili linahakikisha kuwepo kwa uthabiti na amani na usalama kwa taifa lote, hali ambayo husisimua uwekezaji na kuleta changamoto ya ukuaji endelezi wa uchumi na maendeleo. Kando na kutekeleza maslahi ya wanachama, yapasa vyama vihudumie utu wa kijumla wa taifa na kuhakikisha kwamba maslahi ya wananchi

wote katika jamii yanahakikishwa kutekelezwa. Hili litafanywa kwa kuhakikisha mgao wa sawa na rasilmali na usimamizi mwema wa rasilimali hizo.

Ingawa sheria ya marekebisho haishughulikii swali la vyama vya kisiasa sheria hii yazungumzia mengi kuhusu vyombo na muundo wa matumizi ya uwezo wa serikali. Kwa ambavyo chama kinachotawala , au viongozi wake ndiyo asasi muhimu ya matumizi ya uwezo wa serikali, na chama cha upinzani kinashikilia uwajibikaji wa utawala, mambo mengi yanaweza kupatikana katika masharti ya miundo ya matumizi ya uwezo wa serikali, kuhusu uundaji wa vyama na sheria zake. Kwa hakika, sheria ya Marekebisho yahitaji Tume kuanzisha mfumo wa katiba utakaolinda maslahi ya wananchi wote wa Kenya.

Fafanusi nyingi za vyama vya kisiasa zinamulekeo wa utendajikazi. Vyama vya kisiasa vimefafanuliwa kulingana na maoni ya utendakazi na madhumini vinayotekeleza au yanayohitajika kutekeleza. Kwa jumla, vyama vyasemekana kuwa vya wananchi ambavyo kwavyo wanajaribu kuathiri shughuli za umma na taratibu za utawala. Mswada wa Sheria wa Kenya kuhusu vyama vya kisiasa unafafanua chama cha kisiasa kuwa -

> *"Chama chochote au shirika la wananchi ambalo lina vyombo au madhumuni ama kimoja au zaidi ya vyombo vyake au madhumuni, upendekezaji ama kuunga mkono kwa wagombea uchaguzi wa kitaifa au wa mamlaka ya wilayanii kwa maoni ya kuunda ama kuathiri uundaji wa serikali ya Kneya au mamlaka yoyote ya wilayani nchini Kenya."*

Vikiwa vikundi vya mazingira ya kisiasa na kijamii ambamo vimekitwa, vyama vimepewa lawama ya kuwa viharibifu kwa umoja, umashuhuri na uhuru wa taifa au kuonekana kuwa chombo ambacho kwacho wananchi watatumia haki huria na jukumu la kujitawala wenyewe kupitia kwa wawakilishi wao waliochaguliwa katika udemokrasia wa mtazamo usiojifunga, wa vyama vingi na ujamhuri. Ikiwa vyama vitachukua wajibu wao kama machanganyiko na utamkaji wa maslahi machache ya sehemu kama ya kikabila, watengawanya jamii badala ya kuiunganisha. Ikiwa wataona lengo lao kuu

kuwa upataji wa uwezo badala ya ulinzi wa maadili mema, maslahi ya watu wote au maslahi ya kitaifa, watashiriki katika fedheha na ghasia na kukubali desturi za kimsingi ambazo si za kidemokrasia. Katika hali hizi, wanasiasa pia hujitafutia maslahi yao ya kibinafsi na kupoteza uadilifu wao au uwajibikaji wao kwa wapigaji wao kura, wakibadilisha vyama mara kwa mara kwa manufaa na matamanio yao ya kibinafsi. Kwa njia hii, siasa na wanasiasa hawaaminiki tena. Wananchi hupoteza imani yao katika udemokrasia, ambayo waihusisha na vyama na wanasiasa. Watu wengi hutengwa na kujiondoa kwenye siasa - katika hali hizi *mapinduzi* huwezekana na wakati mwingi hukubaliwa na wananachi.

Kufafanua sura za vyama kama asasi za kisiasa ni kwamba vyama ni mbinu zinazounganisha asasi za serikali na zile za jamii. Kwa hivyo, vyama viruhusiwe kuwa vyombo viwakilishi ambavyo kwavyo jamii inajitawala yenyewe katika taifa la jamuhuri ya kidemokrasia kupitia kwa haki za Bunge kudhibiti usimamizi wa kitawaka wa taifa na mapadilishano ya mawasiliano baina ya Bunge na umma ama raia. Kama Oberreuter (1995) anavyosema, *" vyama vinajumlisha jamii na serikali kwa ambavyo nyayo zao zimekitwa kidhati katika jamii, lakini vichwa vyao viko kwenye serikali, kuonyesha kuwa wanatendakazi kama vyombo vinavyotumika kwa malengo tofauti ambapo vinadhibiti serikali na wakati huo huo kuisaidia jamii katika kusululisha matatizo yao"*.

> Kama vyombo vya utawala na usimamizi wa umma, vyama vya kisiasa hutoa nafasi ya kiraia ili wananchi wahakikishe kwamba rasilmali za umma zinatumiwa na kugawanywa kwa usawa.

Vyama vya kisiasa kwa hivyo ni asasi na mbinu muhimu ambazo kiwazo wananchi huteleza matakwa yao na kuamua aina ya utawala utakaoundwa. Katika ufahamu huu, vyama vya kisiasa kinyume na vyama au mashirika mengine kama vile mashirika ya biashara au mashirika yasiyokuwa ya serikali ambayo yanahusiana na siasa ni asasi muhimu ambazo kama vile mahakama, Bunge au viongozi huamua jinsi ambavyo serikali inavyoundwa, inavyoteua watu na kuwatawala.

Vyama vya kisiasa vina wajibu wa kimsingi katika maendeleo na utekelezaji wa Katiba, demokrasia na mfumo wa kisiasa.

Kama vyombo vya mabadiliko, wajibu wa vyama vya kisiasa ni kusaidia kuleta utawala wa kidemokrasia na kikatiba kama njia ya kuhakikisha kupatikana kwa maslahi ya wananchi wote katika jamii nzima. Wajibu wao ni kuufanya utawala uwe wa kidemokrasia zaidi, kikatiba na kijamhuri. Kwa jumla, ni wajibu wa vyama vya kisiasa :-

- Kukusanya maoni kama kwa mfano katika mapigano dhidi ya ukoloni
- Kuleta pamoja maoni na rasilmali, kuwawezesha watu walio na maoni sawa au maslahi yawe ni ya kiuchumi, kijamii, kidini, n.k., wapange na kuratibu shughuli zao na kushawishi.
- Kutoa mbinu ya kimsingi ambayo kwayo wananchi wa kawaida wanaweza kuhusika katika siasa na taratibu za kikatiba na kuweza kutumia haki zao nyingi za kiraia na kisiasa.
- Kupatanisha kwa njia mbali mbali aina ya raia na asasi za serikali.
- Kupata uwakilishaji wa watu katika asasi za serikali, hasa katika sheria, kuwapa nafasi ya kuchagua kisiasa, kijamii na kiuchumi, hususan kupitia utaratibu wa uchaguzi na keletea maoni ya umma katika uzangativu wa sera za utawala.
- Kutoa mbinu za kuipatia sehemu ya wananchi uwezo na kuleta ushikamano na nidhamu serikalini.
- Kuwajibisha serikali kuhusu sheria na wananchi hasa kama vyama vya upinzani.

Katika njia hizi, vyama vina nafasi muhimu katika muungano wa kitaifa, kuwaleta pamoja watu kutoka sehemu tofauti za nchi au kutoka lugha na imani tofauti, katika ushirika mmoja wenye madhumuni ya aina moja, na kusaidia kuendeleza maadili na hadhi ya taifa.

***(b) Mageuko ya vyama vya kisiasa nchini Kenya***

Baada ya kupata uhuru mapambano ya kudhibiti serikali kati ya chama kinachotawala na vyama vya upinzani yalifikia hali za mapigano katika baadhi ya nchi ambayo hatimaye yelileta mazingira yafaayo ya kusaidia hali ya chama kimoja kisichopingika au hali ya kisheria ama kuingilia kwa majeshi. Katika hali hii, muelekeo wa kisiasa ulitia uhalifu katika uibukaji wa vyama pinzani vya kisiasa. Chama kama silaha kwa wale walio na uwezo kilikuwa kifaa cha uwezo wa serikali wala si cha dhamira ya wananchi.

Kama sehemu ya mfumo wa ulimwengu, Kenya imepata mazingira ya tajriba mbalimbali ambapo kwa wakati mmoja, chama cha kisiasa kilifikiriwa kuwa shirika la ziada la serikali lililotenganishwa kabisa na serikali, na ndiyo sababu katiba ya uhuru inayosherekewa na kujulikana kama Katiba ya *majimbo* haikurejelea vyama vya ksisiasa. Lakini katika kuibuka kwa chama kimoja cha kitaifa kisichopingika wakati wa 1964 – 1981 (isipokuwa kwa muda mfupi wa 1966 – 1969), chama kinachotawala (KANU) kilijitokeza kama chama kisichopingwa. Lakini, hili halikulazimisha kukigeuza chama hicho kuwa chombo cha serikali. Hali hiyo iliendelea bila kubadilika hata kipindi ambacho Kenya ilikuwa ya Serikali ya chama kimoja kisheria (1982 – 1991). Ni muhimu kufahamu kwamba kuanzishwa kwa mfumo wa chama kimoja cha kitaifa haukusaidia wajibu wa chama kinachotawala katika utaratibu wa kutawala, kwa njia ambayo kingeingizwa katika muundo wa mgao wa uwiano na hivyo kukifanya chombo cha serikali. Kufutwa kwa sehemu 2A ya Katiba ya nchi ya Kenya mwaka wa 1992, kulishuhudia kuingia kwa demokrasia ya vyama vingi. Licha ya Kenya kutumia demokrasia ya vyama vingi, hakuna maagizo yo yote kwenye Katiba kuhusu uundaji wa vyama pamoja na usimamizi wa ufadhili wake, wajibu, utendakazi na utekelezaji.

Kwa wakati huu, kuna karibu vyama vya kisiasa arobaini na saba (47) vilivyo sajiliwa nchini Kenya na ni vyama vinane tu vinavyowakilishwa Bungeni. Vyama vingi vipo tu kwa kujulikana jina. Kwa vyama ambavyo vinatenda kazi, tatizo la kiutawala katika chama limeendelea kwa miaka mingi na kuna ongezeko la kutaka kuleta demokrasia katika utawala. Vyama hivyo vimeambatana na sura za kiholela, kidikteta na kutowajibika. Karibu katika vyama vyote, uongozi hauvumilii ubishi wa nia nzuri, na

uchaguzi wa kidemokrasia hufanywa nadra au unapofanywa huonyesha uzembe wa kutotimiza wajibu na orodha za wananchama zawezekana kutokuwepo. La ziada:

- viongozi wa chama hawawajibiki kabisa kwa wananchama wao pamoja na umma kuhusu michango iliyofanywa na matumizi ya fedha.
- viongozi wa chama hujichukulia kama kwamba chama ni mali ya kiongozi na hivyo hawafikirii wakati wo wote ule ambapo wanaweza kutokuwa viongozi tena wa chama.
- vyama mara nyingi huwako kwa kuyatekeleza maslahi ya kisiasa ya viongozi ambao huvitumia vyama kama vifao vya majadiliano katika kupigania uwezo na faida za mali.
- uongozi wa chama huingilia utaratibu wa uchaguzi wa chama hasa katika uteuzi wa wagombeaji vyeo vya uchaguzi katika kiwango cha kitaifa na wilayani.
- vyama vingi vya kitaifa nchini Kenya vimechimbuka katika misingi ya kikabila na maslahi ya vitengo fulani na masuala ya kitaifa ni nadra kushughulikiwa.

Kwa sababu ya athari ya vyama kwa mfumo wa kikatiba na nafasi muhimu ilivyonavyo katika utawala, juhudi zimeelekezwa katika miaka ya hivi majuzi katika kuvifanya vyama kuwa na muelekeo wa kitaifa, keundeleza juhudi zao, huduma zao kwa wapiga kura wao na kuhakikisha utawala mwema. Kwa kuwa usimamizi na utendakazi wa vyama vinahusiana sana na mfumo wa uchaguzi, njia moja ya kuathiri vyama ni kubadilisha mifumo ya uachguzi. Njia nyingine ni ya kudhibiti uundaji usimamizi na uvunjaji wa vyama kwa sheria. Kwa kawaida, vyama vya kisiasa vimeonekana kuwa vyama vya kibinafsi, na kumekuwa na udhibiti mchache rasmi. Lakini, sasa vyama yabidi vionekane kuwa asasi za umma, na udhitibi wao uwe ni jambo linalohusu taifa.

Vyama vingi hupata pesa zao kutokana na michango ya wanachama, misaada kutoka kwa "wanaowaunga mkono", harakati za kuchangisha pesa na mauzo ya nyaraka, machapisho na zawadi. Kawaida hufikiriwa kwamba vyama vya kisiasa vinaweza kuchangisha pesa zinazotosheleza shughuli zao hao wenyewe bila usaidizi wa taifa. Fikira hii ingawaje imevifanya vyama kuwa katika hali ya kuandamwa na "nguvu za uovu" zinazojaribu

kuviteka nyara kwa manufaa ya binafsi badala ya kuwa manufaa ya umma. Kwa sababu vyama vya kitaifa vina nafasi muhimu katika kustawisha, kuendeleza na kukita demokrasia, pamoja na usimamizi, uundji na kuleta uhalali wa kisiasa wa vyombo vya serikali kupitia Bunge, kumekuwa na msukumo ili serikali iweze kutoa kiasi fulani cha kufadhili vyama. Hili lingevasaidia vasiwe katika hali ya kuhisi kudaiwa na kuathiriwa bila sababu ni wafadhili, jambo ambalo kwa hali nyingi huzorotesha uhuru wao wa utenadakazi na maendeleo ya kidemokrasia ya kitaifa.

Nchini Kenya, matatizo yanayohusu fedha za chama yameongezwa na umaskini wa watu kwa jumla, kumaanisha kwamba wanachama peke yake si chanzo halisi muhimu cha fedha za vyama na hivyo hali kadhalika kutegemea zaidi fedha za ushirika. Ambapo gharama za chama zaweza kupunguzwa sana kuhusu matumizi ya uchaguzi bado vyama vingehitaji fedha zaidi za kuhakikisha usimamizi na uongozi mwafaka wa shughuli zao. Ili kuondoa athari za upendeleo kuhusu vyama, kiasi cha usaidizi kingetolewa na serikali kwa njia ya wazi, ya usawa na bila upendeleo.

Mtu anapochunguza sura za vyama nchini Kenya, inakuwa wazi kuwa machango wao kwa jamii yenye afya thabiti na ya kidemokrasia kawaida hautakuwa mzuri, kwa sababu zifuatazo:-

- Kuna vyama vingi; pengine sheria zinazotakikana katika uteuzi wa vyama kwa wagombeaji uchaguzi wa bunge na urais zinahimiza hivyo na huendeleza ule mwelekeo wa kujuwana na vyama kiholela.
- Vyama vingi havifanyikazi
- Ni rahisi sana tena ni vigumu sana kusajilisha vyama – rahisi sana kumaanisha kwamba kuna matarajio machache ya kisheria; vigumu sana kumaanisha kwamba usajilishaji una msukumo wa kisiasa. Kwa mfano ni kwa njia gani msajili amekataa kusajilisha kile Chama cha Kiisalamu cha Kenya (IPK) ?
- Vyama vya kisiasa viko katika mamlaka ya utaratibu wa maadili ya kisheria kwa madhumuni ya uchaguzi, na vinaweza kulipishwa faini au kukatazwa kugombea uchaguzi wakati wa ukiukaji mkubwa wa kanuni za Utaratibu

Maadili, ingawa, katika utekelezaji vikwazo hivyo havijafuatwa licha ya ukiukaji uliopakaa.

- Vyama vingi vina msingi wa kikabila, hata muungano wa vyama vya hivi majuzi au majaribio ya kuunganisha vyama yameathiriwa zaidi sana na uwezakano wa muungano wa kikabila.
- Vyama vingi ni mali za kibinafsi za watu.
- Hakuka hisia za dhati kuhusu uaminifu kwa chama kuambatana na watu wengi.
- Vyama si vya kimfumo (havina muelekeo wa kisiasa) na huchukuliwa na wanasiasa kuwa vyombo vya uwezo wa kibinafsi.
- Ni vyama vichache vilivyo na sera za dhati za kijamii, kiuchumi na kifedha.
- Ni nadra ambapo vyama vivapochangia mawazo ya kiutawala, haki za jamii, au maono ya nchi.
- Vyama hutendakazi zaidi wakati wa uchaguzi.
- Sheria na ukatiba wa uhusiano na, au kujiondoa kwenye vyama ni nadra kufuatwa.
- Vyama vingi yasemekana vina vikosi vya wapiganaji na hawa tasita kuzusha vita.

### 9.4.2 Vyama vya Kisiasa katika Katiba

Ingawa Katiba ya Kenya haina utaratibu wa masharti kuhusu vyama vya kisiasa, imeanzisha nafasi muhimu kwa vyama. Ile haki ya uhusiano hata hivyo itaweza kuwaruhusu watu kuunda vyama vya kisiasa – ijapokuwa hali imekuwa kwamba udhibiti wa kiutawala hutumiwa katika usajilishaji wa vyama, ambao hufanywa chini ya Sheria ya Vyama. Katika mwaka 1982, Katiba ilibadilishwa ili kuzuia kuwepo kwa chama chochote isipokuwa KANU.

Ingawaje, baada ya wasiwasi na ghasia nyingi, sharti hili lilifutiliwa mbali mwaka 1991 na mfumo wa vyama vingi ukarudishwa: mwaka 1991, shehemu ilingizwa kwenye Katiba iliyo tamka kwamba "jamhuri ya Kenya itakuwa ni taifa la kidemokrasia ya

vyama vingi (sehemu 1A), lakini muundo wa kisheria wa usajilishaji, usimamizi na kuvunjwa kwa vyama haukubadilishwa. Mwaka huo huo, kile kikwazi kwamba Rais lazima ateue mawaziri kutoka chama chake kiliondolewa, lakini, vikwazo vingine vilianzishwa mwaka 1997, ambavyo vingeifanya Katiba iende sambamba na shughuli za vyama. Hivi ni pamoja na:

- Ni nadra kwa Katiba kukifafanua chama kama kile kilichosajiliwa vilivyo. Hakuna utaratibu maalum wowote kuhusu uundaji wa vyama. Vyama husajiliwa chini ya Sheria ya Vyama na si muhimu kamwe kuonyesha kiasi chochote cha watu wanaounga mkono chama.
- Wagombea uchaguzi wa Rais lazima wateuliwe na chama cha kisasa.
- Wagombea uchaguzi wa Baraza la Wabunge lazima wateuliwe na chama cha kisiasa.
- Vyama vya kisiasa vinateua wale watakaoteuliwa kama wana chama wa Baraza la Wabunge kulingana na viti vyao bungeni.
- Mwanachama wa baraza la bunge aliyechaguliwa ama kuteuliwa hupoteza kiti chake ikiwa mwanachama huyo atajiuzulu na kutoka chama kile kilichounga mkono uchaguzi ama uteuzi wake, ambapo chama hicho bado ni chama cha bunge. Kama mwanachama huyo atajiunga na chama kingine wakati ambapo chama chake asilia hakipo tena, basi huyu atapoteza kiti chake cha bunge.
- Hakuna misaada ya kiserikali kwa vyama vya kisiasa, ingawa madai hufanya mara nyingi kwamba chama kinachotawala hupata usaidizi wa serikali kwa njia mbalimbali.
- Kanuni kuu za Baraza la Wabunge zatambua vyama vya bunge katika kamati na utaratibu wa Bunge.
- Ingawa Rias hufanya uteuzi kwa Tume ya Uchaguzi, maelewano yanaelekea kuwa Rais atashauriana na viongozi wa vyama vya kisiasa kabla ya kufanya uteuzi huo.
- Baraza la wabunge na Sheria ya Uchaguzi wa Rias yaeleza kwamba mtu aliyeteuliwa ama kuchaguliwa kama mwanachama wa Baraza la Wabunge akiungwa mkono na chama cha kisiasa (kando na chama ambacho mgombea

uchaguzi wake amechaguliwa Rais katika uchaguzi) hawezi kuteuliwa kuwa waziri (chini ya sehemu 16 ya katiba) bila maafikiano ya chama kilichomuunga mkono katika uchaguzi au uteuzi (sehemu 17 (5) )

### 9.4.3 Vyama vya Kisiasa katika Katiba Nyingine

Inatambuliwa kimataifa kwamba vyama vya kisiasa vina nafasi muhimu katika utawala wa kidemokrasia. Kama kanuni ya kijumla, hata hivyo, katiba nyingi hutoa mamlaka ya utungaji sheria wa kuwekea mipaka vyama vya kisiasa. Kwa hivyo Ibara 3 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano inataja kuwa:

> *Masuala yote yanayohusu usajili na utawala wa vyama vya kisiasa katika Jamhuri ya Muungano yataongozwa na sheria ya Bunge iliyoundwa kwa ajili hiyo.*

Ibara 69 – 75 za Katiba ya Uganda zinatatanisha zaidi kuhusu suala hili isipokuwa kutaja kuhusu kuharamisha taifa la chama kimoja. Ila tu katika mataifa ambayo bado yanafuata itikadi za kimaksi, kilenin au kimao na ambayo kwa hivyo yanatambua na kuhakikisha kuweko kwa chama mwasisi katika katiba, ni katiba chache mno zenye kanuni wazi kuhusu vyama vya kisiasa.

Sheria ya kimsingi ya Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani ni mfano mmoja tu wa hali hii. kwa mujibu wa Ibara 21 ya sheria,

(1) Vyama vitasaidia kujenga imani ya kisiasa ya wananchi; vinaweza kuanzishwa kwa uhuru; muundo wake wa ndani utafuata kanuni za kidemokrasia;
(2) Vyama ambavyo …… vinajaribu kuhatarisha au kutupilia mbali utaratibu huru wa kidemokrasia……vitakuwa kinyume na Katiba.

### 9.4.4 Waliyosema Wananchi

Yale watu walioambia Tume yanaweza kuelezwa kimuktasari kama ifuatavyo:_

*i)* *Kuhusu ikiwa Katiba itadhibiti uundaji, usimamizi na maadili ya vyama vya kisiasa; watu walikuwa na maoni yafuatayo –*

a. Ukabila katika vyama vya kisiasa umezidi
b. Kuna vyama vingi vya kisiasa
c. Wanasiasa wakati mwingine wametumia majeshi kwa njia mbaya na kuyafanya yaonekana kama magaidi
d. Katiba iliyo sasa hailazimishi vyama vya kisiasa kufanay uchaguzi mwema ndani yake au kuendeleza demokrasia; kwa hivyo tumebaki na vyama vya kidikteta kwa maslahi ya kibinafsi kama kiini cha sababu ya kuwepo kwake.
e. Siku hizi kuna vyama "visivyokuwa na wanachama" (visivyokuwa na afisi) cilivyotayari kwa kuuzwa.
f. Vyama siku hizi huundwa kwa kujiendeleza kibinafsi.
g. Utawala katika mamlaka unaweza kugandamiza upinzani na unhurt wa vyama kwa sheria, uundaji na usimamizi.
h. Ujambazi wa kisiasa umejikata
i. Katiba yahitaji kudhibiti uundaji na usimamizi wa vyama vya kisiasa
j. Uundaji wa vyama vya kisiasa usitegemee msingi ya kikabila
k. Vyama vya kisiasa yabidi view na hisia za kitaifa
l. Vyama vya kisiasa vingekuwa na uhuru katika mambo ya usajilishaji wa uanachama na manifesto.
m. Uundaji na usimamizi wa vyama vya kisiasa uzingatie ujinsia kwamba kuwe na usawa wa kijinsia katika uanachama wa vyama.
n. Kabla ya chama chocote kusajiliwa, kwanza lazima kichunguzwe, hasa kuambatana na:
o. Vyama vya kisiasa yapasa view na manifesto ya wazi, ie kuonyesha kile kinachotarajiwa kufanyiwa wananchi, chama hichi kinapokuwa mamlakani. Jambo lililojitokeza kwa demokrasia na kuhamasisha watu kuhusu amani na umoja wa kitaifa.
p. Uundaji wa vyama vya kitaifa vingeongozwa na sheria za Tume ya Uchaguzi.
q. Kuwe na utaratibu wa maadili, utakaifuatwa na wanachama wote wa chama.

ii) *Kuhusu ikiwa baadhi ya vyama vya kisiasa vingepunguzwa na kama ni hivyo, kwa njia gani, sisi wananchi tulikuwa na maoni kwamba-*

a. Vyama vingi vya kisiasa vimeleta mgawanyiko miongoni mwa Wakenya.
b. Vyama vingi vya kisiasa vimehimiza mfumo wa kugawanya watu na kuwatawala
c. Kuna ugomvi mwingi na wasiwasi miongoni mwa Wakenya na mambo ya kuhama vyama kiholela na bila mpango wo wote.
d. Siasa ya vyama vingi imeleta muongeseko wa ugandamizi wa ukabila.
e. Vingi ya vyama vya kisiasa hunakili sera za vyama vingine.
f. Vyama vingi vya kisiasa hutumiwa kama njia ya kuingilia Bunge.
g. Kuwa na vyama vingi vya kisiasa kumeleta uzorotaji wa uchumi.

iii) *Kuhusu ikiwa mambari ya vyama vya kisiasa ingepunguzwa watu walikuwa na maoni kwamba-*

*a.* Vyama vya kisiasa vingepunguzwa view chini ya vyama vitano (5) vya kitaifa.

*b.* Nchi ingekuwa na zaidi ya vyama vitano vya kisiasa. Kati yao, baadhi walihisi kwamba tungekuwa na vyama vya kisiasa hadi kufikia arobaini.

*c.* Kwa upande mwingine kusiwe na kipimo cha nambari za vyama vya kisiasa. Tunaweza kuwa na vingi kama inavyowezekana.

iv) *Kuhusu kama vyama vya kisiasa vina wajibu mwingine kando na kuunganisha watu kisiasa, wnanchi walikuwa na maoni kwamba-*

*a.* Uadilifu mwingi wa chama cha kisiasa huzorota na kuleta uhuni panapokuwa na ushindani.

*b.* Vipimo na visawazishi vita kavyosaidia kungoa ufisadi na tabia za kiholela haujaritibiwa.

*c.* Utawala na polisi wamekiuka sheria za utoaji wa leseni kwa mukutano ya kisiasa, ili kuadhibu wale wasiopendelewa na serikali.

*d.* Vyama vya kisiasa mara nyingi ni vifaa vya kupigana na utawala na jamii nyinginezoza kimataifa.

*e.* Vyama vya kisiasa vingehusishwa zaidi katika mpango ya maendeleo, ambyo ingeendeleza hadhi ya kijamii na kiuchumi ya wananchi.

f. Vingehusika zaidi katika kuwaleta watu pamoja katika masuala yanayohusu siasa.

g. Vyama vya kisiasa vingehusika na elimu ya jamii.

h. Vyama vya kisiasa vingetekeleza wajibu wa utawala.

i. Wajibu mkubwa wa chama cha kisiasa ni kuendeleza umoja wa kitaifa.

j. Vyama vya kisiasa vihusishwe katika mpango ya usimamizi wa mkasa.

iv) *Kuhusu kama fedha za umma zingetumiwa kufadhili vyama vya kisiasa na kama ni hivyo, kwa masharti gani, wananchi wakikuwa na maoni kwamba-*

a. Kanu isingemiliki jumba la KICC kwa sababu ni jumba la Taifa.

b. Watu maalumu kwa ajili ya hadhi yao ya kifedha, hutawala vyama vya kisiasa.

c. Vyama vingi vya kisiasa havina fedha na hivyo haviwezi kutekeleza shughuli zao kikamilifu.

d. Kadri chama kinavyokuwa na pesa nyingi, ndivyo nafasi yake ya kushinda uchaguzi inavyoongezeka.

e. Kama vyama vya kitaifa havitapewa fedha, vitaomba kutoka nje na vitapoteza uhuru wao kwa ajili ya kiathiriwa.

f. Serikali ngechukua wajibu wa kufadhili vyama vya kisiasa.

g. Vyama vya kisiasa vingejifadhili vyenyewe kifedha kutokana na ada ya uanachama.

h. Vyama vya kisiasa vingedadhiliwa na wadhamini na wengine wanaounga mkono.

i. Ufadhili wa vyama vya kisiasa ungekuwa na msingi katika mfumo wa uwazi na uwajibikaji wa chama.

j. Manufaa ya manifesto za chama ungelazimika kudhiturishwa kabla ya ufadhili kultolewa.

k. Vyama pia vingekuwa na wananchama wa kutosha kabla ya kupewa ufadhili.

l. Ufadhili wa vyama vya kisiasa vingejikita katika uwakilishi wa bunge, yaani, ni wananchama wangapi wa chama wamo Bungeni.

m. Vyama vya kisiasa yapasa vifadhiliwe kwa hali ya usawa lciha ya manifesto zao na uwakishi wao Bungeni.

n. Vyama vya kisiasa vingefadhiliwa tu kwa uchaguzi mkuu.
o. Kuhusu sasuala ya kikumla ya kisiasa, wananchi wahiwa na maoni kwamba:-
    a. Matumizi ya uwezo wa Rais wakati wa uchaguzi unaweza kuathiri kwa njia isyofaa mfumo wa uchaguzi.
    b. Kusumbuliwa na serikali lazima uondolewe.
    c. Kwakuwa mwanachama wa cham cha kisiasa, Rais ana majiribu ya kutumia rasilimali ya umma kwa kuendeleza shughuli za chama chake.
    d. Shughuli za chama kinachotawala na zile za utawala zisichanganyiwe pamoja.
    e. Lazima pawe na ushirikiano baina ya serikali na vyama vya kisiasa vya upinzani.
    f. Kiongozi wa serikali asijihusishe na chama cho chote cha kisiasa.
    g. Chama kinachotawala kisitumie vyombo vya serikali kwa kampeni yao na ikiwa hivyo, basi vyama vyote vya kisiasa vingeruhusiwa kutekeleza kampeni za kupitia kwa chombo cha serikali.

### 9.4.5 Uchanganuzi

Vyama vya kisiasa, kama asasi za utawala wa kidemokrasia na kijamhuri, ni muhimu na zisionekane kama chombo cha kikatiba mabacho kingeongozwa na kudhitibiwa na katiba. Ni vitengo vya asasi ambazo zingefafanuliwa wazi wazi na wajibu na kazi zake kuelezwa katika katiba, kwa njia ile ile ambayo vyombo vile vitatu vingine vya serikali (Mahakama, Bunge na Mamlaka ya Nchi) vimefafanuliwa.

Wajibu wa chombo hiki ungefafanuliwa wazi katika Katiba. Ikiwa vyama vya kisiasa vina nafasi katika kuleta udemokrasia na ukatiba, muunbo wake, mpangilio na shughuli lazima yaelezwe na kudhibitiwa na katiba na undani wa mambo ukiekezwa na sheria iliyojikita kwenye katiba. Kwa hivyo tume inapendekeza kuwa Katiba iingize ndani yake vyama vya kisiasa. Hili lingejumlisha haki ya kuunda na kuunganisha vyama, kuweka utaratibu wa sheria kwa vyama vya kisiasa, vinavyopigania uchaguzi kwa vyama vya kisiasa. Tume inafahamu kuwa kwa sababu Kenya iliingia katika kipindi kipya cha udemokrasia muongo mmoja ulipita, watu wasivunjwe moyo katika harakati zao za

kuunda vyama vya kisiasa au katika uhuru wao wa kujihusisha katika mazingira ya kisiasa. Kwa hivyo, Tume haiungi mkono upunguzaji wa idadi ya vyama vya kisiasa (kwa sababu zilizotolewa hapo juu), ijapokuwa tunakubali kwamba vyama vingi havipendelewi.

Hata hivyo Tume au sheria juu ya vyama vya kisiasa ingetoa masharti ya wazi ya uundaji na usajilishaji wa chama masharti ambayo yatadhibiti idadi ya vyama vya kisiasa. Tunafikiria kuwa idadi ya vyama itapungua ikiwa haitakuwa muhimu tena kwa wagombeaji uchaguzi wa urais na ubunge kuteuliwa na vyama vya kisasa, kama tulivyo pendekeza kwenye sura ya Mfumo wa Uchaguzi na Utaratibu. Idadi ya vyama pia ingepungua ikiwa hali ngumu zingewekwa kuhusu usajilishaji wa vyama (kama tulivyopendekeza hapo chini).

Tume inatambua kwamba demokrasia inamaanisha kuwa raia wana uhuru wa kuunda vyama vya kisiasa kwa uamuzi wao wenyewe na kwamba serikali ingeruhusu haki ya watu kujihusisha. Kuhusu vyama vya kisiasa na uchaguzi, sheira ingeweka mbinu za kulinda umoja wa taifa, amani, usalama, utawala wa sheria, haki, demokrasia na haki za binadamu kutokana na sekta zenye uwezo au nguvu za kikabila ambazo zingekuika kwa urahizi kanuni na maadili haya, ambayo kwayo nchi yetu imeundwa.

### 9.4.6 Mapendekezo

Kwa hivyo Tume imependekeza:-

*(i) Kuhusu Haki ya kuunda Vyama vya Kisiasa,*

a) haki ya kuunda vyama vya kisiasa italindwa kwa muujibu wa masharti ya katiba.

b) Vyama vya kisiasa vinavyotarajia kugombea uchaguzi vitahitajika vijisajilishe kwa Tume ya Uchaguzi sifa za kusajiliwa zilenge kuhakisha kuwepo kwa demokrasia na uwajibikaji wa ndani na uwajibikaji wa nje.

*(ii)* *Kuhusu sifa za Kusajiliwa kama Chama cha Kisiasa,*

a) Tume ya Uchaguzi itakuwa wakala wa usajilishaji wa chama cha kisiasa.

b) Vinapotafuta usajili, vyama lazima vitosheleze kigezo kifuatacho na baada ya kusajiliwa wajitolee kutimiza masharti yafuatayo. Chama kitatakikana:

- Kuendeleza na kushikilia umoja wa taifa. Kila chama cha kisiasa kitakuwa na sura ya kitaifa, na kamati kuu itawakilisha sehemu zote za nchi.
- Kutii kanuni za kidemokrasia, keundelza na kutekeleza demokrasia katika chama kwa njia ya kufanya uchaguzi wenye usawa na usiomapendeleo mara kwa mara.
- Kufuata utaratibu wa kufanya uamuzi kidemokrasia
- Kutofukuza wanachama yeyote kutoka kwenye chama isipokuwa kwa sababu nzuri na baada ya utaratibu unaofaa. Chama kitaheshimu katiba na sheria za nchi.
- Kuendeleza na kuheshimu haki za binadamu, pamoja na usawa wa kijirisia.

c) Iwe kwamba angalau thuluthi moja ya wagombea ucahguzi waliopo kwa viti vya eneobunge la kijiografia ni vya wananwake. Chama kitahimizwa kuwatena wagombea uchaguzi wanawake katika maeneobunge ambayo chama kitayaona kuwa yenye usalama – katika maeneobunge yale ambayo chama kinahakika kitashinda.

d) Chama hakitaundwa katika misingi ya kidini, kilugha, kirangi, kikabila, kijinsia, kishirika au kieneo peke yake, isipokuwa kwa kuendeleza vyombo na kanuni za katiba na sheria za Kenya. Vyama vya kitaifa vimekatazwa kushiriki katika propaganda kuambatana na fikra hizi.

e) Vyama vya kitaifa vimekatazwa kushiriki katika au kuhimiza ghasia ama kutisha wanachama wake, wanaunga mkono ama wapinzani. Havitaanzisha wala kuweka vikosi vya kijeshi au mashirika kama hayo.

(a) Chama lazima kiweke hesabu zilizo sawa na ambazo lazima zikaguliwe kila mwaka. Hesabu zilizokaguliwa lazima ziwekwe kwenye jalada la Tume ya Uchaguzi na umma ili uweze kulipata kwa urahisi kwa uchanguzi. Tume ya Uchaguzi kupitia kwa ushauri wa Mkaguzi Mkuu inatoa maagizo ya utaratibu katika mtindo na viwango vya hesabu za vyama vya siasa. Mkaguzi wa Hesabu anaweza kuvichunguza vitabu na hesabu ya chama chochote kinachopata fedha kutoka kwa serikali (soma hapa chini kuhusu Ufadhili wa serikali).

(b) Punde tu chama kinaposajiliwa, kitalazimika kufuata kanuni za uadilifu (zinazofanana na zile za sheria za uchaguzi za Urais na wanabunge) ambao utahusisha wajibu wa kisheria chamani ili kuadhimisha vipindi vyake mamlakani. Chama kinapovunja kanuni hizo, kinaweza kuadhibiwa.

(c) Chama kitahitajika kuchapisha manifesto yake kabla ya uchaguzi.

*(iii)* *Kuhusu Usajili wa Muda,*

(a) Tume ya uchaguzi itatoa usajili wa muda, uliohalali kwa kipindi cha miezi 12, kwa vyama vya kisiasa vitakavyokutana na kuunda sheria na taratibu za usajili na kushiriki kwenye uchaguzi.

(b) Haki ya vyama wakati wa kipindi cha usajili wa muda inatakikana kutofautishwa na ile ya vyama vilivyo na usajili kamili kama vile kushiriki katika uchaguzi kwa njia ya kuwawasilisha wagombeaji na kushiriki kwenye kampeni za uchaguzi.

*(iv)* *Katika kufuta Usajili wa Vyama,*

(a) Sheria lazima iruhusu kufuta usajili wa vyama vilivyosajiliwa ambavyo vimegunduliwa kuivunja Katiba yake yenyewe, ama ya Katiba hii, ama ya kanuni za utekelezaji wa shughuli za uchaguzi, au sheria yoyote inayohusiana na shughuli za uchaguzi.

(b) Sheria inaweza kuipatia Tume ya Uchaguzi mamlaka ya kutoa ilani inayofaa kwa chama, na chama kisipoonyesha kujitolea au uwezo wa kuafikiana na Tume ya Uchaguzi, kitalazimika kuchukulia hatua utaratibu wa kufuta usajili kisheria. Chama kitakuwa na haki ya kukata rufaa kwenye Mahakama Kuu.

(c) Kama adhabu ndogo, Tume ya Uchaguzi itazuia usaidizi wa Serikali, ambao umevunja wajibu.

(d) Uamuzi kamu huo unahitajika kuwa wazi kwa wanachama ambao wameshindwa kupata fursa ya kurekebisha kupitia kanuni za ndani ya chama.

(e) Vyama, ambavyo havina wagombeaji kwa vipindi viwili vya Uchaguzi Mkuu katika utawala, utafutwa.

*(v) Katika Haki ya kujiunga na Chama cha Kisiasa,*

(a) Kila mmoja ana uhuru wa kujiunga na chama cha kisiasa

(b) Hakuna mtu anayeweza kunyimwa fursa ya kujiunga na chama.

(c) Mtu atakayepatikana na makosa katika uchaguzi na matokeo yake iwe ni kumzuia kupiga kura kwa kipindi kimoja, atanyimwa uanachama wa vyama vya kisiasa kwa kipindi hicho.

(d) Raia peke yake ndio wanaoweza kuwa wanachama wa chama cha kisiasa.

*(vi) Katika Majukumu na Wajibu wa Vyama vya Kisiasa,*

(a) Vyama vya kisiasa vina uhuru wa kushiriki katika kurekebisha nia ya kisiasa ya watu, kusambaza habari katika mawazo ya kisiasa, kijamii na miradi ya kiuchumi ya kitaifa, kudhamini wagombeaji kwa uchaguzi wa afisi ya umma, na kuchagua ushirikiano wa watu kwenye masuala ya umma.

(b) Vyama vyote vitakuwa na kanuni kuu ya kuyaboresha maisha ya Wakenya na vile vile wema wa kila mtu na maslahi ya jamii ima kwenye chama kinachotawala au katika upinzani na mipango yote ya utawala bora nawa kijamhuri.

(c) Taifa litahakikisha hakuna upendeleo wa upande mmoja kati ya vyama halali vya kisiasa. Serikali itatoa fursa ya haki kwa vyama vyote vya kisiasa ili kuwasilisha miradi yao kwa umma kwa kuhakikisha kupata nafasi sawa kwenye vyombo vya habari vya kitaifa na vile vya kibinafsi.

(d) Majukumu au uwezo wa serikali hayawezi kugawanyiwa vyama vya kisiasa.

*(vii) Katika kuvidhamini Kifedha Vyama vya Kisiasa, kwamba*

(a) Udhamini wa kifedha utatolewa tu kusaidia katika

- Kusimamia gharama ya uchaguzi
- Kutangaza sera na miradi ya chama kupitia vyombo vya habari vya umma na vile vya kisiasa
- Elimu ya umma kwenye demokrasia na utaratibu wa uchaguzi
- La ziadi ni kwamba, fedha zisizozidi asilimia 10% kwa gharama ya jumla, zinaweza kugawanyiwa vyama ili kugharamia mipango.
- Vyama vinavyopokea chini ya asilimia 5% za kura zilizopigwa

(b) Mashirika (ya kigeni ama kitaifa) yanafaa kukatazwa kutoa michango ya kifedha, vifaa au michango mingine kwa vyama vya kisiasa isipokuwa kwa hali ambazo zitabainishwa na Tume ya Uchaguzi.

(c) Michango ya kibinafsi itawekewa viwango fulani vya kifedha vitakavyopitishwa katika vipindi fulani na Tume ya Uchaguzi.

(d) Vyama, vilivyosajiliwa na Tume ya Uchaguzi, vina haki ya kusaidiwa na serikali.

(e) Mtindo huu wa haki hiyo kwa vyama na taratibu za mgao huo unafaa kufafanulia kisheria kupitia mapendekezo ya tume ya uchaguzi.

(f) Mtindo huo unafaa kurejelea usaidizi kutoka kwa chama hasa katika Uchaguzi Mkuu uliotangulia. Mahali ambapo chama cha kisiasa kinapopata usaidizi mdogo wakati wa uchaguzi uliopita katika hoja za kuwa na haki ya kupata fedha, na ifaulu kufikia kiwango cha usaidizi hasa kwenye Uchaguzi Mkuu, bila ya maamuzi ya umma, inafaa iwe na mchango katika gharama ya uchaguzi uliolipiwa zamani.

(g) Mchango kutoka kwa fedha za umma unafaa kuwa wa kiwango fulani ili kutosheleza gharama ya uchaguzi, kwa elimu ya umma kupitia katika masuala ya uchaguzi na upigaji kura kwa zaidi ya asilimia 10% ya kiasi hicho kufuata mfumo uliotangulia ambao unaweza kuhusisha gharama ya kuendesha chama kati ya uchaguzi.

*(viii) Katika Usimamizi wa Vyama vya Kisiasa, kwamba*

(a) Uchaguzi wa afisi na kamati za vyama vya kisiasa utaendeshwa na au kusimamiwa na Tume ya Uchaguzi.

(b) Vyama lazima vitoe taarifa ya mwaka ya shughuli zao na hesabu kwa Tume ya Uchaguzi katika uwezo wake kama msajili wa vyama vya kisiasa, ambavyo vitahusisha umma.

(c) Tume inafaa kutumia mamlaka yake kuzuia kufutwa kwa usajili wa vyama ili kuhakikisha uendelezaji wa haki, demokrasia, mashindano ya haki na uchaguzi wa haki.

(d) Tume ya uchaguzi inafaa kuendeleza elimu ya umma ili kuwawezesha watu kujua haki zao za kikatiba, hasa wanapokaribia utaratibu wa uchaguzi, asasi nyingine za kitaifa na vyombo vya elimu ya kijamii.

(e) Tume ya Uchaguzi inafaa kuweka wazi kiwango fulani cha fedha ambacho, chama ama mgombeaji anazoweza kutumia kwenye kampeni, kiasi cha fedha ambacho kinachoweza kutengwa ili kuhakikisha kwamba uchaguzi hauwi wa gharama kubwa hadi kuzuia vyama kushiriki na wagombeaji wa kibanafsi katika utaratibu wa uchaguzi, na kuwapendelea wanaojiweza.

*(ix) Katika kuwafanyia nidhamu wanachama,*

(a) Katiba itahitaji vyama vya kisiasa kuwa na nyenzo za ndani zinazofaa katika kuhakikisha nidhamu inayoambatana na kanuni za demokrasia, haki na utawala wa sheria.

(b) Wabunge hawataadhibiwa ama kuwekwa hatiani na vyama vinavyowadhamini katika misingi ya michango iliyofanywa Bungeni ikiwa ni pamoja na upigaji kura kwa njia ambayo inaweza kuwa kinyume cha hali halisi ya chama kinachodhamini.

*(x) Kuhusu uhusiano kati ya chama kinachotawala na Serikali, kwamba*

(a) Rasilimali ya taifa au serikali haitatumika kuendesha shughuli za chama kwa wale wenye afisi za umma.

(b) Rais na wahusika wengine wakuu wa serikali hawatakuwa na mamlaka yoyote rasmi kwenye vyama vyao vya kisiasa. Anapoteuliwa katika afisi kuu ya umma, yule aliyeteuliwa atajiuzulu kutoka kwenye cheo chochote cha chama alichokuwa nacho kuwacha uanachama wake chamani, mara moja.

(c) Mawaziri wa Baraza la Mawaziri watateuliwa nje ya Bunge na watajiuzulu mara moja katika cheo walichonacho wakati wa uteuzi.

(d) Manifesto za vyama, Katiba, sheria ndogondogo au sera nyingine zozote zitakazoambatana na masharti ya kikatiba katika kanuni kuu za serikali.

(e) Vyama vyote (aidha vitakavyoshinda au vitakavyoshindwa) vitatakikana na katiba kuendesha shughuli zake za kisiasa kwa maslahi ya maisha na ustawi kwa jamii.

(f) Wabunge au wawakilishi wa mamlaka za wilaya pindi wanapochaguliwa watatii na kuwa waaminifu kwa Katiba ya Kenya na wanachama wote waliopo.

*(xi) Kuhusu kuhama vyama, kwamba*

(a) Wabunge na wawakilishi wa serikali ya wilaya wanaoamua kuasi au wanaokimbia vyama vinavyoowadhamini wanapiswa kupata maagizo mapya ya uchaguzi.

(b) Kushiriki kwenye serikali ya mpito si kweli kwamba kunachangia uasi chamani.

*(xii) Kuhusu Sheria ya vyama vya kisiasa, kwamba*

(a) Sheria iundwe kwa ufafanuzi fulani, kwa masharti kwamba chama chochote kinachohitaji usajili chini ya sheria hiyo lazima kitosheleze.

(b) Majukumu na wajibu wa vyama vya kisiasa katika utawala wa kidemokrasia yawekwe wazi.

(c) Demokrasia na utawala wa ndani wa vyama vya kisiasa ukarabatiwe.

(d) Vikwazo vinavyohusiana na kutokubaliana kwa masharti ya sheria iliyowekwa.

(e) Aina za asasi ambazo hazitaruhusiwa kujihusisha na mambo ya kisiasa na shughuli za uchaguzi zitolewe maagizo.

(f) Uanachama ambao si rasmi ama ushirika mara mbili na vyama vya kisiasa utupiliwe mbali.

(g) Hali halisi, ambayo chama cha kisiasa kitajiondoa peke yake au kupigwa marufuku iwekwe wazi.

(h) Uwezo wa Tume ya uchaguzi kusajili (kufuta usajili) wa vyama vya kisiasa ufafanuliwe.

(i) Ushirikiano wa vyama nje na ndani ya Bunge uhimizwe.

(j) Udhamini wa serikali wa vyama vya kisiasa ikiwa ni pamoja na chanzo cha uhalali na kupokea fedha hizo ambazo zinaweza kupokelewa kutoka kwenye hazina yoyote hasa kuambatana na michango na utaratibu wa kupokea misaada hiyo ya fedha kutoka kwenye hazina ya kigeni iliyoundwa.

(k) Uwajibikaji wa vyama vya kisiasa ikiwa ni pamoja na vikwazo vya kutokubaliana na sheria n.k. uundwe.

## 9.5. Taifa Katika Mfumo wa Kilimwengu

### 9.5.1 Kanuni za jumla

***(a) Maana na Uhusiano***

Utandawazi umetumika kuonyesha kasi ya kukua kwa shughuli za uchumi ambazo zinavukisha mipaka ya kisiasa iliyowazi ya kitaifa na kimaeneo.

Kwa kawaida hurahisishwa na kuchochewa kwa kupunguza vikwazo vya shughuli za mipakani kupitia maendeleo ya kiteknolojia kama katika mawasiliano na usafiri au kwa njia ya kupunguza siasa ama vikwazo vya sera kama vile gharama, vikwazo vya uwekezaji, mkanganyiko wa viwango vya ubora vya kitaifa na maagizo ya kimazingira, nguvu kazi n.k.

Utandawazi kwa jumla unaendeshwa na sekta ya kibinafsi hasa kwa misingi ya kupata faida na aghalabu kushinikizwa na msukumo wa mashindano. Kwa hivyo, utandawazi unaendelea kwa kasi mno, hasa katika mawanda ya masuala ya fedha za kimataifa na hii haijasababisha tu kupungua kwa umbali wa uchumi kati ya mataifa bali pia imevuruga hali halisi ya mifumo ya kiuchumi na kisiasa katika ngazi za kitaifa na kimataifa.

***(b) Utandawazi na uchumi***

Kwa kawaida utandawazi si jambo geni. Utandawazi kwa hali yake ya kiasili ni matokeo ya mgawanyiko wa sayari nzima hadi kwa mfumo wa kibepari.

Mawimbi ya kisasa ya utandawazi, yaliyoanza mwaka wa 1980 huku yakiwa sawa, yakifuata na yakiimarika kuambatana na mawimbi ya awali ya kilimwengu yanabainishwa na uwazi wa yaliyomo ambayo yamechangia mabadiliko ya misukumo ya uchumi duni ambao unaiendesha. Inahusisha:

- Kutodhibiti masoko katika mataifa yaliyoendelea;
- Usambazaji wa kisasa wa vyombo vya elektronia vinavyozingatia habari na teknolojia ya mawasiliano;
- Utandawazi wa fedha;
- Tazama mabadiliko ya mfumo wa sera katika maendeleo ya mataifa yaliyokuwa ya kisosholisti.

Ni vipengee hivi ambavyo vinafafanua umbo ambalo sheria ya utandawazi na maadili ya kitandawazi yanavyotekelezwa. Na kutokana na umbo hili, mtu anaweza kuanza

kuelewa asili ya mvurugano wa utandawazi ikiwa ni pamoja na msonge wa madaraka wa kilimwengu wa hivi sasa kuhusu kutokuwepo kwa usawa kwenye mgao wa rasilimali, na katika wajibu unaosaidia mataifa maskini kwenye soko la kilimwengu. Kwa kweli wajibu wa mataifa maskini umepungua kufikia ule wa wasanifu andamizi katika uchumi wa kilimwengu.

Hata hivyo watetezi wa utandawazi, wanauona kama chombo ambacho hakizuiliki na hakikwepeki, kinacholeta faida kama kazi, teknolojia, mapato, uwekezaji, utajiri n.k. kwa mataifa. Mataifa ambayo yangependelea kwa udhabiti wa soko huru kama vile, kubana matumizi ya umma, kubinafsisha huduma za umma, kuondoa mipaka ya uwekezaji wa kigeni, kuimarisha uzalishaji wa bidhaa a kuuzwa nje, kudhibiti kuongezeka na mengine mengi huku wakiwa ndio wafaidi wakubwa. Mataifa ambayo hayawezi kushindana kikamilifu kwa uwekezaji wa kigeni na kupata ruzuku kwenye soko la ulimwengu linalofuatia nyuma kwa kasi isiyoweza kusimamishwa.

Na kwa usambazaji wa rasilimali, manufaa ya utandawazi yamesambazwa kwa migao isiyosawa – miongoni mwa watu, katika mataifa na kati ya mataifa. Idadi ya ulimwengu ya juu yenye asilimia 20% inapokea mara 74 zaidi ya ile ya chini yenye asilimia 20%, na watu 200 matajiri zaidi duniani wana pesa zaidi ya mchanganyiko wa mapata ya idadi ya chini ya watu duniani ya asilimia 40%.

***(c) Mgawanyiko na ushirika wa kimaeneo***

Mjadala wa sera wa kimataifa kwa mwongo mmoja uliopita umekitisha mtazamo wake katika mgawanyiko wa kimaeneo na utandawazi kama pande mbili za sarafu. Mgawanyiko wa kimaeneo unaonekana kama chombo ambacho kinaweza kuunda biashara au kuzidisha utandawazi kwa kupunguza vikwazo vya sera katika kufanya biashara kwenye eneo moja, au kugawanya biashara na kufanya kinyume na utandawazi kwa kupendelea biashara iliyo kwenye eneo moja kwa gharama ya kufanya biashara na mataifa yaliyo nje ya eneo hilo.

Mengi ya mjadala wa sera ya uchumi kuhusu magawanyiko wa kimaeneo hata hivyo yameelekeza kuhusu mapatano ya kimaeneo kama ambaye niya kuunda au kugawanya biashara au zinatekeleza kazi, ama kinyume cha mfumo wa kibiashara wa dunia uliowazi. Katika utekelezaji, mgawanyiko wa kimaeneo unaelekea kuchochea sehemu mbili - lakini inategemea tu, ikiwa mgawanyiko huo wa kimaeneo unachochea mashindano ya ndani na kati ya maeneo (Oman Charles, 1997). Ushirika wa kimaeneo wa kimajukumu unaweza pia, kutekelezeka hata bila ya utaratibu rasmi wa muungano wa kiuchumi, lakini katika hali halisi ya mambo, mantiki ya muungano huo wa kieneo katika mataifa yanayoendelea wakati huu ni miongoni mwa njia zinazoboresha ushiriki wao kwenye uchumi wa kilimwengu.

Masharti ya kisisasa ya ufanisi wa mgawanyiko wa kimaeneo yanahusisha amani, usalama, heshima kwa haki za binadamu, demokrasia na utawala mwema. Masharti ya mwanzo ya kiuchumi ni pamoja na usimamizi wa wazi wa uchumi mdogo hasa kuambatana na fedha, bajeti na sera ya hazina ya serikali. Riba iliyo ongezeka katika mgawanyiko wa kimaeneo imefananishwa kwa njia nyingi na:-

- Nia ya kisiasa iliyofufuliwa tena na kuelezewa katika mapatano ya Abuja mwaka wa 1991.
- Kuundwa wa kuimarishwa kwa kingo za kimaeneo nje ya Afrika kama vile Mikutano ya siri ya uchumi wa wa Asia ya Mashariki huko bara Asia, Umoja wa watu wa Ulaya huko bara Ulaya na Mercosur na NAFTA katika America.
- Masoko madogo madogo ya kitaifa na kwa kiwango fulani kudharauliwa katika ulimwengu unaotawalwa na vigogo vya mataifa ya kibiashara. Masoko ya Afrika ni madogo na yenye viwango fulani kwa sababu ya kuwa pamoja na wengine. Waliotamalaki kwa sekta nyingine za kujipatia riziki. Bila ya msingi dhabiti wa kiviwanda na kiteknolojia, kutakuwa na vizuizi katika biashara iliyopanuka kwenye mataifa ya kiafrika.
- Hatua za kuleta mabadiliko, ambazo zimeunda mazingira yakufaa kwa sera za kiuchumi ambazo hazina mtazamo wa ndani.
- Kuna haja ya kuyatatua matatizo ya uchumi wa ndani ya nchi na migogoro.

- Haja ya kuwavutia wawekezaji wa kigeni wa moja kwa moja.

***(d) Sera ya Kenya ya Maingiliano Kieneo***

Kenya, Uganda na Tanzania zimekuwa na ushirika tokea awamu ya kwanza ya Muungano wa Forodha ulioundwa kati ya Kenya na Uganda mnamo mwaka wa 1917 na Tanzania wakaungana nao mwaka wa 1927. Mipango mingine iliyofuatia ilihusisha Balozi ya Afrika Mashariki (1948-1961); Shirika la huduma za kawaida za Afrika Mashariki (1961-1967) na muungano wa Afrika Mashariki (1967-1977). Baada ya kuvunjika kwa Muungano wa Afrika Mashariki mnamo mwaka wa 1977, nchi tatu za Afrika Mashariki hazikuwa na maagano yoyote rasmi ya kiushirika yanayowahusu hadi mwaka wa (1992-1993), wakati ambapo palikuwa na majaribio ya kufufua muungano huo wa Afrika mashariki. Ijapokuwa imebaki kuwa sera ya Kenya na mataifa mengine ya ngazi za kimabara na kieneo kufanikisha mazingira bora ya mgawanyiko wa kieneo, kati ya jitihada hizo hakuna ambazo zilizofua dafu katika kupata kanuni bora za kuunda soko huru au kuunda Umoja wa Forodha unaotekeleza majukumu yake kisawasawa.

Sera ya Mgawanyiko wakieneo ya Kenya inategemea kanuni zisizofuata mipango fulani, zisizovurugwa katika masuala ya ndani ya serikali, ujirani mwema, maelewano ya amani ya mizozo na kufuatia mkataba wa umoja wa mataifa na muungano wa Afrika. Msukumo mkuu wa mgawnyiko wa kieneo wa Kenya ni kutaka kuunda na kuendeleza mazingira yanayofaaa kwa kufanya biashara na uwekezaji kama matokeo ya vikwazo vya utandawazi na ulegezaji wa masharti.

Jambo moja dhahiri katika sera za kimaeneo za Kenya ni uanachama wake kwa miradi mingi ya mgawanyiko wa miradi ya kieneo, ambayo imefafanuliwa kwa muhtasari hapo chini. Hata hivyo hali hii, inatatiza mgawanyiko huo kwa sababu ya kunakili jitihada na rasilimali na kukosa mwafaka katika sera kama hizo kama sheria za awali na utaratibu wa kaida, upungufu wa habari na mabadiliko ya madaraka kwenye siasa.

*(i) Juhudi za Mipakani (Cross border Initiative – CBI)*

CBI, zilizofahamika kama kikundi cha urahisishaji wa maingiliano ya kieneo (RIF), zilianzishwa mwaka wa 1992 ili kuukimu mgawanyiko wa kieneo na kuleta nguvu za kurudisha ushirika Afrika mashariki. Wanachama wa CBI ni Waburundi, Wakomoro, Wakenya, Wabukini, Wamalawi, Wamauritius, Wanamibia, Warundi, Washelisheli, Waswizi, Watanzania, Waganda, Wazambia na Wazimbabwe. Kwenye muundo wa CBI, mataifa wanachama (pamoja na Muungano wa Afrika Mashariki) mwaka wa 1993 waliunda mradi wa kibiashara wa kulegeza masharti yaliyohusisha:

- Kuondelowea kwa NTB zote katika bishara ndani zote kutoka kwa mataifa washirika (orodha ya bidhaa za biashara-ndani ndogo za afya na usalama ziliondolewa).
- Orodha ya mapunguzo ya viwango vya ushuru vya kimaeneo iliyohitaji punguzo la asilimia 60% kufikia Oktoba 1993, punguzo la asilimia 70% kufikia Oktoba 1994, punguzo la asilimia 80% kufikia Oktoba 1996, asilimia 90% kufikia Oktoba 1999 na asilimia 100% kufikia Oktoba 2000.

- Hatua za CET kwa kuiga ushuru wa kuingiza bidhaa nchini kwa mataifa ya tatu wanachama na viwango vya chini kabisa.
- Kuoanisha viwango vya ushuru (bandi 3-4 za viwango vya ushuru ikiwa ni pamoja na sufuri, viwango vya ushuru vya biashara ya kawaida vilipimwa kwa kiwango cha juu kuwa 155, na viwango vya ushuru vya wastani visvyozidi asilimia 20-25%
- Kuoanisha taratibu za forodha na uwezekano wa kuunda umoja wa forodha.

*(ii)* *Muungano wa Afrika Mashariki*

Juhudi zilianza mwaka wa 1993 kuurudisha muungano wa Afrika Mashariki (EAC) kati ya nchi tatu za Afrika Mashariki Kenya, Uganda na Tanzania kwa kuunda Tume ya Utatu wa chama yakudumu, iliyopelekea kuundwa kwa kituo cha uratibu cha muungano wa Afrika Mashariki mnamo Machi, 1996.

Hatimaye, mapatano hayo yaliyounda muungano huo wa Afrika Mashariki yakatiwa sahihi mnamo Novemba 30, 1999 na Jumuiya hii ikazinduliwa mnamo Januari 2001.

Madhumuni ya jumuiya ya kuunda sera na miradi inayolenga kupanua na kufanya ushirika wa kina miongoni mwa mataifa shirika katika siasa, uchumi, ujamii, mawanda ya kiasili, utafiti, teknolojia, ulinzi, usalama na masuala ya kisheria na kimahakama kwa manufaa ya wote (Ibara ya 5 ya mkataba wa Muungano wa Afrika Mashariki).

Kanuni muhimu zinazotawala Muungano wa Afrika Mashariki (Ibara ya 6) ni pamoja na:

- Uaminifu kwa wote, nafasi ya kisiasa, na usawa wa uhuru;
- Maisha yenye amani ya ujirani mwema;
- Kuondoa mizozo kwa njia ya amani;
- Utawala mwema ikiwa ni pamoja na kufuata kanuni za demokrasia, kanuni za sheria, uwajibikaji, uangavu, haki ya kijamii, nafasi sawa, usawa wa kijinsia na heshima kwa haki za binadamu.
- Mgao sawa wa faida; na
- Ushirika kwa manufaa ya wote.

*(iii) Soko Huru la Afrika Mashariki na kusini (COMESA)*

COMESA iliundwa kama Eneo la Kibiashara lililopendelewa la Afrika Mashariki na Kusini (PTA) mnamo mwaka wa 1981 na kubadilishwa kuwa COMESA mnamo mwaka wa 1994. COMESA ina mataifa wanachama 20 miongoni mwao ni Kenya na Uganda.

Mataifa wanachama wa COMESA yana utaratibu wa kuunda umoja wa forodha kwa kiwango huru cha nje cha ushuru (CET) kufikia mwaka 2004. Imeundwa maalum kujihusisha na udhaifu wa kimuundo na kiasasi kwa mataifa wanachama yake kwa kuchangia rasilimali.

COMESA inalenga katika maeneo yafuatayo yalipopewa kipaumbele:

- Kuongezeka kwa usalishaji wa viwanda, uundaji, uendeshaji na viwanda vya bidhaa za kilimo.
- Kuongezeka kwa usalishaji wa kilimo
- Kutangaza, kupanua na kuhimiza biashara
- Kuendelea kwa usafiri, mawasiliano na huduma nyingine.
- Kuendeleza data za habari zilizo kamili, za kutegewa na za kisasa.

Eneo la COMESA ndio kituo kikuu cha bidhaa zinatoka nchini Kenya. Katika kipindi cha miaka minne iliyopita, bidhaa zilizotolewa nchini kwenda COMESA ziliongezeka kutoka Kshs.51.4 bilioni mnamo 1997 hadi bilioni Kshs.56.7 mwaka wa 2000, ikiwakilisha nyongeza ya jumla ya asilimia 10.3%. Hata hivyo, eneo la COMESA linabakia kuwa chanzo cha kupungua kwa viwango vya kuingiza bidhaa nchini Kenya, wakati ambapo bidhaa zinazoingia nchini zikipungua kutoka Kshs.6.6 billion mpaka Kshs.5.2 billion kati ya mwaka wa 1997 na 2000 (Jamhuri ya Kenya, 2002).

*(iv) Mamlaka ya Kiserikali Kuhusu Maendeleo (IGAD)*

Ili kushughulikia matatizo ya ukame na kuongezeka kwa majangwa kieneo, mamlaka ya kiserikali kuhusu ukame na uongezekaji wa majangwa (IGADD) iliundwa mwaka wa 1977 na Djibouti, Ethiopia, Kenya, Somalia, Sudan na Uganda. Eritrea ikawa ya saba baada ya kujiunga mnamo mwaka wa 1993. Punde baadaye, jina IGADD likabadilika kuwa (IGAD) kwa mtazamo wa kiuchumi, kisiasa, na usalama wa ushirika. Mgawanyiko wa kieneo katika usalama wa chakula, kulinda mazingira, usimamizi wa rasilimali ya jumla ushirika wa kiuchumi, kutangaza amani na usalama vilikuwa ndio kusudi la IGAD. IGAD ina vitengo vitatu: Ushirika wa Kiuchumi, Kilimo na Mazingira na Masuala ya Kisiasa na Kibinadamu.

Shughuli kamili ambayo IGAD imefanya kwa kipindi cha miaka michache iliyopita imekuwa ni kuondoa mizozo na ghasia huko Sudan kusini na Somalia. Katika Mkutano wake wa nane wa viongozi wa mataifa na serikali uliofanyika mwaka 2000, wanachama walionelea ni vyema kuhimiza, kuchangia na kupanua biashara za kati ya mataifa

miongoni mwa mataifa wanachama ya IGAD na tayari Sudan wamesawidi itifaki za kibiashara, ambazo bado zinakaguliwa.

*(v) Umoja wa Afrika, Bahari ya Karibean, na Bahari ya Pacific (ACP) – Bara Ulaya (EU) Mwafaka wa Ushirika (ACP-EU)*

Kenya ni miongoni mwa mataifa yaliosaini umoja wa ACP-EU na mwafaka wa ushirika uliosainiwa huko Cotonou mnamo Juni 23, 2000, kitendo kinachoyafanya mataifa 15 ya bara ulaya kuwa pamoja na mataifa 77 ya ACP. Lengo kamili la ushirika wa ACP-EU ni kupunguza umaskini na hususani, kuundoa kabisa; kulingana maendeleo ya pande zote mbili, mgawanyiko wa kuendelea wa mataifa ya ACP katika uchumi wa dunia.

Ili kuyafikia malengo haya, mwafaka huo unachukua muondoko wa kusisitiza ushirika wa kieneo na mgawanyiko wake kwa dhumuni la:-

- Kuukimu mgawanyiko huo wa mataifa ya ACP yanapoingia katika uchumi wa dunia
- Kuzidisha ushiriki wa kiuchumi na maendeleo humu nchini na kati ya maeneo ya mataifa ya ACP.
- Kutangaza uhuru wa watu kutembea popote, bidhaa, huduma, mtaji, nguvu kazi na teknolojia miongoni mwa mataifa ya ACP.
- Kuzidisha mgawanyiko wa uchumi wa mataifa ya ACP; na uratibu na kuleta mwafaka wa kieneo na sera za ushirika za maeneo wilayani.
- Kuendeleza na kupanua biashara ya ACP ya kimaeneo na mataifa ya mrengo wa kushoto.

Sehemu kamili za mgawanyiko wa uchumi wa kieneo zinahusisha: uwezo wa kujenga katika kuendeleza ushirika wa uchumi wa kieneo na mgawanyiko; kuunda masoko ya kieneo na kuanza kugawanyiana faida kutoka hapo; kuanzisha mageuzi ya sera; kuweza kuikimu biashara na malipo; kuendeleza uwekezaji wa mipakani n.k.

### 9.5.2 Uhusiano wa kilimwengu kwenye Katiba

Mambo matatu yanatiliwa umaanani hapa. La kwanza, ni mkataba wa Kenya kufaulu, la pili, maadili ya kidiplomasia na uhusiano wa kibalozi na la talu ni mamlaka ya kutangaza vita.

***(a) Kufanikisha Mkataba***

Kufanikisha mkataba wa Kenya ni wajibu wa kuamini nadharia ya kwamba mikataba ya kimatiafa ni mifumo tofauti ya kisheria kinyume na sheria za makazi na manispaa. Hivyo basi, mkataba ambao serikali imeidhinisha kuhusishwa hauanzi kutekekelezwa kikawaida hivi hivi. Lazima pawe na utaratibu wa kubadilisha. Sheria inayofaa ya kitaifa lazima ipitishwe ili kuuwezesha mkataba huo kutumika kama wa kawaida. Msukumo huu unaofahamika kama nafasi ya uwili umeigwana takribani mataifa yote yaliyotawalwa na Uingereza.

Hali hii ya ufugaji au "mabadiliko" kwa kawaida hutokea katika mchanganyiko wa taratibu za mkataba kupitia mtindo wa kusawidi ambazo unaipa sheria nguvu katika masharti yaliyowekwa ya mkataba ama mkataba wote.

Mamlaka nyingi za kisheria huupanga mkataba na kuuweka katika sheria ya mabadiliko.

Mtazamo wa pili, unaofahamika kama njia ya kuhodhi ambayo haitofautishi baina ya sheria ya kimataifa na ya kawaida.

Mamlaka nyingi za kisheria sasa zinashikilia njia hii.

Kenya ni mwanachama wa mikataba 93 ya mambo mbali mbali na kuna mikataba mingine 69 inayoambatana na hiyo, ambayo kwa kiasi fulani Kenya ingependelea, na Kenya si mwanachama. Wakati wa Uhuru, Rais alirithi uwezo wote wa kuongoza na mamlaka ambayo Malkia angeweza kudumisha katika uhusiano kwa Kenya. Uwezo huu

haukufanya mabadiliko yanayoambatana na kanuni za masuala ya sheria ya kimataifa. Hii inabaki kuwa hali ilivyo mpaka sasa.

Masuala ya kanuni za sheria ya kimataifa inachukuliwa na kufanywa kuwa chini ya mamlaka aliyopewa Rais kwenye kifungu cha 23 cha Katiba. Zaidi ya hivyo, uwezo na wajibu wa Bunge hautoi nafasi ya kuifanya sheria ya kimataifa kuwa ya kawaida badala yake inachukuliwa kuwa miongoni mwa mamlaka ya kisheria.

Hali hii ya kufanikisha mkataba nchini Kenya inaiga sehemu kubwa ya mafundisho ya kiingereza. Kufanikisha mkataba ni jukumu maalum la kimamlaka. Majadiliano, kutia saini na makubaliano ya mwisho ya mkataba yanoyofanywa na serikali, kupitia kwa Rais ikiwepo wizara ya mambo ya nje na wizara husika. Bunge linahusishwa tu katika utaratibu huo wakati ambapo mkataba hatimaye umefikishwa mbele yake ili kuufanya wa kawaida na kuwezesha masharti ya manispaa kuendelea vyema. Hivyo basi, serikali inalipatia fursa taifa kwenye masuala ya kimataifa kabla ya sheria ya kawaida kuwa mamlakani ili kuuwezesha mkataba kuendesha shughuli zake vyema. Hivyo basi tunaweza kuhitajika kutukuza makubaliano yetu ya kimataifa muda mrefu kabla ya bunge kuyafanya masharti ya kimataifa kuwa ya kawaida.

*(i) Mikataba kabla ya uhuru*

Kwa maelezo yake EXT. 237/003A ya Machi 25, 1964, yaliyoandikwa kwa katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Rais wetu, kisha waziri mkuu, walitoa azimio, ambalo lingaliweza kubainisha hali ya kisheria ya mikataba iliyofanywa kati ya serikali ya uingereza na serikali nyingine na zilizotuma maombi au kufikishwa Kenya. Kenya inatangaza nia yake ya kufaulu katika mikataba iliyokuwepo kabla ya uhuru kwa miaka 2, kama vile kutoka Disemba 12, 1963 mpaka Disemba 12, 1965. Kwa kipindi hicho cha miaka miwili serikali ililazimika kubadilisha mikataba iliyopo na kuamua kwamba watashirikiana ama kutoshirikiana katika uhusiano ulioanzishwa pale awali na serikali nyingine na uingereza kwa niaba ya Kenya, bado itaendelea.

Kulingana na mikataba hiyo ya pande mbili wakati huu ulikuwa kwa maneno ya azimio, "iliyotegemewa kuendesha majadiliano ya kidiplomasia ili kuziwezesha pande zenye nia ya kupata kwa uwezekano wa kuendelea au kukarabati au kukomesha mikataba".

Kuambatana na mikataba ya pande mbali mbali, serikali ilitegemea kwamba kwa kipindi cha miaka 2 kuanzia siku ya uhuru, au siku nyingine itakayotolewa, kudhihirisha kuwa taifa linalotunza au shirika, hatua ambayo serikali inataka kuchukua inayohusu kila mkataba wa pande zote. Ujumbe huo ulihitajika kuwa kwa njia ya aidha kuthibitisha kukomesha kwa mkataba, au kuthibitisha ufanisi au kufikika. Katika kipindi cha muda mfupi wa marekebisho, chama chochote chenye mkataba wa pande zote au uliozidishiwa kwa Kenya wakingojea uhuru, kitaweza kuwa kwenye misingi ya kuzunguka.

Kwa kipindi hicho cha marekebisho cha miaka miwili, haikuwa rahisi kuyamaliza mambo ya mataifa ya kigeni yanayovutiwa. Huku azimio la ziada likatolewea la kuongeza muda huo kwa miaka 2 zaidi mpaka Disemba 12, 1967. Katika kipindi hiki cha pili, maelezo ya marekebisho yalitangazwa kwa niaba ya serikali ya Kenya kwa serikali nyingine mbali mbali wakizialika kukubali kutumia mikataba inayozungumziwa huku wakingoja mikataba mipya tofauti ilioyojadiliwa kati ya serikali ya Kenya na serikali nyingine.

Matokeo ya maelezo ya mabadiliko ya Kenya yalipokelewa kutoka kwa serikali nyingine nyingi zikionyesha nia yao ya kuendelea na uhusiano ulioanzishwa chini ya mikataba inayo zungumziwa. Hivyo basi, mikataba hii ilibakia mamlakani hata baada ya Disemba 12, 1967 ikingoja kurekebishwa au kukomeshwa kama hali inavyoweza kuwa. Lakini mikataba kulingana na kuwa hakuna matokeo yaliyopokelewa na serikali husika, moja kwa moja mikataba hiyo ilitolewa mamlakani nchini Kenya baada ya Disemba 12, 1967. Sera hiyo hiyo ndiyo iliyotumika katika hali ya mikataba ya pande zote ambayo serikali ya Kenya haikulifahamisha taifa linalotunza ama shirika kwa kuendelea kwake. Mikataba kama hiyo ya pande mbili, ambayo haijapitishwa na Kenya inaweza kuchukuliwa kana kwamba imekoma kutumiwa hapa Kenya kuanzia Disemba 12, 1967.

*(ii) Hali ya Kisasa*

Kwa miaka sasa Kenya imeonyesha hali ya kuweka mikataba isiyo na mpango ambayo inapaswa kutatuliwa na Katiba. Swali kuhusu ni vipi Kenya ilichagua kuwa katika mikataba fulani na si katika mingine linahitaji jibu. Kwa kweli, hii inaonyesha kuwepo swala tatizi la mwelekeo wa Kenya na msimamo uliochukuliwa na nchi hii kuhusu mikataba inayojulikana kuwa "ya kikoloni", kama vile swala lililozua mzozo la matumizi ya Maji ya Mto Nile ambalo limezungukwa na mijadala mingi.

***(b) Uhusiano wa kidiplomasia na kikonsela***

Uhusiano wa kidiplomasia na kikonsela ni muhimu katika kuendeleza maslahi ya taifa. Ni vifaa vinavyotumiwa kupata manufaa ya kimataifa kwa njia ya amani bila kusababisha usumbufu. Majukumu ya ubalozi yamefafanuliwa wazi katika mapatano ya Vienna 1961 kuhusu uhusiano wa kidiplomasia kuwa-

(a) Kuwakilisha taifa linalotuma katika taifa linalopokea.

(b) Kulinda maslahi ya taifa linalotuma, pamoja na maslahi ya wananchi wake katika taifa linalopokea, katika mipaka inayokubaliwa na sheria ya kimataifa; kushauriana na Serikali ya taifa linalopokea;

(c) Kuhakikisha kupitia njia zote za kisheria hali na maendeleo katika taifa linalopokea, na kuripoti kwa Serikali ya taifa linalotuma;

(d) Kuendeleza uhusiano wa kirafiki kati ya taifa linalotuma na taifa linalopokea na kuimarisha uhusiano wao kiuchumi, kitamaduni, na kisayansi.

Mataifa, ambayo uwepo wake ni wa kisheria, yanaweza tu kutenda kupitia watu binafsi kama mawakala au wawakilishi wake. Mwakilishi Mkuu wa Taifa ni Kiongozi wa Taifa. Katika kuongezea, kuna mawakala wa kidiplomasia ambao wameelezwa katika

Mapatano ya Vienna kama " *kiongozi wa ujumbe au mwanachama wa wafanyikazi wa kidiplomasia wa ujumbe*"

Viongozi wa jumbe wanaidhinishwa ifuatavyo:

(a) Mabalozi au mabalozi wa Papa na viongozi wengine wa ujumbe wa viwango sawa- Mabalozi ndiyo walio katika kiwango cha juu zaidi miongoni mwa wawakilishi wa kidiplomasia. Awali mabalozi walikuwa wakitumwa tu katika falme kuu, huku jumbe au Wakuu wa Maswala wakitokeza katika uhusiano kati ya Mataifa yasiyo na uwezo mkubwa.

(b) Jumbe, mawaziri, na mabalozi wa Papa waliteuliwa na Viongozi wa Taifa.

(c) Wakuu wa Maswala walioteuliwa na waziri wa Mashauri ya Kigeni - Wakuu wa Maswala anaweza kuteuliwa kupitia uteuzi wa kudumu au wa muda kwa mfano ikiwa kiongozi wa ujumbe hayuko kazini au uteuzi wake bado unasubiri kushughulikiwa.

Uwezo na wajibu wa kuwateua mawakala wa kidiplomasia unatofautiana na kutegemea mamlaka ya kisheria. Uwezo huo huwa kamili pale ambapo umewekwa katika afisi moja ya Taifa hasa Kiongozi mwenye mamlaka makuu. Kisha kiongozi huyo anaweza kuwajibika katika uteuzi wa mawakala wote wa kidiplomasia. Katika mataifa mengine, uwezo huu unaweza kuwekwa tu mikononi mwa Rais au Kiongozi wa Taifa kama kiongozi wa mamlaka makuu. Mataifa kama vile Ujerumani, Uhispania, Argentina, Iraq, Indonesia, Cameroon na Zambia yako katika kundi hili.

Kwa mujibu wa sehemu ya 111(2) ya Katiba iliyopo sasa-

*"Uwezo wa kumteua mtu kushikilia au kufanya kazi katika afisi ya balozi, au mwakilishi mwingine mkuu wa Kenya katika taifa jingine na kumwondoa afisini mtu anayeshikilia au anayefanya kazi katika afisi kama hiyo umewekwa mikononi mwa Rais."*

Hali nchini Kenya kwa hivyo ni ya kipekee kwa kuwa Rais ndiye mwenye mamlaka yote katika utaratibu wa uteuzi.

***(c) Kutangaza Vita na kutoa Majeshi ya Kenya***

Katika mataifa mengi, swala la ni nani anayeweza kutangaza vita na kinachosababisha vita huzua mijadala mikubwa.

Katiba iliyopo sasa haishughulikii swala la kutangaza vita au kutolewa kwa vikosi vya majeshi ya Kenya nje ya taifa hili. Hii hata hivyo inachukuliwa kama mojawapo ya majukumu ya Rais chini ya sehemu ya 23 ya Katiba.

### 9.5.3 Uhusiano wa Kimataifa katika Katiba Nyingine

Kuna masuala matatu ya kimsingi yaliyokuwa na umuhimu kwa Tume: Umilisi wa kufanya mikataba, uhusiano wa kidiplomasia na kikonsela, na mamlaka ya kutangaza vita au kuamuru majeshi ya kushiriki vita ng'ambo. Masuala haya, kama ilivyotajwa, hayashughulikiwi kwenye Katiba. Nchini Uingereza, kwa mfano yanaachiwa kikaida mamlaka ya Nchi au mapenzi ya mfalme/malkia. Katiba ya Marekani hata hivyo ina kanuni mahsusi kuhusu umilisi wa Rais katika kufanya mikaba.

Ibara II (2) inasema kuwa Rais: *ana uwezo kupitia kwa na kwa ushauri na kibali cha seneti, kufanya mikataba, mradi tu thuluthi mbili za Maseneta waliopo wamekubali.*

Mikataba ikifanywa hivyo, huwa sehemu ya Sheria ya Juu ya Marekani. Katika lugha tofauti kidogo, Ibara 55 ya Katiba ya ufaransa imesema kuwa mikataba au mafikiano ya kimataifa yaliyodhinishwa mara kwa mara au kukubaliwa, yana mamlaka ya juu kuliko sheria ya manispaa, tangu tarehe ya kuchapishwa.

Katiba za hivi majuzi kama Uganda, Ghana, na Afrika kusini zina kanuni zinazohusisha mikataba na sheria ya kimataifa ya kaida katika mifumo ya kitaifa ya sheria. Baada ya kuteua maafisa wa kidiplomasia na kikonsela au kuamuru majeshi mataifa mengi kuipa mamlaka ya mamlaka ya Nchi uwezo wa kipekee. Ni katika hali chache sana ambapo mamlaka hayo hugawanywa na Bunge.

### 9.5.4 Waliyosema Wananchi

Wananchi waliiambia Tume itoe utaratibu kuhusu-

*(i) Kuhusu Uundaji wa mikatab, kuwe na kanuni:*

(a) Inayoshughulikia kikamilifu uundaji mikataba badala ya kuliacha kuchukuliwa kuwa kati ya majukumu ya vyombo kadhaa vya Taifa.

(b) Inayohusisha makundi mengine ila Mamlaka ya Nchi katika uundaji wa mikataba.

(c) Mikataba itekelezwe tu baada ya kushughulikiwa na kuidhinishwa na Bunge.

(d) Baada ya kushughulikiwa na kuidhinishwa, mikataba na mapatano na makubaliano ya kieneo na baina ya mataifa mawili, inapaswa kuathiri sheria nchini moja kwa moja.

(e) Mikataba inapaswa kutolewa kwa umma ili waitathmini kabla ya kutekelezwa. Baadhi ya watu walichukulia kuwa Kiongozi wa taifa anapaswa kuendelea kuwa na uwezo mkubwa katika uundaji wa mikataba.

(f) Mikataba iliyoundwa kabla ya Uhuru kama vile kuhusu matumizi ya maji yanayoingia katika Mto wa Nile kama vile Ziwa Viktoria ilizungumziwa sana na watu wanaoishi kando na wale wanaotegemea maji ya Ziwa.

*(ii) Kuhusu maswala ya kidiplomasia na kikonsela*

a) Mipango iliyopo sasa ya kidiplomasia na kikonsela.

b) Uendeshaji wa mashauri ya kigeni haupswi kuwa tu jukumu la mamlaka makuu.

c) Bunge linapaswa kuhusika katika kupima na kuidhinisha mawakala wa kidiplomasia. Wengine walipendekeza kuwa mamlaka makuu hayapaswi kuhusika na kuwa hili linapaswa tu kuwa jukumu la kisheria.

*(iii) Kuhusu kutangaza vita*

a) kuyanyima mamlaka makuu uwezo wa kipekee wa kutangaza vita. Bunge linapaswa kuhusika. Pia kulikuwa na mapendekezo kuwa hili linapaswa kuwa jukumu la kisheria.
b) Rais pamoja na bunge vihusike hivi kwamba Rais atatafuta ushauri wa Bunge kabla ya kutangaza vita.
c) Uidhinishaji wa Bunge uwe kupitia thuluthi mbili ya kura kabla ya kutangaza vita.
d) Majeshi yasitumwe katika mataifa ya kigeni.

### 9.5.5 Uchanganuzi

Kulikuwa na ufahamu mwingi kuhusu jinsi maswala ya ndani ya Kenya yanavyoathiriwa na kwa kiwango kikubwa zaidi yanavyoongozwa na matukio ya kiuchumi na kisiasa ulimwenguni. Vivyo hivyo, watu walifikiri kwamba kufanya uamuzi katika maswala ya kimataifa kunapaswa kugawanywa kati ya mamlaka makuu na wawakilishi wake Bungeni. Dhana kuwa mamlaka makuu yanapaswa kuwa katika nafasi ya kutoa wajibu kwa watu bila idhini au hata kuchunguzwa na Bunge ilikataliwa wazi wazi.

### 9.5.6 Mapendekezo

Kwa hivyo, Tume inapendekeza kuwa:-

*(i) Kuhusu utandawazi na miungano ya kieneo:*

a) Ili kuendeleza uthabiti katika mashauriano, ufuatiliaji na utekelezaji, vyombo vikuu au wizara zinazohusika katika kamati mpya ya kiwizara kuhusu biashara au makubaliano ya kibiashara baina ya mataifa ndiyo inayopaswa kuwajibika kwa mashauriano, kuunda na kutekeleza sera za biashara.
b) Katiba inapaswa kuhakikisha kuwa kama mwanachama wa Umoja wa Mataifa, Kenya itatumia nafasi yake kupinga dhuluma katika muundo wa kijamii, kiuchumi na kifedha wa Kilimwengu, madeni ya nje, utumiaji wa nguvu za kijeshi na ukosefu wa uwazi katika utaratibu wa kufanya maamuzi.

c) Katiba italihitaji Bunge kupitisha Sheria kuhusu biashara ya ndani na muingiliano wa kiuchumi:

- kufanikisha na kuongoza mashauri ya kibiashara kati ya Kenya na taifa jingine au mataifa mengi zaidi.
- kuhakikisha kuwa sera za kiuchumi zinaendelea kuangazia maslahi na manufaa ya taifa, na mahitaji ya watu kuambatana na Katiba.
- kuhakikisha kuwa makubaliano ya kibiashara yanayoihusisha Kenya, yanaambatana na Katiba na sheria za nchi sawa na maslahi na maono ya kitaifa.
- Kuhakikisha muingiliano wa uchumi wa Kenya na uchumi wa ulimwengu na kieneo kwa njia iliyo sawa (informed & strategies).
- Kuanzisha mbinu za kusimamia; kuongoza; na ikifaa, kudhibiti uingiaji nchini wa fedha katika kiwango cha kimataifa; hasa ikiwa uingiaji huo unatiliwa shaka.
- Na ya muda mfupi kwa kawaida

*(ii) Kuhusu kuunda mikataba*

a. Katiba inapaswa kuhakikisha kuwa Kenya inafuata mbinu ya kuwili ya kuunda mikataba inayojumuisha jukumu mahsusi la Bunge kama njia ya Bunge kutoa mchango wake au kusimamia uwezo wa kufanya mikataba wa mamlaka makuu.

b. Muda ambao Bunge linapaswa kutumia kufanya mikataba kuwa sheria za nchi kwa manufaa ya Wakenya ambao maslahi yao yamelindwa chini ya kifaa maalum uelezwe wazi.

c. Sheria ya mila za kimataifa inapaswa kutumika nchini Kenya, isipokuwa ikiwa haiambatani na Katiba au sheria za nchi hii.

d. Katiba inapaswa kuweka wazi, katika kuongezea kutaja kwamba sheria ya kimataifa ni moja wapo ya sheria zinazotumika nchini Kenya, kuwa makubaliano ya kimataifa yanayoihusisha Kenya yataunda mfumo ya sheria, zitakazotafakariwa na kutumiwa katika mahakama kote nchini.

e. Mashauriano na kutia saini kwa mikataba litakuwa jukumu la mamlaka makuu (kupitia kwa Rais au wakala wake) kutegemea Katiba.

f. Idhini ya Bunge itafutwe kabla ya mamlaka makuu kuidhinisha mkataba wowote.

g. Idhini ya wanaohusika inapaswa kuwa kupitia wingi wa Bunge kutegemea Katiba.

h. Tofauti iwekwe kati ya mikataba inayojitekeleza yenyewe na ile isiyojitekeleza yenyewe , na kutekelezwa kwa mikataba kuhitajike tu kwa mikataba isiyojitekeleza.

i. Mikataba (kwa upande wa mikataba isiyojitekeleza yenyewe) ambayo imekwishaidhinishwa itajumuishwa katika kundi la sheria za kitaifa na Bunge katika kipindi cha miezi 12 tangu tarehe ya kuidhinishwa

j. Mikataba iliyoundwa kabla ya uhuru kuihusu Kenya iendelee kutekelezwa lakini kwa masharti ya urudishiano (kama ilivyo nchini ufaransa).

k. Bunge laweza kubainisha mikataba itakayokubaliwa na mamlaka makuu na kuidhinishwa na Bunge baada ya kura ya maoni au kupitia njia nyingine zinazohakikisha uidhinishaji wa moja kwa moja wa wananchi zitakazotolewa na Sheria.

l. Katiba inaweza kutoa ibara kuhusu mikataba itakayotambua shughuli mahsusi, kama zile zinazoathiri mipaka ya Kenya ya kimataifa; ile inayoyashirikisha majeshi ya Kenya katika mipango ya kudumisha amani inayohusu kuipa Kenya madeni ya umma kutoka mataifa ya nje.

m. Bunge litaidhinisha mamlaka makuu kuifanya serikali kuwajibika kwa deni la umma kutoka taifa moja hadi jingine, au mataifa mengi.

n. Bunge litaelezea utaratibu wa kuunda ujumbe wa kuiwakilisha Kenya katika mashauriano na makongamano baina ya mataifa mawili, au mataifa mengi.

*ii)* *Kuhusu uhusiano wa kidiplomasia na ule wa kikonsela:*

a. Kenya itatumia mfumo wa uteuzi wa kushirikiana – Rais atateua viongozi wa ujumbe (mabalozi) kupitia idhini ya Bunge

b. Rais anapaswa kupokea wajumbe wa kigeni au viongozi wa jumbe wanaotumwa nchini Kenya.
c. Katiba inapaswa pamoja na mengine kuhakikisha utegemevu katika taaluma na uaminifu kati ya sifa muhimu zinazohitajika ili mtu ateuliwe katika afisi ya umma humu nchini, au ng'ambo kuwahusu wanadiplomasia, au wawakilishi wa nchi ama katika mikutano kati ya mataifa mawili, au mataifa mengi zaidi.
d. Katiba inapaswa kulifanya Bunge kupitisha sheria kuhusu kinga au upendeleo wa aina fulani wa kidiplomasia na kikonsela kuambatana na Katiba huku ikizingatia:-
    - Mapatano ya Vienna kuhusu uhusiano wa kidiplomasia na kikonsela
    - Umoja wa mataifa chini ya mapatano yake kuhusu kinga na upendeleo wa aina fulani
    - Uakala maalum wa Umoja wa Mataifa chini ya mapatano yao kuhusu kinga na upendeleo wa aina fulani.
    - Makubaliano ya mashirika yanashirikisha serikali tofauti
    - Asasi za kifedha za kimataifa
    - Makubaliano kati ya mataifa mawili
    - Sheria pia inapaswa kushughulikia mashirika ya kimataifa yanayohudumu nchini Kenya lakini hayana kinga na upendeleo wa aina fulani wa kidiplomasia na kikonsela
    - Sheria itaeleza kuwa upendeleo, kutoshirikishwa na kinga kama hizo kutategemea Katiba ya Kenya na maslahi ya jumla ya Wakenya, na kuheshimu uhuru wa taifa la Kenya.

*(iii) Kuhusu kutangaza vita na kupeleka majeshi ya Kenya ng'ambo:*

a. Tangazo la vita linapaswa kutolewa na Rais kwa kushauriana na Baraza la Ulinzi na kwa idhini ya bunge kupitia wingi wa kura.

b. Kupelekwa kwa majeshi ya jamhuri nje ya mipaka ya taifa kushiriki katika mipango ya kudumisha amani kutahitaji idhini ya Bunge kupitia wingi dhahiri wa kura.

c. Bunge litafafanua hali ambapo Kenya itapeleka majeshi yake kushiriki katika mipango ya kudumisha amani, vitendo vinavyohitaji kuvuka upande mwingine wa mpaka au vitendo vya kimataifa, ikiwa ni pamoja na swala la utambuzi wa manufaa ya kushiriki katika mipango ya kudumisha amani.

# SURA YA KUMI

# UTAWALA HUSISHI

## 10.1 <u>Agizo</u>

Agizo la Tume chini ya Sheria ya Marekebisho ya Katiba ni kuhakikisha kuwa Katiba:-

- Inahakikisha amani, umoja na uadilifu wa Jamhuri ya Kenya ili kulinda maslahi ya Wakenya;
- Inaanzisha mfumo wa serikali ulio huru na wa kidemokrasia unaojumuisha utawala mwema, Katiba, utawala wa sheria, haki za binandamu na usawa wa jinsia;
- Kuimarisha ushirikishaji wananchi katika utawala wa nchi kupitia uchaguzi wa kidemokrasia, ulio huru na wa haki, na matumizi ya mamlaka;
- Kuimarisha uadilifu na umoja wa kitaifa;
- Inachunguza miundo kadhaa na mifumo kadhaa ya serikali ikiwa ni pamoja na mifumo ya serikali shirikishi na ya umoja, na kupendekeza mfumo unaofaa kutumiwa nchini Kenya;
- Inachunguza na kutoa mapendekezo ya kuimarisha mfumo wa uchaguzi wa Kenya.

## 10.2 Uhusika na Utawala

### 10.2.1 Kanuni za Kijumla

Dhana kuwa ni lazima watu wote kuhusishwa katika utawala na utaratibu wa maendeleo ya taifa ni dhana muhimu sana. Dhana ya watu kuhusishwa katika utawala wao wenyewe kwa hivyo ni moja wapo ya nguzo za jamii ya kijamhuri na kidemokrasia. Kwa hivyo, katika msingi wa ujenzi wa taifa, kuna lengo muhimu la utawala na maendeleo husishi ya

wananchi.  Kupitia uhusika thabiti na kamili, watu hupata haki na wajibu wa kushiriki katika kujadili malengo, maadili, sheria na mipango yao ya kitaifa inayolenga kuendeleza na kuimarisha maslahi yao.

Uhusika kimsingi ni kuwawezesha watu kujihusisha kikweli na ipasavyo katika uundaji wa miundo, mifumo, sera, sheria na mipango inayojali maslahi ya wote; na vilevile kuwawezesha kutekeleza na kuchangia ipasavyo utaratibu wa maendeleo na kugawa sawa manufaa yake.  Kuhusika ni kushiriki.

Uhusika kwa hivyo ni njia ya kuweza kufikia kitu fulani unachokihitaji.  Kama kifaa cha utawala wa kidemokrasia na maendeleo, uhusika hutoa nyenzo ya kujifunga kwenye utaratibu wa maendeleo unaowahusisha wananchi, na hiari ya wananchi kijitolea na kutumia nguvu zao za kijamii kwa utawala na usimamizi wa nchi.   Kuhusika kunahusu:

- Udhibiti – hasa kuamua sera au uamuzi utakaofuatwa;
- Kuhusishwa – kuwa kati ka kundi linalofanya uamuzi;
- Kuathiri – kuathiri kufanya uamuzi;
- Ushauri – kuuliza mtu anachofikiria kuhusu uamuzi unaolekea kufanywa au hatua inayochukuliwa;
- Habari – kufahamishwa kuhusu ukweli, uamuzi unaofanywa na jinsi unavyotekelezwa;
- Kufuatiliza – kuhusika katika kuchunguza na kutathmini jinsi uamuzi unavyotekelezwa, na jinsi taratibu kama uchaguzi zinavyofanya kazi.

Kwa hivyo, kuimarisha uhusika imekuwa mada muhimu katika utaratibu wa marekebisho ya Katiba ikiwa ni pamoja na maoni yaliyotolewa na Wakenya, mashirika ya kiserikali na mashirika yasiyo ya kiserikali na raia kwa jumla.  Kwa kiasi fulani, hali hii imetokana na sababu kwamba raia wamechoshwa na miundo ya serikali na hasa siasa.  Demokrasia ya uwakilishi inafikiriwa na wengi kuwa haijafaulu.  Watu maskini hutambua kuwa asasi za umma ni fisadi, ziko mbali mno na haziwajibiki.

Isitoshe, imetambuliwa kuwa demokrasia ina mazoea ya kujumuisha, pamoja na kutojumuisha. Wanawake na makundi ya walio wachache kila mara hujipata hawajawakilishwa vya kutosha, kwa sababu mbalimbali, kama vile walivyo maskini. Matakwa ya "wengi" ambayo kwa kweli yanaweza kuwa matakwa ya walio wachache yanaweza kukandamiza, kama yalivyo matakwa ya ufalme au kiongozi wa kiimla. Kwa kweli sio majaribio yote ya kuwahusisha watu ambayo hufaulu. Kila mbinu ina wakereketwa wake, wale wanaoishuku na wanaoitatiza. Kuna hatari inayopatikana katika dhana ya uhusika maarufu. Kwa mfano:-

- Nafasi ya kushiriki au kuhusika inaweza kunyakuliwa na wasomi ikiwa haitapangwa vyema;
- Matatizo yanaweza kutokea kwa sababu wale waliounda mbinu za kuhusisha hawafahamu jinsi asasi za humu nchini zinavyofanya kazi. Wakati mwingine, wanaweza kukosa kujua jinsi watu wanavyoitikia, ni nani anayefika mkutanoni na lini;
- Kuna hatari ya kufanywa kwa udanganyifu, kimaksudi; kwa mfano mikutano ya mabaraza ya vijiji nchini India wakati mwingine imekuwa ikifanywa wakati na mahali ambapo haiwezi kuwa na umuhimu wowote;
- Mipango mingi katika uhusishi imekuwa na lengo mahsusi la kuwahusisha wanawake. Hata hivyo, kuwa na kiasi au idadi fulani pekee ya wanawake hakuwezi kutimiza lengo hilo. Maswala yaliyo muhimu katika muingiliano baina ya wanawake na wanaume yanaweza kupuuzwa. Si maswala yote ya kike yanayowahusu 'wanawake pekee'. Wanawake wanaweza kukubali udhaifu au upungufu wa kitamaduni – je ni sawa kuwakataza?
- Kuanzishwa kwa njia za uhusishi kamili, vijijini au katika jamii zilizo na miundo sugu ya kijamii kunaweza kuzua hali ya taharuki katika jamii hiyo;
- Sio kila mtu anayehusika katika shughuli husishi aliye na lengo moja. Mashirika yasiyo ya kiserikali, ya humu nchini na yale ya kigeni, wafadhili wa kigeni, serikali za wilayani, jamii, serikali kuu n.k. vinaweza kutofautiana katika malengo yao. Kunaweza kuwepo na kuletwa kwa dhana za kigeni zisizofaa au dhana zingine zisizofaa kutoka kwingineko nchini au kutoka katika mfumo wa serikali.

Ijapokuwa uhusishi huenda usiwe suluhisho la matatizo yote ya utawala, unachukuliwa kama njia ya kuifanya serikali kuwajibika zaidi, kuifanya kuwa bora zaidi na kujali mahitaji ya umma – na pia kuifanya kuwa ya haki. Kuwepo kwa serikali iliyo thabiti na inayowajibika kunamaanisha kuwa raia watatosheka na kwa hivyo kutakuwa na uthabiti unaotokana na kujitolea badala ya ule unaotokana na kulazimishwa. Ni dhahiri kuwa msingi wa utawala mwema ni kuwahusisha raia. Hii kwa hivyo inamaanisha dhana ya kilimwengu ya siasa ya kuidhinisha, kukubaliana, uwakilishi, kusadiki, kujitolea, huruma na uwajibikaji. Siasa ya makubaliano huwahusisha raia katika utaratibu ambapo sera, sheria na mipango huundwa na kutekelezwa. Inahusu kuwasikiza raia na kuchukua mwelekeo wa uongozi na serikali kwa kuyazingatia mambo haya. Kwa kufanya hivyo, serikali ina nafasi kubwa ya kupata imani na idhini ya walio wengi, ikiwa sio watu wote, kuhusu hatua inazochukua kwa maslahi ya Taifa.

Utawala mwema unahusu usimamizi thabiti na bora wa mfumo wa siasa, mahusiano ya kijamii, rasilmali, kwa manufaa kamili na yanayogawanywa sawa katika jamii. Utawala mwema huunda mbinu kuu ya kuibadili jamii na kuifanya iwe inayowahusisha raia katika maendeleo na kufanya maamuzi. Jukumu lake ni kuweka hali inayofanikisha maendeleo jumuishi. Lengo ni kuwalinda wasiobahatika na walio hatarini katika jamii.

Haja ya kuunda miundo na mifumo ya utawala inayofaa kwa hivyo ni muhimu hasa ikiwa tutaelewa na kutambua hali ambamo malengo ya taifa yanafaa kutimizwa. Kuunda miundo na mifumo inayofanikisha hakuhakikishi tu matumizi thabiti na bora ya rasilmali, bali pia utoaji wa huduma bora, na zinazozingatia mahitaji ya wapokeaji wake kwa kuunda mipaka inayofaa ya utendakazi na majukumu ya miundo, vyombo na viwango kadhaa vya serikali.

### 10.2.2 Utawala Husishi Katika Katiba

Isipokuwa hali ya jumla ya uhuru wa kukutana na kushirikiana, hakuna lolote mahsusi kuhusu utawala husishi katika Katiba iliyopo. Kwa jumla, Katiba ina upungufu kwa upande wa uhusika wa moja kwa moja wa rais katika maswala ya umma.

Kama zilivyo Katiba nyingine za wakati wake, Katiba iliyopo inachukulia kuwa kuhusika kwa raia kunapatikana kupitia kwa utaratibu wa uchaguzi. Kwa hivyo, sehemu za pekee zinazoshughulikia utaratibu husishi wa kidemokrasia ni zile zinazohusu:

- Mipaka ya maeneobunge;
- Majukumu ya Tume ya Uchaguzi (hasa kuwaelimisha wapiga kura);
- Majukumu ya Wabunge maalum kama vile kuwakilisha 'maslahi maalum';
- Rais kuhitajika kuungwa mkono kote nchini katika uchaguzi wa urais; na
- Sehemu kuhusu haki ya kujielezea, kukutana na kushirikiana pia ni muhimu.

Lakini, Katiba haizingatii serikali za wilaya na asasi nyingine zozote kuleta uwajibikaji kwa, au kuhusika kwa wananchi.

### 10.2.3 Utawala Husishi katika Katiba Nyingine

Swala la utawala husishi limepata nafasi kubwa katika Katiba katika kipindi cha miaka michache iliyopita. Mataifa mbali mbali yakiwemo Uingereza, Afrika Kusini, Uganda, Ureno, Madagascar, Ufini na Ethiopia yametoa nafasi ya kuwahusisha raia katika njia mbali mbali.

Ibara 57 (1) ya Katiba ya Afrika Kusini, kwa mfano, imehakikisha kwa Bunge linaweza kuwa na masharti kuhusu shughuli zake:

> *Kwa kuzingatia uwakilishi na utawala husishi, uwajibikaji, uwazi, na kushiriki kwa umma.*

Katiba ya Ghana imehakikisha, hasa Katiba Ibara 35 (6) kuwa serikali itachukua hatua mwafaka.

> *(d) kuifanya demokrasia hali halisi kwa…… kutoa nafasi zote zinazowezekana kwa wananchi ili washiriki katika maamuzi katika viwango vyote wa maisha ya taifa na serikali.*

Katika Ibara 37 (2) Katiba imehakikisha pia kuwa serikali itatunga sheria:

> *za kuimarisha haki ya kushirika ipasavyo katika taratibu za maendeleo, pamoja na…….haki za kufikia mawakala na maafisa wa serikali ili kuhakikisha uhusika madhubuti katika taratibu za maendeleo*.

Kanuni kama hizo zimo katika Katiba za Uganda, Ureno, Madagascar, Ufini, Ethiopia, Brazil na Msumbiji, pamoja na nchi nyingine.

#### 10.2.4 Waliyosema Raia

Maoni ya raia kimukhtasari, yanaweza kuwasilishwa ifuatayo**:-**

*(i) Kuhusu wanawake kwamba:-*

a. wanawake hawawakilishwi ipasavyo katika utawala na kufanya uamuzi
b. wanawake wanachukuliwa kama raia wa kiwango duni kwa kuwa hawawezi kuidhinishwa kusafiri kwenda ng’ambo bila idhini ya waume zao;
c. wanawake hawana nguvu za kimwili na kwa hivyo wahudumiwe kwa njia maalum;
d. imani zingine za kitamaduni na mila zinawabagua wanawake;
e. wanawake walioolewa wanashughulika na masuala ya familia na hawahusiki katika utawala;
f. wanawake wahusike katika utawala kupitia mfumo wa wa nafasi zilizotengea;
g. thuluthi moja ya watumishi wa umma katika maeneo yote wawe wanawake;

h. serikali ifadhili makundi ya wanawake ili kuwafundisha haki zao na majukumu katika utawala;
i. wanawake wapewe nafasi ya asilimia hamsini katika utawala;
j. idara ianzishwe ili kushughulikia masuala ya wanawake;
k. wanawake wasioolewa wasiwakilishe wanawake walioolewa;
l. wanawake wazawadiwe kwa kushiriki katika shughuli za uchumi na siasa.

*(ii)* *Kuhusu walemavu kwamba:*

a. walemavu wanadharauliwa na watu wenye viungo kamili;
b. walemavu hugaguliwa katika uajiri, shule na asasi nyingine;
c. walemavu hawapewi nafasi katika huduma za starehe, usafiri mawasiliano na miundomsingi kwa jumla;
d. walemavu hawawakilishwi ipasavyo katika vyombo vya serikali na sekta ya kibinafsi;
e. walemavu hawana uwezo kifedha kwa sababu ya uwezo wao;
f. walemavu wahimizwe kushiriki kikamilifu katika siasa, jamii na uchumi;
g. walemavu waombwe ushauri na wajumuishwe katika utaratibu wa maaamuzi;
h. mfuko wa msaada uanzishwe kwa manufaa ya walemavu;
i. walemavu wasaidiwe kuunda makundi yua uwakilishi; na
j. Bunge litenge viti kwa walemavu.

*(iii)* *Kuhusu vijana kwamba:*

a. vijana hawana nafasi nzuri katika utawala na hali ndio wengi;
b. vijana hawana fedha kama watu wengine kutetea maslahi yao, k.m. kampeni;
c. vijana wanaweza kuwa raia na viongozi wema;
d. vijana wanawakilishwa na wazee wasiofahamu matatizo yao;
e. viti vitengwe kwa vijana Bungeni;
f. mfumo wa nafasi zilizotengwa utumiwe kuteua watumishi wa umma na vijana wapewe nafasi zao;
g. vijana wanaojitolea kwa uchaguzi wafadhiliwe na wazawadiwe;
h. ujuzi na vipawa vya vijana vitumiwe katika utawala; na

i. vijana wasimamie na wadhibiti mambo yao kwa kuanzisha idara ya vijana katika utawala.

*(iv) Kuhusu makundi waliowachache kwamba:*

a. makundi waliowachache yanapuuzwa katika elimu, afya, na muundomsingi katika maeneo yao;
b. makundi ya walio wachache hayawakilishwi katika utawala na kuwa maswala yao hayashughulikiwi;
c. makundi ya walio wachache yanadhulumiwa na kubaguliwa;
d. makundi ya walio wachache kama vile Wadorobo na Ogiek wanaoishi katika misitu hayapaswi kutatizwa;
e. makundi ya walio wachache yanapaswa kuwakilishwa Bungeni na Serikalini.
f. matiba inapaswa kuyalinda makundi ya walio wachache; na
g. makundi ya walio wachache yanapaswa kushughulikiwa kwa njia maalum kwa upande wa elimu, utoaji wa vifaa vya afya na usaidizi wa kifedha.

*(vi) Kuhusu Wazee*

a. Wazee hawawakilishwi katika utawala;
b. Wazee huumia sana kwa sababu hawana njia za kujipatia fedha;
c. Hali ya kutojua kusoma na kuandika miongoni mwa wazee inashangaza;
d. Watu hawana heshima tena kwa wazee;
e. Wazee wanapaswa kuwakilishwa Bungeni na katika utawala;
f. Hazina ya maslahi na mfumo wa kilimwengu wa usalama wa kijamii unapaswa kunzishwa kushughulikia mahitaji ya wazee; na
g. Katiba inapaswa kuwalinda wazee.

*(vii) Kuhusu makundi*

a. wanataaluma, watu wa dini, wafanyibiashara, wakimbizi, wakulima, wafugaji wa kuhamahama na makundi mengine maalum yanapaswa kujumuishwa katika utawala.
b. viti muhimu vihifadhiwe kwa makundi haya.

### 10.2.5 Uchanganuzi

Katika mawasilisho yao kwa Tume wananchi walitaka kuhusishwa kikamilifu kwenye uongozi wa masuala ya umma na waliomba kuhusishwa katika kutoa uamuzi katika mambo yanayowahusu na kuwaathiri kama vile matumizi ya pesa za umma, usimamizi wa maliasili, uamuzi wa migogoro, kuandaa sheria pamoja na kubadilisha katiba, sera ya kuratibu na kupanga mipango ya maendeleo. Wanataka serikali iwe karibu na wananchi. Wanawahitaji wanawake, vijana, walemavu, waliowachache na makundi ya wanyonge kuhusishwa.

### 10.2.6 Mapendekezo

Kwa hivyo Tume inapendekeza kwamba:

(i) Tume iimarishe umuhimu wa wananchi na asasi zao katika kuendeleza demokrasia na kanuni za ujamhuri, uadilifu na matendo. Serikali iendeleze na kuhimiza waziwazi au vinginevyo kuhusika kwa umma katika kutoa uamuzi na usimamizi wa masuala ya umma katika ngazi zote za serikali.

(ii) Tume itangaze kwamba wananchi wa Kenya wana haki ya kushiriki kwenye utatuzi wa matatizo ya Taifa, moja kwa moja au vinginevyo kupitia kwa wawakilishi waliochaguliwa kwa haki. Kila raia mwenye umri wa kupiga kura ana haki kushiriki katika siasa au harakati za kuhamasisha vyama na sera za serikali.

(iii) Serikali kila wakati ihimize ushiriki wa wananchi katika uratibu, uangalizi, tathmini ya viwango vya sera na mipango ya maendeleo kitaifa na kiwilaya na pia iwe na wajibu wa kuunga mkono hamasa za wananchi katika jitihada za maendeleo.

(iv) Mamlaka ya umma yataendeleza nafasi ya kila mmoja na jumuia ili kushiriki katika harakati za jamii kuhamasisha katika kutoa uamuzi unaowaathiri.

(v) Taifa libuni vyombo maalum kuhakikisha uwajibikaji wa serikali katika ngazi zote na kuwapa wananchi nafasi za kushiriki kikamilifu katika kusimamia taifa.

(vi) Ushiriki wa moja kwa moja wa raia katika usimamizi wa masuala ya jamii utalindwa na kufanywa kwa kura ya maoni, uchaguzi wa maoni na njia nyinginezo zilizofafanuliwa katika sheria.

(vii) Katiba itoe katika asasi za umma wajibu wa kuwashauri wananchi na kila ripoti ya asasi hizo zieleze ikiwa ushauri wa umma umekubalika.

(viii) Wananchi wahusike katika ushiriki wa kawaida na unaoeleweka katika utawala wa haki kupitia asasi za umma na mahakama maalum ya kimila na baraza la wazee, pamoja na mifumo ya washauri. Serikali ichukue hatua muhimu kuimarisha haki za raia kuenda mahakamani, kuwawakilisha marafiki katika mijadala ya mahakamani, kukabiliana na asasi za umma ili zitoe haki n.k.

(ix) Kila raia ana haki ya kutoa, kibinafsi au kwa kushirikiana na wengine, malalamiko, mawasilisho, madai, na manung'uniko kwa viungo vya mamlaka ya juu au mamlaka yoyote kwa nia ya kuhami haki zao, katiba, sheria au maslahi ya jumla ya jamii na kufahamishwa matokeo kwa mujibu wa sheria.

(x) Serikali iendeleze na kulinda maslahi na haki sawa za wanawake, vijana, walemavu, wazee, mayatima, wajane, mafukara, watoto na waliowachache

ili kuhakikisha kikamilifu na sawasawa kushiriki kwao katika siasa, uchumi na juhudi za maendeleo; pamoja na kufikia huduma na maslahi ya kijamii na kiuchumi.

(xi) Kukabidhi madaraka au aina yoyote ya usawazishaji unaohitajika na katiba ni sharti kuwe na matokeo yanayokubalika kwa kushiriki katika viwango vyote vya uongozi.

(xii) Katiba ieleze kuwa Bunge litatekeleza sheria itakayotoa nafasi ya uongozi wa kitamaduni, sheria za mila na desturi za jamii, kuunda baraza la viongozi wa kitamaduni na masharti yoyote yatakayoonekana yanafaa.

(xiii) Katiba itataka Bunge kuunda vyombo ambavyo vitawezesha:

(a) na kuhimiza wananchi au raia kujadili miswada ya sheria; kuhamasisha mabadiliko na ubunifu wa miswada ya sheria; kutoa malamiko bungeni kwa utungaji wa sheria; kuombwa kufika mbele ya kamati ya Bunge au kuchunguza matukio maalum ya kitaifa au yanayohusu umma; kufikia mtu binafsi au kupitia mapendekezo ya kisheria ya makundi ya kijamii.

(b) kamati za Bunge kuitisha mikutano ya hadhara na kushauriana pia kutafuta msaada wa kiufundi kutoka kwa wataalam wa kutoa ushauri zikiwamo asasi za utafiti; na

(xiv) Katiba ibuni vyombo vya kuwezesha na kuwahimiza watu kudadisi utekelezaji wa wawakilishi waliochaguliwa na kuwaondoa ikiwa utendaji wao wa kazi haufikii kiwango kinachofaa.

## 10.3 Mtindo na Shughuli za Uchaguzi

### 10.3.1 Kanuni za Msingi

Msingi wa utawala wa ushirikiano ni kufanya uchaguzi huru, wa haki na wa mara kwa mara. Uchaguzi hautumiki tu kuwachagua wawakilishi wa watu bali pia kupata au kuamua uchaguzi au uteuzi wa serikali. Wanadhihirisha uhuru wa wananchi na kuwajibika kwa wanasiasa kwa raia. Wanaongoza kwa hiari au muundo wa serikali unaowapa uhalali. Ili haya yatendeke baadhi ya masharti lazima yawepo. Hayo ni pamoja na makubaliano kuhusu mtindo wa uchaguzi utakaotumika, migawanyo sawa ya mipaka ya maeneobunge, na usimamizi wa uchaguzi ulio wazi.

***(a) Mtindo wa uchaguzi***

Mtindo wa uchaguzi hapa humaanisha mbinu inayotumika kuamua jinsi kura zilizopigwa kwenye uchaguzi zitakavyobadilishwa kwenye viti ambavyo vyama au wagombea walijishindia. Kwa hiyo, mtindo wa uchaguzi inatokana na upatanishi kati ya kura na uwakilishi jinsi ulivyobuniwa na sheria ya uchaguzi. Kwa upande mwingine mtindo wa uchaguzi hurejelea usimamizi na utawala wa uchaguzi na mtindo wa uchaguzi.

Yafuatayo ndiyo muhimu katika uthabiti wa mtindo wa uchaguzi:

- Mtindo wa uchaguzi lazima ueleweke vizuri kwa wapigakura, endapo utahamasisha vilivyo na ushiriki wa maana wa wananchi katika sera za uchaguzi. Mtindo wa uchaguzi unaotatiza unaweza kuwanyima haki wapiga kura wengi wenye uwezo hasa wasiojua kusoma na kuandika.
- Pendekezo la mtindo wa uchaguzi lazima lizingatie gharama ya mtindo wenyewe. Gharama ya kutumia aina fulani ya mtindo wa uchaguzi inaweza kuwa ghali sama kuzidi uwezo wa nchi ha huenda ukatumbikiza mtindo wote wa uchaguzi na utaratibu katika ghasia.

- Mtindo wa uchaguzi pia lazima uzingatie tofauti ya mtindo wa nchi kisiasa na kihistoria, kijamii na umbo kijografia, wingi wa makabila na maeneo yao, kielimu, kitamaduni, madhehebu ya dini muundo wa ushirika wa jamii na muungano, uchumi na vinginevyo katika msingi wake na utekelezaji.

Katika kuunda mtindo wa uchaguzi, vitu kama historia ya nchi kisiasa, nguvu za kijamii zinazotumika kama vile madhehebu ya kikabila na kidini, uimara wa harakati za kijamii kama wafanyikazi, mashirika yasiyo ya kiserikali n.k. kiwango cha siasa na/au mwamko wa kijamii, kufikia kiwango cha ujuzi wao kijiografia, muungano wa kidini, na kiwango cha maendeleo kiuchumi na kiteknolojia ni muhimu kati ya mambo mengine.

Mitindo ya uchaguzi hutofautiana. Inayojulikana sana ni pamoja na:

(a) Mtindo wa waliowengi, ambao pia hujulikana kama Atanguliaye Hupata au Mshindi Huchukua Yote, hutumika nchini Kenya kwa sasa. Mtindo huu wa uchaguzi ni mmoja ambao kwao, mgombea anayepata kura za juu zaidi zilizopigwa kwenye uchaguzi akilinganishwa na mshindani/washindani wake, hutangazwa mshindi na huwa mwakilishi wa eneobunge. Mshindi huhitajika tu kupata kura za juu wala si lazima waliowengi wote. Huitwa Atanguliaye Hupata Nafasi kwa sababu ni mgombea mmoja tu anayeweza kutangazwa mshindi. Mtindo huo una tofauti nyingi kulingana na mbinu zinazotumika kuamua mshindi.

(b) Mtindo wa kiwango cha uwakilishi ambacho kwacho viti vya bunge vimepangwa vinalingana na kura zilizopigiwa chama kinachoshinda viti katika baraza la kutunga sheria. Dhana ya mtindo kama huo kwa eneobunge na bunge ni kuhakikisha kuwa matokeo yanaonyesha kwa karibu matumaini ya wapigakura. Kanuni za msingi zinazotegemeza mtindo wote ni kuwa chama kipate viti kulingana na mgawo wake wa kura zote. Kwa mfano, kwenye ngazi ya eneobunge, kutakuwa na wabunge kadhaa kutoka kila eneobunge. Kwa hivyo, chama kikishinda asilimia kumi (10%) ya kura

zilizopigwa kwenye uchaguzi wa bunge la viti mia moja (100), chama hicho kitapewa viti kumi (10). Au kama kuna wabunge watano (5) kutoka eneobunge, kikiwa chama kimeshinda asilimia arobaini (40%) za kura, chama hicho hupata asilimia arobaini (40%) ya viti ambavyo vitatengwa kwa wagombea wawili wa kwanza katika orodha ya eneobunge. Katika ngazi ya kitaifa, kwa hivyo, muundo wa bunge pia utalingana na uungwaji mkono wa kitaifa kutoka katika vyama mbalimbali. Chama kingine kikishinda asilimia moja (1%) ya kura, chama kitapewa kiti kimoja tu. Tofauti inayotumiwa sana ya uwiano wa uwakilishi wa Orodha ya chama ambayo kwayo kura hupigwa kwa ajili ya chama badala ya mgombea na vyama hivyo hupata viti vya bungeni kulingana na mgawo wa kura zote za kitaifa. Kwa hivyo, kila chama kinachotaka kushiriki katika uchaguzi hupanga orodha ya wagombea wake hadi kufikia idadi ya viti vitakavyojazwa. Majina ya orodha yenyewe hupangwa kulingana na kipaumbele. Chama kikishinda viti vitano tu, basi wagombea watano wa kwanza wa chama katika orodha huwa wawakilishi wa chama katika bunge. Kwenye mtindo huu, vyombo vya chama huandika orodha kutoka miongoni mwa wanachama na chama hakina budi kubuni kigezo cha kuchagua wagombea na mfululizo ambavyo watatokeza kwenye orodha ya chama.

Mtindo mwema wa uchaguzi unapaswa kuhakikisha au kuendeleza uwakilishi wa wananchi na maslahi ya wote waliowengi katika mtindo wa kisiasa. Mtindo wa uchaguzi unaotumika katika mfumo wa umma unafaa kuwa wa kujumuisha kadri inavyowezekana kwa kuuwezesha kuwakilisha wenye maslahi na nia tofauti kwa wingi itakavyowezekana. Kutambua maslahi haya ni muhimu ili kuhakikisha kwamba hakuna mtu ambaye maslahi yake yamemilikiwa na kikundi fulani, kwani hiyo itakuwa si demokrasia na ni kutowakilishwa. Katika mfumo wa serikali iliyo huru kama Kenya vyama vya kisiasa vinatoa maelekezo ambayo kwayo makundi tofauti ya uraia na misimamo yanaelekezwa na kushindana kuwakilishwa katika bunge nchini kwa jinsi hii, mtindo wa uchaguzi unaweza kuamua ni

aina gani za vyama vya kisiasa vimeundwa. Kwenye asasi ambako pengine vyama havitatoa mkondo unaofaa kwa maslahi ya mkusanyiko kama vile katika msingi wa kidini, kikazi, kijinsia n.k., mtindo wa uchaguzi uboreshe uwakilishi wao kwa njia ya usawazishaji. Kwa jinsi hii, mbinu za kuchagua wawakilishi utakuwa si wa moja kwa moja kwa mfano kwa njia ya kupendekeza.

Kwa jumla, majukumu makuu ya mtindo wa uchaguzi ni pamoja na:

- Kuendeleza na kuhakikisha uwakilishi imara wa wananchi katika Bunge na viungo vingine vya usimamizi na uamuzi;
- Usajili wa maoni ya watu;
- Chaguo na uundaji wa serikali;
- Masharti ya vyombo vya kudhibiti wawakilishi wa umma na kuwajibika kwa serikali;
- Kuwapatia wananchi chaguo kuhusu sera za umma, mipango na utaratibu; na
- Kuendeleza na kuboresha ushindani wa kisiasa na mtindo wa chama.

Mtindo wa uchaguzi nchini Kenya, hata hivyo hauonekani kutimiza zaidi majukumu haya. Kuna wasiwasi kama kweli mfumo wa uchaguzi nchini Kenya, au unavyoshughulikiwa, unatoa mfumo huru ambako vyama vyote na wagombea wote wana nafasi sawa kuchaguliwa. Matatizo makubwa ya mtindo wa sasa ni:-

- Ukosefu wa uwiano – Rais na chama tawala huenda wakapata kura za waliowachache kwenye uchaguzi; kuna udhia fulani kuwa mtu anaweza kuchaguliwa kuwa Rais ambapo Wakenya waliowengi hawakumpigia kura;
- Vyama vinaungwa mkono katika maeneo fulani maalum kijiografia; mgombea wa chama kilicho katika eneo ambalo chama chake kinajitokeza sana huwa na hakika ya kushinda katika uchaguzi. Kwa hivyo nchi imegawanyika kati ya vyama – ni kama migawanyiko kiuchaguzi. Hutokea fikra kuwa kila sehemu ya

nchi imehifadhiwa kwa ajili ya vyama fulani na vyama vishindani hukabiliana na vizuizi, pamoja na vitisho, vinapofanya kampeni katika sehemu hizo;

- Wazo hili "maeneo salama" au "viti salama" maana yake ni kwamba vyama havijibiidishi hushinda katika maeneo yanayotambulika kuwa yana vyama vyenye ushindani mkali; watu wa sehemu hizo hawana uchaguzi wa haki kati ya wagombeaji;
- Mtindo wa "Aliyefika Kwanza - Ndiye Mshindi" ni mbaya na wa kiadui ambapo wagombea au vyama vyao havina motisha ya kushirikiana;
- Kimsingi upigaji kura umekuwa wa kikabila, ingawa hili si jambo pekee linalodhihiri; aidha hii imedhihirika katika asili ya uanachama – kwa mfano, mnamo mwaka wa 1997 kwenye maeneobunge, wapigakura waliwapigia kura hasa wagombezi wa kijamii, katika msingi wake wa ushirikiano wa kikabila, lakini katika uchaguzi wa urais, waliwapa kura chache kiongozi wa chama cha mgombeaji ambaye alikuwa ni wa kabila tofauti na jamii ya mgombea ubunge. Ushindani kati ya wagombezi umekuwa sasa ni mashindano miongoni mwa makundi ya kikabila ilhali ni muhimu kwa muungano wa kitaifa na uadilifu wa kujiondoa, kutoka katika upigaji kura wa kikabila;
- Kutamalaki kwa ukabila kunamaanisha kuwa masuala ya kijamii au kiuchumi hutokeza kwa nadra katika kampeini za uchaguzi. Kwa hivyo, wapigakura huelezwa machache sana kuhusu masuala haya licha ya kuwa wao ni muhimu kuliko maisha yao ya kikabila;
- Kenya ina vyama vingi vya kisiasa visivyofaa kwa uchaguzi na siasa za nchini licha ya kwamba vingi si imara, na hivi karibuni kumezuka mitindo ya kuelekea kuunganisha vyama. Hata hivyo, kuna mengi ya kufanya kuhusu uchaguzi wa Urais zaidi ya uungwaji mkono katika maeneobunge;
- Vyama vya hongo na malezi vimeenea. Kuungwa mkono kwa wagombezi na vyama hutegemea zaidi uwezo wao wa kitu wanachokitoa kwa manufaa ya mtu binafsi kuliko ahadi zao au uwezo wa kunufaisha nchi;
- Kuna jambo la kuzingatia sasa kuhusu tabia ya kuchezea ama kubadili mipaka ya maeneobunge, yenye alama tofauti za idadi ya wapigakura wa maenobunge

hayo, katika kukiuka kanuni za kimsingi za usawa wa haki za kupiga kura – mtu mmoja kura moja, thamani moja;

- Mtindo huu unahasiri vyama vidogo na vipya ambavyo vingewasilisha nia zao bila kuzingatiwa na vyama vikubwa;
- Kuna malalamishi mengi kuhusiana na hali ya kutoridhisha ya usajili wa wapigakura, inayowaacha wazalendo wenye haki bila kura;
- Mara nyingine wagombezi wanaotoka kuwasilisha karatasi zao za uteuzi wanawekewa vizuizi njiani;
- Yamekuwepo malalamiko kuhusu udanganyifu wakati wa uchaguzi;
- Wakati mwingine watu hutumia fursa ya uchaguzi kuzusha ghasia na uhasama miongoni mwa makabila, unyanyasaji unaotekelezwa na utawala wa mkoa, maafisa wengine, majeshi ya kibinafsi, ubadilishwaji wa mipaka ya maeneo ya uchaguzi na mambo mengine yanayohusu mipango ya uchaguzi kama vile udanganyifu na ufisadi;
- Mfumo wa uchaguzi una mwelekeo wa kuhimiza mizozo miongoni mwa chama na vyama mbalimbali kwani kila chama na mgombezi wake hufanya lolote kadiri ya uwezo walio nao; hii ikiwa ni pamoja na kuzusha ghasia na matukio mengine yasiyokubalika kisheria, kama vile kutoa hongo kwa dhamira ya kupigiwa kura. Vyama havipendi mfumo wa uchaguzi kuambatana na harakati za kutafuta kuungwa mkono na kabila au jamii fulani na hivyo basi kusababisha vita vya kikabila wakati wa uchaguzi; na
- Malalamiko mengine yaliyotolewa kuhusu mfumo wa sasa wa uchaguzi ni kwamba mfumo huo unatoa uwezo sawa kwa wapigakura bila kutathmini ubora wa kila kiwango cha mgombezi pamoja na vyama.

Hivyo basi, mbali na kuimarisha demokrasia, mfumo wa uchaguzi nchini Kenya huunyima utekelezaji wa demokrasia kwani shughuli ya upigaji kura imefinywa mno. Mbali na kuhimiza umoja na ushirikiano, unaleta mgawanyiko miongoni mwa wananchi hususan katika misingi ya kikabila na makundi mbalimbali ya kidini.

***(b) Utaratibu wa uchaguzi***

Utaratibu wa kufanya uchaguzi unajumuisha shughuli zote zilizoratibiwa kuhakikisha kwamba jukumu la Tume ya Uchaguzi linatekelezwa kwa njia itakayoonyesha wazi kwamba matakwa ya wananchi yanazingatiwa.

Vipengele vya utaratibu huo ni kama vifuatavyo;

- haki ya kupiga kura na kugombea kiti uchaguzini;
- uorodheshaji wa majina ya wapiga kura;
- uteuzi wa wagombezi viti;
- muda wa kufanya uchaguzi;
- kuifahamu mipango ya upigaji kura;
- sheria za uchaguzi ili kuhakikisha kwamba unafanywa kwa njia huru na ya haki;
- kampeini za uchaguzi na kusimamia gharama za uchaguzi;
- mfumo wa upigaji kura na kuzihesabu baada ya shughuli hiyo kumalizika;
- usimamizi wa mienendo ya vyama na hatua za kuvingo'a uchaguzini au kutoa adhabu kwa wagombezi au vyama husika;
- upokezaji mamlaka ya afisini kwa njia bora na ya kistaarabu;
- mfumo wa kusuluhisha migogoro ya uchaguzi; na
- usimamizi wa uchaguzi.

***(c) Uwekaji mipaka ya maeneo ya uchaguzi***

Uwekaji mipaka ya maeneobunge na maeneo mengine ya uchaguzi ili utoe fursa ya kuandaliwa kwa uchaguzi huru na wa haki ilmradi uchaguzi ufanywe katika eneobunge husika.

Maeneobunge 117 ya kwanza yalibuniwa mwaka 1963 kutokana na mapendekezo yaliyotolewa kwenye ripoti ya Tume ya Kuthibiti na Kurekebisha Idadi za Maeneobunge. Haya yalifanywa kuwa sheria na sheria za Bunge la Kenya mwaka wa 1963 na kufuatiliwa na marekebisho kwenye sheria za mwaka 1963 za (Uchaguzi) (Marekebisho ya sheria) Mapendekezo ya mwaka 1963.

Katiba iliyokuwepo punde baada ya uhuru ilipobadilishwa kati ya miaka ya 1965 na 1966, vyama vilivyokuwepo wakati huo vilikubaliana kuyabuni maeneobunge mapya kwa wanachama wa Bunge la seneta ambalo lilikuwa linapaswa kuvunjiliwa mbali. Maeneobunge haya yalibuniwa kuambatana na Katiba ya Kenya ya (Marekebisho) (Nambari 4) ya mwaka 1966 – sehemu ya 6 Nyongeza ya Tatu ambayo ilizigatiwa na Tume ya Uchaguzi kwenye arifa ya kisheria nambari 344 ya 19.12.66.

Mnamo mwaka 1996, yalikuwepo maeneobunge 188 na bunge liliiagiza Tume ya Uchaguzi kuyabuni maeneobunge ambayo hadi sasa ni 210. Idadi za wapigakura katika maeneo inahitilafiana sana, kuanzia chini ya watu 4000 huko Mandera na kufikia watu 113,848 walioko eneobunge la Embakasi hapa jijini Nairobi. (Tarakimu za mwaka 1997). Wananchi wengi wanaamini kwamba idadi za maeneobunge katika sehemu za miji zinastahili kuongezwa. Jiji la Nairobi lililo na asilimia 10 ya idadi ya watu wote wa Kenya lina asilimia 3.8 ya viti vyote bungeni. Ni wazi kwamba maelekezo mwafaka yanafaa kufahamishwa Tume ya Uchaguzi kuhusu suala hili.

***(d) Usimamizi wa uchaguzi***

Tume ya Uchaguzi ndiyo yenye mamlaka ya kuzisimamia shughuli zote za uchaguzi nchini Kenya. Ina jukumu la kuandaa uchaguzi (Ibara 42A, ibara ya 7A ya Sheria za Uchaguzi wa Ubunge na Urais). Katiba inaeleza kwamba Tume ya Uchaguzi haina budi kuwa na wanachama wasiopungua wanne wala kuzidi ishirini na wawili, walioteuliwa na rais; wanachama wa sasa ni 22. Ili kuhakikisha uhuru wake, wanachama hawawezi kuwa wabunge, wafanyikazi wa umma au wanaohudumu jeshini. Uhuru wa Tume pia huhakikishwa kwa kuwepo na mtindo maalum wa kuwaachisha kazi wanachama wake. Katiba inaeleza; katika utekelezaji wa kazi yake chini ya Katiba hii Tume haistahili kushauriwa kwa vyovyote vile na mtu au shirika lolote. (Ibara ya 42 (9).

Majukumu ya Tume ya Uchaguzi ni:

- kuamua kuyagawanya maeneobunge nchini Kenya (kulingana na idadi maalum iliyopendekezwa na Bunge);
- kuamua mipaka ya maeneobunge;

- kuwasajili wapigakura, kuweka pamoja na kurekekibisha orodha za wapigakura;
- kushauri na kusimamia uchaguzi wa raia wa urais, ubunge na ule wa mabaraza ya wilaya;
- kuhimiza kuwepo kwa uchaguzi huru na wa haki; na
- kuwaelemisha wapigakura kote nchini Kenya kuhusu umuhimu wa shughuli hiyo.

Kwa bahati mbaya, Tume ya Uchaguzi haina sifa nzuri miongoni mwa vyama vya kisiasa au mashirika ya umma. Haionekani kama ni Tume iliyohuru na isiyo na mapendeleo. Sababu muhimu ya kufikia uamuzi huo ni kwamba Tume hii huteuliwa na Rais, bila maagizo yoyote ya kuzingatiwa au kutafuta ushauri wa mtu au shirika lolote. Katika hali kama hii, pendekezo kwamba Tume hii haifai kuwa katika hali ya kushauriwa na mtu au shirika fulani haitoshi kuiondoa tashwishi kuhusu uhuru wake.

Ingawa Tume ya Uchaguzi inaonekana kuwa na uwezo na mamlaka ya kuhakikisha kwamba uchaguzi huru na wa haki umefanywa – Sehemu ya 42 (A) (c) ya katiba, Sehemu 3 (3), 17, 17 (A), na 34 (A) (5) ya Bunge na sheria ya uchaguzi wa urais, inadai kwamba haina uwezo kwa sababu zifuatazo:

- haipo idara huru ya Polisi ambayo imebuniwa chini ya usimamizi wa Tume ya Uchaguzi;
- Mashtaka dhidi ya Tume yanaweza kutwalika ua kusitishwa na Mwanasheria Mkuu chini ya sehemu ya 26 ya Katiba; na
- Uwezo wake chini ya aya za 8 na 9 za Maadili ya Sheria za Uchaguzi unaweza kurekebishwa au unategemea maagizo ya mahakama - hivyo basi uwezekano wa kuingilia kati haupo.

Si madai yote ya Tume ya Uchaguzi yanayokubalika, (kwa mfano, kitengo cha kuchunguza kampeini za uchaguzi, hotuba za wagombezi, wafuasi wao na wagombezi pamoja na matendo yao ya ukiukaji wa Sheria).

Lakini ipo haja ya kuipatia Tume mamlaka zaidi ili iweze kudumisha sheria na maagizo mengine yaliyowekwa kuhakikisha uchaguzi wafanywa kwa njia huru na ya haki. Jukumu la utekelezaji sheria inayohusu uwajibikaji inapaswa kuwa ile ya Tume ya Uchaguzi. Tume yenyewe imeomba ipatiwe uwezo wa kupambana na aina yoyote ya uvunjaji mwingine wa sheria za uchaguzi ili iweze kusuluhisha mizozo ambayo sababu zake hazijionyeshi waziwazi na pia ambazo ni vigumu kushtumiwa lakini suluhisho lake au hatima yake itasawazisha utekelezaji wa kuwepo na uhuru na pamoja na utendaji (sheria ya Uganda ikinukuliwa, Ibara 65 (f)) ambayo inaipa uwezo *kuyabainisha manung'uniko yanayotokea kabla na baada ya upigaji kura kumalizika.* Hakuna rufani kutoka kwenye maamuzi yaliyoafikiwa itakayokubailwa isipokuwa kama sehemu ya upingaji wa uchaguzi baada ya shughuli yenyewe kukamilika.

Tume ya Uchaguzi huenda ikahitaji kuchukua jukumu la msajili wa vyama la kuviorodhesha na kuvitoa orodhani majina ya vyama vya kisiasa - sheria inamruhusu msajili kukiandikisha chama chochote cha kisiasa hata kama hakina wafuasi mbali na hao wasajili wake wenyewe (suala hili limezungumziwa katika sehemu inayovihusu vyama vya kisiasa).

### 10.3.3 Utaratibu wa uchaguzi jinsi unavyoendeshwa katika Katiba ya sasa

Hapa Kenya haki ya kupiga kura imezingatiwa katika sheria ya bunge ibara ya 32 (2). Haki hiyo imepewa tu mtu ambaye amesajiliwa katika eneo la uwakilishibunge kama mpigakura katika eneo la uwakilishibunge kama mpigakura katika uchaguzi wa wanachama walioteuliwa Ibara ya 43 (a). Mtu huyo pia lazima awe anaishi nchini Kenya kwa muda usiopungua mwaka mmoja kabla ya kujiandikisha au kwa miaka minne katika muda wa miaka minane iliyopita (Ibara ya 43 (b) na lazima awe mkazi ua mwenye uhusiano mwingine wowote na uwakilishibunge ambao anataka asajiliwe kuwa mpigakura (Ibara ya 43 (c)).

Katiba imehakikisha kwamba "katika muda usiopungua miaka minane wala kuzidi miaka kumi, na inapoamriwa na Sheria za Bunge, Tume ya Uchaguzi itaifanyia marekebisho

idadi, mipaka na majina ya maeneobunge ya humu nchini na inaweza kwa agizo, kukubali idadi, mipaka au majina, kulingana na sehemu hii, hadi kufikia kiwango cha kuridhisha walivyokusudia kurekebisha".

Maelezo zaidi kuhusu uchaguzi unavyoendeshwa kutolewa katika Sheria ya Uchaguzi wa Ubunge na Urais (Sura 7).

### 10.3.3 Mfumo wa Uchaguzi na Utaratibu katika Katiba Nyingine

Ijapokuwa kanuni kuhusu utaratibu wa uchaguzi, pamoja na mbinu za kuweka mipaka na kusimamia uchaguzi kwa kawaida hupatikana katika sheria za kawaida za nchi, Katiba nyingi zimeanza kuhakikisha vitu hivi katika ibara zinazoshughulikia uwakilishi kwa jumla au, hasa, uchaguzi wa wawakilishi katika vyombo vya uwakilishi. Kwa mfano, Sura ya Tano ya Katiba ya Uganda imehakikisha, pamoja na mengine, haki ya kupiga kura, uanzishaji wa Tume huru ya uchaguzi, mipaka ya maeneobunge, na mfumo wa kupiga kura. Kuhusu mfumo wa uchaguzi, ibara 66 (1) ya Katiba ya Tanzania imehakikisha, kwa mfano, kwamba:

Kutakuwa na viwango vifuatavyo vya Wabunge:

(a) Wabunge waliochaguliwa kuwakilisha maeneobunge;
(b) Wabunge wanawake wasiopungua asilimia kumi na tano (15%) ya wabunge waliotajwa katika aya (a), (c) na (d) waliochaguliwa na vyama vya kisiasa vilivyowakilishwa Bungeni. Kwa msingi wa uwiano wa wanachama miongoni mwa vyama;
(c) Wabunge watano waliochaguliwa na Ukumbi wa Wawakilishi (k.m Bunge la Zanzibar) miongoni mwa wanachama wake; na
(d) Mwanasheria Mkuu, Rais na Makamu wa Rais hawatakuwa Wabunge.

Sura ya Sita ya Katiba ya Visiwa vya Fiji imetoa kanuni nyingi, pamoja na, zinazohusu ugawaji wa viti vya uchaguzi miongoni mwa maeneo ya uchaguzi, mipaka ya uchaguzi inayowekwa na Tume ya mipaka ya uchaguzi inayowekwa na Tume ya Mipaka ya maeneobunge, kupiga kura na mambo mengine, kuteua wagombea uchaguzi na waliomo

katika ukumbi wa wawakilishi na Seneti. Kanuni kama hizo zimo katika Katiba za Nigeria, Ghana na hizo zimo katika Katiba za Nigeria, Ghana na Afrika Kusini, pamoja na nchi nyingine. Kanuni hizi pia hulipa Bunge nguvu ili liweze kutunga sheria kuhusu masuala haya.

### 10.3.2 Yaliyosemwa na wananchi

Tume ya Uchaguzi ilipokea maoni mengi kuhusu utaratibu wa uchaguzi kutoka kwa wananchi.

Wengi wao waliyatoa maoni yafuatayo:

(i) *Kuhusu uwakilishi kwamba;*

(a) Utaratibu wa uchaguzi unaotumika sasa udumishwe;
(b) Ipo haja ya kuongeza idadi ya uwakilishi Bungeni, katika serikali za wilaya na makundi kama ya; wanawake, walemavu, makabila yenye idadi ndogo ya watu, vijana na makundi mengine nyeti;
(c) Vikundi maalum kama hivyo havina budi kutengewa viti vya uwakilishi kuanzia kiwango cha thuluthi hadi kufikia asilimia arobaini hasa kwa wanawake katika Bunge na serikali za wilaya;
(d) Teknolojia ya tarakilishi yaani kompyuta yafaa idumishwe kwenye utaratibu wa uchaguzi;
(e) Walemavu wanabaguliwa katika utaratibu wa sasa wa uchaguzi wa wabunge na ule wa madiwani na hivyo basi ipo haja maalum wao kutambuliwa na kuwakilishwa ipasavyo;
(f) Vijana hawana budi kuwakilishwa kikamilifu katika viwango vyote vya kufanyia maamuzi ikiwa ni pamoja na uwakilishi Bungeni na katika mabaraza ya wilaya;
(g) Uteuzi wa wabunge maalum ufutiliwe mbali;
(h) Uchaguzi ufanywe kila mara katika tarehe iliyotengwa.

*(ii)* *Kuhusu upigaji kura, kwamba:*

(a) Mfumo wa sasa unaohusisha haki ya kupiga kura na upataji wa kitambulisho cha kitaifa na kadi ya kupigia kura ufutiliwe mbali;

(b) Kadi za kupiga kura na vitambulisho vya kitaifa vitolewe wakati mmoja na kila mara wala si katika vipindi fulani tu au upande mmoja wa kitambulisho cha kitaifa utumiwe kama kadi ya kupigia kura;

(c) Wanawake wanaoolewa kabla ya kupata vitambulisho vya kitaifa na wanaokumbwa na ugumu wa kuyabadilisha majina yao ndio wanaothiriwa mno pamoja na wale waliotakiwa na hivyo basi kupata ugumu wa kuyabadilisha majina yao ili waendelee kuyatumia yale ya awali;

(d) Vijana ambao punde tu wametimiza umri wa utu uzima pia wanatengwa katika shughuli ya upigaji kura kwa sababu ya kushindwa kujipatia vitambulisho vya kitaifa;

(e) Mtindo wa kuchunguza kadi za wapigakura kutoka jamii ya Wasomali, uliolalamikiwa, ni kigezo ambacho hakiwawezeshi kutumia haki zao za kupiga kura na utendaji kazi;

(f) Haki za upigaji kura na makazi zinapashwa kutenganishwa kwa sababu aghalabu wananchi wengi wamelalamika kwamba siku ya upigaji kura huwakuta hawako katika sehemu walikojiandikisha kupiga kura. Haya ni matatizo yanayozikumba jamii nyingi za wafugaji wanaohamahama;

(g) Masanduku ya kupiga kura yanapaswa kuwa yale yanayoonyesha ndani moja kwa moja;

*(iii)* *Kuhusu kuruhusiwa kupiga kura;*

(a) Wagombezi wanaojitegemea wanapaswa kuruhusiwa kushiriki katika uchaguzi;

(b) Wananchi ambao wamethibitishwa kuwa na sifa njema za uongozi ndio pekee wanaofaa kugombea uchaguzi; sifa hii ikihusisha umri, utaalamu, uadilifu, na jinsia;

(c) Inafaa kuwe na viwango maalum vya umri wa chini au juu zaidi kwa nyadhifa mbalimbali;

(d) Umri wa chini zaidi kwa yule anayegombea wadhifa wa Urais unafaa kuongezwa kutoka miaka 35 hadi miaka 40 na ule wa juu zaidi kwa yule anayeshikilia wadhifa huo uwe kati ya miaka 70 na 75;
(e) Yafaa kuwe na viwango maalum vya elimu ya chini zaidi kwa nyadhifa mbalimbali;
(f) Elimu ya chini zaidi kwa yule anayegombea wadhifa wa Urais inafaa kuwa shahada ya chuo kikuu;
(g) Yule anayewania kiti cha Ubunge anafaa kuwa na hati ya elimu ya shule ya upili au shahada ya chuo kikuu;
(h) Kwa madiwani viwango vya elimu huenda vikatofautiana kati ya kiwango cha chini darasa la nane na kile cha juu cheti cha mtihani wa elimu ya shule ya upili;
(i) Wanawake wasihusishwe katika viwango hivyo vya elimu kwani wametengwa kuhusiana na masuala ya kielimu katika sehemu mbalimbali nchini na huenda wasivifikie;
(j) Viongozi wanapasa kuwa waadilifu. Kutokana na hayo mapendekezo yalitolewa juu ya kutangaza mali yao, jinsi walivyoyapata, na kutolewa kwa maelezo kuhusu jamaa zao.
(k) Wale wanaonuia kugombea nyadhifa zozote uchaguzini wasihitajike kujiuzulu nyadhifa katika utumishi wa umma badala yake waruhusiwe kwenda likizoni na hatimaye kujiuzulu iwapo watakuwa wamechaguliwa.
(l) Mtihani wa ufasaha wa lugha kwa yeyote ambaye umehitimu kutoka viwango vya elimu vilivyotajwa hastahili kuufanya hivyo basi hauna budi kupigwa marufuku.
(m) Maadili maalum ya taaluma ya uongozi yanafaa kuweko.

(iv) *Kuhusu matokeo ya uchaguzi ni kwamba:*

(a) Rais achaguliwe kwa zaidi ya asilimia 50 ya kura zote zilizopigwa;
(b) Sheria ya mgombezi kupata asilimia 25 ya kura katika mikoa mitano idumishwe pamoja na ile ya mgombezi kupata asilimia 50 ya jumla ya kura zinazopigwa;
(c) Ama ushindi wa asilimia 25 pekee ya kura katika mikoa mine uzingatiwe;
(d) Katika ugombezi wa urais inafaa kuwe na duru ya pili ya uchaguzi iwapo hakuna mgombezi yeyote atakayepata asilimia 50 ya kura zote zilizopigwa;

(e) Mgombezi wa wadhifa wa Urais hapaswi kugombea kiti cha Ubunge, lakini iwapo hatachaguliwa basi aruhusiwe kuwa Mbunge lakini baada ya kubainiwa kwamba amejipatia kiwango maalum cha kura;

(f) Ama pendekezo jingine ni kwamba mgombezi wa Urais aruhusiwe kugombea kiti hicho pamoja na kile cha Ubunge, lakini yule anayechaguliwa Rais aache kiti cha Ubunge na hivyo uchaguzi mdogo uitishwe ili kujaza kiti cha Ubunge.

(g) Wakati wote Rais anafaa kuchaguliwa moja kwa moja na wananchi.

*(v) Kuhusu Tabia ya Wawakilishi waliochaguliwa kwamba:*

(a) Wawakilishi wazembe wanastahili kuonywa;

- Kama ishara ya uhuru wa wananchi;
- Kuimarisha uhusikaji wa wananchi katika shughuli ya upigaji kura na kumkwamua mwananchi katika hali ambapo amejikuta bila hiari yake;
- Kuwahimiza wapigakura na kutenga vyombo vinavyowasaidia kuchunguza utendaji kazi wa mbunge;
- Itilie mkazo wajibikaji wa mbunge, kutoa maelezo kwa wapigakura na kumtia shime mbunge ili ayatekeleze majukumu yake ipasavyo.

(b) Jukumu la kuwaonya maafisa wazembe lapaswa kusimamiwa vyema kwa sababu hali hiyo;

- Inaweza kuiharibu serikali wakilishi kwa kuwa kizuizi kwa wabunge wenye bidii kazini;
- Inaweza kuwavunja moyo wasomi wanaowania afisi za umma;
- Inaweza kuvipa nafasi vyama vya kisiasa vilivyoshindwa kwenye uchaguzi nafasi nyingine na kujishindia afisi;
- Inaweza kusababisha mateso yasiyokuwa na maana kwa wabunge; na
- Inaweza kusababisha kuachishwa kazi kwa maafisa kwa sababu ndogondogo zisizo na maana.

### 10.3.5 Uchanganuzi

Maoni yaliyotelewa hapa yana athari kubwa sana katika usawiri wa mfumo mpya wa uchaguzi na usimamizi wa utaratibu wa uchaguzi. Ni wazi, kwa mfano, kuwa watu wengi walitaka kuona mfumo mpya ulio wazi, unaofaa na unaweza kubashirika. Walitaka pia kuona viongozi wanaoteuliwa kuwahudumia wakiwa wameelimika zaidi na wenye maadili mema. Wengi wa wale waliofika mbele ya Tume walieleza hali ya kutoridhika na mienendo ya wawakilishi wao, wengi ambao walikuwa, mara tu baada ya uchaguzi, wamepotelea Nairobi kurudi tu miaka mitano baadaye. Wengi walitumai kuwa mifumo mipya ingewekwa ya kutumika wakati wa uchaguzi mkuu ujao. Wengi wao, lakini, walionyesha kuchoka sana na viongozi waliopo kiasi kuwa wanataka uchaguzi ufanywe kwa vyo vyote vile.

### 10.3.6 Mapendekezo

Kwa hivyo Tume inapendekeza kuwa:

*(i)* *Kuhusu muundo wa uwakilishi kuwa:-*

(a) Bunge liundwe na kumbi mbili zitokanazo kufanyiwa uchaguzi katika kiwango cha taifa. Hizi ni ukumbi wa baraza la Taifa na Ukumbo wa Wabunge;

(b) Pawe pia na mabaraza ya mkoa na wilaya kwa madhumuni ya upunguzaji na usambazaji wa madaraka.

(c) Baraza la wabunge:

- kuchukua Mfumo wa Kimseto Wenye Wiano wa Wanachama wa Uchaguzi wa wawakilishi wa baraza la wabunge;
- kuhifadhi maeneo bunge yaliyopo 210 moja kwa moja na wananchi kupitia uchaguzi wa mmoja katika eneobunge kwa kutumia mfumo wa waliowengi;
- kuanzisha viti vingine 90 kwa uwakilishi wa kiwiano;

- kuhusu viti vya uwakilishi wa kiwiano, vyama vya kisiasa vihitajike na sheria kuteua wagombezi wa kiume na wa kike kwa kiasi cha kulingana nusu bin nusu. Katika kila kiwango cha makundi yanayohusika, walemavu, vijana, makabila madogo madogo na makundi mengineyo kadri sheria ya uchaguzi itakavyopendekeza, usawazishi wa kijinsia ufanywe;
- vyama vya kisiasa vitahitajika, na sheria ya uchaguzi, kuainisha thuluthi moja ya wagombezi kuwa wanawake katika orodha ya chama ya kila eneobunge. Vyama vitahitajika pia kuweka asilimia hamsini ya wagombezi kuwa wanawake katika orodha ya uwakilishi wa kiwiano kwa baraza la bunge;
- mfumo wa "zip" utumike katika uandalizi wa orodha ya vyama ya uwakilishi wa kiwiano;
- Vyama vya kisiasa vitateua angalau thuluthi moja ya wagombezi wake kutokana na wanawake kwa viti vya eneobunge moja kwa baraza la wabunge.
- Mfumo wa sasa wa uteuzi ufutiliwe mbali.

(d) Baraza la Kitaifa:

- liwe na wawakilishi 100;
- wawakilishi 70 wateuliwe kutoka wilayani kupitia mfumo utakaomuliwa na sheria ya uchaguzi;
- wanawake thelathini wawakilishi wakiwemo wawakilishi wanne watakaoteuliwa kutoka katika kile moja ya mikoa saba na wawili kutoka Nairobi;
- wawakilishi wanawake wateuliwe kupitia mfumo utakaowekwa na sheria ya uchaguzi.

(e) Baraza la mkoa

- liwe na wawakilishi wawili kutoka kila mkoa na washikadau wengine na makundi ya wengine wa kuhusika watakaoteuliwa

kwa njia itakayoamuliwa na sheria ya uchaguzi na angalau thuluthi moja ya wawakilishi katika viwango vya mkoa watakua wanawake.

- na makundi ya wataalamu jinsi itakavyoamuliwa na Tume ya Wilaya ya Uchaguzi.
- mwenyekiti, mwekahazina na viongozi wengine wa baraza la mkoa watachaguliwa kutokana na wanachama wa kupiga kura ili kuunda kamati kuu ya mkoa;
- msimamizi mkuu wa mkoa (katibu wa mkoa) atateuliwa moja kwa moja na wananchi;
- Watu wanaotaka kuchaguliwa katika baraza wanaweza kuteuliwa na vyama vya kisiasa au kugombea kama wagombezi huria;
- Baraza la mkoa ndilo chombo cha mkoa cha kufanya maamuzi, kuweka sera na kuunda sheria.

(f) Baraza la wilaya

- Kitengo cha uchaguzi kitakuwa kata jinsi ilivyo sasa.
- Angalau thuluthi moja ya wawakilishi watakaochaguliwa katika kata zote za wilaya wawe wanawake.
- Vyama vya kisiasa vitatarajiwa kuteua angalau thuluthi moja ya wagombezi wake kutokana na wanawake kwa uchaguzi wa moja kwa moja katika baraza.
- Mwenyekiti, mweka hazina na maafisa wa barasa la wilaya watateuliwa kutokana na wanachama wa kuchaguliwa na wanachama wapiga kura wa baraza la wilaya ili kuunda kamati kuu ya wilaya.
- Msimamizi mkuu wa wilaya (katibu wa wilaya) atachaguliwa moja kwa moja na wananchi.
- Baraza la wilaya ndilo chombo cha wilaya cha kutoa maamuzi, kuweka sera na cha kuunda kisheria.

(g) Baraza la Kata la Wazee

- Baraza la Kata litakuwa na wazee wawili watakaochaguliwa kutoka kila kijiji kupitia mfumo utakaowekwa na sheria ya uchaguzi;
- Msimamizi wa baraza la kata atachaguliwa moja kwa moja na wananchi;
- Angalau thuluthi moja ya wajumbe wa Baraza la Kata watakuwa wanawake;
- Kijiji kinaainishwa katika misingi ya utamaduni uliopo au ujirani wa kimakundi.

*(ii) Kuhusu utaratibu wa uchaguzi kwamba –*

(a) Bunge litavunjwa moja kwa moja miaka mitano baada ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu uliopita;

(b) Uchaguzi Mkuu utafanywa siku 45 kabla ya kuvunjwa kwa Baraza la Taifa;

(c) isipokuwa katika Uchaguzi Mkuu ujao, itabidi Uchaguzi Mkuu ufanywe jumanne ya kwanza ya Juma kamili la mwezi Agosti kila baada ya miaka mitano;

(d) pale ambapo afisi ya Rais inakuwa wazi kwa sababu ya kujiuzulu, kifo au kutojiweza, au kutenguliwa, uchaguzi wa mrithi utafanywa baada ya siku thelathini. Spika wa Baraza la Taifa atatenda kazi kama Rais katika muda huo;

(e) katika hali nyingine, lazima uchaguzi ufanywe siku 45 kabla ya muda wa kuwa afisini wa Rais aliyepo kuisha;

(f) ujumbe mkuu wa Kanuni za Maadili unahitaji kuwakilishwa kwenye Katiba;

(g) adhabu kadha za ukiukaji wa kanuni zinahitaji kuwekwa;

(h) wagombezi wasitumie vifaa vya serikali katika kampeni zao;

(i) vyama vyote vipewe muda wa kutosha katika vyombo vya habari vya serikali;

(j) vyombo vyote vya habari vya kiserikali vihakikishe kuwa vinasawazisha baina ya vyama vya kisiasa. Vyama vyote viagizwe na sheria kutangaza na kujadili ujumbe wa sera zao kupitia vyombo vya habari vya serikali;

(k) kuzuia matumizi ya fedha na rasilmali kwa uchaguzi;

(l) kura zitahesabiwa katika vituo vya kupigia kura. Kwa mujibu wa wakati ujao Katiba au sheria inayohusika itahitaji kuweka misingi ya uwezekano wa kuwa na mitambo ya kupigia kura ambayo itawezesha kuhesabu kwa kura kutekelezwa katika kituo maalum cha kompyuta;

(m) kauli ya jumla kuwa lazima Tume ya Uchaguzi ihakikishe kuwa vibanda vya kupigia kura vinafikiwa na wote, na kuwa hatua zote za kufaa zinachukuliwa ili kuhakikisha kuwa wapiga kura wote watazipiga kwa faragha;

(n) Katiba itambue thamani ya utazamaji na uchunguzi wa uchaguzi na iruhusu Tume ya Uchaguzi kutekeleza;

(o) Katiba inaweza kurejelea panapohitajika, na kuzingatia kanuni za kimataifa na mapitio ya kufaa ya utazamaji na uchunguzi;

(p) Katiba itambue na kuwezesha haki ya kushiriki kwa jamii katika uchaguzi, utazamaji na uchunguzi hata kama itabidi kuwapunguzia gharama;

(q) pawe na kauli katika ibara ya kitangulizi cha jumla kuhusu kanuni za uchaguzi, kuwa kura hazitanunuliwa;

(r) kanuni ya kukadiria matumizi ya fedha kwa uchaguzi iwekwe katika Katiba;

(s) Katiba ibainishe kuwa kila raia ana haki ya kimsingi ya kupiga kura. Haki hii iongezwe katika Sheria ya Haki;

(t) upigaji kura uchukuliwe kama haki na pia jukumu la msingi la kila raia na ni lazima isitumiwe vibaya bali itekelezwe kwa busara kwa madhumuni ya wema wa jumla wa jamii.

(u) Serikali ina jukumu la kumwezesha kila raia kutekeleza haki yake ya kidemokrasia na jukumu la kupiga kura na kuondoa vizuizi vyote vya upigaji kura;

(v) Katiba ishinikize kanuni kuwa uchaguzi utafanywa kwa kura ya siri;

(w) ithibati za uraia na umri katika usajili wa kupiga kura zizingatiwe kwa kutumia ushahidi mwingine wo wote wa kuaminika, bali si kipande cha uraia tu wala cheti cha usafiri;

(x) Katiba iweke misingi kuwa usajili wa wapiga kura utaendelea mfululizo bali hautawekewa vipindi rasmi;

(y) watu walio kizuizini, walio hospitalini, shuleni na asasi nyingine waruhusiwe kupiga kura kwa kuwezeshwa kuvifikia vituo vya kupiga kura, kadri iwezekanavyo;

(z) vituo vya kupiga kura vya walemavu viweze kufikiwa kadri iwezekanavyo;

(aa) katika maeneo ya wafugaji wa kuhamahama, Tume ya Uchaguzi inaweza kuweka vituo vya kupiga kura vya kuhamishwahamishwa;

(bb) waflis wasiruhusiwe kupiga kura;

(cc) vikosi vya kijeshi viruhusiwe kutekeleza haki yao ya kupiga kura;

(dd) kuhukumiwa kwa hatia ya upigaji kura au kuhusishwa katika kesi ya ombi la haki ya uchaguzi kama ambaye ana hatia, kumfanye mtu azuiliwe katika uchaguzi mkuu mmoja tu, isipokuwa katika hatia nyeti kama vile matumizi ya nguvu, rushwa au udanganyifu wa kura, uchochezi wa kusababisha matumizi ya nguvu, maovu ya chuki;

(ee) kanuni ya kuwa mkazi ihifadhiwe lakini itegemee marekebisho ya muda baada ya muda yanayofanywa na Tume ya Uchaguzi kadri ambavyo teknolojia ya uchaguzi inayobadilika;

(ff) Katiba itaje kuwa Sheria ya uchaguzi iweke masharti ya kufaa kuhusu makazi kwa kuzingatia miundo inyosambaziwa madaraka;

(gg) mamlaka ya Rais ya kumhurumia mtu ambaye amehukumiwa kwa hatia ya uchaguzi ili aweze kusajiliwa kama mpiga kura au kugombea kiti, yafutiliwe;

(hh) Katiba iwahakikishie raia wa Kenya wanaoishi, wanaosoma, wanaosafiri au wanaofanya kazi nje ya nchi na ambao wanatimiza kanuni za jumla za kupiga kura, haki ya kupiga kura katika uchaguzi;

(ii) siku ya kupiga kura itangazwe kama sikukuu ya umma lakini endapo uchaguzi utaendelea hadi siku ifuatayo au zifuatazo, siku zifuatazo za uchaguzi hazitakuwa sikukuu;

(jj) Katiba na sheria vitahakikisha kuwa kuna uchaguzi wa haki na ulio huru; vitu ambavyo ni vya msingi kwa demokrasia;

(kk) haki ya kupiga kura itakuwa sawa na ya siri;

(ll) mfumo wa uchaguzi utalenga kutimiza usawa na ushirikishi;

(mm) wagombezi wote na vyama vya kisiasa watakuwa huru kufanya kampeni bila kuzuiliwa; na

(nn) wagombezi wote na vyama vya sisiasa wajiepushe na fujo.

*(iv)* *Kuhusu Ugombezi wakasema* -

(a) makaratasi ya kuteuliwa kwa wagombezi katika viwango vyote vya mfumo wa uchaguzi yawaagize wagombezi kueleza wazi viwango vyao vya elimu na sifa zao za kitaaluma;

(b) Pia waagizwe kutoa habari kuhusu –

- Mashtaka na vifungo vyao vya awali na endapo mashtaka yangalipo;
- Mali yao ikiwemo utangazaji wa uhamishaji ambao umefanywa katika muda wa miaka mitatu kabla ya tarehe ya uteuzi;

- Madeni yo yote kama yapo, hasa madeni kwa mamlaka ya umma jinsi livyotangazwa India na Mahakama ya Juu. Habari hizi zipatikane kwa urahisi kwa wapiga kura; na
- Cheti cha afya.

(c ) Ushiriki katika utawala katika viwango mbalimbali unahitaji sifa za msingi katika viwango ainaaina. Hili ni muhimu ili kuhakikisha thamani na hali ya kufaa ya utawala ambao utahudumia vizuri maslahi ya umma;

(d) Wagombezi huria wa Urais, Baraza la Taifa na mabaraza yote waruhusiwe, kwa mfano, isiwe lazima mgombezi kuteuliwa na chama cha kisiasa;

(e) Wagombezi wa urais wawe na umri usiopungua miaka 35 na usiozidi miaka 70 wakati wa kugombea afisi;

(f) Mgombezi wa nafasi ya kuchaguliwa anaweza kuharamishwa kwa sababu kadha ambazo zinaweza kuwa pamoja na –

- Akiwa amehukumiwa kifo au amepewa hukumu ya zaidi ya miezi sita;
- Akiwa na akili punguani;
- Akiwa muflis ambaye hajaachiliwa;
- Akiwa na matumaini katika kandarasi na serikali jinsi ambavyo itaelezwa na bunge; na
- Akiwa anashikilia afisi ya umma, ikiwa pamoja na mahakama, serikali ya wilaya au vikosi vya majeshi.

(g) Bunge linaweza pia kuweka kanuni kuwa mtu ambaye ameshikilia afisi, ambayo ni msingi wa kutoruhusiwa, anaweza kutoruhusiwa kwa muda usiozidi miezi sita baada ya kuacha kuishikilia afisi hiyo;

(h) mtu anayetafuta kuchaguliwa katika nafasi ya afisi za raia na za bunge awe na cheti cha kisomo cha shule ya sekondari au kingine kinacholingana na hicho;

(i) mgombezi wa kiti cha Rais awe na angalau shahada ya chuo kikuu;

(j) katika mipaka ya kisheria na yenye mantiki, uwakilishi katika viwango vya utawala vya kitaifa na vya chini unahitajika kuwa wazi na kuwa kustahiki; iwe kwa kijana au mzee, na bila kuzingatia umaskini au utajiri au kukiri imani yoyote ya kidini au jinsia au rangi;

(k) mtu ambaye amehukumiwa kwa kosa la ufisadi au kutokuwa mwaminifu au hatia nyingine yo yote chini ya Katiba na sheria kwa muda unaozidi miaka mitatu asiruhusiwe kusimama kwa uchaguzi kwa kipindi kinacholingana na awamu moja baada ya kuachiliwa kutoka gerezani.

(l) ukiukaji wa kanuni ya Uongozi utamfanya mtu asiruhusiwe kugombea kiti kwa muda wa miaka kumi.

(m) isipokuwa kwa mfanyakazi wa umma ambaye amezuiliwa na Katiba, wafanya kazi wa raia waruhusiwe kuchukua likizo kutoka kazini ili kugombea afisi za uchaguzi, isipokuwa wachaguliwe au hadi watakapochaguliwa;

(n) Rais ambaye amestaafu hataruhusiwa kugombea nafasi yo yote ya uchaguzi

(o) Katiba ifafanue mambo yafuatayo –

- wale ambao wamezuiliwa kabisa kabisa (labda baadhi ya hawa wazuiliwe kwa muda baada ya kuiacha afisi);
- wale wanaozuiliwa kugombea katika maeneobunge ya kijiografia wanaweza kuwa kwenye orodha ya chama ili "kujaliza" viti katika misingi ya mfumo wa Uchaguzi wa Kimseto Wenye Wiano wa Wanachama;
- wale ambao wanaweza kugombea kiti chochote; ingawaje, itabidi wajiuzulu endapo watachaguliwa; na
- wale ambao wanaweza kugombea kiti lakini ambao itabidi wachukue likizo bila malipo ikiwa watateuliwa.

*(v)* *Kuhusu awamu ya Rais kuwa afisini –*

(a) awamu ya Rais kuwa afisini isizidi miaka mitano.

(b) mtu yeyote asiruhusiwe kushikilia afisi ya Rais kwa muda wa kuzidi awamu mbili zisizozidi miaka mitano kila moja;

(c) ikiwa Rais atajiuzulu, atatenguliwa, au atakufa akiwa afisini, na muda wake uliosalia afisini ni chini ya miezi thelathini, muda uliosalia wa awamu hiyo hautahesabiwa kama awamu kwa madhumuni ya kuhesabu marupurupu ya mtu anayechukua nafasi yake ili kuhudumu kwa awamu mbili baadaye;

(d) vizuizi katika awamu ya Rais vitazingatiwa kwa kufikiria mambo ya zamani. Kwamba uzingativu huu utawahusu hata wale ambao wameishikilia afisi hiyo awali; na

(e) mgombezi wa urais anayegombea anatakikana awe ambaye anaweza kupata asilimia ishirini ya kura katika zaidi ya nusu ya mikoa na zaidi ya asilimia hamsini ya kura za kitaifa. Ikiwa hakuna mgombezi anayeyatimiza haya, wagombezi wawili wanaoongoza watafanya uamuzi mkata ambapo mshindi wa moja kwa moja atatangazwa mshindi.

*(vi)* *Kuhusu kutenguliwa na kuondolewa –*

(a) Rais atakabiliwa na mashtaka ya utenguzi kwa ukiukaji wa Katiba au sheria au hatia mbaya kuhusu mashtaka yanayoletwa na wingi wa wajumbe wa Baraza la bunge kuamuliwa na Baraza la kitaifa. Rais wa Mahakama ya Juu atasimamia mashtaka ya utenguzi.

(b) pawe na mbinu za kutosha za kuzuia hatari ya utenguzi kutumiwa kwa malengo ya kisiasa tu.

(c) Katiba ibainishe misingi ya kuondolewa ambayo inaweza kushirikisha:

- Upungufu wa kimwili na kiakili ambao utamfanya mbunge kushindwa kutekeleza majukumu ya afisi yake;
- Ukiukaji au utovu wa adabu ambao unaweza kusababisha chuki, dharau, kiburi au fedheha kwa afisi; au

- Kuwapuuza wanaeneobunge kwa muda mrefu au kudharau majukumu yake ya bunge bila sababu maalum.

(d) mtu hawezi kuondolewa kabla ya miaka miwili isipokuwa pale anapopata upungufu wa kimwili au kiakili.

(e) ili kuanzisha taratibu za kuondolewa, angalau 1/5 ya wapiga kura katika eneobunge au kipengele kingine cha upigaji kura kitakachobainishwa na sheria kitatumia hoja ya maombi ya kisheria kwa spika (katika viwango vya Mkoa, Wilaya au Kata hoja ya maombi itapelekwa kwa mwenyekiti) ili kuondolewa, huku wakiweka misingi ya kuondolewa. Mamlaka yaliyotajwa yataisihi Tume ya uchaguzi kuchunguza mashtaka hayo ikiwa Tume ya Uchaguzi itaridhishwa na mashtaka, spika /mwenyekiti atakitangaza kiti kuwa wazi. Licha ya kupoteza kiti, mbunge au diwani atazuiliwa kugombea uchaguzi katika muda mwingine wa miaka mitano.

(f) Kanuni na maelekezo ya wazi yawekwe na Tume ya Uchaguzi ili kubainisha wakati ambapo mbunge anakigura chama chake (iwe katika maandishi, matendo au matamshi) na kwamba masharti haya yatekelezwe kwa dhati.

*(vii)* *Kuhusu Kusimamia Uchaguzi –*

(a) maneno "uhuru na kutopendelea" yatumiwe katika Katiba kuhusiana na Tume ya Uchaguzi.

(b) uteuzi katika Tume ufanywe baada ya mbinu za kuandaliwa orodha teule, kuchujwa na Baraza la Bunge kufuatia ushauri wa Tume ya Kitaifa ya Maadili na Uaminifu, na uteuzi ufanywe na Rais ambaye ni lazima akubali majina yatakayopendekezwa jinsi ilivyo na uteuzi wa majaji;

(c) Tume iwe na uhuru wa kifedha; matumizi yake yatokane na Mfuko Mkuu wa Fedha za Umma (jinsi ilivyo na majaji, tena hili linamaanisha kuwa pasiwe na kutengewa wala mjadala katika Bunge na wahakikishiwe malipo);

(d) Tume iwe na afisa wake wa kuweka akaunti;

(e) iwe na hadhi ya shirika – awe mtu tofauti kisheria aliye na haki ya kuleta mashtaka na kuwatetea;

(f) vigezo vya uanachama vibainishwe – na viwe pamoja na kigezo cha kutokuwa ameshughulikia harakati za vyama vya kisiasa hivi karibuni;

(g) vyama vya kisiasa visishughulishwe katika uteuzi, hasa katika muktadha wa kuzingatia chuki za kisiasa na hatari ya kuzileta chuki hizi katika Tume yenyewe;

(h) idadi ya wanatume ipunguzwe ili isipungue saba wala kuzidi kumi na moja – nchi nyingi zimeona manufaa ya kuwa na Tume ndogo,;kazi nyingi hufanywa na kikundi cha wafanya kazi wanaofaa;

(i) awamu ya afisi ihakikishe kuwa mwanatume anahudumu kwa muda wa vipindi viwili vya uchaguzi ili mazoea yatumiwe vizuri. Uanachama uwe wa kupangwa nyakati tofauti;

(j) Wanatume wawe na usalama wa awamu ya kazi, waondolewe kufuatia uchunguzi unaofanywa na mahakama maalum ya dhati iliyo huru;

(k) Wanatume wawe watu wenye uadilifu wa kibinafsi, wenye tabia nzuri ya kudhibitika, huduma nzuri ya kiasi kwa umma na wenye kiwango cha kisomo kitakachobainishwa;

(l) Katiba itaje kuwa matokeo ya uchaguzi wa Rais yatatangazwa na Tume;

(m) Maafisa wa polisi wasiwe katika vituo vya kupigia kura – hili ni kinyume na kanuni za kimataifa;

(n) Katiba iipatie Tume uwezo wa kutosha utakaoiwezesha kuunda amri zitakazolenga kuboresha kufaa na ustadi wa taratibu za uchaguzi;

(o) Tume isambazwe hadi kiwango cha wilaya ili kuunga mkono taratibu za uchaguzi katika wilaya;

(p) Wanatume waliostaafu au wa zamani hawatagombea afisi za kuchaguliwa kwa muda unaolingana na awamu moja;

(q) Tume ipewe uwezo wa kushughulikia migogoro ya uchaguzi au hatia za uchaguzi mara moja. Ni vyema kukiwa na njia ya kusuhulisha

migogoro inayozuka wakati wa kupiga kura, ikiwezekana, badala ya kungoja hadi mashtaka ya uchaguzi yawepo katika mataifa fulani, Tume ya Uchaguzi ina uwezo wa kushughulikia migogoro kama hiyo. Kwa mfano, nchini Uganda Tume ya Uchaguzi inapewa jukumu hili.

(r) Kuhusu migogoro ya uchaguzi:

- Iwezekane (kama ilivyokuwa hadi uamuzi wa Mahakama ya Rufani) kwa malalamiko kuelekezwa Mbunge, Rais au Diwani ambaye uchaguzi wake unapingwa. Kupitia taarifa katika Gazeti la Serikali na gazeti la kila siku – ni rahisi mno kwa mtu kama huyo kukataa kuchukua taarifa hiyo yeye mwenyewe;
- Mahakama yawe na majaji wawili badala ya watatu;
- Mahakama yakutane katika Mkoa kunakotoka malalamiko;
- Malalamiko yote ya uchaguzi yasikizwe kufikia mwaka mmoja baada ya uchaguzi.

(viii) *Kuhusu mipaka ya uchaguzi:*

(a) Tume maalum ya Mipaka ya Uchaguzi iundwe kufikia miaka miwili. Baada ya kuanza kwa kutumika kwa Katiba Mpya ili kushughulikia:

- migogoro iliyopo ya mipaka;
- malalamiko kuhusu mipaka mipya ya uchaguzi (eneobunge la mbunge mmoja, lokesheni/mtaa);
- kuunda viwango vingine vya uchaguzi baada ya kupungwa na kusambaziwa madaraka mikoa, wilaya, lokesheni na vijiji.

(b) Katiba iunde kinaganaga kaida ya ukubwa wa eneobunge kwa kugawa idadi ya watu nchini na idadi ya maeneobunge yanayohitajika. Tume ya Uchaguzi iruhusiwe ukiukaji wa asilimia kumi (10%) nje ya kaida; ni katika hali chache mno ambayo asilimia kubwa itaruhusiwa. Wagombeji na Wabunge kutoka maeneobunge mapana (kama Mkoa wa Kaskazini Mashariki) wapewe msaada wa usafiri na fedha.

(c) Utaratibu wa kurekebisha na kupima mipaka ya uchaguzi uwepo kila baada ya miaka kumi kwa kutumia matokeo ya idadi ya watu (sensa). Utaratibu uwe wazi na utoe nafasi ya umma kushauriana, kujadiliana na Katiba iwe na kanuni zitakazozuia Bunge na/au mamlaka ya Taifa kubadilisha mipaka ya uchaguzi kiholela.

# SURA YA KUMI NA MOJA

# VYOMBO VYA SERIKALI

## 11.1 Agizo la Tume

Lengo kuu la marekebisho chini ya sheria ni:

> *… kutambua na kubainisha vitengo vya majukumu miongoni mwa vyombo kadha vya Taifa ikiwemo mamlaka ya nchi, bunge na mahakama ili kuibua vipimo na visawazishi baina yao na kuhakikisha uwajibikaji wa serikali na maafisa wake kwa wananchi.*

Kwa hivyo Tume iliagizwa

> *kuchunguza na kupendekeza muundo na majukumu ya vyombo vya serikali ikiwemo Mamlaka ya Nchi, Bunge na Mahakama na shughuli zao kwa kulenga kutekeleza kikamilifu vipimo na visawazishi baina yao na kupata uhuru wao.*

Pia, Tume iliagizwa kwa njia maalum,

> *kuchunguza na kutoa mapendekezo kuhusu mahakama kwa jumla na kwa njia maalum kuhusu muundo na mipaka ya mahakama, kwa kulenga katika hatua za kufaa ili kuhakikisha umakinifu, uwajibikaji, ufaafu, nidhamu na uhuru wa mahakama.*

## 11.2 Mfumo wa Serikali

Uamuzi muhimu katika uandalizi wa Katiba na majukumu ya katiba ya sasa ni utayarishaji wa ramani ya uwezo wa taifa, yaani mfumo wa serikali. Mfumo wa serikali utaamua umbo la uwezo wa vyombo vya serikali, namna ya kutekeleza uwezo huo hasa kwa kadri unavyoathiri utawala wa wananchi na uainishaji wa

rasilmali na nafasi zilizopo katika serikali. Mfumo ya utawala huamuliwa na uwezo na majukumu ya vyombo vya serikali; muundo wake na uhusiano baina yake. Vyombo muhimu zaidi ni Bunge, mamlaka ya nchi na mahakama.

Kwa hivyo, ni muhimu kufafanua mfumo wa utawala wa nchi kwa sababu mfumo huu huathiri utendakazi muhimu, mipango ya siasa, na ukubalifu wa maslahi ya kimakundi katika jamii, ushiriki wa wananchi katika utawala, na utekelezaji wa kanuni za kufaa, uwazi na uwajibikaji kwa kuongezea. Mfumo huo unaweza kuratitibishwa ili kukuza na kutimiza maadili ya kitaifa, kukuza demokrasia na kuwezesha maendeleo ya wananchi ya kijamii na kiuchumi, kuimarisha umoja wa kitaifa na kulinda uadilifu wa kitaifa.

Hatimaye, Tume iliandaa idadi ya maswali kwa wananchi kuhusiana na vyombo vitatu vikuu vya serikali ikiwemo bunge, mamlaka ya nchi na mahakama. Jambo muhimu kwa Tume lilihusu masuala ya utenganishaji wa madaraka baina ya vyombo hivi.

Kanuni ya utenganishaji wa madaraka inamanisha kuwa kuna haja ya kuwa na mipaka baina ya majukumu na madaraka ya vyombo tofauti vya serikali, yaani, mamlaka bunge na mahakama, ili pasiwe na chombo chenye madaraka ya kupindukia na kuwa kuna vipimo na visawazishi baina yao. Lengo ni kuhakikisha usawazishi na uwajibikaji wa serikali ulio huru kutokana na mizozo ya kirasimu na uzembe.

## 11.3 <u>Bunge</u>

### 11.3.1 Kanuni za kijumla

Bunge zinaweza kuainishwa katika aina mbili kuu: faragha moja na faragha mbili. Bunge za aina ya faragha moja zina ukumbi mmoja, ilhali bunge za aina ya

faragha mbili zina kumbi mbili. Katika aina ya pili, muundo wa ukumbi wa juu ni tofauti toka nchi moja hadi nyingine na majukumu yao yanaweza kuwa mengi.

Katika mifumo ya tawala za kimajimbo kama vile India, Nigeria na Marekani, bunge za faragha mbili huwakilisha maeneo ya nchi. Katika mifumo ya kisiasa ya umoja kama vile ya Kenya, Uganda na Eritrea bunge za faragha moja ndizo huchukuliwa. Bunge za faragha mbili zimetambulika kwa kuwakilisha matarajio ya aina mbalimbali, huku ikiwezesha mwelekeo wa maksudi kuhusu uwekaji sheria na kwa hivyo kuibuka na sheria za hali ya juu. Pia hutoa fursa ya kuangaza mbele na kudhibiti mamlaka. Kwa upande mwingine, bunge za faragha moja zinaweza kufanya maamuzi ya haraka, hutaji gharama kidogo kwa mujibu wa usimamizi wa wakati na rasilmali na hufaa katika mataifa yenye usare na yenye wate wachache.

Bunge hutimiza majukumu matatu makuu ambayo ni:

- Uwakilishi;
- Uundaji wa sheria; na
- Usimamizi wa mienendo ya serikali.

Jukumu la bunge la uwakilishi linatokana na hali ya kuwa katika mamlaka mengi ya kisheria, wabunge huchaguliwa na wananchi na huwa na agizo la kueneza maoni ya wananchi. Kwa hivyo, wabunge huwakilisha uhuru wa kujitawala wa wananchi. Wabunge wa kufaa lazima wawe na mbinu za kufaa za kuunganisha wananchi na serikali yao na ni lazima wawakilishe kibunifu maono ya wananchi kuhusu maisha yao ya umma. Ni lazima wafanye juhudi za kuwakilisha wananchi na matarajio yao kwa njia ya kufaa, jukumu ambalo linahitaji kujitolea ili kuhakikisha kuwa maoni ya wananchi yanawakilishwa katika kila swala la serikali.

Jukumu la Bunge la kuunda sheria pia linatokana na hali kuwa sheria zinapaswa kutokana na bunge kama dhihirisho la haki ya kujitawala ya wananchi. Katika

kuunda sheria, bunge linahakikisha kuwa ndoto na matarajio ya wananchi yanakuzwa na kulindwa. Kwa hivyo, bunge linatakikana kuwa na uwezo na ujuzi wa kubadilisha, kwa njia ya kufaa na iliyo sahihi, matumaini hayo ili yawe ya kutekelezeka. Jukumu la bunge la uundaji wa sheria ndilo muhimu zaidi kwa vile linahusiana na ugawaji wa mamlaka, ugawaji sawazishi wa rasilmali za kitaifa na huduma miongoni mwa raia wote katika kila mahali na, kama kisawazishi, utimizaji kijamii wa kilele cha rasilmali na nafasi za raia wote na macheo yote kufaidi. Kwa kiasi fulani, bunge linashiriki jukumu hili na mamlaka.

Jukumu la Bunge la usimamizi limekuwa la muhimu sana katika nyakati za hivi majuzi. Bunge ndilo mlinzi wa mamlaka ya nchi. Usimamizi ni pamoja na taratibu za kuchunguzia sera na ugawaji na matumizi ya rasilmali ili kuhakikisha utimizaji wa juu wa kijamii. Uchunguzi huhakikisha kuwa sera zinahusiana na maslahi ya wananchi, na taratibu za mapato na matumizi zinasawiriwa vizuri ili kutimiza mahitaji haya. Hali ya kufaa kwa bunge ili kutekeleza vizuri jukumu hili hutegemea uwezo wa usimamizi rasmi unaotokana na katiba na sheria zilizoundwa, rasilmali (pamoja na utaalamu) zilizopo na za kuwezesha usimamizi na nia njema ya kisiasa na urazini wa wabunge wenyewe. Mbinu moja muhimu ya bunge Kudhibiti mamlaka ni matumaini/mjadala au taratibu za hoja ya lawama. Katika demokrasia za bunge zilizoendelea, masuala haya hunukuliwa kwa manufaa ya kudumu kwa serikali.

### 11.3.2 Bunge katika Katiba

#### *(a) Msingi*

Katiba ya uhuru iliweka misingi ya bunge lililoundwa na Malkia katika Bunge na Baraza la Wabunge. Baraza la Wabunge lilikuwa la faragha mbili, likiwemo ukumbi wa wawakilishi kama ukumbi wa chini na senate au ukumbi wa juu. Kulikuwa na maseneta 41 waliochaguliwa kutoka wilaya za kiseneti 41 zilizofafanuliwa kwenye katiba kama eneo la Nairobi, Mto Tana, Lamu, Kwale, Kilifi, Mombasa, Taita, Marsabit, Isiolo, Meru, Embu, Kitui, Machakos, Kiambu,

Thika, Muranga, Nyandarua, Kirinyaga, Nyeri, Turkana, Samburu, Pokot Magharibi, Trans-Nzoia, Elgeyo-Markwet, Baringo, Laikipia, Nandi, Nakuru, Uashin Gishu, Narok, Kajiado, Nyanza ya Kati, Kericho, Kisii, Bungoma, Kakamega, Busia, Mandera, Wajir na Garissa. Seneti ilitakitana kuwa mlinzi wa kisiasa wa majimbo na ilikuwa na jukumu kuu katika marekebisho ya katiba ambamo robo tatu ya wanachama wa kumbi zote mbili walitarajiwa kupiga kura kwa kuunga mkono mjadala ili ufaulu. Maseneta walimchagua Spika wao na naibu wa spika kutokana na wao wenyewe au watu waliostahili kuchaguliwa kama seneta. Maseneta walichaguliwa kwa muda wa miaka sita na uchaguzi huu ulisimamiwa na Tume huru ya Uchaguzi. Tume iliwasajili wapiga kura kwa mujibu wa kila wilaya ya upigakura.

Ukumbi wa wawakilishi ulikuwa na wanachama waliochaguliwa kwa misingi ya maeneobunge yaliyoainishwa na Tume ya Uchaguzi kwa mujibu wa katiba na wanachama waliochaguliwa kwa njia hii maalum waliochaguliwa na wajumbe wa ukumbi wenyewe baada ya uchaguzi mkuu au baada ya kutokea nafasi katika afisi ya mjumbe maalum aliyechaguliwa. Idadi ya wajumbe maalum waliochaguliwa ilikuwa jumla ya idadi ya wajumbe ukigawa na kumi; idadi yao ilikuwa baina ya 11 na 13 kwa vile idadi ya maeneobunge wakati wa uhuru iliwekwa na katiba ili isipungue 110 na isizidi 130. Gavana Mkuu, akishauriwa na waziri mkuu, alikuwa na uwezo wa kuitisha vikao, kuviahirisha au kuvunja bunge. Uhuru wa kuunda sheria ulikuwa katika Baraza la Bunge na ulitekelezwa kupitia kwa sheria. Sheria hizi zingetokana tu na ukumbi wa wakilishi. Mabaraza ya kimaeneo pia yalikuwa na uwezo wa kisheria. Katiba iliweka misingi ya orodha maalum na matukio sambamba ambamo mabaraza ya kitaifa na kimaeneo yangetekeleza uwezo wao.

***(b) Katiba ya sasa***

Sura III ya Katiba iliyopo inatoa msingi kwa Bunge la Kenya ambalo ni la faragha moja, iliyoundwa na Rais and Bunge. Wabunge wanachaguliwa katika vipindi maalum kwa misingi ya maeneobunge yaliyowekwa na Tume ya Uchaguzi ya Kenya au wanateuliwa na vyama vya bunge kwa mujibu wa wingi wao katika Bunge.

Katiba inatoa nafasi kwa wabunge wateule 12. Idadi ya maeneobunge nchini Kenya ni 210. Spika na mwanasheria mkuu ni wanabunge kwa nyadhifa zao. Bunge humteua spika na Naibu wa spika wa Bunge katika kikao chao cha kwanza. Spika si mbunge wa kuchaguliwa. Mahakama kuu hujibadilisha na kuwa Mahakama ya Uchaguzi ili kusikiliza mizozo inayohusu uchaguzi wa wabunge, akiwemo Rais. Katiba pia inatoa kanuni kuhusu afisi ya katibu wa Bunge na wafanyakazi wengine, ambao, kabla ya marekebisho ya 1999 walikuwa afisi za Huduma za Umma. Marekebisho haya yalianzisha Tume ya Huduma za Bunge ambamo sasa katibu wa Bunge anapatikana.

Uitishaji, uahirishi na uvunjaji wa Bunge umo katika mikono ya Rais. Vinginevyo, bunge litavunjwa katika kumbukumbu ya tano ya tarehe ambamo iliapishwa baada ya uchaguzi mkuu. Baada ya kuvunjwa bunge, ni lazima uchaguzi ufanywe katika muda wa miezi mitatu. Katiba haitazamii kupiga kura ya kutokuwa na imani katika serikali ya Kenya inaposema katika sehemu 59 kuwa iwapo Bunge litapitisha kauli inayoungwa mkono na wengi wa wanachama wake na ambayo itakuwa imetolewa ilani ya siku saba, Rais atavunja Bunge katika muda wa siku tatu la sivyo, Bunge litakuwa limevunjwa katika siku ya nne. Mamlaka ya kisheria ya Bunge yatatekeleza kupitia sheria ambazo zimepitishwa na Bunge na kupekekwa kwa Rais ili zikubaliwe katika muda wa siku 21. Rais anaweza kukataa kuikubali sheria; na katika hali hiyo ni lazima kufikia siku 14 aeleze sababu ya kukataa kwake kwa kuandikia Bunge memoranda.

Bunge litawajibika kuiangalia upya sheria hiyo katika muktadha wa mapendekezo ya Rais na ama wayakubali maoni ya Rais na kuiwasilisha sheria ili ikubaliwe au watakataa mapendekezo ya Rais na kuikubali sheria jinsi ilivyokuwa awali. Katika hali kama hii, ni lazima sheria iungwe mkono na zaidi ya asilimia 65 ya wabunge wote. Rais anawajibika kuikubali sheria katika muda wa siku 14. Ni mawaziri tu ambao wanaweza kuanzisha sheria kuhusu fedha Bungeni. Bunge lina uwezo wa kuweka Amri Kuu za Utaratibu (Standing Orders of Procedure) ili kuhakikisha utaratibu katika utekelezaji wa shughuli zake na uwekaji wa kamati za kutekelezea kazi yake. Katika kulifuatiliza hili, Bunge limejiwekea kanuni kuu za Bunge zinazoeleza kwa undani taratibu zake za miundo ya ndani. Kanuni hizi kuu zinaweka kamati kadha za Bunge ikiwemo kamati za kuchunga (kamati ya fedha za umma, kamati ya uwekezaji ya umma) na kamati za idara (Kilimo, Ardhi, Maliasili, Kawi, Mawasiliano, Kazi za Umma, Elimu Utafiti na Teknolojia, Afya, Nyumba, Ufanyakazi na Maslahi ya Kijamii, Utawala, Usalama wa Taifa, Tawala za Wilayani, Fedha, Biashara na Mipango, Utekelezaji wa haki na maswala ya Kisheria, Ulinzi na Mahusiano ya Kigeni. Kuna pia kamati za Bunge, kama kamati ya shughuli, kamati ya makadirio, kamati ya Maktaba, kamati ya spika, kamati ya mahusiano, kamati ya kanuni kuu, kamati ya njia na mbinu, kamati za Bunge zimo na kamati za muda. Kamati muhimu sana ni kamati za Idara. Kwa mujibu wa kanuni kuu 151 ambayo imenukuliwa hivi punde majukumu na uwezo wa kamati za idara, ni:

> "… *kuchunguza, kuulizia na kutoa taarifa kuhusu masuala yote yanayohusiana na agizo, usimamizi shughuli, utawala, utekelezaji na makadirio ya wizara na idara zilizopo*;
>
> *kuchunguza mpango na malengo ya sera za wizara na idara na manufaa katika utekelezaji;*
>
> *kuchunguza na kurekebisha sheria zote baada ya uwasilishaji wa kwanza, kuchunguza, kuhakikisha na kuchanganua mafanikio ya wizara na idara*

*inavyokadiriwa na matokeo yanayopatikana kwa kadri malengo yake yalivyowekwa;*

*kuchunguza masuala yote yanayohusiana na wizara na idara zilizopo kadri yanavyofaa na kadri yanavyoweza kurejelewa na Bunge au waziri, na;*

*kutoa taarifa na mapendekezo kwa Bunge mara nyingi iwezekanavyo, pamoja na mapendekezo kuhusu sheria zinazopendekezwa."*

*Katika shughuli zao, "kamati za idara zitafurahia na kutekeleza mamlaka yote na faida za Bunge ikiwemo kuwaita, mashahidi na kuulizia risiti za makaratasi na nyarake kutoka kwa serikali na kwa Umma …."*

Uwezo, majukumu na faida za Bunge na wabunge zinaelezwa zaidi:

- Sheria ya mapendekezo ya Bunge (Sura 5);
- Sheria ya Bunge, ya (mamlaka na Faida) (Sura 6);
- Sheria ya Bunge na Uchaguzi wa Rais (Sura 7)
- Sheria ya Huduma ya Bunge (Na. 3 ya 2000)

### 11.3.3 Bunge katika Katiba Nyingine

Katiba zote zilizoandikwa au zisizoandikwa zina kanuni za aina fulani ya bunge. Jambo muhimu ni kuchunguza aina mbalimbali za bunge zinazojitokeza kwenye Katiba. Bunge zenye faragha moja zinapatikana katika mataifa yenye serikali kuu ya umoja, iwe uwezo ni wa mfumo wa bunge au mseto wa bunge na urais. Katiba nyingi za mataifa ya Afrika, pamoja na Uganda, Tanzania, Zambia, Botswana, Malawi, Zimbabwe na Ghana ni za mfumo wa faragha moja. Baadhi ya mataifa haya kama Zimbabwe na Botswana yana kumbi maalum (k.m Ukumbi wa Mataifa) ambayo si sehemu ya Bunge. Bunge la faragha mbili ni maarufu katika mfumo ya kishirikisho au ile iliyopunguzwa na kusambazwa madaraka. Katika mataifa haya, mamlaka ya kutunga sheria imo na "Ukumbi wa chini" na "Ukumbi

wa juu", ijapokuwa kiwango cha majukumu hutofautiana. Mataifa haya ni pamoja na Ethiopia, Afrika Kusini, Uingereza, India, Marekani na Jamhuri ya Ujerumani.

Uamuzi wa kuwa na mfumo wa faragha moja au mbili unategemea mara nyingi haja ya uwakilishi imara wa maslahi kadha wa kadha. Hilo pia hutegemea aina ya ya itikadi ya taifa. Kwa hivyo, chuni zenye mpango wa serikali kuu hupenda mfumo wa ukumbi moja. Chuni zenye siasa tofauti tofauti na huria zaidi hupenda kumbi mbili hasa endapo mna upunguzaji na usambazaji madaraka. Jambo la kusisitiza hapa ni kwamba aina ya bunge inayochaguliwa na taifa ni dhihirisho la itikadi ya kisiasa na kiuchumi ya serikali. Kwa hivyo aina ya bune itategemea maslahi yanayolindwa na mfumo huo. Wakati Uingereza inaendelea na imani za ubwanyenye ili kuhalalisha Ukumbi wa Mamwinyi, nchini Marekani, Seneti, iliundwa kama kiashiria cha usawa wa Majimbo katika Muungano na ina majukumu tofauti ya utawala. Aina nyingine ni pamoja na kumbi zinazolinda utamaduni na mamlaka mahsuri au "mataifa", kama katika Ukumbi wa Shirikisho katika Katiba ya Ethiopia.

Majukumu muhimu ya bunge, hata hivyo, ni sawa. Ni:

- Kuwakilisha uwezo wa maeneo;
- Kutunga sheria; na
- Kusimamia na kudhibiti Mamlaka ya Nchi.

### 11.3.4 Waliyoyasema Wananchi

Wananchi waliiambia Tume:

*(i)* *Bunge –*

lichukue jukumu la kuchunguza na kuidhinisha uteuzi wa maafisa wa juu katika afisi kadha za kikatiba na za umma, kutoka kwa Rais. Kwa mfano, uteu

(a) mfano, uteuzi wa Mwanasheria Mkuu, Mhasibu Mkuu, Makatibu wa Kudumu, Jaji Mkuu, Majaji na kadhalika;
(b) liimarishwe kupitia mafumo wa kamati ili kuweza kutekeleza majukumu yake vizuri kwa njia ya kufaa. Kwa mfano, uwekaji wa kamati ya makadirio ili kuchungwe mapendekezo ya bajeti ya serikali, ili kudumisha udhibiti wa fedha za serikali. Mapendekezo mengine yalihusu uwekaji wa Mfumo imara wa Kamati;
(c) liwe na kalenda ya taratibu zake;
(d) liwasilishe matukio yake moja kwa moja katika Radio panapowezekana;
(e) like wengi wanaohudhuria;
(f) liwekewe kiwango cha chini cha elimu kuwa kidato cha nne.

*(ii)* *Wabunge –*

(a) watosheleze kanuni za maadili na uadilifu za uchaguzi wa Bunge;
(b) wawatumikie wote;
(c) wafanye kazi kila wakati;
(d) wasiteuliwe au wanaoteuliwa watoke katika maeneo ya makundi yaliyotiwa pembeni kama vile wanawake, walemavu na walio wachache; na
(e) Mishahara yao iamuliwa na Tume huru.

*(iii)* *Kuwa –*

(a) hatua zichukuliwe ili kuongeza ushiriki wa wanawake katika Bunge na wakafikiana kuwa angalau thuluthi moja ya wabunge na mawaziri wawe wanawake;
(b) kuna hoja ya kuwa na chemba ya pili ingawa maoni yao yalitofautiana kuhusu muundo na majukumu;
(c) Bunge liwe na mamlaka ya kuiondoa serikali iliyopo kupitia kura ya kutokuwa na imani na kumtengua Rais aliyepo.

### 11.3.5 Uchanganuzi –

Wananchi waliambia Tume kuwa wanataka Bunge lijali maslahi yao, ligawane uwezo na kitengo cha Mamlaka ya Nchi na lisimamie shughuli zake bila kuingiliwa na kitengo cha mamlaka ya nchi.

### 11.3.6 Mapendekezo

Kwa hivyo Tume inapendekeza –

*(i)* *uwekaji wa bunge lenye faragha mbili ambalo lina –*

(a) ukumbi wa juu unaoitwa Baraza la kitaifa ambalo lina –

- wajumbe sitini na tisa kutoka kila wilaya,
- mjumbe mmoja kutoka Nairobi.
- wajumbe wa kike thelathini ifuatavyo:
- wanawake wanne kutoka mikoani, na
- wanawake wawili kutoka Nairobi.

Jumla itakuwa wajumbe mia moja.

(b) Ukumbi wa Chini ambao utakuwa na wabunge 210 waliochaguliwa kutoka maeneobunge yote na 90 walioteuliwa kupitia mfumo wa uchaguzi wa kimseto wenye wiano wa wanachama.

(ii) *Awamu ya Bunge idumu* toka wakati wa uchaguzi hadi wakati wa uchaguzi; kwa mfano, itaanza na kuwaapisha wabunge na kuendelea hadi uchaguzi mkuu utakaofuatia.

*(iii)* *Ili kustahili kuchaguliwa bungeni mgombezi analazimika –*

(a) kuwa na angalau cheti cha elimu ya kiwango cha sekondari;
(b) kuwa na umilisi wa lugha za Kingereza na Kiswahili;
(c) awe mtu mwenye uadilifu wa hali ya juu;
(d) awe na umri usiopungua miaka ishirini na moja.

*(iv)* *Majukumu ya Bunge ni –*

(a) kuwakilisha wananchi katika utawala na kuwapatia fursa ambamo mahitaji yao (ya wananchi) yanaweza kuwasilishwa;
(b) Kuunda sheria na sera ili kuiendesha vyema serikali na bunge litapitisha sheria ambazo zitawasilishwa kwa Rais ili azikubali katika wadhifa wake kama kiongozi wa nchi;
(c) Kutimiza jukumu ila kuchunga kitengo cha mamlaka ya nchi utakuwa mfumo wa kufaa wa vipimo na visawazishi kwa uziada wa kupindukia wa kitengo cha mamlaka ya nchi;
(d) Kutathmini na kuafiki shughuli muhimu za rais za kuhusu afisi nyingine za kikatiba. Kwa mfano, uteuzi wa mwanasheria mkuu, mhasibu mkuu, katibu wa kudumu, jaji mkuu na viongozi wa Tume kadha na kadhalika;
(e) Kudhibiti na kusimamia utumizi mbaya wa fedha za serikali kupitia uwekaji wa kamati za kufaa;
(f) Kushiriki katika uwekaji mikataba;
(g) Kuainisha na kuunda wizara, pale inapofaa; na
(h) Kuwa chama cha kisiasa kilicho na wabunge wengi ndicho kitakachounda serikali. Endapo hakutakuwa na chama cha walio wengi, itabidi vyama viunde serikali ya mseto.

*(v) Kanuni zifuatazo zitawale shughuli za serikali*

(a) Bunge litakuwa na uwezo usiokadiriwa kuhusu taratibu zake;
(b) Bunge litakuwa na kalenda yake kuhusu wakati wa kukutana, kupumzika na wakati wa kuvunjwa;
(c) Bunge litakadiria shughuli zake kupitia kanuni za bunge;
(d) Uanabunge uwe ni kazi kamili ya kila wakati;
(e) Mawaziri wote, isipokuwa waziri mkuu na manaibu wake watateuliwa kutoka nje ya Bunge;
(f) Wabunge watakuwa radhi kwa kuondolewa na wapiga kura katika maeneo yao ya uchaguzi;
(g) ili kumaliza upungufu wa uwakilishi wa wanawake na kuhakikisha ushiriki wa kufaa wa wanawake, walio wachache, walemavu na makundi mengine yaliyo na matumaini, mfumo wa kimseto wenye wiano wa wanachama utakubaliwa;
(h) angalau thuluthi moja ya wawakilishi itakuwa wanawake;
(i) Bunge liwe na uwezo wa kuiondoa serikali kupitia kura ya kutokuwa na imani;
(j) shughuli za bunge zitangazwe moja kwa moja katika televisheni na radio;
(k) kutakuwa na spika na Naibu wa spika kwa kila chemba;
(l) kutakuwa na afisi za maeneo bunge kwa kila mbunge;
(m) Bunge liwe na uwezo wa kupitisha kura ya kutokuwa na imani katika Rais;
(n) wabunge wa vyama vya upinzani wachague viongozi wa upinzani rasmi;
(o) viongozi wa upinzani watunukiwe nafasi za juu katika ngazi za afisi za serikali na wapewe heshima inayostahili katika sherehe za serikali;
(p) kiongozi wa upinzani achague mawaziri vivuli; na
(q) afisi ya Mhasibu Mkuu iwasaidie wabunge kuchunguza matumizi ya serikali na kuchunguza ubora na kufaa kwa matumizi haya.

(vi) *Kanuni zifuatazo zizingatiwe ili kudumisha ushiriki wa wananchi katika bunge:*

(a) pawe na mahitaji kuwa mapendekezo ya bunge yawasilishwe kwa makundi yanayofaa katika jamii ili yatolewe maoni;
(b) pawe na ombi la haki kwa Bunge kuweka sheria, kusikiliza malalamishi na kutoa habari (la mwisho linaweza kuwa kuwauliza wabunge kuuliza maswali yanayohusu waziri anayehusika, labda ikiwa swali linalohusika lina umuhimu wa kitaifa kwa jumla, au ikiwa mbunge wa eneobunge atakuwa hajalishughulikia suala lilo;
(c) kanuni ziwekwe ambazo zitayawezesha makundi na raia kutka kufika mbele ya kamati za Bunge ambazo zinajadili au zinachunguza masuala maalum. (jukumu la aina ya *amicus curiae*);
(d) kamati za bunge zitumike hata zaidi ili kudumisha ushiriki wa raia kupitia, kwa mfano, mawasilisho ya hadharani, jijini Nairobi na katika sehemu nyingine za nchi.
(e) Wabunge wahimizwe kutafuta usaidizi wa mashirika na wasomi kwa utafiti n.k.

## 11.4 <u>Mamlaka ya Nchi</u>

### 11.4.1 Kanuni za kijumla

#### *(a) Aina za Mifumo ya Mamlaka*

Kuna aina mbili kuu za mifumo ya mamlaka. *Mamlaka maalum ya Urais* ambapo Rais si mmoja wa baraza la wawakilishi; na *Mamlaka maalum ya bunge* ambapo kitengo cha mamlaka ni sehemu mojawapo ya bunge ikiwa na Mkuu wa Nchi mstahiwa.

Katika *mamlaka maalum ya Urais*, mamlaka ya juu yamo katika Rais ambaye:

- Si mbunge bali anateuliwa moja kwa moja na wananchi.
- Ana awamu maalum ya kuwa afisini, ambayo haitabadilishwa na bunge isipokuwa kupitia utaratibu uliotiliwa masharti ya kutenguliwa.
- Kutaja na kuwaelekeza wajumbe wa serikali yake ambao pia si wabunge.

Katika *mamlaka maalum ya Bunge*, Bunge ndilo lina mamlaka ya juu –

- wajumbe wote wa serikali pia ni wabunge;
- Rais wa Nchi au mfalme hutekeleza majukumu ya nchi ya uwakilishi na kwa hivyo kubainisha ugawaji wazi wa madaraka;
- chama kilicho na wengi katika bunge baada ya uchaguzi huunda serikali na kiongozi wake huchukua jukumu la Mkuu wa Serikali; na
- mawaziri hutekeleza majukumu maalum na wanatakikana kuaminiwa na Bunge.

Tofauti kuu baina ya mfumo wa Bunge na wa Urais ni:

- Katika mfumo wa Bunge, hakuna kutengana kwa wazi baina ya kitengo cha mamlaka na bunge jinsi ilivyo katika mfumo wa Urais;
- Kuna vipimo na visawazishi vingi katika mfumo wa urais, ingawa kuna uwajibikaji wa serikali kwa bunge unaoendelea katika mfumo wa bunge kwa sababu Waziri Mkuu na Mawaziri huhudhuria Bunge na inabidi watetee sera zao na pia wanaweza kupigiwa kura ya kutokuwa na imani;
- Mawaziri ni wabunge katika mfumo wa bunge ilhali katika mfumo wa Urais mbunge hawezi kuwa waziri isipokuwa kama atajiuzulu;
- Katika mfumo wa Uraiss, kuna awamu maalum iliyowekwa kwa kitengo cha mamlaka na cha bunge;
- Katika mfumo wa bunge, Mkuu wa Nchi si Mkuu wa Serikali; na
- Katika mfumo wa Urais, mkuu wa serikali huchaguliwa moja kwa moja lakini atateuliwa katika bunge. Mkuu wa serikali katika mfumo wa bunge

atashiriki madaraka na mawaziri wengine lakini ndiye mwenye madaraka makuu katika mfumo wa Urais.

Aina nyingine ya madaraka ni ile inayoshirikisha sifa za aina hizi mbili na huitwa *mseto wa mamlaka ya Urais na Bunge*. Nchi nyingi zinapatikana katika kategoria hii katika mfumo huu, Rais anachaguliwa na kura ya walio wengi na anaweza kuwa au asiwe mbunge. Katika hali nyingi, Rais ana uwezo wa kuvunja bunge.

Ni kawaida katika mfumo wa mseto kuwa Rais anashughulika moja kwa moja na mawaziri, ambapo anaweza kuwateua au kuwaondoa kadri apendavyo. Baraza la mawaziri hutokana na wabunge wanawajibika kuaminiwa na bunge na wanaweza kuondolewa kibinafsi endapo mswada wa hoja ya lawama utapitishwa. Wakati mwingine, kuna waziri mkuu ambaye ni mbunge na anakuwa Mkuu wa Serikali. Yeye pia anawajibika kuaminiwa na bunge na Rais.

Katika hali nyingine, kitengo cha mamlaka kinaweza kuundwa katika mpango wa kugawana madaraka ambamo makundi tofauti ya kisiasa yanawakilishwa. Hali hii hutokea pale ambapo hakuna chama kilicho na washiriki walio wengi katika bunge kinachoweza kuunda serikali. Hatimaye, vyama vya kisiasa vinavyokubaliana kuja pamoja na mseto wao huunda serikali, mbinu za ugawaji madaraka wa aina hii huzungumiziwa na makubaliano kufikiwa katika vyama vinavyohusika na mara nyingi huwa si jambo la kuzingatiwa kikatiba. Lakini, baadhi ya katiba hulizungumzia jambo hili.

***(b) Aina ya Madaraka ya Kitengo cha Mamlaka ya Nchi***

Kitengo cha mamlaka ya nchi ni kipengele cha serikali ambacho kinatimiza majukumu ya serikali kupitia utekelezaji wa sheria na sera. Sera za umma zinawekwa na kutekelezwa na kitengo cha mamlaka. Kitengo cha mamlaka kina jukumu la kusimamia mapato ya nchi, usalama wa ndani na nje, mahusiano yakigeni na utekelezaji wa sheria katika kazi zake muhimu. Kwa kiasi fulani, kitengo cha madaraka ndicho chombo kikuu zaidi nchini.

Madaraka ya mamlaka yamo katika uhuru wa nchi ambayo yanawakilishwa na Rais katika Taifa la kijamhuri au mfalme katika nchi ya kifalme. Yanaweza kugawanywa baina ya Rais and Waziri mkuu. Lakini, kiutendaji, hutekelezwa na kikundi kipana cha watu ambao wanashirikisha watu wanaosimamia idara kuu za serikali ikiwemo huduma za umma, majeshi, usimamizi wa wilaya na kwa kiasi fulani utawala wa wilayani.

Sifa za kitengo cha mamlaka zina athari kubwa kwa uwezo kinchotekeleza na mbinu kinazotumia katika dhibiti uwezo huo. Mamlaka maalum ya bung eyanaweza kujitolea kudhibitiwa kwa njia ya moja kwa moja na kuendeleza uwajibikaji wake kwa bunge kupitia taratibu za hoja za imani. Kwa upande mwingine, kitengo cha mamlaka cha mseto, kama ilivyo nchini Kenya, kinaonyesha hali ya juu ya Rais kulidhibiti bunge.

### 11.4.2 Kitengo cha Mamlaka katika katiba

***(a) Msingi***

Wakati wa uhuru, madaraka ya mamlaka ya serikali yaliwekwa katika malkia na utekelezaji kwa niaba yake ulifanywa na Gavana Mkuu. Kulikuwa na waziri mkuu aliyeteuliwa na Gavana mkuu kutokana na wajumbe wa ukumbi wa wawakilishi. Afisi za mawaziri ziliwekwa na Bunge. Baraza la mawaziri liliundwa na waziri mkuu na mawaziri wengine wote ambao waliwajibika kwa kumbi mbili za Bunge na ambao waliwajibika kunshauri Gavana mkuu katika utekelezaji wa majukumu yake. Gavana, kwa kushauriwa na waziri mkuu alikuwa na uwezo wa kuwateua makatibu wa Bunge ili wasaidie mawaziri katika utekelezaji wa majukumu yao. Palikuwa na katibu wa Baraza la mawaziri ambaye afisi yake ilikuwa katika Huduma za Umma na ambaye alitakikana kiutawala kuendesha shughuli za afisi za Baraza la mawaziri jinsi ilivyoelekezwa. Madaraka ya juu katika maeneo yalitekelezwa na kile kilichojulikana kama

kamati ya vitengo na fedha ambayo ilikuwa kamati iliyowekwa na Baraza la Kieneo.

Rais wa kieneo aliongoza kamati hii na Makamu wa Rais aliyeteuliwa na Baraza la Kieneo iliyokuwa na madaraka ya kuweka kamati nyingine kwa usimamizi wa kufaa wa shughuli za eneo.

Ni muhimu kufahamu kuwa, asasi ya Urais ni chombo kilichobuniwa mnamo 1964 wakati wa marekebisho ya Kwanza ya Katiba (sheria Na. 28 ya 1964 ya tarehe 24 Novemba, 1964). Kwa kipindi cha 1964 hadi 1969 ukumbi wa wawakilishi ulimteua Rais. Hali hii ilibadilika katika Rekebisho ya Kumi (sheria Na. 45 ya 1968 ya tarehe 12, Julai 1968) ambayo iliweka misingi kuwa, kuanzia hapo Rais angechaguliwa moja kwa moja na wapiga kura wa taifa.

Kuna maoni muhimu yanayoweza kutolewa kuhusu kitengo cha mamlaka wakati wa uhuru. Kwanza, uwezo uliotekelezwa na Kitengo cha Mamlaka ulikuwa wa aina tofauti lakini uliathiriwa baada ya utaratibu wa ushauriano na ama Baraza la Mawaziri au maafisa wengine huria wa kikatiba. Mwelekeo wa upande mmoja ambao umesheheni katika mamlaka ya Rais katika katiba ya sasa ni matokeo ya kuchongachonga kulioondoa vipande vidogo vidogo vya ulinzi wa katiba kufuatia marekebisho kumi na moja ambayo yametokea baina ya 1964 na 1969. Athari za marekebisho haya zilikuwa ni kuweka pamoja uwezo mkuu katika Urais na kusababisha uwezekano wa mwanya unaoweza kutumiwa kutumia vibaya au kutoheshimu madaraka.

***(b) Katiba iliyopo***

Sehemu 23 ya Katiba ya Kenya inampa Rais madaraka ya juu ya serikali ya Kenya, madaraka ambayo yanaweza kutekelezwa na watu wa madaraka ya chini kwake. Sehemu 4 – 21 zinaweka kitengo cha mamlaka ambacho kina Rais, Makamu wa Rais, Mawaziri na Mawaziri wadogo wote ambao ni wabunge. Baraza la Mawaziri linalowekwa katika sehemu 17 ni chombo kikuu cha kufanya

maamuzi katika Nchi na hutenda kazi kumshauri Rais katika utawala wa Kenya. Hata hivyo Rais hafungwi na maamuzi ya Baraza la Mawaziri. Baraza la Mawaziri linaundwa na Rais, Makamu wa Rais na Mawaziri.

Kitengo cha mamlaka jinsi kinavyowakilishwa na Urais kinatekeleza madaraka makuu. Baadhi ya madaraka ni kuwa, Rais –

- Ndiye Amri Jeshi mkuu wa majeshi yote;
- Ana wajibu wa kubuni na kufuta afisi za huduma ya umma;
- Ndiye mkuu wa vyuo vikuu vyote vya umma;
- Huwateuwa wanachama wa utawala ikiwemo katibu wa kudumu;
- Kumteua mwanasheria mkuu na mshauri mkuu wa mambo ya kisheria ambao afisi zao ziko katika Huduma za Umma;
- Humteua Mhasibu Mkuu na Mdhibiti Mkuu;
- Huwateua mabalozi au wawakilishi wakuu wa Kenya katika nchi nyingine;
- Hunteua Jaji Mkuu na majaji wengine wa Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani;
- Humteua kamishna wa Polisi na wakuu wengine wa kikosi cha Polisi;
- Hutekeleza uwezo wa kuhurumia katika Jamhuri;
- Ana uwezo wa kuahirisha na kuvunja bunge;
- Kutoa idhini ya kukubali sheria zote zinazoundwa na Bunge na ana uwezo wa kiasi juu ya sheria kadha;
- Huteua wanatume wa Tume ya Uchaguzi;
- Huteua wantume wa Tume ya Huduma za Umma na watumishi wakuu wa umma;
- Hawezi kufanyiwa mashtaka ya kisheria wakati akiwa afisini;
- Anawajibika, kama mkuu wa nchi kuhutubia Bunge wakati wowote anapoamua, na kama mkuu wa serikali anahudhuria mikutano yote ya

vikao na kushiriki katika shughuli za Bunge ikiwemo kupiga kura kwa masuala yote yanayohitaji kupigiwa kura.

Pamoja na katiba, sheria zingine zimemtunukia Rais mamlaka ya aina tofauti. Kwa mujibu wa sheria ya Tume ya Uchunguzi (sura 102), Rais ana mamlaka ya kuunda, wakati wo wote, Tume ya Uchunguzi ili izingatie masuala muhimu ya umma, na kuteua washika afisi za Tume hizo. Sheria ya Ardhi ya Serikali (sura 280) inampa Rais mamlaka maalum ya kutoa kama msaada au mamlaka ya shamba lolote, matarajio au haki katika au kuhusu ardhi ya serikali ambayo haijatenganishwa.

### 11.4.3 Mamlaka ya Nchi katika Katiba Nyingine

Uchanganuzi wa mifumo ya mamlaka ya nchi umetolewa. Jambo linalohitaji ufafanuzi ni namna Katiba nyingine zinavyoshughulikia masuala kama:

- aina na waliomo katika Mamlaka ya Nchi;
- kugawa madaraka na vyombo vingine vya serikali; na
- uwajibikaji wa vyombo vya Mamlaka ya Nchi.

Kuhusu aina ya Mamlaka ya Nchi, mataifa mengi kama Australia, Canada, Ujerumani, Udachi, na Uingereza yana kiongozi wa nchi Mstahiwa (kwa jina lolote) na kiongozi wa serikali mwenye uwezo (anayeitwa Waziri Mkuu). Katika mataifa haya, kiongozi wa nchi mara nyingi ni malkia/mfalme aliyerithi ilhali kiongozi wa serikali na mawaziri wamechaguliwa Bungeni. Katika mataifa kama Marekani, Nigeria na El Salvador, Rais na Baraza la mawaziri si Wabunge. Mifumo mseto, ambapo kiongozi wa taifa anagawa madaraka yake na kiongozi wa serikali (kama Ufaransa) na ambapo anamteua Waziri Mkuu (kama Tanzania na Uganda).

Masuala ya kugawa madaraka, hasa ya Bunge na Mahakama, na uwajibikaji hushughulikiwa na mfumo imara wa vipimo na visawishi. Hivi ni pamoja na Bunge kuidhinisha uteuzi wa Mamlaka ya Nchi, kutenguliwa kwa kiongozi wa taifa/serikali, marekebisho ya kitendo cha Mamlaka ya Nchi na Mahakama. Hizi ni sifa zinazopatikana katika nchi nyingi zinazoongea Kiingereza.

### 11.4.4 Waliyoyasema Wananchi

Yale ambayo wananchi waliiambia Tume

*(i)* *Kuhusu mfumo wa serikali walisema –*

(a) kuhakikisha kuwa kila chombo kina uhuru kutokana na kingine;
(b) ilipendekezwa na wananchi wengi kuwa, katiba ichukue mtazamo wa mfumoutawala wa bunge ukiwa na Waziri Mkuu kama Mkuu wa Serikali na Rais mstahiwa kwa kiasi kikubwa ambaye atakuwa mkuu wa Nchi;
(c) Rais atachukua nafasi ya Mzee wa Nchi kama ishara ya umoja wa Taifa na kitambulisho. Ili kudumisha nafasi hii, umri wa chini wa mtu anayestahili uliongezwa kutoka miaka 40 hadi miaka 50 na baina ya miaka 70 na 75 kama umri wa juu; na
(d) Pawe na nafasi ya kunyumbulika katika katiba, ili kuruhusu serikali za mseto au ushirikiano wa uwezo.

*(ii)* *Kuhusu afisi ya Rais walisema –*

(a) Rais asiwe nje ya sheria, wengi walisisitiza. Wasiwasi wao ulikuwa ingewezekana kumshtaki Rais kwa hatia akiwa afisini. Katika muktadha huu, ilipendekezwa kuwa katiba iweke misingi ya kuondolewa kwa Rais endapo atapatikana na ukikukaji wa kanuni;
(b) Mamlaka ya Rais yapunguzwe. Wakenya walihisi kuwa Rais asiwe na uwezo wa pekee wa kuteua maafisa wakuu wa serikali. Kwa hakika,

ilipendekezwa kuwa, katika muktadha wa aina nyingi za uteuzi. Bunge liweze kuchunguza kwa makini. Kwamba Rais asiwe na uwezo wa kuamua tarehe za uchaguzi lilikuwa jambo lililopendekezwa na la kuwatia wasiwasi Wakenya wengi;

(c) Wakenya walishauri kuwa mamlaka ya Rais na ya Waziri Mkuu yafafanuliwe katika Katiba;

(d) Ilipendekezwa kuwa Rais asiwe mbunge;

(e) Rais achaguliwe moja kwa moja. Kwa mujibu wa hili, ilipendekezwa kuwa ni lazima mgombezi apate zaidi ya asilimia hamsini ya jumla ya kura sahihi zinazotolewa kote nchini. Pale ambapo atakayepata, pawe na uamuzi mkata baina ya wagombezi wawili wanaongoza ambapo mwenye atapata wingi wa kura ndiye atakeyetangazwa kuwa mshindi;

(f) Rais anatakikana kuungwa mkono na asilimia 25 kutoka katika mikoa mitano. Hili lilikuwa pendekezo ambalo halikuafikiwa na wote. Wengi waliliunga mkono ingawa wengine waliona kuwa ingalikuwa angalau asilimia ishirini katika mikoa minne ilhali wengine walipendekeza ingekuwa asilimia hamsini ya kuungwa mkono katika taifa zima ndiyo ingetosheleza;

(g) Licha ya kisomo na suala la umri, Rais awe mtu aliyeoa/aliyeolewa na familia thabiti na tabia nzuri.

(h) Rais awe na kisomo cha kiasi ili aweze kusimamia shughuli za nchi. Wengi walikuwa na maoni kuwa Rais awe na kisomo cha shahada ya kwanza ya chuo kikuu;

(i) Makamu wa Rais, achaguliwe moja kwa moja na wananchi kama mgombezi mwenza wa Rais katika uchaguzini;

(j) Baadhi ya Wakenya walipendekeza kuwa Rais na Makamu wa Rais wasiwe wabunge.

*(iii)* *Kuhusu wizara za serikali walisema –*

(a) idadi ya wizara za serikali ipunguzwe hadi kumi na tano na ipitishwe na Bunge.
(b) Mawaziri wawe wanaostahili ili kutosheleza majukumu yao ya wizara. Palikuwa na maoni ya pande zote kuhusu iwapo wajumbe wa serikali wangeweza pia kuwa vitengo vya Bunge.

### 11.4.5 Uchanganuzi

Ni wazi kuwa kile ambacho wananchi walikitaka ni mfumo wa kimseto ambao ni tofauti kabisa na vitengo na muundo wa mamlaka uliopo katika Katiba ya sasa. Mfumo wa bunge, ambao unapendekezwa, unatoa misingi ya uongozi wa pamoja na uwajibikaji mwema wa serikali. Isitoshe, unaashiria pia kuwa mamlaka yatatenganishwa hata zaidi kuliko jinsi ilivyo katika mifumo ya kibunge kwa kanuni kuwa huenda mawaziri wasiwe wabunge. Pendekezo hii linatambua hali kuwa Wakenya wengi wametoa maoni ya kupendelea mfumo wa aina ya kibunge. Mfumo maalum wa Urais ambamo mamlaka yote yanawekwa katika Rais huenda usisaidie katika kuushinda utamaduni wa kimabavu. Afisi hiyo, ya Rais, itaendelea kutiliwa makini na uchaguzi, kiini cha mpangilio wa chama na chanzo cha utekelezaji wa mamlaka yote kwa mujibu wa historia ya Kenya, Urais wenye uwezo utalemaza hali ya kufaa (ikiwa si urasmi) ya utenganishaji wa mamlaka na mfumo wa vipimo na visawazishi au ugawaji bora wa mamlaka. Utaendelea vile vile kueneza siasa za kikabila, kwa sababu kila kabila litatoka kuwa na mmoja wa jamii yao akishilikia afisi hiyo. Utadumisha uoga wa kukuza ukabila ikiwa ni pamoja na ubinafsishaji wa mamlaka ya nchi. Rais wa kupendelea upande mmoja atahatarisha dhima ya umoja wa kitaifa.

Sambamba na haya, mfumo maalum wa ubunge huenda usitosheleze mahitaji ya Wakenya. Unaweza kuhamisha mamlaka mengi kwa Waziri Mkuu na kupunguza dhibiti wa wananchi kuhusu uteuzi wa kiongozi wa serikali. Ushwari ambao mara nyingi unahusishwa na mfumo wa Urais unaweza kuwa mgumu kutimiza, hasa kwa kuzingatia utata wa siasa za bunge na uwezekano wa hoja za kutokuwa

na imani. Mfumo unaotekelezwa vizuri wa vyama ni muhimu katika kufaulu kwa mfumo wa ubunge. Mfumo wa ubunge, ukiwa na Baraza la Mawaziri kama chombo kikuu cha kufanya maamuzi, utaruhusu ukataji kauli wa kushirikiana na pia kuvumilia matarajio ya kutofautiana; ikiwemo matarajio ya wingi wa makabila. Utakuwa pia mfumo wa kuwajibika kwa vile uhifadhi wa mamlaka na serikali utategemea uwezo wake wa kuhakikisha kuungwa mkono na Bunge.

Kwa jumla, aina ya mfumo wa ubunge ndio utakaoweza kutimiza kanuni za mfumo wa serikali unaoelezwa hapo juu. Malengo ya marekebisho yatakuwa ni kuibua kitengo cha mamlaka ambacho ni kisawazishi, kilicho na vipimo vya ndani. Kuweka mfumo wa pamoja wa serikali ambayo itawezesha ujenzi wa mseto katika misingi ya ukabila. Itavuka mipaka ya maeneo ya kijiografia na kuweka misingi ya serikali inayofaa na ya kuwajibika kupitia utenganishaji wa kiasi kikubwa wa mamlaka. Kuna vitu vitatu vikuu vya urekebishaji.

Kwanza, kiongozi wa Taifa, Urais, sharti awe zaidi ya kiongozi mstahiwa. Ni lazima na mamlaka ya kiasi. Lakini ni lazima mamlaka hayo yawe na kipimo. Mamlaka ya kupindukia yatavuruga usawazishi wa ndani katika kitengo cha mamlaka. Jukumu kuu la Urais litakuwa ni kuashiria umoja wa kitaifa na kukuza utangamano wa kitaifa, usalama wa Taifa na ulinzi wa katiba – na kuhakikisha shwari ya kiutawala.

Pili, Baraza la Mawaziri litatokana pakubwa nje ya Bunge ili kukuza umakini wa serikali na utenganishaji wa mamlaka Mawaziri watahitaji kuwa wanaostahili nyadhifa zinazotolewa kwao na wala si kushinikizwa na mizigo ya shughuli za maeneobunge au kuathirika kutokana na migongano ya maslahi ya kitaifa na ya eneobunge. Wataweza kujitolea muda na nguvu zao kwa wizara zao. Lakini, ili kuhakikisha uwajibikaji wa wizara kwa Bunge, naibu wa mawaziri watatarajiwa kutekeleza wadhifa katika majukumu ya Bunge na kueleza na kulinda sera za wizara. Mawaziri wenyewe watahitajika kufika mbele ya Bunge ili kueleza sera

kuu na kujibu maswali pale ambapo Bunge litawahitaji kufanya vile. Patakuwa na uhusiano wa karibu na kamati za Bunge zinazofaa.

Tatu, ni lazima Bunge liimarishwe, likiwa na uthibiti juu ya kalenda yake na rasilmali, na uwezo wa kutekeleza usimamizi mkubwa na uwajibikaji wa serikali. Ili kuyatimiza haya, itabidi wabunge waweze kuunda sheria kila wakati, na hali ya kuwa wabunge ichukuliwe kama kazi bali si kipandio cha kufikia uwaziri au aina ya kupandishwa cheo. Ni muhimu kutambua kuwa mfumo wa ubunge, kinyume na ilivyo katika mfumo wa Urais wa Marekani, haiwezekani kuwa na udhibiti mkali wa Bunge kuhusu kuvunjwa kwake na tarehe za uchaguzi mkuu. Jambo muhimu la mfumo wa ubunge ni haki ya wabunge kuondoa kitengo cha mamlaka au angalau kulazimisha uchaguzi mkuu kwa kufuata kura ya kutokuwa na imani.

Hali ilivyo kote ulimwenguni ni kuwa kitengo cha Mamlaka ya Nchi kinatawala Bunge, kikiwa kipengele cha utawala, na mapato yanayopitia mikononi mwake pamoja na urasimu unoihudumia utaongezeka. Hali hii itasababisha kuwepo upungufu katika demokrasia, ambamo vyombo vya bunge vinavyochaguliwa vitazidi kupungukiwa katika kuchukua sheria zao na kuanzisha sera, au kuchunguza na kuthibiti kitengo cha mamlaka. Katika nchi nyingi, ikiwemo Kenya, wanasiasa wachache huona kazi zao kuwa tu wabunge au wanasiasa sugu wanaojitolea kwa manifesto za vyama vyao au kwa manufaa ya maeneobunge au Nchi. Huliona Bunge kama kipandio cha kufikia uwaziri au afisi nyinginge za juu. Hatimaye, hawatilii makini kazi ya Bunge. Matokeo ya mwenendo huu ni kuwa mapendekezo kadha yametolewa ili kuimarisha jukumu na uwezo wa Bunge katika sehemu nyingi za ulimwengu.

### 11.4.6 Mapendekezo

Kwa hivyo Tume inapendekeza kuwa muundo mpya uanzishwe ifuatavyo: -

*(i)* *Rais*

(a) ya kwamba mgombezi wa Urais awe na sifa zifuatazo –

- umri wa chini miaka 35 na wa juu miaka 70;
- awe na shahada ya chuo kikuu kutoka katika chuo kikuu ch kutambulika au awe na mazoea kama mbunge au kiongozi;
- Awe mtu mwenye uadilifu wa hali ya juu;
- Rais atahudumu kwa muda usiozidi awamu mbili za miaka miwili miwili;
- Rais hatakuwa mbunge.

(b) wagombezi wa Urais wachaguliwe moja kwa moja na wananchi kupitia upigaji kura kwa wote, na

- wagombezi wa Urais wateuliwe (wadhaminiwe) na wasajiliwe na vyama vya kisiasa au wagombee wagombezi wa Urais huria.
- Mgombezi wa Urais anayepata asilimia (20%) ishirini ya kura zinazopigwa katika angalau mikoa mitano na jumla ya asilimia hamsini (50%) ya kura zote halali zinazopigwa kote nchini atatangazwa kuwa mshindi. Endapo hakutakuwa na mshindi wa moja kwa moja, kutakuwa na uamuzi mkata katika muda wa mwezi mmoja baina ya wagombezi wawili watakaokuwa na kura za juu zaidi, ambapo mgombezi atakayepata kura nyingi atatangazwa mshindi.

(c) Rais atakuwa na, na pia atatekeleza majukumu yafuatayo –

- aashirie na kukuza umoja wa taifa. Atetee uadilifu wa nchi;

- baada ya kuchaguliwa, akate uhusiano na vyama vya kisiasa. Hatashikilia afisi yoyote ya kuchaguliwa au kuwa mwanachama mtendaji wa chama chochote cha kisiasa;
- kulinda uhuru wa taifa na heshima ya kieneo;
- kulinda usalama wa Katiba na kudumisha utawala wa sheria;
- kukubali miswada kabla ya kufanywa kuwa sheria;
- atakuwa na uwezo wa kuitaka mahakama ya juu ushauri kuhusu masuali ya kikatiba;
- atasimamia ulinzi wa kitaifa Baraza la ulinzi;
- atatangaza hali ya hatari baada ya kushauriana na Waziri Mkuu;
- atakuwa na uwezo wa kutangaza vita baada ya kushauriana na Baraza la mawaziri na Baraz la usalama wa kitaifa kwa kutegemea ukubalifu wa Bunge;
- atateua majaji kwa mujibu wa mapendekezo ya Tume ya Huduma za mahakama na idhini ya Bunge;
- ataidhinisha mikataba ambayo imekubaliwa na serikali na kukubaliwa na Bunge; na
- ataongoza ufunguzi wa Bunge.

(c) Rais –

- atafurahia mamlaka mengine kadri yatakavyotokana tu na Katiba;
- ataweza kutenguliwa kwa ukosefu wa nidhamu wa kupindukia, ukiukaji wa Katiba na hujuma za kiuchumi.

*(ii) Makamu wa Rais*

(a) kila mgombezi wa Urais atamteua Makamu wa Rais ambaye atakuwa mwenzi wake katika ugombezi;

(b) Makamu wa Rais atamsaidia Rais katika utekelezaji wa majikumu ya Urais kwa kutegemea kanuni za katiba;

(c) Endapo patatokea kifo, utenguzi au kujiuzulu kwa Rais, makamu wa Rais, kwa kukubaliwa na Bunge atachukua hatamu za afisi ya Rais kwa muda uliosalia wa awamu ya Rais. Ikiwa muda uliosalia wa awamu unazidi miaka miwili na musu, kipindi hicho kitachukuliwa kama awamu ya kwanza ya Urais wa mtu huyo atakayekuwa ameteuliwa na Rais;

(d) Ikiwa afisi ya makamu wa Rais, itakuwa tupu, Rais atmateua makamu wa Rais kutokana na wanabunge waliochaguliwa;

(e) Endapo patatokea kifo cha Rais na makamu wa Rais, Spika atashikilia wadhifa wa Rais; na

(f) Makamu wa Rais atashikilia wadhifa wa Rais wakati ambapo Rais ameondoka nchini.

*(iii) Baraza la Mawaziri*

(a) Waziri Mkuu

- Waziri Mkuu atakuwa mwenye mamlaka makuu – Kiongozi wa Serikali ya Kenya na Kiongozi wa Baraza la Mawaziri.
- Waziri mkuu atawajibika kwa Bunge.
- Waziri Mkuu atakuwa kiongozi wa chama kikubwa cha kisiasa katika Bunge au mseto wa vyama vinavyowakilishwa katika Bunge.
- Waziri Mkuu atatekeleza mamlaka yafuatayo.
    - Kuandaa na kutekeleza bajeti na sera za kitaifa.
    - Kutekeleza na kusimamia uundaji wa sheria.
    - Kuandaa na kutekeleza sheria za serikali.

- Waziri mkuu atakuwa menyekiti wa mikutano yote ya Baraza la mawaziri na atazidi kumfahamisha Rais Rushusu shughuli za serikali.
- Awamu ya afisi ya Waziri Mkuu itaendelea isipokuwa akistaafu, akifa au akiachishwa kazi.
- Bunge linaweza kumuondoa Waziri Mkuu kutoka afisini kwa kupitisha kura ya kutokuwa na imani kwake.

(b) Manairbu wa waziri mkuu –

- Patakuwa na manaibu wawili wa waziri mkuu watakaoteuliwa na Rais na kuidhinishwa na bunge.
- Majukumu ya manaibu hawa ni kumsaidia waziri mkuu katika utekelezaji wa majukumu yanavyoainishwa na katiba.

(c ) Mawaziri

- Patakuwa na mawaziri wa serikali ya Kenya;
- Afisi za mawaziri hazitapungua saba na hazitazidi kumi na tano;
- Mawaziri wa serikali ya Kenya hawatakuwa wabunge lakini watalazimika kuhudhuria shughuli za Bunge kama wanachama kwa wadhifa wao;
- Mawaziri watakuwa wanastahili kitaaluma kwa wizara ambamo wanateuliwa; na
- Mawaziri watateuliwa na Rais jinsi watakavyoteuliwa na waziri mkuu na kuidhinishwa na Bunge;

(d) Mwanasheria Mkuu

- Patakuwa na mwanasheria mkuu atakayeteuliwa na Rais kwa kuidhinishwa na Bunge;

- Mwanasheria mkuu atakuwa mshauri mkuu wa kisheria wa serikali;
- Majukumu ya mwanasheria mkuu yatakuwa pamoja na –
    - kuwakilisha serikali mahakamani au katika taratibu nyingine za kisheria;
    - kuweka kandarasi, mikataba, makubaliano n.k. ambayo yanaihusisha serikali.
    - majukumu mengine ya aina ya kisheria kadri itakavyo pendekezwa kwake na Waziri Mkuu.

(e) Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma

- Patakuwa na mkurugenzi wa mashitaka atakayeteuliwa na Rais kufuatia mapendekezo ya Tume ya Huduma za Umma;
- Majukumu ya mkurugenzi wa mashtaka ni pamoja na-
    - kuongoza uchunguzi wa aina ya jinai;
    - kuanzisha taratibu za mashtaka ya jinai;
    - kushikilia na kuendelea na mashtaka yoyote. n.k.

## 11.5 <u>Mahakama</u>

### 11.5.1 Kanuni za kijumla

Mahakama hutimiza majukumu ya msingi ya kudumisha ukatiba na usheria. Jambo muhimu sana ya mahakama ni watu wanaoihudumia – wanasheria majukumu makuu ya wanasheria ni –

- kufanya ufafanuzi wa kimamlaka wa sheria bila kuelekezwa au kulazimishwa na kitengo cha mamlaka wala kingine chochote;
- hakikisha ukuu wa katiba kwa kutangaza sheria batili ambazo haziandamani na Katiba;

- kukuza kaida za kikatiba na kusaidia kuzielekeza katika jamii inayobadilika na hali za kiuchumi. Katiba ya marekani imebadilishwa mare chache kiasi kwa sababu mahakma zimetoa ufafanuzi mpya kwa kanuni zake kwa kuandamana na maadili yanayobadilika;
- kutoa maelekezo kwa vyombo vya serikali, mashirika ya binafsi na watu binafsi kuhusu kanuni za katiba na sheria;
- kushinikiza heshima kwa taratibu na maadili ya kikatiba, kwa kushawishi na pia uamuzi wa kitaaluma;
- kuweka wabunga na kitengo cha mamlaka katika madarka yao ya kisheria, na kuzuia udhahania na tartibu zisizokuwa za haki katika serikali na kudumisha kanuni za maamuzi mema;
- kulinda haki na uhuru wa wananchi pamoja na kulinda maslahi ya umma;
- kutatua mizozo ya kisheria ambayo inaelekezwa kwake; na
- katika kutatua mizozo kwa mujibu wa sheria, na kwa jumla kutekeleza kanuni za usheria au utawala wa sheria, kusaidia katika kuweka shwari na kudumisha amani, na kuweka uwezekano wa kubashiri wa wananchi ili kuweka mikataba na makubaliano mengine.

Baadhi ya masuala maalum kuhusu uanasheria yanaweza kubainishwa hapa. Haya ni uhuru wa mahakama, uwajibikaji, uadilifu na ufikiaji wa haki.

Uhuru wa mahakama unahusisha vitu viwili vikuu: -

- *Uhuru wa Kimaamuzi:* yaani mahakama inatakikana kuwa huru kutokana na athari za kutoka nje. Hili litaiwezesha mahakama kutoa uamuzi usiopendelea na ulio elekevu katika kesi maalum. Sheria na ni sheria tu

ambayo inastahili kuyaongoza mahakama katika kuamua kuhusu masuala yaliyo mbele yake.

- *Uhuru wa Kitaasisi:* yaani mahakama ni chombo huria cha serikali na kinalingana vya serikali. Mahakama haitakikani kupata maagizo au kudhibitiwa na chombo kingine chochote cha serikali. Hili lina athari maalum kwa uteuzi na uondoaji wa maafisa wa mahakama, usalama wa awamu, uhuru wa kifedha kwa mujibu wa utengaji wa bajeti na uzingatiaji wa malipo na nidhamu ya kimahakama.

Ni lazima mahakama yaawajibike kwa jamii kwa jinsi ambavyo yanatekeleza mamlaka yao ya kisheria. Yafuatayo ni baadhi ya mambo ya kuzingatiwa kwa mujibu wa uwajibikaji wa mahakama.

- Kanuni za juu za haki ya kimaumbile na matumaini ya utu wa kibinadamu yanawahitaji majaji kutekeleza na kutimiza haki kwa njia elekevu. Vielelezo vya kisheria na ukuu wa kikatiba unabaki vigezo muhimu vya uhuru wa kimaamuzi.
- Utaratibu unaofaa wa rufani utahakikisha kuwa utekelezaji wa mamlaka ya kimahakama unazidi kuhakikiwa na wengi wao.
- Utangazaji wa taratibu za kimahakama na maamuzi huiwezesha mahakama kuhakikiwa na kuchunguzwa na umma.
- Uondoaji wa mahakimu na taratibu za kinidhamu zitazidi kuwa muhimu za kuhakikishia maafisa wa mahakama walipotoka wanazingatiwa. Kufaa kwa mifumo ya aina hii ni kipengele muhimu cha uwajibikaji.

Maadili ya kikanuni na utendaji kazi ya wanasheria maalum katika mahakama yanayopaswa kuutia imani umma. Hili linahusisha yafuatayo –

- umilisi, makini na matokeo ya majaji;
- sharti kuwa majaji wanatarajiwa kutimiza viwango vya juu vya umilisi wa kimahakama kwa jinsi ambavyo wanahusiano na wanajamii wengine;

- sharti kuwa lazima wajiepushe na kushiriki ufisadi na maovu mengine;
- kuunda na kutii kanuni za kimahakama za uadilifu ili kuhakikisha tabia ya kuheshimika ya majaji kila mahali.

Mfumo wa mahakama unaotekeleza wajibu wake vizuri una lazima ya kuhakikisha kuwa unafikika kwa wote. Hili litahakikisha na kukuza usawa wa watu wote mbele ya sheria. Ufikiaji wa haki una masharti kadha, baadhi ambayo yanaweza kuainishwa ifuatavyo-

- Ufikiaji wa mahakama kimahali kwa wote ikiwemo walemavu;
- Suala la msaada wa kisheria kwa wale ambao hawawezi kugharamia ada za mahakama;
- Mbinu badala za kusuluhishia mizozo;
- Mipango ya elimu ya uraia;
- Teknolojia ya habari na utangazji wa mtukio ya mahakama.

### 11.5.2 Mahakama na Katiba

#### *(a) Msingi*

Katiba ya Uhuru ilitoa msingi wa mahakama isiyopendelea na iliyo huru ambayo iliundwa na Mahakama za Chini, Mahakama ya Juu, Mahakama ya Rufani na Kamati za kimahakama za Ukumbi wa mamwinyi

.

(a) *Mahakama za Juu za Kurejelewa* – Mahakama ya Juu iliwekwa na uasili na mamlaka juu ya raia na jinai yasiyowekewa mipaka. Mahakama hii pia ilishughulikia masuala ya ufafanuzi wa kikatiba na masuala ya kuhusiana na utekelezaji wa haki za msingi. Wanachama wa mahakama walikuwa Jaji Mkuu na majaji wengine mashuhuri. Jaji mkuu angeteuliwa na Gavana mkuu kwa kushauriana na waziri mkuu ambaye alishauriana pia na marais wote wa mabaraza ya kimaeneo,

anglau wanae wao walitakikana kumuunga mkono mgombezi. Gavana mkuu aliwateua majaji wengine baada ya kushauriana na Tume ya Huduma za Mahakama.

Idadi ya majaji na awamu zao zilibainishwa na Bunge. Kulikuwa na taratibu za kuwaondoa endapo Gavana Mkuu, Rais wa Baraza la Eneo au Jaji Mkuu angetoa wasilisho kwa mujibu huu. Katika muktadha huu, Kamati ya Mahakama iliundwa. Tume ya Huduma za Umma, kwa mujibu wa Jaji Mkuu na Jaji Mkuu kwa mujibu wa majaji wengine mashuhuri waliwateua wanakamati.

Katiba pia ilitazamia Mahakama ya Rufani ya Kenya kusikiliza rufani kutoka Mahakama ya Juu kuhusu mambo yote ikiwemo ufafanuzi wa Katiba na utekelezaji wa haki na uhuru wa msingi. Ilitazamiwa pia kuwa mahakama za rufani za kimaeneo zingesikiliza masuala yaliyoelekezwa kwake kutokana na nchi wanachama waliohusika. Mahakama ya Rufani ya Afrika Mashariki ilihudumu kama Mahakama ya Rufani kwa nchi zote tatu za Afrika Mashariki hadi jumuiya ilipovunjwa mnamo 1977.

Kamati ya Mahakama ya Ukumbi wa Mamwinyi ilishughulikia rufani kutoka katika Mahakama ya Rufani ya Afrika Mashariki kuhusu masuala ya kikatiba na haki za msingi, masuala ya raia na jinai. Isipokuwa tofauti ilitokana na masuala yaliyotokana na haki na yale ambayo yalitanguliwa na idhini iliyotolewa na mahakama ambamo yalitokezea.

(b) *Mahakama za chini* – Mahakama nyingine zilizowekwa na Katiba zilikuwa mahakama za chini na mahakama za Kadhi. Idadi yao, mamlaka na taratibu zilipendekezwa na Bunge. Mahakama hizi

zilitarajiwa kutekeleza wajibu wao kwa kufuata Katiba lakini Mahakama ya Juu ilitekeleza jukumu na kiusimamizi juu yao.

(c) *Tume ya Huduma za Mahakama* – Katiba ya Uhuru iliweka misingi ya Tume huria ya Huduma za Mahakama. Uanachama wa Tume ulishirikisha jaji mkuu kama mwenyekiti, majaji wawili na watu wawili walioteuliwa kwa kufuata ushauri wa Tume ya Huduma za Umma.

Jukumu la msingi la Huduma hii lilikuwa kufanya uteuzi kwa mahakama, ikiwemo wasajili wa mahakama mbali mbali. Uamuzi wa Tume ulitegemea uamuzi wa wanachama. Tume ya Huduma za mahakama ilitoa pia ushauri kwa Gavana Mkuu kuhusu uundaji wa Tume ya Huduma za Jamii. Katika utekelezaji wa majukumu yake, Tume haikuwajibika kwa maelekezo ya mtu yoyote wala udhibiti wowote.

Sifa za uhuru wa mahakama zilikuwa mahakama ndiyo mpatanishi wa mwisho wa masuala ya kikatiba. Wafanyi kazi wake walifurahia usalama wa awamu na taratibu za uteuzi zilikuwa ngumu kiasi cha kuhakikisha umilisi katika watu walioteuliwa kuwa majaji.

***(b) Katiba Iliyopo***

Katiba ya sasa inatoa misingi ya masuala kadha kuhusiana na mahakama –

*(i) Mahakama za juu za kurejelewa*

Mahakama hizi zinaanzisha Mahakama Kuu na kutoa mamlaka yasiyokadiriwa ya masuala ya raia na jinai. Inatoa misingi kuwa idadi ya majaji katika mahakama hiyo hawatapungua kumi na mmoja kwa kutegemea Bunge ambalo litaweka kanuni kwa majaji wengine (sehemu 60). Maelezo ya ndani yanayohusiana na mpango, utekelezaji

wa mamlaka na taratibu za mahakama yanatolewa katika sheria ya usimamiaji haki ya sheria za Kenya.

Utaratibu wa kuwateua majaji umebainishwa. Rais anateua Jaji Mkuu. Rais kwa kushauriwa na Tume ya Huduma za Mahakama (Ibara 61) anateua majaji hao wengine. Kanuni za kuwaondoa kutokana na ugonjwa au upotofu wa nidhamu zinatanguliwa na kuanzishwa kwa mahakama maalumu na Rais, kutokana na ushauri wa Hakimu Mkuu, kwa kutafakari suala na kumpa taarifa kuhusu suluhisho.

Katiba inalipa bunge uwezo wa kuamua umri wa kustaafu kwa Majaji. Baada ya hapo, sheria ya Mahakama imeweka umri wa kustaafu kwa majaji kuwa miaka sabini na minne (74).

Katiba katika sehemu ya sitini na nne imeunda mahakama ya Rufani ya kushugulikia rufaa zitokazo kwa Mahakama Kuu kama zinavyoidhinishwa na sheria. Sheria halisi inayohusu utaratibu wa anayeomba rufaa, uwezo na usimamuzi wa mahakama unapatikana katika Sheria ya Mamlaka ya Rufaa.

*(ii) Mahakama za Chini*

Mahakama za chini chini yanaanzishwa na kuwa kusimamiwa na Mahakama Kuu. Kufuatia sharti hilo, Bunge lilipitisha Sheria ya Mahakama ya Hakimu (Sura ya kumi 10) ya Sheria za Kenya kufafanua mamlaka na utaratibu wa mahakama hizi. Viwango vya mahakimu ni: Mahakama za Mahakimu Wakuu wa Mahakama, Mahakama za Mahakimu Waandamizi Wakuu, Mahakama ya Hakimu Mkuu, Mahakama ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Mahakama ya Hakimu Mkazi na Mahakama za Mahakimu wa wilaya wa madaraja ya I, II na III.

*(iii) Kadhi Mkuu wa Mahakama ya Kadhi*

Mahakama ya Kadhi, Kadhi Mkuu, na Makadhi wengine, ni afisi za kikatiba zilizoanzishwa na Katiba. Kadhi hasa ni afisa wa sheria, jaji au hakimu anayesimamia mahakama ya Kiislamu yanayoitwa Mahakama ya Kadhi, ambapo sheria ya Kiislamu au

Sheria hutumika na kutegemea mamlaka ya mahakama wanaohusika wanafuata dini ya kiislamu. Lakini Kadhi si lazima awe kiongozi wa imani au Imam.

Katiba inahakikisha kuanzishwa kwa mahakama ya kadhi na idadi nyingine ya makadhi, wasiopungua watatu, kwa mujibu wa sheria. Mamlaka ya Kadhi Mkuu na yule Kadhi mwingine ni kushikilia Mahakama ya Kadhi kuwa na mamlaka katika Kenya kushughulikia maswali ya sheria ya Uislamu inayohusu hadhi ya mtu binafsi, ndoa, talaka au urithi katika mashauri mafupi ambapo wahusika wote wanakiri.

Kadhi Mkuu na Kadhi wengine huteuliwa na Tume ya Huduma za Mahakama.

Sifa za kuweza kuteuliwa katika afisi ya Kadhi (pamoja na Kadhi Mkuu) chini ya sehemu ya 66, sehemu- ndogo 2 ya Katiba ni kwamba lazima mtu awe muumini wa dini ya Kiislamu na kuwa na ujuzi wa sheria ya Kiislamu inayotumika kwa dhehebu au madhehebu yoyote ya Waislamu kama inavyotosheleza Tume ya Huduma za Mahakama.

Kufuatia kanuni za Katiba ya Kenya na kwa utekelezaji bora wa kazi za Kadhi, Bunge lilipitisha Sheria zifuatazo:

1. Sheria ya Mahakama ya Kadhi, (Sura 11;
2. Ndoa ya mtindo wa Mohammed na Sheria ya Usajilishaji wa Talaka, (Sura 55);
3. Ndoa ya mtindo wa Mohammed, Talaka na Sheria ya Urathi, (Sura ya156);
4. Sheria ya Urithi, (Sura 160).

Chini ya Sheria ya Mahakama za Kadhi, Bunge limeanzisha mahakama kumi na mbili. Sheria ya Mahakama za Kadhi zilizopitishwa mwaka wa 1967, awali ilianzisha mahakama sita za Kadhi, zikiwa chini ya Mahakama Kuu, nne zikiwa na mamlaka katika eneo la nchi iliyokuwa chini ya mamlaka ya nchi nyingine zamani; moja ikiwa Nyanza, Magharibi na sehemu za mkoa wa Bonde la Ufa, na ya mwisho kuwa na mamlaka juu ya wilaya za zamani Kaskazini za Garissa, Wajir na Mandera.

Rufani kutoka kwenye Mahakama ya Kadhi yaweza kuwasilishwa kwa Mahakama ya Kadhi Mkuu au katika Mahakama Kuu. Mahakama kuu itashughulikia ombi la rufaa pamoja na Kadhi Mkuu au Kadhi wengine kama wakaguzi. Maoni ya hawa Kadhi kama wakaguzi hayamfungi Jaji wakati wa uamuzi kuhusu rufaa, hasa kama hakubaliani na maoni yao. Ombi la rufaa pia lategemea Mahakama ya rufaa kutoka kwa Mahakama Kuu na katika Mahakama hiyo ya mwisho, Kadhi Mkuu au Kadhi mwingine ye yote hakai hapo hata kama ni mkaguzi.

Mahakama za Kadhi zilikuweko pwani mwa Afrika Mashariki hata kabla ya ukoloni wa Kiingereza. Nchini Kenya, zilikuwa mwambao uliotawaliwa na Sultani wa Zanzibar. Mnamo 1895, Sultani alitoa kibali kwa Uingereza kutawala eneo la maili kumi mradi tu waendelee kuheshimu mahakama ya Kadhi, pamoja na mambo mengine. Waingereza walifanya hivyo na wakatangaza himaya juu ya pwani wakati bara ilikuwa koloni. Sultani, hata hivyo, aliendelea kuwa na uhuru wa kutawala maili hizo kumi za pwani. Wakati kipindi cha kumalizika vita vya ukombozi na mwanzoni mwa mazungumzo ya kikatiba ya ukumbi wa Lancaster, 1961, hadhi na hatima ya maili kumi za Pwani ilirejeshwa. Waingereza wakapanga mazungumzo mbalimbali kwa wajumbe wa Sultani na wa koloni. Serikali ya Kiingereza na Sultan pia wakateua mwanatume, Bw. James R. Robertson, kutatalii suala hili kama eneo la maili kumi ya pwani litajiunga na Kenya huru au litajitenga, au litarudishiwa Zanzibar. Alipendekeza lijiunge na Kenya huru mradi tu serikali ya Kenya iheshimu mahakama ya Kadhi, pamoja na kanuni nyingine. Waziri Mkuu Jomo Kenyatta na Waziri Mkuu sharti (kwa niaba ya Sultan wa Zanzibar), wakaweka sahihi mkataba mnamo Oktoba 1963 kwa kuandikiana barua. Sulatani wa Zanzibar aliacha mamlaka yake juu ya pwani ya Kenya naye kenyatta akaahidi kuendelea kuwepo kwa mahakama ya Kadhi, pamoja ba mambo mengine. Katiba ya uhuru ilipoandikwa, mahakama ya Kadhi yaliingizwa humo.

Hali ya mahakama ya Kadhi ni kama tunavyoeleza hapa chini:

Ingawa Sheria ya Mahakama ya Kadhi yasema kwamba Sheria ya Kiislamu na desturi za ushahidi zitatumika Mahakamani, hili halifanyiki kwa kawaida kwa ambavyo, sheria za

Kiislamu na desturi za ushahidi hazikufanywa na Jaji Mkuu. Badala yake, Kadhi hutumia sheria na desturi za ushahidi zilizoelezwa chini ya Sheria ya Ushahidi (Sura 80). Lakini, Sehemu ya Pili ya Sheria ya Ushahidi yaeleza wazi kuwa itatumika kwa mahakama nyingine zote, isipokuwa zile Mahakama za Kadhi, yaonekana kuna upinzani kati ya sehemu 6 (iii) ya Sheria ya Mahakama ya Kadhi inayoruhusu matimizi ya Sheria ya Ushahidi chini ya Sheira ya ushahidi, na sehemu 2 ya hiyo hiyo Sheria ya Ushahidi iliyoacha nje Mahakama za Kadhi katika matumizi yake.

Tena, Sheria ya Mahakama ya Kadhi yasema kwamba Jaji Mkuu ataunda sheria za ufanyakazi na utaratibu wa Mahakama, lakini hadi sasa, hili halijafanywa. Badala yake, Kadhi hutumia Utaratibu uliochini ya Sheria ya Utaratibu wa Kijamii. Hii imeelezwa chini ya sehemu 8(2) ya Sheria ya Mahakama ya Kadhi. Sharti hili, kama katika sehemu 6(iii) iliyojadiliwa hapo juu, laonyesha kukiuka ile hisia ya sehemu ya sitini na sita ya Katiba na, katika matumizi sehemu hizi mbili zimepata sifa za vifungu vya kufanikiwa kwa jitihada au kushusha hadhi kufikia upeo wa kuwa vimetumiwa badala ya Sheria ya Kiislamu na Sheria ya Ushahidi na matumizi na utaratibu wa mahakama kama ilivyofikiriwa chini ya sehemu 6(i) na 8(i) ya Sheria ya Mahakama za Kadhi.

Kwa sababu Kadhi si mawakili waliosomea kazi yao na wanaoelewa Sheria ya Ushahidi, na Sheria ya Utaratibu wa Rais, haipendelewi kwamba watumie taratibu hizi chini ya Sheria hii katika kusimamizi wa mahakama zao. Sasa kunadharura ya kuhitaji Hakimu Mkuu atakayefafanua taratibu sahihi za Sheria ya Kiislamu, matumizi na ushahidi kwa Mahakama za Kadhi ili ziweze kutekeleza maagizo ya kikamilifu na kwa hali inayofaa. Katika maoni haya ya kutofaulu kwa Jaji Mkuu, kutunga na kufafanua sheria hizi kwa Mahakama za Kadhi, ingekuwa bora kufuata mifano ya nchi nyinginezo ambazo huzipa Mahakama za Kadhi au Kadhi Mkuu uwezo wa kutunga Sheria za Mahakama.

***(d) Tume ya Huduma za Mahakama***

Tume ya Huduma za Mahakama imeanzishwa katika Katiba. Ina Jaji Mkuu kama mwenyekiti, Mwana Sheria Mkuu, majaji wawili walioteuliwa na Rais na mwenyekiti wa

Tume ya Huduma za Umma. Tume huteua mahakimu na wafanyikazi wengine wa Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa kando na majaji.

Sehemu za sitini na saba (67) na themanini na nne (84) zimekabidhi vilivyo Mahakama Kuu, wajibu wa ufafanuzi wa Katiba na utekelezaji wa Mswada wa Sheria za Haki za Binadamu.

### 11.5.3 Mahakama katika Katiba Nyingine

Muundo na mpango wa Mahakama unatofautiana kutoka nchi moja hadi nyingine. Kanuni fulani, kama utekelezaji wa haki na uhuru wa Mahakama, hata hivyo, hazitofautiani. Katiba nyingi huunda viwango vya mahakama mara nyingi kuanzia mashinani (kijiji, kata au wilaya) hadi kufikia kilele cha Mahakama ya Juu au Mahakama ya Rufani. Katika nchi nyingi, kama Afrika Kusini, India, Nigeria, Ghana, Marekani na Uganda, kilele cha Mahakama ni mahakama ya mwisho kuhusu masuala ya kikatiba. Kwingine, kilele cha mahakama ni mahakama ya kikatiba.

Kiwango cha utawanyaji madaraka na aina ya madaraka ya mahakama hutofautiana kutegemea mfumo wa serikali (yaani kama ya umoja au shirikisho) na pia nguvu wa kijamii na kitamaduni. Kwa hivyo, Nigeria ina muundo mgumu wa mahakama ya Kiislamu na kitamaduni miongoni mwa majimbo yake. Licha ya kuonyesha viwango vya mahakama yenye madaraka juu ya kesi za madeni na jinai, Katiba ya Nigeria imehakikisha kuwepo kwa mahakama chini ya Mahakama ya Rufani ya shirikisho ya Sheria na Mila, na madaraka ya kukata rufani juu ya sheria ya binafsi. Kiwango hiki cha ufafanuzi si cha kawaida katika mataifa yanayotayarisha dini na serikali. Katika muktadha huu, sheria ya binafsi yenye msingi wa dini au mila hushughulikiwa katika mahakama za chini. Kwa hivyo, Ibara 129 (1) ya Katiba ya Uganda inawezesha, pamoja na mengine, kuanzishwa kuwa:

> *(d) mahakama za chini, kama ambavyo Bunge, kwa mujibu wa Sheria, itaanzisha, pamoja na mahakama ya Kadhi ya ndoa, talaka, urithi, na usimamizi.*

### 11.5.4 Yaliyosemwa na Watu

Watu waliotoa maoni mengi kuhusu muundo wa Mahakama, uteuzi wa Jaji Mkuu na majaji wengine, usimamizi wa muundo wa Mahakama za Kadhi na kuhusu kanuni za kijumla za utoaji wa haki. Kwa muhtasari ni kama ifuatavyo:

*(i) Kuhusu Mahakama kwa jumla kwamba*

a) uhuru wa Mahakama uwe madhubuti kwenye Katiba;
b) Katiba ihakikishe kwamba hakuna athari katika Mahakama kutoka kwa mamlaka ya nchi na Wabunge;
c) kesi zifanyiwe uamuzi wa haraka;
d) Majaji wawe wamehitimu kwa kazi yao;
e) taratibu za Mahakama zirahisishwe;
f) wananchi wote watendewe haki bila upendeleo na usawa mbele ya mahakama.
g) nafasi ya kuyafikia mahakama ingeboreshwa kwa:
    - Usaidizi wa kisheria usio malipo
    - Upunguzaji wa ada ya mahakama au malipo ya ada hiyo ya mahakama
    - Kurahisisha utaratibu wa kuthibitisha wosia
    - Kuongeza idadi ya majaji na mahakama na kusambaza mamlaka ya mfumo wa mahakama wilayani.
h) kuhusu muundo wa mahakama, watu walikuwa na maoni kwamba kuna haja ya kuanzisha mahakama ya kikatiba, Mahakama ya Juu na Mahakama maalumu za vijijini, zote hizi zikiungwa mkono na Wakenya wengi.

*(ii) Kuhusu uteuzi wa Jaji Mkuu*

a) maoni yalitolewa pia kwamba uteuzi wa Jaji Mkuu na majaji wengine ufanywe na Bunge katika pendekezo la Tume ya Huduma za Mahakama;
b) masharti ya kidini ya kuajiri yalitolewa na majaji wote na hasa kwamba majaji wawe na shahada ya digrii ya sheria.

*(iii) Kuhusu swali la nidhamu la maafisa wa Mahakama, kwamba*

a) mahakama iwe na kanuni za maadili zinazoweza kutekelezwa lakini, zinazozuia kujiingiza katika shughuli za biashara za kibinafsi;
b) kuwekwe utaratibu madhubiti unaofanya kazi vyema katika Katiba;
c) Majaji waadhibiwe kwa kupigwa marufuku kazini, kufukuzwa kazini; kusimamishwa, kufutwa na kushitakiwa;
d) Majaji walio na ufisadi wafutwe kazi; na
e) Jaji asibaki kwenye kituo kimoja kwa zaidi ya miaka mitatu.

*(iv) Kuhusu Kadhi Mkuu na Mahakama za Kadhi*

(a) waislamu lazima washauriwe katika uteuzi wa Kadhi Mkuu na Kadhi wengine. Wangewachagua na kuwa wanachama kwenye mamlaka ya wale wanaofanya uteuzi, yaani, Tume ya Huduma za Mahakama. Kwamba mashirika ya Waislamu kama SUPKEM yashauriwe;
(b) kuwe na kiwango cha chini cha sifa za kufaulu masomoni, kwa Kadhi Mkuu na Kadhi wengine kwa mfano shahada ya digrii ya kawaida na digrii ya Sheria ya Kiislamu kutoka chuo kikuu kinachotambulikana;
(c) mahakama ya Kadhi ipewe uwezo wa kutekeleza kazi zao katika upande wa kutayarisha utaratibu wa huduma zao, kuboresha utaratibu wa huduma na masharti ya kuajiriwa kwa mfano, mishahara, wafanyikazi, vifaa vya mawasiliano, n.k.
(d) kadhi Mkuu apewe hadhi sawa na Jaji wa Mahakama Kuu na Kadhi wawe kama Jaji Mkuu;

(e) idadi ya Mahakama za Kadhi iongezwe na ziwe katika Mkoa na Wilaya;
(f) Mahakama ya Kadhi iwe na Mahakama ya Rufaa tofauti na hakuna rufaa itakayowasilishwa kimakosa katika mahakama;
(g) Majaji wa Kiislamu waliomashuhuri katika Sheria ya Kiislamu wateuliwe katika Mahakama Kuu ili wasikilize Rufaa kutoka kwa Mahakama za Kadhi;
(h) Mahakama za Kadhi zipewe uwezo wa kutoa uamuzi juu ya Sheria halisi na Sheria ya taratibu kuhusu urithi na urathi wa Waislamu; na
(i) Mahakama za Kadhi zipewe uwezo wa kushughulikia sio tu talaka katika ndoa za Kiislamu, lakini pia kuhusu masuala yanayotokana na talaka kwa mfano, kuhifadhi na kuwalinda watoto, malezi upangaji na mgao wa rasilmali a ndoa baada ya talaka na mambo mengine yanayotokana na hayo.

*(v) Kuhusu mahakama za chini kwamba:*

(c) Katiba itambue Mahakam za kitamaduni na mashinani zenye mamlaka juu ya madai madogo na masuala ya sheria ya binafsi; na
(d) Mamlaka ya wazee wa utamaduni yatambuliwe.

### 11.5.5 Uchanganuzi

Madai ya dhati yalifanywa kuhusu mahakama, kama madai yale ya kutotekeleza kazi vyema, kutokuwa na ujuzi wa kazi vyema na ufisadi, kando na hayo, ilikuwa dhahiri kwamba watu hawakuwa na imani na utendakazi wa mahakama kuweza kutoa haki bila mapendeleo kwa hali ya usawa na bila hofu.

Kuhusu Mahakama ya Kadhi, ingawaje ilibainika kuwa kwa Waiislamu hii ilikuwa ishara ya imani yao ya Uislamu na utamaduni. Lakini kuhusu wanawake Waislamu, mahakama

zilikuwa vituo muhimu vya kukataa ugandamizi uliokuwepo katika ndoa na kwenye hali zao za kinyumba katika desturi za jamii iliyogandamizwa na mfumo wa kuumeni. Kupitia mahakama hizi, wanawake Waislamu wamefaulu kupigania ulinzi na utekelezaji wa haki zao, kama zilivyohakikishwa chini ya Sheria ya Kiislamu, na kupinga desturi haribifu kitamaduni na mila za jamii ya Waislamu zinazopotosha haki hizi. Sheria ya Kiislamu hairuhusu mwanamke kushikilia afisi ya Kadhi, lakini jambo hili haliwakatazi wanawake kuteuliwa kama wasaidizi wa Kadhi, kusaidia wakati ambapo wanawake wanaoleta madai mahakamani huhisi ugumu wa kuwaeleza Kadhi wanaume mambo ya faragha na ya kibinafsi kuhusu matatizo ya unyumba wao.

### 11.5.6. Mapendekezo

Kwa hivyo Tume inapendekeza –

*(i)* *Kuhusu mahakama kwamba –*

a) jaji Mkuu atakuwa kiongozi wa Mahakama na Rais wa Mahakama ya Juu;
b) kutakuwa na Tume ya Huduma za Mahakama (JSC) itakayokuwa huru, na majukumu yake yatakuwa ni;
    - kupendekeza kwa Rais watu watakaoteuliwa kama majaji;
    - kubadilisha na kufanya mapendekezo kuhusu masharti na hali za huduma za majaji, mahakimu na maafisa wengine wa mahakama, kando na mishahara na malipo ambayoyataamuliwa na mahakama maalumu inayoshughulikia huduma zote za umma;
    - kuteua, kufundisha adabu mahakimu na maafisa wengine wa mahakama pamoja na watumishi wa kisheria kuambatana na sheria kama ilivyoamuliwa na Bunge;
    - kupokea na kuchunguza malalamiko dhidi ya majaji kuambatana na Katiba;

- kutayarisha na kutekeleza mipango kwa kuelimisha na kuwafundisha majaji, mahakimu na watumishi wa kisheria;
- kushauri utawala katika kuboresha ufanyikazi kwenye utoaji wa haki na kufikia haki pamoja na usaidizi wa kisheria; na
- kuhimiza usawa wa kijinsia katika utoaji wa haki nchini Kenya.

*(ii) Kuhusu mahakama kwamba*

(a) Kutakuwa na Mahakama ya Juu ambayo kazi zake zitakuwa ni:-

- kutoa uamuzi kuhusu mashtaka ya madai na ya jinai;
- itakuwa Mahakama inayopelekewa mashtaka yanayotokana na ugomvi kati ya mabaraza ya wilaya na Mikoa;
- kuwa Mahakama ya Rufaa ya hatima katima masuala yote;
- kutoa maoni ya ushauri kwa utawala au Bunge juu ya masuala yanayohusu au yanayogusia ufafanuzi wa Katiba;
- kusuluhisha mabishano yanayotokana na uchaguzi wa Rais; na
- kutumia mamlaka asilia kama yalivyofafanuliwa katika Katiba na Sheria.

b) Kutakuwa na Mahakama ya Rufaa - itakayosikiza rufaa kutoka kwa Mahakama Kuu juu ya masuala yote.

c) Kutakuwa na Mahakama Kuu itakayokuwa na mamlaka yasiyo kikomo kuhusu masuala yote ya madai na jinai. Mahakama hizi, ziongeze mahakani maalumu inapohitajika miongoni mwake zikiwa -

- Mahakama ya Familia (kama sasa);
- Mahakama ya watoto (kama sasa);
- Mahakama za biashara (kama sasa);
- Kitengo cha Kikatiba na Kitawala;
- Kitengo ya Viwanda;
- Kitengo cha Jinai;
- Mahakama za Kadhi;
- Mahakama za chini (mahakama ya Mahakimu).

d) Kutakuwa na Mahakama maalumu kama zitakavyoanzishwa na sheria.

e) Kutakuwa na Mahakama za Wazee wa Vijiji – kwa kila kijiji au vijiji vinavyohusiana pamoja na mamlaka ya –

- kusikiliza na kuamua ugomvi kuhusu ardhi;
- kusikiliza na kuamua masuala yanayohusu sheria ya kibinafsi.

f) Katiba itafafanua zaidi kwamba -

- mahakama yaweze kufikiwa ni walemavu kwa jumla;
- mawasilisho kwenye mahakama yaendelee katika lugha inayofahamika na wananchi;
- kuweka ilani na matangazo ya kutosha mahakamani ili umma ufahamu mambo yanayoendelea na ikiwa wana shughuli, au kama wanataka kutazama mfumo wa haki ukitekelezwa, wanajua mahali pa kwenda;
- mashtaka mahakamani yaamuliwe kwa haraka; na
- majaji na mahakimu watoe haki haraka na hasa kutoa hukumu, maagizo na uamuzi katika muda wa siku ishirini na moja baada ya kufungwa kwa shitaka au kutekelezwa.

*(iii) Kuhusu sifa zilinganazo na mahakama kwamba*

a) sharti la chini la kuweza kuteuliwa kama Jaji Mkuu au kama Jaji wa Mahakama ya Juu litakuwa ni jumla ya tajriba ya miaka kumi na mitano. Kama Jaji wa Mahakama Kuu au Mahakama ya Rufaa lazima mtu awe anatendakazi ya wakili ama awe anafundisha katika Chuo Kikuu kinachotambulika;

b) sharti la chini kwa uteuzi kama Jaji wa Mahakama ya Rufaa litakuwa ni jumla ya tajriba ya miaka kama jaji wa Mahakama Kuu, akifanyakazi kama wakili, au akifundisha katika Chuo Kikuu kinachotambulika;

c) masharti la chini ya uteuzi wa jaji wa mahakama kuu litakuwa ni jumla ya tajriba ya miaka kumi, akiwa hakimu aliyefuzu au anayefanya kazi kama wakili;

d) Tume ya Huduma za Mahakama (JSC) pia yapasa izingatie uwezo wa kiakili (kisomo) wa wagombea uteuzi, unaopimwa kwa vigezo kama vile hati za kufuzu kisomomi;
e) umri wa kustaafu kwa Majaji wote na mahakimu utakuwa miaka sitini na mitano.

*(iv) Kuhusu Mahakama ya Kadhi, kwamba*

a) washughulikie mashtaka yanayohusu hadhira kibinafsi, ndoa, talaka au urithi katika shughuli ambazo wanaohusika ni waumini wa dini ya Kiislamu. Ingawaje, kando na kushughulikia shughuli za madeni, pia wangepewa uwezo wa kushughulikia mashtaka ya kibiashara yanayowahusu Waislamu;
b) Kadhi Mkuu na Kadhi wengineo wangeteuliwa na Tume ya Huduma za Mahakama kwa ushauri wa mashirika ya Waislamu kama SUPKEM;
c) sharti la chini la kuweza kuteuliwa kama Kadhi Mkuu au Kadhi wengine ni shahada ya digrii ya Kiislamu kutoka chuo kikuu kinachotambulika;
d) Kadhi Mkuu anaweza kupewa hadhi sawa na jaji wa Mahakama Kuu na Kadhi wengine kama Jaji Mkuu;
e) idadi ya Mahakama za Kadhi zingeongezwa na lazima ziwe katika kila Mkoa na Wilaya;
f) Mahakama ya Kadhi yatakuwa na sheira ya rufaa;
g) kila Mahakama za Kadhi iwe na msaidizi mwanamke atakaye shughulikia mashtaka yanayohusu wanawake;
h) Waislamu wa dhehebu la Shia pia wateuliwe kama Kadhi ili washughulikie maslahi ya Waislamu wa Kishia; na
i) Utaratibu wa Mahakama ungerahisishwa bila kutatiza utekelezaji wa haki halisi.

*(v) Kuhusu masharti ya mpito kwamba*

a) majaji wote wastaafu katika umri wa miaka sitini na mitano;
b) majaji wenye uwezo mkubwa, majaji wa rufaa, majaji wa mahakama ya viwanda, Jaji Mkuu na Kadhi Mkuu, anayetoa huduma za mahakama wakati huu aliyefikia umri wa miaka hamsini na mitano atakuwa na haki ya kustaafu na kupata marupurupu yote pamoja na malipo ya uzeeni yatakayolingana na miaka mitano ya huduma. Haki hii lazima itekelezwe katika kipindi cha siku thelathini baada ya kutekelezwa kwa Katiba hii;
c) kuambatana na (b) hapo juu, baada ya kutekelezwa kwa Katiba, jaji ye yote ambaye anashitaka dhidi yake lililobaki bila kusuluhishwa na Tume ya Huduma Mahakama (JSC), Mamlaka Dhidi ya Ufisadi, Tume ya Mawakili, Kamati ya Mawakili ya Kufunza Uadilifu, atachukua likizo bila malipo akingojea kusikizwa na kuamuliwa kwa mashtaka na Tume ya Huduma za Mahakama (JSC) kuambatana na Katiba;
d) ambapo baada ya kutekelezwa kwa Katiba, jaji atakuwa hajatumia vibadala vilivyo chini ya (b) hapo juu, na haitokani na (c) hapo juu, katika kipindi cha muda wa siku sitini, ataiwasilishia Tume ya Huduma za Mahakama nyaraka na ushahidi wote unaohitajika chini ya uongozi uliofafanuliwa katika Katiba hii;
e) ambapo baada ya kupata nyaraka na ushahidi ulioelezwa katika (d) hapo juu na baada ya Tume ya Huduma za Mahakama (JSC) kutoa maoni kwamba jaji yule hatoshelezi kigezo chini ya Katiba au chini ya Kanuni, itamuondoa jaji kazini, bila kupoteza marupurupu yake aliyorundikiza;
f) hakuna jaji atakayelipwa malipo ya uzeeni ama marupurupu mengine ikiwa hakumaliza kutoa uamuzi uliokuwa haujakamilika na hukumu na kuwajibika katika mahesabu ya fedha zote na mali ya mahakama;
g) hakuna jaji atakayestaafu chini ya Katiba hii ambaye atakuwa na nafasi ya kuteuliwa tena;
h) Baada ya utekelezaji wa Katiba hii, Tume ya Huduma za Mahakama (JSC) itaundwa tena, licha ya kutoteuliwa kwa wawakilishi wa Mahakama Kuu

na Mahakama ya Rufani. Kamati ya Bunge ya Mahakama katika kipindi cha siku thelathini baada ya kufunguliwa kwa Bunge itahakikisha ukatiba wa Tume ya Huduma za Mahakama;

i) Katika kipindi cha siku thelathini baada ya utekelezaji wa Katiba, Tume ya Huduma za Mahakama (JSC) itatangaza nafasi zilizoachwa wazi na majaji au Jaji wa Mahakama ya Rufani kama zitakavyohitaji kufuzwa na kutayarisha orodha fupi itakayowasilishwa Bunge, itakayojaza nafasi hiyo kwa muda usiozidi mwezi mmoja baada ya kuwasilishwa kwa orodha;

j) Kuhusu Mahakama ya Juu, Rais atashauriana na Waziri Mkuu na atateua watu wanaofaa katika muda wa siku arobaini na tano baada ya kutekelezwa kwa Katiba kwa idhini ya kamati ya Mahakama ya Bunge;

k) Kuambatana na Sheria ya Mawakili, jaji yeyote atakayeondoka afisini chini ya masharti haya atakuwa na uhuru kufanya kazi ya sheria kama Wakili wa Mahakama Kuu bila pingamizi; na

l) Rais atateua Jaji Mkuu miongoni mwa wale watu walioteuliwa kwenye Mahakama ya Juu.

## 11.6 Huduma kwa Umma

### 11.6.1 Kanuni za Jumla

Ingawa haichukuliwi kuwa chombo cha kitawala ni wazi kwamba huduma umma hubeba mzigo wa utawala wa umma. Ni muhimu, kwa hivyo, kwamba asasi hii ichunguzwe. Hakika kwa kuitaka Tume ichunguze na kufanya mapendekezo juu ya kuanzisha mbinu za kuendeleza utawala mwema na demokrasia kuna agizo dhahiri ambalo lililotolewa la kuchunguza huduma kwa umma.

Huduma kwa umma ni sehemu muhimu ya chombo cha utawala cha taifa. Kuna watu wanaosimamia shughuli za kimsingi na utoaji wa huduma kwa

umma pamoja na uundaji wa sera. Huduma kwa umma ni muhimu kwa mshikamano na uhuru wa taifa.

Kuna kazi mbili ya Huduma kwa umma, yaani;

- Kutekeleza sera na sheria za taifa;
- Kuajiri wafanyikazi wa kutoa huduma kwa umma.

Huduma wa Raia Kenya ina afisi muhimu na idara zifuatazo:

- Makatibu wa Kudumu wote;
- Wafanyi kazi wote wa Wizara za Serikali pamoja na Afisi ya Rais na idara zao na asasi za kufundishia ujuzi;
- Utawala wa Mkoa;
- Polisi na Huduma nyingine za Usalama;
- Afisi za Serikali za Wilaya;
- Maafisi wa mashirika ya kiserikali na mengineyo;
- Maafisi katika Tume za kikatiba na afisi nyingine za Katiba.

Mwaka 1999, kulikuwa na takriban wafanyikazi 683,300 tofauti wa umma nchini Kenya. Wameainishwa kama ifuatavyo:-

| **Idara:** | **Idadi ya Wafanyi kazi wa Umma:** |
|---|---|
| Serikali Kuu | 208,500 |
| Tume ya Huduma za Walimu | 105,200 |
| Serikali ya Wilaya | 78,000 |
| Biashara ambamo serikali ina hisa nyingi | 48,000 |

Kufuatia sehemu ya 107 ya Katiba ya Kenya, Bunge lilipitisha Sheria ya Tume za Huduma (Sura 185) kutoa aina ya waliomo na umbo la utendakazi wa Tume ya Huduma kwa Umma.

### 11.6.2 Huduma kwa Umma katika Katiba

*(a) Msingi*

Katiba ya Uhuru uliunda Tume ya Huduma kwa Umma ya Jamhuri na Tume ya Huduma za Umma kwa kila eneo.

Uanachama wa Tume ulikuwa na mwenyekiti, naibu wa mwenyekiti na wanachama wawili walioteuliwa na Gavana-Mkuu atayetenda kazi kulingana na ushauri wa Tume ya Huduma za Mahakama, na wawakilishi watatu walioteuliwa na Gavana-Mkuu anayetendakazi kulingana na ushauri wa Rais wa Bunge la Kieneo la eneo hilo.

Masharti yanayohitajika kwa uteuzi yalileta vikwazo kwa afisa yeyote wa umma na mwanachama yeyote wa Baraza la Wabunge (au mwanachama wa awali au mtu yeyote aliyewahi kuteuliwa kwa uchaguzi kama mwanachama wa Baraza la Wabunge au Bunge la kieneo la mamlaka ya wilaya kutokana na kuteuliwa).

Tume ya Huduma kwa Umma ilikuwa na maagizo haya:

- Kuteua watu wa kushikilia kazi katika afisi za huduma kwa umma;
- Kufunza adabu na kudhibiti watu wanaoshikilia kazi za afisi hizo;
- Kuwaondoa watu kama hao afisini.

Tume ilishauri Gavana-Mkuu kuhusu uteuzi wa watu wafuatao:

- Mhasibu Mkuu;
- Mwanasheria Mkuu;
- Makatibu wa Kudumu na Katibu wa Baraza la Mawaziri;

- Maliwali na Mudir wa Eneo la Pwani.

Kulikuwa na usalama wa kazi kwa wanachama; wangeondolewa tu baada ya uchunguzi wa mahakama maalum iliyoundwa kwa madhumuni hayo.

Ni Gavana-Mkuu aliyekuwa na mamlaka ya aina ya maafisi na idadi yake nchini Kenya ambapo huduma kwa Umma ilitoa wafanyikazi. Kanuni za Katiba nyingine zinazoshugulikia Huduma kwa Umma huzingatia mambo yafuatayo:

- Utaalamu;
- Uhuru wa kutofungamana na upande wowote kisiasa;
- Taratibu za kupandisha cheo na kuajiri;
- Masharti, utaratibu na hali za huduma;
- Mafunzo na elimu ya kuendelea;
- Haki za malipo ya uzeeni na marupurupu ya kustaafu ya watumishi wa umma na waajiriwa wa sekta ya kibinafsi na kustaafu;
- Kuajiri na kustaafu, upana na umiliki wa huduma; na
- Siri rasmi na haki ya kupewa habari za umma.

***(i) Katiba Iliyopo***

Katiba iliyopo inafafanua kuhusu Tume ya Huduma kwa Umma kazi za Huduma ya Umma zimeelezwa na zinajumlisha; uteuzi, kutekeleza nidhamu na kuwaondoa wafanyikazi wa umma, pamoja na wale walio kwenye utawala wa wilaya, kando na maafisa wengine hasa wale walioachwa kuambatana na uamuzi wa Rais au mamlaka mengine.

Tume ya Huduma kwa Umma ina mwenyekiti na wanachama kumi na sita, wote wakiwa wameteuliwa na Rais. Mwanachama ana awamu ya miaka mitatu lakini anaweza kuondolewa wadhifa wake na Rais. Tume haiko chini ya udhibiti wa mtu yeyote au mamlaka katika utendaji wa kazi zake. Rais amepewa uwezo

kuwastaafisha kwa lazima wafanyi kazi wa kigeni katika Huduma kwa Umma ikiwa wapo Wakenya wanaoweza kuchukua mahali pao.

Katiba zinashughulikia marupurupu ya malipo ya uzeeni ya wafanyi kazi wa umma, umma kwa kueleza kwamba malipo yanakatwa kwenye Mfuko Mkuu wa Fedha za Serikali, na kwamba Tume Ya Huduma za Umma lazima itoe idhini ya kupunguza, kushikilia kusimamisha marupurupu.

Sehemu kubwa ya vifungu vya malipo ya uzeeni inashughulikia wafanyi kazi wa kigeni waliokuwa wakifanya kazi nchini Kenya kabla ya uhuru, kwa kuruhusu utoaji nchini wa malipo ya uzeeni bila kutozwa ushuru au malipo yoyote.

### 11.6.3 Huduma ya Umma katika Katiba Nyingine

Kwa sababu ya nafasi yake katika shughuli za serikali, Katiba nyingi zinafafanua kanuni zinazoongoza utenzi na nidhamu ya watumishi wa umma, kwa kuanzisha asasi maalum itakayowachagua na kuwanidhamisha. Kanuni hizi aghalabu zinahusisha serikali kuu na serikali ya mtaa, na afisi za mashirika ya serikali. Hivyo ndivyo ilivyo nchini Ghana, Singapore, India na Uganda. Wakati mataifa mengi, huunda "Tume kwa Huduma ya Umma" yenye jukumu juu ya huduma nzima, mengine huunda tume kwa sekta maalum. Katiba za Ghana ina tume moja na Uganda ina tume kwa sekta maalum. Kwa hivyo, katiba ya Uganda imeunda, pamoja na Tume kwa Huduma ya Umma,

- Tume kwa Huduma ya Elimu;
- Tume kwa Huduma ya Afya; na
- Tume za Huduma wilayani.

Uchaguzi wa muunda utakaopendelewa hutegemea kiwango cha uhuru kinachotakikana kwa kila sekta na ngumu wa mfumo wa serikali katika nchi husika.

#### 11.6.4 Yaliyosemwa na Watu

Yale yaliyoambiwa Tume na watu yanaelezwa kwa muhtasari ufuatavyo:

*(i) Kuhusu uteuzi, kwamba*

(a) Watumishi wa umma wapasa kuteuliwa na kupandishwa cheo kuambatana na ujuzi wao wa kazi baada ya utaratibu wa kawaida wa mahojiano;

(b) watumishi wa umma wanapasa kuteuliwa na Tume ya Huduma kwa Umma;

(c) nafasi ya Makatibu wa Kudumu yapasa itangazwe kabla ya mtu kufikiriwa kwa uteuzi katika nafasi hiyo;

(d) Rais yapasa achague wanachama wa Tume ya Huduma kwa Umma.

*(ii) Kuhusu uhuru, kwamba*

(a) Tume ya Huduma za Umma ingekuwa chombo huria;

(b) kusiwe na uteuzi wa kisiasa kama njia ya kuimarisha uongozi na wajibu wa ufunzaji nidhamu wa katika Tume ya Huduma za Umma;

(c) Watumishi wa umma yapasa wawe na usalama ya kazi;

(d) Tume ya Huduma za Umma yapasa kuwa chombo huria kitakachokuwa na walioteuliwa kutoka chama kinachotawala.

*(iii) Kuhusu masharti na Hali za Huduma, kwamba*

(a) Taifa lingeboresha masharti na hali za huduma na hasa ujira ya wafanyi kazi wote wa raia pamoja na waalimu;

(b) Polisi walipwe vyema na wapewe makao yafaayo;

(c) Huduma kwa umma yapasa kutoa marupurupu yanayopendeza kwa wafanyi kazi wake ili wawavutie wataalamu Wakenya.

*(iv) Kuhusu Utangazaji wa Mali na Kanuni za Uadilifu, kwamba*

(a) maafisa wote wa umma watatakikana kutangaza mali zao;

(b) maafisa wote wa umma wawe na kanuni za uadilifu zitakazo wafunga kazini.

*(v)* *Kuhusu Nidhamu na Ustadi;*

(a) wale wanaotumia rasilimali za serikali wachunguzwe na wanapopatikana na hatia washtakiwe na rasilimali zote wapokonywe na kurudishiwa serikali;
(b) Bunge litakagua wanachama wa Tume ya Huduma kwa Umma kuhakikisha kwamba hawafanyi ufisadi na kwamba wanaujuzi wa kazi;
(c) maafisa walio na rekodi mbaya wasiaminike na kupewa afisi za umma.
(d) Tume ya Huduma kwa Umma ingewahamisha watumishi wa umma baada ya vipindi maalum ili kuendeleza utendakazi mwema na uadilifu katika huduma za raia;
(e) Watumishi wa umma walioletwa mahakamani wasimamishwe kazi kungojea uamuzi wa kesi;
(f) Watumishi wa umma wasiofanya kazi wasimamishwe kazi na Tume ya Huduma badala ya kuhamishwa na kupelekwa kwenye vituo vingine vya kazi;

(g) Hatua ichukuliwe dhidi ya watumishi wa umma wa viwango vya juu wanaokejeli, kutia hofu na kuwaonea maafisa wa viwango vya chini bila sababu yoyote muhimu;
(h) Tume ya Huduma kwa Umma isikiuke haki za watumishi wa raia.

*(vi)* *Kuhusu kuwakataza watumishi jwa Raia kufanya biashara za kibinafsi, kwamba:-*

(a) Maafisa wa serikali wasiruhusiwe kuendesha biashara;
(b) Madaktari wanofanyakazi katika huduma za raia wasiwe na zahanati za kibinafsi;

(c) Tume ya Ndegwa kuhusu huduma za umma yapaswa kubadilishwa;

*(vii) Kuhusu uwalikilishi wa kieneo wa Tume ya Huduma za Umma, kwamba:-*

(a) Huduma kwa Umma ziwe na uwakilishi katika kiwango cha chama na iwe na usawa wa kijinsia.

*(viii) Kuhusu kustaafu na marupurupu ya uzeeni, kwamba:-*

(a) maoni juu ya umri wa kustaafu wa maafisa wa umma ulitofautiana ama kama utabaki ule ule wa miaka hamsini na tano (55) au utageuka hadi miaka sitini na tano (65);
(b) Wakenya walionelea kwamba marupurupu ya kustaafu yangebadilishwa kwa maafisa wa umma waliostaafu na wanaoendelea kufanyakazi;
(c) wananchi walipendekeza kwamba waliostaafu katika huduma za umma wangepewa marupurupu yao mara moja;
(d) idadi ya kadri ya waliostaafu ilitoa maoni kwamba kuna umuhimu wa kuwapa hadhi wazee waliostaafu kwa kuwaainisha kama raia wa stahiki wenye marupurupu kamilifu ya maslahi ya kijamii.

### 11.6.5 Uchanganuzi

Ilikuwa wazi kwamba watu walikuwa wanaomba kuanzishwa tena kwa kanuni za huduma kwa umma za kutofungamana na upande wowote, kutopendelea na uhuru. Watu wanataka taratibu za uteuzi zilizowazi na nafasi ambazo hazina tu uwajibikaji kwa watu bali pia zinaweza kulinda mali za umma na rasilmali.

Kulikuwa na kutoridhika kwa namna maafisa wa umma hawawezi kutekeleza madaraka yao wakiwa huru bila kuingiliwa na wanasiasa na vile utaratibu wa utenzi, hata wakati sheria iko wazi, ulipuuzwa na kuongozwa na upendeleo. Hali iliyojitokeza wazi ni kwamba uteuzi wa wafanyi kazi wa umma ulitegemea

vigezo vingine wala sio ustahiki, ustadi, au tajiriba inayofaa. Ili kurejesha imani ya wananchi, madai yalitolewa kwa usalama wa kazi, malipo bora na kutopendelea upande wowote.

### 11.6.6 Mapendekezo

Kwa hivyo, Tume imependekeza kuwa:

*(i) Kuhusu kuanzishwa kwa Tume ya Huduma kwa Umma*

(a) kuna uhitaji wa kuanzisha Tume huruia ya Huduma kwa Umma;

(b) Uwezo na majukumu ya Tume ya Huduma kwa Umma utakuwa:

- kumshauri Waziri Mkuu wakati anapofanya shughuli zake;
- kuteua, kupandisha cheo na kudhibiti uadilifu kwa watu wanaoshikilia afisi katika huduma kwa umma nchini Kenya;
- kubadilisha masharti na hali za huduma, kufundisha ujuzi na sifa za kuajiriwa kwa maafisa wa umma na masuala yanayohusiana na usimamizi wa wafanyikazi, na maendeleo ya huiduma za umma na kufanya mapendekezo kwa serikali;
- kuongoza na kuratibisha Tume ya Huduma za Wilaya;
- kusikiliza na kuamua malalamiko kutoka kwa watu walioteuliwa na Tume ya Huduma za Wilaya;
- kutekeleza majukumu mengine kama itakavyofafanuliwa kwenye Katiba au sheria nyengine yo yote.

(c) Tume iwasilishe taarifa Bungeni na kila mwaka juu ya utekelezaji wa majukumu yake;

(d) Kwa mujibu wa sheria, Bunge lingetoa uwezo kwa Tume ya Huduma kwa Umma itunge masharti yatakayosaidia utekelezaji mwafaka wa majukumu yake chini ya Katiba hii na sheria nyingine yoyote;

(e) Cheo cha Mkurugenzi wa Usimamizi wa Wafanyi Kazi kitafutiliwa mbali;

(f) Rais kwa mujibu wa idhini ya Bunge, atateua wanachama wa Tume;

(g) Tume itakuwa na muundo ufuatao:

- Makamishina kati ya wanane na kumi watakaotumika kwa awamu ya miaka mitano (kutegemea mabadiliko yanayoletwa na Bunge).
- Watu wanaoonyesha wingi wa tofauti miongoni mwa Wakenya.

(h) Watumishi wote wa Umma watatia sahihi Kanuni za Uadilifu zitakazowafunga kuzizingatia kama sehemu moja ya majukumu yao ya kuajiriwa;

(i) Ili kufaulu kuteuliwa kwenye Tume, lazima mtu awe na tabia yenye Uadilifu mwingi na uaminifu uliothibitishwa. Uteuzi kwa Tume ya Huduma za Umma utategemea ujuzi na ustahiki wa mtu; kuzingatia sifa za kiusomi na tajriba ya kazi;

(j) Watumishi wa Huduma kwa Umma wanahaki ya kuwa na masharti/mageuzi kama mbinu ya kuwavutia wataalamu Wakenya ili wafanye kazi kwenye huduma za umma;

(k) Mtu anayeshikilia afisi yoyote miongoni mwa hizi zifuatazo, atapoteza cheo chake afisini anapoteuliwa kuwa mwanachama wa Tume:

- Mbunge;
- Mwanachama wa Mabaraza ya Wilaya na Mkoa;
- Mwanachama wa utawala wa chama cha kisiasa au mashirika ya kisiasa;
- Afisa wa Umma

(l) Malipo ya wanachama wa Tume yataamuliwa na Bunge na yatatozwa kutoka Mfuko Mkuu wa Fedha za Serikali;

(m) Ikiwa Mwenyekiti na Naibu wa Mwenyekiti hawapo, Rais atampatia wadhifa wa kuwa mwenyekiti mmoja wa wanachama;

(n) Mwanachama wa Tume ataondolewa afisini na Rais pekee kwa sababu ya:

- kutokuwa na uwezo wa kutekeleza majukumu ya afisi yake kutokana na ugonjwa wa mwili au akili.
- utovu wa nidhamu; na
- kutoweza kazi.

(o) Kuwa watumishi wa umma wanastaafu wakifikia umri wa miaka sitini na tano (65).

*(ii) Kuhusu malipo ya uzeeni na marupurupu mengine, kwamba*

(a) Katiba wa umma ana haki ya kupata haki ya malipo yake anapoacha kazi wakati wa kustaafu;

(b) Sheria ya malipo ya uzeeni ieleze kwamba wafanyi kazi wa raia waliofikia umri wa kustaafu wabaki katika huduma hadi watakapolipwa marupurupu yao yote, malipo ya uzeeni na nyongeza nyinginezo;

(c) Raia stahiki (walistaafu) walipewa maslahi ya utambulisho rasmi (afya na makazi);

(d) Sheria za malipo ya uzeeni na haki za ulinzi yabidi zibadilishwe (malipo ya uzeeni ni haki si fadhila).

(e) Malipo ya uzeeni yatabaki yakitozwa kwenye Mfuko Mkuu wa Fedha za Serikali.

# SURA YA KUMI NA MBILI

# KUPUNGUZA NA KUSAMBAZA MADARAKA

## 12.1 Agizo la Tume

Pamoja na kuchunguza na kufanya mapendekezo kuhusu vyombo vya utawala, sheria ya marekebisho inahitaji Tume ichunguze na kufanya mapendekezo juu ya:

- Muundo na taratibu za utawala pamoja na mfumo wa shirikisho, na serikali ya umoja;
- Nafasi ya utawala wa wilaya katika usimamizi wa kikatiba wa Jamhuri; na
- Upeo wa upunguzaji na usambazaji wa madaraka kwa mamlaka ya wilaya.

Aidha, sheria yahitaji Tume kuhakikisha kuwa utaratibu wa marekebisho:

- Unaendeleza kushiriki kwa wananchi katika utawala wa nchi kupatia kwa upugazaji na usambazaji wa madaraka na matumizi ya uwezo;
- Inaheshimu wingi wa tofauti za kikabila na kieneo na haki za kijamii pamoja na haki za jamii na kusherekea utamaduni wao na kujitambulisha;
- Kuanzisha mfumo wa huru na wa kidemokrasia wa utawala uliohitaji katika utawala mwema na utenganisho wa uwezo na vipimo na visawishi; na
- Kuendeleza uwajibikaji wa mamlaka ya umma.

Kiini cha agizo hili swala la upunguzaji na usambazaji wa madaraka.

## 12.2 <u>Viwango vya Upunguzaji na Usambazaji wa Madaraka.</u>

### 12.2.1 Kanuni za Jumla

Kwa kawaida imefikiriwa kwamba ni serikali thabiti ya kitaifa, iliyo na mfumo wa serikali ya umoja pekee inayoweza kugawanya rasilimali na nafasi. Hoja mara nyingi hufanywa kwamba ni kiini thabiti ndicho kinachoweza:-

- Kuhakikisha umoja wa taifa;
- Kupata ufanisi na ugawanyaji tena na vitu;
- Kuendeleza demokrasia; na
- Kutosheleza uhuru na kufikia kilele cha uwezo miongoni mwa wananchi.

Hata hivyo, kwa ajili ya kutofaulu mara kwa mara kwa mfumo wa serikali ya umoja au mfumo wa kati kwa upande wa kuongezeka kwa makundi ya wachache waliotengwa, matumizi mabaya ya uwezo, mgao usio wa usawa na usimamizi mbaya wa rasilimali za kitaifa, kumekuwa na wito miaka ya hivi karibuni kuhusu usambazaji wa uwezo na majukumu katika miongo miwili iliyopita.

Usambazaji wa uwezo unamaanisha uhamishaji wa mamlaka kulingana na msingi ya kijografia ama ni kwa kusambaza uwezo wa mamlaka ya kitawala kwenda kwa vitengo vya namna moja ya idara au viwango vya utawala, au kwa upunguzaji na usambazaji wa Madaraka hadi vitengo vya serikali za wilaya ama vyombo maalum vya kisheria.

Usambazaji wa uwezo una sifa za kisiasa na za kiutawala. Sura zinazojitokeza katika nchi mbalimbali zinategemea zaidi hali na tajriba zao za kibinafsi. Kinyume cha wazo la usambazaji wa uwezo ni lile wazo la kugawanya uwezo wa serikali kati ya baina ya serikali kuu na pembezoni. Maswala muhimu ya mjadala ni:

- Muundo wa upeo wa namna uwezo na mamlaka ya serikali kuhusu ushuru, matumizi, kupanga, na kutoa huduma, kugawa na kugawanya mara ya pili,

kubainisha na kutekeleza haki na udhibiti wa ardhi na rasilimali nyingine ungesambazwa; na

- Upeo wa namna uwezo ungewekwa pamoja kwenye jozi moja ya asasi au upeo wa ambavyo uwezo kama huo ungesambazwa kote katika maeneo madogo ya kitaifa na asasi za wilaya, kila mojawapo ikiwa na, au ikidhibiti kiasi cha kiwango cha mamlaka au hali ya kuwa huru.

Kusambaza uwezo kunaweza kutumiwa katika mifumo yote miwili ya serikali, ya umoja na ya shirikisho. Kwa hivyo, si muhimu kwa mfano, kuunda mfumo wa serikali ya shirikisho au muundo wa utawala ili kusambaza madaraka katika viwango vya chini, maeneo au asasi. Kusambaza uwezo na mamlaka ya serikali kwa maana pana huchukua pande mbili: yaani kusambaza uwezo na upunguzaji na usambazaji madaraka.

***(a) Kutawanya Mamlaka***

Kutawanya kunamaanisha usambazaji wa utawala na unahusu uhamishaji wa mamlaka ya kutawala, yanayosimamiwa na mwakilishi wa serikali kuu katika eneo hilo, kutoka kati hadi mashinani. Ni ugawaji wa mamlaka kufanya uamuzi wa kutawala kwa niaba ya utawala wa serikali kuu kwa wafanyi kazi wa umma wanaofanya kazi mashinani na kuwajibika kwa kiasi fulani kuhusu sera ya serikali katika maeneo yao.

Hakuna dhamana ya kisheria ya matumizi ya mamlaka yaliyohamishwa. Serikali yaweza kuyaondoa mamlaka haya wakati wowote. Kwa hali halisi jambo hili linahusu kutawanya kwa urasimu wa utawala hadi mashinani. Kutawanya mamlaka ndicho kiini cha utawala wa kila siku wa serikali na viongozi hubainika kupitia kwa huduma za umma za serikali. Mfumo wa utawala wa Mikoani wa Kenya ni mfano mzuri wa utawanyaji wa mamlaka.

Utawala wa umma kwa hali hii unaathiri maisha ya wananchi na njia ambayo unaendelezwa ina umuhimu wa kikatiba. Sharti la kawaida ni kwamba mamlaka lazima yatumike chini ya sheria kwa utaratibu na kimsingi na bila ubaya wowote, kumuondolea raia haki yake ya urithi kwa sheria. Matokeo ni kumpa marupurupu mtu ambaye

hatakikani kuyapata kisheria. Pamoja na utawala wa umma ni matumizi ya tahadhari. Kwa vigezo vya kikatiba, tahadhari ifanywe kimakini na baada ya kuzingatia hoja hadha zinazohusika. Katiba yatakikana kuhalalisha na kufanya vipimo vya uwezo huu, na kuunda mbinu za kutathimini uthabiti wake.

### *(b) Kupunguza na Kusambaza Madaraka*

Kupunguza na kusambanza madaraka ni utaratibu ambapo mamlaka ya kufanya uamuzi katika eneo la sera ya umma hutolewa na sheria kwa mabaraza madogo ya kieneo ya taifa (mfano, serikali za wilaya). Kupunguza na kusambaza madaraka kunajumlisha kuhamisha kwa mamlaka ya utawala au kisiasa na uwezo wa asasi zilizohusika zikiamuliwa na sheria badala ya Katiba.

Hivyo, kwa hali zote, kupunguza na kusambaza madaraka ni mbinu ya kisiasa ya kuhusisha viwango vya chini vya serikali katika sera na kufanya uamuzi katika masuala yanavyowaathiri, ambapo kutawanya mamlaka ni mbinu ya kitengo chake cha utawala. Kupunguza na kusambaza madaraka kama kitengo maalum, maanisha mpango ambapo uwezo na muundo ya kupunguza na kusambaza madaraka umefafanuliwa katika sheria ya kawaida, na hivyo, inaweza kurekebishwa au kufutwa kwa urahisi zaidi kuliko mipango ya kishirikisho kwa kawaida haihitaji idhini ya kitengo kilichopunguziwa madaraka. Upunguzaji na usambazaji uliofanywa na London kwa Scotland ni wa aina hii.

Dhana ya "kupunguza na kusambaza madaraka", inatumiwa kwa kawaida kurejelea zile hali ambazo serikali ya umoja hugawanya (hupunguza na kusambaza) madaraka kwa sehemu/asasi za maeneo kama Uhindi na Nigeria au Kenya wakati wa uhuru).

Mataifa mengi leo ni ya serikali za shirikisho au sifa fani za kupunguza na kusambaza madaraka. Kadirio moja ni kwamba asilimia arobaini (40%) ya idadi ya watu ulimwenguni huishi katika aina fulani ya serikali ya kupunguza na kusambaza Madaraka. Katika jumuiya ya madola, nchi hizi ni pamoja na Canada, India, Malaysia, Australia, Afrika Kusini, Nigeria, Pakistani na Uingereza. Barani Afrika, kuna serikali za shirikisho za Nigeria na Ethiopia. Baadhi ya Katiba za zamani zilizopo leo – Marekani, Switzerland

na Canada ni za shirikisho. Umoja wa Mataifa ya Ulaya ni mfano wa mataifa muhimu yaliyostawishwa yanapotoa uhuru wao mwingi kwa asasi moja ya kisiasa na kitawala. Juhudi za sasa kuelekea upande wa kuunda shirikisho la Afrika Mashariki na mipango ya matamanio ya Umoja wa Afrika ni mfano ya mwelekeo huu wa baadaye. Kwa kila juhudi hizi kuna msisitizo wa kuelekea kwenye mfumo wa kupunguza na kusambaza madaraka.

*i) Sababu ya Msingi*

Kuna sababu nyingi za watu kupendelea kupunguza na kusambaza madaraka. Mifano ya awali yawakilisha mataifa huru tofauti yanayokuja pamoja kuunda shirikisho, kwa madhumuni ya kuwa kufanya ulinzi wao thabiti au kuunda uchumi wao thabiti au kuunda uchumi uliopanuka (hivi ni kusema, kuunda masoko makubwa na rasilimali za mfuko wa jumla), au kusimamia uhuru katika eneo la masafa makubwa. Barani Afrika kwa nyakati tofauti, ombi la kupunguza na kusambaza madaraka lilikuwa ni la kueleza matamanio ya umoja wa kieneo au wa Bara.

Wakati upunguzaji na usambazaji madaraka unapochukua muundo wa kugawa uwezo kutoka kwa mfumo wa kiini kimoja, sababu zake kwa kawaida ni tofauti. Nchini India Nigeria na Ethiopia kwa mfano, kupunguza na kusambaza madaraka kulikuwa ni kuitikia wito wa madai ya makundi ya kikabila, kwa kawaida ya waliowachache, waliotaka sehemu kubwa katika shughuli za serikali, ambayo walifikiria hawawezi kuipata katika mfumo wa serikali ya umoja.

Hali za kupunguza na kusambaza madaraka za siku hizi mara nyingi ni mifano ya kushirikisha na kuunganisha kikabila, kieneo, kilugha na kidini wingi wa tofauti kama ilivyo Bosnia-Herzegovina, Shirikisho la Urusi, Puerto Rico/USA (Marekani), Uspania, Ufilipino na kutambuliwa hivi karibuni kwa maeneo huru ya Waaborijini huko Canada. Katika hali hizi mara nyingine madaraka husambazwa katika maeneo ya kijiografia ili kulinda maslahi ya kikabila na kitamaduni na ujitambulishaji. Kupunguza na kusambaza kwa hivyo huonekana kuwa muelekeo kuhusu wingi wa makabila, au wingi wa sura za kitaifa za idadi ya mataifa, juhudi za kubakisha uhuru na umoja wa serikali.

Katika hali hizi, lengo halikuwa kuondoa wingi wa tofauti zilizopo bali kuzikubali maishani, kupatanisha na kudhibiti wingi huo wa tofauti katika msisitizo wa maelewano na umoja.  Hili linaonyesha, kwamba mfumo mingi ya kisiasa ya serikali shirikisho, kwa kupatanisha mahitaji wa kabila na kutambua wingi wa tofauti za kikabila, kilugha au zilizochimbuka katika historia inafaa kwa makadirio ya asasi na uhalisi wa wingi wa kimataifa katika ulimwengu wa sasa.

Kando na fikra hizi pana, imedaiwa kwamba kutokana na kutawanya madaraka kwa viwango tofauti, kupunguza na kusambaza madaraka kunaendeleza utawala mzuri, kunaonyesha utengaji uwezo, kuongeza nafasi za vipimo na visawazishi, na hutumika kwa kuzidisha utekelezaji, uwazi na uwajibikaji wa mamlaka ya utawala.

Hata hivyo, upeo ambao kupunguza na kusambaza madaraka hufanikiwa kupunguza uwezo na kufikia maadili haya, hutegemea zaidi muundo wa upunguzaji na usambazaji madaraka wenyewe.  Muundo bora, kila siku, ni ule wa mtindo wa kupunguza na kusambaza madaraka kwa tahadhari kuhakikisha kwamba kuna utenganisho ufaao na vipimo vya uwezo na majukumu katika viwango vyote na vitengo vya upunguzaji wa madaraka kinyume na mfumo ambao asasi, mamlaka na majukumu yanachanganyika.  La muhimu ni kwamba, viwango tofauti na vitengo vya upunguzaji na usambazaji wa madaraka huchukua nafasi ya vituo vya uwezo na upanuzi wa nafasi ya kidemokrasia. Hivyo, kuendeleza na kuzidisha demokrasia, mbinu za kidemokrasia na kushirikiana kidemokrasia kwa watu waliomo katika utaratibu wa utawala.  Kuweka mamlaka karibu na wananchi pia hufanikisha kwa hali ndogo uwajibikaji wa umma, kwa ambavyo uwezo ni rahisi kudhibiti katika kiwango cha mashinani kuliko kiwango cha kitaifa.

Sifa mojawapo muhimu ya mitindo ya upunguzaji na usambazaji madaraka ni kwamba wakazi si tu wanashauriwa mara kwa mara kuhusu uamuzi, bali pia ni sehemu mojawapo ya utaratibu wa kufanya uamuzi.  Kushauri na kushirikisha raia mara kwa mara hujenga hisia za umilikaji wa taratibu za maendeleo.  Kwa hivyo, huweza kufanikisha usimamizi ufaao wa rasilimali na taratibu za utawala.

Faida nyingine ya kushiriki kwa umma ni kwamba kunaendeleza hisia za umilikaji wa maendeleo na hivyo kunauwezo wa kuzidisha mgao ufaao zaidi wa rasilimali kwa kupendekeza kigezo cha maendeleo kilichojikita katika mahitaji yaliyopo.

Upunguzaji na usambazaji madaraka umetumika kama mbinu za manufaa kwa maendeleo kwa njia nyingi. Vitengo tofauti vya upunguzaji na usambazaji wa madaraka huwa hivyo yenyewe ni maeneno huru ya maendeleo, na hivyo huashiria mgao wa sawa wa fedha za maendeleo. Kwa njia yoyote huhimiza majaribio, kutaifisha na matumizi mepesi ya sera ya taifa na asasi, ili kutimiza mambo muhimu yaliyobainishwa.

*ii) Hatari*

Hata hivyo, upunguzaji na usambazaji waweza usifafanue demokrasia pana kwa sababu, kwa mara kadha, upunguzaji na usambazaji wa madaraka hutumika tu ili kuweka Uwezo katika mikono ya madikteta wa mashinani. Kwa hivyo, ni muhimu tunapotafakari vibadala vya upunguzaji na usambazaji wa madaraka, tuzingatie haja ya kuhakikisha kwamba wanaopokea upunguzaji na usambazaji wa madaraka wamehamesishwa vya kutosha na kujitayarisha katika kushiriki kwa dhati kwenye usimamizi wa shughuli za mashinani, na mbinu mwafaka kuwekwa ili kuendeleza maadili ya kidemokrasia.

Hali kadhalika, upunguzaji wa usambazaji wa madaraka unaweza kuharibu umoja wa taifa, kuchochea ukabila, wingi wa tofauti za kidini na kitamaduni na una uwezo wa kutengwa kwa walio wachache na waliowachache, hasa miongoni mwa walio wachache.

Aidha, vitengo vya upunguzaji na usambazaji wa madaraka, ambavyo havikuundwa vyema, vinaweza kumaanisha marudio utawala hali usiotenda kazi vyema; kurasimisha utaratibu wa maamuzi na hali kadhalika kuzorotesha utaratibu wa uwajibikaji. Tena, kuongezeka kwa mbinu na taratibu za ushauri baina ya tawala kunaweza kuwa na matokeo ya kugumishe hali serikali na gharama za rasilimali na nafasi.

Upunguzaji na usambazaji hupunguza uwezo wa madaraka na thamani ya serikali ya taifa katika kugawa tena rasilimali. Hili huleta hali ya maonevu kwa vitengo vilivyoendelea kiasi na hivyo kuleta hali ya kutegemea, na ambapo hii imejikita na kuwa na hali ya kawaida, hutokeza hali ya kutokuwa thabiti.

Kwa jumla, ni vigumu kueleza kwa jumla umbo, muundo na njia, vipeo, na matokeo ya upunguzaji na usambazaji wa madaraka kwa sababu kila tajriba ina muktatha wake wa kihistoria au kimaalum. Hata hivyo, matokeo hatimaye ni mfumo mseto wa "utawala uliogawanywa ndanimwe". Masuala mengine yanashughulikiwa na serikali kuu ambapo jamii zote hushiriki. Masuala mengine hushughulikiwa na jamii zenyewe kawaida katika maeneo maalum ya kijiografia katika mchanganyiko tofauti wa umoja na wingi wa tofauti.

*iii) Uzingatifu katika utaratibu wa kupunguza na kusambaza madaraka*

Madhumuni ya kimsingi ya upunguzaji na usambazaji madaraka hubadilika kutoka sehemu hadi sehemu. Kuhusu muundo, mgao na kiasi cha ushirikiano kati ya viwango tofauti vya serikali. Kimantiki, kwa hivyo, kiwango na umbo la upunguzaji na usambazaji wa madaraka kijikite katika na hali za kipekee za kila tukio na sababu zake za kuanzishwa. Hata hivyo fikra muhimu ambazo zinzoweza kutuelekeza katika utaratibu wa kutoa uamuzi.

Kwanza, lazima viwango vya upunguzaji na usambazaji madaraka vizingatiwe, yaani vitengo ambavyo vitagawanyiwa madaraka lazima vibainishwe. Kadri iwezekanavyo, vitengo hivi lazima viwe na tajriba ya sawa au iliyokaribia usawa wa hali za kijamii, kiuchumi, kiidadi na kijiografia.

Pili, kila mara ni muhimu kuzingatia kanuni pana na maadili yatakayoelekeza utaratibu wa upunguzaji na usambazaji wa madaraka na utendakazi wa vitengo vilivyosambaziwa madaraka. Maadili yanakariri vigezo wastani vya kutumiwa katika maswala kama haya,

kama ugawaji wa rasilimali, utoaji wa huduma na upangaji wa uhusiano kati ya magavana na wale wanaotawaliwa.

Tatu, madaraka yaliyosambazwa lazima yabainishwe. Madaraka mengine yanaweza kutumiwa na vitengo pekee ama kutumiwa kwa wakati mmoja na vitengo na serikali ya kitaifa. Madaraka mengi kwa vitengo yanamaanisha uhuru mwingi zaidi wa kujitegemea, lakini kila wakati kuna lazima ya kuhakikisha kwamba uhuru huu wa kujitegemea umesawazishwa dhidi ya matarajio ya kuwa na serikali ya umoja.

Nne, la muhimu zaidi ni mpango wa fedha kati ya serikali kuu na vitengo. Kwa hali hii, inasaidia kwamba hoja za dhati zinazohusu mgao wa rasilimali na nafasi, mgao wa uwezo kuhusu uchangishaji, matumizi, na uhamishaji wa mapato, na zaidi ya hivyo, kuanzishwa kwa vigezo vya kusaida vitengo ambavyo havina uwezo mkubwa wa kiuchumi; zielezwe waziwazi katika nyaraka ya kisheria. Njia za kukusanya na kutumia rasilmali ni kiini cha upunguzaji na usambazaji madaraka wenyewe. Hivyo kuna na haja ya kuunda miundo ya upunguzaji na usambazaji madaraka inayoweza kutekeleza vyema matumizi katika mgao wa rasilimali.

Mwisho, lakini muhimu vile vile, ni kwamba utaratibu wa uhusiano kati ya serikali kuu na vitengo ufafanuliwe. Hili litapatikana kwa kueleza wazi uwezo na majukumu ya kila kitengo, na pia maelezo ya wazi kuhusu eneo linalomilikiwa na sehemu mbili. Vile vile, mbinu za kusuluhisha mafarakano mengi ambayo yanaweza kuzuka zahitaji kutayarishwa. Kinachohusika zaidi baina ya uhusiano wa vitengo na serikali kuu, ni mahitaji ya kugawanya wazi na kusawazisha kati ya uwezo wa kuingilia ambao serikali kuu ingetumia juu ya vitengo, na matarajio ya vitengo kuwa na kiasi fulani cha uhuru wa kujitegemea.

Ingawa upunguzaji na usambazaji madaraka ulimwenguni kote umeundwa katika kiwango cha serika: ni muhimu kieneo, kimkoa, kiwilaya, kimanispaa na jijini kuzingatia mambo tuliyotaja hapo juu katika kuchagua muundo na upunguzaji na usambazaji wa madaraka au katika muktadha wa makubaliano ya kisiasa, ili kuhakikisha uwezekano

wake. Makubaliano ni hoja muhimu zaidi ya zote katika uamuzi wa uwezo na majukumu, na mpango wa muundo wa vitengo vilivyosambaziwa madaraka.

*iv) Mambo ya kupunguza na kusambaza madaraka.*

Kupunguza na kusambaza madaraka kunaweza kuchukua maumbo tofauti kama shirikisho, muungano, au serikali za mashinani. Shirikisho ndilo umbo la juu zaidi la upunguzaji na usambazaji madaraka na huashiria mpangilio wa mashirikisho yaliyopo. Shirikisho ni serikali zinazochanganya vitengo thabiti vya serikali na serikali kuu ya kati. Kila moja ikiwa na mamlaka iliyopewa na wananchi kupitia Katiba, kila moja ikiwa imepewa uwezo wa kushughulikia raia moja kwa moja katika utekelezaji wa sheria, utawala na uwezo wa kutoza ushuru, na kila moja iwe imechaguliwa moja kwa moja na kuwajibika kwa raia.

Kwa mbinu mseto, shirikisho huruhusu serikali thabiti za kieneo na serikali thabiti za kisehemu, kila mojawapo huwajibika moja kwa moja kwa wananchi. Kile kinachozibainisha hasa kutokana na mataifa ambayo yametawanya madaraka kikatiba, ni kwamba kila kiwango cha serikali hupata mamlaka yake kamili kutokana na Katiba, si kiwango kile kingine cha serikali na kwamba ile Katiba hauwezi kubadilishwa katika hali ya umoja na kiwango kimoja cha serikali kinachofanya hivyo peke yake.

Sura nyingine ya kimsingi na bainishi ya mifumo ya shirikisho ni kwamba zote, serikali kuu ya kati wala serikali za kieneo, hazitegemei kila moja nyingine, lakini, badala yake zinalingana kwa cheo. Pia, ndivyo ilivyo katika mfumo wa shirikisho kwamba, mara uwezo unapothibitishwa, unagawanywa kwa vitengo vyote kwa usawa. Vitengo vya shirikisho vinavyounda mfumo vinaweza kuwa na mfumo wa serikali ya wilaya. Hivyo, itakuwa jukumu la vitengo vidogo vya kitaifa vinavyounda shirikisho, kuamua upeo wa majukumu ya mamlaka ya serikali za wilaya. Bunge za vitengo vidogo vya zitaifa vinaweza kugeuza mgao wa uwezo kati yake na serikali za taifa, kwa njia ile ile inayofuatwa katika mfumo wa serikali ya umoja.

Shirikisho hutoa mbinu ya mpangilio wa kisiasa unaoruhusu utekelezi wa serikali kwa madhumuni fulani, pamoja na utekelezi wa vitengo vya serikali vya kieneo au mashinani kwa madhumuni mengine yanayohusu hasa kuhifadhi kwa tofauti bainishi. Hivi majuzi, mfumo ya shirikisho imefikiriwa kuwa vifaa vya kuunganisha sehemu ya vitengo vilivyo na misingi katika mataifa ya kikabila na kama njia ya kuzuia shinikizo za utengano.

Mifumo ya muungano kimataifa, hujumuisha maagizo ya kikatiba mawili au matatu ya serikali. Kiini cha mfumo huu kimeundwa na vitengo vinavyohusika, na serikali ya kati hutumia uwezo uliotolewa na vitengo hivyo.

Chini ya mfumo wa serikali ya shirikisho, baadhi ya vitengo vidogo vya kitaifa vinavyounda mfumo huo, vinaweza kuwa na mfumo wa serikali ya wilaya. Hii itakuwa na wajibu kwa vitengo vidogo vya kitaifa vinavyounda shirikisho ili kuamua upeo wa uwajibikaji wa mamlaka ya serikali za wilaya.

Bunge za ya vitengo vidogo vya kitaifa kwa hivyo, vinaweza kubadilisha mamlaka kati yake na serikali za taifa kwa njia ile ile inayofanywa katika mfumo wa serikali ya umoja.

Kupunguza na kusambaza madaraka kama dhana huweza kuchukua maumbo mbali mbali kuanzia utoaji wa uwezo mchache wa kikatiba hadi kwa mkubwa wa madaraka ya serikali na kusambaziwa mikoa yenye uwezo mwingi wa kutunga sheria na kudhibiti serikali za mikoa. Iliyoteuliwa pekee, kwa serikali iliyotawanywa uwezo kwa makutano katika mikoa yote. Hii inaonyesha kupungua kwingi kwa upeo wa bunge na serikali kuu. Hivyo hata pamoja na miundo kama hii ya utawanyaji wa mamlaka, nchi bado inaweza kuwa na *mfumo ya serikali za wilaya* kwa kuunda mamlaka ya wilaya katika kila mkoa na maeneo. Mifumo ya serikali za wilaya, kwa hivyo, inaweza kutekelezwa chini ya serikali ya umoja na pia chini ya utaratibu wa shirikisho.

Kimsingi, mfumo wa serikali za wilaya uliundwa ili kushughulikia hali maalum ya maeneo ya mijini. Hali hii imebadilika kadri muda unavyoyoyoma. Katika hali ya kisasa ya kisiasa ya mataifa, serikali za wilaya hazijishughulishi tu na maswala ya miji, kwani

pia ni mbinu ya kuwasilishia huduma kadhaa, na kwa mpangilio wa kisiasa kwa jamii za mjini na pia mashambani. Serikali za wilaya hutekeleza majukumu muhimu yafuatayo:

- Kuanzisha asasi za kuwakilisha serikali, zinazoweza kutumiwa kwa huduma za kufaa na shughuli za maendeleo na kuzifanya kuzingatia zaidi matakwa na maslahi ya sehemu hizo;
- Kuwawezesha raia kutekeleza haki ya kujitawala wenyewe;
- Kuhamasisha raslimali za sehemu hizo kwa kuzihusisha jamii za sehemu hiyo;
- Kutoa njia ya mawasiliano ya pande mbili kati ya jamii za mashinani na serikali kuu.

Muundo, sifa na majukumu ya serikali za wiliya hutofautiana kutoka nchi moja hadi nyingine. Na hivyo ndivyo mambo yalivyo kwa upande wa uhuru wa kujisimamia unaotekelezwa na serikali za wilaya. Katika mataifa yaliyokwishapiga hatua, mfumo wa serikali za wilaya si chochote ila kijalizo cha serikali ya kitaifa kinachotoa huduma, kuhamasisha na kusimamia watu na raslimali za nyanjani kwa lengo la kuleta maendeleo.

### 12.2.2. Kupunguza na kusambaza madaraka katika Katiba iliyoko

#### *(a) Msingi*

Wakati wa kupata uhuru, Kenya ilikuwa taifa lilokuwa limepunguza na kusambaza madaraka kikatiba. Kupunguza na kusambaza madaraka kulifanywa kwa misingi ya maeneo ambayo yalikabidhiwa madaraka muhimu na kujumuishwa katika Katiba. Maeneo yalikuwa na uwezo fulani kuhusu kodi na fedha na yalikuwa na mamlaka ya kisheria na mamlaka makuu. Uhusiano kati ya serikali ya kila eneo na serikali ya kitaifa ulikuwa umewekwa wazi katika Katiba na Wakenya walikuwa na haki ya kuishi na kukaa mahali popote nchini; ubaguzi ulipingwa vikali. Mfumo huu wa kupunguza na kusambaza madaraka ulikuwa maarufu kwa jina *'majimbo'*. Kikatiba, mfumo wa *majimbo* unaweza kuchukuliwa kama njia moja ya mfumo wa shirikisho

(hasa, shirikisho nusu) ingawa pia unaweza kuondolewa, na uliondolewa, kupitia uamuzi wa Bunge.

Hivi leo, maana ya, au kinachojumlishwa katika *majimbo* si dhahiri tena. Wakati mwingine, kutegemea vile watu wanavyoongea, na kushughulikia maswala yanayohusu upunguzaji na usambazaji wa madaraka, unaweza kufikiri kuwa neno *majimbo* linamaanisha kuigawa nchi katika maeneo ya kikabila. Wakati mwingine, hutumiwa kurejelea kiungo cha upunguzaji na usambazaji wa madaraka, mkoa, kinyume na wilaya. Baadhi ya tafakari hizi haziambatani kamwe na mfumo wa majimbo uliokuwepo wakati Kenya ilipojinyakulia uhuru. Thamani na sifa kuu za mfumo wa *majimbo* uliokuwepo wakati wa uhuru ni kama zifuatazo:

- taifa liligawanywa katika maeneo saba – Pwani, Mashariki, Bonde la ufa, Nyanza, Magharibi, na Nairobi;
- baraza la eneo liliundwa na wanachama waliochaguliwa na walioteuliwa kupitia njia maalum, ambao idadi yao ilikuwa idadi ya wabunge waliochaguliwa ikigawanywa mara nane (8). Mtu alihitajika kuonyesha kuwa anahusika kikweli na eneo kabla ya kupiga kura;
- Rais wa eneo alichaguliwa na wanachama waliochaguliwa kutoka miongoni mwao au kutoka katika wale walio na sifa za mtu anayestahili kuchaguliwa. Mgombeaji alihitajika kupata wingi wa kura wa theluthi mbili (2/3) za wapiga kura, na angeondolewa kwa ¾ ya wanachama;
- Makamu wa Rais aliyechaguliwa na kuondelewa kupitia utaratibu sawa na ule wa Rais;
- mamlaka makuu ya maeneo yalikuwa katika kamati iliyojulikana kama kamati ya Fedha na Mipango. Kamati hii ilikuwa na uwezo wa kuunda kamati zingine kushughulikia biashara na viwanda, elimu, afya, ardhi, kilimo na misitu, utawala wa serikali za wilaya, nidhamu ya umma na usalama, ujenzi na mawasiliano. Eneo lilikuwa na uwezo wa kutoza kodi kutoka kwa shughuli ndogondogo za kibiashara, na shughuli zinazohusiana na biashara,

huku serikali kuu ikiwajibika kutoa asilimia fulani ya mapato yake kwa maeneo;

- katibu wa umma kwa kila eneo aliteuliwa na Tume ya Huduma kwa Umma kwa mashauriano na Rais wa Eneo hilo. Katibu wa umma alisimamia wafanyikazi wa umma ambao wengi wao walipelekwa huko na Tume ya Huduma kwa Umma kwa mashauriano na Eneo;
- kikosi cha Polisi cha eneo kilichoongozwa na Kamishna wa Polisi wa Eneo aliyeteuliwa na Tume ya Huduma ya Polisi kwa nashauriano na Eneo; na
- orodha ndefu ya sehemu za utendekazi wa kisheria kwa maeneo, ikionyesha maswala yanayoweza kushughulikiwa na Baraza la kieneo, na mengine ambayo yanaweza kushugulikiwa kwa pamoja na Baraza la kitaifa.

Mipaka ya kieneo ingebadilishwa tu baada ya kuidhinishwa na baraza la eneo, na kwa uamuzi uliopitishwa na Kumbi mbili za Baraza la Kitaifa.

Katiba pia ilizingatia mfumo wa serikali za Wilaya. Kila Eneo liligawanywa katika sehemu za mamlaka zilizoongozwa na mabaraza ya mamlaka za nyanjani. Kulikuwepo Tume ya Eneo ya Wafanyikazi wa serikali za wilaya iliyosimamia maslahi ya wafanyikazi wa mamlaka za nyanjani katika Eneo. Kulikuwa na Waziri wa Serikali ya kitaifa aliyesimamia maeneo ya serikali za wilaya na aliyehakikisha kuwa walionyesha maadili ya hali ya juu katika shughuli zao. Maeneo hayo yaliondolewa kupitia mabadiliko ya Katiba yaliyopangwa sawa sawa katika kipindi cha kati ya mwaka 1964 – 1969. Mabadiliko ya kwanza yalifanywa mwaka 1964 na kuondoa uwezo wote kutoka kwa mabaraza ya maeneo, isipokuwa ule uwezo uliokuwa umezingatiwa mahsusi. Mwezi uliofuata, mabadiliko mengine ya Katiba yaliondoa ibara fulani zilizokuwa zimezingatiwa katika Katiba kwa njia iliyo maalum, hasa ibara zilizohusu uhusiano wa maeneo. Mabadiliko hayo pia yalilegeza njia za kubadilisha Mabaraza ya Maeneo.

Mnamo Juni 1965, Katiba ilibadilishwa kwa mara ya tatu kuondoa kuzingatiwa kimaalum kwa sehemu fulani kuhusu uwezo mkuu wa Mabaraza ya maeneo. Mabadiliko hayo yaliondoa Mabaraza ya maeneo na kufuata Mabaraza za Mikoa. Mnamo 1968,

ukumbi wa juu wa Bunge, Seneti, uliunganishwa na Ukumbi wa wawakilishi kuunda Bunge la Ukumbi mmoja. Muda wa Bunge uliongezwa kwa miaka miwili huku wilaya za kiseneti zikiunganishwa na kuunda maeneobunge. Baadaye, Mabaraza ya mikoa yaliondolewa na sehemu zilizozuia kubadilishwa kusikotabirika kwa mipaka ya mikoa na wilaya pia zikaondolewa.

***(b) Katiba Iliyopo Sasa***

Katiba ya sasa haizingatii njia yoyote ya kupunguza na kusambaza madaraka wala kurejelea mfumo wa serikali za wilaya. Mahali pa pekee ambapo serikali za wilaya zimetajwa ni katika sehemu inayoweka ardhi amana chini ya mabaraza ya wilaya. Hata hivyo, mfumo wa serikali za wilaya unatumika.

*(i) Mfumo wa mabaraza ya nyanjani*

Sheria ya Serikali za Wilaya (Sura ya 265) inaunda mfumo kamili wa mabaraza ya mashinani yanayosimamiwa na waziri za serikali wa wilaya.

Kuna aina tofauti ya Mabaraza: Mabaraza ya Wilaya, Mabaraza ya Majiji, Mabaraza ya Jiji, Mabaraza ya mji na Mabaraza ya Miji. Utaratibu zaidi wa kuweka mipaka ya Serikali za Wilaya, Katiba ya mamlaka na uchaguzi, shughuli za baraza, usimamizi wa jumla na kamati za baraza, uwezo, wajibu na majukumu, fedha za baraza na kuarifu, kuchunguza na kidhibiti mamlaka za mashinani unatolewa na sheria hiyo. Waziri wa serikali za wilaya ana uwezo mkuu juu ya mabaraza. Uwezo huu unajumuisha kufanya sehemu yoyote kuwa au kukoma kuwa manispaa, baraza la wilaya, au mji, kutoa au kubadili jina la manispaa, baraza la wilaya au mji ama kuongeza au kupunguza sehemu yake, kuunganisha mabaraza mawili ya wilaya na kulifanya baraza moja, kuchuguza shughuli za mamlaka za mashinani na kutoa agizo la kuvunjwa kwa mamlaka ya mashinani na kuteua tume, miongoni mwa mambo mengine. Mamlaka haya yanaundwa na idadi fulani ya madiwani wanaochaguliwa wanateuliwa. Tume ya Uchaguzi huunda maeneo ya uchaguzi na mipaka inayotumiwa kuwachagua madiwani. Madiwani maalum

hutegemea idadi ya madiwani kutoka vyama vya kisiasa vilivyo na madiwani katika mabaraza hayo.

Uchaguzi wa mabaraza ya mashinani una msingi wake kwenye wodi. Tume ya Uchaguzi imeingilia kati kuleta usawazisho katika wodi kadhaa. Baada ya kusikiza maoni ya wananchi, Tume hiyo ilipunguza kwa kiasi kikubwa idadi ya wodi zilizokuwa zimeundwa bila sababu muhimu na pia kutokana na sababu za kisiasa.

Katika mkutano wao wa kwanza baada ya uchaguzi, Madiwani huchagua viongozi wao, kwa upande wa Mabaraza ya Jiji na Manispaa, Meya na Naibu wa Meya ; na kwa upande wa Mabaraza ya Wilaya na Miji, Mwenyekiti na Naibu wa Mwenyekiti.

Mamlaka za mashinani huendeshwa na maafisa wa serikali kutoka Tume ya Huduma kwa Umma. Mara nyingi mpangilio huu umezifanya mamlaka za mashinani kupata matatizo kwani maafisa wa serikali wanaopelekwa katika mamlaka hizo hukosa kuwatii madiwani waliochaguliwa na, kwa hivyo, mizozo baina ya maafisa hao na madiwani ni jambo la kila mara.

Jukumu la kimsingi la mamlaka za mashinani ni kutoa huduma kwa wakazi katika maeneo ya mamlaka yao kisheria. Hili linajumuisha utoaji wa soko na maslahi ya kijamii, kusimamia uuzaji wa pombe na biashara fulani fulani na kupanga matumizi ya ardhi.

Mamlaka za mashinani kwa kiwango kikubwa hufadhiliwa na serikali kuu ingawa huweza kupata mapato yake moja kwa moja kupitia utoaji wa leseni kwa maeneo ya kufanyia biashara. Sheria ya hazina ya mamlaka za mashinani ya 1998 inaunda hazina ya mamlaka za mashinani ambayo serikali huchagia asilimia tano (5%) ya kodi zote zilizokusanywa kufadhili shughuli za mamlaka za mashinani.

Tume ya Uchaguzi shughuli za mamlaka za mashinani (Tume ya Omamo) na makundi mengine, yakiwemo maoni yaliyotolewa kwa Tume hii, yamebaini matatizo kadhaa yanayozikumba mamlaka za mashinani. Miongoni mwa matatizo hayo ni:

- Majukumu ya serikali za wilaya kwa kiwango kikubwa ni ya kiusimamizi na kiurekebishi, na hayahusu hasa kujisimamia;
- Mikakati ya maendeleo katika mamlaka za mashinani hutegemea mipaka ya serikali kuu;
- Kuwekwa kwa uwezo wote katika wizara za serikali kumezua vizingiti kwa maendeleo ya serikali za wilaya;
- Ufadhili kwa mamlaka za wilaya kutoka kwa serikali kuu hautoshi;
- Kwa jumla hakuna wataalamu wa usimamizi na kiufundi na hali hii imekuwa kizingiti kwa uundaji wa asasi bora za serikali za wilaya na uhusiano bora wa kikazi kati ya serikali za wilaya na serikali kuu;
- Uundaji wa mabaraza hautabiriki na hutekelezwa bila kutafuta ushauri wa wakazi. Ni kweli kuwa mabaraza ya wilaya, miji na manispaa yameundwa bila utaratibu wowote na kwa hivyo hakuna mlingano wa aina yoyote kote nchini;
- Sheria ya serikali za wilaya haitekelezwi kwa njia iliyo sawa kote nchini na haifai katika maeneo mengine. Kwa mfano, sheria hiyo haiweki wazi athari au matokeo ya vyeo au hadhi fulani – Jiji la Nairobi limekuwa na Baraza la Jiji tangu mwaka 1950, licha ya kuwa hakuna utaratibu wa kuundwa kwa Baraza la Jiji, na sheria hiyo pia haielezei wazi wajibu muhimu na manufaa ya baraza la Jiji. Sheria haesemi kuwa kila wilaya itakuwa na baraza la wilaya;
- Utaratibu wa kuunda mamlaka za nyanjani haufai na matokeo yake huwa mabaraza mabovu yasiyofaa. Hakuna utaratibu au sifa za kuteuliwa kuwa diwani wala maelezo ya makundi yaliyo na maslahi maalum. Madiwami maalum hujali tu na hutumikia maslahi ya vyama vilivyowateua au wanasiasa binafsi;
- Wizara ya serikali za wilaya haina vifaa au uwezo wa kusimamia mamlaka za nyanjani ipasavyo. Waziri ana uwezo mkubwa anaoutekeleza kwa uamuzi wake binafsi bila kushauriana na, au kuwahusisha raia. Mawaziri wametumia uwezo kama huo kuunda mabaraza ya wilaya na manispaaa kiholela;

- Hali ya kuwa uwezo na fedha za serikali za wilaya hazilindwi na katiba imeufanya mfumo mzima kuingizwa udanganyifu, ufisadi wa hali ya juu na waziri wa serikali za wilaya kuwa na mamlaka kamili yasiyozuilika.


*(ii) Utawala wa Mkoa*

Licha ya mamlaka za nyanjani, kuna mfumo wa utawala wa mkoa, ingawa Katiba ya Kenya haisemi lolote kuhusu mfumo huu. Kihistoria utawala na mkoa ni asasi za utawala za wakati wa ukoloni, zilizoundwa kuhakikisha kuwa utawala wa wakoloni unapata kufahamu kila kitu kilichokuwa kikiendelea kote nchini. Ulikuwa, kama ilivyo sasa, mfumo wa kuondoa mamlaka kutoka serikali kuu na kuyasambaza kwa kuwapeleka mawakala wa serikali kuu katika vitengo mbali mbali vya kiutawala kote nchini. Moja kati ya sifa kuu ya mfumo huu ni kuwa haukuwahusisha umma katika utawala, na katika kutoa maoni kwa Tume, Mfumo huu umetajwa kuwa ….“unaopinga haki ya wananchi ya kujitawala wenyewe.…”.

Hivi leo, jukumu na hali yake haijabadilika pakubwa, isipokuwa kwamba mfumo huu pia umeendelea kutekeleza jukumu muhimu katika kupanga na kutekeleza sera za serikali, kusimamia umma na kuhakisisha kuwepo kwa usalama kuanzia kiwango cha mkoa hadi kijijini. Wasimamizi wote wa mkoa huhudhuria mafunzo ya usalama kuwawezesha kutekeleza majukumu yanayohusiana na sheria na utangamano. Kwa mfano, katika hati ya mkakati wa kupunguza umaskini, imesemwa kuwa “utawala wa mkoa unawajibika kutoa uongozi, mwelekeo wa sera na hali bora ili kuafikia uthabiti kijamii, kiuchumi na kisiasa”. Muundo wa utawala wa mkoa kama ulivyo katika Mchoro 3 a hapa chini, unajumuisha Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Taarafa, Machifu na Manaibu wa Machifu. Chini ya Sheria ya Machifu (Sura ya 128) machifu na wasaidizi wa Machifu wana uwezo mwingi kiutawala na kisheria na mafaraka ya utangamano. Wana majukumu kuhusiana na afya ya umma (kama vile kuzuia uchafuzi wa maji), kuzuia uhalifu (kama vile kuwatia watu nguvuni na kutwaa ngombe waliyoibwa). Waziri anaweza kumuagiza Chifu kuwataka wananchi kutoa huduma kwa jamii katika nyakati za hatari au kuhifahdi raslimali maliasili.

**Mchoro 3**

**Muundo wa Utawala wa Mkoa**



Utawala huu umekosolewa sana ukitajwa kuwa wa kiimila na unaowanyima wananchi uhuru wa kuchagua wanachokipenda. Malalamiko kuhusu matumizi mabaya ya uwezo, ufisadi na kukiuka haki za raia yametolewa kuhusu mfumo huu umetumiwa.

Pia katika kuzuia siasa za uwingi. Ijapokuwa baadhi ya sifa za mfumo huu zilizochukiza zaidi zilikuwa wakati sheria ya Machifu ilipobadilishwa mnamo mwaka 1977, ukweli ni kwamba uendeshaji wa shughuli za utawala wa mkoa haujabadilika.

### 12.2.3 Upunguzaji na Usambazaji Madaraka katika Katiba Nyingine

Kama tulivyoonyesha, upunguzaji na usambazaji madaraka unaweza kuchukua mikondo mingi. Usambaji wa majukumu baina ya vitengo vya serikali na kiwango cha ugawaji wa madaraka hutegemea muundo wa upunguzaji na usambazaji madaraka. Nchi zenye mifumo yenye muundo mkubwa ni ambazo zinazovuka mipaka ya nchi kishirikisho kama Switzerland na Umoja wa Ulaya. Mifumo kama hiyo huruhusu nchi huru na mbali kuja pamoja kwa malengo maalum, kama masuala ya kigeni na ulinzi, na kuanzia hivi majuzi, uchumi. Nyingine ni mfumo ya shirikisho, kama Marekani, India, Nigeria, Malaysia na Brazil. Katika mifumo ya shirikisho, mara nyingi kuna eneo lenye nguvu na serikali ya kijumla. Kila kitengo hutumia madaraka yake iliyopewa na wananchi. Nchi 23 ulimwenguni ni za shirikisho kirasmi. Pia kuna zile zilizopunguzwa madaraka katika makao makuu zinazofanya kati kutegemea miundo ya kimaeneo au serikali za mitaa. Kiwango cha upunguzaji na usambazaji madaraka katika mifumo hii kinatofautiana kutegemea masuala yanayodhibitiwa na katiba. Katiba nyingi za mataifa ya Afrika zimekitisha mfumo huu. Kwa vyovyote, kanuni za katiba zinazohusu upunguzaji na usambazaji madaraka, huhakikisha, pamoja na mengine:

- Muundo uliowazi kwa kila kiwango cha upunguzaji na usambaji;
- Maeneo maalum ya majukumu kwa serikali ya taifa katika viwango tofauti vya upunguzaji na usambazaji madaraka;

- Mahusiano baina ya serikali miongoni mwa vitengo vilivyopunguziwa na kusambaziwa madaraka na serikali ya taifa;
- Udhibiti wa kifedha na rasilmali katika vitengo vya serikali vilivyopunguzwa na kusambaziwa madaraka;
- Mfumo wa uwakilishi wa wananchi katika vitengo vilivyopunguziwa na kusambaziwa madaraka.

### 12.2.4 Waliyosema Watu

Watu wengi walizungumzia swala la kupunguza na kusambaza madaraka. Maoni yao yanaweza kuwashilishwa kimukhtasari ifuatavyo:-

*(i) Kuhusu muundo, kwamba*

(a) serikali itakiwe kuigawanya faida inayotokana na rasilmali kati ya serikali ya kitaifa na jamii ambamo rasilmali hizi zinapatikana;

(b) huku wengine wakisema madaraka yapunguzwe na kusambaziwa mikoa, wengine walipendelea wilaya kuwa viungo muhimu vya upunguzaji na usambazaji wa madaraka;

(c) watu wengi hasa kutoka mikoa ya pwani na Bonde la Ufa, walipendekeza kuanzishwa kwa mfumo wa majimbo, upande mwingine, watu wengi walipinga kuanzishwa kwa mfumo wa majimbo;

(d) serikali za wilaya ziliungwa mkono sana na watu walipendekeza kuanzishwa kwake ili ziweze kusaidia serikali katika usimamizi utawala na maendeleo nyanjani;

(e) pia kulikuwa na hisia nyingi kuhusu:

  - kutengwa na serikali kuu, kwani uwezo mkubwa umelundikiwa serikali ya kitaifa na kwa kiasi kikubwa Rais. Uwezo pia umewekwa katika mji mkuu;
  - mamlaka za nyanjani zimefanywa kuwa dhaifu;
  - kutengwa na kupuuzwa kutokana na msimamo wao kisiasa.

- kunyanganywa rasilmali kupitia njia isiyo halali;
- matatizo yao yanatokana na sera za serikali wasizoweza kubadili;
- kupunguza na kusambaza madaraka (labda kutokana na muundo tofauti wa maeneobunge). Kunaweza kuipa mifumo ya uwakilishi Bungeni na nyanjani udhibiti mkubwa wa rasilmali, hasa ardhi;
- kuwa panapaswa kuwepo na njia mbalimbali za kupanga jamii ikiwa ni pamoja na kuwapa wazee majukumu;
- kuwa wanapaswa kumezeshwa kufanya uamuzi wao wenyewe na pia kuhusu hali ya maisha kama vile ufugaji wa kuhamahama.

*(ii) Kuhusu kuchaguliwa kwa madiwani kwamba*

(a) Madiwani wote wachaguliwe – kusiwe na madiwani maalum wanaoteuliwa;
(b) Meya na wenyeviti wa mamlaka za nyanjani wanapaswa kuchaguliwa moja kwa moja na wananchi;
(c) Madiwani watahitajika kuwa na sifa za kiwango cha chini cha elimu;
(d) Kunapaswa kuwa na asilimia fulani ya wanawake katika mabaraza ya mashinani;
(e) Uchaguzi wa mashinani usiwe katika misingi ya vyama.

*(iii) Kuhusu usimamizi wa ardhi:-*

(a) Machifu wachaguliwe;
(b) Asasi za kitamaduni ikiwa ni pamoja na wazee zinapaswa kutafutiwa majukumu fulani;
(c) Baraza la wazee liundwe kushughulikia maswala ya utawala na maendeleo vijijini;
(d) Utawala wa mkoa uondolewe kabisa au, viwango vya wilaya kwenda chini pekee vibakizwe huku kiwango cha mkoa kikiondolewa

(e) Utawala wa mkoa uondolewe na nafasi yake kuchukuliwa na utawala wa mamlaka za nyanjani ulioimarishwa, au na makundi yaliyochaguliwa, ili yaweze kuwajibika kwa wananchi.

*(iv) Kuhusu masuala mengine, kwamba*

(a) Jamii zinapaswa kusimamia ardhi yazo zenyewe;

(b) Wilaya zisiwe na majina ya kikabila kama vile Kuria, Kisii na Embu;

(c) Mabaraza ya mashinani yanapaswa kuhusishwa katika kufanya uamuzi katika kiwango cha juu kupitia kuundwa kwa seneti;

(d) Makadirio ya matumizi na mapato ya fedha mamlaka za nyanjani yanapaswa kufanyiwa nyanjani;

(e) Jamii zinapaswa kuhusishwa katika usimamizi wa rasilmali zilizo katika jamii hizo. Jamii hizo pia zinapaswa kunufaika kutokana na rasilmali hizo na kodi inayokusanywa kutoka kwa wananchi. Kampuni zinapaswa kugawanywa kwa njia ya haki kati ya serikali kuu na mamlaka za nyanjani, na kuwa mamlaka za nyanjani zinapaswa kujisimamia kifedha, bila kuingiliwa na Bunge.

*(v) Kuhusu kutawanya madaraka, kwa jumla, kwamba*

(a) tuwe na kupunguza na kusambaza madaraka na majukumu ya serikali kuu;

(b) kuwe na kukomeshwa kwa historia ya wakati wa ukoloni na pia ya baada ukoloni kuzinyima jamii nafasi ya kushiriki katika utawala wa mashinani;

(c) vyombo vya upunguzaji na usambazaji madaraka view ni pamoja na:

- Baraza la mkoa – Mkuu wa Mkoa aliyechaguliwa na naibu wake na wawakilishi wawili wa wilaya;
- aina mbili za mamlaka ya wilaya, mamlaka ya mashambani na baraza mitaa;

- mabaraza ya usimamizi wa serikali ya mitaa zinazofanya kwa ushauriano na mabaraza ya mikoa kusimamia majukumu ya mamlaka ya mashinani;

(d) Majukumu ya mamlaka ya mashinani yawe:

- kutoa huduma za jamii;
- kudumisha miundo msingi mashinani, kama barabara, hospitali, shule, na viwanja vya starehe;
- kuendeleza shughuli za kitamaduni; na
- kuendeleza demokrasia husishi katika jamii.

*(vi) Kuhusu mfumo wa utawala wa mkoa*

a) Kwa kuwa wakuu wa wilaya na wakuu wa taarafa huwa si watu wanaotoka katika maeneo wanakopelekwa, huwa ufahamu mdogo kuhusu hali ya maslahi ya watu;

b) Hivi karibuni kumekuwa na hali ambapo watu wanaoajiriwa katika utawala wa mkoa hutoka katika kabila moja, au maeneo yanayomuunga Rais mkono kisiasa. Mkuu wa Mkoa wa sasa katika mkoa wa kaskazini-mashariki ndiye wa kwanza kutoka sehemu hiyo, na hali hiyo imeleta mabadiliko makubwa katika majukumu ya afisi hiyo;

c) Kumekuwa na malalamiko kuwa tabia ya machifu inaonyesha kuwa Sheria ya Chifu imerekebishwa;

d) Matumizi ya utawala wa mkoa, ulio na ukuruba mkubwa na chama tawala huchukuliwa kama kizingiti cha haki katika uchaguzi kwa sababu utawala wa mkoa ndio hulinda usalama kuhakikisha utangamano katika vituo vya kupigia kura, na kimsingi kuendesha uchaguzi. Tume ya Uchaguzi huutengemea mno wakati wa uchaguzi;

e) Ijapokuwa watu hawautegemei utawala wa mkoa kwa usaidizi, wanawake wamewahi kulalamikia kutoshughulikiwa wakati mwingine hasa katika maswala yanayohusu mizozo ya nyumbani;

f) Watu walilalamikia ufisadi uliokithiri, ukosefu wa wafanyikazi wa kutosha, vifaa duni, na ukosefu wa mbinu za kutatua mizozo, ukosefu wa uwezo wa kusimamia shughuli zinazohusu kuvuka mipaka, utoaji wa huduma duni, na utaratibu duni maendeleo ya mashambani;
g) Kamati za maendeleo ya wilaya kama zinavyoundwa hivi sasa haziwakilishi watu wa jamii husika. Wengi wa wanachama ni wafanyikazi wa serikali wasiotoka sehemu hizo na hukaa kwa muda mfupi mno katika nyadhifa zao;
h) Mfumo huo huathiri vibaya serikali za wilayani. Mara nyingi, utawala wa mkoa umekataa kushirikiana na mamlaka za nyanjani, kupuuza maoni yao, na kuwanyima leseni na ufadhili kutoka kwa serikali kuu;
i) Mfumo wa jumla wa makundi yanayofanya uamuzi katika utawala wa mkoa haupati ufadhili wa kutosha, una urasimu mwingi, na umekitwa zaidi katika mahali pamoja;
j) Utaratibu wa kuundoa utawala wa mkoa pole pole uanzishwe na kuhamishia mfumo mpya wa serikali za wilaya majukumu yake.
k) Ikiwa utawala wa mkoa hautaondolewa, basi unapaswa kuajibika zaidi kwa umma au nafasi yake ichukuliwe na utawala wa mamlaka za nyanjani, utakaowajibika kwa umma; na
l) Maendeleo yoyote, upangaji, uundaji wa sera na utoaji wa fedha za matumizi unapaswa kuzihusisha jamii za maeneo husika.

### 12.2.5 Uchanganuzi

Kuna makubaliano kati ya watu kuwa mamlaka ya Serikali yanapaswa kupinguzwa na kusambazwa.

Ilikuwa pia wazi kwamba watu wametaka majukumu yanayotekelezwa na utawala wa mkoa kutekelezwa na mawakala wa serikali za wilaya. Kulikuwa na makubaliano ya jumla kuwa utawala wa mkoa ulivyo sasa unastahili kuondolewa.

Ijapokuwa kulikuwa na makubaliano ya jumla kati ya Wakenya kuwa kupunguza na kusambaza madaraka ni muhimu, hapakuwa na makubaliano kamili kuhusu muundo na viwango vya upunguzaji na usambazaji wa madaraka vinavyopaswa kutekelezwa. Huku watu wengi katika mkoa kama vile Pwani na sehemu za Kaskazini. Mashariki na Bonde la Ufa wakipendeza mfumo wa kishirikisho (majimbo), watu wengi katika mkoa wa Kati, Nairobi, Mashariki na Magharibi na sehemu fulani za Nyanza walipendekeza mfumo wa umoja. Katika hali zote ni ufafanuzi wa kuridhisha haukutolewa.

Hata hivyo, watu wanajiona kama ambao ni watumwa badala ya wananchi. Kwa hivi sasa, wanaliona kama ambao wamenyimwa uwezo na kutengwa kutokana na serikali. Wanaonelea kuwa maamuzi kuhusu maisha yao yanafanywa katika maeneo yaliyo mbali sana nao, na bila ya kutaka ushauri wao. Wanachukulia kuwa wamebaguliwa na kuumba wamenyang’anywa rasilmali yao kupitia njia isiyo ya haki. Kuna hisia ambayo imesambaa sana kuwa watu wanapaswa kusimamia maisha yao wenyewe. Wanataka kutumia asasi za jamii katika usimamizi wa ardhi na maswala mengine yanayopatikana katika jamii; wanataka uwezo/mamlaka karibu na mahali wanapoishi na kushiriki katika maswala ya umma.

Tume kwa hivyo haina shaka kuwa kuambatana na malengo ya marekebisho, na maoni ya watu, panapaswa kuwepo usambazaji wa kufaa wa uwezo na majukumu hadi kwenye viwango vya mashinani. Ni wazi pia kuwa uhamishaji unapaswa kuwa kwa makundi yanayozingatia demokrasia na yanayohusisha. Watu hawatatosheka na upunguzaji na usambazaji wa madaraka kiutawala.

Tume inaamini kuwa njia bora ni kuunda mfumo wa kupunguza madaraka unaozingatia sababu zilizotolewa na watu katika kupendekeza au kuunga mkono upunguzaji na usambazaji wa madaraka.

Madai haya, yakifungamanishwa ama kuelezwa kwa njia ya upunguzaji na usambazaji wa madaraka, yanaweza kuchukuliwa kuwa ukosoaji wa mfumo wa sasa wa kisiasa na

jinsi ambavyo yametumiwa kama matamanio ya mfumo mwingine tofauti wa kisiasa. Tume inaamini kuwa baadhi ya matatizo ya kutengwa na ugawanyaji wa rasilmali usio wa haki yanaweza kutatuliwa na mfumo wa serikali unaopendekezwa. Mfumo mpya utakuwa husishi na watu watapata fursa na utaratibu wa kuathiri sera na asasi wanazoweza kufikisha malalamiko yao. Wataondolewa mzigo mkubwa wa utawala wa mkoa.

### 12.2.6 Mapendekezo

Tume inapendekeza kwa hivyo:

i) *Kuhusu kanuni za upunguzaji na usambazaji madaraka kwamba*

a) Mtindo wa upunguzaji na usambazaji utakaotumiwa unapaswa kuzingatia uhusiano baina ya gharama na manufaa ya upunguzaji na usambazaji madaraka nchini Kenya – kile ambacho upunguzaji na usambazaji madaraka umelenga kufikia;

b) Viwango vya upunguzaji na usambazji na uwezo kamili utakaopewa vitengo vitakavyohusika utafafanuliwa wazi na sheria ya Bunge;

c) Mtindo wa upunguzaji na usambazaji wa madaraka unapaswa kuzingatia kanuni za jumla zifuatazo:

- Uwekaji wa mipaka ya mujukumu na uwezo kati na miongoni mwa vitengo kwa njia inayohakikisha kuwepo kwa vipimo ya uwezo na kupunguza mizozo inayohusiana na matumizi ya mamlaka;
- Uhamasishaji, ugawanyaji na usimamizi thabiti wa raslimali;
- Haja ya kuimarisha utawala husishi, kutambua na kukubali kuwepo kwa makabila mengi; mahitaji ya makundi yaliyomo hatarini, kama vile wanawake, watoto, wasiojiweza, walio wachache na wanaotengwa au makundi ya pembeni.

d) Mipango ya kifedha kwa vitengo vya upunguzaji na usambazaji wa madaraka na kwa uhusiano baina ya serikali ya kitaifa na vitengo ikiwa ni pamoja na vitengo vya kuratibu ushirikiano baina ya viwango tofauti vya

serikali (kitaifa, kimkoa, kiwilaya na taarafa). Ushirikiano huu uendeshwe kwa njia ambayo inahakikisha uhuru na uwajibikaji na vitendo vilivyopunguziwa madaraka;

e) Katiba mpya inapasa kuweka mbinu za mpito kuhusu uundaji wa hali ilivyo sasa na kuleta utaratibu mpaya;
f) Panapaswa kuwepo mbinu za kutatua mizozo zilizojengeka ndani kwa ndani;
g) Vitengo viliyopunguziwa madaraka vina haki ya kupata kiwango sawa cha mapato ya kitaifa kuviwezesha kutoa huduma za kimsingi na kutekeleza wajibu wavyo;
h) Asasi na idara za kitaifa za serikali zinapaswa kupangwa kwa njia inayohakikisha ugawanyaji sawa wa raslimali kote nchini;
i) Maelezo zaidi ya utekelezaji kazi wa vitengo vilivyosambaziwa madaraka yanaweza kutolewa katika sheria ya Bunge.

*(ii) Kuhusu muundo wa upunguzaji na usambazaji wa madaraka kwamba*

(a) Kuwepo muundo wa matagaa matano wa upunguzaji na usambazaji wa madaraka unaojumuisha asasi katika viwango vya kitaifa, mkoa, wilaya, kata na vijiji, huku wilaya ikiwa kitengo kikuu cha upunguzaji na usambazaji wa madaraka chini ya viwango vya kitaifa vilivyoonyeshwa katika mchoro 12b;
(b) Utaratibu tofauti utawekwa kwa ajili ya maeneo ya miji;
(c) Mfumo wa upunguzaji na usambazaji wa madaraka uwe na msingi wake kwenye mabaraza yaliyochaguliwa na maafisa; waliochaguliwa;watakaowajibika kwa mabaraza katika kila kiwango, watakaokuwa na sifa ya mamlaka yaliyotofautishwa;
(d) Angalau thuluthi moja ya wanachama wa kila baraza watakuwa wanawake;
(e) Mfumo wa uchaguzi utahakikisha uwakilishwaji wa jamii zote za kitamaduni katika kila kiwango;
(f) Sheria ya Bunge itaweka uwezakano wa kuliondoa baraza au kuondolewa na wapiga kura;

(g) Kijiji na kata vinaweza kuwa na mamlaka makuu mradi vitahusika kwa kisiasi kikubwa na utekelezaji wa sera za baraza la wilaya, lakini mabaraza ya vijiji na kata yatajumuisha mipango ya maeneo yao, na utatuzi wa mizozo kupitia njia ya mahakama ndogo ya madai;


(h) Mabaraza ya wilaya na mkoa yatakuwa na uwezo wa kisheria na uwezo mkuu;


(i) Maslahi ya mabaraza ya mkoa na wilaya yanaweza kujalizana lakini yasigongane;

(j) Vitengo vya uchaguzi vitaamuliwa na sheria za uchaguzi.

**Mchoro 12b**

**Muundo wa upunguzaji na usambazaji wa madaraka unaopendekezwa**






*(iii)* *Kuhusu Vitengo vya Upunguzaji na Usambazaji wa Madaraka.*

a) Kuwa mabaraza ya vijiji yanaweza:
   - Kuhamasisha wakazi kuhuzu masuala ya kijijini, na kuwa kiunganishe kati ya kijiji na kata/wodi.
   - Kusimamiwa na kuongozwa na wazee wa kijiji.

b) Kuwa mabaraza ya mashinani:
   - Yatawezesha jamii kusimamia shughuli zao yenyewe.
   - Yatatekeleza tu mamlaka makuu, na hasa kuhusu:
     - o Usimamizi katika kiwango cha mashinani;
     - o Kuanzisha miradi ya maendeleo;
     - o Kushauri baraza la wilaya kuhusu maswala yanayoiathiri jamii;
     - o Kutatua mizozo kwa kutumia njia ya mahakama ndogo za madai;

- Kuwahamasisha watu na kuweka katika vitengo vidogo vidogo ya nyanjani;
- Kuhamasisha na kusimamia raslimali, hazina ya maendeleo na shughuli za jamii.
- Kutekeleza sera zilizoidhinishwa na Baraza la Wilaya kuhusu maendeleo ya kata.

- yataendeshwa na baraza la wazee wa kijiji. Baraza hilo litakuwa na wazee wa kijiji. Baraza hilo litakuwa na wawakilishi wawili kutoka kila kijiji katika kata hiyo. Wawakilishi hao watakaochaguliwa, watawachagua, mwenyekiti, mweka hazina na maafisa wengine.
- kamati kuu ya kata itajumuisha maafisa wa Baraza na msimamizi kama mwanachama kwa wadhifa wake.
- Kutakuwa na kituo kidogo cha Uhasibu wa shughuli za baraza la kata.
- msimamizi wa kata atachaguliwa moja kwa moja na watu kama ilivyoelezwa na baraza la wilaya.

c) Kuwa mabaraza ya Wilaya

- yatakuwa kiwango kikuu cha upunguzaji na usambazaji wa madaraka;
- yatatekeleza majukumu yote ya kisheria na kiutawala;
- yatakuwa na baraza la wilaya kama kiungo chake cha kisheria;
- yatakuwa na kiungo kikuu kitakachowajibika kwa Baraza la Wilaya;
- yatakuwa na uwezo wa kuwaajiri na kuwaachisha kazi wafanyi kazi wake;
- yatakuwa na uwezo wa:-
    - kuunda sera katika maeneo yake kisheria;
    - kutoa huduma za umma na miundo msingi;
    - kutekeleza miradi ya maendeleo;
    - kuwa na mapato yao yenyewe kufuatia utozaji kodi, kima na ushuru na kutumia mapato hayo;
    - kushirikiana na mamlaka makuu;
    - kuajiri na kuwaachisha kazi wafanyi kazi wake.

- yataundwa kwa madiwani kutoka idadi ya wodi zilizoko sasa katika mabaraza ya wilaya watakaochaguliwa ifuatavyo:
    - o Madiwani wachaguliwe kuhudumu kwa awamu ya miaka minne;
    - o Uchaguzi uendeshwe na Tume ya Uchaguzi ya Kenya;
    - o Lazima wagombeaji wawe na elimu ya kiwango cha K.C.S.E.;
    - o Uteuzi wa wagombeaji uwe kupitia vyama vya kisiasa. Hata hivyo wagombeaji wa kujitegemea pia watakubaliwa katika kiwango hiki;
    - o Wagombeaji uteuzi wawe na umri wa miaka isiyopungua 21.

- Kikanuni, yakubaliwe na yaweze kuendesha shughuli zake chini ya sheria za kitaifa wakati ambapo kuna sheria zinazolandana, lakini yatakubaliwa kutumia sheria za kitaifa katika kiwango cha mashinani, kwa kutegemea masharti yaliyowekwa katika sheria ya Bunge. Kwa hivyo yaliyomo na mtindo wa kuandika sheria za kitaifa unapaswa kutoa uwezekano wa sheria hizo kufanyiwa marekebisho na kutekelezwa na Wilaya;
- Kikanuni, yawe nyenzo ambayo kwayo serikali ya kitaifa hutekeleza sera;
- Kikanuni, yaweze kutafuta au kutaka usaidizi wa serikali ya kitaifa katika utekelezaji wa majukumu yake;
- yatakuwa chini ya uwezo wa kisheria wa Mpokea Malalamishi wa Kitaifa, Tume ya Haki za Binadamu, n.k.
- yatachagua mwenyekiti wake katika kikao cha kwanza, ambaye jukumu lake kuu litakuwa kuongoza vikao vya Baraza.
- yatasimamiwa na Gavana wa Wilaya ambaye:
    - o atakuwa Kiongozi wa Kisiasa wa Wilaya;

- atachaguliwa kwa kupigiwa kura na watu wazima katika wilaya kuhudumu kwa awamu ya miaka minne, na aweze kuhudumu kwa awamu mbili pekee;
- ni lazima awe mkazi wa wilaya inayomchagua;
- atakuwa na umri wa miaka isiyopungua 35 na kuzidi 70, na aliyefuzu na kupata shahada katika chuo kikuu kinachotambuliwa.
- ataendesha shughuli za wilaya kwa usaidizi wa watu walio na ujuzi wa kutosha kutoka wilayani. Idadi ya watu watakaomsaidia Gavana itakuwa watu kumi na wataunda Baraza la Mawaziri la Wilaya;
- atawajibika kwa watu katika wilaya moja kwa moja;
- anaweza kuondolewa na wapiga kura, ama kwa kupigiwa kura ya kutokuwa na imani naye na Baraza.

d) Kuwa mabaraza ya mikoa yatajumuisha wenyeviti wa mabaraza ya Wilaya na washikadau wengine. Wanachama wa Baraza la Mkoa watachagua mwenyekiti wao kwa msingi wa kuzunguka. Yatakuwa na mamlaka makuu na mamlaka ya kisheria kuhusu maswala yaliyo chini ya majukumu yake makuu ambayo miongoni mwa mengine yatakuwa

- kuimarisha ushirikiano baina ya wilaya;
- kuongoza uwezo wa wilaya na kufanikisha utekelezaji bora wa majukumu yake;
- kuratibu maswala yanayohusu wilaya katika mkoa;
- kushughulikia maswala ya kimkoa;
- kusimamia taasisi na raslimali za mkoa;
- kupanga kuhusu maendeleo ya mkoa;
- kuendeleza na kusimamia miundomsingi katika mkoa;
- kutoa usaidizi wa kiufundi kwa mabaraza ya wilaya pale inapofaa.

e) Kuwa mabaraza ya miji yataendesha shughuli zake katika mabaraza ya wilaya yanamopatikana ijapokuwa yanaweza kuruhusiwa kubakia na mbinu maalum ya usimamizi kwa kuwa ni "complex mechanisms".
f) Kuwa Nairobi itachukuliwa kama "National Capital Territory" na itasimamiwa kwa mujibu wa sheria ya Bunge.

*(iv)* *Kuhusu uhusiano kati ya Mabaraza ya Wilaya na yale ya Mikoa, kuwa*

Yashirikiane katika utekelezaji wa majukumu yake. Yanaweza kuunda kamati au mamlaka za pamoja kwa madhumuni haya. Uungwaji mkono wa wengi wa wanachama wa kila Baraza utakuwa muhimu kwa ushirikiano. Mipango ya ushirikiano inaweza kukatizwa kupitia kura ya wengi wa Madiwani wa Wilaya.

*(v)* *Kuhusu ugawaji wa maliasili, baina ya Wilaya na Serikali Kuu, kuwa*

Sheria izingatie kuwa kuwa Wilaya zina haki ya kupata mgao wa kutosha kutokana kwa mapato yanayotokana na raslimali zinazopatikana katika wilaya hizo.

*(vi)* *Kuhusu mipango ya kifedha, kwa jumla, kuwa*

(a) Serikali ya kitaifa iwajibike kwa ukusanyaji wa asilimia muhimu za mapato;
(b) mabaraza ya wilaya yanaweza kuweka kodi au ushuru utakaoelezwa katika sheria ya Bunge;
(c) mapato ya kitaifa yagawanywe kwa njia iliyo sawa na mabaraza ya wilaya;
(d) sheria iliyofafanuliwa kwa kina ipitishwe kutoa uwezekano wa:
   - ugawaji wa asilimia fulani kwa jamii ambamo rasilmali zinapatikana;
   - asilimia ya ugawaji wa raslimali za kitaifa zinazopatikana katika maeneo yaliyo chini ya Mabaraza ya Wilaya;
   - kodi na ushuru unaoweza kuwekwa na Baraza la Wilaya;
   - utaratibu wa kifedha na uhasibu wa akaunti za Wilaya.

(e) vituo vya uratibu vya mkoa vifadhiliwe na Mfuko Mkuu wa Fedha za Serikali, michango ya Wilaya mapato yanayopatikana kutokana na mali za mkoa;
(f) wilaya zifadhiliwe na fedha za serikali, “fedha za uhamisho za serikali” na mapato yanaotokana na mali za mashinani;
(g) Akaunti za fedha zilizosambaziwa mashinani zikaguliwe na Mkaguzi Mkuu;
(h) Mapato ya Kitaifa yagawanywe sawa kati ya wilaya na Serikali ya kitaifa.

*(vii) Kuhusu uhusiano baina ya serikali mbali mbali, kuwa:-*

a) Serikali ya kitaifa itaunda wizara (ya upunguzaji na usambazaji wa madaraka/serikali za wilayani), kushughulikia mabaraza ya mikoa na wilaya;
b) Taifa litaunda wizara ya upunguzaji na usambazaji wa madaraka Kushughulikia Mabaraza ya Mikoa na Wilaya.
c) Wafanyikazi wa umma wa serikali kuu wanaopelekwa mikoani na wilayani watashirikiana na Mabaraza ya Mikoa na wilaya kwa madhumuni ya ubadilishanaji wa habari na utaratibu wa sera na usimamizi.
d) baraza la wilaya linaweza kusimamishwa kwa muda iwapo kuna hali ya hatari, vita, ufisadi au ukosefu wa hali ubora uliokithiri mipaka. Isipokuwa kwa hali mbili za kwanza, Baraza lolote lisisimamishwe kwa muda kabla ya tume huru kuchunguza madai yaliyotolewa dhidi yake na Rais kutosheka kuwa madai hayo ni ya kweli. Wakati Baraza limesimamishwa kwa muda, mipango ya kutekeleza majukumu ya Baraza hilo la Wilaya itawekwa, kama ilivyofafanuliwa katika Sheria ya Bunge. Mamlaka hayo yatashirikiana kwa karibu sana na baraza la mkoa. Hakuna kusimamishwa kwa muda kutakakoendelea kwa zaidi ya siku tisini, muda ambao ni lazima uchaguzi mpya wa Baraza hilo ufanywe.
e) Majukumu na raslimali ambazo zitahamishwa mabaraza ya wilaya ziwekwe kuhakikisha kuwa mabaraza yana uwezo unaotakikana.

f) Hakuna mtu yeyote atakaeshikilia afisi ya umma au afisi kisiasa katika serikali kuu, na serikali zilizopunguziwa na kusambaziwa madaraka wakati mmoja.

*(viii) Kuhusu kufutwa wa Utawala wa Mkoa, kuwa:-*

(a) utawala wa mkoa uondolewe.

(b) Serikali kuu inaweza kuwaweka maafisa wake katika mikoa na wilaya kutekeleza majukumu ya serikali kuu.

*(ix) Kuhusu kujumuishwa katika Katiba, kuwa:-*

(a) miundo na viwango vya upunguzaji na usambazaji wa madaraka vijumuishwe katika Katiba.

(b) katiba inapaswa kuoredhesha wilaya na mikoa inayosambaziwa madaraka.

(c) Tume ya Mipaka ambayo tayari imeanzishwa inapaswa kuwa na uwezo wa kuweka, kuondoa, kuunda, kuunda upya, "kunyoosha" mipaka inayohusiana na Mikoa ya Wilaya kwa madhumuni ya Katiba.

*(x) Kuhusu utaratibu wa kutatua mizozo, kuwa:*

(a) Mizozo yote baina ya mabaraza ya wilaya, baina ya mabaraza ya mikoa na baina ya mabaraza ya wilaya na serikali ya kitaifa itashughulikiwa kwanza na mahakama kuu;

(b) Haki ya kukata rufaa ipo kwa Mahakama ya Rufaa na Mahakama ya Juu, katika mpangilio huu.

## SURA YA KUMI NA TATU

## MAZINGIRA NA MALIASILI

### 13.1 Agizo la Tume

Ijapokuwa agizo halitolewi moja kwa moja kuhusiana na mazingira, sheria ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya pamoja na mengine inahitaji Tume kuhakikisha kwamba Katiba ina utaratibu sawa wa ukuaji wa uchumi na kuweza kufikia raslimali za kitaifa. Bila shaka hali ya raslimali asili na mazingira ni muhimu katika changamoto hii.

### 13.2 Hali ya Raslimali Asili Nchini Kenya

#### 13.2.1 Usawazisho wa Raslimali Asili

Maliasili asili huchangia jukumu muhimu katika maendeleo ya kisasa ya kijamii na kiuchumi. Katika kiwango cha jumla, mataifa ya Afrika hutegemea raslimali kama vile maji, madini, misitu na wanyama wa porini kama chanzo cha mapato yake. Katika kiwango cha chini, jamii hutegemea raslimali hizi kwa maisha yao. Masharti yanayowekwa kwenye maliasili hutokana hasa na ukosefu wake na kuendelea kuogezeka kwa mahitaji na matumizi mbalimbali ya maliasili. Kwa kiasi fulani, Kenya ina raslimali za kutosha. Raslimali hizi zinajumuisha kawi, maji, madini, maeneo ya uvuvi, wanyama wa porini na misitu. Takriban asilimia 19% ya kawi, inayotumiwa nyumbani na katika sekta ya viwanda nchini Kenya ni gesi ya mimea, yaani kutokana na kuni kutoka misitu, vichaka na mashamba ya miti.

Matumizi ya kuni kutoa kawi hupunguza sehemu ya misitu ya kitaifa, na pia huchangia katika kuongezeka kwa joto ulimwenguni. Katika maeneo ya taifa yanayokumbwa na ukame uondoaji wa kijani umetatiza uwezo wa 'eco-system' kuweza kutoa upya kuni. Hali hii ni mbaya zaidi katika maeneo yaliyo kame na yale yasiyo kame kabisa ya

kaskazini mwa Kenya – Kakuma, Turkana na Dadaab huko Garissa – ambako mamia na maelfu ya wakimbizi wamekuwa wakikaa kwa zaidi ya mwongo mmoja sasa.

Umeme mwingi wa Kenya hutokana na nguvu za mvuke, lakini madimbwi makubwa nayo pia yanagharama yake, kijamii na kimazingira. Nguvu inayotokana na miale ya jua ndiyo njia bora zaidi ya kutolea kawi nchini Kenya. Baadhi ya Katiba zinapa serikali wajibu wa kutoa na kuhimiza matumizi ya kawi inayoweza kutolewa upya baada ya kutumika.

Rasilmali za maji nchini Kenya zinajumuisha:

- Maziwa ya maji ya chumvi na ya maji yasiyokuwa na chumvi;
- Bahari ya Hindi;
- Mito isiyokauka na ile inayokauka;
- Maeneo maji maji;
- Machimbo ya maji;
- Mabwawa;
- Madimbwi.

Maeneo yanayopaswa kutajwa kwa njia iliyo maalum ni maeneo maji maji, maeneo yaliyoloa, mbuga, na sehemu chepechepe. Maeneo maji maji hutekeleza majukumu mbali mbali na yana manufaa muhimu ikiwa ni pamoja na kuongeza maji ya chini kwa chini, udhibiti wa mafuriko, udhibiti wa mmomonyoko wa udongo, ugavi wa maji na hifadhi za viumbe anuwai. Tishio kubwa zaidi kwa maeneo maji maji ni kufanywa kuwa ardhi isiyo maji maji na uchafuzi wake.

Matumizi ya raslimali ya maji nchini Kenya yanakadiriwa kuwa ifuatavyo:

- Kilimo asilimia 65;
- Matumizi ya nyumbani – asilimia 18;
- Matumizi ya viwandani – asilimia 13; na
- Matumizi mengine – asilimia 4.

Mizozo kuhusu matumizi ya maji inayotokana na ukosefu wa maji ya matumizi ya nyumbani, viwandani na katika kilimo ni mingi sana nchini Kenya. Maswala nyeti ya usawa katika utoaji na ugawaji wa maji, mizozo kuhusu haki za mito na usawazisho wa kiekolojia kwa hivyo huongezeka. Hasa hasa, kunalo swala la utoaji wa maji katika eneo la juu la mto kwa unyunyizaji mashambani, nguvu za mvuke n.k. na madhara yake kwa utaratibu wa mto, idadi ya maji yanayotiririka na kwa hivyo athari kwa watumizi wa maji ya mto walioko maeneo ya chini ya mto huo. Hii hasa ndivyo hali ilivyo kuhusiana na Mto Tana na Mto Uasin Nyiro. Huku mto Uasin Nyiro ukikauka kabisa kutokana na utekaji wa maji yake katika maeneo ya juu ya mto huo, idadi ya maji yanayotiririka katika mto Tana imepungua sana kutokana na kuwepo kwa miradi mingi ya nguvu za mvuke pamoja na matumizi mengine ya maji katika maeneo yake ya juu. Hii imeathiri maisha ya wafugaji wa kuhama hama ambao ndiyo wengi wa watu wanaotegemea maji katika maeneo ya chini ya mito hiyo miwili.

Aidha, kuna swala la ukanda wa maili tatu wa Mto Tana, ambao pamoja na Garissa uliwekwa chini ya mkoa wa Pwani na serikali ya wakoloni na kuzua mizozo kuhusu utekaji maji katika eneo hilo.

Ukuaji wa idadi ya watu ambao kwa sasa ni asilimia 2.9 kila mwaka, na utegemezi wa raslimali za maji uliokithiri utaifanya Kenya kuvuka kiwango cha chini ya mita 5 kwa kila mtu kwa mwaka kufikia mwaka 2025. Tayari Kenya imeorodheshwa miongoni mwa mataifa yaliyo na ukosefu wa maji usiokwisha na Taarifa ya Taasisi ya Ulimwengu kuhusu raslimali ya mwaka 2000. Ni jambo la wazi kuwa maji yanapaswa kutumiwa vyema, na Katiba inapaswa kutoa usawazisho uliosawa na endelevu kuhusu mahitaji ya raslimali ya maji yanayokinzana.

Kenya ina raslimali mbali mbali za madini ya chuma na yasiyo ya chuma ikiwa ni pamoja na: vito, “titanium”, fedha, risasi, ‘soda ash’, chumvi na changarawe. Madini haya yanapatikana, lakini kwa upande mwingine uchimbuaji wa madini, kila mara huambatana na madhara kwa mazingira. Humaanisha uharibifu wa kijani, maeneo ya maji, upotezaji wa viumbe anuwai, uchafuzi wa ardhi, utatizaji wa sehemu zilizo na sifa

muhimu za kitamaduni na kiumbuji. Utata huu unaonekana kwa kuwa huku Wizara ya Mazingira na Mali Asili ikipendekeza hatua kadhaa za kuondoa urasimi na vizuizi vya kisheria vinavyokumba uchimbuaji wa madini, makala ya kikao cha serikali mwaka 1999 yanaiwajibisha serikali kuimarisha ulinzi dhidi ya athari za uchimbuaji madini kwa mazingara. Changamoto iliyopo sasa ni kusawazisha malengo haya na kufafanua wazi majukumu hayo katika pande zote mbili na haki za Taifa na jamii ambamo madini yanapatikana kuhusiana na madini.

Mapato ya kutosha yanapatikana kutokana na uvuvi kwa matumizi ya humu nchini, kuuzwa katika mataifa ya kigeni au michezo ya burudani. Takriban watu milioni moja kote nchini wanategemea maeneo ya uvuvi kwa maisha yao – moja kwa moja, au kwa njia isiyo ya moja kwa moja kupitia huduma jalizi kama vile utayarishaji wa samaki, soko, utengenezaji au ukarabati wa mashua, n.k. Lazima kuwepo tahadhari ya kutosha kuhusu matumizi na usimamizi wa maeneo ya uvuvi, ili kuhakikisha uendelevu wake. Hali ya nyavu, na masharti ya uvuvi yanapaswa kuwekwa.

Wanyama pori wa Kenya wapatikana katika mbunga za wanyama za kitaifa, hifadhi za wanyama na maeneo mengine yanayolindwa – sehemu inayochukua kilomita 44, 564 mraba au asilimia 75 ya ardhi ya Kenya. Hata hivyo idadi ya wanyama pori wanapatikana nje ya maeneo haya pia ni kubwa. Asilimia tisini ya maeneo haya yanapatikana katika maeneo kame na yale yasiyo kame kabisa. Hifadhi za wanyama pori za kibinafsi katika jamii, pia zimeanza kuibuka hivi karibuni.

Mizozo baina ya binadamu na wanyama pori ni jambo la kawaida katika maeneo haya na ni ya aina mbili:

- Wanyama pori kuwaumiza binadamu na kuharibu mimea shambani na mifugo; na
- Binadamu kusababisha uharibifu kwa wanyama pori kupitia ujangili, na uharibifu wa makazi ya wanyama pori.

Mizozo hii isiposhughulikiwa vyema inaweza kusababisha uharibifu wa mali, kupoteza maisha, na hamu ya kuhifadhi wanyama pori.

Jumla ya eneo la misitu nchini Kenya ni asilimia 2.3 ya ardhi na inakadiriwa kuwa hekta 5,000 ya misitu hutoweka kila mwaka kutokana kutengwa ili kufanywa makazi ya binadamu. Raslimali ya misitu nchini Kenya ni muhimu kwa uchumi wa kitaifa na mashinani. Katika kiwango cha mashinani, misitu hutoa chakula, chakula cha mifugo, kuni, vifaa vya ujenzi, himizo la kiroho na kitamaduni na dawa za kitamaduni miongoni mwa mambo mengine. Katika kiwango cha kitaifa misitu ni chanzo muhimu cha bidhaa za misitu za viwandani. Majukumu ya kimazingira na kiekolojia na thamani yake katika ajira pia ni muhimu. Sera ya misitu inashikilia kuwa misitu inaoorodheshwa kuwa miongoni mwa vitu muhimu kwa taifa hili.

Kitamaduni, misitu ilimilikiwa na jamii, na takriban watu 15,000 wanaishi katika misitu ya jadi, ikiwa ni pamoja na Somek kwenye milima Elgon, Ogiek katika msitu Mau, Mijikenda katika misitu ya Kaya na Boni katika msitu wa Boni, katika wilaya za Lamu na Ijara. Inakadiriwa pia kuwa watu milioni 2.9 wanaoishi kando ya misitu wanategemea raslimali za misitu moja kwa moja kwa maisha yao. Sera ya sasa kuhusu misitu inatambua jukumu la jamii katika uhifadhi na usimamizi wa misitu na raslimali za misitu. Hata hivyo usimamizi huo chini ya Sheria ya Misitu bado unaonyesha matumizi ya kanuni na udhibiti uliowekwa wakati wa ukoloni.

### 13.2.2 Maliasili Katika Katiba

Katiba ya Kenya iliyopo sasa inasema machache mno kuhusu maliasili. Chini ya Katiba ya 1963, madini yote, maeneo ya maji, misitu ya kitaifa (iliyochapishwa katika gazeti rasmi la serikali) vilikuwa mali ya Taifa, au katika hali fulani, mali ya maeneo. Baada ya kuondolewa kwa mfumo wa maeneo (majimbo) raslimali hizi zote ziliwekwa chini ya umiliki na udhibiti wa Rais kama msimamizi wa mali ya Taifa. Hivyo ndivyo hali ilivyo leo.

### 13.2.3 Maliasili katika Katiba Nyingine

Masharti ya kusimamia na kudhibiti maliasili k.m maji, misitu, wanyamapori, viumbe anuwai na rasilimali za majini, na vinginevyo sasa hupatikana sana katika katiba nyingi. Haya hupatikana katika miswada ya haki, kanuni za amri za sera ya serikali au sura maalum. Kwa mfano, Katiba ya Uganda inaeleza katika sehemu kuhusu Malengo ya kitaifa na kanuni za Amri za Sera za Serikali kuwa:

> *Serikali italinda maliasili muhimu pamoja na ardhi, maji, vinamasi, madini, mafuta, wanyama wote na maua yote kwa niaba ya* wananchi wa Uganda.

Katiba ya Ghana inaeleza katiba Ibara ya 268 (1) kwamba:

> *Shughuli zozote, mkataba au harakati ianyohusu udhamini wa haki au makubaliano na ua kwa niaba ya wengine au kundi la watu vyovyo vinavyoelezwa, kwa utumiaji wa madini, maji au maliasili yoyote ya Ghana, iliyotengenezwa au kuingizwa kabla au baada ya matumizi ya Katiba hii, sharti kuidhinishwa na Bunge.*

Mtazamo wa jumla sawa na huu kwenye Katiba hizi ni:

- kubuni sheria ya kulinda na kusimamia maliasili kikamilifu; au
- vinginevyo ni kusawazisha uchukuaji na utumiaji wa maliasili hizi.

### 13.2.4 Waliyosema Wananchi

Maoni ya umma kuhusu swala la umiliki, udhibiti na usimamizi wa raslimali asili yalikuwa wazi kabisa. Maoni hayo yanaweza kuelezwa kimukhtasari ifuatavyo;

*(i)* *Kuhusu maji:-*

(a) serikali inapaswa kuchukua jukumu la kuwapa wananchi wote maji safi ya bomba;

(b) kila Mkenya anapaswa kufikia maji safi ya bomba;

(c) Serikali inapaswa kulinda maeneo ya chemi chemi za maji;
(d) mabwawa yanapaswa kusafishwa na kutengenezwa upya;
(e) raslimali za kutosha zinapaswa kutolewa kwa ukarabati wa miradi ya maji iliyokauka na kufanikisha uhifadhi wa maji ya mvua;
(f) serikali inapaswa kuchimba machimbo ya maji na madimbwi katika maeneo kame na yasiyo kame kabisa hasa kaskazini mwa Kenya na katika Mkoa wa Kaskazini Mashariki;
(g) maji yanapaswa kutolewa katika angalau kila umbali wa nusu kipengo kilomita mbili;
(h) raslimali za maji zisizokuwa na athari kwa mazingara zinapaswa kuzingatiwa;
(i) wakazi wa maeneo wanapaswa kufaidika kutokana na raslimali zinazotoka katika maeneo ya makazi yao – kwa mfano watu wa Taita Taveta na chemi chemi za Mzima;
(j) mito inayopita katika maeneo inapaswa kutumiwa kutoa maji kwa wakazi wa maeneo hayo, na mikondo ya mto haipaswi kubadilishwa ili kuhudumia maeneo mengine – kwa mfano mto Uasin Nyiro katika Mkoa wa Kaskazini Mashariki.

*(ii)* *Kuhusu madini, kuwa:-*

(a) uchimbuaji wa madini unapaswa kuzinufaisha jamii zilizo karibu na mahali palipo madini hayo, yaani, asilimia 50 ya mapato yanayotokana na madini itumiwe kwa maendeleo ya maeneo hayo;
(b) sheria kuhusu uchimbuaji wa madini zinapaswa kuzingatia au kuambatana na mahitaji ya jamii ambamo madini hayo yanapatikana;
(c) serikali inapaswa kufanya utafiki zaidi kuhusu uchimbuaji wa madini kwa manufaa ya wananchi;
(d) haki ya kuchimbua madini inapaswa kupewa jamii ambamo madini yanapatikana;

(e) jamii zinazoishi katika maeneo ambako madini yanapatikana zinapaswa kufidiwa ipasavyo;

(f) sera ya uchimbuaji madini inapaswa kufanyiwa marekebisho kwa manufaa ya umma.

*(iii) Kuhusu maeneo ya uvuvi, kuwa:-*

(a) sekta ya uvuvi imekabiliwa na matatizo ya:
- Ukosefu wa usalama: raia wa kigeni huvua katika maji ya Kenya;
- Masharti: Wakenya hawako huru kufikia maeneo yote ya fuo za Kenya;
- Mbinu mbovu za uvuvi;

(b) Wakenya walionelea kuwa wavuvi wanapaswa kupewa usalama na sekta ya uvuvi kufufuliwa;

(c) masharti kuhusu uvuvi yanapaswa kuwekewa raia wa kigeni pekee;

(d) uvuvi wa viwango vidogo vidogo pia unapaswa kuhalalishwa. Ulinzi wa uvuvi unapaswa kutekelezwa;

(e) serikali inapaswa kutoa vifaa na ujuzi wa uvuvi kwa wavuvi, pamoja na nyavu za kuvulia.

*(iv) Kuhusu wanyama pori, kuwa:-*

(a) wanyama pori walindwe dhidi ya ujangili;

(b) mbuga za wanyama za kitaifa zijengewe ua;

(c) aina mpya za wanyama, na zile ambazo hazipatikani kwa urahisi ziongezwe kwenye mbuga za wanyama;

(d) Ukubwa wa mbuga za wanyama upunguzwe, ili ardhi hiyo igawiwe wananchi;

(e) Thuluthi moja (1/3) ya mapato yanayotokana na mbuga za wanyama itengewe maeneo yaliyo karibu na mbuga hizo;

(f) Uharibifu unaosababishwa na wanyama pori kwa jamii zilizo karibu na hifadhi unapaswa kufidiwa. Fidia kwa vifo vya binadamu iwe shilingi milioni tatu (Ksh.3,000,000), nayo fidia kwa uharibifu wa mali isipungue shilingi laki moja (Ksh.100,000). Sheria kuhusu mbuga za wanyama inapaswa kufanyiwa marekebisho ili ijumuishe hifadhi zote za wanyama.

*(v) Kuhusu misitu, kuwa:-*

(a) serikali inapaswa kuongoza upandaji wa miti kwa wingi ili kuzuia kuongezeka kwa jangwa;

(b) ardhi ya misitu haipaswi kugawiwa watu binafsi na haipaswi kutwaliwa kupitia njia isiyo halali;

(c) maswala ya ulinzi wa mazingara kama vile uzuiaji wa ukataji miti katika misitu asilia iliyosalia yanapaswa kujumuishwa katika Katiba;

(d) adhabu kali inapaswa kutolewa kwa watu binafsi na kampuni zinazohusika katika uharibifu wa mazingara kama vile ukataji wa miti katika misitu;

(e) miradi ya upanzi wa miche inapaswa kuanzishwa ili miti iweze kupandwa kote nchini;

(f) ardhi ya misitu haipaswi kuondolewa katika gazeti rasmi la serikali;

(g) Jamii zilizo karibu na misitu zinapaswa kuwa majukumu ya kutekeleza katika usimamizi na ulinzi wa misitu hiyo na zinapaswa kutakiwa kutoa ushauri kuhusu utengaji wa sehemu za misitu hiyo.

### 13.2.5 Uchanganuzi

Wananchi wanataka kumiliki na kuendesha rasilimali zao wenyewe. Walitaka uelekevu wa kisiasa, utakaohakikisha kwamba mapato na manufaa mengine yanayotokana na rasilimali hizo yanatumika kwa, na kutumiwa katika, miradi ya maendeleo kwenye

maeneo yao huko vijijini. Hasa walitilia mkazo kwamba nyingi kati ya rasilmali hizi hufaa sawa katika kuboresha na kumaliza umaskini. Walibishana, kwa mfano, kwamba kwa sababu maji ni mahitaji ya kimsingi, serikali inahitajika kuhakikishia kila Mkenya anapata fursa ya kupata maji safi. Michango mingi kutoka maeneo makame na makame wastani ilisisitiza kuambatana na kuwa wafugaji wa kuhamahama wameteseka pakubwa wakitafuta maji katika maeneo mengine. Walilalamika kwamba hakuna miradi yoyote ya maji ambayo imewahi kuanzishwa maeneo hayo. Pia walieleza baadhi ya vita vya kikabila katika maeneo yao husababishwa na kung'ang'ania maji katika vituo vya maji. Kuhusu madini, walilalamika kwamba jamii zinazoishi katika maeneo yenye madini hayo hazijapata manufaa yoyote kutokana na machimbo hayo na zimepoteza ardhi na mali yao na fidia kidogo, ama hata bila ya fidia yoyote. Wageni wameelekea kuwa na haki zaidi hata kuliko wakazi wenyewe katika masuala ya madini. Kuhusu wanyama pori, watu wengi walilalamika kwamba sheria zilizopo zinalinda wanyama pori binadamu, hasa wanoishi kwenye sehemu zilizotunzwa. Ukweli ni kwamba, sehemu hizo zimeelekea kuwa zenye thamani mbele ya serikali kuliko jamii na, hivyo basi, unapata sehemu kubwa ya ardhi imetengwa kwa ajili ya wanyama pori wakati ambapo jamii mbali mbali zinaishi bila ardhi.

### 13.2.6 Mapendekezo

Kwa hivyo, Tume inapendekeza kwamba:

(i) maliasili ikiwa ni pamoja na madini, maji, ardhi, misitu, uvuvi na ardhi chepechepe ambazo ziko kwenye mamlaka ya kisheria ya Kenya itabaki kuwa ya watu wa Kenya isipokuwa ikiwa umiliki wake uko chini ya watu wengine, ama watu, katika Katiba hii; mtu kama huyo, au watu, atashikilia maliasili na kupewa mamlaka kirasmi ya kusimamia kwa niaba ya watu wa Kenya.

(ii) bunge litakuwa waamana wa watu wa Kenya, kulingana na maliasili na litasimamia maongozi yote kuambatana na makubaliano, kandarasi ama shughuli

za kutekeleza haki au maelewano, ili kuhakikisha ulinzi na matumizi endelevu kwa kizazi kilichoko na cha baadaye.

(iii) makubaliano yoyote, kandarasi ama shughuli zinazohusisha utekelezaji wa haki au tahafifu kwa ama kwa niaba ya mtu yeyote, ikiwa ni pamoja na serikali ya Kenya, kwa mtu yeyote, watu ambao hata hivyo wameelezewa kutumia vibaya, au matumizi bora ya madini, petroli na mafuta, maji, misitu ama bidhaa za misitu, uvuvi, maua yote na wanyama wote ama maliasili nyingine yoyote nchini Kenya, pamoja na mabadiliko mengine makubwa kuhusu matumizi ya ardhi; itaambatana na uthibitisho rasmi wa Bunge kwa kura za thuluthi mbili za waliowengi.

(iv) wakati ambapo Bunge linapoyakubali maidhinisho rasmi, makubaliano, kandarasi, ama shughuli zinazoendelea, litaamua kupitia uamuzi utakaoshawishiwa kwa kura zisizopungua theluthi mbili ya uanachama wote, kwamba kuna, kama inavyotumika, matayarisho ya mipango ya kuridhisha kama ifuatavyo -

(a) mipango ya usimamizi wa mazingira;
(b) mipango ya kurudisha mazingira katika hali yake ya awali;
(c) mipango ya makazi mapya;
(d) mipango ya usimamizi wa mapato, kuhakikisha kwamba mapato ya utumizi mbaya ya maliasili yatatumiwa kwa maendeleo ya kitaifa, ya kijamii na kiuchumi;
(e) Mipango ya maendeleo ya kiviwanda, kuhakikisha kwamba maliasili inaendeleza uzalishaji wa kiviwanda wa taifa na kwa kila namna, thamani inaongezeka kwenye bidhaa zinazotolewa nje ya nchi;
(f) Mipango ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi, kuiweka wazi kwamba makubaliano na matumizi ya maliasili, pamoja na usimamizi wa mapato, itatokea kuwa maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi na manufaaa kwa jamii ya vijijini;

(g) Majaribio ya mgongano wa maendeleo.

(v) taifa litaendelea kukinga maliasili ya Kenya na kuhakikisha usimamizi bora wa rasilmali zote, pamoja na kawi, maji, ardhi, hewa na ardhi chepechepe, hufanywa kwa njia ya kusimamisha maendeleo endelevu kwa kizazi kilichoko na kile kijacho; na kwa kuunda misingi na masharti bora kwa usalama wa kuhusika kwa watu kuyalinda mazingira.

(vi) itakuwa ni jukumu la taifa, kujihusisha na mashirika mbali mbali na kuwa na mafunzo ya uamuzi wa pamoja, ili:

(a) kukinga na kuzuia uharibifu wa mazingira na madhara yake na jinsi ulivyo momonyoka wake kwa ubaya;

(b) kuwa na mipango ya kieneo ili kuunda maeneo sawa kibayolojia;

(c) kuunda na kuendeleza hifadhi za kiasili na mbuga na maeneo ya starehe na kutenga na kulinda mibenuko ya ardhi inayopendeza na maeneo ili kuhakikisha kukingwa kwa asili na kuhifadhi vyombo vya kale vinavyopendwa kihistoria ama kisanii;

(d) kuendeleza matumizi ya maliasili kitaifa ili kulinda uwezo wake wa kuundwa tena na uimara wa elimu ya uhusiano wa viumbe na mazingira.

(vii) taifa lazima lichukue hatua ili kufanya majaribio ya kiekolojia na maliasili nyingine za nchi na itunze data yake itakayobadilishwa kila ya baada ya miaka kumi;

(viii) katika mikakati ya usimamizi wa maendeleo, mkabala wa tahadhari, pamoja na kanuni za tahadhari, majaribio ya mgongano wa mazingiria, ukaguzi wa mazingira, na uchunguzi wa mazingira, zitatumika ili pakiwa na vitisho visivyochujuka, kutokuwa na ujuvi wa kisayansi haukutumika kama sababu ya kuahirisha hatua ya kubana matumizi ili kuzuia kushukishwa hadhi kwa mazingira;

(ix) taifa litalinda kuunda na kuendesha hifadhi asili, mbuga za wanyama, na pia maeneo ya starehe na litahakikisha kuhifadhiwa kwa flora na fauna na kulinda uhanuai kwa kizazi kilichoko na kile kijacho;

(x) uamuzi kuhusu kulinda na matumizi ya maliasili lazima uzingatie masalahi ya watu hasa jamii ambazo zimeathiriwa na desturi na kizazi kilichopita katika eneo husika, au kwa makazi;

(xi) watu na jamii ambazo zinateseka kutokana na taratibu za hifadhi na kulinda maliasili zitalipwa fidia na taifa;

(xii) Hata hivyo ikiwezekana, utawala wa maliasili lazima uhusishe jamii ya eneo lile, bila ya kupoteza uhitaji wa maliasili kulindwa na kuendelezwa kwa manufaa ya taifa kwa jumla. Kanuni hizi zinafaa kutumika katika miradi yote ikiwa ni pamoja wa mbuga za wanyama za kitaifa, matumizi ya madini, maendeleo ya kitalii, mabwawa ya maji, na miradi ya unyunyiziaji maji;

(xiii) Pasiwe na vikwazo vya kiholela kwenye kipindi ambacho ardhi amana itatengwa kwa shughuli za uchimbaji madini, kama ilivyo katika Kifungu cha 115 (3), cha Katiba (miaka miwili);

(xiv) Husisha kwenye katiba masharti kwa kiasi kwamba sheria inayosimamia uchimbaji wa madini irekebishwe na kuwekwa sawa, wakati huo huo kuunganisha masharti yanayoakisi mazingira, kulinda rasilimali na haki ya kijamii/masharti ya makubaliano ya wote ya katiba.

(xv) Yeyote anayetumia vibaya rasilimali za madini atahitajika kusaidia kiyarudisha mazingira yaliyoharibika kwa kutumia teknolojia itakayotakikana na wakala wa umma anayehusika, kuambatana wa sheria.

## 13.3 Mazingira ya Taifa la Kenya

### 13.3.1 Kanuni za Jumla

Neno hili "mazingira" linatumika hapa kumaanisha maliasili yote na muktadha wa pale inapopatikana na kuingiliana, hali kadhalika ujumla wa muundo msingi uliojengwa kusaidia shughuli za watu za kijamii na kiuchumi. Mgongano wa kiteknolojia, matumizi ya binadamu na kuongezeka kwa idadi ya watu imechangia msukumo huu, na kukosa usawa wa mazingira, ambayo yanahitaji usimamizi bora, changamoto ya kimsingi ni kuweza kumudu mazingira endelevu.

Maelezo muhimu yanayotambulika kuhusu maana ya neno hili uendelevu ni: "*maendeleo ambayo yanatosheleza mahitaji ya kizazi cha sasa bila ya kulingania uwezo wa maisha ya baadaye kuyafikia mahitaji yao*". Na dhana hiyo hiyo inatumika kati ya kizazi kilichoko. Katika hali halisi, dhana hii imeoanishwa na kanuni nyingi za utawala na miundo, na kufanywa kuwa sheria katika mamlaka nyingi za kisheria barani Afrika.

Usimamizi endelevu wa mazingira unahitaji uaminifu kwa baadhi ya kanuni na maadili. Hii ikiwa ni pamoja na kukomaa haraka kiakili, usawa katika vizazi vinavyopita, na uwajibikaji wa kuyalinda madhara ya kimazingira. Hivi majuzi, kuhusika kwa umma katika maamuzi yanayoathiri mazingira ikiwa ni pamoja na haki ya kupata habari ilikuwa ni kanuni muhimu kwenye utawala wa mazingira.

### 13.3.2 Mazingira kwenye Katiba

Katiba ya sasa haizungumzii kabisa kuhusu mazingira. Baadhi yao wamepinga, kulingana na uamuzi wa mahakama kwenye mataifa mengine, na kwamba haki ya maisha inahusisha haki ya mazingira ambayo si hatari kwa afya. Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na Uratibu (Sheria Na. 8 ya 1999) hata hivyo, inaeleza

kwamba; “Kila mtu nchini Kenya ana haki ya kupata mazingira safi na yenye kuleta afya”, na zaidi ya hivyo, Kenya ni miongoni mwa mataifa ambayo yametia saini mikataba ya mazingira na mwafaka, ambayo ni pamoja na:

- Mapatano ya Kimataifa ya Kuzuia Uharibifu wa Mazingira ya Bahari kwa mafuta.
- Mapatano ya Maji Makuu (London), 1954.
- Mapatano ya Afrika ya Kuhifadhi Asilia na Maliasili (Algiers) 1968.
- Mapatano ya Ardhi chepechepe yenye Umuhimu wa Kimataifa, hasa kama makazi ya maeneo ya maji Habitat (Ramsar), 1971.
- Mapatano Yanayohusu Ulinzi wa Tamaduni za Dunia na Turathi za Kiasili (Paris), 1972.
- Mapatano kuhusu Biashara ya Kimataifa ya viumbe vilivyo hatarini (CITES) ya Wanyama Mwitu na Maua (Washington), 1973.
- Mapatano ya Umoja wa Mataifa kuhusu Sheria ya Bahari, (1982).
- Mapatano ya Vienaa kuhusu kulinda Tabaka la hewa ya Ozoni (Vienna), 1985.
- Mapatano ya Umoja wa Mataifa kuhusu Unuai wa Kibayolojia (Nairobi), 1992.
- Mapatano ya Mfumo wa Umoja wa Mataifa Kuhusu Mabadiliko ya Hali ya Anga (Rio De Janeiro), 1992.
- Mapatano ya Umoja wa Mataifa Kumaliza Majangwa (Paris) 1994.
- Mkutano wa Azimio la umoja wa Mataifa kuhusu Mazingira ya Binadamu (1972); na
- Azimio la Rio kuhusu mazingira na maendeleo (1992).

Mlima Kenya ni eneo la turathi ya dunia lililo chini ya mapatano kuhusu asilia ya dunia na turathi za kimaumbile, na Kenya lazima “ihakikishe kutambulika, ulinzi, uhifadhi, uwasilishi, na kusambaza kwa kizazi cha baadaye kuhusu tamaduni na turathi za kiasili.” Ziwa Nakuru na ziwa Naivasha ni ardhi chepechepes

zilizolindwa chini ya mapatanao ya Ramsar. Mataifa mengi pamoja na Brazil, Afrika Kusini, Uganda, Namibia, Malawi, Thailand na India, wameiweka juu hali ya mada iliyotolewa katika kifungu cha sheria kwa kiwango cha wajibu wa kikatiba.

### 13.3.3 Mazingira katika Katiba Nyingine

Katiba nyingi za siku hizi sasa zina masharti imara kuhusu mazingira. Licha ya masharti kama hayo kuwekwa kwenye taarifa za kanuni za Amri za Sera za Serikali au Mswada wa Haki, pia hutokeza kwenye ibara zinazohusika na ardhi na maliasili. Katika Katiba ya hivi karibuni zaidi, mara nyingi mazingira hushughulikwa kama swala la pekee.

Mtazamo wa jumla katika Katiba kama hiyo ni:

- kubuni haki kwenye mazingara safi na inayofaa;
- kuamuru utekelezaji kwa serikali, watu binafsi pamoja na wanasheria kutunza na kuhifadhi mazingara;
- kutoa sheria kwa kila mtu kuhifadhi na kulinda amali za kimazingara kwa njia ya kutozwa faini mahakamani;
- kubuni mwundombinu kwa usimamizi wa mazingira;
- kutaka kwamba vyombo vibuniwe kwa ajili ya elimu ya jumla kuhusu mazingira; na
- kutaka kwamba ukaguzi imara wa kimazingira ufanywe na matokeo yapatikane kwenye uamuzi mapema kabla ya rasilimali zozote za kimazingira kuharibiwa au kutumiwa ovyo.

Katiba zinazohimiza mambo haya na kanuni nyingine ni pamoja na za Brazil, Afrika Kusini, Uganda, Malawi, Ureno, Ethiopia na Ghana.

### 13.3.4 Walivyosema Watu

Watu wengi waliambia Tume kwamba: -

(i) Ulinzi wa mazingira unafaa uhusishwe kwenye Katiba;

(ii) Maliasili ambayo imepatikana kutoka eneo fulani inafaa kuinufaisha jamii ya eneo hilo; jamii hiyo kama mshikadau itapata asilimia 60% ya manufaa kutokana na maliasili hiyo;

(iii) Jamii zinazoishi sehemu ambazo maliasili zinavumbuliwa zinafaa mno kupewa fidia na makazi;

(iv) Rasilmali kiasi fulani za kimazingira na zenye thamani isiyopotezeka k.m misitu ya kawaida na spishi zilizo hatarini lazima zilindwe;

(v) Katiba inahitajika kulinda mazingira dhidi ya ukataji wa misitu, uharibifu wa mazingira, ujangili na mmomonyoko wa udongo;

(vi) Jamii na serikali zinahitajika kuwa washirikadau katika kulinda mazingira.

(vii) Sheria kuhusu ulinzi wa mazingira inafaa kutekelezwa na serikali;

(viii) Maliasili inayofaa kulindwa ni pamoja na madini, misitu, wanyama pori, maeneo yenye mikondo ya maji na ardhi;

(ix) Serikali inafaa kumiliki maliasili zote lakini usimamizi wake, ukusanyaji wa mapato yake, uhifadhi na ulinzi wake unahitajika kuendeshwa na wanajamii wenyewe;

(x) Unyakuaji wa ardhi za misitu unaofanywa na wanasiasa wenye mamlaka inafaa wanyang'anywe.

### 13.3.5 Uchambuzi

Ni wazi kwamba, ijapokuwa kiwango cha kuufahamisha umma kuhusu masuala ya kimazingira kilikuwa juu, hali hii haikufanana kutoka eneo moja kwa jingine. Hii inatarajiwa kwani maslahi ya kimazingira hayawezi kufanana kila mahali katika Taifa au kati ya maeneo ya mji na vijijini. Licha ya hayo, haja ya kuhifadhi na kulinda ubora wa rasilmali za kimazingira ilikuwa wazi miongoni mwa matabaka yote ya watu walioelezea Tume.

### 13.3.6 Mapendekezo

Hivyo basi, Tume inapendekeza kwamba:

(i) Katiba mpya ya Jamhuri ya Kenya lazima ihusishe haki za kimazingira na majukumu, na hali kadhalika uhifadhi na matumizi endelevu ya maliasili ya Kenya ili kuhakikisha maendeleo endelevu na usawa wa vipindi vya kivizazi;

(ii) Katiba inahitaji kanuni zifuatazo kwamba zitalinda maamuzi yote yatayofanywa katika miliki za utawala na mahakama kwenye masuala yanoyohusiana na mazingira na maliasili ili kuhakikisha maendeleo:

a) kanuni za kushiriki kwa umma katika maendeleo ya sera, mipango na utaratibu wa usimamizi wa mazingira;
b) kanuni ya usawa wa vipindi vya kivizazi, kuhakikisha kwamba kizazi cha sasa kinatumia na kufurahia mazingira na maliasili bila ya kuhatarisha maslahi ya kizazi cha baadaye;
c) kanuni ya wanaoharibu mazingira – walipe, ambayo inahitaji wale wanaohusika katika kushusha hadhi mazingira na maliasili wana wajibu kwenye gharama ya kurekebisha, pamoja na kuridhisha/fidia;
d) thamani ya kijamii na kiasili, kutoka kitambo imetumiwa na jamii yoyote nchini Kenya kwa usimamizi wa mazingira au maliasili ili yachukuliwe kwa njia sawa na isiwe na maudhi kwa haki na uadilifu ama sheria yoyote iliyotungwa;
e) kanuni za ushirika wa kimataifa kwenye usimamizi wa mazingira na maliasili wakati ambapo rasilmali kama hizo hugawanywa na mataifa mengine au pale ambapo mamlaka inapima Taifa moja kwamba linaweza kuwa liko kinyume au kivingine katika Taifa jingine;
f) kanuni ya hatua ya tahadhari inayohitaji ombi la mkabala wa kuchukua tahadhari, inahusisha majaribio ya athari za kimazingira na kwamba mahala penye tishio kuu la uharibifu mbaya, upungufu wa kutokuwa

na uhakika kamili wa kisayansi hautatumiwa kama sababu ya kuahirisha masuala ya kubana matumizi ili kuzuia upya au kuendelea kwa kupunguza ubora wa mazingira;

g) kanuni zinazohusu hali zinazohitajika sana za kuzuia mazingira inafaa kuunganishwa na mipango ya maendeleo na usimamizi;

h) kanuni ambazo kwa kila kitu kinachohusu mipango ya mzingira, lazima pawe na mfumo wa sera ya kiasasi, ima iwepo au mpya, katika utekelezaji wake.

(iii) Katiba inafaa kuwa na masharti yanayompa kila Mkenya haki ya kulinda mazingira, kwa manufaa ya kizazi cha sasa na cha baadaye, kupitia sheria kamilifu na masuala mengine.

(iv) Taifa litatangaza ubora ulioendelea na wa haraka wenye dhamani ya maisha ya wakenya.

(v) Serikali iwe na wajibu:

- Kulinda wanyamapori, rasilmali za kigeni na unuai wa kibayolojia nchini Kenya;
- Kulinda misitu na kushawishi na wapande miti zaidi;
- Mazoezi, shawishina panapohitaji uwezekano wa kupunguza takatka na urejelezaji;
- Mazoezi, shawishi na panapohitaji uwezekano wa kuhifadhi takataka, na hasa kulinda maeneo ya mikondo ya maji, mito na kulinda maeneo yenye maji ya ardhini;
- Mazoezi, shawishi na panapohitaji uwezekano wa matumizi na maendeleo ya teknolojia ya kawi na matumizi ya taratibu za kurejeleza kawi;
- Kuunda sheria ili kulinda mazingira na kuipa kipaumbele katika kukinga athari za mazingira na kushusha hadhi, lakini pia kutoa uhifadhi ikiwa zipo au athari haziepukiki, na kadhalika kwa fidia kwa wale waliathirika;

- Kuunda na kuhakikisha utekelezaji bora wa mfumo wa uchunguzi wa athari za kimazingira ambao:
    - Unahusisha miradi yote hasa (pekee au na miradi mingine) kuwa na athari iliyowazi kwenye mazingira ama maliasili, pamoja na miradi ya serikali;
    - Iko wazi na inatoa nafasi nzuri kwa maoni ya umma;
    - Inachunguzwa na shirika la kibinafsi la mnadi na maoni ambayo lazima yatiliwe maanani wakati wa uamuzi.

(i) Kuunda mifumo ya ukaguzi wa mazingira na uchunguzi;

(j) Kuhakikisha kwamba viwango vya kimazingira vilivyowekewa Kenya vinapelekana sambamba na viwango vya maendeleo vya kimataifa; na

(k) Kuendeleza elimu ya mzingira katika ngazi zote za kimafunzo na kuzidisha kuufahamisha umma haja ya kuhifadhi mazingira.

(vi) tabia na shughuli zilizokisiwa kuwa zinayadhuru mazingira, kulingana na waharibifu hao, ama wawe ni watu au vitu vya kisheria, hadi kwa wahalifu na adhabu za kitawala, licha ya wajibu wa kukarabati madhara yaliyotokea;

(vii) licha ya masharti ya sheria yoyote yaliyowekwa kuwaruhusu watu kutaka fidia katika mahakama ya sheria kwa kuvunja utaratibu wa mazingira, mkenya yeyote anaweza kutuma ombi kwa mahakama kuu kumtaka waziri na watetezi wa mradi kukubaliana na masharti yaliyowasilishwa Bungeni ikiwa pana dalili ya mgawanyiko;

(viii) Taifa lazima lihakikishe kwamba ulinzi wa mazingira unatolewa wazi wazi kama jukumu la waziri, na mashirika ya utekelezaji lazima yapewe maarifa ya kutosha ili kuyawezesha kuidhinisha kipengele hiki cha Katiba.

(ix) Mawaziri wanaowajibika na mazingira na maliasili watatoa taarifa Bungeni baada ya kila miaka miwili, au wakati unaofaa kabla ya muda huo uliowekwa, wakitoa maelezo ya kutosha kuhusu maendeleo yaliyopatikana kwenye utekelezaji shughuli za mazingira na mipango na labda, kwa azimio, muundo au kutofautiana kwa utaratibu wa utekelezaji;

(x) baada ya Bunge kupokea taarifa linaridhia kwamba kuna ukiukaji wa mipango iliyowekwa mbeleni, inaweza kuwa, kwa azimio, linaloungwa mkono na walio wachache, kukomesha shughuli mpaka pawe na hakikisho la taarifa hiyo inayokusanywa pamoja na masharti;

(xi) taifa litaomba ushirika na mataifa mengine na, panapofaa, mashirika yenye ujuzi kwa minajili ya kuendeleza mikataba ili kulinda mazingira na kutangaza maendeleo endelevu katika maeneo au ngazi za kilimwengu kwa kizazi cha sasa na kile cha baadaye, na kuunda nafasi bora ya utekelezaji wa mifumo ya mikataba hiyo. Ikiwa mitazamo ya wajibu wa Taifa wa kimataifa italeta madhara na uovu wa kimazingira, kisha usalama wa mazingira na uhifadhi wake utatawala;

(xii) Afisi ya Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Kitaifa ya usimamizi wa mazingira itaundwa na kupewa masharti ya usalama.

(xiii) Mkurugenzi Mkuu atateuliwa kati ya wanataaluma watatu katika mawanda ya mazingira baada ya utafiti wa serikali wa mtaalamu kutoka kwa wataalam wakuu nchini na atatumia uwezo wake kulingana na Sheria ya Utaratibu wa Usimamizi wa Mazingira.

# SURA YA KUMI NA NNE

# HAKI ZA ARDHI NA MALI

## 14.1 Agizo la Tume

Agizo la Tume chini ya sheria hii ni:

"*Kuchunguza eneo la haki za ardhi na mali, pamoja na binafsi, serikali na mfumo wa kikatiba wa ardhi ya kwanza na sheria ya Kenya, na maendeleo yaliyopendekezwa ambayo yatawapa furaha bashasha kwa ardhi hiyo na haki nyingine za kumiliki ardhi.*"

Agizo hili lazima lisomwe pamoja na vipengee vingine ambavyo sheria hii inaitaka Tume kuchunguza hasa katika uchumi, mazingira na maliasili.

## 14.2 Suala la Ardhi Nchini Kenya

### 14.2.1 Kanuni za Jumla

#### *(a) Suala la ardhi katika Uchumi na Jamii*

Umiliki wake, kufikia na matumizi – limechukua nafasi kuu kwenye sera ya umma na mazungumzo marefu kuhusu siasa nchini Kenya. Hii ni kwa sababu ardhi imekuwa kama kiini cha tatizo la kitamaduni, uchumi na mabadiliko ya kijamiii na kisiasa.

Ukweli ni kwamba, siasa ya Kenya, uchumi, historia ya kijamii na kiasili tokea kuingia kwa Waarabu huko pwani; na walowezi wa Kiingereza baadaye katika karne ya 19, walitawala na kushawishika katika mbinu zinazohusika na kufikia na

kudhibiti ardhi. Upiganiaji wa uhuru chanzo chake kilikuwa ni kupigania ardhi. Zaidi ya hayo, usimamizi wa uchumi wa Kenya huko nyumbani, katika jamii na ngazi za kitaifa umehusishwa na ardhi.

Kufuatia miaka ya ulazimishaji wa mifumo ya kimagharibi na usimamizi za kisasa wa ardhi, sehemu kubwa ya idadi ya watu inaendelea kwa shida si tu katika kuiga mifumo mipya ya uchumi bali pia kuiga mazingira dhaifu na ya pembeni pembeni, kushuka hadhi kwa ardhi, mapato kidogo ya kilimo, na kuzidisha vurumai kuhusu kufikia kudhibiti ardhi na umaskini. Hali hii imetibua mahitaji mengi ya awamu ya ardhi na masuala ya matumizi ya ardhi kati ya wasomi, waunda-sera, wanasiasa, jamii ya kimataifa, serikali na mashirika ya kimataifa kwa mwongo mmoja uliopita. Wamewekeza vya kutosha katika mipango ya kurekebisha ardhi. Hapa Kenya, Tume ya Njonjo ya kurekebisha sheria za ardhi ni mfano bora. Kuingia ukoloni kulichangia pakubwa katika mabadiliko kuhusiana na ardhi nchini Kenya na, hasa, kwenye mfumo wa umiliki, udhibiti na matumizi ya ardhi na jamii za kiasili. Kwa kitu kama azimio, jamii za Wakenya walinyimwa haki ya kumiliki ardhi zao, na pia maeneo yenye rutuba ya Kenya. Na zikapewa walowezi Wazungu wenyeji walipewa makazi huku vitongojoni ambapo walisimamiwa kama wakadamu ama manokoa wakilimia Wazungu.

Katika pwani ya Kenya inayohusisha kisehemu cha maili kumi kwa utao wa ndani kutoka Vanga kupitia kusini hadi kaskazini mwa Kismayu, hali ilikuwa tofauti sana. Hapa, Sultani wa Zanzibar alipata uhuru wa kutumia ardhi nje ya kisiwa, na mwaka wa 1895, eneo la ukanda wa pwani likawa sababu ya kukodiwa ardhi kutoka kwa Sultani hadi kwa serikali ya uingereza. Baadhi ya hatimiliki zilizotolewa kabla ya 1895 zilionekana. Wakati wa uhuru, baadhi ya wenyeji waliudhika walipogundua kwamba haikumaanisha watarudishiwa ardhi. Uhuru ulipoingia, tatizo la wamiliki wa ardhi wasiokuwepo lilibaki na wenyeji wengi wa pwani wameendelea kuwa maskwota katika ardhi zao.

***(b) Uchumi wa Ardhi***

Uchumi wa Kenya ni wa na utabakia kwa muda mrefu kutegemea kilimo na matumizi ya ardhi kwa ufugaji. Makadirio ya sasa yanaonyesha kwamba kilimo na ufugaji husaidia maisha ya idadi ya Wakenya kwa zaidi ya asilimia 75%, na kusaidia asilimia 70% ya kazi za mishahara, na kuchangia zaidi ya asilimia 80% ya mapato ya bidhaa zinazopetekwa ng'ambo. Mimea inayotawala uchumi wa kilimo ni pamoja na kahawa, majani chai, korosho, miwa, mchele, matunda ya tindi, mawele, mtama, pamba, kilimo cha matunda, na makonge. Hizi hukuzwa kwa sababu ya pesa na matumizi ya kujipatia riziki kwa wakulima wakubwa na wale wadogo katika maeneo ya chini hadi ya juu, kirutuba. Kilimo cha ufugaji cha ng'ombe wa maziwa na nyama kinaendelea vyema, hasa katika maeneo makame na makame wastani ambapo zaidi ya asilimia 50% ya ufugaji wa Kenya inapatikana. Matumizi makubwa ya ardhi nje ya kilimo na ufugaji yanahusisha mavuno ya bidhaa za misitu – kwa mbao na kuni – utalii, uchimbaji wa madini, uvuvi na muundomsingi. Kwa pamoja mambo haya yanafafanua mazingira ambamo uchumi wa ardhi ya Kenya unavyoendesha majukumu yake.

Kuambatana na utafiti wa uchumi wa mwaka 2000, uchumi wa Kenya ulikuwa umeshuka kwa miaka mitatu iliyopita. Sehemu zote za utafiti zilionyesha kwamba viwango vya ukuzaji vilishuka kati ya 1997 na 1999. Ukuaji katika sekta ya utengenezaji ulishuka kufuatia mashindano ya kuingiza nchini bidhaa ambazo bei yake ni rahisi mno, muundomsingi uliozorota na uhitaji wa kiwango cha chini mno. Kwenye kilimo, viwango vya ukuaji vilishuka kutoka asilimia 1.5% mpaka 1.2%, kati ya 1997 mpaka 1999. Uzalishaji wa mimea yote isipokuwa kilimo cha matunda na kahawa kiliteremka kwa kipindi hicho hicho. Hata wakati ambapo palikuwa na mavuno bora, mapato pia yalishuka.

Ukaguzi wa hali hiyo ya umaskini kote nchini ulionyesha kwamba matokeo ya umaskini kwenye ngazi ya kitaifa ni asilimia 52.2%, kumaanisha kwamba baadhi ya Wakenya hawawezi kumudu mahitaji yanayotakikana ya kimsingi, kama vile chakula na bidhaa ambazo si chakula. Ukaguzi huo unaonyesha kwamba

umaskini umefika asilimia 53.9% na 49% mijini na vijijini, mtawalia. Na huko katika maeneo ya vijijini hapa nchini Kenya, suala la umaskini vijijini, linabakia kuwa na uhusiano mkubwa na hali ya uchumi wa ardhi.

Baadhi ya sababu zinalifafanua suala hili la uzalishaji unaosikitisha. Mwanzo, mvua ndogo katika maeneo yanayokuzwa vyakula kufuatia mvua ya El-Nino iliyonyesha miaka michache iliyopita. Pili, ni bidhaa za kilimo na upungufu wa nguvukazi katika mbinu nyingine za ufanyikazi. Pingamizi lilikuwa, kati ya mambo mengine, jukumu la kuondoa magonjwa na vifo miongoni mwa vikosi vya watendakazi wa vijijini kuambatana na kusambaa kwa virusi vya ugonjwa ya ukimwi. Tatu, ni hasara kubwa ya kabla na baada ya mavuno, kufuatia teknolojia duni za uzalishaji na kuhifadhi. Mwisho, ni athari za matatizo ya kimfumo, ambao muhimu kwake ni kupungua kwa ubora wa ardhi na uharibifu unaoshirikishwa na rasilmali kupitia ukataji misitu, kuingilia ardhi zilizotengwa, msukumo wa kuongezeka kwa idadi ya watu, matumizi ya ardhi inayotumiwa na maskini, na kukosa kabisa ardhi bora, na rasilmali inayotumia sera.

### *(c) Siasa za Ardhi*

Mbali na vipimo vya kiuchumi, hata hivyo, ni muhimu kugundua kwamba kuna masuala ya ardhi nchini Kenya, yenye hisia za ndani na kafika siasa na kwa sababu za kisiasa, kijamii na kiasili.

Vipimo vya za kisiasa ambavyo vimeonyesha umbo na kanuni za masuala yanaoizunguka ardhi nchini Kenya ni vile vinavyoingiliana na historia ya nchi hii. Utofautishaji unafaa kufanywa kwa hali hii kati ya maili kumi kwenye ukanda wa pwani ya Kenya (wakati huu ukiwa ni kama pwani yote), na sehemu nyingine za nchi. Kwani hapo awali mpaka ilipofika mwaka wa 1964 iliendeshwa na kutawaliwa na mamlaka ya kikoloni kwa niaba ya na kama mali ya Sultani wa Zanzibar, siasa nyingi za kufikia na kudhbiti ardhi kwenye eneo hilo daima

imekuwa na itabaki kuwa suala kubwa zaidi lenye kuhusisha, kama lilivyo, kuingiliana kwa wenyeji, mabwanyenye wa Kiarabu na Serikali.

Ijapokuwa usimamizi na utawala wa sehemu nyingine za nchi, pamoja na maeneo ambayo hayakuwa chini ya makazi ya Wazungu, yalikuwa wazi zaidi, suala la ardhi bado linabaki kuwa kitendawili katika maongozi na uhusiano wa kisiasa. Ukweli ni kwamba wakati mlowezi anapozungukwa na uhusiano wa kisiasa miongoni mwa walowezi Wazungu na kati yao na Waafrika, daima waliafiki suala la ardhi; manufaa yake, umiliki wake, udhibiti wake, matumizi ya usambazaji wake.

Hiki kikiwa kiini cha mazungumzo ya siasa kote nchini, suala la ardhi lilikuwa, bila kushangaza la kushangaza, chanzo cha kupigania uhuru wa nchi hii. Baada ya uhuru mwaka wa 1963, suala la ardhi lilikita mara moja kama chombo cha kimsingi cha kujitafutia uwezo na kujitegea utajiri miongoni mwa wasomi ambao walikuwa wakisimamia vyombo vya mamlaka ya taifa. Suala la ardhi lilibaki la kutajika katika ajenda za kisiasa na kimaendeleo.

### 14.2.2 Ardhi kwenye Katiba

#### *(a) Msingi*

Chini ya katiba ya mwaka wa 1963, haki zozote za ardhi za serikali ya kikoloni zilipewa eneo ambalo lina ardhi hiyo. Hii ilimaanisha kwamba Ardhi ya Serikali, na riba itokanayo na ardhi ambayo imekodishwa, mkataba huo wa kukodi ulipo, ulipewa serikali. Wakati huo huo, ardhi yote huko “kwenye asili yao” ilifanywa kuwa ardhi amana na ilitolewa kwa mamlaka ya mabaraza ya wilaya. Mabaraza hayo yaliweka ardhi hiyo kwa manufaa ya wakazi wake, na walihitajika kutambua haki chini ya sheria ya kawaida, iliyohusu ardhi hiyo.

Mfumo wa kieneo ulipoondolewa, ardhi amana ilibakia na mabaraza ya wilaya.

### *(b) Katiba ya sasa*

Suala la ardhi limehusishwa katika Katiba iliyopo kwenye ngazi mbili. Kwanza, kama mali, haki kwenye ardhi zimelindwa na kifungu cha 75, kwa hivyo haiwezi kupokonywa bila fidia. Pili, sura ya 9 ya Katiba iliipa haki ardhi amana; umiliki wake, udhibiti na usimamizi katika mabaraza ya wilaya ambayo yatatenga na kuyatumia kwa manufaa ya jamii husika kuambatana na sheria za kawaida. Chini ya sheria ya Ardhi Amana (Sura ya 288) ardhi Amana inatunzwa na Kamishna wa Ardhi kwa niaba ya mabaraza ya wilaya.

Ardhi hiyo kwa mamlaka ya baraza la wilaya inaweza kuamuliwa na kusajiliwa kama mali ya mtu binafsi. Ikitokea hivyo ardhi hiyo humalizika kuwa ardhi amana na inaweza kuwekwa wazi kutokana na uwajibikaji wowote. Ardhi amana inaweza pia kutengwa aidha na baraza la wilaya ama na Rais kwa kushauriana na baraza husika la wilaya, kwa kutumiwa na kukaliwa na shirika la umma au mamlaka, au kwa shughuli za umma.

Licha ya Katiba, masharti yaliyowazi yanayohusu ardhi na usimamizi wa ardhi yanapatikana katika vyombo vingi vya sheria. Mfumo wa kisheria wa sasa kuhusu usimamizi wa ardhi nchini Kenya, unaweza kutajwa waziwazi kuhusisha vitengo vitatu vya ardhi, ikiwa ni Ardhi ya Serikali, Ardhi ya kibinafsi na Ardhi Amana. Hii ni kulingana na jumla ya sheria zinayoweza kugawanywa katika kundi la zile zinazounda na kubainisha haki za mali katika ardhi (Sheria ya Ardhi Iliyosajiliwa (Sura 300), Sheria ya Uhamisho wa Kihindi, 1882); zinazotoa ruhua ya mpito kutoka kwa awamu ya Ardhi ya Kawaida hadi kwa ubinafsishaji wa mfumo wa kiawamu kupitia utaratibu wa usajili (Sheria ya Maamuzi ya Ardhi, (Sura 284), Sheria ya Uimarishaji wa Ardhi (Sura 283); Sheria ya Usajili wa Hati (Sura 281); na zile za marekebisho ya shughuli za utoaji wa ardhi (sheria ya udhabiti wa Ardhi (Sura 302)). Marekebisho ya matumizi ya ardhi yanatawaliwa na baadhi ya vikwazo fulani pamoja na Sheria ya Kilimo (kifungu cha 318),

sheria ya Afya ya Umma (Sura ya 318), Sheria ya Machifu (Sura ya 128), Sheria ya Serikali za Wilaya (Sura ya 265), na Sheria ya Mipango ya Ujenzi (Sheria 6 ya 1996). Sheria ya mila inabakia kuwa sehemu ya mfumo wa sheria ya Kenya na inatumika mradi tu haikinzani na sheria yoyote iliyoandikwa.

Kati ya hizi ni Sheria ya Kilimo na Sheria ya Mipango ya Ujenzi, ambazo zinahitaji maelezo maalum. Ile ya kitambo, ambayo ni chombo cha kimsingi katika marekebisho ya matumizi ya ardhi ya vijijini inahitaji zaidi kutangaza, kuendeleza, na kuhifadhi kilimo, kulinda mchanga na rutuba yake, na kutengeneza maendeleo ya ardhi ya kilimo, kulingana na mafunzo yaliyokubalika ya usimamizi bora wa ardhi na ukulima wa mazao. Sheria hii humpa uwezo mwingi Waziri, pamoja na uwezo wa kufanya marekebisho yanayohusiana na uhifadhi, matumizi bora na maendeleo ya ardhi ya kilimo. Masharti yanayoundwa chini ya sheria hii yanawapa watu wenye mamlaka uwezo wa kupinga kukatwa kwa mazao na kuwanyima mifugo lishe, na kupanda miti, ili kuulinda udongo kutokana na mmomonyoko. Kukataa kufuata kanuni hizo ni hatia ya jinai. Zaidi ya hayo, Mkurugenzi wa Kilimo anapewa uwezo wa kutoa taratibu za kuhifadhi ardhi ambazo zitawataka wenye ardhi kufuata kanuni za uhifadhi ama kupinga shughuli mbaya zinazokinzana na usimamizi mzuri wa ardhi. Masharti haya yanaweza kutumiwa kuleta njia bora za kusimamia ardhi na matumizi yake, ambalo ni sharti zuri sana la maendeleo endelevu.

Hatua za mwisho za sheria hiyo ni chombo cha kudhibiti maendeleo nchini kote na hasa maeneo ya miji. Sheria hii inatumika sana katika ngazi za kieneo, kwa ardhi yoyote ya serikali, ardhi amana ama ardhi ya kibinafsi iliyo kwenye eneo la kimamlaka la baraza la wilaya, kwa lengo la kuimarisha ardhi hiyo na kutoa nafasi nzuri ya maendeleo ya ujenzi katika ardhi hiyo.

Sheria hiyo inatumika kwa kutoa masharti yanayofaa kwa muundomsingi, kama vile, usafiri, kwa manufaa ya umma, biashara viwanda, makazi na maeneo ya burudani, ikiwa ni pamoja na mabustani, maeneo yaliyowazi, na yaliyohifadhiwa

na pia kuweka masharti yanayofaa kwa matumizi ya ardhi ya kujengea. Sheria inatoa fursa ya mipango, kupangilia au kukarabati ardhi yote ama sehemu ya ardhi iliyo chini ya eneo la mpango wa maendeleo ya ujenzi na kudhibiti amri, asili na mwelekeo wa maendeleo kwenye eneo hilo. Katika maeneo ya miji pamoja na miji, sheria hii inatoa nafasi ya maendeleo ya ujenzi ya muda mrefu na muda mfupi, kuandikisha tena au kuendeleza tena kwa minajili ya kulinda na kuratibisha maendeleo ya muundomsingi na huduma, na kwa udhibiti maalum wa matumizi na maendeleo ya ardhi au kwa utoaji wa ardhi yoyote katika maeneo hayo kwa manufaa ya umma.

Kwa jumla, sheria inatoa fursa ya kuyatayarisha maeneo na mipango ya maendeleo ya ujenzi ya wilayani, udhibiti wa maendeleo pamoja na ruhusa za kuendeleza au idhini, mgawanyiko, na kuondoa ardhi, kuzidisha muda wa kukodi n.k ikitegemea masharti ya sheria ya Ardhi ya Serikali, Sheria ya Ardhi Amana na sheria nyingine zozote zilizoandikwa, zinazohusiana na utawala wa ardhi.

Ni muhimu kufahamu kwamba chini ya Sheria ya Mipango ya Ujenzi, mamlaka za kiwilaya zitaendelea kudhibiti na kupinga maendeleo na matumizi ya ardhi kwa maslahi ya maendeleo sawa na yaliyopangika katika maeneo ya mamlaka ya kisheria, lakini kwa utaratibu unaoambatana na masharti ya mipango ya maendeleo ya ujenzi yaliyoidhinishwa na mkurugenzi wa mipango ya ujenzi. Ili kuhakikisha migao hiyo ya ardhi katika maeneo hayo ya mamlaka za kiwilaya imefanyika kimpangilio, wanamipango wa ujenzi waliosajiliwa waendeshe ugawanyaji huo.

#### 14.2.3

#### 14.2.4 Walivyosema Watu

Palikuwa na maoni mengi kuhusu suala la ardhi na, hususan, hali halisi ya Ardhi Amana katika Katiba. Maoni hayo yanaweza kufupishwa kama ifuatavyo –

*(i)* *Kama kanuni ya jumla kwamba-*

(a) ardhi yote itakuwa chini ya watu na si serikali;
(b) Ardhi yote ya serikali "iliyonyakuliwa" inafaa kurudishwa;
(c) Ardhi amana inafaa kuwa haki ya moja kwa moja kwa jamii;
(d) Mgao wa ardhi unafaa kuwa sawa;
(e) Ardhi iliyopokonywa bila haki na serikali ya ukoloni au ya sasa itarejeshewa wenyewe ama isipowezekana, walipe fidia; na
(f) Malipo yatatolewa kwa sababu ya uharibifu uliotokea baada ya ghasia za ardhi ama vita hasa katika bonde la ufa, pwani, kaskazini mashariki na sehemu Fulani za mkoa wa mashariki.

*(ii)* *Kwa hali maalum kwamba-*

(a) Maeneo ya msitu yaliondolewa kwenye "gazeti rasmi la serikali," yaliyopewa watu binafsi, na kuharibu misitu, bila kuzingatia mazingira na kufikiria rasilmali ama hata jamii wenyeji wataharibu hali ya maisha ya watu, (kwa mfano, kusafisha sehemu Fulani za msitu wa Mau ambao utawanyang'anya watu wa Ongiek, na kuharibu jamii yenyewe);
(b) Athari za kunyang'anywa ardhi wakati wa ukoloni bado zinaonekana katika baadhi ya jamii;
(c) Jamii nyingine zimenyang'anywa nafasi za kufikia sehemu muhimu sana za kiasili;
(d) Kuna fursa nzuri ya ardhi isiyotumika wakati ambapo wengine wanalilia nafasi hiyo ya kupata ardhi;
(e) Wengine wanachukua ardhi kama ishara ya uwezo, badala ya kufanya kitu cha kuizalisha;
(f) Wengi wanataka bei ya juu ya ardhi inayoweza kuwa ya mtu binafsi ama, na wengine kwenye miji, wanaishi katika mitaa ya mabanda,

aghalabu kama maskwota wasio na haki, bila ya vifaa, na bila zawadi ya kuboresha maisha yao; na

(g) Wanawake wanafaa kuwa na haki bora zaidi za ardhi; katika hali ya udhibiti wa ardhi wanayolima, mirathi ya haki na haki za mali za ndoa.

### 14.2.5 Uchambuzi

Ushahidi wa kutosha kuhusu umuhimu wa marekebisho ya ardhi na suala la ardhi umetolewa kwa Tume katika vikao vyake kila mahali nchini. Hata hivyo, ni vigumu mno kupata watu ambao hawatatiziki kuhusu vurugu la ardhi. Shughuli zinazosababisha vurumai hilo la ardhi ni pamoja na:

- urithi wa ukoloni na baada ya ukoloni;
- kushusha hadhi sheria za kawaida kulingana na sheria za mtindo wa kizungu;
- matumizi ya mamlaka wakati wa kugawiwa ardhi ili kupandisha maslahi ya kisiasa na kikabila;
- ustadi wa shughuli na msingi wa ufisadi katika kugawanya ardhi ya serikali;
- kunyang'anywa maskini ardhi yao na kuwaondoa watu;
- miliki wa ardhi kuwachwa kwa watu wachache;
- kuzidi kwa ubinafsishaji na ubidhaa wa ardhi na kunyanyaswa kwa haki za watu kutumia na kuishi kwenye ardhi, kuzika wafu na kuwa na fursa ya kukusanya bidhaa za kiasili;
- kukua kwa umaskini na miujiza ya mwanadamu kuliundwa na wasiomiliki ardhi na masharti yasiyosalama katika vijiji na maeneo ya miji;
- kushukishwa hadhi kufuatia kuvunjika kwa usimamizi wa maliasili, hasa rasilmali za kawaida za mali;
- kuondoa kwenye gazeti rasmi la serikali na kugawa hifadhi ya misitu, iliyotumika kwa kipindi kirefu na kuishi wenyeji wake;

- ukosefu wa vyombo vya Taifa kuelezea malalamiko na kuondoa migogoro ya ardhi kwa hali nzuri na iliyopangiwa;
- jinsia na ubaguzi wa umri katika sheria za kawaida na za kitaifa kwenye utawala wa ardhi;
- upungufu wa sera za ardhi kitaifa.

Pamoja na kauli hizi, kuna pia idadi ya watu, ambayo kwa baadhi ya maeneo yamepelekea kugawanywa kwa mashamba mara nyingi kufuatia kwa ngazi zilizo za kiuchumi na kuporomoka kwa uchumi kwa jumla. Virusi vya ugonjwa hatari wa UKIMWI vinasababisha mabadiliko mengi ya kidemografia na hali ya kawaida ya kuwa na ardhi ya kuhamishana. Watu wengi wamenyang'anywa msaada wa familia, bila kutarajia. Wazazi wanarithi ardhi kutoka kwa watoto wao na sio kinyume chake. Wanawake wanaachwa na watoto wadogo ikiwa ndio njia yao ya pekee ya msaada wa ardhi wanayolimia na ambayo hawataimiliki.

### 14.2.6 Mapendekezo

Hivyo basi Tume inapendekeza kwamba kanuni zifuatazo kama zilivyofafanuliwa katika 14.3.5 ihusishwe chini ya Katiba mpya:

(i) Ardhi yote ni ya watu wa Kenya na kwa hivyo –

(a) watu wote watamiliki ardhi kulingana na mfumo wa kimasharti uliofafanuliwa na sheria, na
(b) watu ambao si Wakenya watazuiwa kupata ardhi isipokuwa kwa misingi ya kukodi.

(ii) Ardhi hapa Kenya itagawanywa katika vitengo vya umma, binafsi na jamii na kwamba –

(a) ardhi ya umma itabainishwa na kuwekwa kama amana ya Wakenya kwa misingi ya kisheria kuelezea asili na kipimo cha uaminifu huo.
(b) Ardhi ya kibinafsi ichukuliwe na ipewe watu au wanamamlaka kuambatana na utaratibu wa kiawamu wa sheria.
(c) Ardhi ya jamii ibainishwe wazi wazi na jamii ipewe haki au mawakala wake kulingana na mfumo wa kimamlaka uliofafanuliwa kisheria.

(iii) Haki za mali iliyopatikana kihalali zitalindwa na mali hiyo inaweza kugawanywa bila ya kubagua jinsia, ikitegemea vikwazo kama vilivyo kimsingi kwenye mfumo wa ardhi wa awamu ilioziunda.

(iv) Ardhi yote iliyogawanywa au kumilikiwa itaambatana na uwezo wa kimsingi wa Taifa kupata ama kuishughulikia ardhi hiyo kwa manufaa ama maslahi ya umma.

(v) Pataundwa Tume ya Ardhi ambayo majukumu yake yatakuwa –

(a) kutoa hatimiliki ya ardhi ya umma;
(b) kurekebisha sera na sheria za ardhi baada ya muda fulani;
(c) kuendesha kanuni kwa matumizi endelevu na usimamizi wa ardhi; na
(d) kujifunza utawala wa majukumu ya ardhi iliyobakia.

(vi) Bunge litaweka sheria kwa kipindi cha miaka miwili kwenye kikao chake cha kwanza chini ya Katiba hii –

(a) uhusiano wa kanuni zilizoko hapo juu;
(b) chombo cha kuondoa mizozo ya ardhi chini ya vitengo vya awamu mbali mbali;
(c) kuendeleza kanuni za matumizi endelevu na usimamizi wa ardhi; na
(d) mfumo wa kugawa ardhi kwa haraka na wenye manufaa, usio ghali kuhamisha na kutoa;

(e) mgao wa sawa wa ardhi ikiwa ni pamoja na kutatua tatizo la wale wasio na ardhi, ama makazi ya papo kwa hapo katika maeneo ya miji;
(f) uchunguzi na suluhu ya madai ya kihistoria hasa katika maeneo ya Mkoa wa pwani, Bonde la Ufa na Mkoa wa Kaskazini mashariki na maeneo mengine;
(g) kuanza kutoza ushuru ardhi zisizotumika ama zinazotumiwa vibaya; na
(h) uratibishaji na urahisishaji wa sheria za ardhi.

## 14.3. <u>Awamu na Utawala wa Ardhi</u>

### 14.3.1 Kanuni za Kijumla

*(a) Mfumo wa Umiliki wa Ardhi*

Umiliki wa ardhi unamaanisha taratibu na masharti ambayo yanatoa haki ya kupata ardhi, kubakia nayo, kuitumia, kuitoa kwa, ama kuibadilisha. Mtihani wa awamu ya ardhi ni kiungo cha kuundwa kwa sera ya ardhi. Kuna njia tatu za kuratibisha utawala mkongwe wa awamu za ardhi hapa Kenya.

Kwanza, ni kulingana na eneo lenye hati ya viwango maalum vya ardhi, kama vile, ikiwa "serikali" chini ya Sheria ya Ardhi ya Serikali (Sura 280) au Ardhi Amana. Kama njia ya kumiliki, kuainisha ardhi kama "serikali" kunamaanisha kwamba ardhi kama hiyo ni ya "kibinafsi" kwa serikali na pengine kwa mafunzo, imetumika na ikatolewa kama hivyo. Kwa kweli, hakuna mahitaji ya kisheria chini ya sheria hii, au kanuni nyingine yoyote ya sheria, kuitaka serikali kujibu madai ya umma, yanayohusu ulinzi au matumizi ya ardhi. Hivyo basi, hakuna vitengo vya ardhi ambavyo nivya umma, kwani imetengwa kwa, na imewekwa kutumiwa kwa manufaa ya raia wa Kenya zaidi. Hiyo ikiwa ni "mali" ilioyotengewa serikali iliyo mamlakani, haishangazi kuona kwamba ardhi ya

serikali kwa miongo minne iliyopita imekuwa ndio chanzo cha migawanyiko, kuchukua ardhi kimakosa na uharibifu usio na maana.

Uainishaji wa ardhi kama “amana” inamaanisha, hasa katika misingi ya Katiba na Sheria ya Ardhi Amana, kwamba ardhi kama hiyo iwekwe kwa manufaa ya watu ambao ni wakazi wa maeneo hayo. Utawala mkongwe wa kisheria, unaotawala shughuli za uhusiano wa vitengo vya Ardhi Amana zote ni sheria ya kawaida. Kutolewa kwa haki ya hati zenye siasa kali na udhibiti kwa minajili ya Ardhi Amana ya mabaraza ya wilaya, ya kizungukwa na utoaji wa majukumu ya kiutawala ya Kamishna wa Ardhi, hata hivyo kumaanisha, kwamba kanuni za shughuli za kawaida haziheshimiwi kabisa. Ukweli ni kwamba, dharau za kikatiba kuhusu Ardhi Amana ziko wazi. Pamoja na mengine ukosefu wa usalama kwa haki za ardhi za kiasili na jinsi inavyochukuliwa kama milki ya kimpito inayofaa kuondolewa mara moja kupitia haki za kumiliki, imepelekea jamii kunyang’anywa mali yao katika maeneo mengi ya nchi.

Njia ya pili ambayo utaratibu mkongwe wa ardhi unavyoweza kuratibishwa ni kulingana na misingi ya utawala wa kisheria katika uhusiano wa ardhi, yaani ikiwa utaratibu huo ni wa serikali ama mila. Na ya tatu ni katika misingi ya haki za aina ya haki yaani, milki huru, kukodi au ya wote. Kwa hali ya ile ya kwanza, taratibu hizi mbili zinatawalaiwa na mashirika ya kisheria yaliyo na taratibu zao za kipekee za ugawaji, kutenganisha na kuhakikisha. Kama matokeo yake, sheria ya ardhi ya Kenya inabaki kuwa moja ya zile zilizovunjikavunjika, ngumu na zisizo kuwa na misimamo nchini Kenya.

*(b) Matatizo yanayohusu Umiliki*

Pamoja na ukweli kwamba utawala wa kisheria unaosimamia umiliki wa ardhi ni mgumu na usioweza kutekelezeka, imeeleweka kwamba matatizo mengi yatahitaji kusuluhishwa kama Wakenya watakuwa na usawa katika kupata ardhi.

*(i)* *Hadhi ya Wanawake*

La kwanza kabisa ni kurekebisha hadhi ya wanawake. Wanawake wanachangia takriban nusu ya idadi ya Wakenya na wamechukua nafasi kubwa katika kilimo; asilimia 69% ya idadi ya wanawake wanafanya kilimo cha kijizumbulia riziki, ikilinganishwa na asilmia 43% ya wanaume. Na bado wanamiliki asilimia 10% ya ardhi iliyopo. Wanawake ni maskini zaidi, na familia zinazoongozwa na wanawake ni maskini zaidi ya zile zinazosimamiwa na wanaume. Ukosefu wa umiliki wa ardhi kwa wanawake unapunguza matunda ya uzalishaji, unafanya maendeleo yasinyae na kuchangia umaskini na kupunguza heshima ya mtu binafsi.

Mila za Kiafrika zinaunga mkono urithi kutoka kwa baba na udhibiti wa kiume katika kutoa maamuzi ambayo huwatenga wanawake katika umiliki wa ardhi. Wanawake wanachukuliwa kama wasiohusishwa na ukoo wao wa kuzaliwa au kuolewa, na hawapati ardhi kutoka kwa yeyote yule kati ya jamii hizo. Hata wakati ambapo wanawake wanapokuwa na haki ya ardhi ya familia, jamaa zao wa kiume hupata fursa ya kuwanyang'anya na kuitafutia hati ya kumiliki ili kuwanyima wanawake pato lao. Wakati mwingine kina mama wanaunga mkono mila hizi.

Aghalabu wajane hupokonywa na mashemeji zao na kubakia bila makao. Ijapokuwa wake wengi huwa na mamlaka kidogo kuhusu mapato, wakati wa kutoelewana kwenye ndoa, wanawake wengi hufukuzwa kwa kupewa kitu kidogo cha kujikimu maishani, kama kipo. Hata ikiwa wamewatunzia wazazi wao, kina kaka mara kwa mara huwatimua kina dada wazazi wao wanapokufa. Asilimia 10% ya wanawake wanaoishi kwenye mitaa ya mabanda walihama vijijini kwa sababu ndoa zao zilivunjika, asilimia 8% ni wajane kufuataia msukumo w auzazi wa kutoolewa.

Virusi vya UKIMWI vinaziathiri vibaya haki za wajane wanaoishi na mayatima kwa ardhi ya kiasili. Katika hali nyingine, wanawake hunyang'anywa ardhi yao na mali baada ya waume zao kuaga dunia. Wajane huzingiziwa kuwa wao ndio waliowaambukiza waume zao na kupewa msukumo kuzihama nyumba zao za ndoa. Wajane huwa waamana wa mali, kwa niaba ya watoto. Hawawezi kulipia rehani ardhi hiyo na hupoteza haki ya kubaki nayo anapoolewa tena. Wakati ambapo wanawake hao wanapoolewa bila watoto, ni mila kwao kurejeshwa kwenye familia zao punde marehemu anapozikwa. Watoto, bila ya kuzingatia umri wao, ndio huathirika zaidi. Mayatima kwa desturi huwachwa na jamaa zao wakubwa wa kiume. Haki ya watoto wa mwanamke ambaye hajaolewa wanaokufa kwa UKIMWI wana hatari kubwa kufuatia ile hali ya atakavyochukuliwa mama yao katika jamii na ile aibu ya ugonjwa huo.

Ijapokuwa Katiba inaharamisha ubaguzi kwa misingi ya jinsia, kifungu 82 (4) kinatoa fursa kuambatana na masuala ya sheria ya kibinafsi, pamoja na kugawanga na kusambaza mali baada ya kifo (kumaanisha kwamba sheria ya kawaida, Kiislamu na Kihindi zinapofaa, na vipengele vinavyobagua, haiko kinyume na Katiba). Sheria ya urithi (Sura ya 160), inayompa nafasi mtegemezi kama mume akifariki lakini hakuna wasia, sheria hii inajaribu kupanua dhana ya wategemezi kuhusisha pia wajane na watoto katika ndoa za wake zaidi ya mmoja na vile vila mke mmoja. Fauka ya hilo, kuna jambo la pekee kwenye kifungu cha 32 kwa ardhi ya kilimo, mifugo na mimea katika maeneo yanayotambulika kirasmi, kumaanisha kwamba sheria za mila, hata kama ni za ubaguzi, zinafaa. Na sheria ya waislamu imeondolewa pia katika kifungu hicho cha sheria. Mwanamume anapokufa bila ya kuacha wasia, mkewe anapata mali lakini mpaka atakapofariki ama kuolewa tena. Kama mwanaume atafariki kabla ya wazazi wake na hakuacha wosia, mali kwanza itagawanyiwa babake, lakini, akifa, atapewa mamake – kwa upande mwingine baba hupewa kipaumbele. Mtoto ambaye wazazi walikuwa hawajaoana (mwana haramu) anaweza tu kurithi babake katika mazingira fulani fulani. Baadhi ya sheria hizi huchukuliwa kama zenye kubagua, lakini kuna uwezekano kwamba si kinyume na Katiba.

Kenya haina kipengele kuhusu mgao wa mali chini ya ndoa. Sheria hiyo ni ile ya 1882, sheria ya mali ya wanawake walioolewa ya Uingereza. Ijapokuwa sheri hii inaeleza kwamba mwanamke anapoolewa huhifadhi mali yake, hali ya nyumba ya familia haieleweki. Sheria inaamini kwamba ardhi ni milki ya yule ambaye jina lake limetumiwa katika usajili; hata kama mke amechangia kutumia marupurupu ya mshahara wake, ama kwa shughuli zake za nyumbani kuipata ama kuitengeneza ardhi, hatakuwa na mamlaka kabisa. Kukiwa na talaka, ama mume akaamua kuiuza nyumba, mke anajipata hana haki na anaweza kutolewa nje ya nyumba. Hii inaweza kuwa si haki, lakini pia haiko wazi kwamba ni ya ubaguzi na kinyume cha katiba.

*(ii)* *Jamii za Ufugaji*

Ya pili inahusiana na haki ya idadi ya watu wanaofuga. Njia ambayo wafugaji wa kuhamahama wanavyotumia ardhi ni tofauti na vile ambavyo jamii zenye makao zinavyofanya, na hata kuna msisitizo wa matumizi ya ardhi. Wafugaji wa kuhamahama wanafahamu kwamba ardhi ni milki ya kikundi cha watu ama 'familia' inayoambatana na usasa ama asilia. Haimiliki kwa kiasi kwamba wanaoitumia wanafurahia haki zote za kuigawanya na kuitoa wanapotaka wenyewe. Huwa inawekwa amana kwa kizazi cha baadaye, na wanaoishi kwayo wana haki ya kuitumia ama 'kuilinda' ambako kunaweka mipaka na uwezo wa kutumia. Hii ndiyo haki ya kufurahia matunda ya ardhi, iwapo tu haileti madhara na kupunguza uzalishaji wake wa muda mrefu. Leo hii, dhana hii inaeleweka kwa uchache mno na haiheshimiwi. Matokeo yake yamepingana sana na mfumo wa shughuli za kawaida za ardhi ya ufugaji kwa hasara ya wafugaji. Ardhi iliyotumiwa zamani kwa njia za uendelevu sara imefarakana na aghalabu imeshushwa hadhi.

Mwaka wa 1968, kwa usaidizi wa wadhamini, Kenya ilianzisha sehemu maalum za kulishia wanyama kwenye maeneo makame, jambo lililoleta urasmi na usheria

wa matumizi ya ardhi katika jamiii ya makazi. Baadhi ya wafugaji waliukubali mfumo huo na dhana yenyewe kama njia ya kupata ardhi kisheria ambayo inaweza kuwasaidia kupata mkopo. Hata hivyo, miradi hiyo haikufaulu kwani hakuna hata sehemu moja kati ya sehemu zote iliyofaa kiekolojia ama kuwa katika kitengo cha jamii. Miaka ya 1980, palikuwa na mrundikano wa hati za kumiliki ardhi, ughushi wa upeo mkubwa, na wizi wa ardhi. Leo hii, ruwaza za matumizi ya ardhi na kuwa na mamlaka juu ya ardhi, haiwezi hata kutoa riziki na mahitaji ya kijamii ya watu, na vile vile kuendeleza usimamizi wa rasilmali.

Licha ya utafiti mkali uliotoa thamani ya mtindo huo wa maisha ya ufugaji wa kuhamahama na sera za serikali iliyokuwepo ya kunyang'anya na mijadala inayoazimia kuwapa makazi wafugaji, picha mbaya na kutoyaelewa fika maisha ya wafugaji bado inaonekana. Jamii za wafugaji kama vile Wapokot ni miongoni mwa zile ambazo zilitoa mapendekezo muhimu kwa Tume kuhusu madhara wanayotendewa katika taratibu za maisha yao, hasa kwa kukosa ardhi. Serikali ilijiwajibisha yenyewe katika karatasi ya kipindi No. 6 mnamo mwaka wa 1999, wakiunga mkono ufugaji wa mifugo katika mazingira yanayofaa.

Jaribio na kuokoa haki za ardhi ya ufugaji kadhalika linahitajika kufahamika katika ukweli uliopo kwenye matumizi ya ardhi. Jamii za wafugaji sharti kuhusika kwenye majadiliano yanayohusiana moja kwa moja na maisha yao. Kuokoa haki za ardhi ya wafugaji kunatoa fursa ya sheria kufahamika kwa kuwepo kwao na uhalali wa haki za mali zao. Hizi ndizo haki zinazowapa uwezo kutoka kwa jamii zinapotumika.

*(iii) Mahitaji ya Maskini Mijini*

Ya tatu inahusiana na mahitaji ya ardhi ya maskini wa mijini. Kuambatana na idadi ya watu wa Nairobi ambao ni milioni 2.5, karibu asilmia 60% wanaisha kwenye mitaa ya mabanda. Kibera, mtaa wa mabanda mkubwa zaidi barani Afrika uko jijini Nairobi na ni nyumbani kwa watu takribani milion 0.75%.

Kiwango cha ukusanyaji taka cha manispaa kilishuka kutoka asilimia 90% mnamo mwaka wa 1978 hadi asilimia 33% mwaka wa 1998 mijini Nairobi. Kukinyesha maji hukusanya taka zote hadi katika mikondo ya maji inayotumiwa na maskini. Licha ya hilo, maskini, na wale wasio na ardhi wanazidi kuingia jijini. Matatizo yaya haya yanatokea ndani na katika viunga vya jiji la Mombasa na miji mingine mikubwa.

# SURA YA KUMI NA NNE

# HAKI ZA ARDHI NA MALI

## 14.1 Agizo la Tume

Agizo la Tume chini ya sheria hii ni:

*"Kuchunguza eneo la haki za ardhi na mali, pamoja na binafsi, serikali na mfumo wa kikatiba wa ardhi ya kwanza na sheria ya Kenya, na maendeleo yaliyopendekezwa ambayo yatawapa furaha bashasha kwa ardhi hiyo na haki nyingine za kumiliki ardhi."*

Agizo hili lazima lisomwe pamoja na vipengee vingine ambavyo sheria hii inaitaka Tume kuchunguza hasa katika uchumi, mazingira na maliasili.

## 14.2 Suala la Ardhi Nchini Kenya

### 14.2.1 Kanuni za Jumla

*(a) Ardhi katika Uchumi na Jamii*

Suala la ardhi – umiliki wake, kufikia na matumizi – limechukua nafasi kuu kwenye sera ya umma na mazungumzo marefu kuhusu siasa nchini Kenya. Hii ni kwa sababu ardhi imekuwa kama kiini cha tatizo la kitamaduni, uchumi na mabadiliko ya kijamiii na kisiasa. Hii ni kwa sababu ardhi ni uti wa mgongo wa sera za jamii na siasa nchini Kenya. Kwa hakika siasa, uchumi, jamii na utamaduni tangu Waarabu huko pwani; na walowezi wa kiingereza baadaye katika karne ya 19, zimehusishwa na masuala ya kufikia na kuendesha ardhi. Upiganiaji wa uhuru chanzo chake kilikuwa ni kupigania ardhi. Zaidi ya hayo, usimamizi wa uchumi wa Kenya nyumbani, katika jamii na ngazi za kitaifa umehusishwa na ardhi.

Kufuatia miaka ya wa mifumo ya usimamizi wa awamu za kisasa za ardhi, sehemu kubwa tu ya idadi ya watu inaendelea kwa shida si tu katika kuiga mifumo mipya ya uchumi bali pia kuiga mazingira dhaifu na ya pembeni pembeni, kushuka hadhi kwa ardhi, mapato kidogo ya kilimo, na kuzidisha vurumai kuhusu kufikia na kuendesha ardh, na umaskini. Hali hii imetibua mahitaji mengi ya awamu ya ardhi na masuala ya matumizi ya ardhi kati ya wasomi, waunda-sera, wanasiasa, jamii ya kimataifa, serikali na mashirika ya kimataifa kwa mwongo mmoja uliopita. Wamewekeza vya kutosha katika mipango ya kurekebisha ardhi.

Hapa Kenya, Tume ya Njonjo ya kurekebisha sheria za ardhi ni mfano bora. Kuanzishwa kwa ukoloni kulichangia pakubwa katika mabadiliko kuhusiana na ardhi nchini Kenya na, hasa, kwenye mfumo wa umiliki, udhibiti na matumizi ya ardhi na jamii za kiasili. Kwa kidogo kuliko azimio, jamii za Wakenya walinyimwa haki ya kumiliki ardhi zao na pia maeneo yenye rutuba ya Kenya. Na zikapewa walowezi Wazungu Wenyeji walipewa makazi vitongojini ambapo walisimamiwa kama wakadamu ama manokoa wa kilimia wazungu.

Katika pwani ya Kenya inayohusisha kisehemu cha maili kumi kwa utao wa ndani kutoka Vanga kupitia kusini hadi kaskazini mwa Kismayu, hali ilikuwa tofauti sana. Hapa, Sultani wa Zanzibar alipata uhuru wa kutumia ardhi nje ya kisiwa, na mwaka wa 1895, eneo la ukanda wa pwani ikawa sababu ya kukodiwa ardhi kutoka kwa Sultani hadi kwa serikali ya Uingereza. Baadhi ya hatimiliki zilizotolewa kabla ya 1895 zilionekana. Wakati wa uhuru, baadhi ya wenyeji waliudhika walipogundua kwamba haikumaanisha watarudishiwa ardhi. Kuambatana na uhuru, tatizo la kutokuwa na wamiliki wa ardhi lilikuwepo na wenyeji wengi wa pwani wamebakia kuwa maskwota katika ardhi zao.

*(b) Uchumi wa Ardhi*

Uchumi wa Kenya una na utabakia kwa muda mrefu kutegemea kilimo na matumizi ya ardhi kwa ufugaji. Makadirio ya sasa yanaonyesha kwamba kilimo na ufugaji husaidia maisha ya idadi ya Wakenya kwa zaidi ya asilimia 75%, na kusaidia asilimia 70% ya kazi za mishahara na kuchangia zaidi ya asilimia 80% ya mapato ya bidhaa zinazopelekwa ng'ambo. Mimea inayotawala uchumi wa kilimo ni pamoja na kahawa, majani chai, korosho, miwa, mchele, matunda ya tindi, mawele, mtama, pamba, kilimo cha matunda, na makonge. Hizi hukuzwa kwa sababu ya pesa na matumizi ya kujipatia riziki kwa wakulima wakubwa na wale wadogo katika maeneo ya chini hadi ya juu kirutuba. Kilimo cha ufugaji cha ng'ombe wa maziwa na nyama kinaendelea vyema, hasa katika maeneo makame na makame wastani ambapo zaidi ya asilimia 50% ya ufugaji wa Kenya upo. Matumizi makubwa ya ardhi nje ya kilimo na ufugaji yanahusisha mavuno ya bidhaa za misitu – kwa mbao na kuni – utalii uchimbaji wa madini, uvuvi na muundomsingi. Kwa pamoja mambo haya yanafafanua mazingira ambayo uchumi wa ardhi ya Kenya unavyoendesha majukumu yake.

Kuambatana na utafiti wa uchumi wa mwaka 2000, uchumi wa Kenya ulikuwa umeshuka kwa miaka mitatu iliyopita. Sehemu zote za utafiti zilionyesha kwamba viwango vya ukuzaji vimeshuka kati ya 1997 na 1999. Ukuaji katika sekta ya utengenezaji ulishuka kufuatia mashindano ya kuingiza nchini bidhaa ambazo bei yake ni rahisi mno, muundomsingi uliogawanyika na uhitaji wa kiwango cha chini sana. Kwenye kilimo, viwango vya ukuaji vilishuka kutoka asilimia 1.5% mpaka 1.2% kati ya 1997 mpaka 1999. Uzalishaji wa mimea yote isipokuwa kilimo cha matunda na kahawa uliteremka kwa kipindi hicho hicho. Hata wakati ambapo palikuwa na mavuno bora, mapato pia yalishuka.

Ukaguzi wa hali hiyo ya umaskini kote nchini ulionyesha kwamba matokeo ya umaskini kwenye ngazi ya kitaifa ni asilmia 52.2%, kumaanisha kwamba baadhi ya Wakenya hawawezi kumudu mahitaji yanayotakikana ya kimsingi, kama vile

chakula na bidhaa ambazo si chakula. Ukaguzi huo unaonyesha kwamba umaskini umefika asilimia 53.9% na 49% mijini na vijijini mtawalia. Na huko katika maeneo ya vijijini hapa nchini Kenya, suala la umaskini vijijini linabakia kuwa na uhusiano mkubwa na hali ya uchumi wa ardhi.

Baadhi ya mambo yanalifafanua suala hili la uzalishaji unaosikitisha. Mwanzo, mvua kidogo katika maeneo yanayokuzwa vyakula kufuatia mvua ya El-Nino iliyonyesha miaka michache iliyopita. Pili, ni bidhaa za kilimo na upungufu wa nguvukazi katika mbinu nyingine za ufanyikazi. Pingamizi lilikuwa, kati ya mambo mengine, jukumu la kuondoa magonjwa na vifo miongoni mwa vikosi vya watendakazi wa vijijini kuambatana na kusambazwa kwa virusi vya ugonjwa wa Ukimwi.

Tatu, ni hasara kubwa ya kabla na baada ya mavuno, kufuatia teknolojia duni za uzalishaji na kuhifadhi. Mwisho, ni athari za matatizo ya kimfumo, ambao muhimu kwake ni kupungua kwa ubora wa ardhi na uharibifu unaoshirikishwa na rasilmali kupitia ukataji misitu, kuingilia ardhi zilizotengwa, msukumo wa kuongezeka kwa idadi ya watu, matumizi ya ardhi inayotumiwa na maskini, na kukosa kabisa ardhi bora, na rasilmali inayotumia sera.

*(c) Siasa za Ardhi*

Mbali na vipimo vya kiuchumi, hata hivyo, ni muhimu kugundua kwamba masuala ya ardhi nchini Kenya ni yenye hisia za ndani na kafika siasa kwa sababu za kijamii na kitamaduni.

Zana za kisiasa ambazo zimeipa asili umbo na kanuni za masuala yanayozunguka ardhi nchini Kenya yanaingilia na historia ya nchi hii. Utofautishaji unafaa kufanywa kwa hali hii kati ya maili kumi kwenye ukanda wa pwani ya Kenya (wakati huu ukiwa ni kama pwani yote), na sehemu nyingine za nchi. Kwani hapo awali mpaka ilipofika mwaka wa 1964 iliendeshwa na kutawaliwa na

mamlaka ya kikoloni kwa niaba ya na kama mali ya Sultana wa Zanzibar, siasa nyingi za kufikia na kudhibiti ardhi daima ni suala kubwa zaidi lenye kuhusisha kuingiliana kwa wenyeji, mabwanyenye wa Kiarabu na Taifa.

Ijapokuwa usimamizi na utawala wa sehemu nyingine za nchi, pamoja na maeneo ambayo hayakuwa chini ya makazi ya wazungu, yalikuwa wazi zaidi, suala la ardhi bado linabaki kuwa kitendawili katika maongozi na uhusiano wa kisiasa. Ukweli ni miongoni mwa walowezi Wazungu na kati yao na Waafrika, daima waliafika suala la ardhi manufaa yake, umiliki wake, udhibiti wake, matumizi wa usambazaji wake lilikuwa nyeti.

Hiki kikiwa kiini cha mazungumzo ya siasa kote nchini, suala la ardhi lilikuwa na wala sio jambo la kushangaza, chanzo cha kuupigania uhuru wa nchi hii. Baada ya uhuru mwaka wa 1963, suala la ardhi lilikita mara moja kama chombo cha kimsingi cha kujitafutia uwezo na kujitengea utajiri miongoni mwa wasomi ambao walikuwa wakisimamia vyombo vya mamlaka ya Taifa. Suala la ardhi lilibaki la kutajika katika ajenda za kisiasa na kimaendeleo.

### 14.2.2 Ardhi kwenye Katiba

#### *(a) Msingi*

Chini ya katiba ya mwaka wa 1963, haki zozote za ardhi za serikali ya kikoloni zilipewa eneo ambalo lina ardhi hiyo. Hii ilimaanisha kwamba ardhi ya serikali, na nia ya kupata ardhi ambayo imekodishwa, mkataba huo wa kukodi ulipo, ulipewa serikali. Wakati huo huo, ardhi yote huko "kwenye asili yao" ilifanywa kuwa ardhi amana na ilitolewa kwa mamlaka ya mabaraza ya wilaya. Mabaraza hayo yaliweka ardhi hiyo kwa manufaa ya wakazi wake, na walihitajika kutambua haki chini ya sheria ya kawaida, iliyohusu ardhi hiyo.

Mfumo wa kieneo ulipoondolewa, ardhi amana ilibakia na mabaraza ya wilaya.

### *(b) Katiba ya sasa*

Suala la ardhi limehusishwa Katika katiba mpya kwenye ngazi mbili. Kwanza, kama mali, haki ya ardhi zimelindwa na kifungu cha 75. Kwa hivyo haiwezi kupokonywa bila fidia. Pili, sura ya 9 ya Katiba iliipa haki ardhi amana; umiliki wake, udhibiti na usimamizi katika mabaraza ya wilaya ambayo yatatenga na kuitumia kwa manufaa ya jamii husika kuambatana na sheria za kawaida. Chini ya Sheria ya Ardhi Amana (kifungu cha 288). Ardhi Amana inatunzwa na Kamishna wa Ardhi kwa niaba ya mabaraza ya wilaya.

Ardhi hiyo kwa mamlaka ya baraza la wilaya inaweza kuamuliwa na kusajiliwa kama mali ya mtu binafsi. Ikitokea hivyo ardhi hiyo humalizika kuwa ardhi amana na inaweza kuwekwa wazi kutokana na uwajibikaji wowote. Ardhi amana inaweza pia kutengwa aidha na baraza la wilaya ama na Rais kwa kushauriana na baraza husika la wilaya, ili kutumiwa na shirika la umma au mamlaka, au kwa shughuli za umma.

Licha ya katiba, masharti yaliyowazi yanayohusu ardhi na usimamizi wa ardhi yanapatikana katika vyombo vingi vya sheria. Mfumo wa kisheria wa sasa kuhusu usimamizi wa ardhi nchini Kenya, unaweza kutajwa waziwazi kuhusisha vitengo vitatu vya ardhi; ikiwa ni Ardhi ya Serikali, Ardhi ya Kibinafsi na Ardhi Amana. Hii ni kulingana na sheria inayoweza kuambatanishwa kwenye zile zinazounda na kubainisha haki za mali katika ardhi; Sheria ya Ardhi iliyosajiliwa (Sura 283); Uhamisho wa Sheria ya Mali wa Kihindi, 1882; zile zinazotoa kwa sababu ya mpito kutoka kwa awamu ya Ardhi ya kawaida hadi kwa ubinafsishaji wa mfumo wa kiawamu kupitia utaratibu wa usajili (Sheria ya Maamuzi ya Ardhi, Sura 284); Sheria ya Uimarishaji wa Ardhi (Sura 283), Sheria ya Usajili wa Hati (Sura 281); na zile za marekebisho ya shughuli za utoaji wa ardhi, Sheria ya Udhibiti wa Ardhi (Sura 302). Uelekezaji wa matumizi ya ardhi unatawaliwa na baadhi ya vikwazo fulani pamoja na Sheria ya Kilimo (Sura 318), Sheria ya Afya

ya Umma (Sura 242), sheria ya machifu (Sura 128), Sheria ya Serikali za Wilaya (Sura 265), na Sheria ya Mipango ya Ujenzi (Sheria 6 ya 1996). Sheria ya mila inabakia kuwa sehemu ya mfumo wa sheria ya Kenya na inatumika wakati huu kama ambayo haiambatani na sheria zozote zilizoandikwa. Kati ya hizi ni Sheria ya Kilimo na Sheria ya Mipango ya Ujenzi ambazo zinahitaji maelezo maalum. Ile ya kitambo, ambayo ni chombo cha kimsingi katika marekebisho ya matumizi ya ardhi ya vijijini inahitaji zaidi kutangaza, kuendeleza, na kuhifadhi kilimo, kulinda mchanga na rutuba yake, na kutengeneza maendeleo ya ardhi ya kilimo, kulingana na mafunzo yaliyokubalika ya usimamizi bora wa ardhi na ukulima wa mazao sheria hii itampa haki ya busara kuu Waziri, pamoja na uwezo wa kufanya marekebisho yanayohusiana na uhifadhi, matumizi bora na maendeleo ya ardhi ya kilimo. Masharti yanayoundwa chini ya sheria hii yanawapa watu mamlaka ya kupinga kukatwa kwa mazao na kuwanyima mifugo lishe, na kupanda miti ili kuulinda udongo kutokana na mmomonyoko. Unaposhindwa kufuata kanuni hizo basi unavutia kuidhinisha uhalifu. Zaidi ya hayo, mkurugenzi wa kilimo anapewa haki ya kutoa taratibu za kuhifadhi ardhi ambazo zitawataka wenye ardhi kufuata kanuni za uhifadhi ama kupinga shughuli zenye uhusiano mbaya wa usimamizi mzuri wa ardhi. Masharti haya yanaweza kutumiwa kuleta njia bora za kusimamia ardhi na matumizi yake ambalo ni sharti zuri sana la maendeleo endelevu.

Hatua za mwisho za sheria ni chombo cha kudhibiti maendeleo nchini kote na hasa maeneo ya miji. Sheria hii inatumika sana katika ngazi za kieneo, kwa ardhi yoyote ya serikali, ardhi amana ama ardhi ya kibinafsi iliyo kwenye eneo la kimamlaka la Baraza la wilaya kwa lengo la kuimarisha ardhi hiyo na kutoa nafasi nzuri ya maendeleo ya ujenzi katika ardhi hiyo.

Sheria hiyo inatumika kwa kutoa masharti yanayofaa kwa muundomsingi kama vile; usafiri, kwa manufaa ya umma, biashara viwanda, makazi na maeneo ya burudani, ikiwa ni pamoja na mabustani, maeneo yaliyowazi, na yaliyohifadhiwa na pia kuweka masharti yanayofaa kwa matumizi ya ardhi kwa kujengea. Sheria

inatoa fursa ya mipango, kupangilia au kukarabati ardhi yote ama sehemu ya ardhi iliyo chini ya eneo la mpango wa maendeleo ya ujenzi na kudhibiti amri, asili na mwelekeo wa maendeleo kwenye eneo hilo. Katika maeneo ya miji pamoja na majiji, sheria hii inatoa nafasi ya maendeleo ya ujenzi ya muda mrefu na muda mfupi, kuandiisha tena au kuendeleza tena kwa minajili ya kulinda na kuratibisha maendeleo ya muundomsingi na huduma, na kwa udhabiti maalum wa matumizi na maendeleo ya ardhi au kwa utoaji wa ardhi yoyote katika maeneo hayo kwa manufaa ya umma.

Kwa jumla, sheria inatoa fursa ya kuyatayarisha maeneo na mipango ya maendeleo ya ujenzi ya wilayani, udhabiti wa maendeleo pamoja na ruhusa za kuendeleza au idhini, mgawanyiko, na kuondoa ardhi, kuzidisha muda wa kukodi n.k ikitegemea na masharti ya sheria ya Ardhi ya serikali, sheria ya Ardhi amana na sheria nyingine zozote zilizoandikwa zinazohusiana na utawala wa ardhi.

Ni muhimu kufahamu kwamba chini ya sheria ya mipango ya ujenzi, mamlaka za kiwilaya zitaendelea kudhibiti na kupinga maendeleo na matumizi ya ardhi kwa maslahi ya maendeleo sawa na yaliyopangika katika maeneo ya mamlaka ya kisheria lakini kwa utaratib u unaoambatana na masharti ya mipango ya maendeleo ya ujenzi yaliyoidhinishwa na mkurugenzi wa mipango ya ujenzi. Ili kuhakikisha migao hiyo ya ardhi katika maeneo hayo ya mamlaka za kiwilaya imefanyika kimpangilio wa wanamipango wa ujenzi waliosajiliwa lazima waendesha ugawanyaji huo.

### 14.2.3 Ardhi katika Katiba Nyingine

Kwa jumla Katiba zinashughulikia maswala ya ardhi kwa njia moja au mbili. Kwanza ni kuhusisha kwenye masharti ya jumla yanayolinda haki za mali ili kutotenganisha kati ya ardhi na aina nyingine za mali. Katiba nyingi zilizoachwa na mamlaka ya ukoloni wa Waingereza kwa serikali zinazojitawala ulimwengu mzima, zimefuata mfumo huu. Haki kuhusu mali kwenye ardhi, katika Katiba

kama hizo, hivyo basi, huchukuliwa kama urithi au haki za kimsingi. Pili ni kutenganisha ardhi (yaani mali isiyohamishwa) kutoka katika aina nyingine za mali na kuiainisha kama mali inayohitaji shughuli maalum ya kikatiba kuielezea. Katiba za hivi karibuni zaidi, hasa hizo zilizopitishwa katika Afrika, mnamo mwongo mmoja uliopita, kwa jumla zinachukua msimamo huu. Katiba ya Ugand inasema kwenye ibara ya 237 (I), kwa mfano, kwamba:

> *"Ardhi katika Uganda ni mali ya raia wa Uganda na watapewa kulingana na mtindo wa awamu za ardhi zinavyotajwa katika Katiba hii".*

Ibara ya 40 (3) ya Katiba ya Ethiopia inasema kuwa:

> *"Haki ya umiliki wa ardhi ya mashambani au mijini bila kuwamo maliasili imepewa Serikali na watu wa Ethiopia. Ardhi ndiyo mali ya kawaida ya Mataifa, Wazalendo na Wananchi wa Ethiopia na haiuzwi wala kubadilishwa kwa vyovyote".*

Kutokana na historia ndefu ya ushindi wa kisiasa iliyoanzishwa kuhusu utumiaji wa ardhi, Katiba ya Afrika Kusini ina masharti yanayoeleweka, yaliyo wazi kuhusu ardhi. Kwa mfano ibara 25 inaeleza na zaidi kuwa:

(6) Serikali sharti ichukue sheria ianyofaa na hatua nyinginezo katika maliasili iliyopo kuimarisha hali ambayo itawawezesha raia kufaidi kufikia au kupata ardhi kwa njia na msingi wa usawa……

(7) Mtu au jumuia iliyopokonywa mali baada ya June, 1913, kutokana na sheria za ubaguzi wa rangi au zoezi lilivyopasa, inavyoelezwa na Sheria ya Bunge, ama kurekebisha mali yenyewe au kuleta usawa.

(8) Hakuna sharti la sehemu hii itakayozuia Serikali kuchukua hatua kisheria na mambo mengine kufaulisha ardhi……na kuhusisha mabadiliko kuweka asawa kwenye ubaguzi uliopita wa rangi……

### 14.2.4 Walivyosema Watu

Palikuwa na maoni mengi kuhusu suala la ardhi na, hususan, hali halisi ya Ardhi Amana katika Katiba. Maoni hayo yanaweza kufupishwa kama ifuatavyo –

*(i)* *Kama kanuni ya jumla kwamba -*

(a) ardhi yote itakuwa chini ya watu na si serikali,
(b) Ardhi yote ya serikali "iliyonyakuliwa" inafaa kurudishwa,
(c) Ardhi amana inafaa kuwa haki ya moja kwa moja kwa jamii,
(d) Mgao wa ardhi unafaa kuwa sawa,
(e) Ardhi iliyopokonywa bila haki na serikali ya ukoloni au ya sasa itarejeshewa wenyewe ama isipowezekana, walipe fidia.
(f) Malipo yatatolewa kwa sababu ya uharibifu uliotokea baada ya ghasia za ardhi ama vita hasa katika bonde la ufa, pwani, kaskazini mashariki na sehemu Fulani za mkoa wa mashariki.

*(ii)* *Kwa makubaliano maalum kwamba -*

(a) Maeneo ya msitu yaliondolewa kwenye "gazeti rasmi la serikali," yaliyopewa watu binafsi, na kuharibu misitu, bila kuzingatia mazingira na kufikiria rasilmali ama hata jamii wenyeji wataharibu hali ya maisha ya watu, (kwa mfano, kusafisha sehemu Fulani za msitu wa Mau ambao utawanyang'anya watu wa Ongiek, na kuharibu jamii yenyewe).
(b) Athari za kunyang'anywa ardhi wakati wa ukoloni bado zinaonekana katika baadhi ya jamii.
(c) Jamii nyingine zimenyang'anywa nafasi za kufikia sehemu muhimu sana za kiasili.
(d) Kuna fursa nzuri ya ardhi isiyotumika wakati ambapo wengine wanalilia nafasi hiyo ya kupata ardhi.

(e) Wengine wanachukua ardhi kama ishara ya uwezo, badala ya kufanya kitu cha kuizalisha.

(f) Wengi wanataka bei ya juu ya ardhi inayoweza kuwa ya mtu binafsi ama, na wengine kwenye miji, wanaishi katika mitaa ya mabanda, aghalabu kama maskwota wasio na haki, bila ya vifaa, na bila zawadi ya kuboresha maisha yao.

(g) Wanawake wanafaa kuwa na haki bora zaidi za ardhi; katika hali ya udhibiti wa ardhi wanayolima, mirathi ya haki na haki za mali za ndoa.

### 14.2.4 Uchambuzi

Ushahidi wa kutosha katika umuhimu wa marekebisho ya ardhi na suala la ardhi limetolewa kwa Tume katika vikao vyake kila mahali nchini. Hata hivyo, ni vigumu mno kupata hawatatiziki kuhusu vurugu la ardhi. Shughuli zinazosababisha vurumai hilo la ardhi ni pamoja na –

- Urithi wa ukoloni na baada ya ukoloni;
- Kushusha hadhi sheria za kawaida kulingana na sheria za mtindo wa kizungu;
- Matumizi ya mamlaka wakati wa kugawiwa ardhi ili kupandisha maslahi ya kisiasa na kikabila;
- Ustadi wa shughuli na msingi wa ufisadi katika kugawanya ardhi ya serikali;
- Kunyang’anywa maskini ardhi yao na kuwaondoa watu;
- Umiliki wa ardhi kuwachwa kwa watu wachache;
- Kuzidi kwa ubinafsishaji na ubidhaa wa ardhi na kumomonyoka kwa haki za watu kutumia na kuishi kwenye ardhi, kuzika wafu na kuwa na fursa ya kukusanya bidhaa za kiasili;
- Kukua kwa umaskini na miujiza ya mwanadamu kuliundwa na wasiomiliki ardhi na masharti yasiyosalama katika vijiji na maeneo ya miji;

- Kushukishwa hadhi kufuatia kuvunjika kwa usimamizi wa maliasili, hasa rasilmali za kawaida za mali;
- Kuondoa kwenye gazeti rasmi la serikali na kugawa hifadhi ya misitu, iliyotumika kwa kipindi kirefu na kuishi wenyeji wake;
- Ukosefu wa vyombo vya Taifa kuelezea malalamiko na kuondoa migogoro ya ardhi kwa hali nzuri na iliyopangiwa;
- Jinsia na ubaguzi wa umri katika sheria za kawaida na za kitaifa kwenye utawala wa ardhi;
- Upungufu wa sera za ardhi kitaifa.

Mambo haya lazima yaongezewe kwa idadi ya watu, ambayo kwa baadhi ya maeneo yamepelekea kugawanywa kwa mashamba mara nyingi kufuatia kwa ngazi zilizo za kiuchumi na kuporomoka kwa uchumi kwa jumla. Virusi vya ugonjwa hatari wa UKIMWI vinasababisha mabadiliko mengi ya kidemografia na hali ya kawaida ya kuwa na ardhi ya kuhamishani tofauti. Watu wengi wamenyang'anywa bila kutarajia kwa kupitia usaidizi wa jamaa zao. Wazazi wanarithi ardhi kutoka kwa watoto wao na sio kinyume chake. Wanawake wanaachwa na watoto wadogo ikiwa ndio njia yao ya pekee ya msaada wa ardhi wanayolimia na ambayo hawataimiliki.

### 14.2.7 Mapendekezo

Hivyo basi Tume inapendekeza kwamba kanuni zifuatazo kama zilivyofafanuliwa katika 14.3.5 ihusishwe chini ya Katiba mpya –

*(vii) Ardhi yote ni ya watu wa Kenya na kwa hivyo –*

(a) watu wote watamiliki ardhi kulingana na mfumo wa kimasharti uliofafanuliwa na sheria; na
(b) watu ambao si wakenya watabatilishwa kupata ardhi isipikuwa kwa misingi ya kukodi.

*(viii) Ardhi hapa Kenya itagawanywa katika vitengo vya umma, binafsi na jamii na kwamba –*

(a) ardhi ya umma itabainishwa na kuwekwa kama amana ya wakenya kwa misingi ya kisheria kuelezea asili na kipimo cha uaminifu huo.
(b) Ardhi ya kibinafsi ichukuliwe na ipewe watu au wanamamlaka kuambatana na utaratibu wa kiawamu wa sheria.
(c) Ardhi ya jamii ibainishwe wazi wazi na jamii ipewe haki au mawakala wake kulingana na mfumo wa kimamlaka uliofafanuliwa kisheria.

(ix) Haki za mali iliyopatikana kihalali zitalindwa na inaweza kugawanywa bila ya kubagua jinsia, ikitegemea vikwazo hivyo kama vilivyo kimsingi kwenye mfumo wa awamu inayoziunda.
(x) Ardhi yote iliyogawanywa au kumilikiwa itaambatana na uwezo wa kimsingi wa Taifa kupata amakuishughulikia ardhi hiyo kwa manufaa ama maslahi ya umma.
(xi) Pataundwa Tume ya Ardhi ambayo majukumu yake yatakuwa –

(a) kutoa hatimiliki ya ardhi ya umma;
(b) kurekebisha sera na sheria za ardhi baada ya muda Fulani;
(c) kuendesha kanuni kwa matumizi endelevu na usimamizi wa ardhi; na
(d) kujifunza utawala wa majukumu ya ardhi iliyobakia.

(xii) Bunge litaweka sheria kwa kipindi cha miaka miwili kwenye kikao chake cha kwanza chini ya Katiba hii –

(a) uhusiano wa kanuni zilizoko juu;

(b) chombo cha kuondoa mizozo ya ardhi chini ya vitengo vya awamu mbali mbali;

(c) mfumo wa utawala wa ardhi chini ya vitengo vya awamu mbali mbali;

(d) mfumo wa kugawa ardhi kwa haraka na wenye manufaa yanoyolingana na gharama – uhamisho na utoaji;

(e) mgao wa sawa wa ardhi ikiwa ni pamoja na kutatua tatizo la wale wasio na ardhi, ama makazi ya hapo kwa hapo katika maeneo ya miji;

(f) uchunguzi na suluhi ya madai ya kihistoria hasa katika maeneo ya Mkoa wa pwani, Bonde la Ufa na mkoa wa kaskazini mashariki na maeneo mengine;

(g) kuanza kutoza ushuri ardhi zisizotumika ama zinazotumiwa vibaya; na

(h) uratibishaji na urahisishaji wa sheria za ardhi.

## 14.4. Awamu na Utawala wa Ardhi

### 14.4.2 Masuala na shughuli

*(i) Mfumo wa Umiliki wa Ardhi*

Umiliki wa ardhi unamaanisha taratibu na masharti ambayo yanatoa haki ya kupata ardhi, kubakia nayo, kuitumia, kuitoa kwa, ama kuibadilisha. Mtihani wa awamu ya ardhi ni kiungo cha kuundwa kwa sera ya ardhi. Kuna njia tatu za kuratibisha utawala mkongwe wa awamu za ardhi hapa Kenya.

Kwanza ni kulingana na eneo lenye hati ya viwango maalum vya ardhi, kama vile, ikiwa "serikali" chini ya sheria ya ardhi ya serikali (kifungu cha…) au Ardhi Amana. Kama njia ya kumiliki, kuainisha ardhi kama "serikali" kunamaanisha

kwamba ardhi kama hiyo niya “kibinafsi” kwa serikali na pengine kwa mafunzo, imetumika na ikatolewa kama hivyo. Kwa kweli, hakuna mahitaji ya kisheria chini ya sheria hii, au kanuni nyingine yoyote ya sheria, kwa serikali kujibu katika wajibu wowote wa umma, kulingana na ulinzi au matumizi ya ardhi.

Hivyo basi, hakuna vitengo vya ardhi ambavyo nivya umma, kwani imetengwa kwa, na imewekwa kutumiwa kwa manufaa ya raia wa Kenya zaidi. Hiyo ikiwa ni “mali” ilioyotengwa kwa serikali iliyo mamlakani, haishangazi kuona kwamba ardhi ya serikali kwa miongo minne iliyopita imekuwa ndio chanzo cha migawanyiko, kuchukua ardhi kimakosa na uharibifu usio na maana.

Uainishaji wa ardhi kama “amana” inamaanisha hasa katika misingi ya katiba na sheria ya Ardhi Amana, kwamba ardhi kama hiyo iwekwe kwa manufaa ya watu ambao ni wakazi wa maeneo hayo. Utawala mkongwe wa kisheria, unaotawala shughuli za uhusiano wa vitengo vya Ardhi Amana zote ni sheria ya kawaida. Kutolewa kwa haki ya hati zenye siasa kali na udhabiti kwa minajili ya Ardhi Amana ya mabaraza ya wilaya, ya kizungukwa na utoaji wa majukumu ya kiutawala ya Kamishna wa Ardhi, hata hivyo kumaanisha, kwamba kanuni za shughuli za kawaida haziheshimiwi kabisa. Ukweli ni kwamba, dharau za kikatiba kuhusu Ardhi Amana ziko wazi, pamoja na mengine ukosefu wa usalama kwa haki za ardhi za kiasili na jinsi inavyochukuliwa kama milki ya kimpito inayofaa kuondolewa mara moja kupitia haki za kumiliki, imepelekea kwa jamii kunyang’anywa mali yao katika maeneo mengi ya nchi.

Njia ya pili ambayo utawala huu mkongwe unavyoweza kuratibishwa ni kulingana na misingi ya utawala wa kisheria katika uhusiano wa Ardhi, kama vile, ikiwa utawala huo niwa serikali ama wa kawaida. Naya tatu ni katika misingi ya haki za kikwanta mathalan, milki huru, kukodi au ya wote. Kwa hali ya ile yakwanza, tawala hizi mbili zinatawalaiwa na mashirika ya kisheria yaliyo na taratibu zao za kipekee za ugawaji, kutenganisha na kuhakikisha. Kama matokeo

yake, sheria ya ardhi ya Kenya inabaki kuwa moja ya zile zilizovunjikavunjika, ngumu na zisizona misimamo nchini Kenya.

### *(ii) Matatizo yanayohusu Umiliki*

Kuambatana na ukweli kwamba utawala wa kisheria unaosimamia umiliki wa ardhi ni mgumu na usioweza kutekelezeka, imeeleweka kwamba matatizo mengi yatahitaji kusuluhishwa kama wakenya watakuwa na usawa katika kupata ardhi.

(a) Hali ya Wanawake

La kwanza kabisa ni kurekebisha hali ya wanawake. Wanawake wanachangia takriban nusu ya idadi ya wakenya na wamechukua nafasi kubwa katika kilimo asilimia 69% ya idadi ya wanawake chapakazi wanafanya kilimo cha kijizumbulia riziki, ikilinganishwa na asilmia 43% ya wanaume. Na bado wanamiliki asilimia 10% ya ardhi iliyopo. Wanawake wanaotaka kwa jamii ya maskini wengi, na familia zinazoongozwa na wanawake ni maskini zaidi ya zile zinazosimamiwa na wanaume. Ukosefu wa umiliki wa ardhi kwa wanawake kunapunguza matunda ya uzalishaji, inafanya maendeleo yasinyae na kuchangia umaskini na kupunguza heshima yake.

Mila za kiafrika zinaunga mkono urithi kutoka kwa baba na udhibiti wa kiume katika kutoa maamuzi ambayo huwatenga wanawake katika umiliki wa ardhi. Wanawake wanachukuliwa kama wasiohusishwa ukoo wao wa kuzaliwa au kuolewa, na hawapati ardhi kutoka kwa yeyote yule kati ya jamii hizo. Hata wakati ambapo wanawake wanapokuwa na haki ya ardhi ya familia, jamaa zao wakiume hupata fursa ya kuwanyang'anya na kuitafutia hati ya kumiliki ili kuwanyima wanawake pato lao. Wakati mwingine kina mana wanaunga mkono mila hizi.

Aghalabu wajane hupokonywa na mashemeji zao na kubakia bila makao. Ijapokuwa wake wengi huwa na mamlaka kidogo kuhusu mapato, wakati wa kutoelewana kwenye ndoa wanawake wengi hufukuzwa kwa kupewa kitu kidogo cha kujikimu maishani kama kipo. Hata ikiwa wamewatunzia wazazi wao, kina kaka mara kwa mara huwatimua kina dada wazazi wao wanapokufa. Asilimia 10% ya wanawake wanaoishi kwenye mitaa ya mabanda walihama vijijini kwa sababu ndoa zao zilivunjika, asilimia 8% ni wajane kufuataia msukumo w auzazi wa kutoolewa.

Virusi vya UKIMWI vinaziathiri vibaya haki za wajane wanoishi na mayatima kwa ardhi ya kiasili. Katika hali nyingine, wanawake hunyang'anywa ardhi yao na mali baada ya waume zao kuaga dunia. Wajane huzingiziwa kuwa wao ndio waliowaambuza waume zao na kupewa msukumo kuzihama nyumba zao za ndoa. Wajane huwa waamana wa mali, kwamba niaba ya watoto. Hawawezi kulipia rehani ardhi hiyo na hupoteza haki ya kubaki nayo anapoolewa tena. Wakati ambapo wanawake hao wanapoolewa bila watoto, ni mila kwao kurejeshwa kwenye familia zao punde marehemu anaposikwa. Watoto, bila ya kuzingatia umri wao, ndio huathirika zaidi. Mayatima kwa desturi huwachwa na jamaa zao wakubwa wa kiume. Haki ya watoto wa mwanamke ambaye hajaolewa wanaokufa kwa UKIMWI wana hatari kubwa kufuatia hali ya atakavyochukuliwa mama yao katika jamii na ile aibu ya ugonjwa huo.

Kila sehemu katiba inabatilisha ubaguzi kwa misingi ya jinsia, kifungu 82 (4) kinatoa fursa kuambatana na masuala ya sheria ya kibinafsi, pamoja na kugawanga na kusambaza mali akisubiri kifo (kumaanisha kwamba sheria ya kawaida, kiislamu na kihindi zinapofaa, na vipengele vinavyobagua, haiko kinyume na Katiba). Sheria ya mfuatano wa sheria, inayompa nafasi mtegemezi kama mume akifariki na hakuna wasia, alijaribu kupanua swala la wategemezi kuhusisha wajane na watoto katika vikundi vikubwa na vile vya mtu mmoja. Fauka ya hilo, kuna jambo la pekee kwenye kifungu cha 32 kwa ardhi ya kilimo, mifugo na mimea katika maeneo yanayotambulika kirasmi, kumaanisha kwamba

sheria za kawaida, hata kama niza ubaguzi, zinafaa. Na sheria ya waislamu imeondolewa pia katika kifungu hicho cha sheria. Mwanamume anapokufa bila ya kuwacha wasia, mkewe anapata mali lakini mpaka atakapofariki ama kuolewa tena. Kama mwanaume atafariki kabla ya wazazi wake na hakuwacha wosia, mali kwanza itagawanyiwa babake, lakini, akifa, atapewa mamake – kwa upande mwingine baba hupewa kipaumbele. Mtoto ambaye wazazi walikuwa hawajaoana (mwana haramu) anaweza tu kurithi babake katika mazingira Fulani Fulani. Baadhi ya sheria hizi huchukuliwa kama zenye kubagua, lakini kuna uwezekano kwamba hazifuati katiba.

Kenya haina kipengele kuhusu mgao wa mali chini ya ndoa. Sheria hiyo ni ileya 1882, sheria ya mali ya wanawake walioolewa ya uingereza. Ijapokuwa sheri hii inaeleza kwamba mwanamke anapoolewa huhifadhi mali yake, hali ya nyumba ya familia haieleweki. Sheria inaamini kwamba ardhi ni milki ya yule ambaye jina lake limetumiwa katika usajili; hata kama mke amechangia kutumia marupurupu ya mshahara wake, ama kwa shughuli zake za nyumbani kuipata ama kuitengeneza ardhi, hatakuwa na mamlaka kabisa. Kukiwa na talaka, ama Bwana akaamua kuiuza nyumba, mke anajipata hana haki na anaweza kutolewa nje ya nyumba. Hii inaweza kuwa si haki, lakini pia haiko wazi kwamba niya ubaguzi na kinyume cha katiba.

(b) Jamii za Ufugaji

Ya pili inahusiana na haki ya idadi ya watu wanaofuga. Njia ambayo wafugaji wa kuhamahama wanavyotumia ardhi ni tofauti na vile ambavyo jamii zenye makao zinavyofanya, na hata kuna msisitizo wa matumizi ya ardhi. Wafugaji wa kuhamahama wanafahamu kwamba ardhi ni milki ya kikundi cha watu ama 'familia' inayoambatana na usasa ama asilia. Haimiliki kwa kiasi kwamba wanaoitumia wanafurahia haki zote za kuigawanya na kuipeana wanapotaka wenyewe. Huwa inawekwa amana kwa kizazi cha baadaye, na wanaoishi kwayo wana haki ya kuitumia ama '<u>kuilinda</u>' ambako kunatoa nguvu na uwezo wa

kutumia. Hii ndio haki ya kufurahia matunda ya ardhi, iwapo tu haileti madhara na kupunguza uzalishaji wake wa muda mrefu. Leo hii, dhana hii inaeleweka kwa uchache mno na haiheshimiwi. Matokeo yake yamepingana sana na mfumo wa shughuli za kawaida za ardhi ya ufugaji kwa kutopata manufaa ya wafuagaji. Ardhi inapotumiwa kwa njia za uendelevu huwa imefarakana na aghalabu hushuka hadhi.

Mwaka wa 1968, kwa usaidizi wa wadhamini, Kenya ilianzisha sehemu maalum za kulishia wanyama kwenye maeneo makame, jambo lililofanya urasmi na usheria wa matumizi ya ardhi katika jamiii ya makazi. Baadhi ya wafugaji waliukubali mfumo huo na dhana yenyewe kama njia ya kupata ardhi kisheria ambayo inaweza kuwasaidia kupata mkopo. Hata hivyo, miradi hiyo haikufaulu kwani hakuna hata sehemu moja kati ya sehemu zote iliyofaa kiekolojia ama kuwa katika kitengo cha jamii. Miaka ya 1980, palikuwa na mrundikano wa hati za kumiliki ardhi, kughushi kwa upeo mkubwa, na wizi wa ardhi. Leo hii, ruwaza za matumizi ya ardhi na kuwa na mamlaka juu ya ardhi, haiwezi hata kutoa riziki na mahitaji ya kijamii ya watu na vile vile kuendeleza usimamizi wa rasilmali.

Licha ya utafiti mkali uliotoa thamani ya mtindo huo wa maisha ya ufugaji wa kuhamahama na sera za serikali iliyokuwepo ya kunyang’anya na mijadala inayoazimia kuwapa makazi wafugaji, picha mbaya na kutoyaelewa fika maisha ya wafugaji bado inaonekana. Jamii za wafugaji kama vile Wapokot ni miongoni mwa zile ambazo zilitoa mapendekezo muhimu kwa Tume kuhusu madhara wanayotendewa katika taratibu za maisha yao hasa kwa kukosa ardhi. Serikali ilijiwajibisha yenyewe katika karatasi ya kipindi No. 6 mnamo mwaka wa 1999, wakiunga mkono ufugaji wa mifugo katika mazingira yanayofaa (p.44).

Jaribio na kuokoa haki za ardhi ya ufugaji kadhalika linahitajika kufahamika katika ukweli uliopo kwenye matumizi ya ardhi. Jamii ya wafugaji wanafaa kuhusika kwenye majadiliano yanayohusiana moja kwa moja na maisha yao.

Kuokoa haki za ardhi ya wafugaji kunatoa fursa ya sheria kufahamika kwa kuwepo kwao na uhalali wa haki za mali zao. Hizi ndizo haki zinazowapa uwezo kutoka kwa jamii zinapotumika.

(c) Mahitaji ya Miji Maskini

Ya tatu inahusiana na mahitaji ya ardhi ya miji maskini. Kuambatana na idadi ya watu wa Nairobi ambao ni million 2.5, karibu asilmia 60% wanaisha kwenye mitaa ya mabanda. Kibera, mtaa wa mabanda mkubwa zaidi barani Afrika uko jijini Nairobi na ni nyumba kwa watu takribani million 0.75%. Kiwango cha ukusanyaji taka cha manispaa kilishuka kutoka asilimia 90% mnamo mwaka wa 1978 hadi asilimia 33% mwaka wa 1998 hapa Nairobi. Kukinyesha maji yenye zilzala hukusanya taka zote hadi katika mikondo ya maji inayotumiwa na maskini. Licha ya hilo, maskini, na wale wasio na ardhi wanazidi kuingia jijini. Matatizo yaya haya yanatokea ndani na katika viunga vya jiji la Mombasa na miji mingine mikubwa.

-------------------------------------------

Miongoni mwa mafunzo mengi ambayo watu wamepata kutokana na kutofaulu kwa maendeleo ya miji, la muhimu zaidi ni kwamba, maendeleo lazima yawahusishe wanajamii kwa njia inayofaa. Kujenga uaminifu na ushirika kati ya maafisa wa serikali na wakazi katika makao ambayo si ya kudumu na kuunda masharti ya kutoa huduma za kimsingi (km; maji na usafi, usimamizi wa taka, usalama na ulinzi) ni ya muda. Jitihada ambazo wakazi walizotia kwa makao hayo ili kuboresha na kupanga huduma wakati pakiwa hapana usaidizi wa mhusika yeyote, ni za kupongezwa. Wanatafuta njia za kujenga vyoo bila msaada wa kirasmi. Viongozi wa jamii wamejitokeza na kuchanga fedha za huduma ambazo watu watapanga wenyewe. Maendeleo haya ya chini – juu kwenye usimamizi wa miji na utoaji wa huduma umeweza kujengwa na mamlaka na kutekelezwa kama sehemu ya mradi ili kuleta mipangilio ya shughuli chini ya kanuni za sheria. Walipaji kodi wapya wenye haki za mali wana fursa ya kujijenga maisha yao ya

kijamii na kiuchumi kwa kuwekeza kwenye mali zao, wakijua kwamba nyumba zao hazitabomolewa na watavuna faida ya wafanyikazi wao.

Wanachama wa familia katika makazi hayo yasiyo ya kudumu wanataka kuhakikishiwa kwamba hawataondolewa bila fidia; kwamba watajenga nyumba zao vyema ili kujilinda dhidi ya hali ya hewa, wezi, moto na mafuriko, n.k; kwamba watoto wao watarithi mali hii au watauza ama kuihamisha. Wanaweza kukopa na kutumia mali kama mkopo wa nyongeza. Wanaweza kuomba kupunguzwa kwa ardhi kama kuna mzozano, kuyafikia maji, umeme, kuzoa taka, huduma za afya ya kimsingi, maeneo salama ya watoto kucheza na kukarabati barabara. Wanahitaji mfumo wa utawala wa haki za ardhi yao ambayo si ghali na inayopatikana na kuepuka kutumiwa vibaya na "wenyemabanda". Kuna tajriba kuu katika mataifa mengine ambazo ni za kuigwa.

Taratibu ya kukinga kutimuliwa kwa nguvu itaanzishwa kama njia ya muda, inaweza kuhakikishwa kwamba tangu siku Katiba mpya inapofanywa kuwa sheria (ama hata kabla ya hapo) hakuna kuondolewa kwa lazima kutakakofanywa kwa kipindi fulani. Hii ni kuepuka kuodolewa na wenye ardhi ama wahusika wa umma wanaoshindana ulinzi uliotolewa na Katiba.

*(iv) Vituo vya wanaoishi shambani*

Ya nne, inahusiana na hali ya wanaoishi Shambani, hasa wanaofahamika kama "maskwota". Wafanyikazi wa shamba na familia zao na wanaoitwa "maskwota" huishi kwa mashamba yanayomilikiwa na wengine. Wenye ardhi aghalabu hukiuka haki za kibinadamu za kimsingi (k.m. hadhi ya binadamu, uhuru na usalama, kujikinga na utumwa na kulazimishwa kufanya kazi). Mgao wa mashamba kwa sehemu zilizokuwa za Wazungu ilitibuka kuwa jambo gumu la matumizi ya ardhi na mipangilio ya shughuli za shamba. Kufuatia kuhamia kwa papo kwa hapo, maskini hukosa hati za kumiliki ardhi na huweza kuondolewa, kwa wenye ardhi (aghalabu wasiokuwemo) hutaka kuwa na udhibiti wa mali kuhusu ardhi yao. Matokeo yasiyoepukika ya kuuza ama kuhamisha (au

kusambaza tena) mashamba makubwa na ya serikali ni kwamba wafanyikazi shambani na familia zao wanaweza kutimuliwa bila fidia.

Ni vyema Kenya ianzishe taratibu fulani zitakazolinda wanaoishi shambani na watu na watu wanaoishi humo wasitimuliwe. Kwa sababu ya umasikini, kuna haja ya huduma za ushauri wa kisheria ili kuwafaa maskini ambao hawa au wameachiliwa kabisa kwenye utaratibu wa sasa wa kisheria. Wasiojua kusoma na kuandika na wanaotumikiwa vibaya na huduma za habari za umma, watabaki kutozijua haki zao chini ya Katiba iliyopo au Katiba yoyote mpya na sheria nyingine mpya. Afisi chache mpya za ushauri wa kisheria, zinazoendeshwa na mashirika yasiyo ya kiserikali, hazitatosha kutoa ushauri wao, habari na kuwakilisha maeneo ya mashambani.

*(v) Malalamiko ya Ardhi ya Awali*

Ya tano inahusiana na malalamiko ya kunyang'anywa ardhi wakati wa na baada ya ukoloni hapa Kenya. Ya muhimu zaidi ni ile inayohusiana na milki ya ardhi ya Waarabu katika ukanda wa pwani na utumizi mbaya wa ardhi ya Wamaasai chini ya "maafikiano" yaliyotiliwa saini na mamlaka ya ukoloni mwaka wa 1804 na 1911. Hivi majuzi, unyang'anywaji umetokea kwa sababu ya vita vya kikabila huko kwenye maeneo ya Bonde la Ufa, pwani na maeneo fulani na Mkoa wa Magharibi na Nyanza. Kurudia hali ya kunyang'anywa na kurudishiwa kwa ardhi ya asili kwa wadhulumiwa wa wale waliozimiliki awali ni tatizo kubwa la kisiasa. Jamii za sasa ni kubwa kuliko walioondolewa pale mwanzoni. Itakuwa muhimu kutathmini hali iliyokuwepo kabla ya kuondolewa na kuwafahamu wale wanaofaa kuchukua nafasi za waliokuwpo awali.

Je tatarudi mpaka lini kihistoria kushughulikia suala hili? Ni kigezo gani kitakachotumika kutathmini madai? Si kweli kwamba jamii zote, au watu wote kwenye jamii, wamewekwa pembezoni kwa hali inayofanana. Kutoa huduma bora kwa jamii moja kwa msingi kwa ilinyang'anywa ardhi, itatibua kunufaisha baadhi ya jamii kwa kuwatumia watu wengine ambao hata ndio mwanzo wanataka msaada zaidi pia marekebisho mengine ya ardhi yaliyofanyika kuambatana na uhuru kwa kanuni za

kutaka-kuuza-kununua yamesababisha sehemu kukaliwa na watu ambao sio waliozimiliki kabla ya ukoloni.

*(vi) Mageuzi ya Masharti ya Ardhi*

Ya sita inahusiana na athari za mageuzi ya masharti ya ardhi; mradi kamili ulianza katikati ya miaka ya 1950 kwa lengo kuu la kuwagawanyia watu binafsi umiliki wa ardhi katika maeneo ya Waafrika, yaani katika Africa k.v. maeneo ya Ardhi Amana. Mradi huo ulikuwa na bado uko, kwenye misingi ya imani ya ukristo asilia, yaani, kwa kubadilisha mfumo, badala ya muundo wa ugawanyaji wa ardhi na masharti inawezekana kuwa na uzalishaji kupitia mafunzo bora ya matumizi ya ardhi. Maelezo haya yanapatikana katika tasnifu kwamba umiliki wenyewe hususan ukifanywa kwa mtu mmoja na uko salama kutokana na kuingiliwa na serikali, ndio msingi wa kanuni za uchumi.

Mjadala uliogusiwa hapo juu umependekezwa na wanauchumi huria na wanamipango katika Afrika katika mikabala miwili. Wa kwanza, ulitolewa kama maelezo yaliyodai kutoweza kwa asasi za kawaida kuboresha maendeleo ya kilimo, ikidaiwa kwamba, kwa sababu ya kutosheka na ujina wake wa kiasili, asasi hizi kimsingi haziwezi kumudu mitindo ya uzalishaji ya kisasa, mbinu na mafunzo. Pili, umefafanuliwa kama tiba ya kubaki nyuma kimaendeleo bado kinakodumaza kilimo kote barani Afrika. Hatima ya madai haya ni kwamba suluhu iko chini ya mkondo wa ubinafsihji wa umiliki wa ardhi, badala ya udhibiti wa umma katika matumizi ya ardhi.

Ijapokuwa nchi kadhaa barani Afrika zimelikubali hili, na kwa hivyo zimewekeza rasilmali inayoyumbayumba kwa misingi ya mradi wa marekebisho, inafahamika wazi kwamba athari zake za kisiasa na kiuchumi bado hazijakaguliwa au kupokelewa kikamilifu. Hususan, athari za mfumo wa marekebisho katika uchumi, siasa na ushirika wa kijamii katika jamii ya mashambani haujawahi kupimwa dhidi ya madai ya mchango wa kukua kwa sekta ya kilimo. Utafiti wa hivi pamoja na wa Benki ya Dunia, umeonyesha imefahamika wazi kwamba madai haya yanapotosha. Wanaeleza bila ya

walakini kwamba kinachohitajika ni mageuzi ya ugawanyaji wa ardhi kisawasawa; hivyo ni kusema kuwa, zaidi ya muundo wa rasilmali, kuna haja ya kubadilisha miundo ya uzalishaji na huduma za utekelezaji wa muundomsingi.

***(c) Masuala yanayohusiana na Utawala wa Ardhi***

Utawala wa Ardhi unahusisha shughuli zote zinazoambatana na utaratibu wa kuwasilisha haki za ardhi, mifumo ya haki za ardhi, ulinzi; pamoja na mstari wa mpaka, usororea, usajili, masharti na udhibiti wa matumizi ya ardhi, masharti ya ardhi ya soko, na kushughulikia migogoro ya ardhi.

Udhaifu mkubwa wa utawala wa ardhi wa sasa ni ukosefu wa uangavu na asasi maalum zinazohusika na ardhi ya umma asili, utawala unaochukuliwa kuwa na ufisadi, imeelekezwa sehemu moja, na uko mbali kutoka kwa wanaotumia rasilmali. Serikali inahitaji mfumo huo kuwa sawa kote nchini na uwe endelevu. Inahitaji msingi wa utekelezaji katika kutoza ushuru wa kawaida, matumizi ya ardhi na haki tabaka na wastani, wafanya biashara, na watu maskini. Inahitajika kuwapa watu hati za kumiliki ardhi katika hali ya kufikika na yenye busara na kutoa hati za kumiliki ardhi isiyochukuliwa kuwa hafifu. Masjala ya usoroveya wa ardhi na hatimiliki kwa ardhi ya kibinafsi ni muhimu kukaguliwa ikiwa inani za hatumiliki kwa ardhi za kibinafsi na ardhi ya soko na eneo na uwekezaji itarejeshwa. Usambazaji wa masjala ni muhimu. Hali ya sasa, ambapo hatimiliki hutolewa kwa usambazaji wa usajili wa ardhi. Hali ya sasa ambapo hatimiliki hutolewa kwa wasiofahamika, bila kuzingatia wenye haki wasiorasmishwa, wanaotumia na kuishi kwenye ardhi hiyo, haikubaliki na inawakilisha ukiukaji wa misingi ya haki za kibinadamu.

### 14.3.2 Umiliki na Utawala wa Ardhi katika Katiba Iliyoko

Kama ilivyo hapo juu, Ardhi Amana pekee ndiyo iliyoelezewa kwenye Katiba. Sharti hilo, hata hivyo, linahusika na masuala ya utawala, licha ya umiliki. Kwa hivyo, suala gumu linalohusu hali na masharti ya kupata ardhi yameachiwa sheria ya jumla.

Kwa hali hii, lazima pawe na tofauti kati ya umiliki mkongwe wa masharti ya kitaifa na kiasili. Ile ya kitambo ilihusika katika utungaji mwingi wa sheria muhimu zaidi kama:-

- Sheria ya uhamisho wa Rasilmali ya India, 1882;
- Sheria ya Ardhi iliyosajiliwa (Sura ya 300),
- Sheria wa hatimiliki ya Ardhi (Sura ya 281).
- Sheria ya Usajili wa Nyaraka (Sura ya 285), na Sheria ya Hatimiliki ya Ardhi (Sura ya 282)

Hatua hizo za mwisho zilihusisha masharti na mila zinazotawala ardhi inayofahamika na jamii za kiasili za Kiafrika.

Ardhi yoyote iliyokuwa chini ya umiliki wowote, itachukuliwa na serikali kwa minajili ya Umma ama kama maslahi ya Umma yanaihitaji. Taratibu za kimanufaa kwa minajili ya ardhi iliyo chini ya umiliki wa serikali imewekwa wazi kwenye Sheria ya upataji Ardhi (Sura ya 295). Kuhusu Ardhi iliyo chini ya umiliki kimila, utaratibu, unaotahamika kama "kutenga" umewekwa kwenye Katiba na Sheria ya Ardhi Amana (Kifungu cha 288).

**14.3.3**

### 14.3.4 Walivyosema watu

Tume ilikuwa na maoni marefu na mapana kutoka kwa watu kuhusiana na umiliki wa ardhi na utawala wa ardhi. Hii inaweza kufupishwa kama "ifuatavyo";

i. Ardhi hapa Kenya inaweza kupatikana chini ya mfumo wa umiliki wa kimila, kibinafsi au umma;
ii. Ardhi yote inayotumika na/au ambayo ni makazi ya wenyeji na ndipo

wanapoendeshea shughuli zao za maisha itapewa haki kwao katika misingi ya umiliki wa ardhi ya kawaida au kibinafsi kama vile ambavyo itakavyoamuliwa na kikao cha ardhi cha pale, kitakachozingatia hali zote;

iii. Ardhi yoyote nyingine isiyotumika au kuishi mtu, kama ilivyoelekezwa hapo juu, itahifadhiwa kama ardhi ya matumizi ya baadaye kwa maslahi ya umma, uadilifu, afya na maendeleo.

iv. Katiba inafaa kuanzisha kanuni za sera muhimu kuhusu ardhi inayohusisha pamoja na mengine:

(a) heshima kwa haki za watu na jamii chini ya sheria ya mila;
(b) suluhisho kuhusu haki za mila na zile za taifa;
(c) unyumbufu ili kuruhusu mabadiliko ya umiliki kwa maslahi ya umma na bila kudhuru wenye haki waliopo.

v. majukumu ya yaliyokuwepo na haki za mabaraza ya wilaya zitakuwa chini ya Tume ya Ardhi ya Kitaifa;

vi. ardhi yote inayofahamika kama Ardhi Amana, ambayo bado inashughulikiwa na haijasajiliwa, itafahamika kwetu kama ardhi iliyopo chini ya Umiliki wa kimila;

vii. ardhi yoyote inayotumika na / ama wanayoishi wakazi na ambako wanapata ruzuku yao itatolewa haki katika misingi ya aidha umiliki wa kibinafsi au kiasili kulingana na hali halisi, ya mambo;

viii. ardhi hiyo ambayo haitumiki au haitumiwi kwa wakati ule na wakazi wake wa eneo fulani, itatengwa kwa na kugawanyiwa jamii asilia kama ardhi ya ujina;

ix. ardhi yoyote kama hii ambayo haitumiki au kukaliwa, au iliyotengwa, itahifadhiwa kwa matumizi ya badaye kwa maslahi ya umma au matumizi ya

jamii;

x. Ardhi yoyote amana ambayo muda wake wa kukodi umekwisha, mara moja itapelekwa kwa Tume ya Ardhi ya kitaifa kwa kupewa nafasi tena na Tume ya Taifa ya Ardhi na kutolewa upya na halmashauri ya ardhi na kuanishwa tena kama ilivyoelezwa hapo juu; na

xi. Ardhi ya kibinafsi lazima ilindwe.

### 14.3.5 Uchanganuzi

Ijapokuwa uchunguzi wa kina kuhusu masuala ya ardhi hapa Kenya unafanywa na Tume tofauti, Tume hii ina imani kwamba mabadiliko mengi lazima yafanyiwe sekta ya ardhi. Kuna haja ya kutoa taarifa maalum kuhusu sera ya ardhi, marejeleo na usawa katika sheria za ardhi, na njia bora na mfumo angavu wa utawala wa ardhi.

### 14.3.6 Mapendekezo

**Hivyo basi Tume imependekeza kwamba:**

i) *Paundwe sera mpya ya ardhi itakayoshughulikia matarajio yanayofaa ya wamiliki waliopo na maagizo ya watumiaji, hususan, -*

a) wenye ardhi wa kibinafsi utapewa usalama wa kumiliki ardhi yao, ila kwa kuzingatia maslahi ya umma, utaratibu mwema, uadilifu, afya na maendeleo, ambayo yatachukua nafasi kuu dhidi ya haki za mtu binafsi;

b) Hakuna atakayenyang'anywa ardhi yake au haki ya kumiliki ardhi ila kama ilivyotajwa katika Katiba hii;

c) Hakuna atakayenyimwa ardhi kwa misingi ya kijinsia, hali ya ndoa, au umri ama sababu nyingine zinazotokana na historia, mila au tamaduni; na

d) kukoma kwa haki za mmiliki ardhi wa kibinafsi kutafanyika ikiwa tu kunaambatana na Katiba;

e) Ardhi yote inayoelezewa, kama ardhi ya serikali ambayo haijatenganishwa itakuwa katika hali yao ya uhuru;

f) Ardhi yote ya umma itatumika kwa shughuli za umma pekee na kwa maslahi ya umma;

g) Ubinafsishaji wa ardhi utatokea tu endapo unasaidia maslahi ya umma;

h) Serikali au Serikali ya wilaya, inaweza kutwaa ardhi kwa maslahi ya umma kama ilivyoagizwa na Bunge;

i) Serikali ikielekezwa na Bunge italinda maziwa, mito, ardhi chepechepe, misitu, hifadhi za wanyama, mbuga za wanyama za kitaifa na kuziweka amana kwa maslahi ya wananchi;

j) kutenganishwa kokote na kutolewa kwa maeneo yaliyolindwa, ikiwa ni pamoja na hifadhi ya misitu, itafanywa kwa njia ambayo italinda unuai wa kibayolojia, uzalishaji, uwezo wa ukuaji na pia kuzingatia manufaa yake katika ikolojia ya baadaye, uchumi na wajibu wa kijamii na mahitaji ya ardhi kwa watu wa eneo hilo;

k) ardhi ni rasilmali ya kitaifa na inafaa kutumiwa kwa njia bora itakayokifaa kizazi kilichopo na kile cha baadaye;

l) umiliki wa ardhi unachukuana na kanuni za kijamii kuhudumia jamii kubwa

m) taifa litagundua, litaheshimu na kulinda haki za jamii za kiasili ili kuhifadhi na kuendeleza tamaduni zao, mila na asasi kuhusu ardhi. Itahusisha haki hizi katika kuunda sera na mipango ya kitaifa;

n) Mfumo wa kutangaza ardhi ni bora, unabana matumizi, unaofikiwa kwa urahisi, ni salama, angavu na hauna migogoro.

o) Sera inaheshimu:

- mila na tamaduni na umuhimu wa ardhi katika desturi ya jamii nyingi za Wakenya

- maeneo muhimu ya na tamaduni ambayo hata hivyo sehemu kubwa haitumiwi na jamii hiyo;
- matumizi bora ya ardhi kote mijini na mashambani;
- kanuni za kikatiba za haki za binadamu pamoja na usawa wa kijinsia.

*(ii) Uwezo wa Taifa kupata ardhi kwa lazima, utalingana na kanuni zifuatazo:-*

a) maslahi ya umma ni bora kufahamika na iambatane na usawa wa kumiliki kwa faradhi na haitasababisha matatizo kwa watu na jamii ambao wamenyimwa ardhi
b) ardhi iliyotolewa na haitumiki kwa shughuli za Umma, inafaa kurejeshewa wamiliki wake wa awali.
c) umiliki ardhi utakumbana na changamoto ya wenye ardhi/wanaoishi mle;
d) Katiba inafaa kutoa fidia ili kuakisi mambo fulani kama vile masharti ya Afrika Kusini.
e) haifai kuwa na kanuni zilizoelezewa mno – kama ilivyo katika Katiba wakati huu – hadi kufikia hali kwamba mambo ya kawaida tu ya kisheria kama vile kunyang'anya mtu ardhi kwa sababu ya kutolipa ushuru, ama utekelezaji wa hukumu ya Mahakama, hayapingani na katiba.
f) kiwango cha fidia na wakati na taratibu za malipo, sharti kiwe cha haki na sawa, huku kikiakisi usawa kati ya maslahi ya umma na maslahi ya wale walioathirika, kuambatana na hali fulani fulani, pamoja na historia ya manufaa hayo na matumizi ya ardhi;
g) hata hivyo, inaweza kupendekezwa kuwepo kwa taarifa hata kiwango cha utekelezaji wa matumizi ya ardhi kwa misingi ya kuhifadhi, kulinda mazingira, mipango na maslahi ya umma, isiyonufaisha haki, kuepuka madhara ya watu, wanaofuata hali hasa ya Marekani, unaweza kuzua mjadala kwamba wanaruhusiwa kikatiba kuyapinga masharti hayo au kuomba fidia.

*ii) Tume ya Ardhi ya Taifa ianzishwe ili:*

(a) kushikilia kutawala ardhi yote ya umma na itaweka amana kwa watu wa Kenya, pamoja na kizazi cha baadaye;

(b) kutekeleza udhamini kwa misingi ya Sheria na kueleza aina yake na yaliyomo;

(c) kutekeleza majukumu yafuatayo, ili

- kuhakikisha utekelezaji wa haki na utaratibu wa Katiba kuhusu ardhi ikiwa ni pamoja na kanuni agizi za sera ya taifa na malengo ya kitaifa;
- kutoa nafasi ya majadiliano ya umma yasiyokinzwa kuhusu masuala kadhaa ya ardhi kila wakati;
- kusimamia mwanzo mpya katika usimamizi wa umiliki wa ardhi, kutathamini na kuidhinisha hati za kumiliki mashamba ambazo zimekwishatolewa;
- kusimamia uundaji na usimamizi wa benki za ardhi za umma zinazolenga kuhudumia mahitaji mapya na yanayojitokeza ya maendeleo ya taifa hili;
- kuhakikisha matumizi ya ardhi yaliyo thabiti, na yenye mpango na endelevu kwa madhumuni yanayotambuliwa;
- kufuatilia maeneo ambako makubaliano hayajafikiwa, ikiwa ni pamoja na kushughulikia upya makosa ya kihistoria kupitia fidia, ikiwa inawezekana, kupewa mahali pengine pa makazi, au fidia ya fedha miongoni mwa njia nyingine;
- kuendeleza elimu ya umma kuhusu masuala ya ardhi, hasa masuala ya kikatiba na kisheria;
- kuwa mdhamini wa Wakenya na mlinzi wa haki za watu ikiwa ni pamoja na haki za jamii asili ya kuhifadhi na kuendeleza utamaduni wao, mila na asasi zinahusu ardhi;
- kushauri serikali na vyombo vingine vya taifa kuhusu masuala ya ardhi yaliyo na umuhimu katika Katiba ikiwa ni pamoja na sheria, na masuala ya kisheria na sera.

*iii) Katiba inapasa kuzingatia sheria kuhusu:*

(a) utambuzi wa sheria ya kimila;
(b) utambuzi zaidi wa mahitaji wa waliokuwa wakitegemea panapotokea kifo, ikiwa ni pamoja na haki za wanawake ambao wamekuwa wakilima shamba;
(c) ulinzi wa boma za ndoa za pande zote zinazohusika katika ndoa wakati ndoa hiyo inapoendelea na wakati wa kutamatisha ndoa;
(d) ulinzi wa haki sawa za wanaume na wanawake katika ndoa wakati ndoa inapoendelea, na wakati inapovunjika;
(e) kufurahia umiliki wa pamoja wa ardhi ya mke na mme, mradi ardhi hiyo ndiyo makao makuu ya familia, au ndiyo chanzo kikuu cha mapato ya familia, au ndiyo inayotegemewa kuendeleza familia, au ndiyo chanzo kikuu cha mapato ya familia, au ndiyo inayoteuliwa kuendeleza familia;
(f) kuzuia kufikia kwa ardhi kibaguzi kutokana na sababu za jinsia, hali ya ndoa, umri au tofauti nyingine yoyote;
(g) kutambua na kulinda haki za jamii za wafugaji wa kuhamahama;
(h) kuhakikisha kuhusika kwa jamii za wafugaji wa kuhamahama katika uamuzi utakaoathiri maisha yao;
(i) kuweka njia na utaratibu utakaotumia na kushughulikia upya makosa ya kihistoria;
(j) kuweka hali ikiwa ni pamoja na utoaji wa fedha, utakaowawezesha wananchi kuweza kufikia ardhi ama kwa njia iliyo sawa;
(k) kuhakikisha kuwa ardhi ya umma iliyonyakuliwa kwa njia isiyo halali inarejeshwa kwa Tume ya Ardhi ya Taifa mara moja, isipokuwa anayemiliki ardhi hiyo akilipa fidia inayochukuliwa kuwa ya kutosha kwa mamlaka.
(l) kuanzisha mahakama maalum ya kudumu ya kushughulikia malalamiko kuhusu ardhi itakayochunguza masuala ya kihistoria ya kutotendeana haki kwa watu binafsi au jamii kuhusu ardhi. Hii lazima ifanywe katika kipindi cha miaka miwili kutoka tarehe ya kupitishwa kwa Katiba mpya.

*(iv)* *Mfumo wa usimamizi na ardhi uanzishwe. Mfumo huo:-*

(a) huru kutokana na ushawishi wa kisiasa;

(b) uhusishe jamii kupitia njia inayoruhusu jamii hizo kuhusika kikweli katika kuanzisha mahitaji ya jamii hizo, na katika kufanya uamuzi kwenye viwango vyote;

(c) uwe wazi; katika hali hii, ni lazima maslahi au nia inayohusiana na mali ya kibinafsi isishughulikiwe sana ili kuhakikisha matumizi ya rasilmali za taifa yaliyo thabiti na kudhibiti ufisadi;

(d) uungwe mkono na halmashauri na kamati za nyanjani. Makundi haya yanapasa kuzingatia maslahi ya jamii, ikiwa ni pamoja na maslahi mengine yaliyo hatarini;

(e) Ujumuishe mfumo wa mahakama maalum au mahakama zinazoshughulikia masuala ya ardhi. Mashirika yanawakilisha maslahi nyanjani au ya kitaifa yanapaswa kuweza kutetea mipango yao mbele ya makundi hayo ikihitajika.

### 14.4.4 Haki za mali ya kitaalamu

#### 14.4.4.1 Kanuni za Jumla

Wakati mwingi mijadala kuhusu mali haishughulikii kwa undani masuala yanayohusu mali ya kitaalamu. Mali ya kitalaamu imetambuliwa kama, "kifaa muhimu katika uvumbuzi na maendeleo ya kijamii na kiuchumi". Mali ya kitaalamu:

- Hati ya uvumbuzi – kulinda habari iliyovumbuliwa;
- Hakimiliki – kulinda habari asili katika njia ya kujieleza;
- Nembo – kulinda habari iliyo na ishara;
- Siri za biashara – kulinda habari kuhusu biashara inayotolewa kwa njia ya siri;
- Miundo ya matumizi – kulinda uvumbuzi mpya;
- Usanifu wa kiviwanda – kulinda usanifu wa kuonekana;
- Ufahamu au ujuzi wa kitamaduni au kiasili.

Taasisi kuu zinazoshughulikia masuala ya mali ya kitaalamu hapa Kenya ni Afisi ya Kenya ya Viwanda (KIPO), na sehemu ya hakimiliki katika afisi ya Mwanasheria Mkuu. KIPO inashughulikia masuala ya mali ya viwanda na ilianzishwa chini ya Sheria ya Mali ya Viwanda (Sheria Na. 2 ya 2001). Majukumu yake yanajumuisha usajili wa rembo, uhamishaji wa teknolojia, na kutoa hati ya uvumbuzi wa vyeti vya miundo ya matumizi. Sehemu ya haki miliki hushughulikia masuala ya haki miliki ya miziki, sanaa, filamu na uchapisaji miongoni mwa mambo mengine. Sheria ya haki miliki ya mwaka 2001 inaunda halmashauri ya haki miliki, ya Kenya, inayojumuisha mambo kadha kuhusiana na sekta ya haki miliki. Kwa jumla, huongoza na kusimamia utekelezaji wa sheria ya Haki Miliki nchini Kenya.

#### 14.4.4.2 Masuala ya mali ya kitaalamu katika Katiba iliyoko

Ijapokuwa hakuna lolote kuhusu mali ya kiakili katika Katiba iliyopo, Kenya imetia saini mapatano kadhaa ya kimataifa kuhusu suala hili. Mapatano hayo yanajumuisha mapatano kuhusu viumbe anuwai na mapatano yanayoanzisha Shirika la Kimataifa la Mali ya Kitaalamu (WIPO), na Shirika la Eneo la Afrika la ya Kitaalamu (ARIPO).

### 14.4.3 KIMANI INSERT

### 14.4.4 Waliyosema wananchi

Mambo ambayo wananchi waliiambia Tume yanaweza kuwasilisha kimukhtasari ifuatavyo:

i. wavumbuzi wa mambo, kwa mfano dawa na ndege waendelezwa na serikali;
ii. Katiba inapasa kuzingatia haki za mali ya kitaalamu kwa uvumbuzi unaofanywa na wananchi;
iii. sheria inapasa kulinda haki za kiakili za Wamaasai;

iv. hati za uvumbuzi kuhusu teknolojia zinapaswa kuondolewa baada ya miaka 25;

v. Katiba inapasa kuzingatia kwamba hali ya kijamii inabadilika kila wakati, na kuendelea kwa ufahamu wa binadamu na teknolojia;

vi. Wavumbuzi wazawadiwe na serikali Katiba inapaswa kulinda na kuendeleza haki za mali ya kitaalamu na uvumbuzi;

vii. hati za uvumbuzi zinapaswa kuimarishwa ili kuwalinda wakenya wanaovumbua; wavumbuzi pia wanapaswa kuzawadiwa na dhana zao kutumika;

viii. Kuhimiza kutoa hati ya uvumbuzi ili kuwalinda wawekezaji wa humu nchini;

ix. Uvumbuzi wetu wote unapaswa kupewa hati za uvumbuzi;

x. Usajili wa hati ya uvumbuzi unapaswa kubadilishwa ili kumudu usajili ulio na gharama ya chini;

xi. Serikali inapasa kuhimiza maendeleo ya uvumbuzi wa kiteknojia katika kusaidia wavumbuzi;

xii. wawekezaji wanapaswa kuruhusiwa kumiliki ardhi katika maeneo ya mashambani;

xiii. wanaoiba utafiti au uvumbuzi wanapaswa kuadhibiwa; kodi fulani zinapaswa kuelekezwa upande na utafiti.

#### 14.4.4 Uchanganuzi

Hakuna shaka kwamba watu wa nyanja zote za maisha wanafahamu na kupendezwa na umuhimu wa mali ya kitaalamu na, hasa, mali ya kitamaduni. Maoni yenye kina yaliwasilishwe na watamaduni waliokasirishwa na uharibifu wa misitu unaofanywa na mashirika ya kimataifa yakitafuta mimea yenye dawa. Kwa hivyo, uhifadhi ulionekana kama suala la turathi; na pia suala la maisha.

#### 14.4.5 Mapendekezo

Tume inapendekeza, kwa hivyo kwamba:-

(i) Masharti yatiwe kwenye haki za sheria, ya kumpa kila Mkenya uhuru wa kushiriki katika maisha ya kitamaduni ya jamii yake na kufurahia sanaa, na kugawiwa marupurupu ya maendeleo ya kisayansi.

(ii) Masharti yatiwe kwenye sheria kwa ulinzi wa maslahi yote yanayotokea na yanayosheheni kwa juhudi za kisayansi au kisanaa ya Mkenya yeyote.

(iii) Bunge liunde sheria ya kuendeleza uvumbuzi wa kitamaduni, viwanda na uvumbuzi wa kisayansi na kutoa malipo ya marupurupu yanayopatikana kwa wavumbuzi au waandishi.

(iv) Masharti yatiwe kwenye Katiba ya ulinzi wa ujuzi wa kiasili.

## SURA YA KUMI NA TANO

## RASILMALI ZA UMMA NA KUJENGA UWEZO WA UFANYI KAZI

### 15.1 <u>Agizo la Tume</u>

Kujumlisha ardhi na rasilimali za kiasili, Tume ilitarajiwa na sheria kuchunguza na kufanya mapendekezo kuhusu suala la usimamizi kwa rasilmali za umma ambazo ni muhimu kwa kuanzisha utaratibu wa usawa kwa maendeleo. Hususan, sheria iliipatia Agizo Tume kuchunguza na kurekebisha usimamizi na matumizi ya fedha za umma na kupendekeza mbinu za kuyaboresha matumizi hayo. Kwa kufuatilia agizo lake la jumla, Tume pia ilichunguza masuala yanayohusu ujengaji wa uwezo wa ufanyi kazi hasa katika kuendeleza rasilmali ya kibinadamu, sayansi na teknolojia.

### 15.2 <u>Usimamizi wa Fedha za Umma na Mapato</u>

#### (i) Wajibu wa Serikali

Umuhimu wa usimamizi na udhibiti wa fedha za umma na uwajibikaji hauhitaji kusisitizwa zaidi katika nchi nyingi, mwajiri mkubwa ni serikali. Pesa nyingi huzunguka katika shughuli za serikali ambayo inauwezo wa kutoza ushuru. Matumizi mazuri na matumizi mabaya ya rasilmali za fedha huleta malalamiko zaidi kuliko nyanja yoyote nyingine ya serikali. Kawaida, malalamiko yanahusu ugawanyaji kuambatana na uaminifu wa kisiasa kuhusu mahitaji, unyonyaji wa rasilimali (ambao mwisho unamaanisha pesa), kutoka mahali zinakotengenezwa hadi kule kunakopendelewa kisiasa, uharibifu wa serikali kwa mbinu ya ufisadi au kwa wazi zaidi – wizi.

Pesa zinahusishwa na uovu hasa zinapochukua umuhimu zaidi. Bila pesa, shughuli za serikali haziwezi kuendelea bila vikwazo, lakini inataka uangalifu wa hali ya juu kwa

ambavyo ni rahisi kwa mali ya serikali kutumiwa vibaya. Rasilmali za kifedha zinazopatikana na serikali zinatokana na njia za aina tatu; yaani, kutoza ushuru na kodi nyinginezo, mikopo ya nchini na mikopo ya nje na msaada. *Nchini Kenya njia nyingine za kupata fedha ambazo hazifikii serikali moja wa moja ni "harambee".*

Hivi sasa hakuna, lakini pangekuwa na masharti yanayowataka wale walio na wajibu wa kuchangisha na kutumia pesa za umma ili kuunda maono yanayofaa, dhima, malengo, mikakati, mipango na shughuli zitakazohakikisha mapato ya hali ya juu na mipango ya matumizi. Hakuna masharti ya utekelezaji wa mipango mwafaka na uchunguzi, tathmini na kueleza yaliyotokea, kwa hali itakayosababisha thamani ya pesa kama sehemu mojawapo ya utekelezaji wa kandarasi ya kijamii kati ya watawala na watawaliwa. Masharti kwa hakika yanahusu kuhakikisha kwamba pesa zimekusanywa na kutumiwa na wale waliona mamlaka ya kufanya hivyo, lakini kuna upungufu wa juhudi halisi za kudhibiti hekima ya uamuzi wa kifedha.

Kwa jumla wajibu wa Bunge ni mchache. Kwa sababu ya shinikizo ya wakati, kwa upande mmoja ni kwa ajili ya kutaka utaalamu kuhusu wabunge kibinafsi na upande mwingine kama matokeo ya ukosefu wa mfumo mzuri wa kamati. Kuna shaka pia kuhusu nafasi ya na Bunge ya kugeuza sehemu katika bajeti, na ikiwa matumizi kutoka hazina nyingine kando na Mfuko Mkuu wa Fedha za Serikali yanapitia katika utaratibu wa ukaguzi wa mahesabu. Pia kuna desturi ya mfumo wa Westminister, ambao ni kuhusisha Bunge kiasi kidogo katika mfumo, hasa katika kiwango cha kupanga bajeti. Mwisho, ambapo serikali inaweza bungeni, mjadala utapamba moto kuhusu uadilifu wa chama unavyotekelezwa, kama itakavyokuwa kuhusu masuala ya bajeti; haya ni matokeo mengine ya mfumo wa Bunge.

**(ii) Kugawa Rasimali ya Fedha za Umma**

Rasilmali za fedha za serikali zilizokusanywa kutoka asili tofauti zahitaji kugawanywa katika msingi wa usawazishaji kati ya utendakazi bora na usawa. Wajibu wa sekta ya umma pia ni kuunda mazingira yanayofaa ya kuendeleza uwekaji akiba, kuzalisha

uwekezaji na kutoa huduma na sekta ya kibinafsi. Hili ni jambo linalohitaji uboreshaji na kuendeleza mawasiliano halisi na muundo msingi wa habari, utoaji wa baadhi ya huduma muhimu hauwezi kufanywa na sekta ya kibinafsi, na kwa jumla kuchukua hatua zitakazopunguza kaida ya kutafuta malipo ya kodi ya nyumba na ambao unaongeza utendajikazi bora katika uchumi.

**(iii) Ulinzi na Kutoa Fedha za Umma**

Mara tu pesa zinapopatikana kwa matumizi ya serikali ni muhimu kwamba ziwekwe kwa usalama na kutumiwa tu kwa madhumuni ambayo pesa hizo zimechangishwa kama sheria inavyofafanua. Mapato mengi ya serikali huwekwa kwenye Mfuko Mkuu wa Fedha za Serikali ambapo hazitatolewa isipokuwa kwa idhini fulani. Serikali pia imepewa uwezo na Katiba iliyopo kuunda Mfuko wa Fedha za Dharura na fedha nyinginezo, kama inavyoona umuhimu, kwa kurudisha mapato kutoka mahali fulani. Ni muhimu kuhakikisha kwamba si fedha nyingi zinazotengenezwa kwa sababu, hiyo yaweza kuleta kuchanganyikiwa katika utekelezaji wa kazi ya ulinzi. Lazima pia kuwe na jozi ya masharti ya kifedha yatakayohakikisha usalama wa uwekaji wa fedha, utoaji ufaao, na matumizi ya pesa zilizozalishwa hivyo.

**(iv) Matumizi ya Fedha za Umma**

Matumizi ya mapato yatekelezwe vyema na kwa njia ifaayo, kwa uangalifu mkubwa kwa madhumuni ya kuendeleza matumizi kama hayo kwa Taifa. Mipango ya mikakati makinifu yatakikana kuhakikisha kuwa malengo haya yanafikiwa. Kwa zaidi, masharti magumu ya ulinzi wa utoaji wa Fedha za Umma yangepunguza na hatimaye kunyonga mipango ya matumizi ya serikali na hivyo kuwa kisababisho cha kutofanya vyema. Ingawaje masharti rahisi yangeruhusu matumizi mabaya ya fedha. Kwa hivyo ni muhimu kupata usawazishi kati ya pande hizi mbili.

**(v) Kukadiria thamani ya rasilmali na kukagua mahesabu**

Ni muhimu kwamba kiwango na hali ya rasilmali za fedha za Taifa vijulikane kila wakati ili kurahisisha upangaji makinifu na kufanya uamuzi. Hili linahitaji kuwepo kwa na matumizi ya mifumo ifaayo ya kutathimini na kukadiria chanzo cha rasilmali ya fedha.

Utekelezaji wa wajibu uliotangulia kuelezwa hapo juu unahitaji udhibiti na ukaguzi wa mahesabu ili kuhakikisha kwamba umuhimu wa uadilifu, uwajibikaji wa juhudi umetekelezwa na kwamba utendakazi bora na ufanisi wa kiuchumi umepatikana. Jambo hili lahitaji mipango ya fedha na ukaguzi wa mahesabu ufaayo kwa ajili ya kuhakikisha uzuiyaji wa utovu wa nidhamu na kupata wasaa mzuri wa kusahihisha makosa yoyote ambayo yangetendeka.

**(vi) Ukaguzi wa Matumizi ya Fedha na Taarifa**

Ukaguzi wa matumizi ya mahesabu na kutoa taarifa husaidia ukaguzi kufanywa ili kuhakikisha kwamba rasimali ya umma yatumiwa kama ilivyoidhinishwa na Bunge. Yanahusu shughuli zifuatazo:-

(a) Kuamua kile ambacho lazima kikaguliwe kifedha, vipi, na nani na kuanzisha utaratibu wa ukaguzi wa mahesabu.
(b) Utaratibu wa ukaguzi wa mahesabu.
(c) Upeo wa kukagua mahesabu (Kwa mfano,ikiwa unashughulikia utendakazi mwema na ufanisi).

Swala muhimu kuhusu lile litakalotendewa taarifa za chombo cha ukaguzi mahesabu, taarifa hizo ziende kwa nani, zitashughulikiwa na nani, na nani atakayezifanyia kazi ni nyeti na muhimu. Kwa hivyo, kuna uhitaji wa ukaguzi wa mahesabu yaliyotumiwa na utaratibu wa kutoa taarifa kuhusu fedha za umma.

**(vii) Utaratibu wa Bajeti**

Makadirio ya mapato na matumizi kawaida huwasilishwa bungeni kupitia kwa hotuba ya bajeti ya mwaka na Sheria ya Fedha inayofuatana nayo. Utaratibu wa kutayarisha bajeti kwa kawaida umezingirwa na usiri. Mapendekezo ya Waziri hutolewa tu kwenye hotuba ya bajeti. Baadhi ya vikundi vya ushawishi hutoa maoni yao kwa wizara na huweza kupewa nafasi ya kujadili mapendekezo yao. Lakini hapana kikao cha kufafanua bajeti wazi kwa kushiriki kwa vikundi mbali mbali vinavyohusika. Kiasi fulani cha siri ni cha halali – lakini pangekuwa na nafasi ya changizo ya umma.

Wakati bajeti inapowasilishwa Bungeni kawaida kabla ama tarehe 30, Juni. Kila mwaka Bunge hujigeuza kuwa kamati ya Bunge lote (kamati ya njia na mbinu) na hutoa utaratibu kwa Bajeti kwa siku nyingi ya zile saba. Mjadala huu ni wa jumla kuhusu sera ambayo Bajeti inatarajiwa kuungwa mkono na Bajeti. Siku ile ya Bajeti, bunge hupitisha azimio linalothibitisha mabadiliko ya ushuru na hivyo kuyafanya mageuko haya yatekelezwe mara moja ili kuepuka kutotoa kodi na ghasia wakati watu wanapojaribu kuhepa matokeo ya kodi mpya, au kukataa kuendeleza shughuli hadi upunguzaji uanze kutekelezwa. Azimio hili hupewa msukumo wa mwisho wa kisheria wakati Sheria ya Fedha inapokuwa imepitishwa. Mwisho wa mjadala huu, Bunge hupitisha pendekezo linaloidhinisha matumizi ya nusu ya matumzi yaliyokadiriwa. Siku ishirini hutengwa kwa tafakari makinifu ya Bajeti na Kamati nyingine ya Bunge lote inayoitwa Kamati ya Ugavi. Haya yote hukamilishwa kufika tarehe Oktoba 31, na siku ya mwisho kura zote lazima zipigwe. Baadhi yake yatakuwa hayajajadiliwa kwa sababu ya matumizi ya kichinjio kinachosaidia mjadala kufupishwa. Inawezekana kwa Bunge kubadilisha sehemu ndogo maalum za matumizi, ingawa hili hutokea nadra.

Baada ya kuidhinishwa, utoaji wote wa fedha kutoka kwenye Mfuko Mkuu wa Fedha za serikali lazima udhinishwe na Mdhibiti na Mkaguzi wa Mahesabu Mkuu (CAG).

Mwisho wa mwaka wa fedha, afisi ya Hazina hutayarisha mahesabu. Hili hufanyika kufikia mwisho wa Oktoba. Mdhibiti na Mkaguzi Mahesabu Mkuu ndio wanaokagua na

kufikia mwisho wa miezi saba (ambayo yaweza kuongezwa na Baraza la Wabunge) hupeleka taarifa kwa Waziri ambaye huiwasilisha katika Baraza la Wabunge. Kwa hakika, kwa miaka mingi, ni kama miaka miwili kabla ya taarifa kufika Bungeni. Taarifa ndipo hujadiliwa na kamati ya Mahesabu ya Umma, inayodhihirisha masuala muhimu. Kamati hutoa taarifa Bungeni kwa jumla na afisi ya Hazina hutakikana kueleza hatua iliyochukuwa kuhusu mapendekezo ya Kamati ya Uhasibu ya Bunge (PAC). Kwa hakika ingawa maoni ya Kamati ya Uhasibu ya Bunge (PAC), mara nyingi husababisha hamasa mara moja kwenye magazeti, hili ni kwa wakati mchache na dhuluma huendelea bila kurekebishwa. Kuna utaratibu unaolingana kwa Muungano wa Serikali unaohusisha Mkaguzi wa Mahesabu Mkuu wa Muungano wa Serikali na Kamati ya Uwekezaji wa Umma.

**(viii) Utozaji Ushuru**

Mapato hukusanywa kwa madhumuni ya kufidia matumizi ya kila siku ya serikali na ya maendeleo. Kila mara kuna muelekeo wa kujaribu kukusanya mapato mengi kama inavyowezekana. Jambo hili limeleta dai la kwamba nchi imetozwa ushuru sana. Gharama ya kukusanya mapato yahusu gharama ya moja kwa moja ya kufadhili wafanyikazi na gharama za shughuli za utekelezaji na pamoja na haya, gharama isiyodhahiri ya kuitoa nje sekta ya kibinafsi kwa maana kwamba mapato ya ushuru hayapatikani kwa uwekezaji wa kibinafsi. Kwa hivyo kuna uhitaji wa kupata usawazishi baina ya gharama hizi na mapato yalivyokusanywa ama kuzidi kiwango fulani, ukusanyaji wa mapato ya ushuru ya ziada huwa si wa ufanisi na huharibu uchumi. Hii ni changamoto kwa mamlaka ya ushuru, kutafuta na kuupata usawazisho huo.

**(ix) Deni la Umma**

Uhitaji wa mikopo ya nje hutoka kihalisia kwa madhumuni ya kugharimia matumizi ya maendeleo, ambayo hayawezi kugharimiwa kutokana na utozaji ushuru, na mapato mengine ya Serikali. Wakati mwingine, mikopo ya nje, huweza kutumiwa kugharimia shughuli za awamu fupi kama vile mikopo ya IMF.

Matumizi ya ufadhili kutoka nje kwa kweli yangesaidia katika kuhakikisha kwamba viwango vya ushuru hiviongezeki sana na kwamba udhibiti wa kiwango cha kutoza ushuru haupatikani katika hali ya kutofaidi mipango ya Serikali. Kusipokuwa na uombaji kutoka nje na kwa viwango vilivyodhibitiwa vya utozaji ushuru, njia nyingine inayoweza kutumiwa na serikali ingekuwa mpango ya kupunguza matumizi, ili kufikia bajeti iliyosawazika. Uombaji wa humu nchini, ungeziba pengo la ufadhili. Katika kuomba, ambapo kuwa hakika ni fedha zilizokusanywa kwa njia hya kutoa. Hati za madai ya fedha na Hati za Benki, zaweza pia kutumiwa kudhibiti. Kiwango cha uchapishaji wa pesa kupitia shughuli za masoko ya wazi – mauzo na ununuzi wa udhamini wa serikali – na hivyo kudhibiti upandaji wa gharama za maisha, kwa urahisi ambao pesa zaweza kukusanywa kwa njia hii ukusanyaji ambao wahitaji kudhibitiwa ili kuhakikisha kwamba ni viwango kama vile vya madeni ya nchi tu kama yanavyotakikana kihalisi, kwa chanzo cha kihalali hukusanywa na masharti ya deni kama hilo hayadhuru utekelezaji wa ufanisi wa kiuchumi.

### (x) Benki Kuu

Benki kuu ya Kenya ni asasi muhimu zaidi nchini, lakini haina nafasi katika Katiba. Hili ni kosa linalohitaji kusahihishwa. Sheria ya Benki Kuu ya Kenya imeanzisha Benki na pesa za Kenya. Sheria inaeleza kanuni maalum za benki kuwa:

(a) Kudhibiti utoaji wa noti na sarafu;
(b) Kusaidia katika uundaji na uendelezaji wa mfumo wa pesa, ukopaji na kuweka hazina katika benki, uwe wa kuvutia kwa maendeleo ya kiuchumi ya nchi na uthabiti wa pesa nje;
(c) Kutenda kazi kama mwenye benki na mshauri wa kifedha kwa Serikali.

### (xi) Kupanga Kustaafu

Waliostaafu na malipo ya uzeeni hawabahatiki kwa hali zinazogeuka za kiuchumi, kwa ambavyo haki zao za malipo hazibadiliki na nyakati. Kinyume cha mishahara, malipo ya uzeeni hayana ongezeko la kusaidia gharama za maisha zinazoongezeka.

Watu wengi hustaafu na kupata malipo madogo ya uzeeni ambayo yenyewe hayawezi kukidhi mahitaji ya watu kama hao na familia zao. Isipokuwa mtu anufaike kutokana na changizo kubwa wakati anapofanya kazi na mfanyi kazi pia awekeze kwa busara katika kipindi hicho, mtu huathiriwa vibaya na kiasi kidogo cha malipo ya uzeeni, ambayo yanapunguzwa zaidi na athari ya kupanda kwa gharama za maisha. Isipokuwa mtu apate nafasi ya kuajiriwa baada ya kustaafu, hawawezi kukidhi mahitaji yao bila kupunguza matumizi yao kila siku. Hali hii husababisha kutoinunulia kwa uwezo wa wafanyikazi, huwafanya waajiriwa kupata hali ya hatari ya kiakili na kuhatarisha familia zao kiuchumi. Hali hii huzidishwa na kustaafu mapema na kuondolewa kazini ambako hakuandamwi na mpango ufaao wa kuwasaidia.

Hata hivyo, inatambuliwa kwamba ili malipo ya uzeeni yahusishe kuongezeka, lazima pia kuzingatia mzigo wa ziada wa kifedha utakochukuliwa na wafanyikazi na hasa kuhusu wafanyikazi wa umma. Ikiwa mali hiyo itatolewa kutoka kwenye Mfuko Mkuu wa Fedha za Serikali. Ingawaje usimamizi ufaao na uadilifu wa uwekezaji wa malipo ya uzeeni na fedha za matumizi, fedha kama hizo zingeonekana kiasi kwa muda fulani, ili kufanya nafasi za kuongeza malipo ya uzeeni kwa waliostaafu. Huu ni mpango bora zaidi kuliko ule wa kutafuta fedha kutoka kwa Mfuko Mkuu wa Fedha za Serikali ambao tayari umegandamizwa. Waajiri pia wanatakikana kutoa mafunzo kwa waajiriwa wao kuhusu upangaji wa kustaafu ili waajiriwa kama hao waweze kufanya mipango muhimu ya uwekezaji (kwa mfano uwekezaji) wanapokuwa bado wamo kazini, ambayo itazalisha fedha za uwekezaji wa kibinafsi wanapostaafu.

### (xii) Masuala ya Hazina ya Serikali na Fedha

Masuala yanayohusu Hazina ya Serikali na fedha za Taifa ni ya muhimu zaidi katika utekelezaji wa kandarasi ya kijamii kati ya magavana na wanaotawaliwa. Huamua kiasi

ambacho serikali ya wakati huo hutoa nafasi na mazingira yanayosaidia ukusanyaji wa rasilimali ili kukidhi mahitaji ya kimsingi ya wananchi na kuboresha maslahi yao. Mambo muhimu kama hayo yanataka kutafakariwa kwa makini sana ili yashughulikiwe kwa ujuzi mkubwa uwezekanavyo ili kutekeleza majukumu yaliyowekewa serikali kwenye kandarasi ya kijamii. Hili linaweza kufanikishwa kwa kutoa uwajibikaji kwa kundi huria lililopewa uwezo mwingi chenye wataalamu wenye tajriba katika umbo la tume ya mambo ya kiuchumi na kifedha iliyokuwa kwenye Katiba ili kuwezesha kuanza kwa chombo kama hicho na kufafanua uwezo wake wazi wazi na wajibu. Tume kama hiyo ingechunguza na kupima wakati wote umashuhuri wa muundo na utekelezaji wa sera ya Hazina ya Serikali na fedha na kusimamia kutathmini na kushauri kuhusu uwezo wa sera kama hiyo. Miaka mitano iliyopita, serikali ilianzisha Tume ya Upangaji ambayo haikuundika. Kuzingatia masuala yaliyotolewa mara kwa mara imependekezwa kwamba wakati umefika wa kuanzisha Tume kama hiyo.

### 15.2.2 <u>Fedha na Mapato katika Katiba</u>

Katiba iliyopo katika sehemu 48, inakataza Baraza la Wabunge kuendelea na mswada wa sheria au pendekezo kuhusu za utozaji ushuru, kugeuzwa kwa, ama utoaji wa pesa kutoka kwa Mfuko Mkuu wa Fedha za Serikali au aina ya deni au kusamehewa deni la Serikali ya Kenya isipokuwa kwa pendekezo la Rais, akiungwa mkono na Waziri sehemu ya saba ya Katiba yafafanua masharti ya kuanzisha kwa na matumizi ya Mfuko Mkuu wa Fedha ya Serikali, kuanzisha kwa mfuko wa fedha za dharura, usimamizi wa deni la umma la Serikali ya Kenya na afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu.

Marsharti haya yameelezwa zaidi katika sheria maalum miongoni mwake kuwa ni:

- Sheria ya Wizara ya Fedha na Ukaguzi wa Mahesabu (Sura 412)
- Sheria ya mamlaka ya mapato ya Kenya (Sura 419)
- Sheria ya Mlipaji Mshahara wa Jumla (Sura 413)
- Sheria ya Kandarasi za Serikali (Sura 25) na

- Sheria ya Benki Kuu (Sura 491).

### 15.2.3 Hazina na mapato katika Katiba Nyingine

Masharti kuhusu udhibiti wa fedha na mapato ni ya kiwango sawa katika Katiba zote, ya zamani au mpya. Wajibu kwa sera ya matumizi ya serikali, ushuru, idhini ya kutenga fedha na usimamizi wa uangalifu wa mapato ya umma mara nyingi hugawanywa baina ya viongozi na Bunge. Kanuni za jumla ni kwamba, licha ya kuwa wajibu wa kuinua mapato na kuingia kwenye Uchaguzi wa matumizi katika Serikali Kuu, hili linaweza kutekelezwa tu na, au kuingilia kwa bunge. Baadhi ya Katiba, kama vile ya Afrika Kusini, pia imebuni tume kushauri Bunge na/au Halmashauri Kuu juu ya maswala ya kifedha na matumizi ya Serikali.

### 15.2.4 Waliyosema wananchi

Wananchi waliozungumza juu ya fedha za umma na mapato walihusika zaidi na masuala yafuatayo:

(i) Kuuweka thabiti uhuru na uwezo wa Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu;
(ii) Udhibiti bora wa matumizi ya Mapato ya Serikali, kutokana na bajeti.;
(iii) Uwazi zaidi wa utaratibu;
(iv) Kushirikisha zaidi Umma na Bunge katika kutayarisha na kuidhinisha bajeti;
(v) Uwazi zaidi katika kusamehewa kodi;
(vi) Maafisa wakubwa wa Mamlaka ya Mapato ya Kenya wateuliwe na Bunge;
(vii) Kuanzishwa kwa Afisi ya Bajeti ya bunge;
(viii) Kutenganisha majukumu haya mawili ya udhibiti wa Bajeti na ukaguzi wa mahesabu;
(ix) Kuweka vikwazo katika udhibiti wa Bunge wa kukopa kwa serikali;
(x) Katiba ijumlishe kanuni za utozaji ushuru kwa uadilifu na bila mapendeleo;

(xi) Afisi ya Gavana na Benki Kuu ya Serikali ianzishwe na Katiba na ipewe usalama wa awamu na uhuru wa utekelezaji;

(xii) Kufanya utaratibu wa masharti ya kifedha; kuyakusanya mahali pamoja;

(xiii) Pesa za Taifa ziwe na alama ya kitaifa na si picha ya mtu binafsi;

(xiv) Mapato yapasa kugawanywa kati ya Serikali Kuu na viwango vya chini kwa asilimia zilizokati ya kumi hadi ishirini (10-20%) .

### 15.2.5 Uchanganuzi

Wananchi walifahamu wazi kwamba asili ya kimsingi ya mapato ya serikali ilikuwa ni utozaji ushuru. Lakini pia walikuwa wanafahamu kwamba viwango vilivyopo sasa vya utozaji ushuru si tu kwamba viko juu, lakini pia, ni vya kuadhibu. Tena ukweli ni kwamba wateule waliosoma kisiasa huepuka kodi kwa madharau bila kuadhibiwa ni swala linalojulikana na wengi.

Katika hali hii wananchi walitaka serikali yao ihakikishe kwamba raia wote wanalipa kodi zote wanazodaiwa na Serikali, licha ya vyeo vyao katika jamii. Kulikuwa na kilio kwa Serikali kubadilisha viwango vya ushuru na kuboresha mfumo ya ukusanyaji wa ushuru.

Kuhusu suala la usawa katika ugawanyaji wa mali ya kitaifa, Serikali iliombwa igawe marupurupu kutokana na rasilmali (pamoja na kodi) katika eneo maalum kati ya wananchi wa eneo hilo na Serikali Kuu. Wengi ya Wakenya wanataka Serikali ichukue kiasi cha asilimia ishirini (20%) ya marupurupu na kuacha aslimia thamanini (80%) kwa maendeleo katika eneo ambalo mali hiyo imepatikana.

Aidha, wananchi walikosoa ukopaji wa serikali na, hasa, kuhusu ulimbikizaji wa madeni makubwa ya nje na ndani kama ilivyo sasa. Serikali ilihimiza, lazima iendelee kujitosheleza kwa matumizi ya kipimo kinachowezekana. Uhitaji wa juhudi za Bunge kuhusu suala hili kwa hivyo, ulisisitizwa.

### 15.2.6 Mapendekezo

Kwa hivyo Tume inapendekeza;

**(i) Kuhusu kutayarisha bajeti kwamba:**

(a) Utaratibu wa kutayarisha bajeti uruhusu ushirikiano wa wote wanaohusika, na kuzingatia uhitaji wa kitendo kisawazishi kulingana na vikundi vya watu wasiobahatika katika uchumi.

(b) Yapasa kuwe na kauli ya kanuni kama msingi ambao kwao, uwasilishi wa bajeti umefanywa ili kuwasaidia wanaohusika kufurahia matarajio na malengo ya mapendekezo ya bajeti na vikwazo vitakavyokutwa katika utekelezaji wa mapendekezo kama hayo.

(c) Katiba itoe maelezo ya uundaji wa Kamati ya Utayarishaji Bajeti ya Bunge itakayofanya kazi na Afisi ya Hazina ya Serikali, katika uundaji wa Sheria ya Mwaka ya Fedha na agizo la kusimamia maendeleo ya Bajeti ya Kitaifa, kuzingatia uhitaji wa utendaji kazi bora na usawa kama unavyomulikwa na uwezo wa utendaji na mahitaji ya makundi tofauti na maeneo nchini.

(d) Katiba yapasa kutoa afisi ya Bajeti ya bunge katika aina ya afisi Kuu ya wafanyikazi itakayotao usaidizi wa kitaalamu kwa Kamati ya Bajeti juu ya masuala yanayohusu udhibiti wa fedha na ukaguzi na mahesabu.

(e) Afisi ya Bajeti ipewe uwezo wa utendakazi kwa utafiti huria, watafiti wakutosha na kiasi cha uhuru wa utendaji kwa matumizi ya wataalam ili iweze kusaidia vyema kamati ya Bajeti ya Bunge.

- Kujibu maswali maalumu ya wabunge kuhusu matumizi ya umma;
- Kutafuta na kuratibu maoni ya umma na wataalam kuhusu maswala ya utayarishaji wa bajeti;
- Kutoa tathmini mbali mbali za mapendekezo ya bajeti;
- Kusimamia marekebisho katika bajeti;

- Kupendekeza kwako kwa utaratibu unaohakikisha usawazishaji wa bajeti;
- Kutoa uchunguzi wa kiufundi juu ya bajeti; na
- Kutoa huduma ya uchambuzi saidizi kwa kamati za Bunge zinazoshughulikia sekta mbalimbali za uchumi.

(f) Uzahishaji wote wa mapato, kushikilia fedha na vitengo vya matumizi ya serikali vitatayarisha mpango wa kimsingi wa mikakati ya miaka mitatu, utakaokuwa msingi wa, na kuambatana na matayarisho ya makadirio ya mwaka ya mapato na matumizi.

(g) Bunge litajadili mpango wa mikakati pamoja na bajeti na kupendekeza uboreshaji kulingana na maoni yake, na likiwa halikutosheka na mpango wa mikakati wa kitengo fulani, litoe maagizo kwamba marekebisho yafanywe na yawasilishwe tena mnamo kipindi cha mwezi mmoja wa kalenda.

(h) Bunge pia lingemtaka waziri anayehusika na mpango wa fedha kwa wakati huu atayarishe mipango mingine ya awamu ndefu kama atakavyoona inafaa.

**(ii) Kuhusu afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu kwamba:**

(a) Rais kwa mujibu wa mapendekezo kutoka kwa Tume inayofaa na kuundwa na Katiba, atateua Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu kuambatana na idhini ya Baraza la Wabunge.

(b) Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu ipewe ulinzi wa awamu na utiwe kwenye Katiba na kuwe na matokeo magumu ya kuathiri awamu kama hiyo.

(c) Majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu yaliyofafanuliwa katika sheria ya Wizara ya Fedha na Ukaguzi wa Mahesabu Sheria (Sura 412) sehemu 7 (1-2) yatiwe kwenye Katiba.

(d) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu yapasa awe Mhasibu wa Umma Kenya aliyefuzu miongoni mwa sifa nyingine zitakazofafanuliwa na chombo cha uteuzi.

(e) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu wasiwe wamefika umri wa zaidi ya miaka sitini wakati wa uteuzi wa awali na wasitekeleze majukumu ya afisi ile wakiwa zaidi ya miaka sabini na tano.

(f) Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu isimamiwe na maafisa wawili huru kama ifuatavyo:

- Mdhibiti Bajeti asimamie utekelezaji wa bajeti kama ilivyoidhinishwa na Bunge kwa kuhakikisha kuwa pesa zinatumiwa kulingana na mpango na kutoa mahesabu ya matumizi halisi na matumizi yaliyomo kwenye bajeti kimfululizo.
- Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu, akague haraka matumizi na mapato ya idara zote za Serikali na mashirika ya kitaifa na kutoa taarifa Bungeni kwa wakati ufaao juu ya upeo wa uadilifu katika masharti ya bajeti na taratibu na ufanisi.

(g) Bunge lisiende likizoni kabla ya kujadili taarifa na ikiwa limekwenda likizoni wakati wa kuwasilishwa kwa taarifa na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu lazima Bunge liitwe mara moja lirudi kujadili taarifa hiyo.

(h) Miezi sita baada ya kuwasilishwa kwa taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu, Bunge litajadili na kuchukua hatua zifaazo kutoka hapo.

(i) Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu lazima awasilishe taarifa yake moja kwa moja Bungeni na nakala ipewe waziri anayewajibika na Fedha kwa wakati huu.

(j) Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu apaswa kuwasilisha taarifa yake ya robo mwaka Bungeni kufuatia mfululizo wa kila taarafa ya robo mwaka inayofuata utaratibu wa wakati.

**(iii) Kuhusu utozaji ushuru kwamba:**

(a) Kuwe na msingi wa wazi wa kuweka kwa kila mojawapo ya aina za kodi na jozi ya kanuni za jumla zitakazofuatilia katika utaratibu ambao yapasa ujumlishe miongoni mwa mengine:

- Kusiwe na utozaji kodi bila uwakilishi.
- Utozaji kodi upate usawazishi kati ya mahitaji ya wananchi na uwezo wao wa kulipa kodi, kadri inavyowezekana.
- Kila juhudi ifanywe kuhakikisha kwamba asasi moja au mtu binafsi asilemewe na aina nyingi za kodi iwe kwamba mzigo wa kodi kwa jumla hauwezekani.
- Kanuni ya ulipaji kodi kama jukumu la raia ifanywe kuzoweleka kwenye fikira za walipaji kodi.
- Usawazishi ufaao upatikane kati ya huduma zinazotakikana kutolewa ni mamlaka ya wilaya na kodi zao na misingi mingine ya mapato.
- Bunge lifulilize kuamua visa vilivyo na haki ya kupata msamaha wa kutolipa kodi na msamaha kama huu tu ndio ambao ungeruhusiwa.
- Kila juhudi ifanyiwe kuendeleza uwekezaji kama njia bora zaidi ya kuendeleza chanzo cha mapato ya kodi.

(b) Kauli iliyorahisishwa kuhusu utozaji wa ushuru na ukusanyaji kodi, kuonyesha upeo wa uwezo uliopewa vyombo tofauti vya serikali ingetolewa.

(c) Uwezo wa kulazimisha au kugeuza kodi ungepewa Bunge moja kwa moja na lingeanzisha:

- Mamlaka au chombo kitakachochukua wadhifa huu, lakini bunge lihifadhi udhibiti juu ya utendajikazi wao.

- Mahakama maalum ya kodi itakayoshughulikia masuala yote yanayohusu utozaji kodi, msamaha wa kutolipa kodi ama kugeuka kwa kodi kwa sheira ya Bunge[tazama Uganda 152 (3)].

**(iv) Kuhusu deni la Umma kuwa :**

a) Inabidi sehemu ya 103 irekebishwe ili iagize kuwa madeni yote ya umma yataidhinishwa na Bunge, kabla hayajachukuliwa na katika muktadha huu, Bunge litatoa kanuni za kufaa ambazo kwazo madeni yanaweza kufikiriwa (Madeni ya nje na ya ndani ). Tazama Ghana 181 (1 – 7 ) )
b) Ni lazima masharti na kanuni za kukopa ziwasilishwe Bungeni ili ziidhinishwe katika muda wa siku thelathini kabla ya kandarasi kutekelezwa.
c) Kwa kutumia kura ya wengi, Bunge liruhusu serikali kufanya makubaliano ya kukopesha pesa kutoka katika mfuko wo wote wa umma au kuiweka nchi katika hali ya kuwa na deni lo lote iwe la nje au la ndani.
d) Kiwango cha juu zaidi cha jumla ya mkopo wa Serikali kiwekwe cha asilmia thelathini (30%) cha Mapato ya Jumla ya Serikali (GDP) ya Mwaka wa Fedha mara tu kabla ya mwaka ambamo mapendekezo ya bajeti yalifanywa.

**(v) Kuhusu Benki Kuu kwamba Kanuni ziwekwe katika Katiba kuhusu** :

(a) Uanzishaji wa Benki Kuu ya Kenya kama asasi huria ambayo itakuwa Mamlaka ya Juu ya Fedha za Jamhuri.
(b) Uanzishaji wa afisi ya Gavana wa Benki Kuu ya Kenya ambaye atateuliwa na Rais kutokana na watu wenye sifa katika masomo ya uchumu, fedha na/au uhasibu. Uteuzi huu utategemea idhini ya Bunge.

(c) Mtu anayeteuliwa kuwa Gavana wa Benki Kuu atahudumu kwa muda wa awamu mbili za miaka mitano kila awamu , na katika wakati huo, hatatolewa afisini isipokuwa kwa idhini ya Bunge ikiwa hataweza kutekeleza majukumu yake, kwa hatia mbaya au kwa kutokuwa na umilisi.

(d) Malengo Makuu ya Benki Kuu yatakuwa :
Kulinda thamani ya pesa

- Kulinda thamani ya pesa kwa mujibu wa maendeleo ya nchi ya kiuchumi ambayo ni sawazishi na endelevu;
- Kutoa pesa za noti na sarafu;
- Kuwa mwanabenki na mshauri wa kifedha wa Serikali;
- Kutekeleza sera ya kifedha ya Serikali kwa njia inayofaa kanuni za kisheria zifaazo; na
- Kuhimiza na kudumisha maendeleo ya kiuchumi na matumizi ya kufaa ya rasilmali.

(a) Bunge litaweka sheria ambazo zitatoa misingi ya jinsi ambavyo Benki hii itaratibishwa na kusimamiwa.

**(vi) Kuhusu Mipango ya Kustaafu kuwa: -**

(a) Mamlaka ya Marupurupu ya Kustaafu yakitwe katika Katiba yakitoa kanuni kwamba:

(b) Bunge liweke Mamlaka ya Marupurupu yenye maagizo ya kukadiria na kusimamia uwekezaji wa malipo ya uzeeni na mfuko maalum wa akiba ya uzeeni kwa manufaa ya wafanyikazi ambao kwa niaba yao fedha hizo zimewekezwa, kwa njia inayofuata taratibu ya kanuni ambazo zimeruhusiwa kwa uwekezaji wa amana na zinazoweka vizuizi vya kufaa endapo kutakuwa na ukiukaji.

(c) Fedha za aina hii zitatolewa ifaavyo kila mwezi kwa mfanyikazi ambaye alinuiwa kufaidi kutokana na uwekezaji huo uliofanywa kwa wakati atakapostaafu. Wafanyikazi watatarajiwa kutoa mafunzo ya

msingi kuhusu mipango ya kustaafu kadri itakavyopendekezwa na sheria inayofaa.

**(vii) Kuhusu masuala ya Hazina ya Serikali na Pesa kuwa** :

(a) Kuanzishwe Tume ya Uchumi na Masuala ya Fedha za Serikali iliyo na Mwenyekiti, Mkurugenzi Mkuu, Naibu wa Mkurugenzi Mkuu na wanachama wengine watatu jinsi watakavyoteuliwa na Rais kufuata idhini ya Baraza la Wabunge.

(b) Litakuwa ni jukumu la Tume hii kupendekezea Bunge :

(c) vigezo na kanuni za uundaji , utekelezaji, usimamizi na uhakiki wa sera na mbinu ya kukuza uzalishaji na matumizi ya mapato yanayotokana na kodi na aina nyingine za mapato, upataji wa madeni ya ndani na ya nje, uuzaji wa amali ya Serikali na asasi na masuala mengine yanayohusiana na haya.

(d) mbinu za kiubunifu na njia za kuzalisha mapato zaidi kwa fedha za Serikali pamoja na hatua zinazohitajika kwa uzalishaji wa mapato ya Serikali za wilaya na viwango vingine vya Serikali iliyosambazwa.

(e) hatua zinazohitajika kukuza uwekezaji wa nyumbani na wa kigeni ili kudumisha msingi wa pato la Taifa.

(f) hatua zinazohitajika katika kuleta usawa katika uzalishaji na matumizi ya mapato ikiwemo hatua zinazohitajika ili kufikia kiwango kinachotamanika cha kitendo kisawazishi kwa mujibu wa vikundi visivyobahatika katika jamii na maeneo ya nchi.

(g) Njia na mbinu za huduma na aina nyingine za utumishi katika sekta ya uchumi isiyo rasmi.

(h) Njia na mbinu za uwazi na uwajibikaji za kupata na kukuza amali ya Serikali, mali na asasi na kwa kubinafsisha na kutumia huduma za Serikali kibiashara.

(i) Njia na mbinu za kukuza uhusiano wa kudumu baina ya utozaji ushuru na uwakilishi, na utozaji ushuru na utoaji wa huduma.

(j) Mifumo ya kutathmini utendaji wa asasi zote ambazo zimepewa majukumu ya kifedha.

(k) Bunge linaweza kuweka sheria za kufaa ambazo zitawezesha utekelezaji wa Tume.

**(viii) Kuhusu Mipango ya Maendeleo kuwa :**

(a) uzalishaji wote wa mapato, vitengo vya Serikali vya kuweka na kutumia fedha vitatayarisha mpango wa mikakati inayofululiza kwa miaka mitatu ambao utakuwa msingi wa, na kuambatana na utayarishaji wa makadirio ya kila mwaka ya mapato na matumizi.

(b) Bunge litajadili mpango huu wa mkakati pamoja na bajeti na kupendekeza marekebisho kadri litakavyoona yanahitaji kufanywa ikiwa halitaridhika na mpango wa mkakati wa kitengo maalum na kuagiza kwamba marekebisho hayo yafanywe katika muda wa mwezi mmoja wa kalenda.

(c) Bunge linaweza pia kumhitaji waziri ambaye wakati huo anahusika na fedha na mipango kutayarisha mpango mwingine wa muda mrefu ambao anaweza kuona uanfaa.

**(ix) Kuhusu Mfuko Mkuu wa Fedha za Serikali na Mfuko Mkuu wa Fedha za Dharura kuwa:**

(a) Katiba ingelitaka Bunge liidhinishe kutolewa kwa fedha katika Mfuko Mkuu wa Fedha za Serikali na kuagiza ya jinsi zitakavyotumiwa kwa kutekeleza utoaji huo.

(b) makadirio ya mwaka (sehemu 100) yaambatana na mikakati ya mipango ya kimsingi inayotoa maelezo wazi ya viashiria vya matumizi , usimamizi na ukaguzi, vigezo na mbinu za uthibitishaji (tazama Uganda sehemu 155 (5) . Kufikia hapa, Bunge lapasa kuweka kigezo cha kutumika kwa :

(c) kuingizwa kwa taratibu na mipango ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika makadirio ya bajeti.

(d) makadirio ya mapato na matumizi yanayochukua vipindi vinavyozidi mwaka mmoja, yaingizwe katika makadirio ya bajeti.

(e) Kuanzishwa kwa kamati yenye uwezo (ndani ya Bunge) inayokagua na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya kitu au mfuko mwingine kando na mfuko wa fedha za dharura.

(f) Kipimo cha jumla cha makadirio ya nyongeza, (yaliyopendekezwa kwa kiwango cha asilmia kumi (10%) cha makadirio ya mwaka kwa mwaka huu uliopo wa fedha) kiwekwe.

(g) Katiba iweke kipimo cha jumla cha kiasi cha fedha zinazoidhinishwa kutolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Fedha za Serikali mbele au ugawaji, kiasi kisichozidi thuluthi moja ya mgao uliofanywa kwa huduma za kawaida za Serikali, kulingana na mwaka huu uliopita.

(h) Katiba ifafanue kwamba kiasi cha fedha kama hicho kitolewe mapema mnamo miezi mitatu ya mwaka wa fedha au Sheria inapotekelezwa, lile litakalokuwa la mwanzo.

(i) Bunge liunde sheria za kutoa masharti ya matumizi ya Mfuko Mkuu wa Fedha za Dharura, ili kuhakikisha uwazi wa matumizi na uwajibikaji.

(j) Bunge lapasa kuunda sheria za kuanzisha kigezo cha kuamua ni aina gani ya matumizi ya fedha za dharura zitakazoruhusiwa kwa madhumuni ya Mfuko Mkuu wa Fedha za Serikali.

(k) Vitengo vya kutekeleza matumizi viruhusiwe uhuru wa kiasi wa kugawa tena bajeti zao zilizoidhinishwa hadi kufikia kiasi cha asilmia kumi (10%) juu na chini ya mpaka wa bajeti yoyote ili kuruhusu upangaji wa kati wa mambo muhimu na kuendeleza uaminifu katika ugawaji.

(l) Bunge lifanye sheria za kutoa ulinzi wa usalama, utoaji fedha uanofaa na matumizi mazuri ya rasilmali za Mfuko Mkuu wa Fedha za Serikali.

## 15.3 Maendeleo ya rasilmali ya utendakazi wa binadamu

### 15.3.1 Kanuni za Jumla

Rasilmali ya utendakazi wa binadamu hutakikana hasa katika kila hali ili ujumlishwe na mifumo ya rasilmali nyingine – fedha za Serikali, teknolojia, vifaa, vyombo vya matumizi, ardhi, mahali – kutekeleza athari ya maendeleo na kuboresha mipango ya maslahi ya jamii. Rasilmali ya utendakazi wa binadamu ndiyo rasilmali muhimu zaidi ya mifumo yote hii ya rasilmali, iliyotuzwa kama ilivyo, na muumba wake uwezo wa kufikiri, kutafakari, na matendo. Kwa hivyo, njia ambazo nchi hupata, huendeleza hugawa na kuwakusanya watu kuwahamasisha na kutunza rasilmali zake ya utendakazi wa binadamu husababisha kiwango cha ubora na uthabiti wa muelekeo wa maendeleo na ufanisi wa maslahi ya jamii.

Usimamizi mwema na matumizi ya rasilmali ya utendakazi wa binadamu husababisha matumizi ya hali ya juu ya vipengele vingine vya rasilmali. Mahitaji ya matumizi ya hali ya juu ya upangaji, ugawanyaji unaozidisha maendeleo, ukusanyaji watu na uhamasishaji wa msingi wa rasilmali ya utendakazi wa binadamu, hauwezi hata kidogo kutosisitizwa.

Hadi sasa Kenya ina idadi ya watu milioni thelathini, inayoongezeka kwa kiasi cha wastani wa asilimia 3%.

Ukuaji wa binadamu kama raslimali kwa misingi ya idadi umekuwa kiini cha mizozo kwa muda.

Kwa upande mmoja, kuna wale wanaoenelea hali hiyo kuwa mzigo mkubwa kwa uchumi wa nchi, kwa kiasi cha kuwa changamoto zaidi katika uafikiaji wa mahitaji ya kimsingi kwa wote. Wanashikilia kwa hivyo kuwa jawabu ni kudhibiti ukuaji au ongezeko la

idadi ya watu hivi kwamba kutakuwa na watu wachache tu wanaotarajia kulishwa, kupewa makazi, elimu, afya miundomsingi, huduma na mahitaji mengine ya kimsingi.

Kwa upande mwingine, kuna wale wanaochukulia ongezeko la idadi ya watu kumaanisha kuwepo kwa idadi kubwa ya wafanyikazi itakayohitajika kuimarisha uchumi siku za usoni, baada ya watoto kukua na kuwa watu wazima na kuweza kushiriki kikamilifu katika maendeleo na mipango ya maslahi ya jamii. Wanashikilia kuwa sio idadi tu iliyo muhimu, bali jinsi raslimali za taifa zinavyosimamiwa. Wanasema kuwa ikiwa raslimali zitasimamiwa vyema, basi zitakuwa za kutosha na ongezeko la idadi ya watu halitakuwa tatizo tena. Wanaendelea kusema kuwa msimamo wao unatokana na wao kuonelea kwamba raslimali zinapaswa kuwekwa katika mipango ya maendeleo badala ya kuziharibu katika udhibiti wa ongezeko la idadi ya watu, kwani, kama ilivyotambulika sawa sawa kutokana na utafiti, idadi ya watu huweza kujisimamia yenyewe na kupungua kadri jamii inavyoendelea kuambatana na sheria asilia ya usawazisho wa kijamii.

Misingi yote miwili ina ubora wake. Idadi kubwa ya watu inaweza kuwa mzigo na wakati huo huo iwe pia raslimali. Ni mzigo katika miaka ya awali ya kukua kwa mtoto, hadi kufikia umri wa miaka kumi na minane. Yaweza kuwa raslimali kwa usawazisho wa maisha kuanzia umri wa miaka kumi na minane, hadi kufikia miaka kati ya 18-25 upande wa chini, hadi kati ya miaka 50 na 75 upande wa juu. Mara nyingi mtu akitimu miaka 75 hutegemea idadi ya watu inayozalisha, kwa kuwa uwezo wake wa kuzalisha hupungua.

Hali ya jumla ya binadamu kama raslimali inapaswa kujulikana kila wakati. Hii huanza kwa kuhesabu watu, shughuli inayofanywa kila baada ya miaka 10 inayojumuisha habari ya kina kuhusu idadi ya watu, inayotosheleza sifa fulani za viwango vilivyowekwa. Hii ni muhimu sana.

Muhimu katika uendelezaji wa binadamu kama raslimali ni masuala yanayohusu afya, elimu, kazi na utoaji wa makazi ikiwa ni pamoja na muundo msingi wa kijamii wa kutosha.

### *(i) Afya*

Afya ya watu ni muhimu katika hatua zote za maisha. Watu wenye afya wanaweza kukua na kuwa watu wazima wanaoweza kuzalisha, na ni katika kiwango hiki ambapo afya nzuri huwa muhimu zaidi. Watu wasio na afya hawawezi tu kuzalisha kwa kiwango fulani, bali pia huwa mzigo kiuchumi na pia kijamii kwa wagonjwa na wale wanaowatunza. Huchangia kumaliza raslimali asili, hasa ambapo huduma za afya, vifaa na mashine za raslimali hutolewa katika mataifa ya nje, hali ambao hutendeka kila mara nchini Kenya.

Kenya ina hali ya utawanyaji wa huduma za afya usiopendeza inayoendelea kupanuka kuambatana na tofauti iliyoko ya kuweza kufikia na kumudu huduma hizo za afya kote nchini. Kwa hivi sasa, kwa mujibu wa mpango wa kitaifa wa maendeleo (2002 – 2008), ni asilimia 42% pekee inayoweza kufikia vituo vya afya katika umbali wa nusu kipenyo wa kilomita 4 na, asilimia 75 pekee katika umbali wa nusu kipenyo kilomita 8. Tofauti pia zinapatikana katika ugawaji wa matibabu. Kuna daktari mmoja pekee kwa watu 33,000 katika maeneo ya mashambani ikilinganishwa na daktari mmoja kwa kila wakazi 1,700 wa mijini. Kuwafanya matabibu kusalia hospitalini, vituo vya afya na zahanati za umma limekuwa tatizo kubwa mno kutokana na malipo duni.

Mpango wa Kenya wa Sera ya Afya uliozinduliwa mwaka 1994 ulilenga kutangaza waziwazi msimamo wa serikali kujitolea kuimarisha afya ya wananchi. Hii ilibadilishwa na kuwa mpango wa sera wa kutekelezeka wa mpango wa mkakati wa Afya ya Taifa (1998 – 2004). Pakiwepo mbinu mwafaka kikatiba au kisheria, juhudi za mpango wa mkakati wa Afya ya Taifa (1998 – 2004) zinaweza kuboresha utoaji wa huduma za afya katika maeneo ya mashambani, huku mkazo ukitiliwa huduma za kinga na kuendeleza afya. Masuala ambayo yanaweza kuhitajika kushughulikiwa na serikali kwa ushirikiano na washikadau katika

maendeleo yanajumisha lishe, kuimarisha ubora, kufadhili utunzaji kiafya, mafunzo na utafiti, viwango vya afya na mpango wa udhibiti.

Athari ya ukosefu wa kinga mwilini (Ukimwi) haiwezi kupuuzwa katika kushughulikia masuala ya afya. Janga la Ukimwi limekuwa tishio kubwa kwa maslahi ya familia maskini na kwa wafanyikazi katika sekta ya kilimo na viwanda. Utunzaji wa wanaougua Ukimwi yanaongeza matatizo zaidi kwa vifaa vya afya vilivyopo ambavyo tayari havitoshi.

Kuweza kufikia maji safi na usafi wa kutosha na unaofaa ni nguzo muhimu katika afya ya umma, hasa kwa mukundi yaliyo na mapato ya viwango vya chini. Maji na usafi ni muhimu sana kwa maslahi na hali ya maisha ya familia. Ili kukabiliana na tatizo hili, pana haja ya huduma za kiufundi zinazofaa, usimamizi bora wa jamii na mipango halisi ya kupunguza umaskini na utathmini wa kijamii. Kwa mujibu wa mpango wa kitaifa wa kupunguza umaskini 1999 – 2015, makadirio ya sasa kuhusu ugawaji wa maji yanaonyesha kuwa asilimia 75 ya wakazi wa mijini wanaweza kufikia maji safi ya kunywa, na asilimia 50% ya wakazi katika maeneo ya mashambani wanaweza kufikia maji wanayoweza kubeba na kutumia kwa matumizi mbalimbali.

Katika maeneo ya mashambani, uchimbaji wa maji na kulinda chemichemi kunahitajika zaidi. Mara nyingi, umaskini huhusiana na ukosefu wa maji. Wanawake hutumia zaidi ya nusu ya siku wakisafiri na kupanga foleni za kuchota maji wakati maeneo mengi wanakochotamaji yanapokauka, muda wao mwingi sana hutumiwa kwa shughuli hii.

Katika kuandaa malengo ya kutoa maji safi, ishara muhimu ya kijamii ya kufaulu itakuwa athari yake kwa kazi ya wanawake, kwa kuwa kutafuta na kuchota maji limekuwa tu ni jukumu la wanawake na huathiri mipango yao muhimu kuhusu utunzaji wa familia. Kuna mipango kadhaa kuhusu maji inayoendelea katika wizara ya Raslimali ya Maji, na inatarajiwa kuwa mara itakapokamilika,

itapunguza umaskini kwa kuziwezesha familia zote kufikia miradi ya maji safi yanayoweza kubebwa katika mwendo wa nusu kipenyo kilomita 3 kufikia mwaka 2010. Hati ya Kikao Cha Serikali Na 1 ya 1999 kuhusu sera ya usimamizi na maendeleo ya maji hivi sasa inaongoza usimamizi wa maji. Lengo la jumla la sera ya maendeleo ya maji ni kufanikisha utoaji wa maji ya kutosha na yaliyo bora katika mwendo unaofaa ili kuatosheleza watumizi wote kwa njia endelevu kitaifa na kiuchumi.

***(ii) Maendeleo ya Elimu na Watu wa kufanya kazi***

Tofauti ya kidhana huwekwa kati ya maendeleo ya elimu na watu wa kufanya kazi. Kwa jumla elimu hutumiwa kurejelea utaratibu wa kielimu wa kuimarisha na kukuza uwezo wa kiakili wa mtu katika kujitayarisha kwa ndaro za maisha. Maendeleo ya watu wa kufanya kazi hasa hurejelea dhana ya kufunza kwa minajili ya kutoa ujuzi unaohitajika, kutayarisha au kumaanisha utendakazi wa mtu kama mtaalamu au mtoaji huduma. Kwa hivyo yote mawili, maendeleo ya elimu na watu wa kufanya kazi yanahusu utoaji wa ufahamu au elimu na tajriba inayomuezesha mpokeaji kuwa mtu anayezalisha zaidi katika misingi ya kazi. Vinapaswa kumsaidia mtu kukabiliana na ndaro za maisha akiwa katika hali ya mtu aliyejitayarisha vilivyo, ambayo hukosekana tu ikiwa mtu hakupokea elimu au tajriba kama hiyo.

Kuimarisha kufikiwa kwa elimu na watoto kutoka makundi yaliyo na mapato ya chini kutahitaji kujumuishwa kwa sera na mipango ya usimamizi, na kulenga zaidi usajili unaongezeka katika shule za msingi, na viwango vya wanafunzi wanaokamilisha masomo kwa makundi yasiyo bahatika, hasa wasichana kutoka familia zilizo na mapato ya chini. Sera hizo na mipango ya usimamizi inaweza kujumuisha mtalaa wa shule za msingi unaoanzia ujuzi muhimu wa kilimwengu usimamizi wa shule za msingi ulio thabiti zaidi na uliosambazwa, na kundi la wanafunzi waliojitolea kwa kuongoza utafutaji wa maendeleo mapana ya jamii.

Lengo muhimu la kupunguza umaskini katika elimu huashiria hasa dhana za kifedha na ubora wa ufunzaji na usomaji katika shule za msingi.

***(iii) Kufanya Kazi***

Moja kati ya ndaro kuu zinazolikabili taifa ni kutoa nafasi za kazi kwa idadi ya watu inayoendelea kuongezeka. Baada ya kutimiza umri unaostahiki, watu hupambana ili kuweza kufanya kazi ya aina fulani, ama kwa kuajiriwa au kuanzisha biashara yao wenyewe. Hii ni muhimu kwa madhumuni ya kujipatia ajira inayonufaisha, na pia kwa kuimarisha "kujiheshimu" na hadhi ya binadamu. Inapofikia kiwango kuwa watu binafsi wametayarishwa na mfumo wa kijamii kufanya kazi fulani katika jamii, je watu hao huwa katika nafasi bora ya kuweza kutoa mchango muhimu katika maisha yao wenyewe na maslahi ya jamii? Kufikia kiwango hicho, na pia kadri watu hao wanapopewa wajibu na kupewa vifaa bora vinavyostahili na hali inayofanikisha utenda kazi, wataweza kuimarisha mchango wao kwa maslahi ya jumla ya jamii na ubora wa maisha katika njia muhimu.

***(iv) Makazi na Muundomsingi***

Kuweza kufikia makazi, muundomsingi na huduma kutakuwa na uwezo wa kuimarisha maslahi na ubora wa maisha ya watu kwa njia muhimu. Hii itaimarisha sana uzalishaji wao na utoaji wa bidhaa na huduma, na kwa hivyo utachangia zaidi katika kukuza uchumi na maslahi ya kijamii. Hali ya sasa ya makazi inasikitisha sana. Lakini kuna njia mbalimbali za kuimarisha hali hiyo kupitia kuhakikisha usalama unaoungwa mkono na (mortgages) vile vile kuna uwezekano mkubwa wa kuimarisha hali ya makazi kupitia matumizi ya teknolojia inayofaa kwa utengenezaji wa vifaa, bidhaa na usanifu wa nyumba usiyo ghali na unaoweza kukaa kwa muda mrefu. Uimarishaji kama huo pia unaweza kufanyiwa

muundomsingi na huduma ambazo zimekuwa katika hali duni kwa miongo miwili iliyopita.

### 15.3.2 <u>Maendeleo ya Binadamu kama Raslimali Katika Katiba</u>

Katiba iliyopo sasa haishughulikii swala la maendeleo ya binadamu kama raslimali, wala kama vipengele vya haki na uhuru wa kimsingi. Hata hivyo, kuna sheria zinazoshughulikia maswala haya. Sheria hizo ni pamoja na:-

- Sheria ya Elimu (sura 211)
- Sheria ya Vyuo Vikuu (sura ya 213 B)
- Sheria ya Halmashauri ya Mikopo kwa Elimu ya Juu (Sura ya 21 B
- Sheria zinazoanzisha Vyuo Vikuu vya Umma (sura za 210, 210 A, 210 C, 214 n.k)
- Sheria ya Afya ya Umma (sura ya 224)
- Sheria ya Nyumba (Cap 117); na

### 15.3.3 Maendeleo ya Rasilmali ya Binadamu katika Katiba Nyingine

Masharti yanayohusiana na maendeleo ya rasilmali ya binadamu, hasa kuhusu elimu, mafunzo, maendeleo ya kitaaluma, ubunifu wa kazi na kuongoza ajira kwa kawaida ni sehemu ya Sheria za Haki katika Katiba nyingi. Hata hivyo, wakati mwingine baadhi ya Katiba hubuni au hutoa uanzishaji wa muundomsingi kwa ajili ya maendeleo na usimamizi wa maswala mapana ya rasilmali ya binadamu. Moja kati ya shughuli za Tume ya Huduma ya Elimu ya Uganda, kwa mfano, iko chini ya Ibara ya 168 (1) (C), ili:

> "*kurekebisha taratibu na hali za huduma, taratibu za kudumu, mafunzo na sifa zinazohitajika kwa maafisa wa umma katika huduma ya elimu….*"

Kama kanuni kuu, kwa hivyo, maelekezo kamili kwa maendeleo ya rasilmali ya binadamu yatapatikana katika sheria zilizopitishwa na Bunge.

**15.3.4 Waliyosema Wananchi**

Mambo ambayo wananchi walisema kuhusu Maendeleo ya Binadamu kama Raslimali na maswala mengine yanayohusiana na swala hili yanaweza kuwasilishwa kimukhtasari ifuatavyo:-

*(i) Kuhusu Elimu:-*

a. Seneti za Vyuo Vikuu ziwateue Mkuu na Makamu Mkuu wa chuo.
b. Wanafunzi wanaohitaji msaada wanapaswa kusaidiwa kwa kupewa usaidizi wa karo ya masomo, na mpango huo wa kutoa usaidizi wa karo kwa wanafunzi unapaswa kusimamiwa na kamati huru au machifu.
c. Katiba inapaswa kuhakikisha kwamba serikali inatoa chakula na vifaa vingine vyote vya masomo kwa shule zote.
d. Katiba inapaswa kuhakikisha kwamba serikali inasaidia katika kujenga shule na kuzipa vifaa vya masomo vinavyohitajika.
e. Katiba inapaswa kutoa elimu bila malipo hadi kiwango cha shule za upili.
f. Elimu ni ghali mno, na kwa hivyo wanafunzi wengi hawawezi kuimudu na hivyo huishia ku toka shuleni kabla ya kukamilisha masomo yao.
g. Mfumo wa elimu wa 8-4-4 unazingatia nadharia zaidi na kwa hivyo hauimarishi upataji wa ujuzi halisi wa kutenda
h. Vyuo vya elimu ya juu vinawasajili wanafunzi ambao hawakufuzu na hivyo kupunguza viwango katika vyuo hivyo.
i. Idadi ya vyuo vikuu haitoshi kuwasajili wanafunzi wote wanaofuzu kujiunga na vyuo vikuu.
j. Kuanzisha na kuendeleza shule ni ghali mno na hivyo kuwa mzigo kwa wazazi.

k. Walimu hufanya kazi nyingi sana lakini hawalipwi vizuri wala kupewa motisha.
l. Wanafunzi hawana ufahamu kuhusu Katiba na yaliyomo.
m. Elimu ya kimsingi inapaswa kutolewa kwa wote bila malipo.
n. Katiba inapaswa kufundishwa shuleni.
o. Katiba inapaswa kuhakikisha kuwa serikali inasaidia katika ujenzi wa shule, na kuzipa vifaa vya mafunzo vinavyostahili

p. Adhabu ya viboko inapaswa kuendelezwa shuleni kwa kuwa awali ilitoa matokeo mema katika kuhakikisha kuwa wanafunzi wana adabu.
q. Serikali inapaswa kuweka viwango vya karo ya shule za upili na pia ndiyo inayopaswa kuipunguza.
r. Lugha ya ishara inapaswa kuwekwa katika mitaala yote ya shule.
s. Kusajiliwa katika vyuo vya mafunzo ya juu kunapaswa kuzingatia kufuzu kwa wanafunzi kikamilifu.
t. Mishahara ya walimu inapaswa kutathminiwa na kuongezwa
u. Mfumo wa elimu unapaswa kufanyiwa marekebisho ili uweze kuafikia mahitaji ya ulimwengu wa sasa unaobadilika kila wataki na unapaswa kuwashirikisha walimu.
v. Mfumo wa kwota unapaswa kuondolewa.
w. Mfumo wa elimu wa 8-4-4 unapaswa kuondolewa na nafasi yake kuchukuliwa na mfumo wa 7-4-2-3
x. Walimu wa shule za malezi wanapaswa kulipwa na serikali
y. Mishahara ya walimu inapaswa kuambatana na sifa zao za kufuzu.
z. Katiba inapaswa kuhakikisha kuwa serikali inaanzisha vyuo vikuu katika kila mkoa.

**(ii) Kuhusu Ajira:-**

a. Mfumo wa mtu mmoja kufanya kazi moja pekee unapaswa kuchukuliwa.

b. Katiba inapaswa kuzingatia uhakikisho wa ajira kama haki ya kimsingi kwa Wakenya wote.
c. Wanaume na wanawake wanapaswa kuwa na fursa sawa za kuajiriwa.
d. Malipo ya kustaafu yanapaswa kuongezwa wakati mishahara inapoongezwa.

**(iii) Kuhusu afya**

a. Dawa hazitoshi kutokana na wizi wa dawa hospitalini.
b. Haspitali hazina wafanyikazi wa kutosha.
c. Dawa zinapatikana katika hospitali za kibinafsi kwa bei ghali lakini sio katika hospitali za umma.
d. Maeneo ya utabibu mara nyingi hukosa vifaa.
e. Watu wengi walio maskini hawawezi kulipa ada ya kutibiwa.
f. Mtindo wa kugawanya gharama umekuwa na hasara zaidi badala ya kuwafaidi wananchi.
g. Kuna msongamano hospitalini kutokana na ukosefu wa vifaa.
h. Ufisadi umekithiri miongoni mwa matabibu hasa katika vyumba vya kuhifadhi maiti.
i. Kuna bugudha katika haspitali za umma.
j. Wafanyikazi hospitalini wana mwelekeo hasi kuhusu umma.
k. Idadi ya hospitali haiwezi kuitosheleza idadi kubwa ya watu.
l. Maafisa ambao wameajiriwa na serikali wasiruhusiwe kumiliki kliniki za kibinafsi.
m. Serikali inapaswa kupeleka wafanyikazi wa kutosha hospitalini
n. Mtindo wa kugawana gharama hospitalini inapaswa kukomeshwa
o. Serikali inapaswa kujenga vituo zaidi vya afya na hospitali katika kiwango cha nyanjani au mashinani.
p. Serikali inapaswa kupeleka dawa za kutosha hospitalini
q. Ada inayolipwa hospitalini inapaswa kupunguzwa kote nchini.
r. Kliniki za kibinafsi na maduka ya kuweka dawa yanapaswa kuchunguzwa kwa undani na kuanzishwa kwake kudhitiwe na serikali.

s. Hazina ya Bima ya Matibabu (NHIF) inapaswa kuhimizwa kufanya kazi kwa pamoja na hospitali zote nchini.
t. Wakenya wanapaswa kufurahia huduma bora za matibabu.
u. Serikali inapaswa kushughulikia malipo ya wafanyikazi wa hospitalini.
v. Kliniki sogezi zinapaswa kuanzishwa katika maeneo yaliyo na ukame.
w. Vyumba vya kuhifadhia maiti havipaswi kuwa vya malipo.
x. Wizara ya afya inapaswa kutengewa asilimia 20% ya makadirio ya bajeti pamoja na kupewa fedha nyingine.
y. Uhusiano kati ya madaktari na wagonjwa unapaswa kuchunguzwa.
z. Hospitali zinapaswa kuwa na sera ya kuwatambua walemavu na kuona ikiwa chochote chaweza kufanywa kwa kujaribu kusuluhisha tatizo mapema.

**(iv) Kuhusu maji na usafi**

a. Serikali inapaswa kufufua miradi ya maji iliyoanzishwa zamani, ili kuweza kutoa maji safi kwa Wakenya wote.
b. Serikali inapaswa kuhakikisha kuwepo kwa mfumo bora wa kusambaza maji kote nchini.
c. Serikali inapaswa kuhakikisha kuwepo kwa mfumo bora na wa kufaa wa kupitisha majitaka nchini Kenya.
d. Serikali inapaswa kuhakikisha kuwa maeneo yote ya umma yana vyoo na mahali pa kutupa taka.
e. Serikali inapaswa kuwapa Wakenya wote maji safi ya bomba.
f. Kila wilaya inapaswa kupewa mtambo wa kuchimbia machimbo ya maji ili kuondoa ukosefu wa maji.

**(v) Kuhusu muundomsingi**

a. Serikali inapaswa kuhakikisha kuwepo kwa hali nzuri ya kufanikisha maendeleo ya kiuchmi kwa kuunda muundomsingi bora wa usafiri na mawasiliano.

b. Vifaa vya usafiri na mawasiliano vinapaswa kutolewa katika mkoa wa Kaskazini, Mashariki na katika maeneo mengine ya jamii za wafugaji wa kuhamahama ili kuwavutia wawekezaji.
c. Barabara za mashambani zinapaswa kuwekwa lami.
d. Usafiri wa njia ya reli unapaswa kuimarishwa kwa madhumuni ya kuweza kufikiwa.
e. Serikali inapaswa kuhakikisha kuwa kuna mtandao bora wa mawasiliano nchini.
f. Muundomsingi unapaswa kusambazwa kwa njia iliyo sawa.

### 15.3.5 Uchanganuzi

Umuhimu unaowekewa maendeleo ya binadamu kama raslimali ni wazi kutokana na misimamo ambayo walichukua kuhusu mambo tofauti yanayohusiana na swala hili. Hali ya jumla ya ubovu wa muundo msingi wa kijamii ililalamikiwa kote nchini. Kwa kweli, kwa watu wengi, hiyo ilikuwa ithibati ya serikali ama kushindwa au kutotaka kutekeleza majukumu yake. Mkazo haswa uliwekwa katika elimu, afya na ajira ambavyo watu walionelea kama ufunguo wa kuimarisha hali ya maisha na uimarishaji wa maisha bora. Haja ya kuweka raslimali zaidi katika sekta hii kwa hivyo ilipewa kipaumbele.

### 15.3.6 Mapendekezo

Tume kwa hivyo inapendekeza ifuatavyo

*(i) Kuhusu uchumi na mpango wa jamii*

a. Seneta inapasa kuwekea vikwazo mali ya kibinafsi au biashara ya kibinafsi, endapo zinaonekana kuwa hatari kwa maendeleo yaliyosawazishwa ya mali ya taifa na maisha ya watu;
b. Katiba inapaswa kuzingatia kuwa Wakenya wana haki ya kuimarisha hali au viwango vyao kwa pamoja au mtu mmoja kibinafsi;

c. Sheria ya Haki inapaswa kupanuliwa ili ijumuishe haki za kijamii na kiuchumi;
d. Mwafaka kuhusu utangamano wa kijamii unapaswa kujumuishwa katika katiba;
e. Katiba mpya inapaswa kuanzisha mfumo wa kitaifa wa mipango unaofanikisha kuafikiwa kwa malengo ya kitaifa ya kiuchumi na kijamii;
f. Katiba mpya inapaswa kuzingatia kuwepo kwa mifumo ya udhibiti na matumizi bora ya raslimali;

*(ii)* *Kuhusu elimu*

a. Tume ya Huduma ya Elimu ianzishwe. Tume hiyo iwe ikirejelea mara kwa mara masharti na hali ya huduma, sheria za nidhamu, mafunzo na sifa za kufuzu kwa maafisa wa umma katika huduma ya elimu na maswala yanayohusiana na usimamizi na maslahi, na kutoa mapendekezo kwa serikali;
b. Serikali inapaswa kuwajibika kuendeleza elimu ya lazima bila malipo; na
c. Serikali inapaswa kuchukua hatua mwafaka ili kuweza kutoa nafasi sawa ya kupata elimu ya juu kadri inavyowezekana kwa Mkenya.

*(iii)* *Kuhusu afya*

a. Serikali inapaswa kuunda sera ya Afya ya Kitaifa inayotosheleza mahitaji ya kimsingi ya kitaifa kwa Wakenya;
b. Tume ya Huduma za Afya inapasa kuanzishwa;
c. Ili kuweza kutoa bidhaa zilizopunguzwa gharama kwa wananchi, mikakati bunifu inapaswa kutumiwa ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato ili kusawazisha "utoaji au uzalishaji wa mapato" na "kufikia" malengo kuhakikisha huduma bora na kwa usaidizi wa kifedha wa moja kwa moja kutoka kwa serikali; na

d. Kama ilivyo haki ya kikatiba, afya kwa wote inapiganiwa, na vivyo hivyo muundo wa kisheria unapaswa kubadilishwa ili uweze kuwaendeleza walioko katika huduma ya utabibu.

*(iv)* *Maji na Usafi*

a. Serikali inapaswa kutenga, kuhifadhi na kulinda raslimali za maji zilizopo na utoaji wake katika njia iliyo endelevu, sawazishi na ya kiuchumi kutokana na kupatikana kwake kusiko laini kutegemea na mahala na pia wakati;
b. Utoaji wa maji kwa mahitaji mbali mbali ya maji uzingatiwe;
c. Utupaji salama wa maji yasiyotumiwa tena, na ulinzi wa mazingira uhakikishwe;
d. Mfumo bora na thabiti wa kitaasisi uanzishwe kuafikia maendeleo na usimamizi bora wa sekta ndogo ya maji kwa ukuaji endelevu wa uchumi na kupunguza umaskini;
e. Mbinu bora na endelevu ya ufadhili kwa usimamizi bora wa raslimali za maji pamoja na utoaji wa maji na maendeleo na usimamizi wa usafi inapaswa kuundwa;
f. Serikali inapaswa kuhakikisha kuwa Wakenya wote wanaweza kufikia maji safi na yaliyo salama; na
g. Serikali inapasa kuzingatia sheria na mbinu tekelezi ili kuafikia maendeleo na usimamizi bora wa sekta ndogo ya maji kwa maendeleo endelevu ya uchumi na kupunguza umaskini na kusimamia utekelezaji wake.

*(v)* *Kuhusu Barabara*

a. Barabara za umma zinapaswa kufanywa kuwa za kibiashara (commercialized) kwa usimamizi na utunzaji bora;
b. Halmashauri kuu iliyo huru, inayohusisha pakubwa sekta ya kibinafsi, ianzishwe kusimamia hazina ya Ushuru wa utunzaji na ukarabati wa barabara;

*(vi)* *Kuhusu nafasi za ajira*

a. Sheria mpya ya Haki inapaswa kutangaza kuwa Wakenya wana Haki ya:-

- Kufanya kazi chini ya hali ya kuridhisha na salama
- Mshahara sawa kwa kazi sawa;
- Siku za kuridhisha za kupumzika pamoja na siku za taifa;
- Kuunda au kujiunga na chama cha kutetea maslahi ya wafanyikazi na kwa kila mwajiriwa kujiunga na chama cha kutetea masalahi ya wafanyikazi; na
- Kufanya majadiliano na makubaliano ya bei ya jumla;

b. Sera mpya ya kuongera ajira ibuniwe na kutekelezwa.

## 15.4 Sayansi na Teknolojia

### 15.4.1 Kanuni za Jumla

Kijumla, teknolojia ni mkusanyiko wa njia, mbinu na vifaa ambavyo pamoja na watu wanaovitumia vinaweza kuchangia kwa umuhimu mkubwa katika kusuluhisha matatizo mbali mbali ya kimaendeleo ya binadamu. Teknolojia inayofaa kwa hivyo inamaanisha kuwa licha ya kuwa ya kufaa kwa upande wa sayansi, teknolojia pia inakubalika kwa wale wanaoitumia kwa madhumuni ya kujikimu katika maisha.

Jukumu la sayansi katika uzalishaji wa kiviwanda bado ni dogo mno nchini Kenya. Hii kwa upande mmoja inaweza kuelezwa na sababu kuwa sekta ya viwanda inahusiana zaidi na kampuni kubwa katika mataifa yaliyostawi ambapo sekta hii hutoa ujuzi wa kisayansi. Kwa kweli, karibu mipango yote ya kandarasi ambayo imeihusisha Kenya na utoaji wa teknolojia nje inahakikisha uhamishaji wa ujuzi mpya wa kisayansi na teknolojia. Hata hivyo, wakati kampuni zinapoanza kufanya kazi, hukabiliana na matatizo ya kinyumbani,

yanayohitaji kusuluhishwa kwa kutumia ujuzi wa kisayansi uliovumbuliwa hapa nyumbani. Kwa hakika ni kupitia kwa kuendelezwa kwa ujuzi wa kinyumbani wa sayansi na teknolojia ndipo taifa huweza kuendelea na kuweza kujitegemea.

Maeneo yanayokua na kupanuka katika sayansi na teknolojia yanajumuisha uwasilishaji wa habari, utabibu, lishe, kilimo na teknolojia viumbe. Ni lazima uundaji wa Katiba utambue mabadiliko katika maisha ya kijamii na kiuchumi yanayotokea kutokana na maendeleo katika sayansi na teknolojia.

### 15.4.2 Sayansi na Teknolojia katika Katiba

Katiba ya sasa haisemi lolote kuhusu sayansi na teknolojia. Hata hivyo, kuna sheria zinazohusu uzalishaji na usimamizi kiasi wa teknolojia. Sheria hizi zinajumuisha sheria ya kampuni (Sura ya 514) na sheria ya mali ya kiviwanda (sura ya 509). Katiba za mataifa mengi sasa zinazingatia sayansi na teknolojia.

### 15.4.3 Sayansi na Teknolojia katika Katiba Nyingine

Masharti ya kikatiba yanayohusu sayansi na teknolojia si ya kawaida sana katika mamlaka ya kisheria. Kasi ambayo kwayo elimu ya sayansi na teknolojia inaendelea labda ndiyo sababu masharti maalum ni adimu kupitwa na wakati katika maandishi ya kikatiba. Mamlaka ya sheria, ambayo ni yenye maswala haya hufanya hivyo kuhimiza uwekezaji kwenye utafiti na maendeleo ya teknolojia mpya. Katiba ya Ecuador, kwa mfano, hutarajia kupewa kipaumbele na vyuo vikuu, vyuo vya ufundi, vyuo vya juu vya ufundi na shule, kuchunguza na kwenye mafunzo ya sayansi na teknolojia. Katiba hiyo pia inatarajia asasi za utafiti kushirikisha maswala ya sayansi na teknolojia katika uzalishaji na usimamizi bora wa maliasili. Pia huhakikisha haki ya kufikia chanzo cha habari za kisayansi na kiteknolojia, na kutafuta kupokea na utumia habari kama hizo.

Ibara ya 71 ya Katiba ya Ufilipino, inatoa pamoja na mambo mengine kwamba:

*"Sayansi na teknolojia ni muhimu kwa maendeleo na ustawi wa kitaifa. Serikali inapaswa kutoa kipaumbele kwa utafiti na maendeleo, uvumbuzi, ukarabati, na matumizi yao, na kwa elimu ya sayansi na teknolojia, fundi na huduma".*

Karibu na nyumbani, Sura ya 12 ya 1998 Katiba ya Jamhuri ya Sudan inaeleza kuwa:

*"Serikali ihamasishe rasilmali zake rasmi na asasi zinazojulikana ili kupigania kutojua kusoma na ujinga, kuimarisha mfumo wa elimu, na kuboresha sayansi, utafiti, ushirika wa kisayansi na kurahisisha kufikia elimu na utafiti………"*

### 15.4.4 Waliyosema Wananchi

Ijapokuwa maswala ya sayansi na teknolojia hayakutolewa kwa wananchi moja kwa moja, kulikuwa na maoni kuhusu maswala yanayohusiana na sayansi na teknolojia:-

(i) Kuhusu utengenezaji na matumizi ya kawi:-

a. Katiba inapaswa kuhakikisha kuwa serikali inatoa nguvu za umeme kwa wananchi wote walioko maeneo ya mashambani na mijini, na kupunguza gharama yake kwa kuondoa kodi ya thamani iliyoongezwa (VAT) katika bili za nguvu za umeme
b. Serikali pia inapaswa kuziruhusu kampuni nyingine za kibinafsi kushindana na Kampuni ya Ugavi wa Umeme Nchini Kenya KPLC ili kupunguza ukiritimba
c. Katiba inapaswa kuzingatia swala la kuwa jamii inaendelea kukua na kupanuka, kuendelea kwa ujuzi wa binadamu na teknolojia
d. Serikali inapaswa kupunguza ada ya umeme ili kuhakikisha kuwa gharama ya uzalishaji katika viwanda inapungua
e. Kampuni za kutengeneza na kusambaza umeme zinapaswa kujitayarisha kuafikia mahitaji ya viwanda ambavyo vimeendelea kiteknolojia. Usambazaji huo unapaswa kuwa ule ambao kampuni zinaweza kumudu. bora na wa kutegemewa

f. Kuwapelekea wateja zaidi umeme kutaimarisha uchumi, sawa na hali ya maisha ya Wakenya na kwa hivyo maendeleo kwa jumla.

*(ii)* *Kuhusu ustawi wa kiviwanda*

a. Viwanda nchini Kenya vinapaswa kusambazwa, na kugawanywa kwa njia iliyo sawa katika mikoa, na asilimia sitini ya mapato yavyo yatumike huko.
b. Serikali inapaswa kuhakikisha kuwa shughuli ya ustawi wa viwanda inaafikiwa kutumia raslimali za humu nchini kwa mfano, mnazi na mazao yake.
c. Viwanda vya humu nchini vinapaswa kulindwa kutokana na ushindani usiofaa kutoka kwa viwanda vya nje, kwa kupitisha sera za kuhakikisha msimamo huu.
d. Sera zinapaswa kuwekwa kuzuia uuzaji wa mali ghafi yanayopatikana humu nchini katika mataifa ya nje, na wakati huo huo kuunda sera za kuimarisha ushindani kati ya viwanda vya humu nchini
e. Viwanda vya sukari na korosho vinapaswa kufufuliwa ili kuwapa Wakenya kazi kutokana na maembe na nazi
f. Serikali inapaswa kuunga mkono viwanda vyote vilivyo na msingi wake katika kilimo ili visiangamie, kwa mfano KCC, KMC, Rivatex n.k
g. Serikali inapaswa kuzingatia zaidi sekta ya Jua Kali kupitia kwa njia za ufadhili kama vile mikopo, na kutangaza na kuendeleza bidhaa za Jua Kali.
h. Viwanda vya kutengeneza bidhaa vinapaswa kuwekwa katika maeneo ya kilimo ya uzalishaji na kuwa viwanda hivyo vinapaswa kuanzishwa katika kila mkoa.
i. Serikali inapaswa kuvipa leseni viwanda vya kibinafsi vya kuzalisha umeme nchini Kenya.
j. Serikali inapaswa kushughulikia uwezekano wa kuanzisha vituo vya kawi ya nuklia, kupanua kawi inayotokana na upepo na mvuke.

k. Vituo vya kutayarisha samaki vinapaswa kuanzishwa karibu na maji ili viweze kunufaisha jamii zinazoishi katika maeneo hayo; na tume ya Nyama nchini Kenya iliyo Nairobi hivi sasa iwekwe katika mkoa wa Kaskazini –Mashariki ili iweze kufikia wanyama na vichinjio kwa urahisi.
l. Serikali inapaswa kulazimishwa na Katiba kuwasaidia kifedha Wakenya wanaobuni mambo mapya na inapaswa kulinda na kuendeleza haki za kiakili na ubunifu.

*(iii) Kuhusu habari na Teknolojia*

a. Katiba inapaswa kuhakikisha kuwa vyombo vya habari, magazeti, redio na runinga vinakuwa huru kabisa katika shughuli zake, mradi tu vyombo vya habari vinajitegemea na viko huru kutokana na ushawishi wowote ule
b. Vyombo vya habari vya umma havipaswi kuangazia tu chama tawala na kuvipuuza vyama au wanasiasa wengine.
c. Vyama vyote vya kisiasa na maeneo yote yanapaswa kushughulikiwa kwa njia iliyo sawa na vyombo vya habari vinavyomilikiwa na serikali.
d. Vyombo vya habari vinapaswa kuwajali walemavu, kwa mfano ukalimani kwa viziwi, na katika lugha zote za kwanza pamoja na magazeti kuchapishwa katika maandishi ya Breli.
e. Kampuni za kibinafsi zinapaswa kuruhusiwa kuanzisha vituo vya redio na runinga kwa gharama ya chini.
f. Ijapokuwa Katiba inapaswa kuvipa vyombo vya habari uhuru wa kutangaza mambo, inapaswa kuweka mbinu za kusimamia na kuamua aina ya vipindi vinavyotangazwa.
g. Vyombo vya habari vinapaswa kuzuiwa kuleta vipindi visivyozingatia maadili ambavyo vimewafanya Wakenya kupoteza maadili yao, na vinaendelea kufanya hivyo.
h. Hakupaswi kuwepo vizuizi katika utoaji wa leseni kwa vituo vya kurushia matangazo, lakini muda wa majaribio kabla ya kupewa leseni wa siku 30 unapaswa kutolewa.

i. Vizuizi vyote vya kisheria vilivyowekewa utangazaji wa redio na runinga vinapaswa kuondolewa
j. Serikali inapaswa kuruhusu kuundwa kwa baraza la kulisimamia vyombo vya habari. Wataalamu kutoka huduma za vyombo vya habari ndiyo wanaopaswa kulisiamia.
k. Serikali inapaswa kuunga mkono vyombo vya habari vinavyoendeleza demokrasia.
l. Wanawake hawapaswi kutumiwa kama vifaa vya ngono kwenye runinga. Vipindi vya runinga na redio vinapaswa kudhibitiwa ili kuwalinda watoto dhidi ya habari mbovu.
m. Kampuni za kibinafsi zinapaswa kuruhusiwa kuanzisha vituo vya redio na runinga kwa gharama ya chini. Utoaji wa huduma za mtandao wa intaneti haupaswi kuwekewa vizuizi.
n. Kunapaswa kuwepo sheria ya vyombo vya habari inayohakikisha kuwa nakala mbili za kila gazeti zinapelekwa kwa Mkuu wa Sheria kabla ya kuanza kuuzwa barabarani.
o. Matangazo ya biashara ya sigara na pombe kwenye vyombo vya habari yanapaswa kukomeshwa.
p. Shughuli za bunge zinapswa kutangazwa moja kwa moja
q. Vyumba vya habari vya umma havipaswi kupendelea upande wowote wakati wa kampeini za uchaguzi.
r. Watumizi wanapaswa kupewa ukweli unaostahili ili waweze kuchagua kwa kufahamu na walindwe kutokana na matangazo ya biashara yasiyo maaminifu na ya kupotosha kupitia uundaji wa mipango ya kuwapa watumizi habari
s. Lugha ya biashara inapaswa kuwa rahisi.

*(iv)* *Kuhusu utafiti wa sayansi na mafunzo*

a. Kuna matatizo kuhusu elimu ya sayansi na kwa hivyo kuna haja ya kutoa motisha ya kusoma sayansi shuleni hasa miongoni mwa wasichana. Kupitia tajriba ya kihalisi inayohusisha matumizi ya vinyago na michezo

b. Serikali inapaswa kutoa fedha zaidi kwa utafiti na maendeleo katika teknolojia ya habari.

### 15.4.5 Uchanganuzi

Mataifa yanayostawi, Kenya likiwemo, yanaweza kufaidika sana kutokana na teknolojia mpya, lakini pia yana ndaro kubwa ya kusimamia hatari inayoambatana na teknolojia hiyo. Isitoshe, huku hatari nyingine zikiweza kushughulikiwa katika kiwango cha ulimwengu, nyingine ni lazima kushughulikiwa kinyumbani.

Tatizo kubwa zaidi ambalo bara la Afrika linakabiliana nalo hivi sasa ni maendeleo ya kiwango cha chini yanayojitokeza kupitia umaskini, maradhi, kukosa ufahamu na mambo mengine mengi. Ni jambo la kusikitisha kutambua kuwa kutokana na ukosefu wa fedha na raslimali nyingine, mataifa mengi ya Afrika yamebakia kuwa maskini kwa miaka mingi. Hali dhaifu ya kifedha na matumaini madogo ya kuimarika mara moja kwa uchumi mara moja vikiandamana na usimamizi mbovu, ufisadi na utawala wa kidikteta regimes barani Afrika pia hutatiza sana uungwaji mkono wowote wa kinyumbani unaohitajika kutatua tatizo la maendeleo ya kiwango cha chini.

Wakenya walio na vipawa wanaofanya kazi katika maeneo ambako mali ya humu nchini hutumika hawatambuliwi na serikali kupitia tuzo au kupandishwa vyeo. Ni wachache mno kati ya Wakenya kama hao wanaopewa mikopo kutumia kuimarisha uzalishaji wao.

### 15.4.6 Mapendekezo

(i) Kuhusu uundaji wa sera

a. Serikali ya Kenya inapaswa kuzingatia kupitia njia ya kanuni za maongozi za taifa kujumuisha sayansi na teknolojia kama msingi wa ustawi wa kiviwanda na kwa hivyo ukuaji wa uchumi na maendeleo, hasa katika sekta ya afya.

b. Sera fulani zinapaswa kufuatwa, kuhusiana na mipango ya muda mrefu. Sera hizo zinaweza kuisaidia Kenya kuimarisha msingi wake wa teknolojia kama chombo cha kuimarisha hali ya maisha ya wananchi na kuendeleza ushindani wake katika soko la kimataifa.
c. Serikali inapaswa kuwateua watu watakaohusika na sayansi bungeni ili waweze kulipa bunge ujuzi wa kiufundi unaohitajika kuhusu sayansi na teknolojia.
d. Teknolojia inayofaa inapaswa kufuatwa na kuchukuliwa kama njia ya kuchochea ukuaji wa uchumi kwa kutumia kikamilifu raslimali inayoweza kupatikana. Teknolojia hiyo Inapaswa kufanikisha maendeleo ya kijamii kwa kuwawezesha wengi wa idadi ya watu kugawana manufaa ili isiwe tu ni wachache wanaobahatika.
e. Sera ya sayansi na teknolojia inapaswa kuwekwa ili kuimarisha uthabiti wa mfumo wa kitaifa wa ubunifu, kuunga mkono utafiti wa umma na elimu, na kuendeleza ushindani katika sekta ya biashara.

**(ii) Kuhusu Habari, Elimu na Mafunzo**

a. Kwa kuwa kiwango cha habari iliyopo kuhusu shughuli za kiviwanda ni muhimu kwa utayarishaji na utekelezaji wa miradi inayostahili, utathmini wa shughuli za kiteknolojia kama njia ya kupunguza upendeleo unaoweza kusababisha kuongezeka kwa gharama au miradi kukosa kufaulu ni muhimu.
b. Tukizingatia mabadiliko ya kiteknolojia yanayodhihirika hivi sasa katika soko la kimataifa, ni muhimu kufuatilia maendeleo yoyote kila mara na kutambua njia tofauti zilipo na ambazo zitafaa katika hali nchini Kenya
c. Elimu inapaswa kupangwa na kuwasilishwa kwa njia ambayo itachangia katika jukumu la kuondoa mwelekeo hasi uliopo kuhusu kazi na bidhaa zilizotengenezwa humu nchini.
d. Mielekeo ya kikoloni inapaswa kuondolewa katika vitabu vinavyotumiwa kufunza shuleni.

e. Njia zinapaswa kuwekwa kuhakikisha kuwa elimu ya kiufundi na mipango ya mafunzo inatekelezwa bila kuchelewa ikiwa malengo ya kiteknolojia na ustawi wa kiviwanda wa haraka yataafikiwa.
f. Kuna haja ya kuimarisha ujuzi unaokubalika wa teknolojia ya kinyumbani za humu nchini ili kuimarisha uwezo wa nchi wa kupokea na kufuata ujuzi wa kigeni.
g. Serikali inapaswa kufanikisha ukuaji wa utamaduni wa kiteknolojia kwa kufanikisha mafunzo ya kiufundi, ikiwezekana hadi kiwango cha Chuo Kikuu.
h. Taasisi za kiwango cha kati zinapaswa kuimarishwa ili ziweze kutoa wafanyikazi wanaohitajika.
i. Mtalaa wa mafunzo katika taasisi za kiwango cha kati unapaswa kuundwa upya ili uweze kuendelza biashara na ajiria ya kibinafsi.
j. Serikali inapaswa kuhakikisha kuwa mbinu husishi zaidi zinawekwa kati ya viwanda na taasisi za mafunzo kuhakikisha kuwa mafunzo ya kiufundi yanakuwa ya kufaa na yanayostahili.
k. Wakati mtalaa unapotathminiwa, mitihani inapaswa kufanyiwa marekebisho ili kuweka mkazo kwenye kuendeleza vipawa, fikra ubunifu, na kuendeleza dhana ya kubuni mambo mapya.
l. Teknolojia ya jadi ni muhimu; kwa hivyo serikali inapaswa kuiendeleza kupitia elimu, mafunzo na utafiti kama msingi wa ukuaji haraka wa uchumi na ustawi wa kiviwanda.
m. Wafanyikazi wanaotoa mafunzo wanapaswa kufunzwa ipasavyo na kupewa mafunzo ya kila mara baada ya kufuzu.
n. Serikali inapaswa kuwatambua Wakenya walio na vipawa kwa kuwapa motisha kupitia usaidizi kifedha. Kama vile kuwapa mikopo na/au kuwaendeleza wao wenyewe pamoja na ubunifu wao.

**(iii) Kuhusu Utafiti**

a. Kunapaswa kuwepo ushirikiano thabiti na wa karibu zaidi kati ya sekta ya umma na taasisi za utafiti na sekta na kibinafsi ili kuimarisha matumizi ya matokeo yake ya utafiti katika sekta ya viwanda ya humu nchini.

b. Serikali inapaswa kutoa motisha kwa sekta ya kibinafsi ili kuimarisha ufadhili wake na kuiunga mkono sekta hiyo kwa upande wa utafiti na maendeleo katika shughuli zao.

c. Serikali inapaswa kuongeza kiwango cha gharama ya jumla ya utafiti kwa utafiti wa kiviwanda na shughuli za maendeleo na kuweka wazi ufadhili kama huo kwa ushindani kutoka taasisi zote za umma na za kibinafsi za utafiti.

# SURA YA KUMI SITA

# KUSIMAMIA UKATIBA

## 16.1 <u>Agizo la Tume</u>

Swala muhimu katika uundaji wa Katiba ni kuunda miundo na kanuni zitakazofanikisha kuielewa Katiba kwa undani na usimamizi wa ukatiba. Kwa hivyo Sheria ya Marekebisho iliitaka Tume kuchunguza na kutoa mapendekezo kuhusu:

- Tume, taasisi na afisi za kikatiba zilizopo na kuanzishwa kwa nyingine zaidi ili kufanikisha utawala wa kikatiba
- Kuchukua afisi na mfumo wa ………. na uhamishaji mamlaka ulio na hadhi baada ya uchaguzi au vinginevyo.
- Swala jingine lolote muhimu kwa maendeleo ya siku za usoni.

Katika kutekeleza agizo hili, Tume ilichunguza maswala yafuatayo

- Tume za Kikatiba
- Afisi za Kikatiba
- Kuchukua na uhamishaji wa mamlaka.

Maswala mengine ya agizo hili kama vile mamlaka ya kisheria na uwezo wa mahakama, usimamizi wa kikatiba na utaratibu wa kufanya mabadiliko yameshughulikiwa katika sura nyingine.

## 16.2 <u>Tume za Kikatiba</u>

### 16.2.1 <u>Kanuni za Jumla</u>

Tume za kikatiba hutekeleza jukumu muhimu sana katika mfumo wowote wa kikatiba.

Vyombo hivi, kila kimoja *kivyake* hutafuta kulinda na kutekeleza kanuni za kikatiba jinsi zilivyo katika Katiba na pia kuhakikisha utekelezaji wake. Ili kuyafanya haya, ni lazima Tume zionekane zikiwa huru kabisa kutokana na uathirifu wa vyombo vya serikali katika kila hali.

Tume za kikatiba zina shabaha na malengo ya jumla ya pamoja. Kwa hivyo katika kushughulikia Tume yo yote ya kikatiba ni lazima izingatie kanuni pana zifuatazo, ambazo kwazo mapendekezo ya kuzihusu Tume zote hufanywa.

Kwanza ni uhuru. Tume ya kufaa ni ile ambayo inaweza kutenda mambo yake kwa njia iliyo huru na serikali, na siasa ya vyama, vyombo na hali zingine zote ambazo zinaweza kuathiri kazi zake.

Uhuru wa Tume unategemea mambo kadha:

- Namna ya kuundwa
- Uhuru wa kifedha, na
- Taratibu za kuteuliwa na kuondolewa.

Pili ni ufafanuzi wa uwezo na majukumu. Ni lazima haya yawe wazi. Hili litazuia kuingiliana kwa majukumu ya Tume na kuhakikisha kuwa Tume zinachangiana bali hazibishani moja kwa nyingine. Sheria inayounda Tume lazima pia ihakikishe kuwa Tume hiyo inaweza kutekeleza majukumu yake vizuri.

Tatu ni kufikika. Ni muhimu kanuni zinazounda Tume zibainishe watu ambao wanaweza kuweka madai kwa Tume. Hii inaweza kuwa ama watu binafsi ambao wamedhulumiwa, watu wa familia kwa niaba ya mdhulumiwa, mashirika yasiyokuwa ya serikali au makundi yaliyodhulumiwa. Isitoshe, taratibu za kuweka madai kwa asasi ziwe rahisi za wazi na zisizokuwa na vizuizi. Hali ya kutamanika ingekuwa pale ambapo mdhulumiwa atahitaji tu kuweka madai kwa matamshi.

Nne ni uwajibikaji. Suala hili hushughulikiwa kupitia majukumu ya kutoa taarifa. Tume zinawajibika kutoa taarifa zenye undani wa maelezo kuhusu shughuli zake kwa bunge na/au serikali kupitia Rais ili zishughulikiwe. Tume inatakikana kuwajibika kwa umma. Ni lazima taarifa zao ziwe wazi kwa uhakiki wa umma.

### 16.2.2 Tume za Kikatiba katika Katiba ya sasa

Katiba ya sasa inaweka Tume zifuatazo za kiKatiba:

- Tume ya Uchaguzi
- Tume ya Huduma za Bunge
- Tume ya Huduma za Mahakama, na
- Tume ya Huduma za Umma.

Ingawa zimewekwa na Katiba na kuungwa mkono na sheria ambatano ambazo hubainisha uwezo na majukumu yake, nyingi ya Tume hizi hazifurahii uhuru kutokana na kitengo cha Serikali cha Mamlaka. Uteuzi hufanywa na Rais,

kuondolewa huanzishwa na Rais, na fedha zao zinadhibitiwa na wizara za serikali.

### 16.2.4 Waliyoyasema Wananchi

Wananchi walikuwa na mengi ya kusema kuhusu Tume za kikatiba, mamlaka na majukumu yao, namna ya kuanzishwa, na ufadhili wao wa kifedha. Maoni haya yameelezwa kimuhtasari ifuatavyo:

**(i)** *Kuhusu Tume kwa Jumla kuwa* **-**

(a) Tume ziwe na mamlaka na majukumu yao yakielezwa wazi katika sheria inayoziweka au inayoziunda

(b) ziwe huru

(c) ziwe na uwezo wa kutekeleza mapendekezo yao

(d) panapohitajika, zipewe mamlaka ya kufanya mashtaka.

(e) zipewe nguvu za kutekeleza sheria katika sekta mbalimbali za serikali.

(f) zifuate kanuni zilizowekwa katika utekelezaji wa shughuli zake

(g) zijitoe kwa dhati kulinda haki za raia

(h) wenyeviti wa Tume hizi wawe na usalama wa awamu za afisini

(i) majukumu yao ni kuwaleta wananchi pamoja katika maeneo yao tofauti ya utendajikazi ili kutambulisha, kuunganisha, na kuamua

kuhusu habari na jamii ili kuziwezesha kufanya maamuzi ya kufahamika.

(j) Ziwe na mipango ya habari za umma na masomo katika maeneo yao.

*(ii) Kuhusu Tume Zilizopo kuwa -*

(a) Tume ya Huduma za Umma iagizwe kuondoa -

- ufisadi, ubaguzi na upendeleo wa ndugu katika uajiri ukosefu
- wa uwazi katika taratibu za kuajiri
- utangazaji wa kazi usiokuwa wa dhati
- upandishaji cheo usiokuwa wa haki
- ulazima wa kustaafu usiokuwa na utu

(b) Tume ya Uchaguzi iwe na wafanyakazi ambao ni Wakenya walioelimika na ambao wameteuliwa na Bunge bali si Kitengo cha Mamlaka, na

(c) Tume ya Huduma za Mahakama:

- iwe na wanachama wake ambao wanatokana na jamii ya wanasheria, majaji na vyombo vya wataalamu, wahubiri na makundi mengine yanayohusika
- uteuzi katika Tume utafanywa na Rais baada ya Bunge, kupitia kamati ya bunge ya mahakama, kuidhinisha.
- Tume itashughulikia masuala ya nidhamu.

*(iii) Kuhusu uanzishaji wa Tume Mpya kuwa -*

(a) Tume mpya zifuatazo zianzishwe

- Tume ya Haki za Bindamu na Utekelezaji wa Haki,
- Tume ya Maadili na Uaminifu,
- Tume ya Mishahara na Marupurupu,

- Tume ya Jinsia,
- Tume ya Malalamishi ya Vikosi vya Majeshi.

(b) Walipoulizia Tume ya Haki za Binadamu na Utekelezaji wa Haki, wananchi walipendekeza kuwa -

- iwe mlinzi dhidi ya maovu mengi yaliyopo dhidi ya haki za binadamu;
- ihakikishe ulinzi, maendeleo na utimizaji wa haki za binadamu;
- ichunguze madai ya ukiukaji wa haki za binadamu;
- ifanye mipango ya kuwaelimisha wananchi kuhusu haki zao;
- ishughulikie mapigano ya ardhi ya 1991-1997;
- ishughulikie ukiukaji wa haki za binadamu wa nyakati zilizopita;
- ishughulikie mauaji yaliyopita ya wanasiasa;
- ichunguze na kuzingatia maovu ya kihistoria miongoni mwa wafugaji wa kuhamahama katika mkoa wa kaskazini mashariki wakati wa ukoloni na katika kipindi kilichopita cha ukoloni;
- ikuze mazungumzo na usuluhishaji wa mizozo kwa njia ya amani kupitia upatanishi na uwakilishi;
- ishughulikie hali za kupoteza ardhi na kuondolewa katika ardhi;
- ishughulikie uwakilishi mbaya wa kisiasa na dhuluma;
- ishughulikie maonevu ya kijamii na kiuchumi kama vile ukabila, ufisadi, na kupendelea undugu uliotendwa dhidi ya Wakenya tangu nyakati za ukoloni; na
- iwaandame wale ambao wameiba fedha za umma tangu 1963 na kuhakikisha kuwa wanaweka masharti.

( c) Walipoulizia Tume ya Jinsia, wananchi walipendekeza kuwa:

- Tume iunde sera ya kulinda na kukuza haki za wanawake na kutekeleza uondoaji wa sheria ambazo zina kanuni za ubaguzi wa kijinsia;
- Sheria nyingi za kitamaduni na matendo ambayo yanawabagua wanawake kwa jumla na hasa mtoto wa kike zifutiliwe.

(d) Katika kuulizia Tume ya Malalamishi ya Vikosi vya Majeshi wananchi walisema kuwa -

- maafisa wa polisi wasiofuata taratibu za kisheria wafutwe;
- watuhumiwa wasiuawe kabla ya kufanyiwa mashtaka kwa sababu mtu huchukiliwa kutokuwa na hatia mpaka ithibitishwe kuwa ana hatia;
- maafisa wenye ufisadi washtakiwe;
- pawe na kikosi maalum katika polisi cha kuchunguza ufisadi;
- polisi na wengine katika vikosi vya majeshi wasiwe na mapendeleo ya kisiasa;
- Kamishna wa polisi awe huru na ateuliwe na Rais kufuatia idhini ya Bunge;
- Watu wanaodhulumiwa kutokana na ukatili wa polisi au wale wanaoteswa na polisi walipwe fidia;
- pasiwe na kushika watu kiholela na watuhumiwa wafehamishwe sababu za kushukwa;
- pasiwe na msako wa kiholela katika mijengo na wanaohusika wapewe vibali vya kusaka;
- hatua ichukuliwe dhidi ya maafisa wa polisi ambao hushiriki katika vitendo vya uhalifu au wanasaidia au wanaruhusu utekelezaji wa hatia.

(e) Katika kuulizia Tume ya Maadili na Uaminifu, wananchi

walipendekeza kuwa -

- Tume huru Dhidi ya Ufisadi iundwe na ishinikizwe katika Katiba;
- Mamlaka Dhidi ya Ufisadi nchini Kenya yafufuliwe;
- Paanzishwe Tume ya Maadili;
- pawe na kamati za kupinga ufisadi ambazo wanachama wake watachaguliwa na watakuwa na usalama wa awamu uliowekwa awali. Wanachama hawa watatoka mashirika ya kidini, ya kitawala na kitaaluma.

(f) Katika kuuliza Tume ya Mishahara na Marupurupu, wananchi walikubali kuwa na:-

- Uamuzi wa mishahara ya wafanyikazi wa serikali na wafanyakazi wa sekta ya umma ili kuzuia ufisadi na matukio ya migomo
- Kuchunguza marupurupu, mishahara na masharti ya kazi ya wabunge
- Kuchunguza mishahara kila baada ya miaka mitatu
- Kutoa malipo ya uzeeni kwa wafanyikazi waliostaafu
- Kuchunguza masharti ya kazi ya wafanyikazi wa mabaraza ya wilaya na mabaraza ya miji

### 16.2.5 Uchanganuzi

Wananchi wengi wa Kenya wanaonelea kuwa tume za kikatiba ni njia ya kuondoa ufisadi, ubaguzi, dhuluma katika utafutaji wa kazi, ukatili na unyanyasaji wa polisi, ukiukaji wa haki nyinginezo za binadamu. Hata kama watu hawa walikuwa na imani kubwa kuhusu njia hizi, uchunguzi wao kuhusu sera ya Kenya ulikuwa sahihi. Zaidi, Tume ilipokea taarifa asili kuhusu maovu mengi katika kazi zote za Serikali na umma.

### 16.2.6 Mapendekezo

Tume inapendekeza kwamba –

(i) ubunifu wa Tume za kikatiba ni sharti ufuate kanuni zifuatazo -

**(a) Mfumo wa ubunifu**

- Tume za kikatiba zilizopendekezwa ni sharti zibuniwe na katiba na kukubaliwa na sheria.

**(b) Kujitawala kifedha**

- Bajeti ya Tume ni sharti isihusishwe na wizara yoyote ya serikali au idara yoyote.
- Bajeti ya kila Tume ni sharti itayarishwe na wanachama wa Tume na ikabidhiwe bunge ili iidhinishwe
- Tume itawajibika kwa bunge katika matumizi yake.

**(c) Mbinu za uteuzi**

- Idadi ya wanachama wa kila Tume itakuwa tofauti kulingana na utaratibu wa Tume lakini idadi hiyo isizidi kumi
- Wanachama wa Tume watateuliwa na Rais na kuidhinishwa na Bunge kupitia kwa Kamati ya Bunge inayohusika
- Uteuzi wa wanachama ni sharti uzingatie madhehebu mbalimbali kama vile hali ya kiuchumi ya jamii, asili, ukabila, jinsia, dini, umri, kazi, masomo, walemavu na wasiobahatika.
- Wafanyikazi wa Tume ni sharti wateuliwe na Tume kwa ushauriano na Tume ya Huduma kwa Umma.
- Wafanyikazi ni sharti walipwe na Tume inayohusika

**(d) Kigezo na sifa za uteuzi**

- Wanachama wa Tume ni sharti wawe wa uwakilishi na wawe na wawakilishi kutoka miongoni mwa, mashirika yasiyo ya serikali, mashirika ya wafanyikazi, waledi na mashirika ya kidini.
- Kwa ujumla, wanachama ni sharti wawe na elimu inayotambulika katika sehemu inayoshughulikiwa na tume.
- Wanachama sharti wawe watu wenye ufahamu unaotambulika katika uwanja maalum unaoshughulikiwa na tume
- Wanachama wa Tume wa Kudumu wasiwe na kazi nyingine zaidi na ya tume hiyo
- Wanachama ni lazima watii masharti ya kanuni za uongozi.

**(e) Muda wa uteuzi**

- Uteuzi utakuwa wa muda wa miaka mitano
- Muda wa uteuzi unaweza kuongezwa mara moja
- Muda wa kustaafu uwe miaka sitini na mitano

**(f) Kuwachishwa kazi kwa wanachama**

- Kufutwa kazi kunaweza kusababishwa na utovu wa nidhamu, kutohitimu au kutokuwa na uwezo wa kutekeleza majukumu kwa sababu ya udhaifu wa mwili au akili
- Suala la kufutwa kazi kwa mwanachama ni sharti liwasilishwe kwa kamati ya Bunge ambayo itachunguza na kuamua kumwachisha kazi mwanachama au kumwacha.

**(g) Majukumu na uwezo**

- Kwa ujumla, tume zote ni sharti ziwaelimishe wananchi kuhusu majukumu, kusudi na wajibu wao.
- Tume ni sharti ziwe na uwezo wa kufanya uchunguzi
- Tume ni sharti iwe na uwezo wa kuwaita mahakamani watu wenye mamlaka, watu binafsi au mashirika
- Masharika au watu wanaochunguzwa ni lazima watoe habari zinazohitajika kwa kusema au maandishi.
- Endapo kuna kutotekeleza masharti, tume itakuwa na uwezo wa kumpeleka mtu au kikundi mahakamani ili kujibu mashtaka ya kutotii.
- Masharika yawe na uwezo unaohitajika kwa upatanishi na kujadiliana kwa minajili ya kusuhuhisha jambo ambalo litakubalika kwa mlalamishi
- Wanachama ni sharti wawe na kinga ya kisheria katika matendo yaliyotendeka wakiwa afisini isipokuwa kama matendo yenyewe yalitendwa kwa nia mbaya.

**(h) Kufikika**

- Malalamishi yanaweza kuwasilishwa moja kwa moja na mlalamishi, familia zao au kikundi kinachopenda kufanya hivyo – kama vile mashirika yasiyokuwa ya serikali.
- Malalamishi yanaweza kuwasilishwa kwa mdomo au kwa maandishi bila kuzingatia kanuni zozote za lugha au mbinu.

- Ni lazima tume iweze kuanzisha uchunguzi au kutafuta habari kwa juhudi zao.
- Matawi ya tume sharti yabuniwe katika ngazi za wilaya na mkoa.
- Huduma za tume zitatolewa bila malipo.

**(i) Uwajibikaji**

- Tume ni sharti ziwajibike kwa bunge na Rais
- Ni sharti tume zitayarishe ripoti ya utekelezaji wa shughuli na shabaha zao pamoja na hali yao ya kifedha
- Ripoti maalum zinaweza kutayarishwa zinavyohitajika au zikihitajika
- Taarifa ikiwasilishwa bungeni na kwa Rais, bunge pamoja na Rais ni sharti watoe maoni kuhusu taarifa hiyo wakieleza hatua zilizochukuliwa au kwa nini hazikuchukuliwa.
- Ni sharti bunge litumie kamati zake kuchunguza taarifa kwa undani

**(ii) Tume zifuatazo zibuniwe**

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala wa haki ihusishe:

- Wakili wa umma
- Kamishna wa Haki za Binadamu

Kamishna wa jinsia na maagizo ya kimsingi ili:-

- Achunguze na abuni taswira kamili kuhusu, hali sababu na kiwango cha ukiukaji wa haki za kibinadamu uliotekelezwa
- Kutoa fursa kwa wahasiriwa na familia zao kueleza matukio hayo mahakamani au njia nyingine
- Kujadili swala la kutoa msamaha kwa watu waliohusika na wakaeleza matukio yaliyohusiana na makosa yao.
- Kutoa mapendekezo ya ulipaji fidia na kuwawezesha kuishi maisha ya kawaida wahasiriwa au familia za wahasiriwa.
- Kupendekeza mbinu za kurudisha hadhi ya utu na ya umma kwa mhasiriwa
- Kuwasilisha matukio yao kwa Taifa
- Kueneza heshima ya usawa wa jinsia
- Kuchunguza na kusuluhisha malalamishi ya kijinsia
- Kushiriki katika uundaji wa sera za kitaifa za kiuchumi na kusimamia utekelezaji wa sera hizo kuhusiana na jinsia na maendeleo.
- Kuunda utaratibu na kushauri kuhusu ubunifu na kuzipa nguvu njia/asasi ambazo zinaendeleza usawa wa jinsia katika nyanja zote za maisha hasa katika elimu, ajira na rasilimali za umma.
- Apange, asimamie na aratibishe mipango ya elimu ili kuhamasisha umma na kuunga mkono masuala ya kijinsia.
- Kushirikiana na wizara za serikali na idara zinazohusiana na masuala ya jinsia.

- Kushauri serikali kugawanya rasilimali kuhakikisha mwelekeo wa kijinsia
- Asimamie, atathmini sera, atekeleze na ashikilie sheria za taifa na kimataifa kwa -
  - Viungo vya serikali katika viwango vyote
  - Mabaraza yaliyokubalika kisheria
  - Mabaraza ya umma, biashara na asasi
  - Mabaraza ya kibinafsi biashara na asasi
- Kupokea na kuchunguza malalamishi kuhusu nidhamu ya maafisa wa kujeshi n.k. kuhusiana na mambo kama unyanyasaji, uzembe na ushiriki mbaya katika kusuluhisha mambo.
- Kuchunguza na kupatanisha malalamishi kwa njia bora
- Kuandaa mafunzo ya umma kuhusu majukumu ya polisi na majukumu ya wananchi.
- Kutoa amri kuhusu kutolewa kwa nyaraka zinazohitajika
- Kutoka kutoa habari kamili kama inavyohitajika
- Kutaka mtu ama kikundi cha watu kujiwasilisha mbele ya mahakama kwa kutotii kwa kukosa kuhudhuria au kukosa kutoa habari inayohitajika au habari kamili
- Kupendekeza kushtakiwa au kuadhibiwa kwa afisa wa polisi
- Kuamrisha kutolewa kwa fidia wahasiriwa wa mateso ya polisi na unyanyasaji
- Kutoa huduma zinazifikika na urekebishaji wa tabia.

- Kuboresha hali ya ustadi, uaminifu, heshima na uwazi katika huduma zinazotolewa na umma.

**(b) Tume ya Huduma kwa Umma na maagizo ya kimsingi ili-**

- Ihusishe si huduma ya umma pekee bali pia polisi, walimu na wafanyikazi wa bunge
- Ihusishe jukumu la kuangalia upya vipengele mbalimbali vya huduma ya umma na kuwasilisha mapendekezo hayo bungeni na kwa Rais
- Wafanye uteuzi kwa ushauriano na sekta za huduma ya umma zinazohusika
- Iwe na wanachama kati ya wanane na kumi waliochaguliwa katika sekta mbalimbali

(c) Tume ya Uchaguzi iliyo na majukumu sawa na yale yaliyopo katika katiba

(d) Tume za Huduma ya Mahakama huundwa kama zifuatazo:

- Jaji aliyechaguliwa kutoka Mahakama ya Juu na majaji wa mahakama hiyo
- Jaji aliyechaguliwa kutoka Mahakama ya Rufani na Majaji wa Mahakama hiyo
- Jaji aliyechaguliwa kutoka Mahakama Kuu na majaji wa mahakama hiyo
- Kadhi Mkuu
- Mahakimu wawili kutoka Mahakama za Chini zilizoteuliwa na shirika au mashirika yoyote yanayowakilisha mahakimu

- Mawakili wawili walioteuliwa na shirika la wanasheria la Kenya kuwakilisha shirika
- Watu wa kawaida wa umma walioteuliwa na wanachama waliotajwa hapo juu katika mkutano wao wa kwanza
- Wanachama wawili waliochaguliwa na vitivo vya sheria vya vyuo vikuu vya Kenya
- Mwanachama atakayewakilisha Tume ya Huduma kwa Umma.
- Mwanasheria Mkuu atakayekuwa mwanachama kwa sababu ya wadhifa wake na atakayekuwa na mamlaka ili
- Kuchunguza upya kutayarisha na kuchunguza malalamishi dhidi ya mahakimu na majaji yaliyowasilishwa na umma au shirika lolote linalowakilisha mahakimu. Kwa sasa mkuu wa sheria pekee ndiye anayeweza kuwasilisha uchunguzi dhidi ya majaji
- Kuanzisha uchunguzi dhidi ya majaji na mahakimu kwa hiari yake
- Kuratibu mfululizo wa elimu na mafunzo ya maafisa wote wa mahakama
- Kushauri serikali kuboresha utawala wa haki na kupatikana haki
- Kupendekeza kwa Rais kuhusu uteuzi wa Jaji Mkuu na majaji

**(e) Tume ya jamii na maadili yenye maagizo kimsingi ili :-**

- Itilie mkazo kanuni za uongozi ili kuzuia ufisadi
- Kuhakikisha kwamba maafisa wote (wale wanaoshikilia afisi kikatiba, maafisa wa tume zote na wabunge). Wametangaza mali yao na ya wake au waume wao.

- kati ya miezi mitatu ya kuanzishwa kwa kanuni hiyo
- kati ya miezi mitatu ya kuchukua mamlaka
- baadaye, baada ya kila mwaka
- kufuata kanuni zinaweza kuzuia utekelezaji wa uaminifu, uadilifu na maadili ya maafisa – mwenendo huo utashughulikiwa kisheria.

- Kuweka mbinu zifaazo zenye lengo la kuzuia ufisadi
- Kuchunguza shughuli na mipango ya mashirika ya umma kuhakikisha hayatoi fursa ya kuwepo kwa ufisadi
- Kuelimisha umma kuhusu hatari za ufisadi

**(f) Tume inayoshughulikia mishahara na marupurupu**

- Mishahara, marupurupu na kiinuamgongo kwa maafisa ushikilizi mamlaka kikatiba na wananchama wa tume za kikatiba akiwepo: Rais, makamu wa Rais, Waziri mkuu, mawaziri, manaibu wa mawaziri, mahakimu, Mwanasheria Mkuu, Mkurugenzi Mkuu, Mwendeshaji Mashtaka ya umma, Mkurugenzi mkuu, Mkaguzi wa Hesabu na maafisa wote wa tume.
- Mishahara, kiinuamgongo na marupurupu ya wabunge
- Mishahara, kiinuamgongo na marupurupu ya watumishi wa umma na wale wa mashirika ya serikali.
- Kiinuamgongo kwa maafisa walioorodheshwa katika (1-111) hapo juu.

**(g) Tume ya Kikatiba yenye majukumu ya kimsingi ili -**

- Kuhakikisha masharti ya kikatiba yanayohitaji kushughulikiwa kisheria na kiutawala yametekelezwa kulingana na mfumo uliowekwa katika masharti ya mpito kwa njia na wakati unaofaa.
- Kufanya kazi kwa ushirikiano na viongozi wa Tume za kikatiba na washikilizi mamlaka kuhakikisha masharti ya ulinzi wa katiba yamefuatwa.
- Kuhakikisha kuwa shughuli za katiba zinachunguzwa upya kila wakati
- Kupendekeza kuhusu sheria au mbinu za utawala kuhakikisha maadili ya katiba
- Kuripoti kuhusu mapendekezo ya marekibisho ya katiba kabla au baada ya mswada kuwasilishwa na kwa sababu hii watafute maoni ya umma.
- Kushauriana mara kwa mara na Rais ambaye jukumu lake kuu kulingana na mapendekezo yetu ni kulinda katiba.
- Kuripoti mara mbili kwa mwaka kwa umma kupitia bunge kuhusu maendeleo ya utekelezaji na kueleza matatizo maalum yanayozuia kutekelezwa kwa katiba.
- Wanachama watano waliochaguliwa na Rais na kuidhinishwa na bunge na kuwahusisha watu wanaohusiana na utawala, uchumi, siasa, utamaduni na maadili ya jamii. Itapewa mamlaka ya kuajiri washauri na kuunda kamati zinazohusisha watu kutoka nje.

## 16.3 Afisi za Kikatiba

### 16.3.1 Kanuni za Kimsingi

Malengo na shabaha na Tume za kikatiba kama zilivyoelezewa zinaruhusu kuundwa ofisi za kikatiba na washikilizi wa afisi hizo na wana ulinzi wa kazi wakati wa kipindi chao.

### 16.3.2 Afisi za kikatiba katika katiba ya sasa

Licha ya kuundwa kwa afisi za kikatiba sehemu ya kisheria au vuingo vya mamlaka ya serikali, katiba itaunda nyadhifa zifuatazo.

- Jaji mkuu
- Majaji wa Mahakama ya Rufani
- Majaji wa Mahakama Kuu
- Kadhi Mkuu
- Makadhi
- Mwanasheria Mkuu
- Kamishna wa Polisi
- Msimamizi na Mkaguzi mkuu wa Hesabu
- Makatibu wa Kudumu
- Mabalozi
- Karani wa Baraza la Mawaziri
- Mkurugenzi wa Uajiri (Ajira)

Kama sheria ya kimsingi, wanaoshikilia mamlaka wanapaswa kutekeleza majukumu yao bila kutatizwa na mtu yeyote. Hata hivyo, ni vigumu kufanya hivyo hapa Kenya ambapo Rais ana mamlaka makuu kuhusu viungo vyote vya serikali.

Ni muhimu kutambua kuwa katiba haisemi lolote kuhusu sifa zinazohitajika kwa kuteuliwa kama Jaji Mkuu. Katika Mahakama kuu na Mahakama ya Rufani majaji wanapaswa kuwa na sifa zifuatazo:-

- Awe amepata kuwa jaji wa mahakama na kuwa na uwezo usio na mipaka katika sehemu yoyote ya jumuia ya madola au katika Jamhuri ya Ireland au katika mahakama iliyo na mamlaka ya rufaa kutoka mahakama hiyo.
- Ni lazima awe wakili mahakama kuu kwa muda usiopungua miaka saba.

Kuhusu Kadhi Mkuu, na Kadhi, Katiba imeeleza wazi kuwa ni lazima awe:-

- Amekiri dini ya Kiislamu, na
- Awe na elimu ya sheria za Kiislamu kuthibitishia tume ya huduma za mahakama.

Mwanasheria Mkuu ni lazima awe:-

- Mtu aliyefuzu kuteuliwa kuwa jaji wa mahakama kuu. Hakuna kitu kilichozungumziwa kuhusu sifa zinazohitajika kwa mtu kuteuliwa kama Kamishna wa Polisi, Msimamizi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, katibu wa kudumu, karani wa baraza la mawaziri, balozi au mkurungezi wa uajiri.

### 16.3.3 Afisi za Kikatiba katika Katiba Nyingine

### 16.3.4 Waliyosema Wananchi

Watu wengi walilalamikia kuhusu upendeleo na ukosefu wa uhuru katika kutekeleza majukumu na washikilizi wa afisi za kikatiba. Wanachama wa mahakama walilalamika kuhusu mambo hayo. Kwa muhtasari walisema –

*(i)* *Kuhusiana na mahakama kuwa:*

(a) Jaji mkuu ateuliwe na Rais kwa idhini ya bunge

(b) Tume kwa Huduma za Mahakama iteue majaji kwa idhini ya bunge

(c) Ni lazima jaji mkuu awe na shahada ya chuo kikuu ya sheria na awe na tajriba isiyopungua miaka kumi kama jaji wa mahakama kuu

(d) Ni sharti maafisa wa mahakama wawe na usalama wa kazi zao

(e) Maafisa wa mahakama wapaswa kustaafu kati ya miaka 55 na 65

(f) Kanuni za maadili ziundwe kusimamia majaji.

(g) Maafisa wa mahakama wafisadi sharti wapigwe marufuku, wasimamishwe au kushushwa vyeo wakati wa kuchunguzwa.

*(ii) Kuhusu Mwanasheria Mkuu, afisi yake:-*

(a) isiingilie majukumu ya Mwendeshaji Mashtaka huru, mbunge au ya watu wenye mamlaka serikalini.

(b) haiwezi kutekeleza majukumu yake ya kushtaki kwa sababu ya ushawishi wa watu wenye mamlaka.

(c) haitekelezi majukumu yake vizuri ikiingilia mambo ya kibinafsi

(d) haiwezi kufurahia uhuru wake kwa sababu Mwanasheria Mkuu huteuliwa na Rais moja kwa moja na ni mwanachama wa Baraza la mawaziri na anatakikana kutekeleza yale yalipopitishwa na baraza la mawaziri.

(e) Isiingilie mashataka yaliyoanzwa kibinafsi.

(f) Isiingilie siasa katika mashtaka kuhukisha kuna haki inayotekelezwa

(g) Ihakikishe kuwa mashtaka yote yameongozwa na wanasheria waliohitimu.

*(iii) Kuhusu Kadhi Mkuu, Makadhi na Mahakama ya Kadhi kwamba:-*

(a) ni lazima washauriane na Waislamu kuhusu kuteuliwa kwa Kadhi mkuu na makadhi wengine. Wanapaswa wawachague au wateuliwe na Tume ya Huduma kwa Mahakama. Mashirika ya kiislamu kama 'SUPKEM' ni sharti yahusishwe

(b) Kadhi Mkuu na makadhi ni sharti wawe na shahada kuhusu sheria na sheria ya kiislamu kutoka chuo kikuu kinachotambulika

(c) Mahakama ya Kadhi ipewe mamlaka ya kushughulikia kazi zake na kupanga ratiba za shughuli zake. Ishughulikie masharti ya kuajiri kama mishahara, wafanyikazi, vyombo vya mawasiliano n.k.

(d) Kadhi Mkuu apewe hadhi kama ya jaji wa Mahakama kuu na kadhi kama hakimu mkuu.

(e) Idadi ya mahakama ya kadhi iongezwe na iwe katika kila mkoa na wilaya

(f) Mahakama ya kadhi iwe na mahakama yake ya rufani na rufaa yoyote isipelekwe mahakama kuu

(g) Majaji wa kiislamu ambao ni wataalamu wa sheria ya Kiislamu wateuliwe katika Mahakama Kuu ili wasikilize rufaa kutoka mahakama za makadhi

(h) Mahakama ya kadhi ipewe uwezo wa kuamua. Uthibitisho na utaratibu wa sheria zinazohusu urithi – katika jamii ya Kiislamu

(i) Mahakama ya Kadhi ipewe mamlaka kamili kushughulikia talaka katika ndoa za Kiislamu na mambo yanoyoandamana na talaka kama vile kuwakimu na kuishi na watoto, ulezi, kutwaa watoto, kugawa mali baada ya talaka na mambo yanayohusiana na matukio haya.

(j) Kwa sababu makamishna wa wakfu ambao huteuliwa chini ya sheria ya Makamishna na Wakfu wameshindwa kusimamia mali iliyowekwa wakfu, chini yao kuwatosheleza mahitaji ya wanaotegema, na hawajaonyesha uwazi na uwajibikaji, zapaswa kuvunjiliwa mbali na badala yake uwezo huo ipewe mahakama ya kadhi katika wilaya ambazo tume hiyo ilihudumu sheria ya wakfu ishirikishe sehemu zote za nchi na si mkoa wa pwani pekee.

(k) Kila kadhi lazima awe na msaidizi mwanamke kushughulikia masuala nyeti yanayohusu wanawake.

(l) Uwezo wa Mahakama ya Kadhi uongezwe ili kushughulikia masuala ya umma na ya viwanda, yanayohusu Waislamu

(m) Ijapokuwa Mahakama ya Kadhi ina majukumu ya kimsingi kikatiba kutumia sheria ya Kiislamu katika mahakama yao, sheria hiyo haijatekelezwa vizuri kulingana na ukosefu wa asasi za kisheria zenye mfumo mzuri zilizopitishwa kisheria na mbinu za utekelezaji.

(n) Kazi ya Kadhi iwe ni ya kisheria pekee na waislamu wachague wao wa kiroho ambaye atakuwa msemaji wao rasmi na mshauri wa serikali kuhusiana na masuala ya Kiislamu nchini Kenya.

(o) Makadhi na Kadhi Mkuu sharti wasijihusishe na mambo yoyote yanayohusiana na sherehe za Idd na mambo yoyote yasiyohusiana na kazi za mahakama.

(p) Mahakama ya Kadhi yabadilishwe jina yaitwe Mahakama ya Sharia ya Kiislamu. Irejelee sheria ya Mohammed iitwe sheria ya Kiislamu au Sharia.

(q) Sheria ya Kiislamu ifunzwe katika vyuo vikuu na sheria za kibinafsi za Waislamu ziidhinishwe kuwa sheria kamili.

(r) Waislamu wa dhehebu la Shia pia wateuliwe kuwa makadhi ili kushughulikia mahitaji ya waislamu wa Shia.

Ukuu wa sheria ya kibinafsi ya Kiislamu dhidi ya sheria zote za Kiislamu kuhusiana na masuala ya kibinafsi ni sharti isisitizwe.

### 16.3.4 Uchanganuzi

Kinga ya maafisa washikilizi wa afisi za kikatiba ni muhimu kwa utawala wa utaratibu wa kikatiba kuna umuhimu basi kuchunguza muundo na wahusika katika afisi hizi za kikatiba. Tume ilipendekeza kama ifuatavyo.

### 16.3.5 Mapendekezo

Tume inapendekeza kuwa :-

(i) *Zaidi ya afisi za kikatiba, katiba pia iunde zifuatazo* -

- (a) Mkurugenzi Mkuu Mwendeshaji mashtaka ya umma
- (b) Wakili wa Umma
- (c) Msimamizi wa bajeti
- (d) Mkurugenzi mkuu na Mkaguzi wa Hesabu
- (e) Gavana na naibu wa Gavana wa Benki Kuu ya Kenya
- (f) Mkurugenzi wa Huduma ya Urekebishaji
- (g) Mkurugenzi wa Shirika la Takwimu
- (h) Mkurugenzi wa Huduma ya Polisi

*(ii) Jaji Mkuu na Majaji*

(a) Ateuliwe na Rais kwa mapendekezo ya Tume ya Huduma kwa Mahakama kwa ushauriano na Kamati ya Bunge inayoshughulikia masuala haya.

(b) Kuhusu Jaji Mkuu

- Ni lazima awe amefanya kazi kama jaji katika mahakama kuu au mahakama ya juu kuliko hii kwa muda usiopungua miaka kumi na miwili au amefanya kazi kama wakili kwa muda kama huo au
- Awe amefanya kazi kama Jaji wa Mahakama akiwa na uwezo usiokuwa na mipaka kuhusu mambo kesi za umma na kesi za jinai
- Awe amefanya kazi kama mwalimu kamili wa sheria kwa muda wa miaka kumi na miwili.

*(iii) Kutokana na jaji*

- Ni lazima awe amefanya kazi kama jaji wa mahakama akiwa na uwezo usiokuwa na mipaka kuhusu kesi za umma na kesi za jinai kwa muda usiopungua miaka saba,
- Amefanya kazi kama hakimu kwa muda usiopungua miaka saba

- Awe amefanya kazi kama wakili mhudumu kwa muda usiopungua miaka saba.
- Anaweza kuachishwa kazi kwa kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa sababu ya ulemavu wa mwili au akili, utovu wa nidhamu, ufisadi au kutokuwa na ujuzi wa aina hiyo na kumfanya kutoweza kushikilia afisi ya mahakama.
- Malalamishi yanaweza kupelekwa kwa Tume ya Huduma ya Mahakama – haya yanaweza kutolewa na watu binfasi, makundi au mashirika, na yakiwa na msingi, malalamishi haya yatachunguzwa na baraza la majaji maarufu watakaosikiliza malalamishi hayo. Rais atateua baraza hilo kati ya muda wa siku 30 baada ya kupokea mapendekezo.
- Kama jaji anachunguzwa na baraza la mahakama, tume inayoweza kumfukuza jaji bila kupoteza kiinuamgongo na marupurupu kwa muda wa uchunguzi na kusikizwa.

*(iv) Mkurugenzi Mkuu Mwendesha Mashtaka*

(a) awajibike kuhusu uchunguzi wa jinai na mashtaka

(b) ateuliwe na Rais kufuatana na mapendekezo ya Tume ya Huduma za umma na kuidhinishwa na kamati ya bunge inayohusiana na maswala ya kisheria na kikatiba.

(c) Awe na sifa kama za jaji wa mahakama kuu.

(d) Awe na kinga ya kazi yake na anaweza kuondolewa kwa sababu kama zile za jaji wa mahakama kuu

(e) Ahakikishe kama zile za jaji wa mahakama kuu

(f) Ahakikishe kuwa mashtaka katika mahakama zote nchini Kenya yanaendeshwa na watu waliohitimu kisheria wakifanya kazi kwa kufuata maongozi ya Mkurugenzi Mkuu Mwendesha Mashtaka

*(v)* *Mwanasheria Mkuu sharti*

(a) atoe ushauri wa kisheria na huduma za kisheria kwa serikali kuhusu swala lolote – mshauri mkuu wa kisheria

(b) kudurusu na kuweka mkataba, mkataa, makubaliano na nyaraka ambazo serikali inahusika au serikali ina shauku na jambo hili.

(c) Kuwakilisha serikali mahakamani au katika kikao cha kisheria ambapo serikali inahusika

(d) Ateuliwe na Rais na kuidhinishwa na kamati ya bunge inayohusika na sheria na masuala ya kikatiba; na

(e) Awe na sifa kama zile za Jaji wa Mahakama Kuu.

*(vi)* *Kadhi Mkuu, Kadhi Mteule na Makadhi*

(a) atakuwa na hadhi, marupurupu na kinga kama za jaji wa mahakama, kadhi mteule kama hakimu mkuu na kadhi kama hakimu mkazi.

(b) Wanasheria waislamu ambao ni wataalamu wa sheria za Kiislamu wateuliwe kama majaji wa mahakama kuu kusikiliza kesi za rufaa kutoka mahakama ya Rufani ya Kadhi

(c) Waislamu nchini Kenya ni lazima washauriwe wakati wa kumteua Kadhi Mkuu na Makadhi kwa kushiriki katika uteuzi kupitia uchaguzi au waakilishi wao.

(d) Kutokana na Kadhi Mkuu

- Ni lazima awe Mwislamu mwenye umri wa miaka thelathini na mitano (35) au zaidi lakini awe na umri wa chini ya miaka sitini na mitano (65).
- Awe wakili wa mahakama kuu au amehitimu kuteuliwa na amekuwa mwanasheria kwa kipindi kisichopungua miaka kumi (10) na
- Lazima awe na shahada kuhusu sheria za kiislamu katika chuo kikuu kinachotambulika au
- Awe na tariba ya sheria za kiislamu isiyopungua miaka kumi (10), amekuwa kadhi kwa muda kama huo na awe na shahada ya sheria za kiislamu kutoka chuo kikuu kinachotambulika

(e) Kutokana na kadhi kama (a) hapo juu kwa njia ya kipekee miaka ya tajriba itakuwa miaka mitano (5) katika kila kikundi.

*(vii)* *Kulingana na maswala muhimu kwenye afisi imependekezwa kwamba*

(a) Katiba mpya itakapoanza kutekelezwa, maafisa wote wa kikatiba ni sharti wakubaliane na masharti haya pamoja na masharti ya sifa na kanuni za uongozi.

(b) Maafisa ambao hawatumizi masharti mapya ya kikatiba au hawajahitimu kushikilia afisi katika masharti ya katiba mpya watalipwa marupurupuru yao, bahashishi, fidia au malipo yoyote yatakayokubalika.

(c) Sheria itatekelezwa kuhusu marupurupu, bahashishi, fidia na marupurupu mengine yoyote kwa washikilizi wa afisi za kikatibu, na itatekelezwa kulingana na sheria iliyopo wakati wa kutolewa kwa marupurupu hayo.

## 16.4 Urithi na Kupokeza Mamlaka

### 16.4.1 Kanuni za Kimsingi

Kwa kutaka tume ichunguze maswala yanayohusiana na urithi na mapokezo ya kisiasa, sheria ya marekebisho ilichunguza mpito kutoka kwa Rais wa sasa hadi kwa mrithi wake. Hili ni jambo ambalo limetatiza Wakenya wengi tangu katiba ifanyiwe marekebisho mwaka wa 1992 na kupunguza muda wa Rais afisini kuwa vipindi viwili vya miaka mitano kwa kila kipindi. Hata hivyo tume imechukua jukumu katika sura nyingine imefuatilia swala hili na mambo muhimu ya upokezaji yanayoshughulikia mpito huu kutoka katiba ya zamani hadi hii mpya.

### 16.4.2 Urithi na upokezanaji wa mamlaka kikatiba

Katiba ya sasa, kwa sababu dhahiri, haizingatii kipengele cha upokezanaji mamlaka. Hata hivyo, katiba hiyo inaelezea suala la upokezanaji wa mamlaka

kutoka kwa Rais mmoja hadi mwingine. Kwanza kabisa, Makamu wa Rais ndiye anayestahiki upokezi wa mamlaka na endapo hawezi kutekeleza jukumu hilo, waziri aliyeteuliwa na Baraza la Mawaziri, atatekeleza jukumu hilo. Hata hivyo, hakuna masharti yatakayomlazimu Rais kuteua makamu wake kufuatia uchaguzi wa Rais, ama nafasi wazi inapotokea kwenye Afisi ya Makamu wa Rais.

Pili, katiba inaeleza kwamba mtu aliyechaguliwa kuwa Rais, atachukua mamlaka mara moja na isipokuwa tu afisi yake ni wazi kwa sababu ya kifo chake, kujiuzulu ama kuacha kutekeleza majukumu yake kwa sababu nyinginezo, ataendelea na mamlaka hayo hadi pale Rais atakayechaguliwa amechukua mamlaka hayo. Kutokana na masharti haya, ni wazi kwamba hapatakuwa na masharti dhahiri kati ya Rais anayeondoka na yule aliyechaguliwa.

Hapatakuwepo, hata hivyo na masharti katika katiba ya muda wa upokezi wa mamlaka ya Urais bali kuandika kwa Makamu wa Rais.

### 16.4.3 <u>Watu Walivyosema</u>

Masuala ya upokezi wa madaraka bila shaka yalikuwemo kwenye mawazo ya wengi waliozungumza na Tume. Watu wengi walipendekeza pamoja na mambo mengine kwamba:

(i) Kama Sheria ya Kimsingi -

- (a) Mbinu mwafaka ya urithi ibuniwe ili kuzuia mikanganyiko pindi Rais anapoaga dunia ama kujiuzulu.
- (b) Makamu wa Rais achukue mamlaka ya Urais kwa kipindi kilichosalia.
- (c) Kuwa na tarehe maalum ya kuapishwa kwa Rais atakayechukua mamlaka baada ya kuchaguliwa.
- (d) Muda maalum wa kuhudumu kama Rais sharti uwe vipindi viwili vya miaka mitano.

*(ii) Kwa hakika, watu:*

(a) Wanataka matokeo ya uchaguzi wa Urais yatangazwe na Tume iliyo huru ya uchaguzi.

(b) Wanapendekeza kwamba matokeo ya uchaguzi yatangazwe kupitia vyombo vya habari. Wakenya wanahitaji uchaguzi wazi bila kutatiza matokeo ya uchaguzi. Wengine walipendekeza kwamba matokeo yatangazwe katika vituo vya upigaji kura na wengine kutaka hayo kufanywa mbele ya wagombea na wawakilishi wao.

(c) Wanataka kutangazwa kwa matokeo ya kura za uchaguzi kwingineko mara moja. Mapendekezo yao walisema kati ya saa 24 hadi siku 90 baada ya uchaguzi huku wengi wa Wakenya wakipendekeza kati ya muda wa saa 24 na siku 30.

(d) Huku wengine wakipendekeza Rais achukue mamlaka ya Urais mara moja, wengine walikuwa na mawazo tofauti na kusema tarehe maalum iteuliwe ambapo Rais ataanza kutekeleza mamlaka hayo.

(e) Hawataki kuacha hofu iwapo Rais mpya aliyechaguliwa na kuhakikisha kwamba nafasi bado ipo rufani ikihitajika hivyo. Hii ndiyo sababu inayowafanya Wakenya kuachwa muda fulani baada ya uchaguzi na kuapishwa kwa Rais.

(f) Wanataka Jaji Mkuu kupewa mamlaka ya kumwapisha Rais mpya, wachache wanataka kazi hiyo apewe Spika wa Bunge, viongozi wa kanisa, mahakama ya Rufaa ama Bunge lenyewe.

(g) Wanataka vyombo vya mamlaka kupokezwa mara moja. Wengine wanafikiria upokezaji zana za mamlaka kutocheleweshа huku wengine wakisema wangependa taratibu zifaazo kufuatwa katika kupokeza zana (mamlaka) hizo.

(h) Wanataka shughuli za kitaifa/sherehe ziandaliwe wakati Rais anayeondoka anapomkabidhi Rais anayeingia mamlaka.

(i) Wanapendekeza njia nyingine rasmi ya kupokeza mamlaka ambapo Tume ya Bunge na Jaji Mkuu au Spika wa Bunge

ataongoza sherehe hizo, huku wengine wakisema kwamba chuo cha uchaguzi kinachojumuisha Tume ya uchaguzi ya Kenya, majaji na watumishi wa umma washuhudie mpito huo.

(j) Wanapendekeza kwamba tarehe maalum za upokezaji na kuapishwa zitengwe katika katiba, na katiba ieleze mbinu za upokezaji huo wa mamlaka.

(k) Wanahitaji taratibu mwafaka za upokezaji mamlaka. Hawataki kupigwa na butwaa kuambiwa ati Rais aliapishwa leo asubuhi. Wanataka njia bora zifaazo zinazokadirika ili mambo yote yawe barabara.

(l) Wanataka Rais aliyechaguliwa kuchukua mamlaka baada ya siku 30. Wengine walipendekeza tarehe maalum itengwe katika katiba na wengine wakasema achukue mamlaka mara tu baada ya uchaguzi.

(m) Wanataka Rais anayeondoka kumkabidhi mamlaka Rais anayechukua wadhfa huo.

(n) Wanataka masharti mwafaka ya kikatiba yatayohakikisha usalama wa Rais wa awali wengine walisema kwamba Rais anayeondoka apewe walinzi kipindi cha mpito.

(o) Hawataki sheria ya kinga kwa Rais wa awali lakini wengine wanafikiria Katiba ishughulikie jambo hilo.

(p) Wanataka katiba ishughulikie maslahi ya marais wa awali. Wanataka malipo na masurufu ya kustaafu kwa marais hao.

### 16.4.4 Uchanganuzi

Masuala yanayohusiana na njia za mpito zinazohitajika kwenye katiba mpya kutumika hazijaelezwa kwa sababu muhimu. Yamegusiwa katika sura nyingine. Katika tukio lolote, masuala mengi yaliyotajwa yalikuwa ya kiufundi dhahiri na yatashughulikiwa kwenye mswada.

### 16.4.5 Mapendekezo

Mapendekezo haya yaliyotolewa yanazuia masuala ya urithi na upokezi mamlaka kutoka kwa Rais mmoja hadi mwingine. Tume inapendekeza kwamba:-

*(i)* *Taratibu za urithi sharti ziwe -*

(a) Makamu wa Rais

(b) Waziri ateuliwe na Rais

(c) Waziri ateuliwe na Baraza la Mawaziri

(d) Spika wa Bunge

Hivyo basi, Rais asipokuwa nchini ama ameshindwa kutekeleza majukumu ya afisi yake, Makamu wa Rais atatekeleza majukumu katika afisi yake hadi Rais atakaporejea ama anaweza kuyatekeleza yote.

*(ii)* *Rais aliyechaguliwa atachukua mamlaka baada ya kuapishwa au kuthibitisha uaminifu na utii wake kwa Jamhuri ya Kenya na katiba ya Kenya katika sherehe za umma za uapishaji zitakazoandaliwa siku kipindi cha awamu kumalizika.*

## SURA YA KUMI NA SABA

## HITIMISHO NA MUHTASARI WA MAPENDEKEZO

### 17.1 Hitimisho

Harakati ya marekebisho ya Katiba yalikuwa marefu, yenye kutatanisha na magumu. Tume ilipokea taarifa mwafaka nchini na kutoka kwa watu wa matabaka mbali mbali. Asilimia kubwa ya taarifa hiyo, ilijumuisha masuala ya kimsingi ya maisha. Hivyo ndivyo inavyostahiki kwa sababu ni masuala hayo ambayo yanabadili moyo wa taifa lolote lile. Lilikuwa ni jukumu la Tume kufafanua na kufasiri haya masuala katika kanuni za kikatiba. Mpangilio ufuatao umejitokeza kutoka tathmini ya mwanzo simulizi na iliyoandikwa na kupokelewa na tume kulingana na maandishi haya -

Jumla memoranda - 35.413

Imepangaliwa katika kurasa 34,157 kwenye jedwali kama ifuatavyo -

| Nambari | Suala/Sehemu + husika: | Kutoka: | Hadi: | Kurasa: |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Utangulizi | 1 | 464 | 464 |
| 2. | Kanuni na sera za nchi | 465 | 778 | 314 |
| 3. | Ukuu | 779 | 1438 | 660 |
| 4. | Uraia | 1439 | 2713 | 1275 |
| 5. | Ulinzi na usalama wa kitaifa | 2714 | 3613 | 900 |
| 6. | Vyama vya upinzani | 3614 | 4717 | 1104 |
| 7. | Mfumo na mtindo wa serikali | 4718 | 6331 | 1614 |
| 8. | Bunge | 6332 | 10034 | 3703 |
| 9. | Mamlaka ya nchi | 10,035 | 12908 | 2874 |
| 10. | Mahakama | 12,909 | 14608 | 1700 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 11. | Serikali za wilaya | 14,609 | 16654 | 2046 |
| 12. | Mfumo wa Uchaguzi | 16,655 | 19447 | 2793 |
| 13. | Haki za Kimsingi | 19,448 | 22647 | 3200 |
| 14. | Haki za makundi ya wachache | 22,648 | 23687 | 1040 |
| 15. | Haki za ardhi na mali | 23,688 | 25852 | 2165 |
| 16. | Utamaduni, Jamii na madhehebu ya kieneo | 25,853 | 26606 | 754 |
| 17. | Usimamizi na matumizi ya maliasili | 26,607 | 28011 | 1405 |
| 18. | Mazingira na maliasili | 28,012 | 28632 | 621 |
| 19. | Serikali shirikishi | 28,633 | 29021 | 389 |
| 20. | Uhusiano wa kimataifa | 29,021 | 29197 | 177 |
| 21. | Tume za kikatiba, asasi na afisi | 29,198 | 29939 | 742 |
| 22. | Urithi na upokezi wa mamlaka | 29,940 | 30529 | 590 |
| 23. | Haki za wanawake | 30,530 | 31046 | 517 |
| 24. | Sera za kimataifa | 31,047 | 31071 | 25 |
| 25. | Sera za kieneo | 31,072 | 31082 | 11 |
| 26. | Sera za kitaifa/kisehemu | 31,083 | 33471 | 2389 |
| 27. | Desturi, mashirika, sheria na miswada ya kiislamu | 33,475 | 33870 | 396 |
| 28. | Maudhui ya jumla ya kimsingi | 33,871 | 34157 | 288 |

Ni wapi kwamba Tume ilipokea maoni mengi kupita yale yanayohitajika ili kutunga mswada wa Katiba. Kwa hivyo kuna mapendekezo yaliyotolewa kwa Tume au na Tume lakini hayako kwenye mswada wa Katiba.

## 17.2 Muhtasari wa Mapendekezo

Muhtasari ufuatao, ndio wenye mapendekezo, ambayo Tume imerekebisha na kuyaunganisha katika mtindo wa mswada wa katiba. Haya ni kama yafuatayo:-

**Katika Ukuu wa kikatiba, Katiba mpya lazima -**

1. iwe na masharti madhubuti, ambayo hata Bunge lenyewe halitakuwa na uwezo wa kuunda sheria pasi kupata maoni kwanza kwa wananchi.

2. ishughulikie masuala ya uhusiano katika viungo vya serikali na ni sharti vishughulikie usawazishaji na usambazaji madaraka.
3. iwe na ibara katika ukuu na sharti ieleze kwamba katiba inawaunganisha watu wote na viungo vyote vya serikali katika viwango vyote.
4. isipokuwa kama sehemu ya (1) hapo juu, iliyopendekezwa na irekebishwe na angalau asilimia 75% ya wabunge.

**Katika ufafanuzi wa katiba, katiba mpya -**

5. iwe na ibara fafanuzi ambayo itawasaidia wafasiri ili wapendezwe na maadili ya kimsingi ya kikatiba bila kutoa ubunifu wa mahakama ambao unaruhusu katiba kuwa haki ya kudumu.
6. iwe na masharti ambayo yanaelezea kanuni za utawala fafanuzi ambao ni lazima ujumuishe kupanda cheo kwa maadili yanayoweka wazi demokrasia katika jamii, katika msingi wa haki za binadamu, usawa na uhuru.
19. ibuni mahakama kuu ya kutoa uamuzi juu ya ufafanuzi wa katiba.

**Katika uhuru wa wananchi kujitawala, katiba mpya -**

20. itambue uhuru wa wananchi kujitawala.
21. itambue kwamba serikali inapata nguvu kutoka kwa wananchi.

**Katika utaifa na uraia, katiba mpya -**

22. impe mume wa mke usawa kulingana na uraia hata kama mke ameolewa na Mkenya ama Mkenya amemwoa mke mgeni.
23. ielezee kwamba raia wote wana haki ya kupata kitambulisho cha kitaifa na paspoti ya usafiri.
24. itoe uraia maradufu, kwa kuzaliwa, kusajiliwa na katika hali ya makao ya kudumu.
25. kuunda na kubuni shirika huru litakalokuwa na jukumu la kushughulikia masuala ya uraia ili kuzuia usumbufu wa haki za uraia.
26. itoe uraia kwa watoto wa kupanga na wa kihalali
27. itoe uraia kwa watoto walio na umri fulani waliopatikana humu nchini ambao wazazi wao hawako (hawapatikani).

28. itoe usawa kwa raia wote bila kujali asilia ya rangi, kabila, umri, mahali pa kuzaliwa, jinsia ama tofauti zozote zilizopo.

**Katika utawala na ulinzi, Katiba mpya -**

29. ibainishe maeneo ya kimataifa ya Kenya na kutangaza utawala kwenye maeneo hayo.
30. ibuni walinzi na jeshi la usalama ambalo haliungi mkono vyama vyoyote vya siasa, wenye nidhamu, wazalendo na ambao watadhibitiwa na umma.
19. ielezee kikamilifu namna ambavyo hali ya kivita inavyoweza kutangazwa, ama vikosi vya usalama wa taifa vyenye utendaji kazi nje ya maeneo ya Kenya.

**Katika maadili ya nchi, malengo na itikadi katiba mpya -**

20. iwe na utangulizi ambao pamoja na mengine: unatambua umuhimu wa Mungu kwa watu wa Kenya; unatambua harakati za kupigania uhuru na majukumu ya wapiganiaji uhuru, kutambua umuhimu na utawala wa wananchi katika kubuni katiba na kuweka mbinu za utawala wao na vizazi vya baadaye, msingi wa kidini, utamaduni na madhehebu mbali mbali ya Kenya, kuthibitisha kuwepo kwa Kenya kama taifa lisilogawanyika, linalonuia kuponya majeraha baada ya uhuru yaliyosababishwa na vita vya kisiasa, kuthibitisha uwajibikaji katika haki za jamii, na kuthibitisha uwajibikaji katika kupata demokrasia, kikatiba na sheria ya uongozi.
21. pia iwe na kanuni zinazoelekeza sera za nchi zinazomtaka kila mtu na vyombo vya serikali, kuheshimu sheria ya uongozi, kulinda kanuni za demokrasia, kulinda haki za kimsingi, kutekeleza mamlaka kwa haki na kutawala maliasili ya nchi vema.
22. ibuni maadili mazuri ya utawala katika taifa, demokrasia na sheria ya uongozi
23. kutangaza kwamba Kenya ni Jamhuri huru ambayo hupata mamlaka yake kutokana na kugawa mamlaka hayo kwa manufaa ya kila mwananchi.
24. kutangaza kwamba Ujamhuri huu utakuwa wa demokrasia ya vyama vingi vyenye kutaka kushirikisha kila mwananchi katika utawala wa masuala ya umma moja kwa moja ama katika njia nyingine isiyo dhahiri.

25. kutangaza kwamba mamlaka yote yatumikayo yatatekelezwa kwa niaba ya wananchi.
26. kufafanua wazi na kueleza kanuni na itikadi za kimsingi za kitaifa na maadili ambayo yanaelekeza jamii mpya, kisiasa, utamaduni, kiuchumi na ugawaji wa kimazingira.

**Katika mfumo wa kisheria, katiba mpya iweze -**

27. kufafanua wazi asili ya sheria za Kenya.
28. kutambua kuwepo na maadili ya sheria ya utamaduni wa Afrika, sheria ya Kiislamu na ile ya Wahindu.
29. kutangaza sheria za utamaduni wa kimataifa na mikataba inayowaunganisha Kenya ni mojawapo ya sheria za jamii.

**Katika mswada wa Haki, Katiba mpya ihakikishe -**

30. pamoja na haki za wa siasa na kiraia, izingatie haki za jamii, kiutamaduni, kiuchumi na maendeleo.
31. ufafanuzi kwamba sheria ya haki haiathiri watu waliopo serikalini pekee bali kati ya watu pia.
77. mahakamani kunafikika na kwamba kuna utawala wa haki.
78. kubuni kuweko kwa asasi mbali na mahakama ya usimamizi wa mswada wa kisheria.
79. kueleza hasa haki na mahitaji ya wanawake na watoto.
80. inaweka masharti yatakayotambua haki za walemavu.
81. inaweka masharti yatakayotambua haki za wazee.
82. inatambua haki za wakimbizi.
83. serikali itachukua msimamo mkali kuhusiana na makundi ya wachache yaliyokandamizwa kijinsia, kiidadi, kilemavu, umri ama sababu zilizobuniwa kihistoria, kimila au kidesturi.
84. kubuni utaratibu/mpango wa kisheria utakaothibitishwa na habari ifaayo, matumizi ya mbinu na malengo yatakayoendeshwa kwa uwazi na muda ukizingatiwa na kuchunguzwa mara kwa mara.
85. ifutilie mbali adhabu ya kifo.

86. itoe kinga ya kimsingi ya faragha katika familia, kukubaliana na njia nyingine za mawasiliano.

87. itoe kinga katika vyombo vya utangazaji, pamoja na kinga dhidi ya serikali kutatiza mashirika hayo.

88. itambue maadili ya lugha nchini, haki za watu kutumia lugha hizo, na jukumu la serikali kuwasiliana na kuzitumia na kubuni mbinu za maendeleo panapohitajika .

89. itoe hakikisho la kufikika katika habari za serikali, labda kwa sababu zisizoepukika kwa minajili ya usalama wa nchi, na habari muhimu zilizofichwa na wengine ili kushinikiza haki.

90. ilinde haki ya utawala.

91. ilinde haki ya watu walio kizuizini ama korokoroni.

92. ihakikishe haki za wateja katika matumizi bora ya bidhaa kutoka kokote, utangazaji ufaao na mashauriano bora.

**Katika utamaduni, dini na lugha mbalimbali, Katiba mpya inapaswa**

93. kuhakikisha kwamba uhuru wa kuabudu hautumiwi kuasi uhuru wa dini za watu wengine.

94. kufafanua kwamba hakuna kipimo cha kidini kitakachohitajika kama mojawapo ya sifa ili kupata mamlaka ama ithibati ya umma chini ya serikali ya Kenya.

95. kutangaza kwamba Kenya ni taifa lisiloendeshwa na dini, kwamba Kenya itafanya lolote iwezalo kusaidia, kutia moyo ama kukuza dini fulani.

96. kuweka mbinu ambazo zitakwamua vikwazo vinavyohusiana na utamaduni na maadili ya jamii, dini, pamoja na kuleta maadili ya kitaifa na umoja wake.

97. kuhakikisha kwamba hakuna mtu hata mmoja atakayelazimishwa kushiriki katika shughuli yoyote ama tambiko ama kula kiapo, kumiliki silaha, kufanya kazi ama kusomea wakati wowote, na iwapo hayo yote hatatendwa basi huo utakuwa ukiukaji wa uhuru wa mtu dini na mawazo yake.

98. kubuni sera mwafaka ya lugha na kutekeleza mbinu zifaazo.

99. kutambua Kiswahili kama mojawapo ya lugha za kitaifa na kuipa kipaumbele wakati wa sherehe za kitaifa.

100. kutambua lugha zote, Kiswahili na Kiingereza, kama lugha rasmi za kitaifa na kuhakikisha kwamba taarifa za kitaifa vitawasilishwa katika lugha hizo mbili.

101. katika harakati za ukabidhi wa mamlaka, Kiswahili kitambuliwe, Kiingereza, lugha ya ishara na lugha nyinginezo, zilizopendekezwa, za maeneo fulani kuwa lugha rasmi katika kiwango cha wilaya.

102. kubuni utekelezaji wa sheria katika asasi za kuendeleza Kiingereza, Kiswahili, lugha ya ishara na ile ya breli itumiwayo na vipofu.

103. kutoa jukumu kwa serikali ili itenge fedha fulani ili kuendeleza lugha za kitaifa, lugha ya ishara na ile ya breli ya vipofu.

104. kulinda haki za isimu za lugha na utamaduni wa wananchi wote.

**Katika vyama vya kisiasa, Katiba mpya inapaswa -**

105. kulinda haki za Wakenya wote katika kubuni vyama vyao vya kisiasa.

106. kuruhusu vyama vya kisiasa vinavyonuia kugombea uchaguzi, viweze kujisajili kwa Tume ya Uchaguzi.

107. kuruhusu Tume ya Uchaguzi kusajili na kusimamia vyama vya kisiasa.

108. kukataza vyama vyovote vya kisiasa vinavyobuniwa katika misingi ya kidini, kilugha, msingi wa rangi, kabila, jinsia, kimashirika ama misingi ya kimaeneo.

109. kukataza vyama vya kisiasa kushiriki katika vitendo vinavyotatiza taratibu za umma ama amani ya umma.

110. kutaka vyama vyote vya upinzani pindi vinaposajiliwa, viweze mara moja kufuata kanuni za kisheria zilizowekwa.

111. kufafanua namna na jinsi gani ambapo chama cha kisiasa chaweza kufutiliwa mbali ama kusajiliwa upya.

112. kufafanua masharti yanayowezesha vyama vya kisiasa, kulingana na shughuli zao, jinsi vinavyoweza kupewa pesa za umma, ama msaada zaidi.

113. kwamba kila mtu yuko huru kujiunga na chama chochote cha kisiasa, hakuna sharuti ya chama; na hivyo basi raia pekee ndio wanaoweza kuwa wanachama wa chama fulani.

114. kukataza kupokeza majukumu ya kitaifa kwa, ama matumizi ya rasilimali za nchi na, vyama vya kisiasa.

115. kutaka uchaguzi wa mamlaka na kamati za vyama vya kisiasa kushughulikia na kusimamiwa na tume ya uchaguzi.

116. kutoa masharti katika utumizi wa fedha kwa vyama vya kisiasa.

117. kutaka vyama vya kisiasa kubuni mbinu zitakazohakikisha kwamba nidhamu imedumishwa kulingana na kanuni za demokrasia, haki na sheria ya uongozi.

118. kuzuia vyama vya kisiasa kutoadhibu wabunge kutokana na misingi ya kuchangia hoja bungeni pamoja na upigaji kura kinyume na matakwa ya chama pendekezi.

119. kumtaka Rais na wakuu wa serikali kutokuwa na nyadhifa zozote kuu katika vyama vyao vya upinzani.

120. kutaka vyama vya kisiasa kuchapisha manifesto ya chama kabla ya kushiriki uchaguzi.

121. kulitaka Bunge kutekeleza sheria kuhusu vyama vya kisiasa.

**Kwenye taifa na mfumo wa kilimwengu, katiba mpya inapaswa -**

122. kulitaka Bunge kutekeleza sheria itakayosaidia kuunganisha malengo yanayohusu uchumi wa Kenya katika ulimwengu na maeneo ya kiuchumi, kwa njia yenye umakini na ufahamu.

123. itake Kenya kukubali mtazamo uwili wenye uwezo sawa katika utaratibu wa kuweka mkataba (makubaliano) yanayohusu jukumu maalum la Bunge kama sehemu yake ya “pembejeo” katika ama usimamizi wa mamlaka ya uwezo wa makubaliano hayo.

**Katika ushiriki na utawala, Katiba mpya inapaswa -**

125. kuthibitisha umuhimu wa wananchi na asasi zao katika kukuza demokrasia na kanuni za Jamhuri, maadili na utekelezaji.

126. kutaka kwamba Wakenya wote wawe na haki ya kushiriki katika masuala ya serikali ama moja kwa moja au kupitia uchaguzi huru wa wawakilishi.

127. kutaka kwamba ni jukumu la maafisa wa umma kukuza mtu binafsi na jamii katika kushiriki kwenye shughuli mbalimbali na kushawishi uamuzi unaowaathiri.

128. kubuni mbinu mwafaka ili kuhakikisha uwajibikaji wa serikali katika viwango vyote na kuwawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika utawala wa nchi.

129. kubuni mbinu za kuwezesha watu kufanya uamuzi kwenye maswala ya kikatiba kupitia ukabidhi wa mamlaka ama vinginevyo.

130. kutaka asasi za kitaifa kuongoza uchunguzi wa umma kabla ya kuundwa au kutekeleza masuala nyeti yanayoathiri maslahi ya umma.

131. kumpa mtu ama makundi haki ya kuwasilisha ombi au malalamishi yake katika asasi za umma na wenye mamlaka likiwemo bunge na kusisitiza kwamba hayo yashugulikiwe.

132. kulipatia Bunge jukumu la kutekeleza sheria itakayofafanua jukumu la uongozi wa kitamaduni, sheria ya kitamaduni na mila za jamii.

133. kubuni mbinu na njia zitakazowawezesha wananchi kuchunguza uwezo wa wawakilishi waliochaguliwa na kuwaachisha mamlaka iwapo kazi zao hazifani.

**Katika mfumo wa uchaguzi katiba mpya inapaswa -**

134. kukubali mfumo wa mseto wa uwiano kwa uchaguzi wa wawakilishi bungeni unaohusisha:

- kubakiza maeneobunge 210 kupitia mbunge mmoja katika maeneobunge hayo
- kutambulisha wawakilishi 90 wenye usawa huku orodha ya chama ikizingatiwa kupata viti sawa baina ya wanaume na wanawake bila kusahau kwamba Kenya ni taifa lenye makabila mengi kutona maeneo tofauti.

135. kutaka kwamba theluthi tatu ya wagombea uchaguzi wawasilishwe na vyama vya kisiasa, theluthi nyingine kuchaguliwa ama kuteuliwa katika nyadhfa hizo kutoka katika asasi za umma, na kuhifadhiwa wanawake.

**Katika utaratibu wa uchaguzi, Katiba mpya inapaswa -**

136. kufafanua kwamba ni haki ya kimsingi na jukumu kwa kila raia wa nchi hii kupiga kura ama kushiriki kikamilifu katika utaratibu wa uchaguzi.

137. taifa kulinda haki ya kila raia, katika kutekeleza jukumu la haki katika upigaji kura.

138. kuona kwamba vifaa vya upigaji kura, vituo vya kupigia kura na msimamizi wa upigaji kura yuko karibu na wapiga kura walemavu, jamii zenye kuhamahama na zile za walio wachache.

139. kusisitiza kanuni kwamba kura zitakuwa za siri.

140. kudhamini haki ya kupiga kura ya majeshi yenye nidhamu, watu walio vizuizini, wafilisi na wale walio hospitali.

141. kuona kwamba usajili wa wapiga kura uwe na taratibu zinazofululiza bila kuwekewa muda fulani (maalum).

142. kuona kwamba katika uchaguzi wa urais mpiga kura aliyejisajili anaweza kupigia kura kokote katika jamhuri bila kujali kituo alichojisajili.

143. kujua kwamba uchaguzi wa ubunge utengewe siku maalum ama kukadirika kila baada ya miaka mitano.

144. kuwapa uwezo wapigaji kura ili kuwatimua wajumbe wao katika baraza na maeneo ya ubunge kwenye Tume Maalum au kuachishwa mamlaka kulingana na sheria mwafaka zilizowekwa.

145. kuhitaji kiwango fulani cha elimu kwa wagombeaji uchaguzi na wawe na sifa nyingine na kuwasilisha taarifa nyingine ambazo sheria za Tume zitahitaji.

146. kuacha huru wagombeaji wa kiti cha urais na kile cha uchaguzi wa ubunge.

147. kutaja hali maalum ambayo inamkataza mgombeaji katika kushiriki uchaguzi.

148. kuwa kwamba wafanyikazi wa serikali wapewe likizo ya kutofika kazini ili kushiriki katika uchaguzi, maadam wafanyikazi wa umma wanakubaliwa kufanya hivyo kikatiba.

149. kubuni sheria inayoorodhesha maadili ya utawala wa uchaguzi na tabia ya mgombea na kuweka adhabu maalum kwa wagombea wanaovunja sheria hizo.

150. kutaka vyombo vya habari nchini kuvipa vyama vya kisiasa muda sawa ama watu wanaoshiriki uchaguzi.

151. kutambua na kurahisisha haki za raia na mashirika mengine ya kijamii na asasi zote kushiriki katika usimamizi wa uchaguzi, pamoja na msaada wa kifedha.

**Katika usimamizi wa uchaguzi, katiba mpya inapaswa -**

152. kubuni tume huru na Tume ya Uchaguzi ya haki, inayojumuisha makamishna wenye maadili walioteuliwa na Rais baada ya kupata idhini kutoka bungeni na kupata fedha moja kwa moja kutoka Hazina kuu ya Serikali.

153. kupendekeza kwamba makamishna wahudumu kwa muda wa vipindi viwili vya miaka mitano na wapewe ulinzi wakiwa bado wanashikilia nyadhfa hizo.

154. Tume ipewe mamlaka/uwezo wa kushughulikia mizozo ya uchaguzi na makosa mengine kwa haraka.

155. kubuniwa kwa Tume Maalum ya maeneo kati ya kipindi cha miaka miwili ijayo ili kuchunguza mipaka ya maeneobunge na maeneo yenye kuhitaji maeneo mengine kuongezewa kulingana na kigezo maalum cha kimsingi katika sheria za uchaguzi.

**Katika sheria, katiba mpya -**

156. iwe na mabunge mawili, moja lijulikane kama Bunge la Juu yaani Baraza la Kitaifa na Bunge la Chini yaani Bunge la Kitaifa. Mabunge haya yatakuwa na jina moja – Bunge.

157. Baraza la Kitaifa liwe na wanachama 100 ambapo wanachama 70 watachaguliwa katika wilaya zote (pamoja na Nairobi) na wanawake 30

kuchaguliwa katika mikoa yote (4 kutoka kila mkoa na 2 kutoka mkoa wa Nairobi.

158. kupendekeza kwamba baraza la kitaifa lijumuishe kama ilivyo kwenye nambari 89 hapo juu.

159. kupendekeza kipindi cha Bunge kuwa miaka mitano kutoka uchaguzi mmoja hadi mwingine.

160. kufafanua kwa undani majukumu ya Bunge.

161. kupendekeza kwamba vyama vya kisiasa vyenye wanachama wengi au vyama hivyo pamoja viunde serikali (Mseto)

162. kupendekeza Bunge liwe na uwezo usio na mipaka kwenye taratibu zao na liwe na uwezo kabambe kwenye takwimu yao.

163. kupendekeza kwamba wabunge wafanye kazi kwa muda kamili.

164. kueleza kwamba Bunge lina mamlaka ya kupiga kura ya kutokuwa na imani na serikali.

165. kuwataka wabunge kubuni afisi za maeneobunge.

166. kuelezea kwamba afisi ibuniwe ya kiongozi wa chama cha wasio wengi na kutambuliwa na Bunge.

167. kuzidisha uwezo wa Bunge ili kusimamia utendaji kazi wa mamlaka ya matawi.

**Kuhusu mamlaka ya nchi katiba mpya -**

168. itekeleze mamlaka katika matawi yanayojumuisha Rais, Baraza la Mawaziri likiongozwa na Waziri Mkuu.

169. ielezee kwamba mgombea wa Urais ateuliwe na chama cha kisiasa au awe mgombea huru mwenye umri wa miaka kati ya 35 hadi 70, msomi kutoka chuo kinachotambulika, mwenye maadili mema na tabia njema.

170. ielezee kwamba Rais achaguliwe na watu moja kwa moja katika misingi ya upigaji kura kwa wote.

171. ielezee kwamba mgombea urais, atakayeibuka na wingi wa kura asilimia 20% katika angalau mikoa mitano ya jumla ya kura asilimia hamsini (50%) ya kura zote zilizopigwa nchini, atangazwe kuwa mshindi na iwapo

hapana mshindi, uchaguzi utarudiwa kati ya wagombea wawili wa kwanza. Atakayeshinda kati yao ndiye atakayetangazwa kuwa mshindi.

172. kufafanua bila kuchanganya, mamlaka ya Rais na hali inayoweza kumfanya ayaache mamlaka na utaratibu wa kutenguliwa.

173. mgombea urais amteue mtu mwenye sifa bora kuwa Naibu wake, ambapo katika harakati za uchaguzi atakuwa makamu wake.

174. ielezee kwamba kifo kinapotokea, kutenguliwa ama kujiuzulu kwa Rais, makamu wake atachukua wadhfa huo kwa muda uliosalia.

175. ielezee kwamba iwapo afisi ya Makamu wa Rais imebakia wazi, Rais atateua Makamu kati ya wabunge waliochaguliwa.

176. ielezee kwamba katika harakati za kifo cha Rais na Makamu wake, Spika wa Bunge atachukua wadhfa wa Urais.

177. ielezee kuteuliwa kwa Waziri Mkuu atakayewajibika kwa Bunge na mkuu wa Baraza la mawaziri katika serikali ya Kenya.

178. ielezee kwamba Waziri Mkuu ateuliwe kutoka chamani au vyama vya mseto vilivyo na wanachama wa muda mrefu katika bunge, na atakuwa kiongozi wa Baraza la Mawaziri.

179. Ielezee kwamba Waziri Mkuu atakuwa wa kudumu katika Bunge, lakini endapo atajiuzulu, afe ama kuachishwa kazi na Bunge baada ya kura kupigwa ya kutokuwa na imani naye.

180. ielezee kwamba manaibu wawili wa Waziri Mkuu wateuliwe ili kumsaidia katika kutekeleza majukumu yake.

181. ielezee kwamba mawaziri wasiwe zaidi ya kumi na watano na mawaziri hao wateuliwe nje ya Bunge lakini Bunge liwaidhinishe.

182. ielezee uteuzi wa mtu mwenye sifa kuwa jaji wa Mahakama kuu na Mwanasheria Mkuu awe Mshauri Mkuu wa Kisheria wa Serikali.

183. ielezee kuwepo kwa Afisi tofauti na huru za Mkurugenzi Mkuu Mwendeshaji Mashtaka ya Umma.

**Kuhusu mahakama, sheria mpya yapaswa -**

184. kubuni Afisi ya Jaji Mkuu ambaye atakuwa kiongozi na mwanachama wa Mahakama na Rais wa Mahakama ya Juu.

185. kubuni Tume Huru ya Huduma za Mahakama na kufafanua uanachama wake na majukumu hayo.

186. ibuni mfumo mpya na mahakama unaojumuisha -

Mahakama ya Juu

Mahakama ya Rufani

Mahakama Kuu

Mahakama ya Kadhi

Mahakama Ndogo

Mahakama Maalumu

187. ielezee kwamba Mahakama ya Juu iwe Mahakama ya kikatiba na ya mahakama ya mwisho ya rufaa kwa vyovyote vile.

188. ielezee kuhusu kubuniwa kwa mahakama maalum yanayojumuisha wazee wa mitaa ili kuamua masuala yanayohusu Ardhi sheria ya kibinafsi na katika kiwango cha mitaa.

189. ifafanue waziwazi kiwango cha elimu inayohitajika katika uajiri na maafisa katika ngazi yoyote ya kisheria.

190. Itenge umri wa miaka 65 kuwa muda rasmi wa kustaafu wa Majaji, Makadhi au Mahakimu.

191. Kadhi Mkuu atambuliwe katika kiwango sawia na Jaji wa Mahakama Kuu.

192. Ihakikishe kwamba mara inapoanza kutumika, Majaji wote wa Mahakama Kuu, Mahakama ya Rufani na Kadhi Mkuu wanazingatia kanuni na masharti ya muda wao wa kuhudumu kama yanavyoelezewa katika hali yake ya utekelezaji.

193. Kuhusu huduma ya umma, Katiba mpya -

194. Ianzishe Tume Huru ya Utumishi wa Umma na kuelezea ni kina nani wanaofaa kuwa wanachama, wajibu wake, mamlaka na masharti ya uteuzi.

**195.** Ihakikishe kwamba uteuzi wote katika Utumishi wa Umma unatekelezwa na Tume hiyo na pia iwe ya kipekee inayohakikisha nidhamu ya watumishi hao**.**

196. Ihakikishe kwamba watumishi wote wa umma hawana budi kustaafu watimiapo umri wa miaka 65.

197. Kuhusu upunguzaji na usambazaji madaraka, Katiba mpya -

198. Ihakikishe utaratibu wa daraja nne za mamlaka katika ngazi za mikoa, wilaya, kata na vijiji.

199. Ihakikishe kwamba Nairobi liwe jiji kuu la Kenya na kuongozwa kuambatana na sheria maalum.

**200.** Ihakikishe kwamba sehemu nyingine za manispaa ziongezwe kwa kutambua sheria iliyobuni ngazi (nne) hizo za utawala**.**

201. Ihakikishe sheria ya taratibu za upunguzaji na usambazaji wa madaraka.

202. Ihakikishe kwamba punde baada ya kuanza kutumika utawala wa mikoa ufutiliwe mbali.

**Kuhusu usimamizi wa maliasili, Katiba mpya sharti -**

203. Iweke maliasili yote ikiwa ni pamoja na madini, maji, ardhi, misitu, uvuvi na sehemu chepechepe mikononi mwa Wakenya wenyewe isipokuwa pale umilikaji umo mikononi mwa watu wengine au wananchi katika sheria hii.

204. Ihakikishe kwamba serikali chini ya usimamizi wa bunge inawajibika katika kusimamia rasilmali za nchi kwa niaba ya raia.

205. Ihakikishe kwamba kumeanzishwa utaratibu mwafaka ambapo jamii mbalimbali zinapata fursa ya kushiriki katika usimamizi wa raslimali za kitaifa.

**Kuhusu mazingira Katiba mpya**

206. Ihakikishe kwamba kuna haki maalum kuhusu uhifadhi wa mazingira pamoja na kanuni za kuzingatiwa katika kutekeleza wajibu na uhifadhi wa mazingira.

207. Ihakikishe kwamba ipo sheria zinazompa kila Mkenya haki ya kuishi katika mazingira safi, kwa manufaa ya vizazi vya sasa na hata vijavyo.

208. Ihakikishe kwamba Tume ya Taifa ya Usimamizi wa Mazingira imebuniwa ili kuhifadhi mazingira.

**Kuhusu ardhi, Katiba mpya sharti:**

209. Ihakikishe kwamba umilikaji wa ardhi unawekwa mikononi mwa raia binafsi au jamii ya Wakenya.

210. Ihakikishe kwamba watu wasiokuwa raia wa Kenya hawaruhusiwi kumiliki ardhi hapa nchini, isipokuwa tu wanaweza kukodisha.

**211.** Ihakikishe kwamba ardhi imechukuliwa kuwa mali ya umma, jamii ama watu binafsi na ziwekwe kanuni za kufuatwa katika utambuzi wa umiliki wa ardhi katika viwango hivyo vitatu**.**

212. Ihakikishe kwamba imetoa ulinzi wa haki ya umilikaji ardhi kwa wenye ardhi wote, bila kuzingatia muda wa mapatano.

213. Ianzishe Tume ya Kitaifa ya Ardhi ili, pamoja na mengine, imiliki na isimamie ardhi ya umma.

214. Ihitaji Bunge kuanzisha utaratibu wa kuchunguza na kutwaa ardhi yote ya umma inayomilikiwa kiharamu na ichunguze utolewaji ardhi wakati wa ukoloni na hali nyingine.

215. Ihitaji serikali kuunda na kuchapisha sera ya kitaifa ya ardhi.

216. Ihakikishe usalama wa haki za ardhi kwa wamiliki ardhi wote bila kujali muda wa ukodishaji.

217. Ihitaji serikali katika viwango vyote ianzishe mfumo wa uwajibikaji na usio na gharama kubwa ya usimamizi wa ardhi.

218. Ihakikishe kwamba inaheshimu sheria ya kitamaduni katika haki za kumiliki ardhi na kupokezwa kwa haki hiyo kwa vizazi vijav**yo** kama sehemu ya sheria ya kibinafsi ya wananchi wa Kenya.

219. Itambue haki ya mali ya waliooana na kuwa na haki ya mali kama hayo kwa maharusi wakati na baada ya kuoana.

**Katika haki za kitaaluma, Katiba mpya lazima:**

220. Ihifadhi elimu za kimsingi na vipawa na kuviendeleza kwa kuvidhibiti.

221. Bunge lihakikishe kwamba sheria ya kuukuza utamaduni, viwanda na taaluma bunifu za kisayansi ili kuwavutia wawekaji rasilmali ambazo pia zitawafaidi waanzilishi kwa juhudi zao.

**Katika usimamizi wa fedha na mapato, Katiba mpya lazima:**

222. Ianzishe Baraza la Kushughulikia Ufufuzi wa Uchumi uliozorota na usimamizi wa hazina kuu litakalowajumuisha wataalamu katika taaluma husika na wakati huo huo kudumisha mamlaka hayo au kutekeleza jukumu hilo kama itakavyofafanuliwa katika sheria.

223. Ianzishe Kamati ya Bajeti ya Bunge ambayo itafanya kazi kwa ushirikiano na Hazina Kuu ya Serikali kuboresha mgao wa Bajeti wa Matumizi ya pesa za Serikali kwa mwaka.

224. Ihakikishe kuanzishwa kwa afisi ya Bunge kuhusu bajeti ambayo itatoa ushauri mwafaka kwa Kamati ya Bajeti kuhusu usimamizi wa kifedha na uhasibu.

225. Ihakikishe Benki Kuu ya Kenya imekuwa asasi ya kujisimamia ambayo itakuwa Hazina Kuu ya pesa za Kenya, ikiongozwa na Gavana na Msaidizi ya Gavana watakaokuwa na mamlaka ya kutekeleza majukumu yao kama itakavyoratibiwa katika sheria.

226. Izuie ongezeko la ushuru wa mara kwa mara bila idhini ya Bunge.

227. Izuie kuwepo kwa deni la umma katika Serikali ya Kenya kabla haijaidhinishwa na Bunge kwanza.

228. Ihakikishe kubuniwa kwa afisi mbili za kisheria, ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu na ya Msimamizi wa Bajeti na hatimaye kuelezea jukumu la kila mojawapo ya afisi hizo.

**Katika usimamizi wa wafanya kazi Katiba mpya lazima:**

229. Ilihimize Bunge lipitishe sheria itakayohakikisha kuwapo kwa sekta ya utumishi wa umma thabiti, yenye uadilifu na inayowajibika.

230. Iwahakikishie Wakenya kwamba elimu ya shule ya msingi itakuwa ni ya bila malipo na ya lazima.

**Katika muundomsingi wa kijamii Katiba mpya sharti:**

231. Iweke katika sheria ya haki ya kimsingi ya afya, nyumba na miundomisingi ya kuutosheleza umma.

**Katika sayansi na teknolojia, Katiba mpya sharti:**

232. Ihakikishe Kenya imebuni na kutekeleza mfumo wa Sayansi na Teknolojia ili kuuboresha mfumo wa taifa wa utafiti na uvumbuzi.

**Katika Tume na afisi za kikatiba, Katiba mpya sharti -**

233. Ibuni na kuelezea uwezo na uwajibikaji wa Tume na afisi za kikatiba kusimamiwa Kikatiba.

234. Ibainishe wazi kwamba uteuzi wa maafisa katika tume na afisi za kikatiba, upitishwe na Bunge.

235. Ianzishe Tume ya Mishahara na Marupurupu ili kubainisha kiwango cha marupurupu na masurufu kinachostahili kuliwa wahudumu katika afisi za kikatiba.

**Katika uongozi wa jamii, Katiba mpya lazima:**

236. Ibuni mfumo wa kutathmini uwajibikaji katika afisi zote za umma ikiwa ni pamoja na wale wanaozisimamia afisi zote za kikatiba.

237. Ianzishe Tume ya Maadili na Hadhi ili kusimamia kanuni za uongozi.

**Katika urithi na upokezaji mamlaka, katiba mpya sharti -**

238. Ibuni mwongozo mwafaka unaohusiana na usimamizi wa upokezanaji mamlaka kama inavyostahili punde baada ya kuanza kazi.

239. Ieleze kwamba mtu yeyote ambaye alikuwa akishikilia wadhfa wa urais zaidi ya awamu mbili chini ya Katiba ya zamani apigwe marufuku kuwania wadhifa huo chini ya Katiba hiyo.

## NYONGEZA

## IBARA YA 3A

## SHERIA YA TUME YA MAREKEBISHO YA KATIBA YA KENYA

## MPANGILIO WA IBARA

## SEHEMU YA KWANZA – DIBAJI

**Ibara**

1 - Anwani fupi
2 - ufafanuzi
3 - Nia na madhumuni ya marekebisho ya Katiba
4 - Viungo vya marekebisho
5 - Kanuni za mwelekezo

**SEHEMU YA PILI – KUANZISHWA NA KUUNDWA KWA TUME**

6 - Uanzilishi na uanachama wa Tume
7 - Utaratibu wa kuwateua makamishna
8 - Sifa za kubalika na kutokubalika kuteuliwa kuwa makamishna
9 - Mwenyekiti na Naibu Mwenyekiti
10 - Kuanzishwa kwa Kamati Teule ya Bunge
11 - Masjala
12 - Watumishi wa Tume, Wataalam na Washauri
13 - viapo vya afisi na matamko ya dhati
14 - Kanuni za maadili
15 - awamu za afisi kwa makamishna na Katibu
16 - Kuondolewa kwa makamishna kwenye uchaguzi

**SEHEMU YA TATU – SHUGHULI, UWEZO NA FADHILA ZA TUME NA MAKAMISHNA**

17. Shughuli za Tume
18. Uwezo wa Tume
19. Kamati za Tume
20. Vikao (baraza) vya kikatiba vya eneobunge
21. Utaratibu
22. Usambazaji wa rekodi za Tume
23. Vituo vya hifadhi za nyaraka
24. Elimu ya uraia
25. Fadhila za Makamishna na Katibu wakati wa kuwa afisini (kazini) na kinga nyinginezo.

**SEHEMU YA NNE – TAARIFA YA TUME NA HATUA ZAKE**

26. Ukamilisho wa kazi, ripoti na hatua zake
27. Kongamano la kitaifa la Ripoti ya Tume
28. Utambulisho wa ripoti ya Tume kwenye bunge

**SEHEMU YA TANO – MATUMIZI YA SHUGHULI ZA MAREKEBISHO**

29. Pesa za matumizi ya shughuli za marekebisho
30. Hazina ya marekebisho ya Katiba ya Kenya
31. Malipo na marupurupu ya makamishna
32. Akaunti (hesabu) na uhasibu

**SEHEMU YA SITA – UVUNJAJI WA VIUNGO VYA MAREKEBISHO NA MASHARTI YA MWISHO**

33. Uvunjaji wa Tume na kutangua agizo hili
34. Kanuni
35. Agizo la kuhusisha Serikali

**JEDWALI LA KWANZA** – Viapo na kauli za dhati

**JEDWALA LA PILI** – Kanuni za maadili kwa wanatume na watumishi

**JEDWALI LA TATU** – Kanuni za usalama wa shughuli za kidemokrasia kwa ajili ya marekebisho ya Katiba.

## SHERIA YA 3A

## SHERIA ZA MAREKEBISHO YA KATIBA YA KENYA

**Nambari**

6 ya 1998 | 5 ya 2000 | 2 ya 2001

Sheria ya Bunge kurahisisha utambuzi wa wananchi wa Kenya kuhusu marekebisho ya Katibana madhumuni ya mshikamano.

KUTEKELEZWA na Bunge la Kenya ifuatavyo:

**SEHEMU YA KWANZA – DIBAJI**

Anwani fupi

**1.** Sheria hii inaweza kutumiwa kama Sheria ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya.

Ufafanuzi
6 ya 1998 kifungu cha 4
5 ya 2000 kifungu cha 3
2 ya 2001 kifungu cha 3

**2.** Katika Sheria hii isipokuwa muktadha tofauti huhitaji-:

"Mwenyekiti" na "manaibu wenyekiti" huumaisha mwenyekiti na makamu mwenyekiti kuteuliwa chini ya kifungu cha 9 cha Sheria hii;

"Tume humaanisha kuwa Tume ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya ilianzishwa chini ya kifungu cha 6;

"Kamishna" humaanisha kuwa Kamishna huteuliwa chini ya sheria hii;

Ibara ya 7

"Eneobunge" lina maana kugawiwa kwake katika kifungu cha pili cha bunge na Sheria ya Uchaguzi wa Urais;

"Baraza la Kikatiba la Eneobunge" humaanisha baraza

lililoanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 20;

“Katiba humaanisha Katiba ya Kenya”;

Ibara ya 265

“Baraza la mji” lina maana kuwa limewekwa katika kifungu cha 2 cha Sheria ya Serikali za Wilaya, na kwa nia ya Sheria hii, ni pamoja na Baraza la Jiji la Nairobi;

Ibara ya 221

“Shirika la Habari la Kenya” humaanisha kuwa Shirika la Habari Kenya lilibuniwa chini ya Sheria ya Shirika la Habari la Kenya.

Ibara ya 225

“Baraza la Huduma ya Maktabaya Kitaifa Kenya” humaanisha kuwa Baraza lilianzishwa chini ya Sheria ya Baraza la Huduma ya maktaba ya kitaifa Kenya;

“Kongamano la Kikatiba la kitaifa humaanisha kuwa kongomano la kikatiba la kitaifa linarejelewa katika ibara ya 27 (1) (c).

Nambari 19 ya 1990

“Shirika lisilo la Kiserikali” maana yake ni kwamba shirika lisilo la kiserikali limesajiliwa chini ya Sheria ya Utaratibu wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali, 1990;

“Katibu humaanisha kuwa Katibu huteuliwa chini ya kifungu cha 11.

Nia na madhumuni ya marekebisho ya kikatiba
6 ya 19998
kifungu cha 2 ya 2001

**3.** Nia na madhumuni ya marekebisho ya Katiba ni kulinda masharti yaliyomo:-

(a) Kuhakikisha amani, umoja wa kitaifa na uadilifu wa Jamhuri ya Kenya ili kulinda hali njema ya wananchi wa Kenya.

(b) Kubuni mfumo huru na wa kidemokrasia wa serikali ambayo

kifungu cha 4

inahifadhi uongozi bora, ukatiba, kanuni ya sheria, haki za binadamu na usawa wa kijinsia.

(c) Kutambua na kuweka mipaka ya uwajibikaji miongoni mwa viungo vya serikali pamoja na utawala, bunge na mahakama ili kwamba kubuni usambazaji na usawazishaji wa mamlaka kati yao na kuhakikisha uwajibikaji wa serikali na maafisa wake kwa wananchi wa Kenya.

(d) Kuhamasisha ushiriki wa wanainchi katika uongozi wa nchi kupitia uchaguzi huru na wa haki na usambazaji na utumiaji wa mamlaka.

(e) Kuheshimu makabila na maeneo mbalimbali na haki za umma pamoja na haki ya jumuia ya kuandaa na kushiriki katika harakati za kitamaduni na dhihirisho la utambulisho wao.

(f) Kuhakikisha utoaji wa mahitaji ya kimsingi kwa Wakenya wote kupitia kubuniwa kwa mfumo wa usawa kwa minajili ya ukuaji wa kiuchumi na usawa wa kufikia rasilimali za kitaifa.

(g) Kutangaza na kuhamasisha ushirika wa kieneo na kimataifa kuhakikisha kuwa maendeleo ya kiuchumi, amani na uthabiti na kuunga mkono demokrasia na haki za binadamu.

(h) Kuimarisha uadilifu na umoja wa kitaifa.

(i) Kubuni mazingira bora ya uhuru wa kubadilishana mawazo.

(j) Kuhakikisha ushiriki kamili wa wananchi katika usimamizi wa maslahi ya umma; na

(k) Kuwawezesha Wakenya kuyatatua masuala ya kitaifa katika misingi ya makubaliano.

Viungo vya marekebisho
6 ya 1998 kifungu cha 5
2 ya 2001 kifungu cha 5

**4.** (1) Viungo ambavyo kwavyo mbinu za marekebisho zitatekelezwa zitakuwa:-

(a) Tume
(b) Baraza la kikatiba la Eneobunge
(c) Kongomano la kikatiba la kitaifa
(d) Kura ya maoni; na
(e) Bunge

(2) Viungo vilivyotajwa katika vipengele (1) (a), (b) na (c) havitavunjwa isipokuwa kwa mujibu wa kifungu cha 32.

Kanuni ongozi
6 ya 1998
2 ya 2001 kifungu cha 6

**5.** Katika utumiaji wa mamlaka au utekelezaji wa shughuli zilizotunukiwa na sheria hii, viungo vilivyotajwa kwenye kifungu cha 4(a), (b), (c) na (e):-

(a) vitawajibika kwa wananchi wa Kenya;

(b) vitahakikisha kwamba shughuli za marekebisho zinajumuisha wingi wa watu mbali mbali wa kenya ikiwamo hali ya jamii kiuchumi, rangi, kabila, jinsia, imani za kidini, umri, kazi, mafunzo, wasiojiweza na wasiobahatika;

(c) kuhakikisha, hasa kupitia uchunguzi wa kanuni katika Jedwali la Tatu kwamba shughuli za marekebisho:-

(i) zitawapatia wananchi wa Kenya fursa ya kushiriki kikamilifu, waziwazi na kwa dhati katika kutoa na kujadili mapendekezo ya kubadili Katiba;

(ii) kulingana na sheria hii shughuli ziongezwe katika hali ya uwazi: na

(iii) shughuli zinaongozwa kwa heshima kwa ajili kanuni za kiulimwengu za haki za binadamu, usawa wa jinsia na demokrasia;

(iv) kuhakikisha kwamba matokeo ya mwisho ya shughuli za marekebisho kwa uaminifu zinawakilisha matarajio ya wananchi wa Kenya.

## SEHEMU YA PILI – KUANZISHWA NA KUUNDWA KWA TUME

Uanzilishi na Uanachama wa Tume

**6.** (1) Kuna Tume iliyobuniwa itakayojulikana kama Tume ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya.

(2) Tume hiyo itakuwa shirika pamoja na mafanikio ya kudumu na mshikamano wa pamoja na katika shirika la jina lake, itakuwa na uwezo wa:-

(a) kushtaki na kushtakiwa;

(b) kuchukua, kununua au kujipatia, kumiliki, kugharimia, au kupanga mali inayohamishika na isiyohamishika; na

(c) kufanya au kutekeleza shughuli nyingine zote muhimu kwa utekelezaji kamili wa harakati zake chini ya sheria hii ambayo huweza kufanywa kisheria au kutekelezwa na shirika.

Ibara ya 446

(3) Masharti ya Sheria za Mashirika ya Serikali hayatatumika kwenye Tume.

(4) Tume itakuwa na:-

(a) Mwenyekiti atakayeteuliwa kutoka miongoni mwa wanatume kwa mujibu wa kifungu cha 9.
(b) Wanatume ishirini na saba waliopendekezwa na Bunge na kuteuliwa na Rais kwa mujibu wa kifungu cha 7.
(c) Mwanasheria Mkuu au mwakilishi wake na Katiba ambaye atakuwa mwanatume kwa mujibu wa wadhifa wake bila haki ya kupiga kura.

(5) Katika kuwapendekeza watu au uteuzi kama wanatume, bunge litaangalia kwa makini – kuhusu:

(a) Kenya kikabila, kijiografia, kitamaduni, kisiasa, kijamii na kiuchumi mbalimbali; na
(b) Kanuni ya usawa wa jinsia.

Utaratibu wa kuwateua
6 ya 1998 kifungu cha 7
5 ya 2000 kifungu cha 6
2 ya 2001 kifungu cha 8

**7.** (1) Bunge katika siku saba ya kuanza utekelezaji wa sheria hii, itaalika maombi kutoka kwa watu wenye sifa zinazohitajika chini ya sheria hii ili kupendekezwa kama makamishna kwa njia ya matangazo gazetini na kwenye angalau magazeti matatu ya kila siku ya kitaifa.

(2) Maombi chini ya kipengele (1) yatafikishwa Bungeni mnamo siku kumi na nne za matangazo na huenda yakafanywa na:-

(a) mtu yeyote mwenye sifa zinazohitajika, au
(b) mtu yeyote, shirika au kundi la watu wanaounga mkono mapendekezo ya yeyote mwenye sifa zinazohitajika.

(3) Bunge litashughulikia maombi yaliyopokelewa ya waombaji katika siku kumi na nne za kumalizika kwa muda ulioelezwa katika kipengele cha pili (2), na litateua watu kumi na saba kuwa makamishna.

(4) Kwa kuzingatia maombi chini ya kifungu, Bunge litalazimika kushauri kwa mapana na marefu.

(5) Bunge litakabidhi orodha ya wateuliwa chini ya kipengele (3) kwa Mwanasheria Mkuu ili kufikishwa kwa Rais.

(6) Mwanasheria Mkuu hatimaye atakabidhi orodha ya majina ya wateuliwa aliowapokea chini ya kipengele (5) kwa Rais.

(7) Rais atapokea majina aliyokabidhiwa chini ya kipengele (6) kuidhinisha majina ya watu ishirini na saba walioteuliwa chini ya kipengele (3) kuwa makamishna.

Sifa zinazostahili na kutostahili katika kuteuliwa Makamishna
6 ya 1998 kifungu cha 8
5 ya 2000 kifungu cha 7
2 ya 2001 kifungu cha 9

**8.** (1) Kutokana na kipengele (3) cha majina ya makamishna ishirini na saba yaliyorejelewa katika kifungu cha 6:-

(a) kumi na mmoja wanapaswa kuwa na elimu ya angalau miaka mitano ya ujuzi au tajriba katika masuala yanayohusu sheria; na
(b) kumi na sita watakuwa na elimu ya, pamoja na ujuzi kuhusu maslahi ya jamii:

Bora tu:
(i) watu waliofaulu kulingana na aya (b) watakuwa wawili wawili katika kila mkoa;
(ii) jumla ya wanachama wa Tume haitakuwa na zaidi ya watu wane kutoka katika mkoa mmoja; na
(iii) angalau wanachama sita wa Tume wawe wanawake.

(2) Mbali na masharti ya kipengele (1), hakuna mtu atakayefaa kuteuliwa kama kamishna.

(a) isipokuwa mtu huyo:-

(i) ni mwenye mawazo bora sana; na

(ii) mwenye sifa njema na uadilifu; au

(b) endapo mtu kama huyo ni muflisi asiyeachiliwa

(3) Makamishna wote pindi wakishateuliwea watakoma kushughulikia ushiriki wa vyama vya kisiasa au mashirika mengine yoyote yaliyosajiliwa au la, kutangaza maoni ya mshiriki wa chama fulani kulingana na shughuli za marekebisho ya Katiba.

Mwenyekiti na manaibu wenyeviti
6 ya 1998 kifungu cha 9
5 ya 2000 kifungu cha 8
2 ya 2001 kifungu cha 10

**9.** (1) Kutakuwapo na mwenyekiti wa Tume ambaye atateuliwa na Rais kutoka miongoni mwa makamishna walioteuliwa chini ya kifungu 8 (1) (a),

(2) Kutakuwa na manaibu wenyeviti watatu wa Tume, ambapo mmoja atakuwa mwanamke aliyechaguliwa na makamishna kutoka miongoni mwa idadi yao.

(3) Mwenyekiti ataitisha mkutano wa tume katika siku kumi na tano za uteuzi wa makamishna ambao kwao Makamishna watachagua manaibu wenyekiti watatu wa Tume jinsi inavyoelezwa kwenye kipengele cha (2) ambapo mmoja ataenziwa kama mwenyekiti wa kwanza.

Kuanzishwa kwa Kamati Teule la Bunge
5 ya 2000 Kifungu cha 9

**10.** Bunge, kulingana na kanuni zake za usimamizi, kubuni kamati teule yenye wanachama wasiopungua watano na wasiozidi wanachama ishirini na saba ni kusaidia katika utekelezaji wa shughuli zake chini ya sheria.

2 ya 2001
kifungu cha 11

Masjala
5 ya 2000
Kifungu cha 10
2 ya 2001

**11.** (1) Kutakuwa na Katibu wa Tume ambaye atateuliwa na Rais kutokana na watu wawili waliopendekezwa na Bunge.

(2) Katibu atahudumu wakati wote

(3) Panapotokea nafasi katika afisi ya Katibu wa Tume, majina matatu ya wanaofaa yatakabidhiwa kwa Kamati Teule ya Bunge mnamo siku kumi na nne za kutokea nafasi hiyo ili kujaza nafasi chini ya sheria hii.

(4) Mnamo siku saba za kuyapokea majina kutoka kwa Tume, Kamati Teule itakabidhi majina ya wawili Bungeni ambayo kwayo Rais atamteua Katibu.

(5) Rais atamteua Katibu mnamo siku saba za kuyapokea majina yaliyotolewa chini ya kipenge cha (4).

(6) Watakuwapo angalau manaibu wenyekiti watatu wa Katibu walioteuliwa na Tume kumsaidia Katibu katika usimamizi, utafiti na kusawidi na majukumu mengine au shughuli za Tume.

Watumishi
wa Tume
wataalam na
washauri
6 ya 1998
kifungu cha 10
5 ya 2002
kifungu cha 11

**12.** (1) Utumishi wa Tume utakuwa na:-

(a) Kama vile maafisa na watumishi wengine Tume itakavyoteua ni kuisaidia katika utekelezaji wa shughuli chini ya sheria; na

(b) Kama vile maafisa wa umma itakavyokuwa muhimu kwa nia ya Tume itakavyotaka, kulingana na mahitaji ya Tume, kuungwa mkono pamoja na hayo na Tume ya Huduma ya Jamii, Tume ya Huduma ya Bunge, Tume ya Mahakama au Tume ya kuwaajiri walimu, mambo yatakavyokuwa na maafisa wa umma watakavyokuwa, wakati wa kuungwa mkono, kuchukuliwa kuwa

maafisa wa Tume na kufungamana na mwelekeo na udhibiti wa Tume.

(2) Tume itaweza kuwaajiri weledi (wataalam) au washauri wa kuisaidia Tume inavyofaa na muhimu chini ya sheria hii.

Viapo vya afisi na matamko ya dhati
6 ya 1998 kifungu cha 11

**13.** (1) Kamishna, Katibu na manaibu wa Katibu wanaoteuliwa chini ya Sheria hii, kulingana na dini zao au imani nyingine:-

(a) Wataandaa na kuelekeza kiapo kiliochoagizwa kwenye Jedwali la kwanza; au

(b) kuandaa tamko la dhati kwa muundo ulioelezwa kwenye Jedwali la kwanza mbele ya Jaji Mkuu, kabla ya kuanzisha shughuli za Tume.

(2) Kila kiapo na tamko la dhati iliyoandikwa na kuelekezwa chini ya kifungu hiki itahifadhiwa na Katibu na Jaji Mkuu.

Kanuni za maadili
6 ya 1998 kifungu cha 12

**14.** (1) Kwa utekelezaji bora wa shughuli za Tume pamoja na Masjala ya Tume chini ya Sheria hii, kanuni za maadili zilizoelezwa kwenye Jedwali la Pili zitatumika.

(2) Mtu atakayevunja masharti ya kanuni za maadili awe ni:-

(a) Kuhusu Kamishna au Katibu, kulingana na masharti ya kifungu cha 15 (4), ataondolewa kutoka katika kushikilia afisi kama hiyo; na
(b) Kuhusu mtumishi wa Tume, atahusika kwenye hatua hiyo ya kinidhamu itakavyoelezwa na Tume.

Awamu ya

**15.** (1) Awamu ya afisi kwa Kamishna (mbali na cheo chake cha

Makamishna na Katibu afisi 5 ya 2000 kifungu 22 2 ya 2001 kifungu 14

Kamishna chini ya kifungu 6 (2) (c) au Katibu itakuwa kuanzia tarehe ya uteuzi chini ya kifungu cha (7) au 11 mbalimbali na isipokuwa Kamishna huyo au Katibu huyo ajiuzulu chini ya kipengele (2) au afisi ibakie wazi mapema kutokana na sababu iliyoelezwa katika kipengele cha (4) atimuliwe mnamo tarehe ya kutangua sheria hii chini ya kifungu cha 32, kutegemea masharti ya kifungu hicho kama ukamilisho wa kifedha ya, na maswala ya Tume ya utawala.

(2) Kamishna au Katibu anaweza wakati wowote baada ya kuteuliwa, kujiuzulu, kwa arifa ya maandishi kwa Rais kupitia kwa Mwenyekiti wa Tume na Kujiuzulu kutatekelezwa mnamo siku saba za tarehe ya arifa hiyo.

(3) Rais ataidhinisha kila kujiuliza katika Gazeti rasmi mnamo siku kumi na tano na zaidi.

(4) Afisi ya Kamishna au Katibu itabaki wazi ikiwa mtu:-

(a) aage dunia; au
(b) ajiuzulu kutoka afisini; au
(c) ametangazwa kuwa muflisi; au
(d) amefanya uhalifu na kuhukumiwa kufungwa kwa muda wa miezi sita au zaidi bila kulipa faini; au
(e) amevunja kanuni za maadili zilizoelezwa chini ya kifungu cha 14 au;
(f) bila sababu maalum, kukosa kuhudhuria mikutano mitatu mitawala ya Tume; au
(g) kwa sababu ya athari za kimwili au kiakili kutokuwa timamu, kutoweza kutekeleza wajibu wake kama kamishna au kama katibu; au

(h) kwa sabau nyingine, kutoweza au kutotaka kutumika kama kamishna au katibu, na kwa sababu yoyote ambayo aya (e), (f), (g) na (h) zinahusika, ukiukaji, kutofaulu, kutojiweza au kutotaka zikigunduliwa na Tume katika rekodi zake za kuungwa mkono na makubaliano ya theluthi ya waliowengi wa wanachama na mtu mwenyewe afahamishe kwa barua kusimamishwa kwake kazini kwa maandishi kupitia kwa katibu au ambapo mwathiriwa ni Katibu, kupitia kwa mwenyekiti.

(5) Nafasi inapotokea katika Tume, basi, Tume yenyewe mnamo siku za kutokea nafasi hiyo, itakabidhi kwa Kamati Teule ya Bunge orodha ya majina matatu ya watu wenye sifa zinazostahili chini ya sheria hii ili kujaza nafasi.

(6) Mnamo siku saba za kukabidhiwa majina ya chini ya kifungu cha (5), Tume teule ya Bunge itawasilisha Bungeni majina ya watu wawili kwa Rais, ambayo kwayo atamteua Kamishna.

(7) Kwenye siku saba za kupokea majina aliyopewa chini ya kifungu cha 6, Rais atateua Kamishna au Makamishna kuchukua sifa wadhifa huo huo na kutoka katika mkoa huo huo kwa heshima za Kamishna aliyeiwacha nafasi wazi.

(8) Hakuna sheria ya Tume itakayohitajika kusailiwa kwa msingi wa kuwapo tu kwa nafasi yoyote ndani au kujiondoa katika Katiba ya Tume.

Sifa za makamishna kutokubalika kwa uchaguzi.

**16.** Afisi ya Kamishna itaangaliwa kuwa ni afisi kwa nia za vipengele (1) (f) vya kifungu cha 35 ya Katiba.

## SEHEMU YA TATU - MAJUKUMU, MAMLAKA NA MARUPURUPU YA TUME NA MAKAMISHNA

Majukumu ya Tume
6 ya 1998
kifungu 15
5 ya 2000
Kifungu 26
2 ya 2001

**17.** Majukumu ya Tume yatakuwa:

(a) kuongoza na kusaidia elimu ya uraia, ili kuchangamsha mijadala ya umma na kutambua maswala ya kikatiba.

(b) kukusanya na kuweka pamoja maoni ya wananchi wa Kenya kuhusu mapendekezo ya kurekebisha katiba, na katika misingi hiyo, kuandika mswada wa marekebisho ya katiba kwa kifungu 15 uwasilishaji Bungeni.

(c) kutekeleza au kusababisha kutekelezwa kwa uchunguzi, utafiti na tathmini kuhusu katiba na Katiba nyingine na mifumo ya kikatiba kama, katika maoni ya Tume, inavyoweza kuelekeza Tume na wananchi wa Kenya kuhusu hali ya katiba ya Kenya;

(d) bila kuleta athari katika aya (b) na (c) katika kuhakikisha marekebisho ya katiba, wananchi wa Kenya;

(i) wachunguze na kupendekeza kuundwa kwa viungo vya serikali na majukumu yake, pamoja na mamlaka ya nchi, bunge na mahakama na utendaji wake unaolenga vipimo na visawiazishi pasi hofu ya uhuru wao.

(ii) wachunguze baadhi ya miundo na mifumo ya serikali, pamoja na serikali ya shirikisho na ya umoja, na kupendekeza muundo bora kwa Kenya.

(iii) wachunguze na kupendekeza maendelezo ya tume ya kikatiba iliyopo, asasi na afisi na kuimarisha nyingine za ziada ili kurahisisha utawala wa kikatiba na kuheshimu haki za binadamu na usawa wa jinsia nchini Kenya, kama na sehemu muhimu na isiyotengeka ya Kuwezesha mazingira ya kiuchumi, kijamii, kidini, kisiasi na maendeleo ya kitamaduni;

(iv) wachunguze na kupendekeza mafanikio kwa mfumo wa Kenya;

(v) bila kuleta athari katika aya ndogo (i) wachunguze na kufanya mapendekezo
katika mahakama kwa jumla, na haswa, kuimarisha mamlaka ya mahakama, yanayolenga kipimo kifaacho, kuhakikisha umilisi, uwajibikaji, utendaji bora, nidhamu na uhuru wa mahakama.

(vi) wachunguze na kutafakari sehemu ya serikali za wilaya katika mfumo wa
kikatiba wa Jamhuri ya Kenya na upunguzaji na usawazishaji wa mamlaka kwa serikali za mitaa.

(vii) wachunguze na kutafakari nafasi ya mali na haki za umiliki ardhi, inayojumuisha haki za kibinafsi, haki za Serikali na za ardhi muamana katika mfumo wa kikatiba na sheria za Kenya na kupendekeza marekebisho yatakayohakikisha kunufaishwa na ardhi na haki nyingine za mali;

(viii) wachunguze na kutafakari uongozi na matumizi ya fedha za umma na kupendekeza maendelezo yake.

(ix) wachunguze na kutafakari haki ya uraia na kupendekeza maendelezo ambayo, hasa, yatahakikisha usawa wa jinsia katika kufaidi haki;

(x) wachunguze na kutafakari vizuizi vya kijamii na kitamaduni vinavyoendeleza njia mbali mbali za ubaguzi na kupendekeza mafanikio ili pasiwe na hofu ya haki kwa wote

(xi) wachunguze na kutafakari haki za mtoto na kupendekeza maendeleo ili kuhakikisha ulinzi huo;

(xii) wachunguze na kutafakari urithi katika afisi na kupendekeza mfumo mwafaka na wenye staha wakati wa kupokezana mamlaka baada ya uchaguzi au vinginevyo;

(xiii) wachunguze na kupendekeza kuhusu uwezo wa Jamhuri kufanya mkataba na kutekeleza na hali nyingine muhimu zitakazowezesha utawala bora na ufuataji wajibu wa Kenya, chini ya sheria za kimataifa.

(xiv) wachunguze na kufanya mapendekezo kuhusu haja ya kanuni za maelekezo za sera ya serikali.

(xvi) Kuanzisha na kuunga mkono kanuni za uwajibikaji wa umma au afisi za kisiasa. (xvi) Wachunguze na kufanya mapendekezo kwa kila jambo linalohusiana na au kuambatana na hay yaliyotajwa na yanayofaulisha malengo ya jumla ya marekebisho ya katiba.

Mamlaka ya Tume
5 ya 2000
kifungu 28
2 ya 2001
kifungu 16

**18.** (1) Tume itakuwa na mamlaka muhimu katika kutekeleza majukumu chini ya sheria hii, na bila athari kwa ujumla yaliyotangualia, Tume:

(a) itatembelea kila eneobunge nchini Kenya ili kupokea maoni ya watu kuhusu katiba .

(b) Bila kuchelewa au kizuizi, itapokea taarifa, kuandaa hafla za umma au za kibinafsi kote nchini Kenya na katika njia zozote za kukusanya na kuweka pamoja maoni na mawazo ya ya kila Mkenya, awe mkazi nchini au nje ya nchi, na kwa nia hiyo Tume inaweza kuita vikao vya umma vya wakazi wa sehemu yoyote kwa midahalo ya mada muhimu katika majukumu ya Tume.

(c) Inaweza kumwita afisa yeyote wa umma kujitokeza binafsi mbele ya Tume au mbele ya kamati au kutoa stakabadhi au kitu au habari itakayochukuliwa kuwa muhimu katika majukumu ya bunge.

(2) Afisa yeyote wa umma atakayekosa kufika, bila sababu ya kisheria, kwa Tume, kufuatia mwito wa Tume chini ya kipengele (i)(c) atakuwa ametenda kosa na ataweza kutozwa faini ya shilingi elfu kumi au kifungo cha muda kisichozidi miezi mitatu au kutumikia vyote.

Kamati ya Tume

**19.** (1) Tume inaweza kuanzisha kamati ndogo za Tume kama

6 ya 1998 kifungu 17 5 ya 2000 kifungu 29 2 ya 2001 Kifungu 17

itakavyoonelea umuhimu wake katika kutekeleza majukumu chini ya sheria hii.

(2) Kwa nia ya kipengele (i) mkutano wa kamati yoyote iliyoanzishwa kwa madhumuni ya kukusanya maoni ya umma wakati wa marekebisho, utadhihirika kuwa mkutano wa Tume.

Mabaraza ya kikatiba ya Eneobunge 6 ya 1998 kifungu 18 2 ya 2001 kifungu 18

**20.** Tume inaweza, wakati wa kutekeleza majukumu yake chini ya sheria hii, kusaidia kuweka pamoja maoni ya umma kwenye maoni ya kurekebisha katiba.

**21.** (1) Kufuatia kifungu hiki, Tume itadhibiti utaratibu wake na ule wa kamati zake.

(2) Kufuatia kipengele (3) Tume itaandaa mikutano kama hiyo mahali hapo, kwa wakati huo na kwa njia ambayo Tume itafikiria ni muhimu katika kutekeleza majukumu yake chini ya sheria hii.

(3) kila mkutano wa Tume wa kukusanya maoni ya umma, utaandaliwa mahali wazi. Ila kwamba hakuna chochote katika sehemu hii, kitakachozuia Tume katika kupata ushahidi kwa siri, itakapohitaji kufanya hivyo.

(4) Mwenyekiti:-

(a) ataongoza mikutano yote ya Tume, na iwapo mwenyekiti hayupo, mwenyekiti wa kwanza ataongoza, na iwapo wote hawajahudhuria basi naibu mwenyekiti anaweza kuongoza kama Tume itakavyobainisha.

(b) atakuwa msemaji wa Tume, na kama mwenyekiti hayupo, naibuwenyekiti wa kwanza atakuwa Msemaji na endapo wote hawapo basi yeyote kati ya manaibu hao anaweza kuwa msemaji Tume kadri itakavyobainisha.

(c) Kusimamia na kuelekeza kazi za Tume. Mradi tu ikiwa mwenyekiti na naibu wake wote hawapo, makamishna waliopo wanaweza kumchagua mmoja kwa mujibu ya kifungu hiki, wakati wa kutofika kwao.

5. Akidi ya Tume na kamati zake zozote itakuwa nusu ya wanachama wake.

6. Maswali yote mbele ya Tume au ya kamati hiyo yataafikiwa kwa makubaliano, lakini endapo hakuna makubaliano, uamuzi wa Tume utafikiwa kwa kura ya wengi wa wanachama waliopo wakati wa kupiga kura.

7. Katibu atakuwa na wajibu wa:

(a) Matukio ya kila siku ya utawala wa Tume.

(b) Uratibu wa uchunguzi wa Tume, utafiti na tathmini.

(c) Kurekodi kumbukumbu na

(d) Kuhifadhi rekodi zote na stakabadhi za Tume.

Chapisho la rekodi za Tume
6 ya 1998 kifungu 20
2 ya 2001 kifungu 20

**22.** (1) Isipokuwa kama itakavyoelezwa katika kanuni, Tume itatoa rekodi za kumbukumbu za kila mkutano wa Tume kupitia:

(a) vituo vya kuhifadhi nyaraka vilivyoanzishwa chini ya kifungu 23;

(b) maktaba yaliyotolewa na Baraza la Huduma za Maktaba ya Kitaifa nchini kote; na

(c) kupitia kwenye vyombo vya habari vya uchapishaji na mitambo.

Na. 2 ya 1998

(2) Tume, kwa nia ya kipengele (1) (c), itashauriana na Shirika la Utangazaji la Kenya na mashirika mengine ya utangazaji yaliyopata kibali chini ya sheria ya mawasiliano ya Kenya, 1988 ili kuweka mipango ifaayo na salama kwa: -

(a) Kutenga muda wa utangazaji hewani kwa madhumuni ya kusambaza ripoti ya

Tume kupitia vyombo vya habari na uchapishaji; na

(b) Kuhakikisha lugha ya ishara au tafsiri za mazungumzo ya vipindi vyote Vinavyotangazwa kwenye runinga kwa madhumuni ya aya (a), watangazaji wote, vipindi vya elimu ya uraia na katika vipindi vyote vinavyoelezea habari za marekebisho ya katiba.

3. Mahali ambapo kituo cha utangazaji kimeshauriwa na Tume chini ya kipengele (2) kituo hicho kitafanya mipango ifaayo ili kutangaza vipindi hivyo ambavyo utangazaji wake umebainishwa na Tume.

Kituo cha kuhifadhia nyaraka
6 ya 1998
kifungu 20

**23.** (1) Bila kuzingatia wa sheria yoyote ya kuandikwa, baraza la wilaya katika kila wilaya itasaidia kuimarishwa na Tume kituo cha uandikaji hati katika wilaya, ili kuhifadhi na kusambaza kwa umma taarifa za yaliyoafikiwa na kumbukumbu za Tume na habari nyingine kama hizo, kama itkavyoelezwa na Tume.

(2) Mtu yeyote wakati wa saa za kazi, anaweza kuchunguza katika kituo cha uandikaji hati, taarifa zozote zilizohifadhiwa hapo, na anaweza kupata nakala hizo baada ya malipo fulani kama yatakavyopendekezwa na Tume.

Elimu ya uraia
2 ya 2001
kifungu 21

**24.** Tume, itasaidia na kuendeleza elimu ya uraia wakati wa kipindi chake cha kuhudumu ili kuhamasisha mijadala ya umma na ufahamu wa masuala ya kikatiba.

Fadhila za Makamishna na Katiba wakiwa afisini na malipo mengine

**25.** (1) Kamishna au katibu hatawajibika katika mashtaka yoyote ya umma kwa au kuhusiana na jambo lolote au kitu kilichofanyika au kutofanywa kwa imani kama kamishna au kama katibu.

(2) Hakuna kamishna au katibu atakayepaswa kutiwa nguvuni chini ya utaratibu wa umma, wkati taratibu za kushiriki katika au kurudi kutoka, mkutano wa tume au mkutano wowote ule;

(3) Hakuna mtu yeyote atakayefika mbele ya Tume, ikiwa kufika kwake ni kuitwa kwa lazima na Tume chini ya sheria hii au la atakayewajibika kujibu mashtaka ya jinai au deni au kupigwa faini yoyote au kupoteza chochote kwa sababu ya ushahidi wowote au habari zilizotolewa kwa Tume na mtu huyo.

## SEHEMU YA NNE – RIPOTI YA TUME NA HATUA ZAKE

Kumaliza kazi, ripoti na shughuli nyinginezo

**26.** (1) Tume itakamilisha kazi yake kwa muda usiozidi miezi ishirini na minne baada ya sheria hii kuanzishwa.

(2) Kwa sababu za kipengele (1) kazi za Tume zitakuwa ni kutembelea maeneobunge yote ya Kenya, kukusanya taarifa za mabaraza ya kikatiba ya maenaobunge, kuongoza na kurekodi uamuzi wa kura ya maoni iliyotajwa katika kifungu 27(6), na katika misingi hiyo kurasimu mswada na kuuwasilisha bungeni ili kuidhinishwa kuwa sheria.

(3) Endapo Tume imeonelea kuwa muda huu hautoshi, Tume inaweza kuomba kuongezewa muda na Bunge angalau miezi kumi na miwili baada ya kuanzisha kazi zake.

4. Licha ya kuongezwa kwa muda huu katika kipengele (3) Tume inaweza kupendekeza Marekebisho machache ya katiba ili kutosheleza mahitaji yoyote ya marekebisho ambayo yatachunguzwa na kushughulikiwa na Bunge kulingana na sheria zilizoko.

5. Baada ya kuwasilisha maombi ya kuongezwa kwa muda kulingana na kipengele (3), Bunge linaweza kuamua kuongeza muda wa Tume hii kwa muda ambao Bunge litaonelea kuwa unafaa.

6. Ikiwa Tume imeongezewa muda kulingana na kifungu hiki basi itaendelea na shughuli zake kulingana na sheria hii.

7. Tume itakusanya ripoti yake pamoja na muhtasari wa mapendekezo yake na kwa msingi huo mswada utabadilisha katiba

Kongamano la kitaifa kuhusu ya Tume

**27.** (1) Tume:

(a) Baada ya kukusanya ripoti na kutayarisha mswada rasmi ripoti uliotajwa katika kifungu (26)

(i) Ichapishe mswada huu kujulisha umma kwa njia iliyotajwa katika kifungu 22 kwa muda wa siku thelathini; na

(ii) Kuhakikisha kuwa ripoti hiyo na mswada rasmi umetolewa kwa watu au vikundi vya watu vinavyoongoza elimu ya uraia.

(b) Baada ya muda uliotajwa katika kifungu (a) (i), Tume iandae Kongamano La Kitaifa La Katiba ili wajadiliane, wazungumze, warekebishe na waikubali ripoti na mswada rasmi.

2. Kongamano la Kitaifa la Katiba litakuwa na wanachama wafuatao: -

(a) makamishna ambao kulingana na nyadhifa zao hawatakuwa na haki ya kupiga kura;

(b) wabunge wote;

(c) wawakilishi watatu kutoka kila wilaya na angalau mmoja awe mwanamke, na mmoja pekee anaweza kuwa diwani na wote wachaguliwe na mabaraza ya wilaya kulingana na sheria zitakazotolewa na Tume;

(d) mwakilishi mmoja kutoka kila chama cha kisiasa kilichosajiliwa wakati sheria hii ilipowekwa na asiwe mbunge wala diwani.

(e) wawakilishi wa mashirika ya kidini, makundi ya wataalau, mashirika ya wanawake, vyama vya wafanyikazi na mashirika yasiyo ya kiserikali yaliyosajiliwa wakati sheria hii ilipoanzishwa na makundi mengine yenye maslahi kwa mujibu wa maoni ya Tume;

Mradi tu:-

(i) Wanachama katika aya (e) hawatazidi asilimia ishirini na tano ya jumla ya wanachama

wa Kongamano la Taifa la Katiba lililozungumziwa katika aya (a), (b), (c) na (d); na

(ii) Tume itajadiliana na kuweka sheria zitakazoongoza ugawaji wa uwakalishi katika makundi mbalimbali ya uwakilishi yaliyowekwa katika aya (e).

3. Mwenyekiti wa Tume ndiye atakayekuwa mwenyekiti wa Kongamano la Taifa la Katiba .

4. Akidi ya Kongamano la Taifa la Katiba itakuwa nusu ya wanachama wa Kongamano hilo.

5.Maswali yote yatakayoulizwa katika Kongamano hili yataamuliwa kwa makubaliano lakini endapo hapatakuwa na makubaliano, uamuzi utafikiwa kwa upigaji kura na walio wengi ndio utakaokubaliwa.

Mradi tu:

(i) Kama kuna swali ambalo linapendekeza jambo fulani liongezwe katika katiba basi uamuzi wa Kongamano la Taifa la Katiba utaafikiwa na wanachama wasiopungua thuluthi mbili kwa kupiga kura; na

(ii) Katika kupiga kura kwa sababu ya kifungu 5 (1), kama pendekezo halijaungwa mkono na thuluthi moja au zaidi ya wanachama waliohudhuria Kongamano hili basi kwa sababu ya upungufu huo na masharti yaliyowekwa na Tume katika sheria basi wanaweza kupiga kura tena; na

(iii) Endapo wamepiga kura tena kulingana na aya (ii) na hawajaamua kuhusu kuongezwa kwa pendekezo katika katiba, Kongamano la Taifa la Katiba linaweza kutoa uamuzi ambao ni sharti uungwe mkono na wanachama waliohudhuria wasiopungua thuluthi mbili kuwa pendekezo hilo lirudishwe kwa wananchi ili liamuliwe katika kura ya maoni .

6. Tume itarekodi uamuzi uliochukuliwa na Kongamano la Taifa la Katiba kuhusu ripoti na mswada rasimu kufuatia mamlaka iliyopewa katika kifungu (i) (c) na kuwasilisha swali au maswali yaliyoungwa mkono na uamuzi uliopendekezwa katika kifungu 5 (iii) kwa wananchi ili swali au maswali hayo yabainishwe kupitia kura ya maoni.

7. Kura ya maoni ya Kitaifa kulingana na kifungu (6) itaandaliwa katika muda wa mwezi mmoja wa Kongamano la Taifa la Katiba.

Kuwasilisha ripoti Bungeni
2 ya 2001
kifungu 24

**28.** Tume itatayarisha ripoti ya mwisho na mswada wa Katiba kulingana na uamuzi wa watu katika Kura ya Maoni kama ulivyopangwa na Kongamano la Kitaifa la Kikatiba

(2) Tume itawasilisha ripoti ya mwisho na mswada rasmi kwa Mwanasheria Mkuu ili auwasilishe Bungeni.

(3) Mwanasheria Mkuu atachapisha mswada rasmi wa Katiba kama mswada wa kubadilisha katiba katika muda wa siku saba wa kupokea mswada wa Katiba.

(4) Siku saba baada ya mswada wa kubadilisha katiba kuchapishwa, Mwanasheria Mkuu atawasilisha Mswada wa Katiba na ripoti ya Tume Bungeni ili uidhinishwe kuwa sheria katika muda wa siku saba.

## SEHEMU YA TANO – GHARAMA YA MAREKEBISHO YA KATIBA

Fedha za matumizi ya shughuli za marekebisho
6 ya 1998
kifungu 23
2 ya 2001
kifungu 25

**29.** (i) Gharama ya marekebisho ya katiba yaliyogharimia itokanayo na Tume, mabaraza ya Kikatiba ya maeneobunge, Kongamano la Taifa la Katiba na kura ya maoni kulingana na sheria, yatatolewa kutoka Mfuko wa Jumla bila kutenga fedha nyingine zaidi kulingana na sheria hii.

(2) Bila kuleta athari katika kipengele(i) Tume inaweza kupewa misaada, tunu, michango au urithi utakaotumiwa kutekeleza

majukumu yoyote kwa mijajili ya marekebisho ya katiba kulingana na sheria iliyoko katika sehemu 3.

Hazina ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya
6 ya 1998 kifungu 23
2 ya 2001 kifungu 26

**30.** (1) Hazina imeanzishwa itakayoitwa Hazina ya Marekebisho ya Katiba ambayo itasimamiwa na katibu kwa niaba ya Tume.

(2) Malipo yatafanywa kwa Hazina kutoka kwenye

(a) pesa ambazo zimetengwa kutoka mfukoni mwa jumla ili kushughulikia marekebisho ya katiba kulingana na sheria hii; na

(b) misaada yoyote, michango,z awadi na urithi kulingana na kifungu 29 (2) .

(3) Katika kutekeleza sheria hii gharama zote zitalipwa kutoka kwenye hazina hii.

(4) Katika kusimamia hazina hii, katibu ni sharti ashauriane na Katibu wa Kudumu wa Hazina na kutegemea kanuni za sheria ya utoaji wa uhasibu wa hazina asimamie mfuko kwa njia ambayo itawezesha itaweza kufikia malengo ya marekebisho ya katiba.

(5) Baada ya kuvunjwa kwa Tume kulingana na kifungu 33, rasilimali zozote ambazo zilitokana na michango au zawadi zitatolewa kwa Hazina Kuu ya Serikali.

Malipo na marupurupu ya Wanatume
2 ya 2001 kifungu 27

**31.** Kwa ushauriano wa Kamati Teule ya Bunge, Waziri anayesimamia maswala ya Kifedha atabainisha Makamishna na marupurupu ya Tume na kuchunguza ili kuidhinisha bajeti ya Tume

.

Akaunti na Ukaguzi wa Fedha
6 ya 1998 kifungu 23
Ibara ya 412

**32.** Akaunti ya Hazina ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya ni sharti itunzwe, ikaguliwe na kuwasilishwa Bungeni kulingana na kifungu 18 na 19 cha Wizara ya Fedha na Sheria ya Hazina na ukaguzi wa Fedha.

## SEHEMU YA SITA – KUVUNJWA KWA VIUNGO VYA MAREKEBISHO NA HATUA ZA MWISHO.

Kuvunjwa kwa Tume
6 ya 1998 kifungu 24
2 ya 2001 kifungu 28

**33.** (i) Baada ya utekelezaji wa Mswada uliowasilishwa Bungeni kulingana na kifungu 28 kufanywa kuwa sheria ili kubadilisha Katiba, Tume itakuwa imevunjwa na awamu za Wanatume kuwa afisini zitamalizika, isipokuwa katibu na idadi fulani ya wafanyikazi kulingana na uhitaji maalum, watabaki afisini kwa muda wa miezi mitatu ili kukamilisha maswala ya Kifedha na usimamizi wa Tume.

Taratibu
2 ya 2001
kifungu 29

**34.** (1) Tume itapanga utaratibu utakaofaa ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu katika Sheria hii.

(2) Bila kuleta athari katika kifungu (1), utaratibu katika kifungu hiki, Tume inaweza:

(a) kuagiza kitu chochote kinachohitajika kuagizwa kulingana na Sheria hii.

(b) kulingana na sheria hii, kuamuru kuagizia utaratibu wa

(i) kumchagua makamu mwenyekiti na kujaza nafasi zilizobaki wazi.

(ii) kusaidia na kuendeleza utoaji wa elimu ya uraia.

(iii) kuanzisha mabaraza ya Kikatiba ya Eneobunge.

(iv) Katiba na maandalizi ya Kongamano la Kitaifa la Kikatiba

(v) utatuzi wa migogoro yoyote inayotokea wakati wa Marekebisho ya Katiba.

(c) kueleza hatua za kinidhamu ambazo zinaweza kuchukuliwa kwa mfanyakazi wa Tume.

(d) kuamuru taratibu zinazofuatwa katika kuandaa kura ya maoni iliyotajwa katika kifungu 27. Mradi tu utaratibu katika aya hii utatekelezwa kwa ushauriano na Tume ya Uchaguzi ya Kenya

Sheria kufungamanisha Serikali
2 ya 2001 kifungu 30

35. Sheria hii itafungamanisha Serikali.

**JEDWALI LA KWANZA (sehemu ya 13)** **6 ya 1998**

**5 ya 2000**

## KIAPO CHA AFISI YA KAMISHNA

Mimi………………………… kwa kuteuliwa kuwa Kamishna chini ya Sheria ya Tume ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya, ninaapa kwa dhati kwamba nitakuwa mwaminifu na kujitolea, kwa uadilifu na kwa uwezo wantu wote, nitatmikia kwa uaminifu na kutekeleza shughuli na kutumia uwezo nilio nao kwa mujibu wa uteuzi huu bila woga, upendeleo, maonevu, nia mbaya au chuki hadi mwisho wa utekelezaji wa shughuli na uwezo wangu kama Kamishna, sitashawishiwa na mwanasiasa yeyote, shirika la kidini au mashirika mengine au mtu ambaye huenda amenipendekeza kwa uteuzi. Mungu unisaidie.

………………………

**KAMISHNA**

………………………

**JAJI MKUU**

**TAMKO LA DHATI LA KAMISHNA**

Mimi ………………………… kwa kuteuliwa kuwa Kamishna chini ya sheria ya Tume ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya, ninaapa kwa dhati kwamba kwa uaminifu na kujitolea, uadilifu na kwa uwezo wangu wote nitatumikia kwa haki na kutekeleza majukumu na kutumia uwezo niliopewa kwa mujibu wa kuteuliwa bila woga, upendeleo, ubaguzi, unyanyasaji, nia mbaya au chuki na kwamba hadi mwisho wa utekelezaji wa majukumu na uwezo kama Kamishna, sitashawishiwa na chama chochote cha kisiasa, shirika la kidini au mashirika mengine au ya watu ambayo huenda yalipendekeza niteuliwa.

………………………….

**KAMISHNA**

…………………………

**JAJI MKUU**

**KIAPO CHA AFISI YA KATIBU AU NAIBU WA KATIBU**

Mimi………………….. kwa kuteuliwa kuwa Katibu/naibu wa Katibu chini ya Sheria ya Tume ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya, naapa kwa dhati kwamba kwa uaminifu na kujitolea, kwa uadilifu na kwa uwezo wangu wote nitakuwa mwaminifu na kutekeleza majukumu na kutumia uwezo nilio nao kwa mujibu wa kuteuliwa bila woga, upendeleo, ubaguzi, athari, nia mbaya au chuki na kwamba hadi mwisho wa utekelezaji wa majukumu na uwezo kama Katibu/naibu Katibu, sitashawishiwa na chama chochote cha kisiasa, kidini au maslahi mengine, au mtu yeyote. Mungu unisaidie.

……………………………………

**KATIBU/NAIBU WA KATIBU**

…………………………………….

**JAJI MKUU**

**TAMKO LA DHATI LA KATIBU NA NAIBU WA KATIBU**

Mimi ………………………………..., kwa kuteuliwa kuwa Katibu/naibu wa Katibu chini ya Sheria ya Tume ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya, kwa dhati na kwa uaminifu ninatangaza na kuthibitisha kwamba kwa uaminifu na kujitolea, kwa uadilifu na kwa uwezo wangu wote nitatumikia kwa haki na kutekeleza majukumu na kutumia uwezo niliopewa kwa mujibu wa kuteuliwa kwangu bila woga, upendeleo, ubagazi, athari, nia mbaya au chuki na kwamba hadi mwisho wa utekelezaji wa majukumu na uwezo kama Katibu/naibu wa Katibu, sitashawishiwa na chama chochote cha kisiasa, kidini au maslahi mengine au na mtu yeyote.

……………………………..

**KATIBU/NAIBU KATIBU**

…………………………….

**JAJI MKUU**

**JEDWALI LA PILI** **6 ya 1998**
**5 ya 2000**

## KANUNI YA MAADILI YA WANATUME NA WATUMISHI WA TUME

**Uadilifu na Kujitegemea kwa Wanatume**

1. (1) Kila mwanachama wa Tume atahudumu kwa uadilifu na kujitegemea na kutekeleza shughuli za afisi yake kwa nia njema bila woga, upendeleo au chuki.
2. (1) Mwanatume yeyote hatakuwa na haki ya uteuzi au mapendekezo ya ofisi yoyote ya kisiasa katika wakati wake wa kutumikia afisini.
3. Mwanatume yeyote hataruhusiwa-:
   (a) kwa uanachama wake, muungana, taarifa, vitendo au kwa namna yoyote ile kuhatarisha uhuru uliopo wa mwanatume, au katika hali ya chuki, kuaminika, uadilifu uhuru au uaminifu wa Tume.
   (b) Kufanya matumizi ya kibinafsi au manufaa kutokana na taarifa fiche anayopata kutokana na kuwa kwake mwanachama wa Tume.

Kufichua maslahi yanayoleta migogoro:

4. Endapo mwanachama wa Tume waziwazi ua kisirisiri ana hamu au nia ya kandarasi, kandarasi iliyopendekezwa au masuala mengine mbele Tume. Mwanachama kama huyo atafichua ukweli na hatahusika katika kufikiriwa au mjadala wa, au kura kuhusu swali linalolenga kandarasi hiyo au masuala mengine, ama asihesabiwe katika akidi ya mkutano huo wakati wa kujadili suala lenyewe.

5. Kanuni hii itatumika pamoja na marekebisho muhimu kwa watumishi wa Tume.

## KANUNI KUHUSU SHUGHULI ZA KIDEMOKRASIA NA UTHABITI KWA MAREKEBISHO YA KATIBA

Serikali ya Jamhuri ya Kenya, vyombo vya marekebisho ya Katiba, vyama vya kisiasa, mashiriko yasiyo ya kiserkali, na Wakenya wote.

(i) watambua umuhimu wa kujenga imani, kusababisha uaminifu na kuendeleza muafaka wa kitaifa wa shughuli za marekebisho;

(ii) kujiandaa kutonyima au kuingilia uhuru wa mtu wa kufanya mikutano au kuhudhuria mikutano ya umma au mikusanyiko, uhuru wa kibinafsi, na uhuru wa kujieleza na kutoa mawazo wakati wa shughuli za marekebisho, okoa kulingana na sheria;

(iii) hakikisha kwamba polisi watalinda usalama wa watu wote wanaohudhuria mikutano au kushughulikia haki zao nyingine dhidi ya ghasia kutoka kwenye asili yoyote ile.

(iv) kuhakikisha kwamba mikutano ya viungo vyote vya marekebisho inafanyika kwa amani;

(v) kuhesabu uhuru wa Tume na wanachama wake; na

(vi) kujizuia kutokana na kitendo chochote cha kisiasa au kiutawala ambacho kitaathiri vibaya utekelezaji au mafanikio ya shughuli za marekebisho.